# Fatawa Arkaanul-Islam

## Maswali na Majibu Kuhusu Nguzo Za Uislam

**Mtunzi: Shaykh Muhammad Bin Swaleh Al Uthaymeen (Allah amrehemu)**

**Mfasiri: Jopo La Wanafunzi**

**Wapitiaji: Abubakari Shabani Rukonk-wa**

**Yunus Kanuni Ngenda**

# فتاوى أركان الإسلام

المؤلف: فضيلة الشيخ: محمد بن صالح العثيمين

المترجم: مجموعة من طلبة العلم

المراجعة: أبوبكر شعبان رو كونكوا

يونس كنون نغندا

بسم الله الرحمن الرحيم

**KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHMA MWENYE KUREHEMU**

## Utangulizi

Allah ni mwenye kusikia na ni mwenye kujibu dua, Sifa zote njema zinamstahiki Mwenyzi Mungu ambaye yeye peke yake ndiye tunaye mtukuza na kumtegemea na kumuomba msamaha na kwake tunajikinga kutokana na shari za nafsi zetu na ubaya wa matendo yetu, mwenye kuongozwa na Mwenyzi Mungu hana wa na kumpoteza na yule mwenye kupotea hana wa kumuongoza isipokuwa Yeye, na ninashuhudia ya kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu mmoja tu na Muhammad rehma na amani ziwe juu yake ni Mja wake na ni Mtume wake.

**Baada ya hayo:**

Hakika vimeendelea kutoka vitabu vya Maswali na majibu vya Sheikh wetu Muhammad Swaleh Al-Uthaymin Mwenyezi Mungu amrehemu kuanzia: [1410-1420.H] na kwa uwezo

wa Mwenyezi Mungu vimekubalika vitabu hivi ndani na nje ya Saudi Arabia, kisha wakaomba baadhi ya watu tutoe kitabu kimoja ambacho kitazungumzia mambo ya nguzo za Uislamu na hii ni kwa ajili ya kufanya wepesi katika kutafsiri kutoka kwenye lugha ya kiarabu na kwenda lugha nyenginezo ili faida zienee kwa watu wote .

Akapeleka maombi Sheikh Fahad bin Ibrahim Al-Suleiman kwa Sheikh Muhammad bin Swaleh Al-Uthaymin atoe kitabu kama hicho, na Sheikh Mwenyezi Mungu amrehemu akakubali ombi hilo, na Sheikh Fahdi Ibn Ibrahim Al-Suleiman akaanza kukusanya kutoka katika vitabu mbali mbali vya Sheikh na maswa na majibu ya mambo yanayo husu Tauhidi, hukumu za Swala, Zaka, Swaumu na Hija.

Kikaendelea kutolewa kitabu hiki kila mwaka na kutafsiriwa kwa lugha nyingi na wamefaidika watu wengi kutokana na kitabu hiki na tafsiri zake na hiyo yote ni kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu.

Mwisho tunamuomba Mwenyezi Mungu aijalie kazi hii iwe ni kwa ajili yake na kutafuta radhi zake, na amlipe Shekh wetu malipo mema na amlipe Pepo ya juu kabisa, hakika Mwenyezi Mungu ni muweza.

****

**Swali la 1: Ni nini Tauhidi, na ni vipi vigawanyo vyake?**

**Jibu**: Neno Tauhidi katika lugha ya kiarabu, ni kukifanya kitu kuwa kimoja na hilo haliwezi kukamilika isipokuwa kwa kukataa baadhi ya vitu na kuthibitisha baadhi ya vitu, kwa mfano tunasema: haitokamilika Tauhidi ya mtu mpaka kwanza ashuhudie ya kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu Mmoja tu, atakapo kuwa amesema maneno haya atakuwa amekataa ya kuwa hakuna Uungu kwa yeyote isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu peke yake.

Na kukataa huku hakumaanishi kuwa hakuna vinavyo abudiwa visivyo kuwa Mwenyezi Mungu hapana, vipo viabudiwa vingine lakini kuabudiwa kwake sio sahihi.

Ni kama unapo sema: Mtu Fulani amesimama maneno haya hayamaanishi kuwa hakuna mwingine aliye simama bali inawezekana kuna watu wengine wamesimama pia, lakini unapo sema: Hakusimama yeyote, ina maana hakuna mtu yoyote aliye simama, hapa umekataa kusimama kwa yeyote yule na unapo sema: Hakusimama isipokuwa Zaidi hapa unamaanisha hakuna yeyote aliye simama isipokuwa huyu mmoja tu ambaye ni Zaidi, na hii ndiyo Tauhidi, haiwi isipokuwa kwa kukataa vitu na kuthibitisha vitu.

Na Tauhidi katika sheria ya Kiislamu ni: kumpekesha Mwenyezi Mungu katika yale mambo yanayo muhusu.

**Vigawanyo vya Tauhidi.**

**Wanachuoni wamesema Tauhidi imegawanyika katika sehemu tatu nazo ni:**

**1-Tauhidi Rububiyyah** (kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika umbaji, umiliki na upangaji).

**2-Tauhidi Uluhiyyah** (kumpwekesha Mwenyezi Mungu katka ibada). **3-Tauhidi Asmaa wa** Swifaat (kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika majina na sifa zake).

**2-**Wanachuoni wamevipata hivi vigawanyo kwa kuangalia Aya na Hadithi za Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Zilizo zungumzia mas'ala ya Tauhidi ndio wakapata ya kuwa imegawanyika katika sehemu hizo tatu, na tutaeleza kila kigawanyo kwa urefu zaidi.

1-**Aina ya kwanza ni**: Tauhidi Rububuyyah, nayo ni kumpwekesha Mwenyezi Mungu katka uumbaji, umiliki na upangaji, na ufafanuzi wake ni kama ifuatanyo;

Katika kigawanyo hiki kuna vitu vitatu muhimu:

**1-kuhusu kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika uumbaji wake:**

Mwenyezi Mungu peke yake ndiye muumba wa kila kitu, hakuna muumbaji asiyekuwa yeye anasema Mwenyezi Mungu: **[Je kuna muumba mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu ambaye anapekuni riziki kutoka katika mbingu na ardhi, hapana Mola mwingine ila Yeye** ] [Suratul Nahli].

Mwenyezi Mungu peke yake ndie muumba, ameumba kila kitu kisha akakikadiria makadirio yake mpaka vitendo afanyavyo mwanadamu Mwenyezi Mungu ndie aliye viumba kwa ajili hiyo utaona katika ukamilifu wa kuamini makadirio ya Mwenyezi Mungu ni kuamini kuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba matendo ya waja kama alivyo sema Mwenyezi Mungu :[**Na hali Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuumbeni nyinyi na hivyo mnavyo vifanya!**]. [Surat Swaafaati: 96], na hilo ni kwa kuwa matendo ya Mwanadamu ni katika sifa Zake na Mja ni kiumbe wa Mwenyezi Mungu na mwenye kukiumba kitu ndie muumba wa sifa zake.

**Mtu anaweza kuuliza:** tutatofautishaje kati ya uumbaji wa Mwenyezi Mungu na uumbaji ambao unaweza kutokea kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu, kama ilivyo katika maneno yake Mwenyezi Mungu: [**Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji.**] [Suratul Muuminuna: 14], na maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa wale wenye kupiga picha: (**Kutasemwa kuwaambia vitieni roho vile mlivyo viumba**) [Imeipokea Bukhary /2105/na Muslim /2107/].

**Jibu la swali hilo ni kama ifuatavyo:**

Asiekuwa Mwenyezi Mungu haumbi kama anavyo umba Mwenyezi Mungu, kwasababa yeye hawezi kukileta kitu ambacho hakipo na wala hawezi kumfufua aliye kufa bali uumbaji wa asiye kuwa Mwenyezi Mungu unakuwa ni kukibadilisha kitu kutoka kwenye sifa fulani kwenda kwenye sifa nyingine bali ni kile kile kiumbe cha Mwenyezi Mungu ndio amekibadilisha.

Mfano mtu akipiga picha kitu chochote hakuleta kitu kipya bali atakuwa amebadili kitu kukipeleka kwenye kitu kingine, kama vile ambavyo mtu anaweza kubadili udongo akaufanya kama ndege au akaufanya kama picha ya Ngamia.

Na hii ndio tofauti kati ya uumbaji wa Mwenyezi Mungu na uumbaji wa asiye kuwa Mwenyezi Mungu, na kwa ajili hiyo anakuwa Mwenyezi Mungu ni mpweke kwa uumbaji unaomhusu Yeye tu.

**1-Kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika umiliki wake.**

Mwenyezi Mungu peke yake ndiye mmiliki wa kila kitu kama alivyo sema: [**Ametukuka yule ambae katika mikono yake kuna ufalme naye kwa kila kitu ni muweza**] [Suratul Mulku] akasema tena Mwenyezi Mungu: [**Sema ni nani mko-**

**noni mwake umo Ufalme wa kila kitu ,naye ndiye anaye linda wala hakilindwi asicho taka,kama mnajua**] [Suratui Muuminun].

Mwenye Ufalme wa wafalme wote ni Mwenyezi Mungu peke yake ufalme ambao umeenea katika kila kitu na kunasibisha ufalme kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu ni kunasbisha kwa ziada tu, na Mwenyezi Mungu amethibitisha ufalme kwa asiye kuwa Yeye pale alipo sema: **[Isipo kuwa kwa wake zao au wale walio wamiliki katika mikono yao**] [Suratul Muuminun].

Na Aya nyingene nyingi zinazo thibitisha ufalme kwa asiye kwa Mwenyezi Mungu, lakini ufalme huu sio kama ufalme wa Mwenyezi Mungu, kwani ni ufalme ambao una mapungufu na ni ufalme ambao unamipaka hauenei katika kila kitu, kwa mfano, nyumba anayo imiliki Omar haimiliki Zaid na nyumba anayo imiliki Zaidi haimiliki Omar.

Kisha umiliki huu una mipaka, kuwa haruhusiwi mtu kukitumia kile anacho kimiliki isipokuwa atumie kama alivyo amrisha Mwenyezi Mungu, utaona kwa ajili hiyo amekataza Mtume rehma na amani ziwe juu yake! kupoteza mali hovyo, na amesema Mwenyezi Mungu: [**Wala msiwape wasio na akili mali yenu ambayo Mwenyezi Mungu ameijaalia iwe ni kiamu yenu**] [Suratul An Nisaa], na hii ni Ushahidi ya kuwa umiliki wa mwanadau una mapungufu kisha ni wenye mipaka, na hii ni kinyume na Ufalme wa Mwenyezi Mungu kwani ufalme wake ni wenye kuenea kila kitu

usio na mipaka, na Mwenyezi Mungu hufanya analotaka na wala haulizwi kwa lile analo lifanya, lakini Mwanadamu ni mwenye kuulizwa kwa kila anacho kifanya.

**3-Kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika upangiliaji wake**.

Yeye Mwenyezi Mungu ndie anaye pangilia mambo yote ya viumbe wake na yeye ndiye anaye endesha mambo yote katika aridhi na mbinguni amesema Mwenyezi Mungu: **[Fahamuni! Kuumba na amri zake Ametukuka Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe nyote]** [Suratul Araaf].

Na kupangilia huku kumeenea kila kitu hakuna kizuizi wala hakuna mwenya kupinga upangaji wake.

Na kupangilia anako pangilia mwanadamu mambo yake ya kila siku kama kupangilia kuhusu mali zake aziendeshe vipi, na watoto wake awalee vipi na mengineyo, huo ni mpangilio mfinyu na wenye mipaka ni tofauti na mipangilio ya Mwenyezi Mungu ambayo ni mipana na haina mipaka.

**2-Aina ya pili katika aina za Tauhidi ni Tauhiidul Uluuhiyyah**

**(Kumpekesha Mwenyezi Mungu katika Ibada)**

Nayo ni kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika Ibada, mwanadamu asiabudu pamoja na Mwenyezi Mungu kitu kingine na asijikurubishe kwa kitu chochote kama anavyo jikurubisha kwa Mwenyezi Mungu.

Na aina hii ya Tauhidi ndio ambayo wamepotea kwayo wengi katika Washirikina ambao Mtume Rehma na amani ziwe juu yake! aliwapiga vita na kuhalalisha damu zao, mali zao, ardhi yao, nyumba zao na wanawake zao pamoja na watoto wao. Na ndio Tauhidi ambayo Mwenyezi Mungu aliwatuma kwayo Mitume na akashusha Vitabu pamoja na Tauhidi Rububuyya na Tauhidi Al-Asmaa wa Swifaat, lakini zaidi walicho kuwa wanakitibu Mitume kwa watu wao ni Tauhidi hii, ambayo ni Tauhiidul Uluuhiyyah, ili Mwanadamu asimfanyie Ibada yeyote asiye kuwa Mwenyezi Mungu, awe Malaika au Mtume au Walii au Mtu mwema, au kiumbe chochote katika viumbe vya Mwenyezi Mungu, kwasababu Ibada haiswihi kwa kitu chochote isipokuwa Mwenyezi Mungu.

Mwenye kuikosa Tauhidi hii ni Mshirikina, na mwenye kuikubali Tauhidi Rububiyya au akaikubali Tauhidi Al-asmaa wa Swifaat lakini akawa anabudu pamoja na Mwenyezi Mungu kitu kingine hakutomfaa huku kukubali kwake hizo Tauhidi nyingine.

Kwa mfano: Mtu ameikubali Tauhidi Rububiyya na Tauhidi Al-samaa wa Swifaati lakini akawa anakwenda makaburini anawaabudu walioko ndani ya hayo makaburi au anawaomba walioko kwenye hayo makaburi au anachinja mnyama kwa ajili wa kujikurubisha kwa watu hao, mtu huyu atakuwa ni Mshirikina na ni Kafiri, akifa katika hali hiyo atakaa Motoni milele. Amesema Mwenyezi Mungu: [**Anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu,hakika Mwenyezi Mungu atamharamishia pepo, na mahala pake ni Motoni. Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru**] **[**Al-Maida: 72].

Hakika ni kitu kinajulikana kwa kila mwenye kusoma kitabu cha Mwenyezi Mungu ataona ndani yake kuwa wale Washirikina ambao Mtume rehma na amani ziwe juu yake: aliwapiga vita na akahalalisha damu zao, mali zao, na akahalalisha kuwateka wanawake wao, na watoto wao, wote hao walikuwa wanakubali kwamba Mwenyezi Mungu ni Mmoja na Yeye ndiye Mlezi na Muumba wa viumbe vyote, lakini walipo kuwa wanaabudu pamoja na Mwenyezi Mungu vitu vingine, wakawa ni washirikina zikahalalishwa damu zao na mali zao.

**3-Aina ya tatu katika aina za Tauhidi ni Tauhidul- Asmaai wa Swifaat**:

Nayo ni kumpwekesha Mwenyezi Mungu kwa yele majina ambayo ameyaitia Nafsi yake, na akiisifia kwayo Nafsi yake katika Kitabu chake, au kupitia Ulimi wa Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake, na hilo la kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika majina yake na sifa zake linakuwa kwa kuyathibitisha yele yote aliyo yathibitisha Mwenyewe pasina kubadili, wala kupunguza, wala kufananisha. Hapana, na katika aina hii ya Tauhidi, kundi kubwa la Watu limepotea, na ni katika wanao jinasibisha na Uislam.

Kuna miongoni mwao wamechupa mipata katika kuzikataa kuchupa ambako kunawapelekea kutota katika Uislamu, kuna miongoni mwao wapo katikati katika mas'ala haya na wengine wapo karibu na watu wanao fuata mwenendo wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake: lakini njia ya Wema walio tangulia katika Tauhidi hii ni kuwa: Mwenyezi Mungu aitwe kwa majina aliyo jiita Mwenyewe, na asifiwe kwa sifa alizo jisifu Mwenyewe, kama alivyo jiita na kujisifia, pasina kupindisha wala kuondoa jina au sifa, wala kufananisha.

Mfano ya hayo ni: Mwenyezi Mungu amejiita (Al Hayyu Al Qayyuum) yani aliye hai, basi inatupasa sisi kuamini ya kuwa hilo ni jina miongoni mwa majina ya Mwenyezi Mungu, na inatupasa tuamini maana zilizopo kwenye jina hili ambao ni Uhai mka-

milifu ambao haukutanguliwa na kutokuwepo, na wala hauishi.

Na mfano mwingine: Mwenyezi Mungu amejiita (As Samii) Mwenye kusikia, ni lazima kwetu kuamini kuwa hilo ni jina miongoni mwa Majina ya Mwenyezi Mungu na ni lazima tuamini sifa iliyo katika jina hili nayo ni, kusikia nayo ndio maana iliyo katika jina hilo na ndio sifa iliyo katika jina hilo.

Na mfano mwingine: anasema Mwenyezi Mungu: [**Na Mayahudi walisema: Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba. Mikono yao ndiyo iliyo fumba, na wamelaaniwa kwa sababu ya waliyo yasema. Bali mikono yake iwazi. Hutoa apendavyo**] [Al-Maida: 64], katika Aya hii amesema Mwenyezi Mungu: [**Bali mikono yake ipo wazi**]. Amethibitisha Mwenyewe mikono miwili yenye sifa ya ukunjufu, yenye kutoa kwingi, ni lazima kwetu kuamini kuwa Mwenyezi Mungu ana mikono miwili yenye ukunjufu katika kutoa na kuwanemesha waja, lakini haifai kufikiria katika nafsi zetu au kutamka kwa ndimi zetu, kuwa hiyo mikono ya Mwenyezi Mungu labda ipo hivi au hivi, na wala hatuifananishi na mikono ya viumbe wake, kwa kuwa Mwenyezi Mungu anasema: **[Hapana kitu kamamfano wake. Naye ni Mwenye kusikianMwenye kuona]**, na anasema Mwenyezi Mungu: [**Sema: Mola Mlezi wangu ameharimisha mambo machafu ya dhaahiri na ya siri, na dhambi, na uasi bila ya haki, na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na asicho kiletea uthibitisho, na kumzulia Mwenyezi Mungu msiyo yajua**] [Suratul Al-Araaf: 33], na anasema Mwenyezi Mungu: [**Wala usiyafuate usiyo na ujuzi nayo. Hakika masikio, na macho, na moyo - hivyo vyote vitasailiwa**] (Suratul Al Israa: 36), yeyote atakae fananisha hii mikono miwili na mikono ya viumbe hakika amekadhibisha maneno yake Mwe-

nyezi Mungu pale alipo sema: [**Hapana kitu kama mfano wake**] [Suratul Shuuraa: 11], na atakuwa amemuasi Mwenyezi Mungu katika maneno yake [**Basi msimpigie Mwenyezi Mungu mifano**] [Suratul Annahal: 71].

Tutoe mifano mingine ya sifa za Mwenyezi Mungu: Kulingana kwa Mwenyezi Mungu katika Arshi yake, hakika Mwenyezi Mungu amelithibitisha hilo katika nafsi yake, kuwa amelingana sawa katika Arshi juu ya mbingu saba, sehemu nyingi katika kitabu chake kitukufu na sehemu zote ametumia neno (kulingana) na akatumia neno (Juu ya Arshi) na tutakapo yarejea maneno hayo katika Lugha ya Kiarabu tunalikuta linapotumika na neno (Alaa) halimaanishi ipokuwa ni kuinuka na kuwa juu, kwa hiyo inakuwa maana ya maneno yake Mwenyezi Mungu [**Arahamani, Mwingi wa Rehema, aliye tawala juu ya kiti cha Enzi**] [Suratul Twaha: 5]. Na mfano wa Aya nyingine kama hii zote zina thibitisha kuwa, Mwenyezi Mungu yupo juu ya Arshi yake kukaa maalumu sio kukaa kama wanavyo kaa viumbe wengine, bali Mwenyezi Mungu amekaa kukaa kunako lingana na Yeye.

Hakika amekosea kukosea kukubwa Yule atakae sema: Maana ya (Istawaa alaa Arshi) ina maana ya (Istaulaa), kwa sababu kusema hivyo ni kupindisha maneno ya Mwenyezi Mungu, na pia ni kwenda kinyume na vile walivyo kubaliana Maswahaba radhi za Mwenyezi Mungu ziwashukie na wale walio wafuata kwa kufanya matendo mema bali neno lenyewe katika lugha ya Kiarabu halina maana isipokuwa ni kuwa juu, na maana hiyo ndio yenye kuendana na maana katika lugha ya Kiarabu yani yupo

juu ya Arshi kuwa juu maalumu kwa ajili yake ambako kunalingana na Mwenyewe Mwenyezi Mungu, na mwenye kutafsiri kwa maana ya (Istaulaa) atakuwa amebadili maneno kutokana na maana yake halisi pia atakuwa amekwenda kinyume na ilivyo fahamisha Qur`an tukufu.

Kisha wema walio tangulia wametafsiri kwa maana hiyo na haikupokelewa kutoka kwao isipokuwa tafsiri hiyo, na linapo kuja neni katika Qur'an au Sunnah na haikupokelewa kutoka kwa wema walio tangulia tafsiri inayo kwenda kinyume na maana yake dhahiri (iliyo wazi) basi wao hubakiza neno hilo katika asili yake, kisha hufuata vile inavyo amrisha ile Aya.

Atakapo sema Mtu je kuna maneno ya wazi kutoka kwa wema walio tangulia ambao wametafsiri neno ( istawa) kwa maana ya Alaa?

Tunasema: ndio, limepokelewa hilo kwao Mwenyezi Mungu awarehemu na hata kama tutajalia kuwa hakuna Tafsiri ya wazi kutoka kwao hakika asili ya neno lenyewe katika Qur'an na Sunnah inafahamisha kwa maana hiyo, na itabaki katika maana hiyo muda wa kwamba hakuna tafsiri nyingine isiyo kuwa hiyo.

Mambo ambayo ni lazima na ni batili kwa yule mwenye kutafsiri Istiwaa kwa maana ya Istilaa ni:

**1-** Kuwa Arshi kabla ya kuumbwa mbingu na Aridhi sio milki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwani Mwenyezi Mungu anasema:

[**Hakika Mola wenu ni Mwenyezi Mungu aliye ziumba mbingu na Ardhi katika siku sita. kisha akatawala juu ya kiti cha enzi**] [Suratul Al-Araaf: 54] kutokana na Aya hii hawi ni mustaulia katika Arshi kabla ya kuumba mbingu na Ardhi.

**2-** Inakuwa maana ya maneno yetu kuwa: kulingana sawa kwa Mwenyezi Mungu Katika Arshi na kulingana sawa kwa kitu chochote katika viumbe wake kupo sawa, na maana hii bila shaka ni batili kabisa haifai kuambiwa Alla Mtukufu.

**3**-Na tafsiri hiyo ni kutafsiri maneno kinyume, tofauti na maana yake halisi.

**4-** Na kutafsiri kwa tafsiri hiyo ni kwenda kinyume na maafikiano ya wema walio tangulia radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao.

Kwa ufupi katika Tauhidi hii ya majina ya Mwenyezi Mungu pamoja na sifa zake inatupasa sisi kuthibitisha yale yote aliyo yathibitisha katika Nafsi Yake au amethibitisha Mtume wake katika majina na sifa pasina kupindisha wala kuziacha wala kuzifananisha.

****

**Swali la 2: Ni Shirki ipi ambayo washirikina waliifanya mpaka akatumwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake?**

**Jibu:** Ama Shirki waloifanya Washirikina mpaka akatumwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwao, sio Shirki katika Rububuyya (Uumbaji) kwa sababu Qur`an inaonesha kuwa walikuwa wakifanya Ushirikina katika Ibada tu.

Ama katika Rububiyya walikuwa wakiamini kuwa Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mlezi wa viumbe wote, na kwamba Yeye ni mwenye kujibu dua za wenye matatizo, na Yeye Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuondoa mabaya na mengine Yasiyo kuwa hayo ambayo ameyataja Mwenyezi Mungu kuwa walikuwa wakikubali kuwa Mwenyezi Mungu peke yake ndiye mwenye kufanya hayo.

Lakini wao washirikina walikuwa wakiabudu pamoja na Mwenyezi Mungu kitu kingine, na hiyo ni Shirki inayo mtoa Mtu katika Uislamu, kwasababu Tauhidi ni kukifanya kitu kuwa kimoja, na Mwenyezi Mungu Mtukufu Yeye ni lazima apwekeshwe, na haki hii inagawanyika katika vigawanyo vitatu:

1- Haki ya Ufalme.

**2**- Haki ya Ibada.

**3**- Haki katika Majina yake na Sifa zake.

Na kwa ajili hiyo Wanachuoni wakaigawa Tauhidi katika vigawanyo vitatu; Tauhidi ya Uumbaji, Tauhidi ya Ibada na Tauhidi katika Majina yake na Sifa zake.

Na washirikina walimshirikisha Mwenyezi Mungu katika Tauhidi ya Ibada, ambapo walikuwa wakimuabudu Mwenyezi Mungu pamoja na vitu vingine na amesema Mwenyezi Mungu: [**Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na kitu chochote**] [Suratu An Nisaa: 36], yaani msimshirikishe katika Ibada yake.

Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Kwani anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu,hakika Mwenyezi Mungu atamharamishia pepo,na mahala pake ni Motoni.Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru**] [Suratul Maaida: 72] na amesema tena Mwenyezi Mungu**: [Hakika Mwenyezi Mungu hamsamehi (dhambi ya) kushirikishwa, na husamehe mengineyo kwa amtakae**] [Suratu An Nisaa: 48] na amesema tena Mwenyezi Mungu: [**Na Mola wenu anasema: Niomben nitaku-Jibuni. Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu mimi wataingia Jahannamu wadhalilike**] [Suratul Ghafir: 60].

Na amesema Mwenyezi Mungu katika Surat  Ikhlas:

**1-** Sema Enyi makafiri.

2- Siabudu mnacho kiabudu.

**3-** Wala nyinyi hamuabudu ninaye muabudu.

**4-** Wala sitaabudu mnacho abudu.

**5-**Wala nyinyi hamuabudu ninaye muabudu.

**6**- Nyinyi mna dini yenu, nami nina Dini yangu.

Na maneno yangu kuwa katika Suratul Ikhlas: Nakusudia Ikhlasi katika matendo, hii ni Suratul Ikhlas ya Matendo japo inaitwa Suratul Kafiruun lakini kwa hakika ni Suratul Iklas katika matendo, kama vile ambavyo Suratul (Qulhuwa Allah ahadu) inaitwa Suratul Ikhasi katika Aqida.

****

**Swali la 3: Ni ipi misingi ya Ahalu Sunnahh Waljamaa katika Tauhidi na mambo mengine katika mambo ya Dini?**

**Jibu:** Misingi ya Ahalu Sunnah Waljamaa katika Tauhidi na mambo mengine katika mambo ya Dini, ni kushikamana kikamilifu na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume rehma na amani ziwe juu yake! na yale walokuwa nayo Makhalifa wanne waongofu katika uongofu na Sunnahh, amesema Mwenyezi Mungu: [**Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi,Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakusameheni madhambi yenu**][Suratul Al-Imran: 31] Na amesema tena Mwenyezi Mungu: [**Mwenye kumtii Mtume basi kwa hakika ndio amemtii Mwenyezi Mungu.Na ane kengeuka ,basi sisi hatukutuma wewe uwe ni mlinzi wao**] [Suratul An- Nisaa: 80] na amesema Mwenyezi Mungu: [**Na anacho kupeni Mtume, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho**] [Suratul Al- Hashir: 7], na hii ni katika kugawana ngawira (mali zinazo patikana kwenye vita ) inapo kuwa katika mambo ya kisheria ni bora zaidi; kwa sababu :Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akuwahutubia watu siku ya Ijumaa Anasema: (**Ama baada ya hayo, hakika maneno yaliyo bora ni maneno ya Mwenyezi Mungu, na uongofu ulio bora kabisa ni uongofu wa Muhammad (rehma na amani ziwe juu yake), na katika mambo yaliyo mabaya kabisa ni uzushi, hakika kila jambo lenye kuzuka ni Bidaa,na kila bidaa ni upotevu,na kila upotevu ni Motoni**) [Annasaai /1578].

Na amesema tena Mtume merahma na amani ziwe juu yake: ((**Shikamaneni na Sunnahh zangu, na Sunnahh za Makhalifa wangu waongofu baada yangu, shikamaneni nazo, zishikeni kwa meno ya Magego, na tahadharini na mambo ya uzushi, kwani hakika kila chenye kuzuka ni Bidaa, na kila Bidaa ni Upotevu**)) [Abuu Daudi /460, Ibun Maajah /43]. Na ushahidi wa hayo ni mwingi.

Njia ya Ahalu Sunnahh Wal Jamaa ni kushikamana kikamilifu na Kitabu Cha Mwenyezi Mungu, na Sunnahh za Mtume rehma na mani ziwe ju yake na Suna za Makhalifa wake waongofu walokuja baada yake, na hiyo ni kwa sababu wao husimamisha Dini kikamilifu na wala hawawagawanyi watu; na wanafanya hivyo kufuata amri ya Mwenyezi Mungu pale alipo sema: [**Amekuamrisheni Dini ile ile aliyo muusia Nuhu na tuliyo kufunulia wewe,na tuliyo muusia Ibrahim na Musa na Isa,kwamba kamateni dini wala msifarikiane**] [Suratul Ash-Shuura: 13], na kwao hata kama itatokea tofauti kati yao hutokea katika mambo ambayo wameruhusiwa kujitahidi ndani yake, na ikhitilafu hizo hazipelekei kutofautiana nyoyo zao, bali utawakuta ni wenye kushikamana na kupendana, japo kumetokea tofauti kati yao kwa njia ya kujitahidi.

****

**Swali la 4: Ni kina nani hao Ahalu Sunnahh Waljamaa?**

**Jibu:** Ahalu Sunnahh Wal Jamaa ni wale ambao wameshikamana na Sunnahh, na wakakusanyika katika kuifuata hiyo Sunnahh, na hawakufuata mambo mengine yasiyo ya Kisunnah, sio katika mambo ya kiitikadi wala mambo ya kimatendo, kwa ajili hiyo wameitwa Ahalu Sunnahh, kwa sababu wao wameshikamana nayo.

Na wameitwa Al Jamaa; kwasababu wao wamekusanyika katika kuifuata hiyo Sunnahh.

Ukiwaangalia vizuri watu wa Bidaa kwa mazingatio, utawaona kuwa ni wenye kutofautiana katika yale wanayo yafuata katika mambo ya kiitikadi na kimatendo, na hilo ni jambo linalo fahamisha kuwa wapo mbali na Sunnahh, kwa yale walio ya zusha katika mambo ya Bidaa.

****

**Swali la 5: Ametuhabarisha Mtume rehma na amani ziwe ju yake juu ya kutofautiana Umma wake baada ya kufa kwake, tuna kuomba Sheikh utubainishie jambo hili**

**Jibu:** Ametuhabarisha mtume rehma na amani ziwe ju yake! katika Hadithi sahihi iliyo pokelewa kutoka kwake [Ilio pokelea na Abu Daud 4598, Tirmidhi 2640 na Ibnu Maja 3991]: Kuwa Mayahudi waligawanyika makundi sabini na moja, na Manaswara waligawanyika makundi sabini na mbili, na Ummah huu utagawanyika makundi sabini na tatu, na Makundi hayo yote yataingia Motoni isipokuwa kundi moja, nalo ni lile litakalo kuwa ni lenye kufuata yale alikuwa nayo Mtume rehama na amani ziwe ju yake!na Maswahaba zake, na hili kundi ndilo kundi lenye kuongoka, ambalo limeongoka katika Dunia na mambo ya Uzushi, na litaokoka kesho Akhera na Moto, nalo ni kundi lililo nusuriwa

mpaka siku ya Kiama, na kundi hili halitoacha kuwa ni kundi lenye kudhihiri na kusimama mpaka siku ya Kiyama kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukukufu.

Na haya makundi sabini na tatu, ambapo moja kati yake ndio kundi la haki, na yaliyo baki ni batili, wamejaribu baadhi ya watu kuyahesabu, na wakawagawa watu wa Bidaa makundi matano, na wakaweka katika kila kundi matawi yake, ili kufikia katika ile idadi alio isema Mtume rahma na amani ziwe jun  yake, wakaona baadhi ya watu kilicho bora ni kuacha kuhesabu, kwa kuwa makundi haya sio haya tu katika walio potea, bali kuna watu wamepotea kupotea kuliko kukumbwa sana kuliko ilivyo kuwa huko nyuma, na wakazusha mambo mengine baada ya kuhesabiwa haya makundi sabini na tatu, na wakasema: Hakika hii idadi haiishi na wala haiwezekani kujua kuisha kwake, isipokuwa mwisho wa zama hizi wakati wa kusimama Kiyama, na kilicho bora kwetu ni kufanya kama alivyo fanya Mtume rehma na amani ziwe ju yake  tunasema: Hakika Umma huu utagawanyika makundi sabini na tatu, yote yataingia motoni isipokuwa kundi moja, kisha tunasema: Kila mwenye kwenda kinyume na yale alokuwa nayo Mtume na Maswahaba zake, basi huyo ataingia katika hayo makundi, anaweza kuwa Mtume rehma na amani ziwe ju yake ameashiria kwenye misingi na hatukujua katika hiyo kwa sasa isipokuwa kumi, na anaweza kuwa ameashiria katika misingi ambayo ina matawi ndani yake kama walivyo sema baadhi ya watu, Mwenyezi Mungu ndio mjuzi zaidi.

****

**Swali la 6: Niyapi mambo muhimu na maalumu katika kundi hili lenye kuokoka? Na je kupungua kitu katika hayo mambo kunamtoa mtu katika kundi hilo?**

**Jibu:** Mambo muhimu na maalumu katika kundi hili lenye kuokoka ni: kushikamana na yale alokuwa nayo Mtume rehma na amani ziwe ju yake! katika mambo ya Itikadi, na Ibada, na Tabia, na kushirikiana na watu, hayo mambo manne utayakuta katika kundi hili lenye uongofu ni yenye kudhihiri:

Ama katika Itikadi unalikuta kundi hilo limeshikamana na yale yaliyo elekezwa katika kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnahh za Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake, ikiwa ni pamoja na kuwa na Tauhidi Uluhiyyah, na Tauhidi Rububiyyah, na Tauhidul Asmaai Wa Swifaati.

Na katika Ibada, utalikuta kundi hili ni lenye kushikamana na Ibada kushikamana kikweli kweli, kama alivyo kuwa akishikamana Mtume rehma na aziwe ju yake na Ibada katika aina zake, sifa zake, wakati wake, sehemu zake na sababu zake, hutoweza kukuta kutoka kwao mambo ya Uzushi katika Dini, bali wao ni wenye kuwa na adabu mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu pamoja na Mtume wake rehma na amani ziwe ju yake! Hawatangulizi mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake katika kuingiza kitu katika Ibada ambacho hakuruhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na katika Tabia, utawakuta ni wenye tofauti na wengine, kwa tabia nzuri, kama vile kuwapendelea Waislamu kheri, na kuwa wakunjufu wa nyoyo, na kuwa na uso wenye bashasha, na ni wenye maneno mazuri na ukarimu, na ni wenye Ushujaa, na mengine mengi katika mambo ya Tabia nzuri.

Na katika kushirikiana na watu, utawakuta wanashirikiana na watu kwa ukweli na uwazi, kama vile alivyo ashiria Mtume rehma na amani ziwe juyake katika maneno yake: (**Wawili wenye kuuziana ni wenye khiyari muda wa kwamba bado hawaja achana, na ikiwa wote wawili watasema kweli na wakaweka wazi biashara yao, watabarikiwa katika biashara yao, na iwapo watasema uongo, na wakafichiana aibu za biashara yao, itatoweka baraka katika biashara yao**) [Bukhar /2079, Muslim /1532]. Na upungufu katika mambo haya hakumtoi mtu katika kundi hili, lakini kila mwenye kufanya kitu ana daraja yake, na upungufu katika Tauhidi huenda ukamtoa Mtu katika kundi hili la wenye kuokoka, mfano upungu katika Ikhlasi, na vile vile katika Bidaa, huenda akafanya Bidaa ikamtoa katika kundi hili la wenye kuokoka.

Ama katika mambo ya tabia na Ushirikiano haumtoi mtu kwenye kundi, japo kuwa hiyo inapunguza daraja yake.

Na tunaweza kuhitaji kuweka wazi zaidi mambo ya tabiya, hakika katika mambo muhimu katika tabia ni watu kukusanyika katika neno moja, na kuafikiana katika haki ambayo ametuusia

Mwenyezi Mungu katika maneno yake pale alipo sema: [**Amekuamrisheni Dini ile ile aliyo muusia Nuhu na tulio kufunulia wewe, na tulio wausia, Ibrahimu na Musa na Isa, kwamba kamateni Dini wala wala msifarikiane**] [Suratul Ash- Shura: 13] na akatupa habari kuwa wale ambao wamefarikisha watu katika Dini yao na wakawa makundi makundi, kuwa Mtume rehma na amani ziwe ju yake yupo mbali nao akasema Mwenyezi Mungu: [**Hakika wale ambao wameigawa Dini yao na wakawa makundi makundi,wewe si katika wao kwa chochote**] [Suratul Al-Anaam /159].

Watu kuafikiana katika neno moja, na kuziunganisha nyoyo ni katika vitu muhimu maalumu katika kikundi hiki chenye kuokoka, na kama itatokea kutofautiana katika kitu ambacho ni cha kujitahidi ambacho watu wameruhusiwa kutoa juhudi zao, hawawekeani wao kwa wao vifundo, wala uadui, wala kuchukiana, bali huitakidi kuwa wao ni ndugu, mpaka mmoja wao anaweza kuswali nyuma ya Mtu anaeona hatawadhi kwa udhu wake, mfano: Mmoja katika wao anaweza kuswali nyuma ya mtu anaekula nyama ya Ngamia, yani Imamu anaona kula nyama ya Ngamia hakutengui Udhu, na maamuma anaona kula nyama ya Ngamia kunatengua Udhu, kila mmoja anaona Swala nyuma ya Mwenzake inasihi japo wametofautiana katika hilo, yote hiyo ni kwa kuwa kila mmoja anaona kuwa khilafu imetokea katika kitu cha jitihada, sio katika mambo yenye khilafu ya kweli, kwa sababu kila mmoja amefuata kile anacho paswa kufuata kutokana na ushahidi, wanaona ya kuwa watakapo tofautiana na ndugu yake katika kitendo ambacho amefuata ushahidi, hiyo kwa hakika ni kama wameafikiana, kwa sababu wao wote hulingania katika kufuata ushahidi popote

watakapo kuwa, atakapo tofautiana nao kwa ajili ya kufuata ushahidi alionao, basi yeye kwa hakika atakuwa ameafikiana nae, kwa sababu yeye anafuata kwa kile kinacho linginiwa, na wanaongoka kwa kuhukumiwa na kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah za Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Na wala halifichiki kwa watu wengi wenye elimu, kile kilicho tokea baina ya Maswahaba, katika mfano wa mambo hayo, hata wakati wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake yalitokea lakini hawakuchukina, kwa hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu alipo rejea kutoka katika vita ya Ahzab, akamjia Jibril, na akamuashiria kuwa atoke kwenda kwa banii Quraydhwa ambao walivunja ahadi, Mtume rehma na amani ziwe ju yake akawahimiza Maswahaba zake akasema: (**Asiswali mmoja wenu swala ya Alasili isipokuwa awe amefika bani Quraydhwa**) [Bukhar 946/ na Muslim 1770].

Wakatoka Maswahaba kutoka Madina kuelekea banii Qurayidhwa, ikawakuta Swala ya Alasiri wakiwa njiani, kuna walio chelewesha swala mpaka walipofika banii Quraydhwa, ukiwa umesha pita wakati wake kwasababu Mtume amesema: (**Asiswali mmoja wenu swala ya Asr isipokuwa awe amefika bani Quraydhwa**). Kuna miongoni mwao walio swali katika wakati wake, na wakasema : Hakika Mtume rehma na amani ziwe ju yake: alikusudia tufanye haraka katika kutoka, na wala hakukusudia tucheleweshe Swala kutoka katika wakati wake- na hawa ndio walio sahihi- lakini pamoja na hilo Mtume rehma na amani ziwe ju yake: hakumkemea yoyote kati ya makundi hayo mawili, na wala kundi moja hawakuwachukia wala kufanya uadui katika kundi lingine, kwa sababu ya tofauti zao katika kuyaelewa maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake:

Kwa ajili hiyo naona kuwa ni wajibu juu ya Waislam ambao wanajinasibisha na Sunnah wawe ni kitu kimoja, na wala isitokee kati yao Makundi, huyu anajinasibisha na kundi hili, na yule anajinasibisha na kundi lile, na watatu anajinasibisha na kundi lingine na mfano wa hayo kiasi kwamba husababisha kutupiana maneno makali, na kufanyiana uadui, na kuchukiana, kwa sababu ya ikhtilafu iliyotokea ni kwa kujitahidi, na wala haina haja ya kuweka wazi ni kundi gani, lakini mwenye akili anafahamu na inambainikia kila kitu.

Ninaona kuwa ni wajibu kwa Ahlusunah Waljama, kushikamana hata kama wakitofautiana kwa yale wanayo tofautina, hakika katika jambo hili kuna upana na ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu, na muhimu ni kuunganisha nyoyo na kuungana katika neno moja, na wala hakuna shaka kuwa maadui wa Uislam wanapenda Waislam watofautiane, sawa wawe ni Madui wanao dhihirisha uadui wao, au wale ambao wanadhihirisha mapenzi kwa Waislam, na ukweli wa mambo wao hawapo hivyo.

Ni wajibu kwetu tujipambe kwa sifa hizo ambazo ni sifa za kundi lililo okoka, nayo ni kujipamba kunako endana na mambo yetu.

****

**Swali la 7: Ni nini makusudio ya mtu kati na kati katika Dini?**

**Jibu:** Mtu kuwa kati na kati katika Dini, ni kwamba asizidishe Mwanadamu akuchupa mipaka aliyoiweka Mwenyezi Mungu, na wala asipunguze ndani yake mpaka akavuka mipaka alomuwekea Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na usawa katika Dini: Ni kushikamana na Sera ya Mtume rehma na amani ziwe ju yake!

Na kuchupa mipaka: Ni kuvuka mipaka au kupunguza, pale alipo kuwekea Mwenyezi Mungu.

Mfano wa kuvuka mipaka katika Ibada, ni Mtu kusema: Mimi nataka kuswali Usiku mzima na sito lala kamwe, na nafanya hivi kwa sababu Swala ni katika Ibada zilizo bora kabisa, kwa hiyo nataka kuhuisha usiku mzima. Tutasema kumwambia wewe umepetuka mipaka katika dini ya Mwenyezi Mungu, na kufanya kwake hivyo hayupo sahihi, na lilitokea tukio kama hili wakati wa Mtume rehma na amani ziwe ju yake walikuja Watu kwa Mtume rehma na amani ziwe ju yake wakasema baadhi yao: Mimi nitasimama usiku mzima kwa ajili ya kuswali na wala sitolala kamwe, na mwingine akasema: Mimi nitafunga na wala sitoacha kufunga hata siku moja, na akasema wa tatu: Mimi sitooa wanawake kabisa, nita ishi hivi hivi, nitafanya Ibada tu, likamfikia hilo Mtume rehma na amani ziwe juu yake! akasema: (**Wana nini watu wanasema hivi na hivi? Mimi ninafunga na ninafungua, na ninasimama**

**kuswali na pia ninalala, na ninaoa wanawake, Mwenye kuiacha Sunnah yangu huyo sio katika mimi**) [Ameipokea Bukhar /5063 na Muslim /1401].

Watu hawa walikuwa wamepetuka mipaka katika Dini, wamezidisha kiasi alicho amrisha Mwenyezi Mungu, walipo semaa hivyo Mtume rehma na amani ziwe ju yake akawaambia Mwenye kufanya hivyo yupo mbali na Mimi, amefanya hivyo kwa sababu wao wameiacha Sunnah ya Mtume rehma na amani ziwe ju yake! ambayo ni, kufunga na kufungua, na kuoa wanawake.

Ama Mwenye kupunguza katika Ibada, ni yule anae sema: Mimi sina haja na Sunnah, mimi sitafanya Sunnah yoyote nitafanya faradhi tu. Na mwenye kupunguza katika faradhi, pia huyu ni mwenye kupunguza.

Ama mwenye kufanya usawa katika Ibada, Ni yule ambaye anafanya Ibada kwa kufuata mwenendo wa Mtume rehma na amani ziwe ju yake na Makhalifa wake waongofu, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao.

**Na mfano mwingine**: Kulikuwa na watu watatu, mbele yao kulikuwa na Mtu muovu, mmoja wao akasema: Mimi simsalimii huyo muovu, na ninamhama kabisa, na kujiweka mbali nae na wala sito msemesha.

Na wapili akasema: Mimi nitatembea na huyu muovu, na nitamsalimia, na nitakuwa na bashasha katika uso wake, na nitamuita kwangu, na iwapo ataniita nitaitikia wito wake, huyu kwangu ni kama Mtu mwema.

Akasema watatu: Huyu Muovu namchukia kwa Uovu wake, na ninampenda kwa Imani yake, na wala sito mhama isipokuwa ikiwa kumhama kwake ni sababu ya yeye kuwa mwema, na ikiwa kuwa naye ni sababu ya kuzidisha uovu wake basi nitamhama. Tunasema: Huyu wa kwaza amezidisha katika kumchukia, na wapili amepunguza, na watatu yupo kati na kati.

Na hivi ndivyo tunavyo sema katika Ibada zote na mahusiano mengine: watu wapo hivyo, kuna wenye kuzidisha, wenye kupunguza, na walio kati kwa kati.

**Mfano wa tatu**: Mtu amekuwa kama mtumwa kwa mke wake, anamuongoza popote atakapo, hamkatazi mke wake kufanya uovu wala hamuamrishi kufanya wema, mwanamke ameimiliki akili yake imekuwa kama ndio miguu anayo simamia.

Na mtu mwingine, anamnyanyasa, anamfanyia kibri, na kujikweza kwa mke wake, na hamjali kwa kitu chochote, mke wake kwake hana thamani zaidi ya kijakazi.

Na mtu wa tatu, yupo kati na kati, anamfanyia mke wake kama alivyo amrisha Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake rehma na amani ziwe ju yake: kama alivyo sema Mwenyezi Mungu Mtukufu**: [Nao wanawake wanayo haki kwa Sharia kama ile haki iliyo juu yao**] [ Suratul Al-Baqara/ 228], na amesema Mtume rehma na amani ziwe ju yake: (**Asimuache Muumini Mwanaume Muumini Mwanamke, iwapo atachukia kwake tabia falani, atapenda tabia nyingine**) [ Ameipokea Muslim /1469 ].

Huyu Mtu wa mwisho, yupo kati na kati, na wa pili amepetuka mipaka, na watatu amepunguza, na tumia kipimo hicho katika matendo yote na Ibada zote.

****

**Swali la 8: Ni ipi Maana ya Imani kwa Ahlu Sunnah Waljamaa? Na je inazidi na kupungua?**

**Jibu:** Imani kwa Ahlu Sunnahh Waljamaa ni: (Kukiri kwa Moyo na kutamka kwa Ulimi na kufanya kwa vitendo) nayo inakusanya mambo matatu:

**1-**Kukiri kwa Moyo.

**2**-Kutamka kwa Ulimi.

**3-**Kufanya  kwa Vitendo.

Imani itakapo kuwa hivyo basi itazidi na kupungua, na hilo ni kwasababu kukiri kwa Moyo kunazidiana, kwani kukiri  kwa kusikia jambo ni tofauti na kukiri kwa kuliona mwenyewe kwa macho, na kukiri kwa Mtu mmoja sio kama kukiri kwa watu wawili, na mifano mingine, kwa ajili hiyo amesema Ibrahim Amani ya Mwenyezi Mungu iwe pamoja nae: [**Na alipo sema Ibrahim: Mola wangu Mlezi, nionyeshe vipi unavyo fufua wafu. Mwenyezi Mungu akasema: Kwani huamini? Akasema: hapana lakini ili moyo wangu utulie**] [Suratul  Al-Baqara /260].

Imani huwa inazidi kwa moyo kukiri na kutulia, na Mwanadamu atapata huo utulivu katika nafsi yake kwa kuhudhuria vikao vya kutajwa Mwenyezi Mungu, na mawaidha ya Pepo na ya Moto mpaka mtu atahisi kama anaviona vitu hivyo kwa macho yake, na wakati kutakapo patikana kughafilika, na mtu akawa si mwenye kuhudhuria kwenye vikao hivi, inapungua yakini hii katika moyo wake. Vile vile imani huongezeka kwa maneno, kwani kumtaja Mwenyezi Mungu, mara kumi sio sawa na alomtaja mara mia moja, wapili amemzidi wa kwanza.

Na hivo hivo mwenye kufanya Ibada kwa njia iliyo kamili, inakuwa imani yake juu zaidi ya yule alofanya kwa njia ya upungufu.

Hivo hivo katika matendo, hakika mwanadamu anapo fanya matendo kwa vitendo zaidi ya mwenzake imani yake inaongezeka zaidi kuliko alofanya matendo kwa upungufu, na hilo limekuja katika Qur`an na Sunnah: Nakusudia kuzidi kwa imani na kupungua, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Na hatukujalia walinzi wa huo moto isipokuwa ni Malaika wala hatukujalia idadi yao isipokuwa mtihani kwa wale waliokufuru, ili wawe na uhakika waliopewa vitabu,na walioamini wazidi katika imani yao**] [ Suratui Al- Mudathir /31] na akasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Na inapo teremshwa Sura wapo miongoni mwao wasemao: Ni nani miongoni mwenu Sura hii imemzidishia Imani? Ama wale walio amini inawazidishia Imani, nao wanafurahi /124 Ama wale wenye maradhi katika nyoyo zao, basi inawazidishia uchafu juu ya uchafu wao; na wanakufa hali ni makafiri**] [Suratul Atawba /125/] .

**Lakini ni zipi sababu za Imani kuzidi?**

Kuzidi kwa Imani kuna sababu;

**1**- Kumjua Mwenyezi Mungu, kwa majina yake na sifa zake, hakika Mwanadamu kila anapo zidisha kumjua Mwenyezi Mungu, kwa majina yake na sifa zake, bila shaka Imani yake huongezeka, kwasababu hiyo utakuta kuna watu wenye elimu ambao wanaya-

jua majina ya Mwenyezi Mungu na sifa zake, majina hayo na sifa hizo hawazijui watu wengine, utawaona wao wana imani kuliko wale wasiyo yajua majina hayo na sifa hizo.

**2**- Kuangalia na kutafakari Ushahidi wa kuwepo Mwenyezi Mungu wa Kidunia na Kisheria, hakika Mwanadamu kila anapo angalia ushahidi wa kuwepo Mwenyezi Mungu katika Dunia, ambao ni viumbe basi imani yake huzidi amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Na katika Ardhi zipo Ishara kwa wenye yakini./20/ Na katika nafsi zenu- Je Hamuoni?**] [Suratul Adhariyat /21/], na Aya zenye kufahamisha juu ya hilo ni nyingi, nakusudia zinazo fahamisha kuwa Mwanadamu anapo angalia na kufikiria viumbe wa Mwenyezi Mungu vilivyopo kwenye Dunia hii Imani huongezeka.

**3**- Kuzidisha utiifu kwa Mwenyezi Mungu, Mwanadamu kila anapo zidisha kumtii Mwenyezi Mungu, ndivyo Imani yake inavyo ongezeka, ni sawa utiifu huo uwe ni wa maneno au wa vitendo, maneno kama kumtaja Mwenyezi Mungu, na vitendo kama Swala, Swaumu na Hijja, yote hayo yanazidisha Imani.

**Ama sababu za kupunguza Imani, ni kinyume na hizo tulizo zitaja ambazo ni:**

**1**-Kuto kujua majina ya Mwenyezi Mungu na sifa zake, kuna wajibisha kupunguza Imani, kwasababu Mwanadamu atakapo kuwa ni mchache wa kuyajua Majina ya Mwenyezi Mungu, Imani yake hupungua.

**2-**Kutokufikiria juu ya alama za kuwepo Mwenyezi Mungu za Kidunia na Kisheria, kwasababu kutofikiria Alama hizo kunasababisha kupungua kwa Imani, au kama isipopungua basi itabaki hapo hapo bila kuzidi.

**3**-Kufanya Maovu, hakika kufanya Maovu kuna athari kubwa sana katika Moyo, na kwa ajili hiyo amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (**Hazini mzinifu, wakati anapo zini hali ya kuwa ni Muumini**) [Ameipokea Bukhar/ 2475 na Muslimu / 57].

**4**-Kuto kumtii Mwenyezi Mungu, kwani kuacha twaa ni sababu ya kupungua imani, lakini ikiwa utiifu alouacha ni wajibu, na ameacha bila udhuru wowote, basi imani itapungua, na atalaumiwa kwa kuacha huo utiifu na ataadhibiwa, na ikiwa sio wajibu au ni wajibu lakini ameiacha kwa dharura, basi itapungaza imani lakini hatalaumiwa, na kwa ajili hiyo amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Wanawake ni wapungufu wa akili na dini, na akatoa sababu ya upungufu katika dini ni kwasababu anapo kuwa katika hedhi haruhusiwi kuswali wala kufunga, pamoja na kwamba hawalaumiwi kwa kuacha kwao Swala na Swaumu bali wameamrishwa kuacha hizo ibada, lakini alipopitwa na kitendo anacho kifanya na mwanaume, ndiyo akawa ni mpungufu wa akili katika upande huo.

****

**Swali la 9: Ni vipi tunakusanya kati ya Hadithi ya Jibril ambayo Mtume rehma na amani ziwe juu yake, alitafsiri Imani kuwa ni (Kumuamini Mwenyezi Mungu,na Malaika wake, na Vitabu vyake,na Mitume wake, na siku ya mwisho, na kuamini Qadar kheri zake na Shari zake) [Apokea Muslimu /8 na Hadithi ya wageni wa Abdul-Qaysi ambao Mtume rehma na amani ziwe juu yake: alitafsiri Imani kuwa ni (Kushuhudia ya kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mmoja hana Mshirika, na kusimamisha Swala, na kutoa Zaka, na kutoa asilimia tano ya Ngawira) [Ameipokea Bukhari /53, na Muslimu /17].**

**Jibu**: Kabla ya kujibu swali hili napenda kusema: Hakika kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah za Mtume rehma na amani ziwe juu yake, haziwezi kupingana milele, na wala hakuna katika Qur'an aya zinazo pingana zenyewe kwa zenyewe, na wala hakuna katika Sunnah za Mtume rehma na amani ziwe juu yake sahihi zinazo pingana zenyewe kwa zenyewe, na wala hakuna katika Qur`an wala katika Sunnah, zinazo pingana na hali halisi kamwe, kwasababu hali halisi hutokea kwa haki, na Kitabu na Sunnah ni vya haki, na wala haiwezekani haki zikapingana, utakapo fahamu msingi huu utaondokewa na matatizo mengi. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Hivi hawazingztii hii Qur`an? Na laiti ingekuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila shaka wengeli kuta ndani yake khitilafu nyingi**] [Surat Al-Nisaa: 82].

Ikiwa mambo yako hivo ni kwamba hadithi za Mtume rehma na amani ziwe juu yake haziwezi kupingana, Mtume rehma na amani ziwe juu yake akiitafsiri imani kwa maana Fulani, na akaitafsiri sehemu nyingine kwa maana nyingine inayopingana na maana ya kwanza kutokana na uelewa wako, hakika ukizingatia hautakuta kuna kupingana katika maana hizo, kwa mfano:

Katika hadithi ya Jibril, Mtume rehma na amani ziwe juu yake ameigawanya Dini katika sehemu tatu:

**1**-Uislamu.

**2**-Imani.

**3**-Ihsani.

Na katika hadithi ya wageni wa Abdul Qaysi, hakutaja isipokuwa kigawanyo kimoja tu, nacho ni Uislamu.

Kwani ukitaja Uislamu kwa ujula bila mipaka inaingia ndani yake imani; kwasababu haiwezekani kupatikana Uislam bila ya imani, kwa hivyo ukitajwa Uislamu peke yake inaingia ndani yake imani, na ikitajwa imani peke yake huingia Uislamu, na vikitaja vyote kwa pamoja, inakuwa imani inaambatana na nyoyo na Uislamu unaambatana na matendo, na huu ni msingi muhimu kwa wanafunzi.

Uislamu ukitajwa peke yake huingia Imani amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Hakika Dini ya haki mbele ya Mwe-**

**nyezi Mungu ni Uislam**] [Suratul Al-Imrani /19].

Na ni kitu kinacho julikana kuwa Dini ya Kiislamu ni Misingi, Imani, na Sheria.

Na inapo tajwa imani peke yake huingia Uislamu, na vinapo tajwa vyote inakuwa imani inaambatana na moyo na Uislamu unaambatana na matendo, na kwa ajili hii walisema baadhi ya wema waliotangulia: (**Uislam ni kwa uwazi na imani ni kwa Siri**); kwasababu imani inakuwa moyoni, na kwasababu hiyo ndiyo utaweza kumuona mnafiki anaswali, anatoa sadaka, anafunga, huyu ni Muislamu kwa kumuangalia lakini sio Muumini, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Na miongoni mwa watu wapo wanao sema tumemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, wala wao si wenye kuamini**] [Suratul Al-Baqara /8].

****

**Swali la 10: Ni vipi tunakusanya baina ya Imani ni Kumuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake, na siku ya mwisho, na kheri zake na shari zake na maneno yake Mtume  rehma na amani ziwe juu yake: (Imani ni mafungu zaidi ya sabiini) [Ameipokea Bukhar /9, na Muslim/ 35].**

**Jibu:** Imani ambayo ni itikadi inamisingi sita, nayo ndiyo ambayo imetajwa kwenye Hadithi ya Jibril wakati alipo muuliza Mtume  rehma na amani ziwe juu yake: Ni nini imani? Akasema: (**Ni kumuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake,na Vitabu vyake, na Mitume wake, na siku ya mwisho na kuamini kheri zake na shari zake**) kama ilivyo thibiti katika hadithi  tulio itaja hapo juu.

Ama imani ambayo inakushanya Matendo yake, aina zake na mgawanyiko wake, hizo ndio  zipo zaidi ya sabini, na kwa ajili hiyo ameiita Mwenyezi Mungu Swala kua ni imani katika maneno yake: [**Na Mwenyezi Mungu hakuwa ni mwenye kuipoteza Imani yenu kwani Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa watu na Mwenye kuwarehemu**] [Suratul Al-Baqara /143], wamesema wema walio tangulia Mwenyezi Mungu awarehemu: (Imani yenu) yani Swala zenu wakati mkielekea Baiti L-Maqdis, kwa sababu walikuwa Maswahaba kabla ya kuamrishwa kuelekea katika Al-kaabah wakiswali hali ya kuwa wanaelekea Masjidi Al-Aqswa (Msikiti ulioko Palestina).

****

**Swali la 11: Je tunaweza kumshuhudilia Mtu kuwa ana Imani kwa kuzoea kwake Msikiti kama ilivyo kuja kwenye hadithi?**

**Jibu:** Ndio, hakuna shaka kuwa kila mwenye kuhudhuria Swala zote Msikitini, kuhudhuria kwake huko ni Ushahidi ya kuwa ana imani; kwa sababu hakuna kilicho mpelekea kutoka nyumbani kwake na kutembea kwenda Msikitini, isipokuwa ni imani ya kumuamini Mwenyezi Mungu.

Ama maneno ya muulizaji kama ilivyo kuja katika hadithi hilo limeashiriwa kwa kile kilicho pokelewa kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (**Mtakapo muona Mtu ameizoea Misikiti, mshuhudilieni kuwa, ana imani**) [Ameipokea Tirmidhii /2617, na Ibnu Maja /802], lakini Hadithi hii ni dhaifu haikusihi kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake .

****

**Swali la 12: Mtu anatiwa wasiwasi Sana na Sheitani Kuusiana na Mola wake, na yeye analiogopa sana hilo, Ni upi muongozo wenu kwa Mtu huyu?**

**Jibu:** kilicho tajwa kuhusu tatizo la muulizaji ambaye anaogopa matokeo ya wasiwasi wake; ninasema kumwambia: Nambashiria ya kuwa hatakuwa na matokeo ila mazuri tu, kwasababu wasiwasi huo hutiwa na Shetani kwa Waumini; ili azitikise imani zao zilizo salama kwenye nyoyo zao, na ili awatie karaha katika nafsi na katika fikra, na fujo katika imani, bali awatilie fujo katika maisha yao ikiwa ni Waumini.

Na hali yake si ya kwanza kuwatokea watu wa imani, na wala siyo mwisho wa kutokewa na hilo, bali itabaki kwake muda wa kwamba ni Muumini na yupo duniani, na hali kama hizi zilikuwa zikiwatokea Maswahaba wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, imepokelewa hadithi kutoka kwa Abuu Hureyra radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake amesema: Walikuja watu katika Maswahaba wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, wakamuuliza: **(Hakina sisi tunakuta katika nafsi zetu mambo makubwa, ambayo anashindwa mtu kuyaeleza,** akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (**Ni kweli mmeyakuta katika nafsi zenu**?) wakasema: Ndio, akasema: (**Hiyo ndio imani ya wazi**) [ameipokea Muslim /132], na katika Sahihi Bukhary na Sahihu muslimu imepokewa pia kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake : amesema: (**Anamjia Shetani mmoja wenu kisha anamuambia: Nani ameumba kitu flani? Nani ameumba kitu flani? Mpaka anamuambia: Nani kamuumba Mola wako? Litakapo mfika mmoja wenu hilo basi na ajikinge kwa Mwenyezi Mungu na Sheitwani na aliache hilo**) [Ameipokea Bukhar /3276, na Muslimu /134].

Na imepokelewa kutoka kwa Ibnu Abas radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Kuwa Mtu mmoja alimjia Mtume rehma na amani ziwe juu yake akasema: Hakika mimi huwa naisemesha nafsi yangu kwa kitu kinachonitia wasiwasi na sipendi kukiongelea, akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (**Sifa njema zina mstahiki Mwenyezi Mungu ambae amelirudisha jambo la wasiwasi**) [Ameipokelewa Abu Dauda, na akapokelewa na Ahmadi].

Amesema Sheykh Al-Islaam Ibn Taymiyah katika Kitabu (Al-Imaan) Muumini anapewa mtihani wa wasiwasi na Shetani, kwa wasiwasi wa Ukafiri mpaka kifua chake kinanyongea kama walivyo sema Maswahaba

kumuambia Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika mmoja wetu anajikuta katika nafsi yake kiasi kwamba anahisi mbingu inataka kuanguka katika ardhi, na sipendi kuliongelea jambo hilo, akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu: (**Hiyo ndiyo imani ya wazi**) na katika mapokezi mengine: jambo linakuwa kubwa mpaka nashindwa kuliongelea, akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (**Sifa njema zina mstahiki Mwenyezi Mungu ambae amelirudisha jambo la wasiwasi**) yani kupatikana wasiwasi huu na karaha kubwa na Moyo kuwa na wasiwasi, hiyo ndiyo imani ya wazi, hiyo ni kama Mwenye kupigana Jihadi amemjia adui akapigana nae mpaka akamshinda, na hii ni Jihadi kubwa, mpaka alipo sema na kwa jambo hilo hupatikana kwa wanafunzi na waja wengine wasiwasi na mambo yenye kufanana na hayo, mambo ambayo hayapatikani kwa Mwingine; kwa sababu wengine hawakufuata sheria ya Mwenyezi Mungu na wala hawafuati njia yake, bali wao ni wenye kufuata matamanio

yao na kughafilika na kumtaja Mwenyezi Mungu, na hawa wote ni wenye kutafutwa na Sheitwani, ni kinyume na wale walio elekea kwa Mola wao kwa ujuzi na ibada.

Sasa ninasema kwa huyu muulizaji: Utakapo jua kuwa wasiwasi huo unatokana na Shetani, basi mpige vita sana, na jua kuwa hawezi kukudhuru kwa lolote, ni wajibu wako kupigana nae, na kujiepusha nae na kujiepusha kupita katika mapito yake.

Kama alivyo sema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (**HakikaMwenyezi Mungu, amewasamehe Ummah wangu kwa yale mambo ambayo wana wasiwasi katika nyoyo, muda wakuwa hakufanya wala hakuzungumza**) [Imepokelewa na Bukhar /2528, na Muslimu /127].

Na wewe lau kama utaambiwa: Je unamin yale ambayo unawasiwasi nayo? Na je unayo yaona ni haki? Na je sifa hizo anaweza kusifiwa nazo Mwenyezi Mungu? Ningesema: haiwi kwetu kuongea mambo hayo, umetakasika Mwenyezi Mungu huu ni uongo mkubwa kabisa, na ungelikataa hilo kwa moyo wako na ulimi wako, na ukawa ni miongoni mwa watu wenye kumkimbia, kwa kuwa huo ni wasiwasi unao pita katika nyoyo, na ujikinge na Shetani ambaye hupiata kwa Mwanadamu katika mishipa inayo pita Damu, ili akuchanganye katika Dini yako au akurudishe katika ukafiri.

Ndio maana utamkuta Shetani vitu ambavyo havina maana haviweki katika moyo wako shaka au kuweka kasoro, kwa Mfano, wewe unasikia kuwa kuna miji muhimu na mikubwa, imejaa watu na majengo mazuri, katika mashariki ya ardhi na magharibi yake, lakini haikuwahi kupita shaka katika akili yako, hukusu kupatikana majengo hayo, au hayapo, au yameharibika, hayafai kuishi watu tena, na hakuna Mtu anae ishi tena humo, na mifano mingine, kwasababu Shetani hana lengo la kutia watu shaka kwenye mambo hayo, lakini Shetani ana lengo kubwa, nalo ni kuharibu imani ya Muumini, kwani yeye anakwenda mbio katika kuzima nuru ya elimu na uongofu katika moyo wake, na ndio maana humtupa mtu katika giza la shaka, na Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ametubainishia dawa yenye mafanikio na yenye kuponyesha, nayo ni maneno yake: (**Na ajikinge kwa Mwenyezi Mungu,na kisha, aache jambo hilo**), na atakapo liacha Mwanadamu jambo hilo, na akaendelea katika ibada ya Mwenyezi Mungu, hali ya kumuomba Mwenyezi Mungu na kujikurubisha kwake, litaondoka hilo kwake kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, kitu cha muhimu ni kujiweka Mbali na makadirio yote yanayo pita katika moyo wake katika mlango huu, ghafla utajikuta ukimuambudu Mwenyezi Mungu, na kumuomba na kumtukuza, na kama utamsikia yoyote anaelezea mambo ambayo hutia wasiwasi katika nyoyo, ungeweza hata kumuuwa kama ungeliweza hilo.

Kwa hiyo mambo ambayo hutia wasiwasi, sio mambo yenye uhakika, bali ni mambo ambayo hupita tu moyoni, lakini hayana asili kabisaa.

Kama vile inavyo mtokea mtu ambaye ana nguo twahara amezifua vizuri, kisha akashikwa na wasiwasi kuwa huenda zi-

menajisika, na huenda hazifai kuswali akiwa ameva nguo hizo, yatakapo mtokea hayo haifai kwake kuyaangalia hayo.

Ufupisho wa nasaha zangu ni kama ifuatavyo:

**1**-Kujikinga kwa Mwenyezi Mungu, na kuacha kukadiria hayo yote, kama alivyo tuamrisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake.

**2**-Kumtaja sana Mwenyezi Mungu na kuidhibiti nafsi kutouendelea na wasiwasi huo.

**3**-Kujishughulisha na Ibada na matendo mema, kwa ajili ya kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu, na kutafuta radhi zake.

**4**-Kuzidisha kuomba hifadhi kwa Mwenyezi Mungu, kwa kumuomba akuondoshee jambo hilo.

Ninamuomba Mwenyezi Mungu akupe afya na uzima na akuepushe na kila baya.

****

**Swali la 13: Je ni lazima kwa Kafiri kuingia katika Uislam?**

**Jibu:** Ni lazima kwa kila Kafiri kuingia katika Uislamu, awe Mkiristo au Yahudi, kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema katika kitabu chake kitukufu: [**Sema Enyi watu, hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi wote,kutoka kwa Mwenyezi Mungu mwenye ufalme wa mbingu na ardhi. Hapana Mola anayefaa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye(Mwenyezi Mungu)anaye huisha na anaye fisha. Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake asiyejua kusoma na kuandika, ambaye ana muamini Mwenyezi Mungu na Mneno yake, na mfuateni yeye ili mpate kuongoka**] [Suratul Al-Aaraaf /158].

Ni lazima kwa watu wote wamuamini Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Isipokuwa Dini hii ya Uislamu kutokana na huruma zake na hekima zake imeruhusu kwa wasiokuwa Waislamu kubaki katika Dini zao kwa sharti wawe katika hukumu za Kiislamu Amesema Mwenyezi Mungu: [**Piganeni na wasio muamini Mwenyezi Mungu wala siku ya Mwisho,wala hawaharamishi alivyo haramisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala hawashiki Dini ya Haki, miongoni mwa walio pewa Kitabu, mpaka watoe kodi kwa khiyari yao, hali wametii**.] [Suratul At-Tawba /29], na katika Sahihi Muslim, katika Hadithi ya Buraydah, alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu akimuamrisha kiongozi wa Jeshi, kumuogopa Mwenyezi Mungu, na pia alokuwa nao katika Waislamu na akisema kuwaambia ((**Walinganieni katika mam-**

**bo matatu, yeyote atakaye yakubali hayo basi mkubalieni, na msimpige vita**)) [Ameipokea Muslim /1731]. Na miongoni mwa vitu hivyo vitatu mojawapo ni kutoa kodi.

Na kwa ajili hiyo imekuwa kauli sahihi katika kauli za wana chuoni, kuwa kodi hukubaliwa kwa wasio kuwa Mayahudi na Manaswara.

Uhakika wa jambo ni kuwa: Wasio kuwa waislamu ni lazima kwao ima kuingia katika Uislaam au kutii sheria za Kiislamu. Mwenyezi Mungu ni mwenye kuwafikisha.

****

**Swali la 14: Nini hukumu ya mwenye kudai kuwa anajua mambo yaliyo ghaibu (yalio jificha)?**

**Jibu:** Hukumu ya mwenye kudai kuwa anajua mambo yaliyo jificha ni Kafiri, kwa sababu yeye amemkadhibisha Mwenyezi Mungu, anasema Mwenyezi Mungu [**Sema: Hapana katika mbingu na ardhi anaejua ya ghaibu isipokuwa Mwenyezi Mungu. Wala wao hawajui lini watafufuliwa**] [Suratul An-Naml /65]. Iki-

wa Mwenyezi Mungu anamuamrisha Mtume wake atangaze kwa watu wote kuwa hakuna anaye jua katika mbingu na ardhi mambo yalio jificha isipokuwa Mwenyezi Mungu tu; kwa hiyo mwenye kudai anajua mambo yalio jificha atakuwa amemkadhibisha Mwenyezi Mungu katika jambo hilo; na tunasema kwa watu hawa: Itawezekana vipi kujua mambo yalojificha? Na Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Mwenyewe hajui mambo hayo? Jee nyie ni wabora sana kuliko Mtume wa Mwenyezi Mungu? na iwapo watasema: ndio sisi ni wambora kuliko Mtume wa Mwenyezi Mungu, watakuwa wamekufuru kwa neno hilo, na wakisema yeye ni mbora tutasema: sasa kwanini yeye hajui mambo yalojificha haliyakuwa nyinyi mnajua? Na Mwenyezi Mungu mwenyewe amesema kuhusu Nafsi yake kuwa [**Yeye ndio mwenye kujua ya siri, wala hamdhihirishii yeyote siri yake /26, Isipo kuwa Mtume wake aliye mridhia. Naye huyo humwekea walinzi mbele na nyuma Yake**] [Suratul Al-Jinn /27, hii Aya ya pili inaonesha ukafiri wa mwenye kudai anajua mambo ya siri na Mwenyezi Mungu amemuamrisha Mtume wake awatangazie watu wote, akasema: [**Sema: Mimi sikwambii kuwa ninazo khazina za Mwenyezi Mungu. Wala sijui mambo yaliyo fichukana. Wala sikwambii kuwa mimi ni Malaika Mimi sifuati ila yanayo funuliwa kwangu**] [Suratul Al-An’aam /50].

****

**Swali la 15: Tutayaoanisha vipi maneno ya Madaktar wa sasa, wanao tutajia aina ya mtoto Wa kike au Wa kiume na maneno yake Mwenyezi Mungu alipo sema [Yeye ndiye ajuaye yaliyo katika matumbo] na iliyo kuja katika tafsiri ya Ibnu Jariri kutoka kwa Mujahid, kuwa Mtu mmoja alimuliza mtume wa Mwenyezi Mungu, ni nini atazaa mke wake, akateremsha Mwenyezi Mungu Aya hii, na ile ilopokelewa kutoka kwa Katada? Ni kitu gani kinaifanya Umumi katika Aya hiyo kwa Khaswa?**

**Jibu:** Kabla sijaongelea mambo hayo, ninapenda kubainisha kuwa haiwezekani Qur`an iliyo wazi ikapingana na hali halisi, na iwapo itatokea katika hali halisi kitu ambacho kilicho dhahiri kinapingana na Qur`an, ima iwe hiyo hali halisi sio hakika ni maneno tu, au iwe Qur`an haikuweka wazi upingaji wake; kwa sababu Qur`an iliyo wazi na hali halisi zote ni ushahidi wa kukata, na wala haiwezekani ushahidi wa aina mbili wa kukata kupingana.

Na iwapo hilo litakuwa lipo hivo, hakika imesemwa: Hakika wao wamefikia kujua kilichoko katika tumbo la uzazi kwa kutumia vyombo vya kisasa, na kujua kwao mtoto ni wa kike au wa kiume, ikiwa maneno yao yatakuwa sio sahihi basi hakuna la kusema, na ikiwa ni kweli, basi hayapingani na Aya, kwa sababu Aya inafahamisha juu ya jambo la siri, ambalo nimefungamana na ujuzi wake Mwenyezi Mungu katika yale mambo matano, na mambo ya siri kwa kiumbe kilichiko tumboni ni: Kiasi cha muda wake kwenye tumbo la mama yake, Uhai wake, Matendo yake, Riziki yake, na wema wake au uovu wake, kuwa kwake wa kiume au wa kike

kabla hajaumbwa, ama baada ya kuumbwa kujua kuwa ni wa kike au wa kiume sio siri tena, kwa sababu kwa kuumbwa kwake amekuwa katika vitu vyenye kuonekana, isipokuwa yeye yupo kwenye viza vitatu ambavyo kama vingetolewa basi lingekuwa wazi jambo lake, na wala hiiwi mbali kwa alivyo viumba Mwenyezi Mungu miongoni mwa vitu mbali mbali kupenya katika viza hivi na kubainisha hali ya kiumbe tumboni kuwa cha kike au cha kiume, na haikuja katika Aya kutaja kwa uwazi ujuzi wa kuwa mtoto ni wa kike au wa kiume, na pia halikuja kwenye Sunnah.

Ama kuhusu aloyanukuu muulizaji, kutoka kwa Ibnu Jariri kutoka kwa Mujahid, kuwa Mtu alimuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu, kile anacho kizaa mwanamke, Mwenyezi Mungu akateremsha Aya hii, nukuu hii imekatika kwa sababu Mujahid ni katika Taabiin.

Ama tafsiri ya Kataada, inaweza kuchukuliwa kuwa ujuzi unao mhusu Mwenyezi Mungu katika hilo ni kabla hajaumbwa, ama baada ya kuumbwa anaweza kujua asiyekuwa Mwenyezi Mungu; Amesema Ibnu Kathir katika tafsiri ya Aya ya Luqman; Na vile vile hawajui kilichoko katika matumbo katika vile anavyo taka kuviumba, lakini anapo amrisha kuwa kwake cha Kiume au cha Kike, Chema au Kiovu, Malaika walio wakilishwa kwa hayo wanajua, na mwingine atakae penda Mwenyezi Mungu ajue.

Ama swali lenu, katika maneno ya Mwenyezi Mungu [**kila kilichoko kwenye matumbo ya uzazi**] kuwa inaenea katika kila kitu, ni ushahidi gani unaotoa baadhi ya vitu.

Tunasema: Ikiwa Aya inamkusudia Mwanaume na Mwanamke baada ya kuumbwa, basi ushahidi unaotoa baadhi ya vitu ni Akili ya kawaida na hali ya kawaida, na wametaja Wanachuoni wa Usulu kuwa, ukija ushahidi wa kuenea vitu vyote, kitu ambacho kinaweza kutoa baadhi ya vitu ni Kitabu na Sunnahh, au Ijimaa (makubaliano ya wanachuoni) au Qiyas, au Al-Hisi (Akili ya kawaida) na maneno yao katika hilo ni maarufu.

Ama ikiwa Aya haizungumzii baada ya kuumbwa, lakini inazungumzia kabla, hakuna kupingana, kwa yale yalosemwa kujua kiumbe ni cha kike au cha kiume.

Na tunamshukuru Mwenyezi Mungu haikupatikana, na wala haitopatikana katika hali ya kawaida kitacho kwenda kinyume na Qur`an ilokuwa wazi. Ama yale ambayo wameyatia kasoro maadui wa Waislaamu juu ya Qur`an kwa kuleta mambo ambayo dhahiri yake yanapingana na Qur`an, hakika hutokea hilo kwa ufinyu wa ufahamu wao kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu, au upungufu wao katika hilo ni kwa ajili ya nia zao mbaya, lakini kwa Watu wa Dini na Elimu, wenye kutafuta misingi ya Ukweli na Uhakika haziwasumbui hizo shubha zao. Na tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa hilo.

Na Watu katika hili wamegawanyika makundi mawili:

**Kundi la kwanza:** Ni kundi ambalo limeshikamana na dhahiri ya Qur`an, ambayo haipo wazi, na wakakataa kila kilicho tofauti, katika kila jambo linalo tokea katika mambo yenye uhakika, likawapelekea hilo, kutia kasoro, nafsi zao au kutia kasoro Qur`an Tukufu,

Na kundi linguine: Wameyapuuza yale yalio elekezwa na Qur`an, na wakachukua mambo yenye kuonekana tu, wakawa kwa hilo ni katika wapingaji.

Ama walio wa kati na kati, wamechukua ushahidi wa Qur`an, na wakakubali hali za kisasa, na wakajua kuwa yote hayo ni ya kweli, na wakajua haiwezekani Qur`an iliyo wazi kupingana na mambo yanayo julikana kwa kuyaona, wakakubaliana kufanyia kazi ushahidi ulio nukuliwa na wa kiakili, ikasalimika kwa hilo Dini yao na Akili zao, na Mwenyezi Mungu akawaongoza katika haki walio amini pale walipo tofautina, Mwenyezi Mungu humuongoza amtakae katika njia iliyo nyooka.

Mwenyezi Mungu atupe Taufiki pamoja na ndugu zetu katika hilo, na atukusanye katika Uongofu, na katika viongozi wema, na hakuna Taufiki isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu, kwake ndiko niliko tegemea na kwake ndiko ninako geukia.

****

## Swali la 16: Je jua huzunguka katika Ardhi?

**Jibu:** AliJibu kwa kusema, ushahidi wa Kisheria ulio wazi, unathibitisha kuwa Jua ndio linalo zunguka katika Ardhi, na kwa mzunguko wake ndio hupatikana Usiku na Mchana katika Uso wa Ardhi, na haitupasi sisi kuvuka mpaka wa dhahiri ua ushahidi huu isipokuwa kwa ushahidi wenye nguvu zaidi ya huo, kwa wakati huo tunaweza kutafsiri dhahiri ya Aya.

Na katika Ushahidi kuwa jua linaizunguka Ardhi mzunguko ambao husababisha Usiku na Mchana ni kama ifuatavyo:

**1**-Maneno ya Mwenyezi Mungu kutoka kwa Ibrahim alipokuwa akijadiliana na yule aliye mhoji kuhusu Mola wake: [**Ibrahim akasema: Mwenyezi Mungu huchomozesha jua mashariki, basi wewe lichomozeshe magharibi**] [Suratul Al-Bakara /258]. Kule kuwa jua huchomozea Mashariki ni Ushahidi ya kuwa ni lenye kuzunguka katika Ardhi.

2-Na akasema tena kuhusu Ibrahim [**Na alipo liona jua linachomoza akasema: Huyu ndie Mola wangu. Huyu mkubwa kuliko wote, lilipo tua, alisema: Enye watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayo fanyia ushirikina]** [Suratul Al-An'aam /78].

Amejalia kupotea ni kwa jua sio kwa Ardhi, na lau kama ingalikuwa Ardhi ndio inazunguka angalisema (wakati ilipo potea)

3-Amesema Mwenyezi Mungu: [**Na utaliona jua linapo zama linainamia kuliani kwao kutoka hapo pangoni na linapo kuchwa linawakwepa kushoto**] [ Suratul Al- Kahf 17]. Amejalia kuinama na kukwepa ni kwa jua, nao ni ushahidi kuwa harakati ni za jua, na lau kama ingekuwa ni kutoka kwenye Ardhi, angalisema, kama vile kuchomoza na kuchwa kumeegemezwa kwenye jua, hili hufahamisha kuwa lenyewe ndio huzunguka.

**4**-Amesema Mwenyezi Mungu: [**Na yeye ndiye aliye umba Usiku na Mchana na jua na mwezi, vyote katika anga vinaogelea**][SuratulAl-Anbiyaa/ 33]. Amesema Ibnu Abass linazunguka katika falaki zake.Na maneno hayo yamekuwa ni maarufu kwake.

5-Amesema Mwenyezi Mungu: [**Huufunika usiku kwa mchana ufuatao upesi upesi**] [ Suratul Al-Aaraaf /54]. Amejalia Mwenyezi Mungu kuwa usiku ni wenye kuutafuta Mchana, na ni kitu kinajulikana kuwa usiku na mchana ni vyenye kufuata jua.

**6**-Amesema Mwenyezi Mungu [**Ameumba mbingu na ardhi kwa Haki. Hufunika usiku juu ya mchana na hufunika mchana juu ya usiku.Na amefanya jua na mwezi vitumike.kila kimoja wapo kinakwenda kwa kipindi kilicho wekewa, jueni na Mtanabahi! Yeye ndiye mwenye nguvu, na mwenye kusamehe**] [Suratul Azu-Zumar /5].

Katika Aya kuna ushahidi kuwa mzunguko wa mbigu na ardhi unatokana na jua, na maneno yake Mwenyezi Mungu **[Jua na mwezi vyote vinakenda]** hapa kuna ubainifu kuwa jua na mwezi

vinazunguka.

7- Amesema Mwenyezi Mungu: [**Naapa kwa jua na mwangaza wake /1, Na kwa mwezi unapo lifuatia**] [Suratul Shams /2]. Maana ya (talaaha) kuja baada yake, nayo ni ushahidi wa kutembea kwake na mzunguko wake, na kama ingalikuwa ardhi ndio inalizunguka jua na mwezi, basi mwezi usinge lifuata jua, bali ingekuwa wakati mwingine jua hufuata mwezi na wakati mwingine mwezi hufuata jua, kwa sababu jua lipo juu zaidi ya mwezi, na kutoa ushahidi wa Aya hii kunahitaji kufikiria.

8. Amesema Mwenyezi Mungu: [**Na jua linakenda mpaka kituoni kwake.Hayo ni makadirio ya mwenye nguvu, Mwenye elimu. Na mwezi tumeukadiria vituo, mpaka unakuwa kama karara kongwe, Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kuupita mchana. Na vyote**

**vinaoglea katika njia zake**] [Suratul Yasin 38-40].

Kuegemeza kuzunguka kwenye jua, na kujalia makadirio ya Mwenyezi Mungu ndani yake hiyo ni ushahidi kuwa mzunguko wake ni wa kweli tena wa hali ya juu, kwa sababu hutokea ndani yake kupishana kwa mchana na usiku na nyakati.

9. Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu kumwambia Abii Dhary jua likiwa limezama ((**Unajua linakwenda wapi**)) akasema: Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanajua: akasema: **((Hakika linakwenda mpaka linasujudu chini ya Arshi (kiti cha enzi) kisha linaomba ruhusa na kuruhusiwa, nachelea lije liombe ruhusa na lisiruhusiwe kisha liambiwe: Rudi ulipo toka, kisha lichomoze upande wa magharibi yake)**) [Ameipokea Bukhar /3199, na Muslim /159] au kama alivyo sema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Rudi ulipo toka, kisha lichomoze upande wa magharibi yake**)) yapo wazi sana, kuwa jua linazunguka juu ya ardhi, na kwa mzunguko wake huo hupatikana kuchomoza na kuzama.

**10**- Hadithi ni nyingi, zinazo unesha kuegemezwa, kuchomoza, kuzama na kuondoka kwenye jua, hakika hilo lipo wazi katika kutokea hilo kwa jua, na sio katika Ardhi.

Na huenda kukawa na shahidi nyingine, lakini hazikunijia hivi sasa, lakini kwa nilizo zikumbuka zimefungua mlango ambao nilikuwa naukusudia. Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuwafikisha.

****

**Swali la 17. Aliulizwa Sheikh Mwenyezi Mungu amrehemu, kuhusu Shahada mbili?**

**Jibu**: Shahada mbili: ((Ni kushuhudia ya kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu, na Muhammad rehma na amani ziwe juu yake ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, nazo ni funguo za Uislamu, na haiwezekani kuingia katika Uislamu bila hizo Shahada mbili; na kwa ajili hiyo Mtume rehma na amani ziwe juu yake alimuamrisha Muadhi bin Jabal wakati alipo mtuma kwenda Yemen**: ((Iwe kitu cha kwanza atakacho walingania (kuhubili) Ni kushuhudia ya kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu,na Muhammad rehma na amani ziwe juu yake ni Mtume wa Mwenyezi Mungu)) [**Ameipokea Bukhari/1359, na Muslim 19].

Ama neo la kwanza: Ni kushuhudia ya kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Munguikiwa atalikubali Mtu kwa Ulimi wake na Moyo wake, kuwa hakuna mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, haya maneno yamekusanya nafii (kukataa) na ithbati (kuthibitisha) ama nafii ni: (Hakuna Mola) na ithbati ni: (isipokuwa Mwenyezi Mungu), neno hilo linakusanya kumtakasa Mwenyezi Mungu peke yakekwenye kufanya Ibada na kukataa kuwa hairuhusiwi kufanya Ibada kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu.

Kuna swali ambalo watu wengi hujiuliza nalo ni: Vipi mnasema kuwa: Hapana Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu, na kuna

Miungu wengi wasio kuwa Mwenyezi Mungu huabidiwa, na Mwenyezi Mungu amewaita Miungu, na wale wenye kuwaabudu wanawaitwa Miungu, amesema Mwenyezi Mungu: [**Na Miungu yao walokuwa wakiiomba badala ya Mwenyezi Mungu haikuwafaa kitu ilipo kuja amri ya Mola wako**.] [ Suratul Hud /101], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Wala usifanye pamoja na Mwenyezi Mungu miungu mingine**] [Suratul Al-Israaa /39] na amesema Mwenyezi Mungu: [**Wala usiombe pamoja na Mwenyezi Mungu miungu mingine**] [Suratul Qaswasw /88] ana amesema: [**Hatuta omba asiye kuwa Mwenyezi MunguMungu mwingine**] [Suratul Kahafi /14].

Ni vipi tutaweza kusema: Hapana Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu, pamoja na kuthibitisha Uungu kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu, ni vipi tutaweza kuthibitisha Uungu kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu na Mitume wanasema kuwaambia watu wake [**Muabuduni Mwenyezi Mungu, mna nini mna miungu isiyokuwa Mwenyezi Mungu**] [Suratul Al-Araaf /59].

Majibu ya tatizo hilo: Inabainika kwa kuikadiria habari katika, (hapana Mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu) Tunasema: Hii miungu ambayo huabudiwa kinyume na Mwenyezi Mungu, ni Miungu lakini ni Miungu ya baatili sio Miungu ya kweli, na hilo linathibitiswa na maneno yake Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Hivi ni kwa sababu, hakika Mwenyezi Mungu ndiye wa kweli, na hakika wanacho kiomba ni cha uongo, na kwamba hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mtukufu na ndiye Mkubwa**] [Suratul Luqman /30], na pia neno Lake Mwenyezi Mungu: [**Je!**

**Mmemuona lata na Uzza** /19. **Na Manaata mwingine wa tatu?** /20. **Je! Nyinyi mnao wanaume na yeye ndio awe na wanawake** /921. **Huo ni mgawanyo wa dhulma**! /22. **Hayo hayakuwa ila ni majina mliyowapa nyinyi na baba zenu, Mwenyezi Mungu hakuleta uthibitisho wowote juu ya hayo**] [Suratul An-Najmi], na maneno yake Mwenyezi Mungu kutoka kwa Yusuf [**Mnavyo viabudu visivyo kuwa Mwenyezi Munguisipokuwa ni majina mlio waita nyinyi na baba zenu hakuteremsha Mwenyezi Mungu katika hiyo Ushahidi**] [Suratul Yusuf].

Kwa hivyo maana ya, (Hakuna Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu) hakuna Muabudiwa wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu.Ama waabudiwa wasiokuwa Mwenyezi Mungu, hakika Uungu wake anao dai mwenye kuabudu sio wa haki, yani ni mwenye Uungu wa baatili, bali Uungu wa haki ni Uungu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ama maana ya shahada ((Hakika Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu) ni kukiri kwa Ulimi na kuamini kwa Moyo kuwa Muhammad bin Abdillah ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa viumbe wote Majini na Watu, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Sema: Eyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi vyote, kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi. Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwaYeye Mwenyezi Mungu Anaye huisha na anaye fisha. Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake asiyejua kusoma na kuandika, ambaye anamuamini Mwenyezi Mungu na maneno yake.na mfuateni yeye ili mpate kuongoka**]

[Suratul Al-araf /158], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Ametukuka aliye teremsha Furkani kwa mja wake, ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote**] [Suratul Alfurqan /1]. Na kinacho takiwa katika hii shahada ni kumswadikisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa kile alicho tuhabarisha, na kufuata amri zake alizo amrisha, na kujiepusha na yale aliyo yakataza, na usimuabudu Mwenyezi Mungu ila kwa kile alicho kiamrisha.

Na kingine kinacho takiwa katika shahada hii pia ni usiitakidi kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake anayo haki katika uumbaji wala katika uendeshaji wa Ulimwengu, au ana haki katika kuabudiwa, bali yeye ni Mja haabudiwi, na ni Mtume hakadhibishwi, na wala hamiliki kwa nafsi yake wala ya mwingine manufaa wala madhara isipokuwa kile atakacho kitaka Mwenyezi Mungu, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Sema:Mimi sikwambii kuwa ninazo hazina za Mwenyezi Mungu wala sijui mambo yaliyo fichikana, wala sikwambii kuwa mimi ni Malaika. Mimi sifuati isipokuwa yale ninayo funuliwa kwangu**] [Suratul Al-An,aam /50]. Yeye ni mja aloamrishwa hufuatwa kwa kile alicho amrishwa, amesema Mwenyezi Mungu: [**Sema Mimi sina mamlaka ya kukudhuruni wala kukuongozeni /21. Sema: Hakika mimi hakuna yeyote awezae kunilinda na Mwenyezi Mungu wala sita pata pa kukimbilia isipokuwa kwake Yeye tu]** [Suratul Al-Jinn /22], na amesema Mwenyezi Mungu [**Sema: Siimiliki nafsi yangu kwa manufaa wala madhara, isipokuwa apendavyo Mwenyezi Mungu. Na laiti ngekuwa nayajua ya ghaibu ningezidisha mema mengi, wala ovu lisinge nigusa. Mimi si chochote isipokuwa ni mwonyaji na mbashiri kwa watu wanao amini**] [Suratul Al-Araf /188). Hii ndio maana ya shahada

(Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na Muhammad ni mtume (rehma na amani ziwe juu yake Mwenyezi Mungu.

Kwa maana hii utajua kuwa hakuna anaye stahiki Ibada, sio Mtume rehma na amani ziwe juu yake  wala yeyote katika viumbe, na kwamba Ibada si ya yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake, Amesema Mwenyezi Mungu: [**Sema: Hakika swala yangu,na ibada zangu,na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote/162/Hana mshirika wake,Na hayo ndio niliyo amriswa,na mimi ni wa kwanza wa Waislam**] [Suratul Al-An,aam /163]. Na hakika haki ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake  ni kuwekwa sehemu ambayo Mwenyezi Mungu amemuweka, nayo ni Mja wa Mwenyezi Mungu na ni Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake .

****

**Swali la 18: Ni vipi imekuwa (Hapana Mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu) imekusanya aina zote za Tauhidi?**

**Jibu:** Yenyewe imekusanya aina zote za Tauhidi ima kwa ushirikishwaji au Kulazimiana na hilo kwa sababu ya maneno ya mwenye kusema (Nashuhudia ya kuwa hapa Mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu). Kinacho pita katika ubongo ni kuwa makusudio ya Tauhidi hapo ni Tauhidi ya Ibada, ambayo huitwa Tauhidi Uluhiya, nayo imekusanya Tauhidi Rububiyya, kwa kuwa kila mwenye kumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake, hakika hawezi kumuabudu mpaka awe ni mwenye kukiri Tauhidi Rububiyya, na vile vile imekusanya Tauhidi Asmaa wa Swifat, kwa sababu Mwanadamu hawezi kuabudi mpaka ajue kuwa huyu anastahiki Ibada; kwa majina yake na sifa zake, na kwa ajili hiyo alisema Ibrahim kumwambia baba yake: [**Alipo mwambia baba yake:Ewe baba yangu! kwa nini unaabudu kisichosikia, na kisicho ona, na kisicho kufaa chochote**?] [Suratul Maryam /42]. Kwa hivyo Tauhidi ya Ibada imekusanya Tauhidi Rububiyya na Tauhid Asmaa Waswifati.

****

## Swali la 19: Ni ipi hekma ya kuumbwa Majini na Watu?

**Jibu:** Kabla sijazungumza kuhusu swali hili, ninapenda kukumbusha kuhusu Msingi wenye kuenea katika vile anavyo viumba Mwenyezi Mungu, navile anavyo viwekea Sheria, na msingi huu umechukuliwa kutoka kwenye maneno ya Mwenyezi Mungu: [**Na Yeye ni mwenye kujua Mwenye hekima**] (**hekima**) [Suratul Ataharim /2], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kujua mwenye hekima**] [Suratul An-Nisaa /42]. Na Aya nyingine zisokuwa hizo zinazo fahamisha juu

ya hekima za Mwenyezi Mungu kwa kile anacho kiumba na kile anacho kiwekea Sheria: Katika hukumu zake za Kidunia na Kisheria, kwani hakika hakuna kitu chochote anacho umba Mwenyezi Mungu isipokuwa kuna hekima katika kukiumba, ni sawasawa kwa kupatikana kwake au kukosekana, na ni sawaswa kikawa ni katika kukiwajibisha au kukiharamisha, au kukiruhusu, lakini hekima hii ambayo hukusanya hukumu za Kidunia na Kisheria, tunaweza kuwa tunazijua au hatuzijui, na inaweza kuwa zinajulikana kwa baadhi ya watu na wengine hawazijui, kwa kiasi anacho wapa Mwenyezi Mungu Elimu na Ufahamu.

Litakapo kuwa hilo hakika tunasema: Hakika Mwenyezi Mungu amewaumba Majini na Wanadamu kwa hekima kubwa na kwa lengo tukufu, nalo ni kumuabudu, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Na sikuwaumba Mjini na Watu ila waniabudu**] [Suratul Dhariat /56] na amesema Mwenyezi Mungu: [**Hivi mnadhani ya kwamba tumewaumba burebure na kwake hamtorejea**] [Suratul Al-Muuminun 115], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Je anadhani Mwanadamu kuwa ataachwa hivi hivi**] [Suratul Qiyama /36], na Aya nyingine nyingi zinazo fahamisha kuwa Mwenyezi Mungu ana hekima na malengo makubwa kwa kumuumba Majini na Watu, nayo ni kumuabudu,na Ibada ni kujidhalilisha kwa Mwenyezi Mungu, kwa kumpenda na kumtukuza, kwa kufanya aloamrisha na kujiepusha na aliyo yakataza, kwa muJibu wa ilivyo kuja Sheria, amesema Mwenyezi Mungu: [**Nahawakuamrishwa isipokuwa wamuabudu Mwenyezi Mungu, na wamtakasiye Dini**] [Suratul Al-Bayyina /5]. Hii ni hekima ya kuumbwa Majini na Watu, na kwa ajili hii mwenye kufanya ukaidi juu ya Mola wake na akaleta kiburi katika kumuabudu Mwenyezi Mungu, haki-

ka anakuwa ni mwenye kutupa hekima hii, ambayo ameumbiwa Mwanadamu kwa ajili yake, na matendo yake hayo yanaonesha kuwa Mwenyezi Mungu amewaumba viumbe bure bure na kwa ujinga, na yeye hata kama atakuwa hakuweka wazi hilo, lakini mwenendo wake unaonyesha hivyo.

****

**Swali la 20: Ni kwanini Mwanadamu anaomba dua na wala hajibiwi na Mwenyezi Mungu anasema: [Niombeni nami nitawaJibu]?**

**Jibu:** Sifa zote njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu mlezi wa viumbe wote, kisha Rehma na Amani ziende kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake na familia yake na Maswahaba zake wote, na ninamuomba Mwenyezi Mungu kwangu na kwa ndugu zangu Waislamu kuwafikishwa kwa Aqida iliyo sawa kwa maneno na vitendo, anasema Mwenyezi Mungu: [**Na Mola wenu anasema: Niombeni nitakuJibuni.Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kiniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhalilike**] [Suratul Ghafir /60]. Anasema muulizaji, hakika amemuomba Mwenyezi Mungu lakini Mwenyezi Mungu hakumjibu, anapata tatizo kwa hali hiyo pamoja na Aya tukufu, ambayo ameahidi Mwenyezi Mungu ndani yake kuwa atamjibu kila mwenye kumuomba, na Mwenyezi Mungu si mwenye kukhalifu Ahadi.

Jibu juu ya hilo: Hakika katika kujibiwa dua kuna sharti lazima zitimie ndio dua ijibiwe masharti hayo  ni:

**1**- Kuwa na Ikhlas, inatakiwa Mwanadamu awe na Ikhlasi katika Dua zake, aelekee kwa Mwenyezi Mungu kwa moyo Mkunjufu, na kwa ukweli wa kumuomba, na kuwa na Imani kuwa Mwenyezi Mungu atajibu Dua yake, na awe na matarajio kuwa Mwenyezi Mungu atamjibu maombi yake.

**2**-Ahisi wakati wa kuomba dua, kuwa ni mwenye haja sana ya kujibiwa Dua yake,bali ni mwenye haja sana na Mwenyezi Mungu, na kwamba Mwenyezi Mungu peke yake ndiye mwenye kujibu Dua za wenye matatizo, naye ndio Mwenye kuondosha mabaya.

**3**- Awe ni mwenye kujiepusha na kula haramu, kwa sababu kula haramu ni kizuizi kati ya Mwanadamu na kujibiwa Dua, kama ilivyo thibiti kutoka kwa Mtume  rehma na amani ziwe juu yake kuwa amesema**: ((Hakika Mwenyezi Mungu ni mzuri, hakubali isipokuwa vitu vizuri, na hakika Mwenyezi Mungu amewamrisha Waumini kwa kile alicho waamrisha Mitume**)). Akasema Mwenyezi Mungu: [**Enyi watu mlio amini kuleni katika vile vizuri alivyo kuruzukuni, na mumshukuru Mwenyezi Mungu ikiwa kweli nyinyi ni wenye kumuabudu**] [Suratul Al-Baqara /172] na amesema Mwenyezi Mungu: [**Eyi Mitume kuleni katika vile vizuri. Na mtende mema**] [Suratul Al-Muuminun /51].

Kisha akamtaja Mtume rehma na amani ziwe juu yake Mtu ambaye, amekuwa ni mwenye safari ndefu, ni mwenye nywele zilizo timuka, na ni zeenye mavumbi ananyoosha mikono yake mbinguni: Huku akisema Ewe Mola Ewee Mola, na Mavazi yake ni haramu, na Amelelewa kwa haramu akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Ni vipi atajibiwa dua zake**)) [Ameipokea Muslimu /1015], akaweka mbali Mtume rehma na amani ziwe juu yake kujibiwa dua zake kwa huyu Mtu, ambaye amesimama kwa sababu za wazi za kujibiwa Dau, ambazo ni:

**1**-Kuinua mikono yake mbinguni; Yani amenyoosha kwa Mwenyezi Mungu, kwakuwa Mwenyezi Mungu yupo Mbinguni juu ya kiti cha enzi, na kunyoosha kwa Mwenyezi Mungu ni katika sababu za kujibiwa Dua kama ilivyo kuja katika Hadithi ambayo ameipokea Imamu Ahamad ((**Hakika Mwenyezi Mungu yupo hai na ni Mkarimu, anaona haya kwa mja wake anapoinua Mikono yake kumuomba,**

**amrudishe patupu**)) [Ameipokea Ahamad /438/5/, Abuu Daudi /1488/, na Tirmidhii /3556].

**2**-Huyu Mtu alimuomba Mwenyezi Mungu kwa jina la Rabbu,na kumuomba Mwenyezi Mungu kwa jina hili ni sababu za kujibiwa Dua; kwa sababu Rabbu, ni Muumbaji, Mfalme, Mwenye kupanga mambo yote, katika Mikono yake kuna Ufalme wa mbingu na ardhi, na kwa ajili hiyo utakuta Dua nyingi katika Qur`an zipo kwa jina hili [**Mola wetu! Hakika sisi tumemsikia mwenye kunadi, akiitia Imani kwamba: Muaminini Mola wenu, nasi tukaamini. Basi tusamehe madhambi yetu, na utufutie mako-**

**sa yetu,na utufishe pamoja na watu wema/193/ Mola wetu!Na utupe uliyo tuahidi kwa Mitume wako, wala usitufedheheshe Siku ya Kiama. Hakika Wewe huvunji ahadi/195/ Mola wao, akayakubali maombi yao akasema: Hakika mimi sipotezi kitendo cha Mtendaji miongoni mwenu, akiwa mwanaume au mwanamke, kwani ni nyinyi kwa nyinyi**.] [Suratul Al-Imran 193-195/] Kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa jina hili ni miongoni wa sababu za kujibiwa Dua.

**3**-Huyu mtu alikuwa ni msafiri, na safari mara nyingi ni miongoni wa sababu za kujibiwa Dua kwa kuwa Mwanadamu katika safari anakuwa na haja kwa Mwenyezi Mungu, na mahitajio kwake wakati huo ni zaidi ya anapokuwa nyumbani kwa watu wake. Na alikuwa ni mwenye nywele zilizo timka na ni mwenye mavumbi, asio jali nafsi yake, kana kwamba umuhimu wake kwake yeye ni haja zake kwa Mwenyezi Mungu zijibiwe tu dua, na ndio maana alimuomba katika hali yoyote alokuwa nayo, ni sawasawa anamavumbi au nywele chafu au hapana, na kuwa katika hali hiyo ina athari katika kujibiwa Dua, kama ilivyo katika Hadithi ambayo imepokelewa kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu, hushuka katika uwingu wa Dunia, akiwa anajisifu kwa Malaika walio simama katika mbingu, na anasema: ((**Wamenijia wakiwa na nywele zilizo timka na mavumbi,kutoka katika kila pande za Dunia**)) [Ameipokea Imamu Ahamad /305/2/, na Al-Hakimu /465/1/ ].

Hizi ni katika sababu za kujibiwa Dua, lakini hakupata kitu, kwa kuwa, chakula chake ni cha haramu, na mavazi yake ni ya haramu, na amekulia katika vitu vya haramu, akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Anawezaje kujibiwa Dua yake**)). Kwani hizi ni katika sharti za kujibiwa Dua, zisipo timia hakika majibu yanakuwa mbali sana, na kama zitatimia kisha Mwenyezi Mungu hakumjibu muombaji, hakika si vinginevyo ila ni kwa hekma anayo ijua Mwenyezi Mungu, na wala haijui mwenye kuomba, na mnaweza kupenda kitu, na kitu hicho kikawa ni shari kwenu.

Pia zikitimia sharti hizi na Mwenyezi Mungu hakujibu Dua zake, hakika hilo ima hakujibu ili amuondoshee baya zaidi ya alicho kiomba, au amuwekee malipo yake mpaka siku ya Kiyama amlipe malipo makubwa zaidi, kwa kuwa huyu muombaji ambaye ameomba na amekamilisha sharti na hakujibiwa, na wala hakuondoshewa baya zaidi, anakuwa amefanya sababu na amekataliwa kujibiwa kwa hekma, na atalipwa malipo yake mara mbili, moja kwa ajili ya Dua yake, na ya pili kwa matatizo yake ambayo hakujibiwa, atalimbikiziwa kwa Mwenyezi Mungu lililo kubwa na jema zaidi.

Na katika mambo muhimu pia katika Dua, asifanye haraka katika kujibiwa, kwani hiyo pia ni katika sababu za kuto kujibiwa, kama ilivyo kuja katika Hadithi kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Hujibiwa Dua ya mmoja wenu muda wa kuwa hakufanya haraka**)) Maswahaba wakasema: ni vipi atafanya haraka ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema ((**Anasema: Nimeomba, nikaomba, nikaomba, lakini sikujibiwa**)) [Ameipokea Bukhari /6340/, na Muslim /2735/].

Haitakikani kwa mtu kufanya haraka katika kukubaliw Dua, ili asije akapata hasara katika Dua yake, bali inatakiwa amlalamikie Mwenyezi Mungu kwa matatizo yake, kwani kila Dua anayo iomba kwa Mwenyezi Mungu, hakika hiyo ni Ibada inayo mkurubisha zaidi kwa Mwenyezi Mungu na humzidishia malipo zaidi, basi ni juu yako ewe ndugu yangu kumuomba Mwenyezi Mungu katika kila jambo lako, liwe la watu wote au maalumu.

****

**Swali la 21: Nini maana ya Ikhlas? Na atakapo taka mja kufanya Ibada kwa kitu kingine ni nini hukumu ya yake?**

**Jibu**: Kufanya Ikhlas kwa Mwenyezi Mungu maana yake Akusudie Mtu katika Ibada zake, kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, ili kufika katika nyumba ya ukarimu.

Na anapo taka Mja katika Ibada zake kitu kingine, kuna upambanuzi kwa mujibu wa vigawanyo vifuatavyo:

**1**-Awe anataka kujikurubisha kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu kwa kufanya Ibada hiyo na kupata sifa juu yake kutoka kwa viumbe, hakika hili hubomoa matendo yote alio yafanya nayo ni katika Shirki, imepokelewa hadithi katika vitabu vya swahihu bukhary na swahihi muslim kutoka kwa Hadithi ya Abu Huraira, kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ((**Mimi nimejitosheleza na washirika juu ya kushirikishwa, mwenye kufanya matendo, akanishirikisha ndani yake Mimi pamoja na vitu vingine, nitamuacha na Shirki yake**)) [Imepokelewa na Muslim /2985].

**2**-Awe anakusudia katika Ibada yake hiyo malengo ya kidunia, kama Urais, au Cheo, au Mali, na hakuna ndani yake kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, hakika matendo hayo ni yenye kuporomoka, hamuombi Mwenyezi Mungu kwa Matendo hayo, wala hamuombi kwa maneno yake Mwenyezi Mungu aliposema: [**Wanao taka maisha ya dunia na mapambo yake tutawalipa humo vitendo vyao kamili. Na wao humo hawato punjwa. /15 Hao ndio ambao hawatakuwa na kitu Akhera ila Moto, na yataharibika walio yafanya, na yatapotea bure walio kuwa wakiyafanya**] [Suratul Huud /16].

Na tofauti ya huyu na wa kwanza, kuwa wa kwanza amekusudia asifiwe kuwa yeye ni mwenye kumuabudu Mwenyezi Mungu, ama huyu wa pili, hakukusudia kusifiwa kuwa ni mwenye kuabudu, na wala halitilii umuhimu jambo hilo.

**3**-Awe anakusudia kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, lakini na malengo mengine ya kidunia yapatikane ndani yake Mfano: Akusudie pamoja na Nia, kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kujitwaharisha, lakini pamoja na hilo pia kuchangamsha mwili na kuusafisha, na katika Swala kuufanyisha mazoezi mwili, na katika Swaumu kupunguza mwili na kutoa uchafu, na katika Hijja ili akaone sehemu za Hijja pamoja na Mahujaji, jambo hilo linapunguza malipo na Ihklas, lakini ikiwa kilicho zidi katika Nia yake ni kufanya Ibada, yatakuwa yamempita malipo kamili, lakini halito mdhuru hilo, amesema Mwenyezi Mungu kwa Mahujaji: [**Si vibaya kwenu kuzitafuta fadhila za Mola wenu.**] [Suratul Al-Baqara /198].

Na ikiwa Nia yake zaidi sio kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, atakuwa hana malipo ya Akhera,hakika malipo yake ni yale atakayo yapata duniani,na ninahofia kuwa atapata madhambi kwa hilo, kwa sababu ameifanya Ibada ambayo ndio lengo kuu,kuwa ndio njia ya kuipata dunia, na huyu ni kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Na miongoni mwao wapo wanao kusengenya katika kugawa sadaka. Wanapo pewa waohuridhika.Na wasipo pewa hukasirika**] [Suratul At-Tawba / 58].

Na katika Sunanu Abi Daud kutoka kwa Abu Huraira, kuwa Mtu mmoja alisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mtu anataka kupigana Jihadi, naye analengo katika malengo ya kidunia. Akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (**Hana malipo**) [Ameipokea Abu Daud /2516]. Yule Mtu akarudia mara tatu, na Mtume rehma na amani ziwe juu yake akanasema: (**Hana mali-**

**po**) na katika Sahihi mbili,kutoka kwa Omar Ibnu khatwab, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: (**Yule ambaye kuhama kwake ili kupata dunia au Mwanamke amuowe, basi kuhama kwake ni kwa ajili ya alohamia**) [Ameipokea Bukhar/1), na Muslim /1907].

Na kama itakuwa sawa nia yake, haikuzidi Nia ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu wala nia nyingine, hapo ni mahala pa kutizamwa, na lililo karibu ni kuwa hana thawabu, ni kama alofanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtu mwingine.

Na tofauti ya kigawanyo hiki na vingine vilivyo tangulia, kuwa malengo yasiyo kuwa ya kuabudu katika vigawanyo vilivyo pita, vimepatikana kwa dharura, kutaka kwake ni kutaka kulikotokea kwa matendo ya dharura, kana kwamba ametaka kufanya matendo kwa ajili ya dunia.

**Ikiwa kutasemwa:** Ni kipi kipimo katika hiki kigawanyo, kuwa makusudio ya nia hapa ni kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na yasiyo ya kujikurubisha kwake?

**Tutasema:** Kipimo ni ikiwa hatilii umuhimu isipokuwa Ibada hayo mambo mengine yametokea au hayakutokea, hakika itakuwa imefahamisha kuwa niya yake zaidi ilikuwa ni kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, na ikiwa kinyume na hapo, tunajua kuwa nia yake siyo kujikurubisha kwake.

Katika hali yoyote ile hakika jambo la Niya ni jambo kubwa, na ni jambo la hatari, linaweza kumpandisha Mtu mpaka kwenye daraja la Watu wakweli, na linaweza kumshusha akawa chini ya walio chini. Wamesema baadhi ya wema waliotangulia Mwenyezi Mungu awarehemu**: ((Sikuwahi kupigana Jihadi na nafsi yangu zaidi, kuliko kupigana nayo katika Ikhlas)).** Tunamuomba Mwenyezi Mungu kwetu na kwenu Ikhlas katika Niya na matendo mema.

****

## Swali la 22: Ni upi mwenendo wa Ahalu Sunna Waljamaa, katika kutaraji na kukhofu?

**Jibu:** Wametofautiana wana chuoni, Mwenyezi Mungu awarehemu. Je Mwanadamu atangulize kutaraji au atangulize kuhofu? Amesema Imamu Ahmad, Mwenyezi Mungu amrehemu **((Inatakiwa iwe khofu yake na kutaraji kwake ni kumoja, isishinde khofu wala isishinde kutaraji))** na **akasema ((Yoyote itakayo shinda basi ameangamia mwenye Nafsi hiyo))** kwa kuwa ikishinda kutaraji Mwanadamu ataangukia katika kujipa matumaini kutokana na adhabu za Mwenyezi Mungu, na iwapo khofu itashinda ataangukia Mwanadamu katika kukata tama na Rehema za Mwenyezi Mungu.

Na wamesema baadhi ya Wana chuoni Mwenyezi Mungu awarehemu**: ((Inatakiwa kutaraji kushinde khofu kama Mtu ni mwenye kufanya Ibada, na inatakiwa khofu ishinde wakati wa kufanya Maovu))** kwa sababu akifanya Ibada hakika amefanya kitu ambacho inatakiwa awe na dhana nzuri, inatakiwa kutaraji kushinde, nako ni kukubaliwa Matendo yake, na anapo kusudia kufanya Maovu inatakiwa khofu ishinde ili asiangukie kwenye kumuasi Mwenyezi Mungu.

Wakasema wengine**: ((Inatakiwa kwa Mtu mzima, khofu ishinde, na kwa Mtu mgonjwa kutaraji kushinde))** kwa sababu Mwenye afya nzuri ikishinda upande wa khofo basi atajiepusha na Maovu, na Mgonjwa ukishinda upande wa kutaraji atakutana na Mola wake hali ya kuwa ana dhana nzuri kwake.

Na kile nilicho kuwa nacho katika mas-ala haya: Hakika hii inatofautiana kwa kutofautiana hali, kuwa utakapo kuwa upande wa khofu umezidi, na akaogopa kukata tama na Rehema za Mwenyezi Mungu, ni waJibu kwake kurudi, kwa kuikabili hali hiyo kwa kutaraji, na pindi atakapo ogopa itakapo shinda upande wa kutaraji, kujipa matumaini na adhabu za Mwenyezi Mungu, ni waJibu kwake kurudi kwa kutanguliza khofu, na Mwanadamu kiuhakika ni mzuri wa Nafsi ikiwa Moyo wake utakuwa hai, ama ambaye Moyo wake ni Maiti, ambaye hautibu Moyo wake,na wala haangalii hali ya Moyo wake huyu halimuhusu jambo hili.

****

**Swali la 23: Je kufanya sababu kunapingana na kumtegemea Mwenyezi Mungu? kuna baadhi ya Watu wakati wa vita vya Khaliji walijitengenezea sababu za kujikinga wasidhurike na wengine wakaacha na wakasema: Hakika wao ni wenye kumtegemea Mwenyezi Mungu.**

**Jibu**: Kitu kilicho muhimu kwa Muumini ni kuuegemeza Moyo wake kwa Mwenyezi Mungu, na awe mkweli katika kumtegemea Mwenyezi Mungu, katika kuleta manufaa na kuondoa madhara, kwani hakika Mwenyezi Mungu peke yake katika Mikono yake ndio kuna ufalme wa mbingu na ardhi, na kwake hurejeshwa mambo yote, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Ni vya Mwenyezi Mungu tu vyote vilivyo fichikana katika ardhi na mbingu, na mambo yote yatarejeshwa kwake. Basi muabudu yeye na umtegemeeYeye. Na Mola wako haghafiliki na yale mnayo yatenda**] [Suratul Hud: 123]. Na alisema Musa Rehema na Amani ziwe juu yake kwa watu wake: [**Na Mussa alisema: Enyi watu wangu ikiwa nyinyi mmemuamini Mwenyezi Mungu basi mtegemeeni Yeye, ikiwa nyinyi ni Waislamu /84 Wakaema Tumemtegemea Mwenyezi Mungu. Ewe Mola wetu! Usitufanye wenye kutiwa misukosuko na hao watu madhalimu /85 Na utuokoe kwa rehema yako na watu makafiri**] [Suratul Yunus].

Na amesema Mwenyezi Mungu: [**Na kwa Mwenyezi Mungu wategemee Waumini**] [Suratul Al-Imaran: 160], na amesema tena Mwenyezi Mungu: [**Na mwenye kumtegemea Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu atamtosheleza hakika Mwe-**

**nyezi Mungu anatimiza amri yake. Amejalia kila kitu na kipimo chake**] [Suratul Al Twalaaq: 3]. Ni waJibu kwa Muumini amtegemee Mola wake, ambaye ni bwana wa mbingu na ardhi hali ya kuwa anadhana nzuri kwa Mola wake, lakini afanye sababu za kisheria na za kiqadari ambazo ameamrisha Mwenyezi Mungu kuzifanya kwa sababu kuchukua sababu ni kwenye kuleta kheri na ni kwenye kuzuia shari, ni katika kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu na hekma zake, na wala hakupingani na kumtegemea Mwenyezi Mungu, huyu hapa Bwana wa wategemezi kwa Mwenyezi Mungu Muhammad rehma na amani ziwe juu yake alikuwa akifanya sababu za kisheria na kiqadari, alikuwa akijikinga kwa Mwenyezi Mungu wakati wa kulala kwa kusoma Suratul Ikhlasi pamoja na Suratul Naas na Suratul Falaq, na alikuwa akivaa kofia ya chuma wakati wa vita, na alichimba Mahandaki Madina wakati walipo kusanyika makundi ya Washirikina; kwa jili ya kujihami na Washirikina, na hakika amejalia Mwenyezi Mungu kitu atakacho jikinga nacho Mja wakati wa vita, na hii ni katika neema za Mwenyezi Mungu ambazo

tunastahiki kumshukuru juu ya Neema hizo akasema Mwenyezi Mungu kuhusu Nabii Daud Rehema na Amani ziwe juu yake: [**Na tukamfundisha kutengeneza mavazi ya vita kwa ajili yenu ili yakuhifadhini katika kupigana kwenu. Je mtakuwa ni wenye kushukuru**?] [Suratul Al-Anbiyai: 80]. Hakika Mwenyezi Mungu alimuamrisha Nabii Daud atengeneze vizuri nguo zake za chuma kwa ajili ya vita; kwa sababu hizo ni zenye kukinga vizuri.

Kutokana na hivyo hakika watu wa miji ya karibu ambako kumetokea vita, na wanaogopa kupatwa na athari za vita hapana ubaya juu yao kutoka katika miji yao hali ya kuwa wamejikinga na

vitu mbalimbali ili wasipatwe na athari za vita; kwa sababu hizo ni katika sababu za kujikinga na shari, na wala hapana juu yao ubaya kujiwekea chakula ambacho wanadhani baadae wanaweza kukihitaji na wasikipate, na kila inapo zidi hofu, ndivyo inavyo kuwa kuchukua tahadhari inavyo zidi.

Lakini ni lazima kutegemea kwao kuwe ni kwa Mwenyezi Mungu, wazitumie sababu hizi kama tu ilivyo amrisha sheria ya Mwenyezi Mungu na hekima zake; kwa kuwa ni sababu ambazo Mwenyezi Mungu ameturuhusu kuzitumia, sio kwamba zenyewe ndio asli ya kuleta manufaa na kuondosha madhara, na wamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwafanyia wepesi, mfano katika sababu hizi, na akawaruhusu kuzitumia.

Nina muomba Mwenyezi Mungu atukinge wote, na sababu za fitna na maangamivu, na atuhakikishie sisi na ndugu zetu Imani yenye nguvu pamoja kumtegemea Yeye, pamoja na kuchukua sababu ambazo ameturuhusu kwa namna ambayo anairidhia kwetu sisi hakika Yeye ni Mwingi wa kutoa na Mkarimu. Mwisho Rema na Amani zimshukie Mtume wetu rehma na amani ziwe juu yake na Maswaba zake wote.

****

**Swali la 24: Ni nini hukumu ya kujiegemeza katika sababu?**

**Jibu:** Kujiegemeza katika sababu kuna vigawavyo:

**1**-Kuna ambayo inapingana na Tauhidi katika asili yake, nayo ni Mwanadamu kutegemea kitu ambacho hakina athari kwake, na anakikitegemea kikamilifu hali ya kuwa amemuacha Mwenyezi Mungu, mfano: Kutegemea Ibada za makaburi kwa kuwaomba waliomo katika makaburi hayo wakati wa kupatwa na matatizo, na hii ni Shiriki kubwa inayo mtoa Mtu katika Uislamu, na hukumu ya mwenye kufanya ni kama alivyo itaja Mwenyezi Mungu katika maneno yake: [**Hakika mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika amemharamishia Mwenyezi Mungu Pepo, na makazi yake ni Motoni. Na madhalimu hawana wa kuwanusuru**] [Suratul Al-Maaida /72].

**2**-Kutegemea katika sababu ya kisheria na sahihi, lakini ameghafilika na mwenye kusababisha, ambaye ni Mwenyezi Mungu, na hii ni katika aina za Shirki, lakini haimtoi mtu katika Uislamu, kwa sababu ameegemea katika sababu akasahau mwenye kusababisha ambaye ni Mwenyezi Mungu.

**3**-Ajiegemeze katika sababu, kujiegemeza kwa kuwa ni sababu tu, pamoja na kutegemea kwa asli kwa Mwenyezi Mungu, anaitakidi kuwa hizi sababu ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na kama

atataka Mwenyezi Mungu ataikata, na kama atataka ataibakiza na kwamba hakuna athari za sababu katika matashi ya Mwenyezi Mungu, hii haipingani na Tauhidi sio kwa asili wala ukamilifu.

Pamoja na kupatikana sababu za kisheria na sahihi, inatakikana kwa Mwanadamu asiegemeze nafsi yake katika sababu, bali ategemee kwa Mwenyezi Mungu, mfanyakazi ambaye anategemea mshahara wake kuutegemea kikamilifu, pamoja na kughafilika na mwenye kusababisha, ambaye ni Mwenyezi Mungu, hii ni aina ya Shiriki, ama atakapo tegemea mshahara wake na kujua kuwa msababishaji mkuu ni Mwenyezi Mungu, hii haipingani na kutegemea, kwani Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akichukua sababu pamoja na kuamini kuwa msababishaji mkuu ni Mwenyezi Mungu Mtukufu.

****

**Swali la 25: Ni ipi hukumu ya Ruqyah? Na ni ipi hukumu ya kuandika maandishi ya Aya katika shingo ya Mgonjwa?**

**Jibu**: Ruqyah ya mgonjwa aliyepatwa na uchawi au kitu chochote kingine miongoni mwa Maradhi, haina ubaya ikiwa ni kwa Qur`ani Tukufu, au katika Dua zilizo sahihi, hakika imethibiti kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa alikuwa aki-

wafanyia Ruqyah Mashahaba zake, na katika Dua alizo kuwa akitumia ni: ((**Ewe Mola wetu mlezi uliye mbinguni, limetukuka jina lako, amri zako ziko mbinguni na ardhini, kama zilivyo kuwa Rehema zako ziko mbinguni zifanye pia katika ardhi, na teremsha Rehema katika Rehema zako, na Umponyeshe Kwa uponyeshaji wako Mgonjwa huyu**)) [Ameipokea Abu Daud/3892/ na anapona.

Na katika Dua ambazo zimepolewa **((Kwa jina la Mwenyezi Mungu. Nina kufanyia Ruqyah kwa kila ugonjwa unao kuudhi, na shari ya kila nafsi au kijicho cha mwenye husda,Mwenyezi Mungu akuponyeshe,kwa jina la Mwenyezi Mungu nakufanyia Ruqyah))** [Ameipokea Muslim].

Na pia vilevile aweke mkono wake katika sehemu yenye maumivu ambayo inamuuma katika mwili wake na aseme: ((**Nakukinga kwa Mwenyezi Mungu kwa nguvu zake na shari ambazo mimi sizioni na kuzihofia**)) [Ameipokea Muslim /2186].

Na nyingine zisokuwa hizo ambazo wamezitaja wana wa vyuoni, Mwenyezi Mungu awarehemu, katika Hadithi ambazo zimepokelewa kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake :

Ama kuandika Aya na nyiradi na kuzivaa, hakika wametofautina wana vyuoni, Mwenyezi Mungu awarehemu, katika hilo Kuna miongoni mwao walio ruhusu, na miongoni mwao wamekataza,

na ambalo lipo karibu na haki kukataza hilo kwa sababu hilo halikupokelewa kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Kilicho pokelewa kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ni kumsomea Mgonjwa, ama kumtundikia Mgonjwa katika shingo yake, au mkono wake, au katika mto wake, na vinavyo fanana na hivyo, hakika hilo ni katika jambo lilokatazwa, katika kauli yenye nguvu kwa sababu ya kutopokelewa kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake: kila Mwanadamu atakaye lifanya jambo ni sababu ya jambo lingine, bila ya ruhusa ya kisheria, hakika tendo lake hilo huhesabiwa ni aina katika aina za Shirki kwa sababu ni kuthibitisha sababu ambayo Mwenyezi Mungu hakuijalia kuwa ni sababu.

****

### Swali la 26: Je Ruqyah inapingana na (Tawakul) kumtegemea Mwenyezi Mungu?

**Jibu**: Tawakul: Ndio ukweli wa kumtegemea Mwenyezi Mungu katika kuleta manufaa, na kuondosha madhara pamoja na kufanya sababu ambazo ameamrisha Mwenyezi Mungu kwazo, na sio kumtegemea Mwenyezi Mungu bila kufanya sababu, hakika kumtegemea Mwenyezi Mungu bila kufnya sababu, ni kufanya utani kwa Mwenyezi Mungu, na katika hekima zake; kwa sababu Mwenyezi Mungu amefungamanisha mwenye kusababisha na sababu zake.

**Na hapa kuna swali**: Ni nani katika watu mwenye kumtegemea Mwenyezi Mungu zaidi?

**Jibu**: Ni Mtume wetu rehma na amani ziwe juu yake, Je alikuwa akifanya sababu ambazo humkinga na madhara?

**Jibu**: Ndio, alikuwa anapo toka kwenda vitani huvaa kofia ya chuma ili kujikinga na Mishale, na katika vita vya Uhudi alivaa Dirii mbili (nguo ya kivita ) [Ameipokea Abu Daud/ 2590/, na Ibnu Maja /2806], yote hayo ni kujiandaa kwa kitu ambacho kinaweza kutokea, na kujitengenezea sababu hakupingani na kumtegemea Mwenyezi Mungu, atakapo tegemea Mwanadamu hizi sababu kwa kuzitegemea tu na kuwa hazina athari yoyote isipokuwa idhini ya Mwenyezi Mungu, kwa hiyo kusoma Mwanadamu juu ya nafsi yake au kumsomea ndugu yake Mgonjwa hakupingani na kumtegemea Mwenyezi Mungu.

Hakika imethibiti kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa alikuwa akiifanyia Ruqyah nafsi yake kwa kusoma Muawidhatain (Surat Nasi na Surat Falaq) [Ameipokea Bukhari /4439), na Muslim /2192] na imethibiti kuwa alikuwa akiwasomea Maswahaba zake walipo kuwa wagonjwa. Mwenyezi Mungu ndie mjuzi zaidi.

****

**Swali la 27: Ni ipi hukumu ya kutundika au kuvaa Hirizi na vizuizi (Vikuku)?**

**Jibu**: Haya masuala yamegawanyika katika sehemu mbili:

**1**-Iwe kilicho tundikwa ni katika Qur`an, na hakika wametofautiana wana chuoni, wa zamani na walio kuja baada yao.

Kuna miongoni mwao walio ruhusu hilo, na wakaona kuwa linaingia katika maneno yake Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Na hatukuiteremsha Qur`an isipokuwa ni ponyo na ni rehema kwa Waumini**] [Suratul Al-Israa /82] na maneno yake Mwenyezi Mungu: [**Kitabu Tumekishusha kwako ni chenye baraka**] [Suratul Swadi 29]. Na kwamba katika baraka zake ni kutundikwa ili iondoshe vitu vibaya.

Na kuna miongoni mwao wamekataza hilo, na wakasema: Hakika kuitundika hakukuthibiti kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kuwa ni sababu ya kisheria huondoshwa kwayo mambo mabaya, na asli ya vitu kama hivi ni kuvinyamazia. Na hii ndio kauli yenye nguvu, ya kuwa haifai kutundika hirizi hata kama itakuwa ni katika Qur`an, na wala haifai pia iwekwe kwenye mto wa mgonjwa, au kuitundika katika ukuta, na yanayo fanana na hayo, hakika anatakiwa amuombee mgonjwa na amsomee moja kwa moja kama alivyo kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake akifanya.

**2**-Iwe chenye kutundikwa sio katika Qur`an, katika vitu ambavyo havifahamiki maana yake, hakika hivyo havifai kwa hali yoyote, kwa sababu haijulikani vinaandika kwa kitu gani, kwani hakika baadhi ya watu huandika talasimu na vitu vyenye kutundikwa kwa herufi zinazo ingiliana, na hukaribia kutojulikana, na nyingine hazisomeki, hakika hii ni katika bidaa iliyo haramishwa, na wala haifai kwa kila yoyote. Mwenyezi Mungu ndie mjuzi zaidi.

****

**Swali la 28: Je inafaa kuandika baadhi ya Aya katika Qur`an Tukufu, Mfano Ayat Kursiy katika chombo cha chakula au kinywaji kwa lengo la kujitibu?**

**Jibu**: Ni lazima tujue kuwa Kitabu cha Mwenyezi Mungu ni kitukufu na ni cha kuheshimiwa, na si kufanyiwa udhalili kwa kiasi hicho. Ni vipi inaweza Nafsi ya Muumini, akifanye Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Aya Tukufu kama Ayatul Kursiy, aiweke kwenye chombo na anywe ndani yake, akifanyie udhalilifu, na akitupetupe ndani ya Nyumba Watoto wachezee?! Kitendo hiki hakuna shaka kuwa ni haramu, na kwamba ni wajibu kila mwenye kuwa na chombo kama hiki, afute Aya hizo, aende kwa mwenye kuweza kufuta afute, na kama hawezi hilo ni lazima kwake akichimbie shimo katika sehemu iliyo Twahara kisha akizike humo.ama kukiacha katika hali hiyo ya udhalili, watoto wanakunywa ndani yake, na wanacheza nacho, hakika uponyaji kwa Qur`an kwa njia hii

haikupokelewa kutoka kwa wema walio tangulia, rehema na Amani ziwe juu yao.

****

**Swali la 29: Wanajifunza wanafunzi wa Madrasa katika baadhi ya Miji ya Kiislamu, kuwa Msimamo wa Ahlu Sunna Waljamaa ni ((Kuamini Majina yake, na Sifa zake, bila Kugeuza wala Kuziacha, wala kuziwekea namna, wala Kuzifananisha)). Je kugawanya Ahalu Sunna katika vigawanyo viwili: Madrasa ya Ibnu Taymiyah na Wanafunzi wake, na Madirasa ya Al-Ashaira na Al-Maturudia vigawanyo hivi ni sahihi?. Na ni upi msimamo wa Muislamu kwa Wanazuoni wenye kufanya Taawili?**

**Jibu:** Hakuna shaka kuwa wanayo jifunza Wanafunzi katika Madrasa kuwa Msimamo wa Ahalu Sunna ni (Kuamini Majina yake, na Sifa zake, bila Kugeuza wala Kuziacha, wala kuziwekea namna, wala Kuzifananisha). Hivyo ndivyo inavyo afikiana na Msimamo wa Ahalu Sunna, kama inavyo shuhudiwa katika vitabu vyao ilivyo kwa urefu na ilivyo fupishwa, nayo ndio haki iliyo afikiana na yale yalokuja katika Kitabu na Sunna, na Maneno ya wema walio tangulia, na huo ndio mtizamo Sahihi, na akili iliyo wazi, na hatulazimiki kuleta Ushahidi kwa kuwa Muulizaji hajataka hivyo, hakika si vinginevyo,tujibu swali alotaka, nalo ni kugawanya Ahlu Sunna katika makundi mawili katika Madrasa mbili:

Ya kwanza: Madrasa Ibnu Taymiyyah na Wanafunzi wake, Mwenyezi Mungu awarehemu, wanao kataa kuubadili ushahidi na dhahiri yake.

Na ya pili: Madrasatul Al-Ashaaira na Al- Maturudia, ambao wanaruhusu kubadili ushahidi katika dhahiri yake kwenye Majina ya Mwenyezi Mungu na Sifa zake.

**Tunasema**: Ni kitu kinajulikana kuwa katika Madrasa mbili hizi, kuna Ikhitilafu ya wazi katika Manhaji kuhusu majina ya Mwenyezi Mungu na Sifa zake.

Madrasa ya kwanza inawalazimisha Walimu wake kuwa ni lazima kubakiza ushahidi katika dhahiri yake, katika yanayo husiana na Majina ya Mwenyezi Mungu na Sifa zake, na kukataa yale ambayo yanapaswa kukataliwa yanayo muhusu Mwenyezi Mungu, katika Kufananisha,au kuweka namna.

Na Madrasa ya pili wanawalazimisha walimu wao, ni lazima kubadili ushahidi kutoka katika dhahiri yake, katika yanayohusu, Majina ya Mwenyezi Mungu na Sifa zake.

Hizi njia mbili zimetofautiana sana, na itadhihiri tofauti yake katika mifano ifuatayo:

Amesema Mwenyezi Mungu: [**Bali mikono yake imekujuka hutoa vile atakavyo**] [Suratul Al-Maida /46]. Na akasema akimuelezea Iblisi hali ya kumsimanga wakati alipo kataa kumsujudia Adamu kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Amesema Mwenyezi Mungu: [**Akasema Ewe Iblisi ni kipi kilicho kuzuiya kumsujudua kwa yule niliye muumba kwa mikono yangu**] [Suratul Swad /75].

Hakika wametofautiana Walimu wa Madrasa mbili hizi, katika makusudio ya Mikono miwili, ambayo ameithibitisha Mwenyezi Mungu katika Nafsi yake.

Wakasema watu wa Madrasa ya Kwanza: Ni wajibu kubakisha maana zake katika dhahiri yake, na kuithibitisha mikono miwili ya hakika kwa Mwenyezi Mungu, katika hali inayo lingana na utukufu wake.

Na wakasema watu wa Madrasa ya pili: Ni wajibu kubadili maana zake kutoka katika udhahiri wake, na ni haramu kuthibitisha mikono miwili ya uhakika kwa Mwenyezi Mungu, kisha wakatofautiana makusudio ya mikono hiyo miwili. Je ni nguvu au neema.

Kwa mfano huu, imebainika njia ya watu wa Madrasa mbili, zenye kuhitalafiana na kutofautiana, na wala haiwezekani baada ya tofauti hizo ziwe pamoja katika sifa moja ya (Ahalu Sunna).

Kwa ajili hiyo, hakuna budi kuwa sifa za Ahalu Sunna kuwa ni maalumu kwa kundi moja bila kundi lingine, na tuhukumu kati ya makundi mawili haya kwa uadilifu, na tuyaweke katika mizani ya uadilifu, nayo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume rehma na amani ziwe juu yake  na maneno ya Maswahaba na wenye kuwafuata kwa wema katika umma zilizo pita.

Na hakuna katika mizani hii, kinacho onesha kwa kile walichoenda nacho watu wa Madrasa ya pili, bali katika mizani hii, kuna ushahidi wa wazi, au za dhahiri, au kuashiria kwa kile walicho kwenda nacho watu wa Madrasa ya kwanza.

Na kwa ajili ya hayo, inabainika ya kuwa sifa za Ahlu Sunna ni maalumu kwa wao, hawashirikiani watu wa Madrasa ya pili, kwa sababu kuhukumu kushirikiana ni dhulma, na kukusanya vitu ambavyo ni tofauti havikutani na dhulma imekataliwa kisheria, na kukusanya vitu ambavyo havikutani haikubaliki kiakili.

Ama kauli ya watu wa Madrasa ya pili (wenye kubadili): kuwa hakuna ubaya kubadili Majina ya Mwenyezi Mungu na sifa zake, iwapo hakuta pingana na ushahidi wa Kisheria.

Tunasema; kule kubadili neno kutoka katika maana yake ya dhahiri bila Ushahidi ya kisheria, ni kwenda kinyume na ushahidi, na ni kumsemea Mwenyezi Mungu bila kuwa na elimu, na hilo ameliharamisha Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Sema:Mola**

**wangu ameharamisha mambo machafu ya dhdhiri na ya siri, na dhambi na uasi bila ya haki na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na asicho kiletea uthibitisho na kumzulia Mwenyezi Mungu na msiyo yajua**] [Suratul Al-araaf /33]. Na maneno yake: [**Wala usiyafuate usiyo na elimu nayo. Hakika masikio, na macho, na moyo hivyo vyote vitaulizwa**] [Suratul Al-Israai /36].

Na hawa wenye kubadili majina ya Mwenyezi Mungu na sifa zake, hawana elimu kwa yale waloyabadili, wala mtizamo wenye kuingia akilini, isipokuwa ni shubha ambazo huzitolea hoja, na kisha hupingana zenyewe kwa zenyewe,na inawalazimu kupunguza katika Dhati ya Mwenyezi Mungu na sifa zake na wahai wake, zaidi kuliko walivyo zua katika kuyathibitisha katika dhahiri yake, na hapa sio sehemu ya kueleza kwa upana sana juu ya hilo.Hakika makusudio hapa ni kubainisha sifa za Ahalu Sunnahh, kuwa haziwezi kupewa makundi mawili yenye kubadili njia zake upeo wa kubadili,na hakika anastahili yule ambaye maneno yake yanaafikiana na Sunna tu, na hakuna shaka kuwa watu wa Madrasa ya kwanza sio wenye kubadili, sifa za haki zilizo tajwa kama walivyo badili watu wa Madrasa ya pili, na mwenye kuangalia katika njia zake kwa elimu na usawa, haifai kuwagawanya watu wa Sunna katika makundi mawili, bali wao ni kundi moja.

Ama kutolea ushahidi kwao maneno ya Ibnu Al-jauzi katika mlango huu, tunasema: Maneno ya wana wa wachuoni huwa yanahitaji ushahidi na wala hayawi ushahidi, na maneno ya mwanachuni mmoja hayawi ushahidi kwa wengine.

Ama maneno yao kuwa Imamu Ahmad alibadilisha katika Hadithi ((**Miyo ya wanadamu ipo kati ya vidole viwili miongoni mwa vidole vya Arhamani**)) na Hadithi ((**Jiwe jeusi ni Mkono wa kulia wa Mwenyezi Mungu katika ardhi**)). Na maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema [**Nae yupo pamoja na nyinyi popote mtakapo kwenda**] [Suratul Hadidi/ 4].

Tunasema: Haikusi kwa Imamu Ahmad kuwa alibadili hizo Hadithi mbili zilizo tajwa. Amesema Sheikhul Islam Ibnu Taymiya katika [Fatawa/5/398/ katika Ibnu Qasimu]: ((Na ama alioyasimulia Abu Hamid  Al-Ghazali kuwa Ahmad hakubadili isipokuwa vitu vitatu: ((**Jiwe jeusi ni Mkono wa kulia wa Mwenyezi Mungu katika ardhi**)).

Na ((**Mioyo ya wanadamu ipo kati ya vidole viwili miongoni mwa vidole vya Al Rahmani**)) na ((**Mimi naiona Nafsi ya Rahamani upande wa Yeman**)).

Hizi simulizi zote ni uongo kwa Imamu Ahmad,hakuinakili yoyote kutoka kwake kwa sanadi, na wala hajulikani yoyote katika watu wake amenukuu hilo kwake.)) yameisha maneno yake.

Ama maneno ya Mwenyezi Mungu [**Nae yupo pamoja na nyinyi popote mtakapo kwenda**]. Hakika Imamu Ahmad hakubadili lakini alitafsiri, kwa baadhi ya vitu vinavyo lazimiana navyo, nayo ni ujuzi, kuwafanyia radi Aljahamia, ambao walitafsiri

kinyume na makusudio yake, wakati walipo zua, kuwa inaonesha kuwa Mwenyezi Mungu yupo kila sehemu kwa Dhati yake-ameepukana Mwenyezi Mungu na maneno yao-Akabainisha hilo Mwenyezi Mungu amrehemu, amrehem kuwa upamoja hapa ni upamoja kwa maana ya kuvizunguka viumbe katika jumla yake kuvijua kwa ujuzi wake kwa sababu upamoja haulazimishi kuwa pamoja na kuchanganyikana, bali katika kila sehemu na Maana yake, na kwa ajili hii husemwa:Ameninywesha maziwa pamoja na Maji. Na husemwa: Nimeswali pamoja na jamaa. Na husemwa: Fulani pamoja na mkewe.

Katika mfano wa kwanza: Inaonesha, kuwa pamoja na kujichanganya, na wapili:inaonesha kushirikiana katika sehemu na matendo bila ya kuchanganyikana, na watatu: Inaonesha kuwa pamoja hata kama hakuna kushirikiana katika sehemu na matendo, itakapo bainika kuwa, kuwa pamoja kunatofautiana kutokana na kuegemezwa kwake, hakika kuwa pamoja kwa Mwenyezi Mungu na viumbe wake, kunatofautiana na kuwa pamoja kwa viumbe wake, na wala haiwezekani kuwa pamoja kwa Mwenyezi Mungu, kukahukumiwa kuwa amejichanganya na viumbe wake, au anashirikiana nao katoka sehemu, kwa sababu hilo haliwezekani kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuwa imethibiti utofauti wake na viumbe wake, na kuwa kwake yupo juu yao.

Na kwa ajili hiyo, anakuwa pamoja nasi Naye yupo katika kiti cha enzi juu ya mbingu, kwa sababu anatuzunguka sisi kwa ujuzi wake, na uwezo wake, na kwa utawala wake, na kwa kusikia kwake, na kwa kuona kwake, na kwa mpangilio wake, na men-

gine yasiyo kuwa hayo yanayo onesha Uleziwake na Uumbmbaji wake, kwa hivyo atakapo tafsiri mwenye kutafsiri kwa (Ujuzi) anakuwa hakutoka katika maana yake halisi, na anakuwa si mwenye kubadili, isipokuwa kwa mwenye kufahamu kuwa Upamoja ni kushirikiana katika sehemu au kuchanganyikana kwa kila hali.

Na haya ndio tunayo yasema kuhusu Imamu Ahmad, Mwenyezi Mungu amrehemu, katika kubadili huu ushahidi wa aina tatu.

Ama kwa kuangalia katika Aya, hakika imetangulia kuwa hakuna kubadili katika Aya ile tukufu, pindi atakapo tafsiri mwenye kutafsiri kwa elimu(ujuzi), kwa sababu hiyo ni tafsiri yake kwa baadhi ya mambo, hatusemi ndio maana yake, bali ni katika maana zake.

Ama katika Hadithi: ((**Mioyo ya wanadamu ipo kati ya vidole viwili miongoni mwa vidole vya Arhamani ni kama moyo mmoja anauendesha vile atakavyo**)) hakika ameipokea Muslimu katika sahihi yake katika kitabu Alqudra, na katika mlongo wa tatu namba /17/ ukurasa /2045/. Hakuna kubadili ndani yake kwa Ahlu Sunna, kwa kuwa wao wanaamini kile kilicho semwa kuwepo vidole kwa Mwenyezi Mungu, katika hali ambayo inalingana Naye, na wala haiwajibishi kuwa, kwa kuwa Miyo yetu ipo katika vidole vyake iwe inagusika; hakika Mawingu yapo kati ya mbingu na ardhi lakini hayagusi mbingu wa ardhi, hivyo hivyo Nyoyo za wanadamu zipo katika vidole viwili vya Mwenyezi Mungu katika

vidole Arahamani, na wala haliwajibishi hilo kuguswa.

Ama Hadithi: ((**Jiwe jeusi ni Mkono wa kulia wa Mwenyezi Mungu katika ardhi**)) [Ameipokea Ibnu Adiyi kwa ukamilifu/342/1].

Hakika amesema Sheikhul Islaam Ibnu Taymiyah katika [Fatawa/6/397/ katika Majumuu Ibnu Qasimu]. Hakika imepokewa kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa Sanadi ambayo imethibiti, na ni Mashuhuri, hakika si vinginevyo ni kutoka kwa Ibnu Abas Amesema: ((**Jiwe jeusi ni Mkono wa kulia wa Mwenyezi Mungu katika ardhi, yule atakaye ligusa kwa mkono wake na akalibusu, ni kana kwamba amempa mkono Mwenyezi Mungu na akaubusu mkono wake wa kuliya**)) [ameipokea Abdurazaq / 8919].

Na katika[3/44/ kutoka katika Majuumuu Al-Madhikur]: ((Ameweka wazi kuwa jiwe jeusi sio lenyewe ni sifa ya Mwenyezi Mungu na wala sio lenyewe ndio mkono wake wa kuliya kwa sababu yeye amesema **((Ni mkono wa kulia wa Mwenyezi Mungu katika Ardhi)),** amewekea mipaka katika ardhi na hakuweza kuwa ni kila sehemu, anasema: Ni mkono wa kulia wa Mwenyezi Mungu, na hukunu ya neno ambalo lina mipaka linatofautiana na lisilo na mipaka)). Na akasema: ((yule atakaye ligusa kwa mkono wake na akalibusu, ni kana kwamba amempa mkono Mwenyezi Mungu na akaubusu mkono wake wa kuliya)), ni kitu kinajulikana kuwa, chenye kufananishwa sio sawa na kile cha asili)) yameisha maneno yake.

Nikasema: Kwahiyo haziwi Hadithi katika sifa za Mwenyezi Mungu ambazo zimebadiliswa katika maana ambayo zinatofautiana na dhahiri, hakuna kubadilisha ndani yake kabisa.

Ama kuhusu maneno yao: Kuwa kuna Madrasa mbili: Ya kwanza ni Madrsa ya Ibn Taymiyah, Mwenyezi Mungu amrehemu,kumesemwa imenasibishwa Madrasa hii na Ibnu Taymiya ili kuwazuga watu kuwa anacho kifanyahakija wahi kufanywa, na hili ni kosa; Hakika alokwenda nayo Ibn Taymiyah ni yaleyale walokuwa nayo wema walio tangullia, na viongozi wa Ummah, na sio kuwa yeye ndio amezua Madrasa hii, kama yanavyo onesha maneno ya msemaji, ambaye anataka alifanye dogo jambo lake, Mwenyezi Mungu ndio mwenye kutegemewa.

Ama msimamo wetu kutokana na Maulamaa wenye kubadili Tunasema: Mwenye kujulikana miongoni mwao kwa nia nzuri, na amekuwa na utangulizi mzuri katika Dini, na ni mwenye kufuata Sunnahh,basi yeye atakuwa ni mwenye udhuru endapo atabadili kubadili kwenye kukubalika, lakini udhuru wake huo hauta mzuiya kuwa amefuata njia ya wenye kwenda kinyume na wema walio tangulia, na kuifuata Ushahidi kama ilivyo elekeza, na kutegemea kile kilicho fahamishwa katika Ushahidi ya wazi, pasna kufananisha wala kuleta namna yake, kwani ni lazima kutofautisha kati ya maneno na msemaji, na kitendo na mtendaji, na maneno ya kimakosa yatakapo kuwa yametoka kwa kujitahidi, na makusudio mazuri, huwa hatukanwi mwenye kuyasema, bali anakuwa na malipo kwa kujitahidi kwake, kwa maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake ((**Atakapo hukumu Hakimu,akajitahidi**

**kisha akapatia basi ana malipo mawili, na atakapo hukumu, akajitahidi kisha akakosea anamalipo moja**)) [Ameipokea Bukhar/7352/na Muslimu1716].

Ama kumpa sifa ya kuwa ni mpotevu, ikiwa inakusudiwa kupotea kwa ujumla, ambako hutukanwa nako mwenye upotevu huo, na huchukiwa, hayo hayaelekezwi kwa mfano wa mtu huyu ambaye ni mwenye kujitahidi, ambaye imejulikana kutoka kwake kuwa ana Nia nzuri, na ana utangulizi mzuri katika Dini, na ufuataji mzuri wa Sunna, na iwapo utakusudiwa upotevu kwa kuacha kauli iliyo sawa, hakuna ubaya kwa hilo; kwa sababu mfano wa haya sio upotevu wa jumla;kwa kuwa ni njia ya kufika katika haki, kwa kuwa ametoa juhudi zake katika kutafuta haki, lakini kwa kuzingatia matokeo amepotea, kwa kuwa amekwenda kinyume na haki.

Na kwa ufafanuzi huu utaondoka mushkili. Mwenyezi Mungu ndiye msaidizi kwa kila jambo.

❋❋❋❋

**Swali la 30:Ni ipi Aqida ya Ahlu Sunnahh katika majina ya Mwenyezi Mungu na Sifa zake? na ni nini tofauti kati ya jina na sifa? je inalazimu mwenye kuthibitisha jina athibitishe sifa yake? na mwenye kuthibitisha sifa athibitishe jina?**

**Jibu**: Aqida ya Ahlu Sunnahh Waljamaa katika majina ya Mwenyezi Mungu na sifa zake ,ni kuthibitisha kile alicho kithibitisha Mwenyezi Mungu katika nafsi zake katika majina na sifa pasina kubadili,wala kuzizcha,wala kiziwekea namna,wala kuzifananisha.

Na tofauti kati ya jina na sifa ni: Jina ni lile aloitwa nalo Mwenyezi Mungu kwalo, na sifa Ni zile alosifiwa nazo Mwenyezi Mungu kwazo na kati yake kuna tofauti iliyo wazi.

Jina huzingatiwa kuwa ni alama kwa Mwenyezi Mungu,ilokusanya sifa Na inamlazimu mwenyenye kuthibitisha jina athibitishe na sifa, mfano wake**: [Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kusamehe mwenye huruma] (**ghafuru) ni jina linalo lazimiana na kusamehe, (Rahimu) linalazimisha kuthibitisha Rehema. Na wala hailazimu katika kuthibitisha sifa kuthibitisha jina, mfano( maneno) hailazimu tuthibitishe kwa jina la Mwenye kuongea, kutokana na hilo zinakuwa sifa ni kujufu zaidi; kwa sababu kila jina limekusanya sifa, na si kila sifa imekusanya jina.

****

**Swali la 31: Je majina ya Mwenyezi Mungu ni yenye kuhesabika?**

**Jibu**: Majina ya Mwenyezi Mungu si yenye kuhesabika kwa idadi maalumu, na Ushahidi ya hilo ni maneno yake Mtumerehma na amani ziwe juu yake katika Hadithi sahihi ((**Ewe Mola wangu, hakika mimi Mja wako, na ni Mtoto wa Mjakazi wako**,)) mpaka alipo sema: ((**Ninakuomba kwa kila jina ambalo ni lako, Umeitia kwayo Nafsi yako, au Umelishusha katika Kitabu chako, au Umemfundisha yoyote katika waja wako, au umelificha katika elimu ya siri ulokuwa nayo**)) [Ameipokea Ahmed/391/1].

Na yale aliyo yaficha Mwenyezi Mungu katika elimu ya siri, hayawezi kujulikana, na kitu ambacho hakijulikani si chenye kuhesabika.

Ama maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Hakika, Mwenyezi Mungu ana majina tisini na tisa,mwenye kuyahifadhi ataingia Peponi**)) [Ameipokea Bukhar /2736 / na Muslimu / 2677 ] Haina maana kuwa hana majina mengine ipokuwa hayo, lakini maana yake mwenye kuyaifadhi hayo tisini na tisa ataingia peponi. Na mfano wa maneno hayo ni maneno ya Waarabu wanapo sema: Nina Farasi mia moja nimewaandaa kwa ajili ya Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, haina maana kuwa hana wengine isipokuwa hao mia moja, bali hao miamoja wameandaliwa kwa kitu hicho tu.

Hakika amenuku Sheikh Islaam Ibnu Taymiyya, Mwenyezi Mungu amrehemu, wameafikiana watu wanao jua katika Hadithi, kuwa kuhesabika na kuyaorodhesha haikuswihi kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ( Majmuu fatawa).Na mwenye kujaribu kuisahihi Hadithi hii amesema: Hakika jambo hili ni jambo kubwa; kwa sababu humpelekea mtu kwenda Peponi, halikuwa pita Maswahaba kumuomba Mtume rehma na amani ziwe juu yake awabainishie, hilo linaonesha kuwa hayo majina yamebainishwa kutoka kwa Mtumerehma na amani ziwe juu yake: Lakini hujibiwa hilo Hakika hilo sio lazima, na lau kama engelikuwa hivyo, yengekuwa majina haya tisini na tisa yanajulikana zaidi kuliko jua na mwezi, na kasha lingepokelewa katika vitabu vya sahihi mbili na nyinginezo kwa sababu ni katika mambo ambayo watu wanahaja nayo sana, na hupupia katika kuyahifadhi, ni vipi haikupokelewa ispokwa katika njia moja na pia katika sura ambayo wametofautiana, Mtume rehma na amani ziwe juu yake, hakubainisha  kwa sababu ya hekma kubwa, nayo ni watu wayatafute katika Kitabu na Sunna, mpaka abainike mwenye kupupia katika kheri na asopupia katika kheri.

Na haikuwa maana ya kuyahifadhi kuyaandika, kisha kuyakariri na kuyahifadhi, lakini maana yake ni:

**1**-Kuyajua maneno yake.

**2**-Kuyafahamu maana yake.

**3**-Kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa majina hayo, na hilo linakuwa kwa namna mbili:

**1**-Kumuomba Mwenyezi Mungu kwa Majina hayo amesema Mwenyezi Mungu: [**Muombeni kwayo**] [Suratul Al-Imran /180], uyafanye kuwa ni njia ya kukufikisha kwenye matakwa yako, chagua jina ambalo linanasibiana na haja zako, wakati wa kuomba msamaha unatumia: Ewe mwenye kusamehe nisamehe, inakuwa sio sawa kuomba msamaha kwa kusema: Ewe mkali wa kuadhibu nisamehe, hii inakuwa kama kufanya istihizai na Mwenyezi Mungu, bali inatakiwa useme: Niweke mbali na adhabu yako.

**2**-Yawe yanakupitia katika ibada zako maana ya majina haya. Jina la Rahimu linamaanisha Rahma, mwenye kufanya jambo jema ambalo huleta Rehema za Mwenyezi Mungu, hii ndio maana ya kuyahifadhi, atakapo kuwa hivya atakuwa ni mwenye kustahiki wakati huo kuingia peponi.

****

**Swali la 32: Ni yapi Madhehebu ya wema walio tangulia Mwenyezi Mungu awarehemu, katika kuwa juu kwa Mwenyezi Mungu? Na ipi hukumu ya mwenye kusema: Mwenyezi Mungu yupo katika pande sita, na kuwa Yeye yupo katika moyo wa Muumini?**

**Jibu:** Madhehebu ya wema walio tangulia Mwenyezi Mungu awarehemu, ni kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa dhati yake yupo juu ya waja wake.na ameseama Mwenyezi Mungu mtukufu: [**Mkitatizana katika jambo basi rirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume ikiwa mnamuamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho. Na hayo ni bora zaidi na ndio yenye mwisho mwema**.] [Suratul An-Nisaa /59]. Na amesema tena Mwenyezi Mungu: [**Na mkikhitalifiana katika jambo lolote, basi hukumu yake ipo kwa Mwenyezi Mungu**] [Suratul Ash-Shuraa /10] na akasema tena Mwenyezi Mungu: [**Haiwi kauli ya Waumini wanapo itwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ili ahukumu baina yao, ila ni kusema: Tumesikia, na tumetii! Na hao ndio wenye kufanikiwa /51/. Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakamuogopa Mwenyezi Mungu na wakamcha, basi hao ndio wenye kufuzu**] [Suratul An-Nuur: 52].

Na amesema Mwenyezi Mungu: [**Haiwezekani kwa Muumini Mwanaume wala Muumini mwanamke kuwa na khiyari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapo kata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake hakika amepotea upotevu ulio wazi**]

[Suratul Al-Ahzab: 36]. Na amesema Mwenyezi Mungu [**Naapa kwa Mola wako! Hawata amini mpaka wakufanye wewe ndiye hakimu wao katika yale wanayo khitalifiana, kisha wasipate uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu uloitoa, na wanyenyekee kabisa**] [Suratul An-Nisaa: 65]. Itakapo bainika kuwa njia ya Muumini wakati wa kutofautiana ni kurudi kwenye kitabu cha Mwenyezi Mungu, na Sunna za Mtume wake, na kuwaskiliza na kuwatii, na kuto kuchagua zisizo kuwa amri zake, na kwa Imaani haiwi isipokuwa kwa hiyo, na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu kikamilifu, hakika kutoka katika njia hii kunamuwajibisha Mtu kwa yale aliosema Mwenyezi Mungu: [**Na mwenye kumpinga Mtume baada ya kumdhihirikia uongofu, na akatafuta njia isiyo kuwa ya waumini, tutamuelekeza aliko elekea, na tutamuingiza katika Jahanamu. Na hayo ndio marejeo mabaya**] [Suratul An-Nisaa: 115].

Kwa sababu hiyo utaona mwenye kufikiria vizuri katika masala haya-mas-ala ya kuwa Mwenyezi Mungu yupo juu ya viumbe wake kwa dhati- baada ya kurudisha kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume rehma na amani ziwe juu yake itambainikia kuwa Kitabu na Sunnahh zimebainisha ubainisho wa wazi kuwa Mwenyezi Mungu yupo juu ya Waja wake kwa dhati yake, kwa ibara tofauti miongoni mwake ni hizi:

1-Ni kuweka wazi kuwa Mwenyezi Mungu yupo juu ya mbigu kama maneno yake Mwenyezi Mungu: [**Au mnadhani mko salama kwa alioko juu kuwa Yeye hukupelekeeni kimbunga chenye changarawe? Mtajua vipi maonyo yangu**] [Suratul Al-

Mulku: 17], na maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake wakati akimfanyia Ruqiyyah Mgonjwa: ((**Mola wetu ni Mwenyezi Mungu ambaye yupo mbinguni**)), mpaka mwisho wa Hadithi.Ameipokea Abuu Daudi (Imetangulia takhariji yake).

Na maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake ((**Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake, hakuna mwanaume yoyote atakaye muita mke wake katika tandiko lake akakataa kuitikia wito wa mme wake, isipokuwa huwa ambaye yupo mbinguni ni mwenye kumkasirikia mpaka mume amridhie mke wake**.)) [Ameipokea Muslimu/ 1436].

**2**-Kuweka kwake wazi kuwa Yupo juu,kama alivyo sema: [**Naye ndiye mwenye nguvu juu ya waja wake,na ndiye mwenye hekima na mwenye khabari zote**] [Suratul Al-An,aam: 18], na maneno yake: [**Vinamkhofu Mola wao aliye juu yao na vinafanya vinanyo amrishwa.**] [Suratul A,-Nahl: 50].

Na maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Hakika Mwenyezi Mungu alipo maliza kuumba aliandika kwake juu ya Arsh Yake: Hakika huruma yangu imeitangulia hasira yangu**,)) [Ameipokea Bukhari/3194] na Muslimu: 2751].

**3**-Kuweka wazi kwake kuwa vitu vinapanda kwake na kushuka kutoka kwake,na kupanda hakuwi isipokuwa kwa juu, na kushuka hakuwi isipokuwa kwa kutoka juu kwenda chini,kama alivyo sema

Mwenyezi Mungu: [**Kwake Yeye hupanda neno zuri,na amali njema**. **kwendea kwake**]. [Suratul al-Maariji], na maneno yake: [**Anapitisha mambo yote yaliyo baina ya mbingu na ardhi, kisha yanapanda kwake**]. [Suratul As-Sajidah: 5], na pia maneno yake Mwenyezi Mungu: [**Hautaufikia upotevu mbele yake wala nyuma yake. Kimeteremshwa kwa mwenye hekima Msifiwa**]. [Suratul Fusilat: 42],na Qur`an ni maneno ya Mwenyezi Mungu kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Na ikiwa mmoja wapo katika washirikina akikuomba ulinzi, basi mpe ulinzi apate kusikia maneno ya Mwenyezi Mungu**]. [Suratul At-Bawba: 6]; ikiwa Qur`an ni maneno ya Mwenyezi Mungu, nayo yameshushwa kutoka kwake, hilo huonesha  Mwenyezi Mungu yupo juu kwa dhati yake. Na pia maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Hushuka mola wetu mpaka katika uwingu wa Dunia wakati inapo baki theluthi ya mwisho ya usiku, na husema: Ni nani mwenye kuniomba**)) mpaka mwisho wa Hadithi, nayo ni sahihi iliyo thibiti katika sahihi mbili na nyingenezo.

Na katika Hadithi ya Baraa Ibnu hazib, kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alimfundisha maneno ya  kusema atakapo ingia katika tandiko lake, miongoni mwake ((**Nimekiamini kitabu chako ambacho Umekiteremsha,na Mtume wako ambaye umemtuma**)). Nayo ipo katika sahihi Bukhari na nyinginezo.

**4**-Kuweka wazi kwake kwa kujisifia kuwa Yupo juu, kama alivyo sema: [**Litukuze jina la Mola wako aliye juu**]. [Suratul Al-Alaa: 1), na maneno: [**Na wala haemewi na kuvilinda hivyo. Na Yeye ndiye aliye juu, na ndiye Mkuu**]. [ Suratul Al-Bakara:

255]. Na maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Ametukuka Mola wangu Mlezi aliye juu**)). [Ameipokea Muslimu/ 772].

**5**-Kuashiria Mtume rehma na amani ziwe juu yake mbinguni alipokuwa akimshuhudilisha Mwenyezi Mungu katika kisimamo cha Arafa, nacho ni kisimamo kikubwa na mkusanyiko mkubwa ambao aliushuhudia Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa Ummah wake, wakati alipo sema kuwaambia**: ((Je nimefikisha?**)) wakasema: Ndio! Akasema: ((**Ewe Mola wangu Shuhudia**)), na huku akiwa ananyosha vidole vyake

mbinguni na huku akiwaelekezea watu. Nayo ni Ushahidi ya wazi kuwa

Mwenyezi Mungu yupo mbinguni, ingekua hayupo mbinguni ingekuwa kunyoosha kwake mbinguni ni bure.

**6**-Alimuuliza Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Kijakazi wakati alipo sema ((**Yuko wapi Mwenyezi Mungu**)), akasema: Mbinguni, akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Muache huru hakika yeye ni muumin**)). [Ameipokea Muslimu /537], kutoka katika Hadithi ndefu kutoka kwa Muawiya Ibn Hakamu Asulamiy, nayo ipo wazi katika kuthibitisha kuwa juu kwa Mwenyezi Mungu kwa dhati yake; kwa sababu neno (Ayinaa) katika Lugha ya Kiarabu hutumika kuulizia sehemu, na hakika aliamrisha Mtume (rehma na amani ziwe juu yake Mwanamke huyu wakati alipo muuliza yuko wapi Mwenyezi Mungu? Akakiri Mtume rehma na amani ziwe juu yake: kuwa Mwenyezi Mungu

yupo mbinguni, na akabainisha kuwa hilo ni katika mambo yanayo onesha kuwa huyu ni Muumini wakati alipo sema ((**Muache huru hakika yeye ni Muumini**)).

Hato amini Mja wa Mwenyezi Mungu, mpaka akiri na kuitakidi kuwa Mwenyezi Mungu yupo mbinguni. Hizi ni katika Ushahidi za kusikia na kukhabarisha kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume rehma na amani ziwe juu yake zinafahamisha juu ya kuwa juu kwa Mwenyezi Mungu kwa dhati yake, ama kiujumla Ushahidi ni nyingi hatuta weza kuzika zote katika sehemu hii, hakika wamezikusanya Wema walio tangulia Mwenyezi Mungu awa rehemu, kwa kuziangalia Ushahidi huu na kinacho elezwa ndani yake, na wakathibitisha kuwa Mwenyezi Mungu yupo juu kwa dhati yake, kama vile ambavyo wameafikiana kuthibitisha kuwa juu kwa Mwenyezi Mungu kwa kimaana yake, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Naye ndiye mwenye mfano bora mbingu na ardhi. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima**]. [Surati Ar-Rum: 27]na amesema Mwenyezi Mungu: [**Mwenyezi Mungu ana majina mazuri, basi muombeni kwayo**]. [Suratul Al-A,aarf: 180], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Basi msimpigie Mwenyezi Mungu mifano. Hakika Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui**]. [Suratul An-Nahl: 74], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Basi msimfanye Mwenyezi Mungu kuwa ana mshirika, na halikuwa mnajua**]. [Suratul Al-Baqara: 22]. Na nyingine zisizokuwa hizi katika Aya zinazoonesha juu ya Ukamilifu wake katika dhati yake na sifa na matendo yake.

Kama vile ambavyo kuwa juu kwa Mwenyezi Mungu kwa dhati yake, kumeoneshwa kwa Kitabu na Sunnahh na kuafikiana Wema walio tangulia, pia Akili na Maumbile yanaonesha hivyo.

Ama Ushahidi ya kiakili: husemwa: Hakuna shaka kuwa, kuwa juu ni sifa ya ukamilifu, na kinyume chake ni sifa ya upungufu, na Mwenyezi Mungu imethibiti kwake sifa ya ukamilifu.

Kilicho wajibu ni kuthibitisha kuwa juu kwa Mwenyezi Mungu, na wala haitupasi kuthibitisha kwa Mwenyezi Mungu upungufu, hakika sisi tunasema kuwa kwake juu hakuna maana kuwa kuna baadhi ya viumbe wake wanamzunguka Yeye, mwenye kudhani kuthibitishi kuwa juu kwa Mwenyezi Mungu, kunalazimu kuzungwakwa na viumbe wake, atakuwa amejichanganya mwenyewe, na imepotea akili yake.

Ama ushahidi wa kimaumbile ya kuwa juu kwa Mwenyezi Mungu kwa dhati yake: Hakika kila mwenye kumuomba Mwenyezi Mungu dua ya kiibada au dua ya mas-ala katika mas-ala, hauelekei moyo wake wakati wa kuomba isipokuwa mbinguni, na kwa hivyo utamuona anainua mikono yake mbinguni, na hiyo ni kwa kimaumbile yake, kama alivyo sema Hamdani kumwambia Abiyi Al-maali Aljuweni**: ((Hakusema mwenye kujua**

**katu: Ewe Mola isipokuwa hupata katika moyo wake, umuhimu wa kumuomba aliye juu)),** akawa Al-juweni, anajipiga makofi katika kichwa chake na huku akisema ((Alinikhiyarisha Al-Mahadani alinikhiyarisha Al-Mahadani)). Hivi ndio ilivyo nukuliwa kutoka kwake, ni sawa sawa imesihi kutoka kwake au

haikusihi, hakika kila mmoja linampata hilo, na katika ((Sahihi mbili)) kutoka katika Hadithi ya Abuu Huraira, Mwenyezi Mungu awe radhi naye, kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Alimtaja Mtu ananyoosha mikono yake mbinguni, huku akisema ewe Mola ewe Mola, mpaka mwisho wa Hadithi (Umetangulia upokezi wake).

Kisha unaweza kumuoni mtu anaswali na moyo wake umeelekea upande wa mbinguni, na khaswa anapo sujudu. Na anasema: ((Ametukuka Mola wangu aliye juu)) [Umetangulia upokezi wake].

Kwa sababu anajua kuwa anaye muabudu yupo mbinguni ametukuka Mwenyezi Mungu mtukufu.

Ama maneno yao: ((kuwa Mwenyezi Mungu hayupo katika pande sita)), Maneno hayo kwa ujumla wake ni batili; kwa sababu yanapelekea kwenye kubatilisha yale aliyo yathibitisha Mwenyezi Mungu katika nafsi yake, na kisha akailithibitisha hilo mwenye kumjua Yeye katika viumbe wake, naye ni Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ya kuwa Mwenyezi Mungu yupo mbinguni ambapo ni upande wa juu, bali kauli yao hiyo inamhukumu Mwenyezi Mungu kuwa hayupo; kwa sababu pande sita ni juu, chini, kulia, kushoto, nyuma na mbele, na hakuna kitu chochote ambacho kipo ila huambatana na moja ya pande hizi, na jambo hili linajulikana kwa kimaumbile na kiakili, utakapo zikataa pandi hizi kwa Mwenyezi Mungu, itakulazimu kusema kuwa hayupo, na japo kuwa

ubongo unaweza kuhukumu kuwa Mwenyezi Mungu haambatani na pande hizi, lakini kitu hicho ni kitu ambacho inakihukumu akili tu, na wala hakipo katika uhalisia wake, na sisi tunaamini na tunaona kuwa ni lazima kwa kila Muumini aamini kuwa Mwenyezi Mungu yupo juu ya viumbe wake, kama ilivyo onesha hivyo Kitabu, Sunna, Makubaliano ya Wanachuo, pamoja na wema walio tangulia, akili na maumbile pia, kama tulivyo likaririsha hilo kabla ya hapo, lakini sisi pamoja na hivyo tunaamini kuwa Mwenyezi Mungu amekizunguka kila kitu, na Yeye hazungwukwi na kitu chochote katika viumbe wake, na Mwenyezi Mungu amejitosheleza hahitaji chochote kutoka kwa viumbe wake. Na tunaona pia kuwa haifai kwa muumini kutoka kwenye kile kilicho fahamiswa na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna kwa maneno ya watu kwa hali yake yoyote itakavyo kuwa, kama zilivyo tuelekeza ushahidi katika mwanzo wa jibu letu.

Na ama maneno yao kuwa: ((Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu yupo katika Moyo wa Muumini)), hakika hilo halina Ushahidi katika kitabu cha Mwenyezi Mungu, wala Sunnahh za Mtume rehma na amani ziwe juu yake: na wala maneno ya yoyote katika wema walio tangulia,Mwenyezi Mungu awarehemu, na kauli hiyo kiujumla ni batili. Ikiwa atakusudia kuwa Mwenyezi Mungu hayupo kabisa katika Moyo wa Muumini, basi hilo ni batili moja kwa moja, hakika Mwenyezi Mungu mtukufu ni Mkubwa na mwenye Utukufu kuliko hilo, na katika mambo ya ajabu ni Mtu kukikimbia kile ambacho kimeelekezwa na Qur`an na Sunnahh kuwa Mwenyezi Mungu yupo mbinguni kisha achukue lile ambalo halikufahamishwa katika Qur`an na Sunna, katika uzushi kuwa Mwenyezi Mungu mtukufu yupo katika Moyo wa Muumini, kwa

sababu hakuna katika Kitabu na Sunnahh hata herufi moja inayo fahamisha juu ya hilo.

Na ikiwa atakusudia kuwa Mwenyezi Mungu yupo katika Moyo wa Muumini kwa kuwa kila wakati humtaja Mwenyezi Mungu katika Moyo wake, basi hilo ni la haki, lakini ni lazima aliseme hilo kwa ibara zinazo fahamisha juu ya uhakika wake, na inayo kataa kuelekezwa katika baatili, aseme kwa mfano: Hakika kumtaja Mwenyezi Mungu daima kupo katika Moyo wa Muumini.

Lakini kinacho dhihiri katika maneno ya mwenye kuongea ni kuwa anataka abadili kutoka kuwa Mwenyezi Mungu yupo mbinguni, na kwa maana hiyo ni batiili kama ilivyo tangulia.

Na atahadhari Muumini na kupinga kile kilicho fahamishwa katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna, na wakakubaliana juu yake wema waliotangulia kuwa ibara zilizo kusanya mafumbo hukusanya maana ya sawa, na isiyo ya sawa, ni wajibu kwake kujilazimisha na njia ya wale wa mwanzo miongoni mwa Muhajirina na Answari mpaka aingie kwenye maneno yake Mwenyezi Mungu **[Na wale walio Tangulia ,wa mwanzo katika Muhajirina na Aswari, na walio wafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu amewaridhia na wao wameridhika naye; na amewaandalia bustani zipitazo mito kati yake, wakae humo milele.huku ndiko kufu-**

**zu kukubwa**]. [Suratul At-Tauba: 100]. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujalie ni miongini mwao, na atupe kwa ujumla Rehema zake, hakika Yeye ni mwenye kutoa sana.

****

**Swali la 33: Hivi tafsiri ya kulingana kwa Mwenyezi Mungu katika kiti Chake cha Enzi kwamba ni kuwa Kwake juu ya kiti Chake cha Enzi, kwa namna inavyo lingana na utukufu wake, hiyo ni tafsiri ya wema walio tangulia?**

**Jibu:**Tafsiri ya kulingana kwa Mwenyezi Mungu katika kiti Chake cha Enzi, kwamba ni kuwa Kwake juu ya kiti Chake cha Enzi, kwa namna inayo lingana na utukufu Wake, hiyo ni tafsiri ya wema walio tangulia, Mwenyezi Mungu awarehemu Amesema Ibn Jariri Imamu wa wenye kutafsiri, katika Tafsiri yake: ((Katika maana ya Istiwaa) (kulingana sawa) ni: Kuwa juu na kunyanyuka, kama maneno ya mwenye kusema: Amelingana sawa fulani katika kitanda chake, yani amekuwa juu yake) (Tafsiri ya Ibn Jariri [1/457].

Na akasema katika kutafsiri maneno ya Mwenyezi Mungu [**Al Rahamani amelingana katika kiti chake cha Enzi**] [Suratul Twaha: 5] ((Anasema Aliye tukuka utajo wake: Arahamani yupo katika kiti chake cha Enze Amekuwa juu na kuinuka)) [Tafsiri ya Ibnu Jariri 11/16]. Yameisha maneno yake.

Na haikupokewa kutoka kwa wema waliotangulia Mwenyezi Mungu awarehemu, kauli nyingine inayo kwenda kinyume na hiyo.

Na Ushahidi ya kuwa Istiwaa katika Lugha hutumika kwa maana tofauti tofauti ni:

1- Iwe ni yenye kuenea sio yenye kuwekewa mipaka, inakuwa maana yake ni ukamilifu, kama ilivyo katika maneno yake Mwenyezi Mungu aliposema: [**Na Musa alipo fikia utu uzima**] [Suratul Al-Qasas: 14].

2- Iwe ni yenye kuambatana na (Wau), inakuwa kwa maana ya kulingana, kama wanavyo sema: Yamelingana maji na kizingiti.

3-Iwe ni yenye kuambatana na (Al), inakuwa kwa maana ya kukusudia; kama ilivyo kwenye maneno yake Mwenyezi Mungu aliposema [**Kisha akalingana sawa katika kiti chake cha Enzi**]. [Suratul Al-Baqara: 29].

**4**-Iwe ni yenye kuambatana na (Alaa), inakuwa kwa maana kuwa juu na kunyanyuka; kama ilivyo katika maneno ya Mwenyezi Mungu [**Arahamani amelingana katika kiti chake cha Enzi**]. [Suratul Twaha: **5**].

Wameeleza baadhi ya wemawalio tangulia Mwenyezi Mungu awarehemu, ya kuwa Istiwai ikiambatana na (Ila)ni sawa na ile iloambatana na (Alaa), inakuwa maana yake ni kuwa juu na kunyanyuka.

Kama walivyo sema baadhi yao ya kuwa Istiwaa iliyo ambatana na (Ala), inakuwa kwa maana ya kupanda na kutulia, ikiwa itaambatana na (Ala).

Ama tafsiri ya kukaa, hakika ameinukuu Ibnu Qayyim, Mwenyezi Mungu amrehemu,katika ((Aswaaiq)) [4/1303 ], kutoka kwa Kharijatu Ibnu Mus-abu katika maneno yake Mwenyezi Mungu: [**Arahamani amelingana katika kiti chake cha Enzi**]. [Suratul Twaha: 5.maneno yake ((Na jee inakuwa kulingana billa ya kukaa)), yameisha maneno yake.

Hakika imekuja kutajwa neno kukaa katika Hadithi aloipokea Imamu Ahmad kutoka kwa Ibnu Abasi Mwenyezi Mungu awe radhi naye, Imeinuliwa mpaka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi.

****

**Swali la 34: Fadhilatu Sheikh Mwenyezi Mungu akuhifadhini, Umesema: kulingana kwa Mwenyezi Mungu katika kiti chake cha Enzi kuwa ((Ni kulingana kwa Mwenyezi Mungu juu ya kiti chake cha Enzi kunako lingana na utukufu wake na ukubwa wake)), tunakuomba kwa ukarimu wenu kuliweka wazi zaidi suala hilo?**

**Jibi:** Maneno yetu katika kulingana kwa Mwenyezi Mungu katika kiti chaake cha Enzi kunalingana na ukumbwa wake na utukufu wake ((Hakika huko ni kuwa juu maalumu kunako lingana na ukubwa wake na utukufu wake,)) Tunakusudia kuwa ni kuwa juu maalumu kwake tu katika kiti chake cha Enzi, hakuenei kwa viumbe wake, na kwa sababu hiyo haifai tuseme: Istiwaa (kulingana) kwa viumbe, au katika mbingu,au katika ardhi pamoja ya kuwa yupo juu ya hivyo, bali tunasema: Yeye yupo juu kuliko viumbe vyote, yupo juu ya mbingu, na mfano wa hivyo. Ama katika arshi (kiti cha Enzi)tunasema: Hakika Mwenyezi Mungu mtukufu yupo juu ya kiti chake cha Enzi na amelingana sawa katika kiti chake, kulingana kwake ni maalumu kutoka katika kuwa juu kwa pamoja. Na kwa sababu hiyo imekuwa kulingana kwa Mwenyezi Mungu katika kiti chake cha Enzi ni katika sifa za kivitendo zinazo ambatana na matakwa yake, ni kinyume na kuwa kwake juu, hakika ni katika sifa za kibinafsi ambazo huwezi kuzitenganisha.

Na hakika ameweka wazi haya nilio yasema Sheikkh Islaam Ibnu Taymiya Mwenyezi Mungu amrehemu, katika kusherehesha Hadithi ya Nuzul [5/522 /Majuu fatawa] jamiu Ibn Qaasimu Iwapo

kuta semwa: Pindi itakapo kuwa kulingana kwa Mwenyezi Mungu katika kiti chake cha Enzi ni baada ya kuumba mbingu na ardhi katika siku sita, kabla ya hapo hakuwa katika kiti hicho cha Enzi.

Husemwa: Istiwaa (Kulingana) ni kuwa juu maalumu, kila mwenye kulingana katika kitu huwa juu yake, na sio kila mwenye kuwa juu ya kitu ni mwenye kulingana juu ya kitu hicho, na kwa sababu hiyo haisemwi kwa kila kilicho kuwa juu kuliko vingine kuwa kimelingana juu yake, kila kilicho semwa ndani yake kuwa kimelingana juu ya vingine Hakika hicho kipo juu yake, mwisho wa nukuu.

Na ama maneno yetu: ((Kanalingana na Ukubwa na Utukufu wake)), makusudio hapo ni kulingana kwake katika kiti chake cha Enzi ni kama sifa zake nyingine, zinavyo lingana na utukufu wake na ukubwa wake, haufananishwi na kulingana kwa viumbe, yenyewe inarudi kwenye namna ambayo upo ulingano huo; kwa sababu sifa hufuata chenye kusifiwa, kama vile ambavyo Mwenyezi Mungu mwenye hafananishwi na kitu, hivyo hivyo sifa zake hazifanani na za viumbe, amesema Mwenyezi Mungu: [**Hakuna mfano wake kitu chochote Naye ni mwenye kusikia na ni mjuzi**]. [Suratul Ashuraa: 11], hana mfano wake katika Dhati yake wala sifa zake. Na kwa ajili hiyo amesema Imamu Maliki Mwenyezi Mungu amrehemu alipo ulizwa kuhusu kulingana kwa Mwenyezi Mungu, wakati alipo ulinzwa ni vipi amelingana katika kiti chake cha Enzi? Akasema ((Kulingana kwake sio kwamba hakujulikani na naman yake sio kua haijulikina, na kuamini ni lazima, na kuuliza ni bidaa)). [Ameipokea Al-Baihaq / 866 ]. Na hii ni mizani

kwa sifa zote, hakika hizo zimethibiti kwa Mwenyezi Mungu kama alivyo zithibitisha katika nafsi yake, kwa namna ambayo inalingana na Mwenyezi Mungu pasina kubadili, wala kuziacha,wa kuziwekea namna wa kuzimananisha.

Na kwa ajili hiyo imebainika ule msingi wa maneno kuwa, kulingana sawa katika kiti cha Enzi ni kuwa juu maalumu juu ya kiti cha Enzi kunako lingana na Mwenyezi Mungu; kwa sababu kuwa juu kwa Mwenyezi Mungu kwenye kuenea kumethibiti kwa Mwenyezi Mungu kabla ya kuumba mbingu na ardhi, na wakati alipo ziumba, na baada ya kuziumba kwa sababu ni katika sifa zake mwenyewe zenye kulazimiana kama vile kusikia na kuona na kuweza na nguvu na mfano wa hayo; ni kinyume na kulingana.

****

**Swali la 35: Ni mambo gani ambayo ni lazima kuyaegemeza kwenye matakwa ya Mwenyezi Mungu, na ni mambo gani ambayo haifai kuyaegemeza kwenye matakwa ya Mwenyezi Mungu?**

**Jibu**: Kila kitu kinacho kuja mbeleni, ilivyo bora ni kuegemeza kwenye matakwa ya Mwenyezi Mungu,kama alivyo sema MwenyeziMungu: [**Wala usiseme kamwe kwa jambo lolote lile: Hakika nitarifanya hilo kesho**. 23 **Isipokuwa Mwenyezi Mungu akipenda**]. [Suratul Al-Kahf].

Ama katika kitu kilicho pita haifai kukiegemeza katika matakwa ya Mwenyezi Mungu, isipokuwa akiwa anakusudia kwa hilo kutoa sababu.

**Mfano**: kama atasema Mtu kukwambia: (Umeingia Mwezi wa Ramadhani mwaka huu usiku wa siku ya pili akitaka Mwenyezi Mungu; haihitaji kusema (Akitaka Mwenyezi Mungu) kwa sababu limesha pita na limesha julikana.

Na kama atasema mwenye kusema kukwambia: (Nimevaa nguo akipenda Mwenyezi Mungu), na hali ya kuwa amevaa haiwi vizuri aiegemeze kwa Mwenyezi Mungu; kwasababu limepita na limekwisha isipokuwa akikusudia kutoa sababu, yani akikusudia kuwa kuvaa nguo kulikuwa ni kwa matashi ya Mwenyezi Mungu, hakika hilo halina ubaya.

Lau kama atasema mwenye kusema wakati anapo swali: (Nimeswali akitaka Mwenyezi Mungu) na makusudia yako, kufanya Swala hakika kunyambua huko haitakiwi kwa sababu amesha swali, na kama atakusudia akitaka Mwenyezi Mungu Swala ni yenye kukubaliwa itasihi kusema (akitaka Mwenyezi Mungu); kwa sababu hajui imekubaliwa au haikukubaliwa.

****

**Swali la 36: Ni vipi vigawanyo vya kutaka (Al-iraadah)?**

**Jibu:** Kutaka yamegawanyika katika sehemu mbili: 1- Kutaka kwa jumla (Al-Kauniya)

2-Kutaka kwa kisheria (Ashariya)

Yale yatakayo kuwa kwa maana kutaka hiyo ni Iradatu Kauniya (Jumla) na yatakayo kuwa kwa maana ya Mapenzi hayo ni ya Kisheria.

Mfano wa kutaka kwa kisheria ni maneno yake Mwenyezi Mungu [**Na Mwenyezi Mungu anataka kukuhafifishieni kwenye utiifu wake**]. [Suratul An-Nisaa: 27] kwa sababu neon (kutaka) lina maana ya (kupenda), na wala haliwi kwa maana ya Al-Mashia; kwa sababu ingekuwa na maana (Na Mwenyezi Mungu anataka akuhafifishieni) engewahafifishia waja wote na jambo hilo halikuwa, kwa wengi katika binadamu ni makafiri, kwa ajili hiyo inamaanisha (Anapenda akuhafifishieni) na wala sio lazima katika kupenda kwa Mwenyezi Mungu kuambatane na matakwa, kwa sababu hekima ya Mwenyezi Mungu ni kubwa inaweza kuhukumu kuto tokea.

Na mfano wa Iradatu Kauniya (kutaka kwa jumla) ni maneno ya Mwenyezi Mungu [**Ikiwa Mwenyezi Mungu anataka kukuacheni mpotee**]. [Suratul Hud: 34] kwa sababu Mwenyezi Mungu hapendi kuwapoteza Waja, kwa hiyo haifai kuwa maana (Ikiwa Mwenyezi Mungu anapenda akupotezeni) bali maana yake (Ikiwa Mwenyezi Mungu anataka kukupotezeni.

**Lakini imebaki kwetu tuseme**: Ni ipi tofauti ya Iradatu Kauniya na Iradatu Shariiya (kutaka kwa kisheria na kutaka kwa jumla) katika kutokea linalo kusudiwa?

Tunasema Kauniya (jumla) hapana budi lazima itokee lile lililo kusudiwa, pindi anapo taka kitu Mwenyezi Mungu ni lazima kitokee amesema Allah [**Hakika amri yake anapo taka kitu ni kukiambia tu kuwa na kikawa**]. [Suuratu Yaasin : 82].

Ama kutaka kwa kisheria, kunaweza kutokea lile lililo kusudiwa na linaweza lisitokee, anaweza kuwa Mwenyezi Mungu anataka hiki kitu kisheria na anakipenda, lakini kisitokee; kwa sababu kinacho pendwa kinaweza kutokea au kisitokee.

**Atakapo sema mwenye kusema**: Je Mwenyezi Mungu anapenda maaswi?

**Tunasema**: Anapenda Kaunia (Kijumla) sio Kisheria; kwa sababu kutaka kwa kisheria kuna maana ya kupenda, na Mwenyezi Mungu hapendi maasi, lakini anayapenda kwa Mashia (kutaka), kila kilicho katika mbingu na ardhi ni kwa kutaka Mwenyezi Mungu.

****

**Swali la 37: Ni ipi Ilhadi (upingaji) katika majina ya Mwenyezi Mungu, na ni zipi aina zake?**

**Jibu:** Upingaji katika lugha ya Kiarabu: ni kuelemea sehemu moja, amesema Mwenyezi Mungu: [**Lugha ya huyo waneye muelekezea ni ya kigeni, na hii ni lugha ya Kiarabu iliyo wazi**]. [Suratul An-Nahli: 103], na miongoni mwake (Lahdi) katika kaburi, kwani imeitwa hivyo kwa kuegemea kwake upande mmoja, na wala Ilhadi haiwezi kujulikana isipokuwa kwa kujua Istikama (kuwa na msimamo); kwa sababu ni kama kulivyo semwa: kwa kinyume chake ndio hubainika vitu.

Istikama ni katika milango ya majina ya Mwenyezi Mungu na sifa zake, ni lazima tuyachukue majina hayo na sifa hizo kwa uhakika wake ambao unanasibiana na Mwenyezi Mungu bila kubadili wala kuyaacha wala kuyawekea nama wala kuyafananisha; katika misingi ambayo wanakwenda nayo Ahlu Sunna Waljamaa katika mlango huu, tutakapo jua Istikama katika mlango huu, hakika kinyume chake ndio Ilhadi, hakika wana wa zuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, wameitaja Ilhadi katika majina ya Mwenyezi Mungu aina ambazo zinakusanya ni tuseme: Ni kuelemea katika kitu kingine kinyume na kile anacho takiwa kukiitakadi, nazo zipo kwa aina:

1-Kupinga kitu katika majina ya Mwenyezi Mungu, au zile tulizo fahamishwa katika sifa zake, na mfano wake: Mwenye kukanusha kuwa jina la Arahani ni katika majina ya Mwenyezi Mungu

kama walinyo fanya Al-Jahamia, au ayakubali majina lakini anapinga kile kilicho maanishwa katika majina hayo, kama wanavyo sema baadhi ya Wazushi: kuwa hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kusamehe bila kuwa na huruma, ni mwenye kusikia bila kuwa na masikio!.

2-Kumuita Mwenyezi Mungu kwa jina ambalo hakuitia nafsi yake jina hilo, na ushahidi wa kuwa hiyo ni Ilhadi, ni kwa kuwa majina ya Mwenyezi Mungu ni Taukifiya, haifai kwa mtu yoyote kumuita Mwenyezi Mungu kwa jina ambalo hakuitia kwayo nafsi yake kwa sababu hilo ni katika kumsemea Mwenyezi Mungu bila kuwa na ujuzi,na ni katika kumfanyia Mwenyezi Mungu uadui na hilo ni kama walivyo fanya Manaswara, wakamuita Mwenyezi Mungu kwa jina la (baba) na mifano mingine.

3-Kuitakidi kuwa majina haya yanafahamisha sifa za viumbe, akayafanya kuwa ni yenye kufanana na viumbe.

Na ushahidi wa kuwa huu ni upingaji ni kuwa mwenye kuitakidi kuwa majina ya Mwenyezi Mungu yanaonesha kufanana Mwenyezi Mungu na viumbe wake, hakika atakuwa ameyatoa majina hayo kwenye kile kilicho elekezwa, na kwenda kwenye kitu kingine, na atakuwa amefanya maneno ya Mwenyezi Mungu na ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni yenye kupelekea kwenye ukafiri kwa sababu kumfananisha Mwenyezi Mungu na viumbe wake ni ukafiri kwa kuwa ni kuyapinga maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Hakuna kitu mfano wake, naye ni**

**Mwenye kusikia Mwenye kuona**]. [Suratul Al-Shurura: 11], na maneno Yake: [**Je mnamjua mwenye jina kama lake**]. [Suratul Maryam: 65], amesema Nuemu bin Hamad Al-khuzai Sheikh wa Bukhari Mwenyezi Mungu amrehemu ((Mwenye kumfananisha Mwenyezi Mungu na viumbe wake hakika amekufuru,na mwenye kupinga alicho kisifu Mwenyezi Mungu katika nafsi Yake hakika amekufuru,na hakuna katika alicho kisifia Mwenyezi Mungu katika nafsi yake mfano,au chenye kufanana nacho)). [Ameyapokea Al-lakai katika sherehe itikadi Ahalu Sunnahh wa Aljamaa, /936].

4-Achukue katika majina ya Mwenyezi Mungu, na kuyaitia masanamu mfano wa jina hilo, kama walivyo chukua jina Lata kutoka katika jina Al Ilaaha, na Al-Uzza kutoka kwenye jina la Mwenyezi Mungu Al-Azizi, na jina Manata kutoka kwenye jina la Mwenyezi Mungu Al-manan.

Na ushahidi wa kuwa mwenye kufanya hivyo atakuwa amepingi ni: Kuwa majina ya Mwenyezi Mungu ni maalumu kwa ajili yake, haifai kuhamisha maana ya majina hayo kwenda kwa yoyote katika viumbe wake, ili kiumbe hicho kipewe ibada ambayo hastahiki isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hizi ni katika aina za upingaji katika majina ya Mwenyezi Mungu aliyetukuka.

****

**Swali la 38: Ni vipi vigawanyo katika vitu alivyo viegemeza Mwenyezi Mungu kwake mfano: Uso wa Mwenyezi Mungu, Mkono wa Mwenyezi Mungu, na mengine mfano wa haya?**

**Jibu:** Vigawanyo katika vitu alivyo viegemeza Mwenyezi Mungu katika nafsi yake ni vitatu:

1-Kitu kilicho simama kwa nafsi yake, kukiegemeza kwake kwa Mwenyezi Mungu ni katika mlango wa kukiegemeza kiumbe kwa Muumba wake, na kuegemeza huku kunaweza kuwa ni katika njia ya kuenea (Al-umumu) kama ilivyo katika maneno ya Mwenyezi Mungu [**Hakika ardhi yangu ni pana**]. [Suratul Al-Ankabuti: 56], na inaweza kuwa ni kwa njia maalumu sio yenye kuenea (Al-khususwi) kimeegemezwa kwa Mwenyezi Mungu kwa utukufu wake kama ilivyo katika maneno ya Mwenyezi Mungu [**Na itwaharishe nyumba yangu kwa wenye kutufu**]. [Suratul Alhaji: 26], na maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema [**Ngamia wa Mwenyezi Mungu na kinywaji cheke**]. [Suratul Ashamsi: 13], na hiki ni kigawanyo cha viumbe.

2-Kitu ambacho kinasimama kwa kitu kingine, mfano maneno ya Mwenyezi Mungu aliposema: [**Na ni roho iliyo toka Kwake**]. [Suratul An-Nisaai: 171], kuegemezwa kwa roho hii kwa Mwenyezi Mungu ni katika mlango wa kukiegemeza kiumbe kwa Muumba wake kwa kukitukuza, kwani ni roho katika roho alizo ziumba Mwenyezi Mungu, na wala sio fungu katika Yeye, kwa

ajili hiyo roho hii imekuwa kwa Issa nayo ni kitu kilicho jitenga kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na kigawanyo hiki kimeumbwa vilevile.

3-Iwe ni sifa halisi inakuwa imeegemezwa kwenye sifa ya Mwenyezi Mungu, na kigawanyo hiki hakijaumbwa; kwa sababu sifa zote za Mwenyezi Mungu hazijaumbwa, nazo katika Qur`an zipo nyingi.

****

**Swali la 39: Ni ipi hukumu ya kupinga kitu katika majina ya Mwenyezi Mungu au sifa Zake?**

**Jibu**: Kupinga kumegawanyika katika sehemu mbili:

**1**-Kupinga kwa kukadhibisha, na hii ni ukafiri bila shaka yoyote, lau kama mtu atapinga jina katika majina ya Mwenyezi Mungu, au sifa katika sifa zake zilizo thibiti katika Kitabu na Sunna,

kwa mfano aseme Mwenyezi Mungu hana mkono, basi yeye ni kafiri kwa makubaliano ya wana chuoni; kwa sababu kukataa habari ya Mwenyezi Mungu na Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni ukafiri unao mtoa mtu katika Uislamu.

**2**-Kupinga kwa kutafsiri, nayo ni kuto kuyakataa majina hayo na sifa zake, lakini anayatafsiri na hii imegawanyika katika sehemu mbili:

**1**-Iwe tafsiri hii ni yenye kukubalika katika Lugha ya kiarabu, na hii haimkufuurishi, hawi kafiri.

**2**-Isiwe tafsiri hii ni yenye kukubalika katika lugha ya kiarabu, na hii inamkufurisha anakua kafiri kwa sababu ikiwa haikubaliki katika lugha basi itakuwa ni kupinga, na mfano wake aseme: Mwenyezi Mungu hana mkono wa kikweli, wala kwa maana ya neema wala kwa maana ya nguvu, huyu atakuwa ni kafiri, kwa sababu amekanusha kukanusha kwa moja kwa moja naye amekataa kitu ambacho ni hakika, na lau atasema katika maneno yake Mwenyezi Mungu [**Bali mikono yake iwazi**], [Suratul Al-Maida /64] makusudio ya mikono hapa ni mbingu na ardhi basi atakuwa amekufuru kwa sababu haikusihi katika lugha ya kiarabu, na wala haikubaliki katika sheria, basi yeye atakuwa ni mkanushaji na mpingaji. Lakini akisema: makusudio ya mikono hapa ni neema au nguvu hakufuru; kwa sababu mkono katika lugha ya kiarabu hukusudiwa pia neema au nguvu.

****

**Swali la 40: Ni ipi hukumu kwa mwenye kuitakidi kuwa sifa za Muumba ni kama sifa za Viumbe?**

**Jibu:** Mwenye kuitakidi kuwa sifa za Muumba ni kama sifa za Viumbe amepotea, na hilo ni kwa sababu sifa za Muumba hazifanani na za viumbe, kwa ushahidi katika Qur`an, amesema Mwenyezi Mungu: [**Hapana kitu mfano wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona**]. [Suratul Shuraa: 11], na wala hailazimu kufanana vitu viwili katika majina au sifa, vifanane katika uhakika; na huu ni msingi unaojulikana.

Je Mwanadamu si ana uso, na Ngamia pia ana uso? Vitu hivyo viwili vimeafikiana katika jina lakini vimetofautiana katika uhakika; Ngamia ana mkono na Mwanadamu ana mkono je mikono hii inafanana?

Jibu ni hapana! Kwa ajili hiyo kwanini hatusemi: Mwenyezi Mungu ana Uso na wala haufanani na uso wa viumbe wake, na Mwenyezi Mungu ana Mkono lakini haufanani na mikono ya viumbe wake? Amesema Mwenyezi Mungu: [**Siku tutakapo zikunja mbingu kama mkunjo wa karatasi za vitabu.**] [Suratul Al-Anbiyaa: 104], je kuna mkono katika mikono ya viumbe utakao kuwa kama mkono huu? Hapana, ikiwa ni hivyo ni lazima tujue kuwa Muumba hafanani na viumbe; sio katika dhati yake wala katika sifa zake; [**Hapana kitu mfano wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona.**] [Suratul Shuraa: 11] kwa ajili hiyo hai-

fai milele kudhani sifa katika sifa za Mwenyezi Mungu ni kama sifa za Viumbe wake.

****

**Swali la 41: Ni kitu kinajulikana kuwa usiku huzunguka katika tufe la ardhi, Mwenyezi Mungu hushuka katika uwingu wa Dunia inapobaki theluthi ya mwisho ya usiku, hilo linaonesha kuwa usiku mzima huwa katika uwingu wa Dunia, ni lipi Jibu juu ya hilo?**

**Jibu:** Kitu ambacho ni lazima kwetu ni kuamini kwa kila alicho kisifu Mwenyezi Mungu na akakiitia kwacho nafsi Yake katika Kitabu, na kwa kupitia ulimi wa Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake pasina kubadili wala kuziacha wala kuziwekea namna wala kuzifananisha katika sifa zake, ni wajibu kuwa mbali Aqida yetu na mambo haya manne tulotahadharishwa nayo. Na ni wajibu kwa kila Mwanadamu aizuiye nafsi yake na maswali ya (kwanini) na (vipi); katika mambo yanayo husu majina ya Mwenyezi Mungu na sifa zake, na vile vile aizuiye nafsi yake na kufikiria katika namna, njia hii atakapo ifuata Mwanadamu atapata raha sana, na hii ndio ilikuwa hali ya wema waliotangulia Mwenyezi Mungu awarehemu, na kwa ajili hii alikuja mtu kwa Anas bin Malik akasema: Ewe bake Abdillah! Arahamani yupo juu ya kiti cha enzi amelingana sawa ni vipi amelingana sawa? Akakataa kwa kutikisa kichwa chake na akasema: ((Kulingana kwake sio

kama hakujulikani, na namna alivyo katika kiti hicho haijulikani, na kuamini hivyo ni wajibu, na kuliza kuhusu hilo ni uzushi, na sikuoni wewe muulizaji isipokuwa ni mzushi)), [umetangulia upokezi wake].

Na huyu ambaye anasema: Hakika Mwenyezi Mungu huteremka kwenye uwingu wa dunia wakati inapo baki theluthi ya mwisha ya usiku, hiyo inawajibisha kuwa usiku mzima anakuwa katika uwingu wa dunia; kwa sababu usiku huzunguka ardhi nzima, theluthi huzunguka kutoka katika sehemu hii kwenda sehemu nyingine.

Jawabu letu katika hili tunasema: Swali hili hawakuuliza Maswahaba Mwenyezi Mungu awe radhi nao, na lau kama hili hutokea katika moyo wa Muumini aliye jisalimisha angelibainisha Mwenyezi Mungu na Mtume rehma na amani ziwe juu yake na tunasema Muda wa kwamba theluthi ya mwisho ya usiku ipo katika upande huu, kushuka katika upande huo ni jambo la uhakika, na pale usiku unapo isha, huondoka suala la kushuka Kwake, na sisi hatuwezi kujua namna ya ushukaji wa Mwenyezi Mungu, na wala hatuna ujuzi wa hilo, na tunajua kuwa  Mwenyezi Mungu hana mfano wake, na ni juu yetu tujisalimishe katika hilo, na tuseme: Tumesikia na tumeamini na tumefuata na tumetii, na hii ndio kazi yetu.

****

**Swali la 42: Ni upi msimamo wa wema walio tangulia katika kuonekana kwa Mwenyezi Mungu? Na ni ipi hukumu kwa mwenye kudai kuwa ((Hakika Mwenyezi Mungu haonekani kwa macho, na kuwa kuonekana kwake ni jambo la ukamilifu wa kuwepo kwake))?**

**Jibu:** Anasema Mwenyezi Mungu katika Qur`an wakati alipotaja Kiyama: [**Nyuso siku hiyo ni zenye kumelemeta. Zinamuangalia Mola wao Mlezi**]. [Suratul Al-Qiyamah: 22-/23], kule kuegemezwa kuangalia katika nyuso, na kitu ambacho kinaweza kuangalia katika nyuso ni macho, basi katika aya hizi kuna Ushahidi ya kuwa Mwenyezi Mungu ataonekana kwa Macho, lakini kumuona kwetu Mwenyezi Mungu hakupelekei kumjua vilivyo, kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema [**Wala wao hawawezi kumjua Yeye vilivyo**]. [Suratul Twaha: 110].

Itakapo kuwa hatuwezi kumjua Mwenyezi Mungu kwa kila jambo, hilo huonesha kuwa hatuwezi kumjua vilivyo kwa kumuona kwa macho, na hilo limeelezwa kwenye maneno yake Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Macho hayamfikii bali Yeye anayafikia macho. Naye ni Mjuzi Mwenye khabari**]. [Suratul Al-Anaam: 103], macho hata kama yatamuona hayawezi kumjua vilivyo, kwa hiyo Mwenyezi Mungu ataonekana kwa macho kuonekana kwa uhakika, lakini huwezi kumfahamu vilivyo kwa uoni huu; kwa sababu Yeye ni mkubwa kwa kujulikana kwa hilo tu, na msimamo huu ndio walio kwenda nao Wema walio tangulia, Mwenyezi Mungu awarehemu, na wanaona kuwa neema kubwa atakayo neemeshwa nayo Mwanadamu ni kuangalia katika uso wa Mwenyezi Mungu;

na kwa ajili hii ilikuwa katikadua za Mtume rehma na amani ziwe juu yake ((**Ninakuomba ewe Mwenyezi Mungu ladha ya kuangalia katika Uso Wako)) Wako**)). [Ameipokea Ahmadi /264/4/, na Nasaii /1305].

Amesema ((**Ladha ya kukuangalia**)); kwa sababu kuangalia huku kuna ladha kubwa mno, mtu hawezi kuijua ila yule atakaye ipata kwa neema ya Mwenyezi Mungu na fadhila zake, na ninatarajia kutoka kwa Mwenyezi Mungu anijalie pamoja na nyiye tuwe ni miongoni mwa wenye kuipata radha hiyo. Na hii ndio hakika ya kumuona Mwenyezi Mungu ambako umekubaliana Ummah mzima.

Ama mwenye kudaikuwa hakika Mwenyezi Mungu haonekani kwa macho, na kuwa kuonekani kwake ni jambo la ukamilifu wa kuwepo kwake, hakika maneno yake hayo ni baatili yanayo kwenda kinyume na Ushahidi, na hali halisi pia inamkadhibisha; kwa sababu ukamilifu wa uhakika unapatikana katika dunia pia. Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Katika kutafsiri Ihsani: ((**Ihsani: Ni kumuabudu Mwenyezi Mungu kama unamuona,ikiwa humuoni basi Yeye anakuona)**)). [Umetangulia upokezi wake], na ibada zako kwa Mwenyezi Mungu ziwe kama unamuona huu ndio ukamilifu wa Yakini, madai ya kuwa Ushahidi zilizo kuja katika kumuona Mwenyezi Mungu zinakusudia ukamilifu wa Yakini, kwa sababu mwenye yakini iliyo kamili ni kama mwenye kushuhudia kwa macho haya ni madai ya baatili na

ni kubadili Ushahidi, na sio tafsiri bali ni kubadili kuliko baatili, ni waJibu kumfanyia radi anaye sema hayo. Na Mwenyezi Mungu ndio mwenye kutegemewa kwa kila kitu.

****

**Swali la 43: Je Majini yana athari kwa Mwanadamu? Na ni ipi njia ya kujikinga nao?**

**Jibu**: Hakuna shaka kuwa Majini wana athari kubwa kwa Mwanadamu katika maudhi ambayo yanaweza kufikia mpaka kwenye kuuwa, na

huenda wakamuudhi kwa kumrushia mawe, na wakati mwingine huwatishia Wanadamu na mambo mengine katika mambo ambayo Sunna imeyathibitisha na mazingira yakaonesha hivyo, hakika imethibiti kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake aliwapa baadhi ya Maswahaba ruhusa ya kwenda kwa watu wao katika moja ya vita, na ninadhani vilikuwa nivita ya Handaq na kulikuwa na kijana ambaye alikuwa ni mgeni katika ndoa, kijana huyu alipo fika nyumbani kwake, akamkuta mke wake yupo mlangoni, akalikataa hilo kwa mke wake, mke wake akamuambia: Ingia ndani akaingia ghafla akaona nyoka yupo katika kitanda, na alikuwa na mkuki akamchoma na mkuki mpaka akafa, na wakati alipo kufa nyoka yule kijana naye akafa na haikujulikana nani alitangulia

nyoka au yule kijana, lilipo mfikia hilo Mtume rehma na amani ziwe juu yake akakataza kuwauwa Majini ambayo huingia katika Majumba, [Ameipokea Muslimu /2236] .

Na hii ni Ushahidi ya kuwa Majini wanaweza kumfanyia uadui Mwanadamu na wanaweza kuwaudhi kama hali halisi inavyo shuhudia, hakika zimepokewa khabari nyingi na ikaeneye kuwa Mwanadamu anaweza kwenda katika sehemu akawa anarushiwa mawe na wala asimuone yoyote katika ile sehemu, na wakati mwingine zinaweza kusikiwa sauti, na kunaweza kusikiwa sauti kama sauti za matawi ya miti na mfano wa hayo katika mambo ambayo yanaogopesha na yanaudhi, na vile vile Jini anaweza kuingia katika mwili wa Mwanadamu, ima kwa mapenzi, au kwa makusudio ya kumuudhi, au kwa sababu katika sababu, na ina ashiria hivyo maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Wale wao kula riba hawasimami ila kama anavyo simama aliye zungwa na Shetani kwa kuguswa**] [Suratul Baqara: 275], na katika aina hii anaweza kuongea Jini kwa kupitia Mwanadamu Mwenyewe, na akawa anamsemesha yule mwenye kumsomea Aya katika Qur`an Tukufu, na huenda akachukua ahadi kwa msomaji kuwa ataondoka na hata rudi, na mengine yasokuwa hayo ambayo yameenea katika watu, kutokana na hilo hakika kinga yenye kumzuiya Mwanadamu na shari ya Majini ni kusoma katika vile vilivyo kuja katika Sunna kuwa vinaweza kumlinda na shari zao, mfano Ayatul Kursiy, hakika Aya hii atakapo isoma Mwanadamu usiku haachi kuwa katika hifadhi ya Mwenyezi Mungu na wala hamkaribii Sheitwani mpaka asubuhi, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuhifadhi.

****

**Swali la 44: Je Majini wanajua mambo ya ghaibu (ya siri)?**

**Jibu:** Majini hawajui mambo ya siri, na wala hakuna katika mbigu na ardhi mwenye kujua mambo ya siri isipokuwa Mwenyezi Mungu, soma maneno yake Mwenyezi Mungu aliposema: [**Na tulipo mhukumia kufa, hapana aliye wajulisha kufa kwake ila mnyama wa ardhini aliye kula fimbo yake. Na alipo anguka Majini walitambua lau kuwa wangalijua mambo ya ghaibu (siri) wasingeli kaa katika adhabu hiyo ya kufedhehesha.**] [Suratul Sabaa/ 14].

Na mwenye kudai kuwa anajua mambo ya ghaibu basi huyo ni kafiri,na mwenye kumswadikisha mwenye kudai kuwa anajua mambo ya ghaibi huyo pia nae ni kafiri; hilo ni kwa ajili ya maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Sema hakuna mwenye kujua mambo ya ghaibu katika mbingu na ardhi isipokuwa Mwenyezi Mungu**] [Suratul Namli /65], hakuna anaye jua mambo ya ghaibu katika mbingu na ardhi isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake.

Na hawa wanaodai kuwa wanajua mambo ya ghaibu, katika mambo yajayo wote hao ni katika Makuhani, na hakika imethibiti kutoka kwa Mtumerehma na amani ziwe juu yake: ((**Kuwa mwenye kumwendea mpiga ramli akamuliza jambo hatokubaliwa swala zake siku arobaini**)), [Ameipokea Muslimu 2230].

Na iwapo atamswadikisha hakika yeye atakuwa ni kafiri kwa sababu akimuamini kuwa anajua mambo ya ghaibu atakuwa amekadhibisha maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Sema hakuna mwenye kujua mambo ya ghaibu katika mbingu na ardhi isipokuwa Mwenyezi Mungu**], [Suratul Namli 65].

****

**Swali la 45: Ni ipi hukumu ya mwenye kumsifu Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa ni habibu LLah, Mwenye kupendwa na Mwenyezi Mungu?.**

**Jibu:** Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni habibu LLah, hiyo haina shaka, kwani yeye ni mwenye kumpenda Mwenyezi Mungu na anapendeka kwa Mwenyezi Mungu, lakini kuna sifa ya juu na nzuri kuliko hiyo nayo ni Khalilullah (Kipenzi cha Mwenyezi Mungu), kwani Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni kipenzi cha Mwenyezi Mungu kama alivyo sema mwenyewe: ((**Hakina Mwenyezi Mungu amenifanya mimi ni kipenzi chake kama alivyo mfanya Ibrahim kipenzi chake**)), [Ameipokea Muslimu /532].

Na kwa ajili hiyo mwenye kumsifu kwa kupendwa tu hakika atakuwa amemshusha katika daraja lake, kwani mapenzi ya Mwenyezi Mungu kwake ni makubwa kuliko kumpenda

kwake,Waumini wote ni wenye kupendwa na Mwenyezi Mungu, lakini Mtume rehma na amani ziwe juu yake yupo katika daraja la juu katika hilo, nayo ni upenzi, hakika Mwenyezi Mungu alimfanya kuwa ni kipenzi kama alivyo mfanya Ibrahim kuwa ni kipenzi, kwa sababu hiyo tunasema Hakika Mohammad rehma na amani ziwe juu yake ni kipenzi cha Mwenyezi Mungu, na hili lipo juu kuliko tunapo sema: Mpendwa wa Mwenyezi Mungu kwa sababu hilo linakusanya kupendwa na ziada; kwa sababu ndio upeo wa kupenda.

****

**Swali la 46: Ni ipi hukumu ya kumsifu Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuifanya kuwa ni biashara?**

**Jibu:** Hukumu ya hilo ni haramu, na ni lazima ijulikane kuwa kumsifu Mtume rehma na amani ziwe juu yake imegawanyika katika vigawanyo viwili:

**1**- Iwe kumsifu ni katika sifa ambazo anastahiki, pasina kufikia katika daraja ya kupetuka mipaka hili halina ubaya yani hakuna ubaya kumsifu Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa sifa

ambazo anastahiki nazo, katika sifa nzuri za ukamilifu wa umbile lake na uongofu wake rehma na amani ziwe juu yake .

**2**-Kumsifu ambako kunampelekea mwenye kumsifu katika kupetuka mipaka ambako amekataza Mtume rehma na amani ziwe juu yake akasema: ((**Msinisifu kama walivyo msifu Manaswara Issa mtoto wa Maryamu, na hakika si vinginevyo Mimi ni mja, basi semeni: Mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake**)), [Ameipokea Bukhari /3445]. Mwenye kumsifu Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa yeye ni msaidizi kwa wenye kutaka msaada, na ni mwenye kujibu maombi kwa wenye matatizo, na Mtume rehma na amani ziwe juu yake amemiliki dunia na akhera, na yeye anajua mambo ya ghaibu, na yanayo fanana na hayo katika maneno ya kusifu hakika kigawanyo hiki ni haramu, bali inaweza kufikia katika Shirki kubwa yenye kumtoa mtu katika mila ya Uislamu, haifai kumsifu Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa sifa ambazo hufikia kwenye hatua ya kupetuka mipaka, kwa ajili ya makatazo ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake katika hilo.

Kisha turudi kwenye kufanya kumsifu Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni chumo analochuma kwayo Mwanadamu tunasema vilevile Hakika hiyo ni haramu na haifai kabisa kwa sababu kumsifu Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa kile anacho stahiki, na kwa kitu ambacho anacho ni katika tabia njema na ni katika sifa nzuri na ni uongofu katika njia iliyo nyooka kwa sababu kumsifu kwa sifa hizo ni katika Ibada ambayo mtu hujikurubisha kwayo kwa Mwenyezi Mungu, na kitu ambacho kimekuwa ni Ibada haifai kukifanya kuwa ni njia ya kuipata dunia; kwa maneno

yake Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Wanao taka maisha ya dunia na mapambo yake tutawalipa humo vitendo vyao kamili. Na wao humo hawata punjwa**. **Hao ndio ambao hawata kuwa na kitu Akhera ila Moto, na yataharibika waliyo yafanya, na yatapotea bure waliyo kuwa wakiyatenda]** [Suratul Huud: 15-16], Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuongoza kwenye njia ya sawa.

****

**Swali la 47: Mwenye kuitakidi kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni nuru katika nuru za Mwenyezi Mungu na si Mwanadamu, na kuwa anajua mambo ya ghaibu, kisha anajikinga kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake akiamini kuwa ananufaisha na kudhuru, ni ipi hukumu ya hilo? Na je inafaa kuswali nyuma ya mtu huyu au ambaye anafanana naye? Tupeni faida katika hilo Mwenyezi Mungu akulipeni kila la kheri.**

**Jibu:** Mwenye kuitakidi kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni nuru katika nuru za Mwenyezi Mungu na si Mwanadamu, na kuwa anajua mambo ya ghaibu atakuwa amekufuru kumkufuru Mwenyezi Mungu na Mtume wake rehma na amani

ziwe juu yake, naye ni katika maadui wa Allah na Mtume wake, na si katika mawalii wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa sababu katika maneno yake hayo kuna kumkadhibisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mwenye kumkadhibisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake huyo ni kafiri, na Ushahidi kuwa maneno yake hayo ni kumkadhibisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake ni maneno yake Mwenyezi Mungu: [**Sema: Hakika si vinginevyo mimi ni Mtu mafano wenu**], [Suratul Al-Kahafi /11]na maneno yake Mwenyezi Mungu: [**Sema: Hakuna anaye jua katika mbingu na ardhi mambo ya ghaibu isipokuwa Mwenyezi Mungu**], [Suratul An-Namli: 65], na maneno Yake Mwenyezi Mungu: [**Sema: Similiki katika nafsi yangu manufaa wala madhara, ila apendavyo Mwenyezi Mungu. Na lau kuwa ninayajua ya ghaibu ningejizidishia mema mengi, wala ovu lisinge nigusa. Mimi si chochote ila ni mwonyaji na mbashiri kwa watu wanao amini.**] [Suratul Al-Araaf: 188], na maneno yake: [**Sema: Mimi sikwambii kuwa ninazo hazina za Mwenyezi Mungu. Wala sijui mambo yalio fichikana. Wala sikwambii kuwa mimi ni Malaika.Mimi sifuati ila yanayo funuliwa kwangu**] [Suratul Al-An'aam: 50], na maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake : ((**Hakika si vinginevyo mimi ni mtu mfano wenu ninasahau kama mnavyo sahau nitakapo sahau nikumbusheni**)), [Ameipokea Bukhari /401/, na Muslimu /572].

Na mwenye kujikinga kwa Mtume hali ya kuwa anaitakidi kuwa anamiliki manufaa na madhara basi huyo ni kafiri na mwenye kumkadhibisha Mwenyezi Mungu na ni mwenye kumshirikisha, na hilo ni kwa ajili ya maneno yake Mwenyezi Mungu alipo-

sema: [**Na Mola wenu mlezi amesema: Niombeni nitakujibuni. Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia Jahanam wadhalilike**] [Suratul Ghafir: 60], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Sema: Mimi sina mamlaka ya kukudhuruni wala kukuongozeni** (21) **Sema: Hakika hapana yoyote awezae kunilinda na Mwenyezi Mungu, wala sitapata pa kukimbilia isipokuwa kwakeYeye tu**] [Suratul Jinni: 22].

Na maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa watu wake wakaribu: ((**Mimi siwezi kukusaidieni kwa Mwenyezi Mungu na kitu chochote**)), [Ameipokea Bukhar /2753/, na Muslimu /351].

Na kama alivyo sema hivyo hivyo kwa Fatima Mtoto wake na Sofia Shangazi yake Mwenyezi Mungu awe radhi nao. Na wala haifai swala nyuma ya mtu huyu, na yoyote mwenye kuwa kama yeye pia haifai kuswali yuma yake, na wala haifai kumfanya kuwa ni kiongozi wa Waislamu.

****

**Swali la 48: Je Hadithi za kutoka Al-Maahadi ni sahihi au sio sahihi?**

**Jibu:** Hadithi za kutoka kwa Al-Maahadi zimegawanyika katika sehemu nne:

1-Hadithi za uongo.

2-Hadithi dhaifu.

3-Hadithi hasani lakini kwa mkusanyiko wake hufikia mpaka kwenye daraja ya usahihi, inakuwa ni sahihi kwa nyingine.

Na wamesema baadhi ya wana chuoni Mwenyezi Mungu awarehemu: Hakika kuna miongoni mwazo ni sahihi kwa dhati yake, na hiki ndio kigawanyo cha nne. Lakini sio Al-Maahadi aliye zushwa kuwa yupo Sardabi kule Iraqi, hakika huyu hana ushahidi wowote, nao ni uzushi usio na uhakika, lakini Al-Maahadi ambaye amekuja katika Hadithi sahihi zilizo thibiti ni mtu kama watu wengine katika wanadamu, huumbwa na huzaliwa katika wakati wake, na atatoka kwa watu katika wakati wake, hiki ndicho kisa cha Al- Maahadi, kukipinga moja kwa moja ni kosa, na kukithibitisha moja kwa moja pia ni kosa; kwa sababu kulithibitisha katika hali ambayo itamjumuisha Al-Maahadi wenye kungojewa ambaye husema kuwa yupo katika Sardabi, hili ni kosa; kwa sababu kuitakidi kwa Al-Maahad alojificha ni mapungufu katika akili na ni upotevu katika sheria, na ni jambo ambalo halina Ushahidi, na kumthibitisha Al-Maahadi ambaye amemuelezea Mtume  rehma

na amani ziwe juu yake na ziko Hadithi nyingi juu ya jambo hilo ambaye atazaliwa katika wakati wake na atatoka katika wakati wake hilo ni jambo la kweli.

****

### Swali la 49: Ni nani hao kina Yaajuja na Maajuja?

**Jibu:** Yaajuja wa Maajuja ni Mataifa mawili katika wanadamu, ambayo yapo, amesema Mwenyezi Mungu [**Hata alipo fika baina ya milima miwili, alikuta nyuma yake watu ambao hawakuwa wanafahamu lolote**. **Wakasema: Ewe Dhul-Qarnain hakika Yajuja wa maajuja wanafanya uharibifu katika ardhi. Basi je, tukulipe ujira ili utujengee baina yetu na wao ngome?**. **Akasema: Yale Mola wangu aliyo niwezesha ni bora zaidi. Lakini nyinyi nisaidieni kwa nguvu zenu. Nileteeni vipande vya chuma. Hata alipo ijaza nafasi iliyo kati ya milima miwili, akasema: Pulizeni, hata alipo fanya (chuma) kama moto akasema: Nileteeni shaba iliyo yayuka niimwagie**. **Basi hawakuweza kuukwea, wala hawakuweza kuutoboa**. **Akasema: Hii ni rehema itokayo kwa Mola wangu Mlezi. Na itakapo fika ahadi ya Mola wangu Mlezi atauvunja vunja. Na ahadi ya Mola wangu Mlezi ni kweli tu**} [Suratul Kahafi: 93-98].

Na anasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake ((**Atasema Mwenyezi Mungu siku ya Kiama Ewe Adam simama na upeleke kundi katika kundi la motoni miongoni mwa kizazi chako**)) mpaka aliposema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Nakupeni bishara hakika katika nyinyi mmoja katika Yajuja wa Maajuja elfu**)) [ameipokea Bukhar /3348), na Muslimu /222].

Na kutoka kwao ambako ni katika Ushahidi za Kiama zilipatika ishara zake katika zama za Mtume rehma na amani ziwe juu yake, katika Hadithi ya Ummu Habiba Mwenyezi Mungu awe radhi naye amesema: alitoka Mtume rehma na amani ziwe juu yake siku moja akiwa amefadhaika uso wake ukiwa mwekundu na huku anasema: ((**Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, ole wao Waarabu na shari ambayo imekaribia, limefunguliwa leo shimo la Yajuja wa Majuja mfano wa huu, akakutanisha kidole chake kikubwa na kinacho fuata**)) [Ameipokea Bukhari /7059], na Muslimu /2880].

****

**Swali la 50: Kwanini Mitume waliwatahadharisha watu wao na Dajali pamoja ya kuwa hatotoka isipokuwa katika zama za mwisho?**

**Jibu:** Fitna kubwa katika ardhi toka ameumbwa Adamu mpaka kusimama Kiama ni fitina ya Dajali kama alivyo sema hilo Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa ajili hiyo hakuna Mtume yoyote kuanzia Nuh mpaka Mohammad rehma na amani ziwe juu yake isipokuwa aliwatahadharisha watu wake [Ameipokea Bukhari /7127], kuhusu mambo yake, na ukubwa wa jambo hilo na kujitahadhari naye, hakika Mwenyezi Mungu anajua kuwa hato toka isipokuwa zama za mwisho, lakini aliwaamrisha Mitume wawaonye watu wao na Dajali ili iwe wazi ukubwa wake na ukali wake, na hakika aliweka wazi hilo Mtume rehma na amani ziwe juu yake na akasema: ((**Ikiwa atatoka na mimi nipo na nyiye basi mimi nitakuzuiyeni naye, na isipo kuwa hivyo kila mtu atakuwa ni mlinzi wa nafsi yake, na Mwenyezi Mungu ndie mrithi wangu kwa kila Muislamu**)), [Ameipokea Muslimu /2937]. Mbora wa warithi ni Mwenyezi Mungu aliye tukuka.

Huyu Dajali jambo lake ni kubwa, bali ndio fitna iliyo kubwa zaidi, kama ilivyo kuja katika Hadithi, toka ameumbwa Adamu mpaka Kiama kisimame, ikawa ni lazima iwekewe tahadhari maalumu katika kujikinga na fitna hii katika swala, ((**Najikinga**

**kwa Allah na adhabu ya Jahanamu, na kutokana na adhabu ya kaburi, na fitna za uhai na umauti, na fitna za Masihi Dajali**)) [Ameipoke Bukhari /1377, na Muslimu /575].

****

**Swali la 51: Ni ipi hukumu ya mwenye kukataa maisha ya kesho Akhera, na akadai kuwa huo ni uzushi wa zama za kati? Ni vipi tunaweza kuwakinahisha wapingaji hawa?**

**Jibu:** Mwenye kukataa maisha ya kesho Akhera, na akadai kuwa huo ni uzushi wa zama za kati basi huyo ni kafiri, kwa ushahidi wa maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Na walisema: Hakuna mengine ila maisha yetu haya ya duniani, wala sisi hatuta fufuliwa. Na lau ungeliona watakavyo simamishwa mbele ya Mola wao mlezi, akambiwa: Je si kweli haya? Na wao watasema:Kwanini? Tunaapa kwa Mola Mlezi wetu ni kweli. Yeye atasema: Basi onjeni adhabu kwa sababu ya vile mlivyo kuwa mnakataa.]** [Suratul Al-Anaam: 29-30].

Na akasema Mwenyezi Mungu: [**Ole wao siku hiyo kwa wanao kadhibisha**. **Ambao wanaikadhibisha siku ya malipo**. **Wala haikadhibishi ila mwenye kuruka mipaka mipaka mwenye dhambi**. **Anapo somewa Aya zetu husema: Ni visa vya watu wa kale**. **La hasha!bali yametia kutu juu ya nyoyo zao hayo waliokuwa wakiyachuma**. **La hasha! Hakika hao siku hiyo bila shaka watazuiliwa na neema za Mola wao Mlezi**. **Kisha wataingia Motoni**. **Kisha! Waambiwe:Haya ndiyo mlikuwa mkiyakadhibisha.**] [Suratul Mutwafifina: 10-17].

Na amesema Mwenyezi Mungu: [**Bali wanaikadhibisha saa (ya Kiyama**). **Na Sisi tumemuandalia Moto mkali kabisa huyo mwenye kuikanusha saa**] [Suratul Al-Furqaan: 11], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Na wale walio zikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu na kukutana naye, hao ndio wenye kukata tama na rehema yangu, na hao ndio wenye kupata adhabu yenye kuumiza**] [Suratul Al-Ankabuti: 23].

Ama kuwa kinahisha hawa wenye kupinga ni kwa vitu vifuatavyo:

**1**-kwamba jambo la kufufuliwa umekuja Ushahidi nyingi kutoka kwa mitume na katika vitabu vya Mwenyezi Mungu, na sheria za mbinguni, na Ummah zote zimelipokea hilo na kulikubali, ni vipi mnalikataa hilo, na nyinyi mnayakubali yale yalio letwa kwenu kutoka kwa Mafailasufi, au watu wa fikra, hata kama haikuwafikia kile kinacho fikIsha habari, kwa Ushahidi wa vitabu au wenye kushuhudia hali halisi!

**2**-kuwa suala la kufufuliwa hakika akili imelishuhudia kwa kuwezekana kwake kutokea, na hilo ni kwa njia zifuatazo:

**1**-Kila mmoja hapingi kuwa yeye ameumbwa baada ya kuwa alikuwa hayupo, na kwamba yeye ametokea baada ya kukosekana, basi yule aliye muumba na akafanya apatikane katika dunia hii baada ya kuwa alikuwa hayupo ni muweza wa kumrudisha alipo kuwa mara ya mwanzo, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: **[Na Yeye ndiye anaye anzisha uumbaji, kisha ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi kwake. Naye ndiye mwenye mfano bora katika mbingu na ardhi. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima]** [Suuratul Al Ruum: 27], na amesema Mwenyezi Mungu: **[ Kama tulivyo anza umbo la mwanzo tutalirudisha tena. Ni ahadi iliyo juu yetu. Hakika Sisi ni watendao]** [Suratul Anbiyaa: 104].

**2**-Kila mmoja hapingi ukubwa wa umbo la mbingu na ardhi kwa ukubwa wake na uzuri wa uumbwaji wake, basi ambaye ameviumba viwili hivyo ni muweza wa kuwaumba watu kisha kuwarudisha walipo kuwa katika umbile la mwanzo; Amesema Mwenyezi Mungu: **[Bila ya shaka kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko kuwaumba watu. Lakini watu wengi hawajui.]** [Suratu Al-ghafir: 57], na amesema Mwenyezi Mungu: **[ Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, aliye ziumba mbingu na ardhi, na hakuchoka kwa kuziumba, kuwa ni Muweza wa kuwafufua wafu? Kwani? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu]**, [Suratul Al-Ahqaaf: 33], na amesema Mwenyezi Mungu: **[Kwani aliye ziumba mbingu na ardhi hawezi kuwaumba mfano wao? Kwani! Naye ndiye Muumbaji Mkuu, Mjuzi. Hakika amri yake**

**anapo taka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa]** [Suratul Yasin: 81-82].

**3**-Kila mwenye akili huishuhudia ardhi ikiwa kavu yenye mimea iliyo kufa, pindi inapo shuka mvua tu, hupata rutuba na kuwa hai mimea yake baada ya kuwa ilikufa, basi muweza wa kuihuisha ardhi baada ya kufa kwake, ni muweza wa kuwapa uhai wafu na kuwafufua, amesema Mwenyezi Mungu: [**Na katika Ishara zake ni kwamba unaiona ardhi nyonge, lakini tunapo iteremshia maji mara unaiona inataharaki na kuumuka. Bila shaka aliye ihuisha ardhi ndiye atakaye huisha wafu. Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu**] [Suratul Fusswilat: 39].

**4**-Hakika jambo la ufufuo imeshuhudia hisia juu ya kuwezekana kwake, katika yale alotuhabarisha Mwenyezi Mungu katika matukio ya kuwahuisha wafu, hakika amelitaja hilo katika Suratu Al-Baqara kwenye matukia matano miongoni mwake ni katika maneno yake: [**Au kama yule aliye pita karibu na mji ulio kwisha kuwa magofu, akasema: Ataufufuaje Mwenyezi Mungu mji huu baada ya kufa kwake? Basi Mwenyezi Mungu alimfisha yeye muda wa miaka mia.Kisha akamfufua. akamuuliza: Je umekaa muda gani? AkaJibu: Labda nimekaa siku moja au sehemu ya siku. Akamuambia: Bali umekaa miaka mia. Hebu angalia chakula chako na vinywaji vyako, havikuharibika. Na muangalie punda wako. Na ili tukufanye uwe ni ishara kwa watu iangalie hii mifupa yake jinsi tunavyo inyanyua kisha tunaivisha nyama. Basi yalipo bainika alisema: Najua kwamba Mwenyezi Mungu ni mwenye uweza juu ya kila kitu**] [Suratul Baqara: 259].

**5**-Hakika hekma ya kukufuliwa inahukumu hivyo ili kila nafsi ilipwe kwa kila ilicho kichuma, lau kama sio hivyo ingekuwa kuumbwa kwa Mwanadamu ni bure na mchezo tu hakuna faida kabisa, wala hakuna hekma yoyote, na wala kusinge kuwa na tofauti kati ya Mwanadamu na wanyama katika haya maisha, amesema Mwenyezi Mungu: [**Je! Mlidhani ya kuwa tulikuumbeni bure na kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa**? **Ametukuka Mwenyezi Mungu Mfalme wa haki, hapana Mola ila Yeye, Mola Mlezi wa Arshi Tukufu**: 115-116] [Suratul Al-Muminun], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Hakika saa itakuja bila shaka. Nimekaribia kuificha, ili kila nafsi ilipwe kwa iliyo yafanya**] [Surat Twaha: 15], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu ukomo wa viapo vyao kwamba Mwenyezi Mungu hatomfufua aliye kufa.Kwani! Ni ahadi iliyo juu yake kikweli; lakini watu wengi hawajui**. **Ili kuwabainishia yale waliyo khitalifiana, na ili wajue walio kufuru kwamba wao walikuwa ni waongo**. **Hakika si vinginevyo kauli yetu kwa kitu tunacho kitaka kiwe, ni kukiambia: kuwa! Basi kinakuwa.**] [Suratul Nnahali: 38, 39-40], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Wale walio kufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa. Sema: Kwanini? Naapa kwa Mola wangu Mlezi hapana shaka mtafufuliwa, na kisha hapana shaka mtaambiwa mloyafanya, na hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu**] [Suratul-Taghaabun: 7].

Utakapo kuwa umebainishwa ushahidi huu kwa wenye kupinga kufufuliwa, kisha wakaendelea kupinga, basi wao watakuwa ni wenye kufanya kibri kisha niwapinga haki, na watajua kesho wale walio dhulimu ni marejeo gani watakayo yarejea.

****

## Swali la 52: Je adhabu ya kaburi imethibiti?

**Jibu:** Adhabu ya kaburi imethibiti kwa ushahidi wa Sunna zilizo wazi na Qur`an iliyo dhahiri kabisa, na pia ndio makubaliano ya wana vyuoni, kwa Ushahidi hizo tatu.

Ama ushahidi wa Sunna hakika amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Jikingeni kwa Mwenyezi Mungu kutokana na adhabu ya kaburi, jikingeni kwa Mwenyezi Mungu kutokana na adhabu ya kaburi, jikingeni kwa Mwenyezi Mungu kutokana na adhabu ya kaburi**)) [Ameipoke Muslimu 2867].

Na ama makubaliano ya Wanavyuoni, ni kwa sababu Waislamu wote wanasema katika swala zao, (( Najikinga kwa Mwenyezi Mungu kutokana na adhabu ya Jahanam, na kutokana na adhabu ya kaburi)), mpaka Watu wa kawaida ambao hawajasoma ambao si katika Watu wa Ijmaa wala si Maulamaa pia husema hivyo.

Ama ushahidi katika Qur`an, mfano ni maneno yake Mwenyezi Mungu kuwaambia Watu wa Fir-auni: [**Wanaoneshwa Moto asubuhi na jioni. Na itakapo fika saa ya Kiama patasemwa: Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali kabisa**], [Suratul Ghafir: 46]. Hakuna shaka kuingizwa kwao katika Moto si kwa ajili wajifariji humo ndani yake, bali ni kwa ajili iwapate adhabu ya Moto huo, na amesema Mwenyezi Mungu: [**Na lau ungeliwa-**

**ona madhalimu wanavyo kuwa katika mahangaiko ya mauti, na Malaika wamewanyoshea mikono wakiwaambia: Zitoeni roho zenu**], Mwenyezi Mungu ni mkubwa wanazionea ubakhili nafsi zao hawataki zitoke, Mwenyezi Mungu anawaambia: [**Leo mtalipwa adhabu ya fedheha kwa sababu ya mliyo kuwa mkiyasema juu ya Mwenyezi Mungu yasiyo ya haki, na mlivyo kuwa mkizifanyia kibri Ishara zake**], [Suratul Al-An'aam: 93].

Kwa hivyo, adhabu ya kaburi imethibiti kwa ushahidi wa Kitabu, Sunna na Ij'maa ya Waislamu, na hili lipo wazi katika Qur`an kwa sababu Aya mbili tulizo zitaja zipo wazi juu ya hilo.

****

**Swali la 53: Pindi atakapo kuwa Maiti hajazikwa ameliwa na mnyama au amepukutika akachukuliwa na upope. Je ataadhibiwa adhabu za kaburi?**

**Jibu:** Ndiyo, na itakuwa adhabu ni katika roho kwa sababu mwili umekwisha na umeharibika, japo kuwa jambo hili ni katika mambo ya ghaibu siwezi kuwa na uhakika kuwa mwili haupati adhabu hii hata kama utakuwa umekwisha kwa sababu mambo ya Kiakhera hawezi Mwanadamu kuyafananisha na ya kidunia.

****

**Swali la 54: Ni vipi tutamjibu mwenye kupinga adhabu ya kaburi, na anatoa hoja kuwa lau kama tutalifukuwa kaburi tutalikuta halikubadilika na wala halikubana wala kutanuka?**

**Jibu:** Hujibiwa mwenye kupinga adhabu za kaburi kuwa ushahidi wa kuwa lau kama atalifukuwa atakuta hakuna mabadiliko, hujibiwa kwa majibu mengi miongoni mwake:

1- Kuwa adhabu ya kaburi imethibiti katika Sheria, amesema Mwenyezi Mungu: [**Wanaoneshwa Moto asubuhi na jioni. Na itakapo fika saa ya Kiama patasemwa: Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali kabisa**] [Suratul Ghafir: 46]. Na maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Na lau kama nisinge hofia msije mkaacha kuzikana, ningemuomba Mwenyezi Mungu akusikilizisheniadhabu za kaburi ambazo Mimi huzisikia**)), kisha akawaelekea kwa uso wake akasema: ((**Jikingeni kwa Mwenyezi Mungu kutokana na adhabu ya Moto**)), wakasema: Tunajikinga kwa Mwenyezi Mungu kutokana na adhabu ya Moto akasema: ((**Jikingeni kwa Mwenyezi Mungu kutokana na adhabu za kaburi**)), wakasema: Tunajikinga kwa Mwenyezi Mungu kutokana na adhabu za kaburi. [Upokelewaji wake umetangulia].

Na maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa Waumini: ((**Hutanuliwa kaburi lake upeo wa kuona macho**))

[Ameipokea Bukhar /1374/, na Muslimu /2870]. Na ushahidi mwingine usokuwa huu tuloutaja, basi haifai kuupinga ushahidi huu kwa maneno ya kudhania, bali kilicho cha wajibu ni kuukubali na kuusadikisha.

**2**-Kiasili adhabu ya kaburi ni katika roho, na sio jambo lenye kuhusiwa katika mwili, na lau kama lingekuwa ni jambo lenye kuhisiwa katika mwili lisinge kuwa ni katika mambo ya ghaibu, na isinge kuwa kuliamini jambo hilo kuna faida, lakini katika mambo ya ghaibu, na hali katika maisha ya barzaha (kaburini) hayifananishwi na maisha ya duniani.

**3-**Hakika adhabu, neema na upana wa kaburi na ufinyu wake, hakika si vinginevyo anavijua maiti tu na sio mtu mwingine, Mwanadamu anaweza kuona katika usingizi hali ya kuwa amelala katika kitanda chake, kuwa amesimama, anakwenda anarudi, anapiga anapigwa, na anaweza kuona kuwa yupo kwenye nafasi finyu yenye kutisha, au yupo kwenye sehemu pana nzuri, na yule aliye pembeni mwake hayaoni hayo wala hayahisi. Kilicho cha lazima katika mambo kama haya ni kusema: Tumesikia na tumetii na tumeamini na tumekubali kuwa ni kweli

****

**Swali la 55: Je hupunguzwa adhabu ya kaburi kwa Muumini ambaye ni mwenye kuasi?**

**Jibu:** Amejibu kwa kusema: ndio; anaweza kupunguziwa kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake: alipita katika makaburi mawili akasema: ((**Hakika hawa wawili wanaadhibiwa, na si kwamba wanaadhibiwa kwa mambo makubwa, bali ni makubwa; ama mmoja wao alikuwa hajiepushi na cheche za mkojo wakati akikojoa, na ama mwingine alikuwa akitembea huku anaeneza umbea**)), kisha akachukua tawi la Mtende vibichi akalichana vipande viwili, akachomeka katika kila kaburi kipande kimoja na akasema: ((**Huenda wakapunguziwa adhabu muda wa kwamba havija kauka**), [Ameipokea Bukhar/1378/, na Muslimu /292].

Huu ni ushahidi kuwa huenda adhabu ikapunguzwa, lakini ni yapi mahusiano ya matawi haya mawili na kupunguzwa adhabu kwa hawa wawili wenye kuadhibiwa?

**1-**Kumesemwa: Kwa kuwa matawi haya ni yenye kumsabihi Mwenyezi Mungu muda wa kuwa hajakauka, na tasbihi ni yenye kupunguza adhabu kwa maiti, hakika wametoa katika hekma hii walio itoa kwenye Hadithi hii, kuwa ni Sunna kwa mwanadamu anapokuwa makaburini awe anamsabihi Mwenyezi Mungu hapo makaburiri kwa sababu ya kuwapunguzia adhabu walioko pale wale wanao adhibiwa.

**2-**Na wamesema baadhi ya Maulamaa Mwenyezi Mungu awarehemu: Sababu hii ni dhaifu kwa kuwa matawi mawili yale yanamsabih Mwenyezi Mungu ni sawa yakiwa mabichi au yamekauka ushahidi wa hilo ni maneno ya Mwenyezi Mungu: [**Zinamtakasa mbingu saba na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake. Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa sifa zake. Lakini nyinyi hamfahamu kutakasa kwake**] [Suratul Al-Israa /44], na hakika ilisikiwa tasbihi ya jiwe mbele ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake pamoja ya kuwa jiwe ni kavu, kwa hiyo ni nini tatizo kwenye tawi kavu?.

Tatizo kwenye tawi kavu: Ni kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alitarajia kutoka kwa Mwenyezi Mungu wapunguziwe adhabu muda wa kuwa matawi haya mawili ni mabichi, ina maana Muda sio mrefu, na hilo ni kwa ajili ya kutahadharisha katika kitendo chao hicho kwa sababu kitendo hicho ni kikubwa kama kilivyo kuja katika baadha ya riwaya ((kwani hakika hilo ni jambo kubwa)), mmoja wao alikuwa hajiweki mbali na cheche za mkojo, ikiwa hajiweki mbali na cheche za mkojo ina maana huswali pasna Twahara, na mwingine alikuwa akitembea huku anaeneza Umbeya anafanya ufisadi kati ya waja, na anapandikiza kati yao uadui na chuki, ikiwa ni hivyo basi jambo ni kubwa, na hili ndilo lililo karibu kuwa ilikuwa ni Shafaa ya muda kwa ajili ya kuutahadharisha Ummah na sio ubakhili kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuto kuwaombea Shafaa ya yenye kudumu.

**Tunasema**: Hakika baadhi ya Maulamaa Mwenyezi Mungu awasamehe-wamesema: Ni Sunna kwa Mwanadamu kuwekewa tawi bichi, au kipande cha mti, au mfano wake katika kaburi ili kiwapunguzie adhabu, lakini uvumbuzi wao huo upo mbali sana, na wala haifai tufanye hivyo kwa mambo yafuatayo:

1-Hakika sisi haijafunuliwa kwetu kuwa Mtu huyu anaadhibiwa, ni kinyume na Mtume rehma na amani ziwe juu yake:

2-Hakika sisi tutakapo fanya hivyo tutakuwa tumemkosea Maiti; kwa sababu tutakuwa tumemdhania dhana mbaya kuwa anaadhibiwa, na ni lipi litakalo tujulisha huenda akawa ananeemeka, huenda huyu Maiti ni katika wale alowanemesha Mwenyezi Mungu kwa msamaha kabla ya kupatwa na Umauti, kwa sababu ya kuwepo sababu nyingi katika sababu ya kusamehewa ambazo ni nyingi basi akafa hali ya kuwa Mola wa waja amemsamehe, na wakati huo akawa hastahiki adhabu.

3-Hakika uvumbuzi wao huu unakwenda kinyume na yale walokuwa nayo Wema walio tangulia, Mwenyezi Mungu awarehemu, ambao wao walikuwa ni wajuzi zaidi ya Sheria za Mwenyezi Mungu miongoni mwa Watu na hakufanya hivyo hata mmoja katika maswahaba Mwenyezi Mungu awe radhi nao, kwa nini sisi tufanye!?

4-Hakika Mwenyezi Mungu ametufundisha lililo bora zaidi kuliko hilo, alikuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake anapo maliza kumzika Maiti husima katika kabuti lake na anasema: ((**Matakieni msamaha ndugu yenu na mmuombee uthibitifu hakika yeye hivi sasa anaulizwa**)), [Ameipoke Abuu Daud 3221].

****

**Swali la 56: Ni nini Shafaa? Na ni vipi vigawanyo vyake?**

**Jibu:** Neno Shafaa, limechukuliwa katika neno Al Shufaa, nalo ni kinyume na witri, nayo ni kuifanya witri kuwa shufaa, mfano ni kuifanya moja kuwa mbili, na tatu kuwa nne, na kuendelea; na hii ni katika Lugha ya Kiarabu.

Ama katika Istilah ((Ni kupitia kwa mwingine kwa ajili ya kuleta manufaa au kuondosha madhara)), inamaana: awe muombaji kati ya muombewa na mwenye kuombwa katika kuleta manufaa

kwa mwenye kuombewa, au kuondosha madhara kwake.

Na Shafaa imegawanyika vigawanyo viwili:

1-Shafaa ambayo imethibiti na ni sahihi, nayo ni ile ambayo ameithibitisha Mwenyezi Mungu katika kitabu Chake, au ameithibitisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na haiwi isipokuwa ni kwa Watu wenye Tauhidi na Ikhlaswi; kwa sababu Abu Huraira Mwenyezi Mungu awe radhi naye amesema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni nani mwenye furaha zaidi kwa Shafaa yako? Akasema: ((**Mwenye kusema: Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu kwa Ikhlasi kutoka katika Moyo wake**)), [Ameipokea Bukhari 99].

Na Shafaa hii ina sharti tatu:

1-Mwenyezi Mungu kumridhia mwenye kuomba.

2-Mwenyezi Mungu kumridhia mwenye kuombewa.

3-Idhini ya Mwenyezi Mungu kwa mwenye kuomba aombe hiyo Shafaa.

Sharti hizi zipo katika maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa chochote isipokuwa baada ya Mwenyezi Mungu kutoa idhini kwa amtakaye na kumridhia**] [Suratul Najm: 26].

Na zikawekwa wazi zaidi katika maneno yake: [**Ni nani huyo awezae kuombea mbele yake bila idhini yake**] [Suratul Al-Baqara: 255], na maneno yake: [**Siku hiyo uombezi haufai kitu ila kwa wale aliyo waruhusu Arhamani Mwingi wa Rehema na akamridhia kusema**] [Suratul Twaha: 109], na maneno yake: [**Wala hawamwombei yeyote ila yule anaye mridhi Yeye**] [Suratul Anbiyaa: 28], hapana budi kupatikana sharti hizi tatu ili Shafaa ikamilike.

Kisha hakika Shafaa iliyo thibiti wameitaja Maulamaa Mwenyezi Mungu awarehemu, kuwa imegawanyika katika sehemu mbili:

**1-Shifaa kwa wote**: Na maana ya Shafaa kwa wote ni kuwa Mwenyezi Mungu atawaruhusu anao wataka katika waja wake wema kuwaombea Shafaa kwa wale alio wapa idhini Mwenyezi Mungu kuwaombea Shafaa, na Shafaa hii inakuwa kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake na kwa wengine katika Mitume, na wale Wakweli, na Mashahidi, na Wema, na ni kuwaombea Shifaa watu wa Motoni miongoni mwa Waumini walio asi ili watoke katika Moto.

**2-Shifaa maalumu**: Amabayo ni maalumu kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na kubwa ni Shafaa ambayo itakuwa siku ya Kiama, wakati watakapo kutana watu na huzuni na dhiki ambazo hawaziwezi, watamtafuta mwenye kuwaombea Shafaa kwa

Mwenyezi Mungu ili awapumzishe na hali hiyo kubwa, watakwenda kwa Adam, kisha kwa Nuh, kisha kwa Ibrahim, kisha kwa Mussa, kisha kwa Issa, wote hao hawata omba Shafaa mpaka watakapo fika kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake atasimama na ataomba Shifaa kwa Mwenyezi Mungu ili awaondoe waja wake katika hali hiyo ngumu, Mwenyezi Mungu atamjubu dua yake, na ataikubali Shafaa yake, na hii ndio Makamu Mahmuda mbayo Mwenyezi Mungu alimuahidi katika maneno yake: [**Na amka usiku kwa ibada;ni ziada ya Sunnahh khaswa kwako wewe.Huenda Mola wako mlezi akakunyanyua cheo kinacho sifika**], [Suratul Al-Israa: 76]. [Ameipokea Bukhari 4776/, na Muslimu, 193].

Na katika Shifaa ambayo ni maalumu kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni uombezi wake kwa watu wa peponi waingie peponi, hakika watu wa peponi watakapo kuwa wamevuka njia na wakasimama katika daraja kati ya Pepo na Moto, zitafitinika nyoyo za badhi yao mpaka watakapo chaguliwa, kisha wataitwa kuingia peponi, basi itafunguliwa Milango ya peponi kwa Shifaa ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake [Ameipokea Bukhari: 2440].

2-Shifaa ya batili ambayo haimsaidii mwenye kuombewa, nayo ni ile wanayo idai washirikina kutoka kwa waungu wao kuwa watawaombea mbele ya Mwenyezi Mungu, hakika shafaa hii haita wafaa kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Haitawafaa wao shafaa ya wenye kuwaombea**], [Suratul Al-Mudathir: 48], na hilo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu haridhiki kush-

irikishwa na washirika hawa, na wala haiwezekani kuwapa idhini hawa waombe shafaa kwa sababu hakuna shafaa isipokuwa kwa yule Mwenyezi Mungu alomridhia, na Mwenyezi Mungu haridhii kwa waja wake ukafiri wala ufisadi, Washirikina kufungamana na miungu yao hii wakiwaabudu kinyume na Mwenyezi Mungu na huku wanasema: [**Hawa ndio waombezi wetu mbele ya Mwenyezi Mungu**], [Suratul Yunus: 18]. Huku ni kufungamana kwa batili kusiko na manufaa, bali hakuwazidishii wao kwa Mwenyezi Munguisipokuwa kuwa mbali zaidi na Mwenyezi Mungu, na hilo ni kwa sababu wanataraji shafaa kutoka kwa masanamu yao kwa njia ya batili, nayo ni kuyaabudu masanamu haya, na huu ni katika ujinga wao, kwa kufanya kujikurubisha kwao kwa Mwenyezi Mungu ni kwa kitu ambacho hakiwazidishii isipokuwa kuwa mbali zaidi.

****

### Swali la 57: Ni yapi mafikio ya watoto wa Waumini na watoto wa Washirikina wale ambao wamekufa wakiwa wadogo?

**Alijibu Sheikh kwa kusema**: Mafikio ya watoto wa Waumini ni peponi kwa sababu wao ni wenye kuwafuata Baba zao amesema Mwenyezi Mungu: [**Na wale walio amini na vizazi vyao wakawafuata kwa Imani tutawakutanisha na vizazi vyao, na wala hatuta wapunja hata kigogo katika vitendo vyao. Kila mtu lazima atapata alicho kichuma**.] [Suratul Tuuri: 21].

Ama watoto wasio kwa wa Waumini, inamaana: Watoto ambao wamekuwa hali ya kuwa Wazazi wake sio Waislamu, maneno yaliyo sahihi kwao ni tuseme: Mwenyezi Mungu anajua kwa yale walokuwa wakiyafanya, wao katika hukumu za kidunia ni kama Baba zao, ama katika hukumu za Akhera hakika Mwenyezi Mungu anajuwa kwa yale walokuwa wakiyafanya, kama alivyo sema Mtume rehma na amani ziwe juu yake. [Ameipokea Bukhari 1383, na Muslimu 2660], Mwenyezi Mungu anajua mafikio yao. Na hayo ndio tunayo sema sisi, na ukweli wa mambo jambo hili halituhusu sana, hakika jambo linalo tuhusu sana ni katika hukumu zao za kidunia, na hukumu zao katika Dunia hakika wao ni kama Washirikina hawaoshwi, wala hawavushwi sanda, wala hawaswaliwi, na wala hawazikwi kwenye makaburi ya Waislamu, Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi.

****

**Swali la 58: Imetajwa kuwa Wanaume watakuwa na Mahurul-Ayni Peponi je Wanawake nao watakuwa nao?**

**Jibu:** Anasema Mwenyezi Mungu katika kuzitaja neema za Watu wa peponi: [**Na humo mtapata kila kinacho tamaniwa na nafsi zenu, na humo mtapata mtakavyo vitaka** 31**. Ni takrima itokayo kwa Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu**], [Suratul Fusswilat: 32], na anasema Mwenyezi Mungu: [**Na vitakuwemo ambavyo nafsi zinzvipenda na macho yanavifurahiya,na nyinyi mta kaa humo milele**], [Suratul Zuhuruf: 71].

Na ni kitu kinajulikana kuwa kuoa au kuolewa ni katika vitu ambavyo nafsi inavipenda, basi hilo litapatikana Peponi kwa Watu wa Peponi kwa Wanaume na Wanawake, Mwanamke Mwenyezi Mungu atamuozesha Peponi Mwanaume amabaye alikuwa ndio mume wake Duniani, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Mola wetu Mlezi waingize katika Bustani za milele ulizo waahidi. Na uwape haya pia wale walio fanya mema miongoni mwa wazee wao na wake zao na vizazi vyao. Hakika ni mwenye nguvu, mwenye hikima**] [Suratul Al-Ghafir: 8], na iwapo atakuwa alikuwa hajaolewa duniani basi Mwenyezi Mungu atampa Peponi yule ambaye jicho lake litatulizika kwake.

****

## Swali la 59: Je yanayo tajwa kuwa wengi katika Watu wa motoni ni Wanawake ni kweli? Na ni kwanini?

**Jibu:** Hilo ni kweli, hakika Mtume rehma na amani ziwe juu yake alisema kuaambia Wanawake akiwa anawahutubia; ((**Enye kongamano la Wanawake toeni sana Sadaka hakika mimi nimewaona ndio wengi katika Watu wa motoni, na hakika lililetwa tatizo hili kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake ambalo muulizaji amelileta, wakasema Wanawake:Kwanini ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu,akasema**: ((**Mnazidisha kutukana na kulaani na mnawakataa watu wa karibu yen u ambaye ni mume**)) [Ameipokea Bukhari 304/, na Muslimu 889].

Amebainisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake sababu ya kuwa wengi Motoni kuwa ni kuzidisha kwao kutukana na kulaani, na wanawapinga watu wa karibu ambao ni waume zao, wakakawa kwa hilo ni wengi katika Moto.

****

**Swali la 60: Ni upi muongozo wenu kwa asiyetaka kusoma Aqida hasahasa mambo ya Qadari kwa kuogopa kuwa watateleza?**

**Jibu:** Mas’ala haya ni kama mas’ala mengine muhimu ambayo hapana budi mtu kuyajua kwa ajili ya Dini yake na akhera yake, hapana budi azame ndani yake na aombe Mwenyezi Mungu amsaidie kuhakikisha anayajua mas’ala haya vizuri ili imbainikie kila kitu kwake, kwa sababu hatakiwi kuwa na shaka katika mambo haya muhimu, ama katika mas-ala ambayo haya haribu dini yake hata kama atayaacha na wala haiogopewi hiyo ikawa ni sababu ya kupotea kwake, basi hakuna ubaya kama atayaakhirisha muda wa kuwa mengine ni muhimu zaidi ya hilo, na mas-ala ya Qadari ni katika mambo muhimu ambayo mtu anatakiwa ayajue vizuri ili awe ya yaqini, na Mas’ala haya kiuhakika sio katika masala yenye matatizo, na jambo linalo tia uzito katika darsa za Aq-

ida kwa baadhi ya watu kwamba wao kwa machukivu makubwa wanarajihisha upanda ((vipi)) kuliko upande wa ((kwanini)), na mwanadamua ataulizwa kuhusu matendo yake kwa dhana mbili katika dhana za kuulizia nazo ni ((kwanini)na ((vipi)) kwanini umefanya hivi? Hii ni Ikhlaswi.Vipi umefanya hivi? Huku ni kumfuata Mtume rehma na amani ziwe juu yake ,na watu wengi hivi sasa wanashughulika na kutafuta jibu la ((vipi)) wameghafilika na kutafuta jibu la (kwanini)), na kwa sababu hiyo utawakuta katika upande wa Ikhlasi hawazami sana, na katika upande wa (mutaabaa) kumfuata Mtume rehma na amani ziwe juu yake  wanazama sana mpaka kwenye mambo ya ndani kabisa, watu kwa sasa wanatilia umuhimu katika upande huu, wakighafilika katika upande muhimu nao ni upande wa Aqida, upande wa Ikhalas, na upande wa Tauhidi.

Kwa hiyo utawakuta watu katika mambo ya kidunia wakiuliza maswala madogo sana tena sana, na moyo wake ukiwa umezama katika dunia ameghafilika na Mwenyezi Mungu kabisa katika kuuza kwake na kununua kwake vipando vyake, makazi yake, nguo zake, wanaweza kuwa baadhi ya watu kwa sasa ni wenye kuiabudu dunia hali ya kuwa yeye mwenyewe hajui, na anaweza kuwa ni mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu katika dunia hali kuwa mwenyewe hajui, kwa sababu kwa machukivu makubwa hatalii umuhimu upande wa Tauhid na upande wa Aqida, na hilo sio kwa wale ambao hawakusoma tu hata kwa baadhi ya wanafunzi, na jambo hili ni lenye hatari sana, kama vile ilivyo kuwa kujikita katika Aqida tu bila matendo ni kosa vilevile, kwa sababu sisi tunasikia katika maredio na tunasoma katika magazeti kutilia mkazo kuwa Dini ni itikadi nyepesi na zinazo fanana na hizo katika ibara, na ukweli ulivyo hakika hilo huogopewa ndani yake kuwa ni mlango wa kuingia mwenye kuingia katika kuhalalisha baadhi ya

mambo ya haramu kwa hoja kuwa Aqida ipo salama, lakini hapana budi kuangalia mambo yote mawili kwa pamoja ili liwe sawa Jibu la ((kwanini)) na ((vipi)).

**Na jibu kwa ufupi**: Hakika inampasa mtu kusoma elimu ya Tauhidi na Aqida, ili awe na uoni kwa Mola wake anaye muabudu, na awe na ujuzi katika majina ya Mwenyezi Mungu na sifa zake na matendo yake, na awe na ujuzi katika hukumu za Kauniya na Shariiya, na awe na ujuzi katika hekima za Mwenyezi Mungu, na siri za sheria yake na umbaji wake, ili asipoteze nafsi yake na asipoteze wengine.

Elimu ya Tauhidi ndio elimu bora kabisa kwasababu ya ubora wa yule iloambatana nae ambaye ni Mwenyezi Mungu, kwa ajili hiyo baadhi ya wanachuoni wakubwa wameita (Al-Fiqh Al-Kabir), na amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Yule ambaye Mwenyezi Munguhumtakia kheri humpa ujuzi katika dini**)), [Ameipokea Bukhari 71/, na Muslimu/1037].

La kwanza linalo ingia hapo na la muhimu zaidi ni elimu ya Tauhid na Aqida, lakini ni wajibu kwa kila mtu aangalie anachukuaje hii elimu, na anaichukua kutoka katika vyanzo gani, achukue katika elimu hii kwanza ile ilokuwa safi na imesalimika na shubhati, kisha aende katika hatua nyingine kuangalia mambo yalowekwa katika bidaa na shubhati ile asimame kuzifanyia radi na kuzibainisha kutokana na kile alicho kichukua katika Aqida iliyo safi, lakini viwe vyanzo halisi anavyo chukua Aqida hiyo ni kitabu cha

Mwenyezi Mungu na Sunnah za Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kisha maneno ya Maswahaba Mwenyezi Mungu awe radhi nao, kisha yale walosema waliokuja baada yao miongoni mwa Tabiyyina na walio wafuata, kisha yale walosema wana vyuoni wenye kuaminika kwa elimu yao na uaminifu wao, hasahasa Sheikh Al-Islam Ibnu Taymiya na mwanafunzi wake Ibnu Al- Qayim Rehema na amani ziwe juu yao na Waislamu wote kwa ujumla.

****

**Swali la 61: Tunatarajia kwa fadhila zenu utuwekee wazi mas-ala ya Qadar? Je asili ya kitendo chenyewe kimesha kadiriwa ile namna ya kufanya ndiyo anayo ichagua Mwanadamu? mfano wa hilo: Pindi Mwenyezi Mungu anapo mkadiria mja wake ajenge Msikiti hakika hakuna budi atajenga lakini amemuachia akili yake ichague namna ya kujenga, na hivyo hivyo katika maasi Mwenyezi Mungu atakapo mkadiria Mtu atafanya hakuna namna ya kukwepa, lakini amemuachia katika akili yake namna ya kuyafanya, na ufupisho wa rai hii ni kuwa Mwanadamu anachagua namna ya kulifanya lile alilo kadiriwa na Mwenyezi Mungu, Je hiyo ni sahihi?**

**Jibu:** Katika mas'ala haya kumetokea mijadala mikubwa baina ya watu katika zama za zamani, kwa ajili hiyo watu wamegawanyika katika hilo makundi matatu, mawili yapo katika ncha na moja kati na kati.

**Ama makundi yaliyo katika ncha**:

**1**-Upande wa kwanza: Wameangalia kwa ujumla katika Qadar za Mwenyezi Mungu,hawakuona kwenye uchaguzi wa mja. Wakasema: Hakika Mja ni mwenye kulazimishwa katika matendo yake, na hana katika hilo uchaguzi wowote,kuanguka mtu kutoka katika paa la nyumba kwa sababu ya upepo na mfano wake ni kama kushuka kwake katika ngazi kwa kupenda mwenyewe.

**2-Ama upande wa pili:** Wameangalia kwawa Mja ni (Mtendaji/Muachaji) kwa matakwa yake, hawakuona kwenye Qadar ya Mwenyezi Mungu. Wakasema: Hakika Mja anajitegemea kwenye matendo yake, na wala hakuna uhusiano na Qadar ya Mwenyezi Mungu ndani yake.

**Ama kundi la kati na kati:** wameona sababu mbili, wameangalia Qadar za Mwenyezi Mungu kiujumla na wakaangalia uchaguzi wa Mja, wakasema: Hakika matendo ya Mja huwa kwa Qadar ya Mwenyezi Mungu na kwa uchaguzi wa Mja, hakika yeye anajua tofauti ya kuanguka Mwanadamu kutoka kwenye paa la nyumba kwa upepo au kitu kingine na kuteremka mwenyewe kwa kupenda kwa kutumia ngazi, huyu wa kwanza kitendo kimefanyika kwake lakini si kwa kutaka yeye, lakini wa pili kitendo

kimefanyika kwake kwa kutaka yeye mwenyewe, na yote matendo mawili yametokea kwa Mwenyezi Mungu kutaka na kwa Qadar yake, haiwezi kutotea katika umiliki wake kitu ambacho hakitaki, lakini kitu kinacho tokea kwa Mja kuchagua ni kwa lengo la kuwaagizwa, na wala haiwi ni ushahidi kwake kwa kwenda kinyume na yale aliyo amrishwa miongoni mwa amri au makatazo, na hilo ni kwa sababu yeye huliendea kosa wakati anapo liendea hali ya kuwa hajui lile ambalo Mwenyezi Mungu amemkadiria juu yake, basi huwa kuliendea kwake ni kwa uchaguzi wake kufanya kosa hilo, nayo inakuwa ni sababu ya kuadhibiwa ni sawa sawa imekuwa ni duniani au akhera, na kwa sababu hiyo la kama atamlazimisha mwenye kumlazimisha kufanya kosa haiwezi kuthibiti juu yake hukumu ya kosa hilo na wala hatoadhibiwa kwa kosa hilo kwa sababu atakuwa na udhuru juu ya hilo kwa wakati huo.

Atakapo kuwa Mwanadamu anajua kuukimbia kwake moto kwenda katika sehemu ambayo atakuwa salama na moto huo ni kwa kuchagua kwake, na kwamba kwenda kwake katika nyumba nzuri pana yenye makazi mazuri ili akaishi hapo inakuwa ni kwa kuchagua kwake vile vile, pamoja na kuamini kwake kuwa kuliepuka jambo hilo na kuliendea kwake kulikotajwa kunatokeya kwa kutaka Mwenyezi Mungu na kwa uwezo wake, na kwamba kubaki kwake mpaka moto umpate, na kuchelewa kwake kwenye kuishi katika ile nyumba nzuri huhesabiwa ni makosa yake na kupoteza kwake nafasi na anastahiki kulaumiwa kwa hilo, kwa nini asiliendee hili ambalo litampeleka katika kuokoka na moto na kwenda katika pepo!?.

Ama kutoa mfano kuwa Mwenyezi Mungu akikadiria jambo kwa Mja wake kuwa ajenge msikiti kwamba atajenga huo msikiti hakuna namna, lakina ameiachia akili yake kuchagua namna ya ujenzi, mfano huu sio sahihi, kwa sababu atafahamishwa kuwa namna ya kujenga huhusishwa na akili na wala haiingii kwenye makadirio ya Mwenyezi Mungu, na kuwa asili ya fikra ya kujenga huhusishwa na na qadar ya Mwenyezi Mungu na wala hakuna kuingia uchaguzi ndani yake.

Na ukweli ulivyo kuwa asili ya fikra ya kujenga huingia kwenye uchaguzi wa Mja; kwa sababu hakulazimishwa juu ya jambo hilo, kama ambavyo halazimishwi katika fikra ya kurudia kuijenga nyumba yake mwenyewe au kuiimarisha, lakini fikra hii ameikadiria Mwenyezi Mungu kwa Mja wake kwa namna ambayo hahisi; kwa sababu hajui kuwa Mwenyezi Mungu amemkadiria kitu flani mpaka kitokee hicho kitu ndio atajua, kwa kuwa qadari ni siri ilofichwa haijulikani isipokuwa Mwenyezi Mungu amfahamishe kwa wahai, au kwa kuhisi.na hivyo hivyo namna ya ujenzi hiyo ni kwa kukadiria Mwenyezi Mungu hakika Mwenyezi Mungu amevikadiria vitu vyote kwa ujumla na kwa kimoja kimoja, na wala haiwezekani kwa Mja kuchagua kitu ambacho hakukitaka Mwenyezi Mungu na wala hakukikadiria, bali atakapo chagua Mja kitu na akakifanya jua kujua kwa yakini kuwa Mwenyezi Mungu amelitaka hilo na amelikadiria, kwani Mja huchagua kutokana na sababu za hisia zilizo wazi ambazo amezikadiria Mwenyezi Mungu ili litokee jambo lake, na wala hahisi Mja wakati wa kufanya jambo kuwa kuna yoyote amemlazimisha kulifanya, lakini yeye atakapo kuwa amelifanya hilo kutokana na sababu ambazo amezifanya Mwenyezi Mungu kuwa ni sababu, tutajua wazi kuwa Mwe-

nyezi Mungu amelikadiria hilo kiujumla na kwa kupambanua.

Na hivo hivo tunasema katika kufananisha na kufanya maovu Mwanadamu wakati mlipo sema: Hakika Mwenyezi Mungu amemkadiria kufanya maasi basi yeye atayafanya hakuna namna, lakini ameacha kwa akili yake nam na ya kuyafanya na kuyaendea hayo maasi.

***Tunasema:** katika hili yale tuliyo yasema katika kujenga msikiti, hakika Mwenyezi Mungu kumkadiria kwake kufanya maovu hakumzuii yeye kuchagua, kwa sababu alipo chagua hayo maovu alikuwa hajui kile alicho mkadiria Mwenyezi Mungu kwake, yeye aliyaendea hayo kwa uchaguzi wake na hakuhisi kuwa kuna yeyote kamlazimisha, lakini atakapo liendea na akalifanya tutajua kuwa Mwenyezi Mungu amelikadiria kulifanya hilo, na hivyo hivyo katika namna ya kuyapitisha maovu na kuyaendea hutokea kwa Mja kuchagua na hakupingani na makadirio ya Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu amekadiria vitu vyote kiujumla na kwa kimoja kimoja, na akakadiria sababu zake zenye kulifikisha katika kulitekeleza kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Je hujui kwamba Mwenyezi Mungu anayajua yaliomo mbinguni na ardhini? Hakika hayo yamo Kitabuni. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi**], [Suratul Hajj: 70].

Na akasema tena Mwenyezi Mungu: [**Na hivyo hivyo tumemfanyia kila Nabii maadui masheitwani na watu, na kijini,wakifundishana wao kwa wao maneno ya kupamba**

**pamba, kwa udanganyifu. Na angalipenda Mola wako Mlezi wasinge fanya hivyo. Basi waache na wanayo yazua**], [Suratul An’am: 112]na akasema tena Mwenyezi Mungu: [**Na hivyo hivyo hao washirika wao wamewapambia wengi katika wasirikina kuwauwa watoto wao ili kuwaangamiza na kuwavurugia dini yao. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angali penda wasinge fanya fanya hayo. Basi waache na hayo wanayo yazua**.][ Suratul Al-An'am /137], na amesema tena Mwenyezi Mungu: [**Lau Mwenyezi Mungu angalitaka wasingeli pigana walio kuwa baada yao baada ya kuwajia hoja zilizo wazi. Lakini wakakhitalifiana. Basi wapo kati yao walio amini, na wengine kati yao walio kufuru. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angalipenda wasnge pigana. Lakini Mwenyezi Mungu hutenda atakayo**], [Suratul Al-Baqara: 253].

Na baada ya ushahidi huo hakika kilicho baro kwa mtu asitafute katika nafsi yake wala ya mwingine mambo kama haya ambayo huleta tashiwishi, na hupelekea kwenye kuipinga sheria kwa kuikataa qadari, hakika hilo sio katika adabu za Maswahaba Mwenyezi Mungu awe radhi nao, na wao ndio wapupiaji wakubwa katika kuijua haki na kweka wazi mambo yalio fichikana, na katika (Swahihi Bukhar) kutoka kwa Ally bin Abi Twaalibi Mwenyezi Mungu awe radhi naye, kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema: ((**Hakuna yoyote katika nyiye isipokuwa ameandikiwa makazi yake katika pepo na makazi yake katika moto**)). Tukasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu je tusitege-

mee? (Na katika mapokezi mengine je tusitegemee katika kitabu chetu na tukaacha kufanya matendo?) akasema: ((**Hapana fanyeni yote ni yenye kufanyiwa wepesi**)], ameipokea Bukhar /6605, na Muslimu 2647].

Na katika mapokezi mwengine ((**Fanyeni kila mmoja ni wenye kufanyiwa wepesi katika jambo aloumbiwa, ama atakaye kuwa ni katika watu wema atafanyiwa wepesi katika kufanya matendo ya watu wema, na ama atakaye kuwa ni katika watu waovu atafanyiwa wepesi katika kuyafanya matendo ya watu waovu**)), [Ameipokea Bukhar /1362/, na Muslimu/2647].

Kisha akasoma: [**Ama mweye kutoa na akamcha Mwenyezi Mungu**. **Na akaliwafiki lililo jema**. **Tutamsahilishia yawe mepesi**. **Na ama mwenye kufanya ubakhili, na asiwe na haja ya wenzake**. **Na akakadhibisha lililo jema**. **Tutamsahilishia yawe mazito**. [Suratul Al-Layli: 5, 6, 7, 8, 9-10].

Amekataza Mutume rehma na amani ziwe juu yake utengemezi katika kitabu na kuacha kufanya matendo na akatolea Ushahidi kwa Aya ambayo inaonesha kuwa mwenye kuamini kisha akafanya matendo mema atasahilishiwa kuwa mepesi, na hii ndio dawa yenye matunda na yenye kufaulu, ambayo Mja anapata ndani yake afya na utukufu.

****

**Swali la 62: Je dua ina athari yoyote katika kubadilisha yale aloandikiwa Mwanadamu kabla ya kuumbwa kwake?**

**Jibu:** Hakuna shaka kuwa dua ni yenye kuathiri katika kubadili yale aloandikiwa Mwanadamu, lakini mabadiliko hayo yameandikwa pia yatatokea kwa sababu ya dua, wala usidhani kuwa utakapo muomba Mwenyezi Mungu kuwa utakuwa unaomba kwa kitu ambacho hakikuandikwa, bali dua imeandikwa na kile kinacho tokea pia kimeandikwa, kwa sababu hiyo utakuta msomaji anamsomea mgonjwa na anapona, na kile kisa cha kikosi cha jeshi ambacho Mtume rehma na amani ziwe juu yake alikituma, wakafikia hali ya kuwa ni wageni kwa watu flani, lakini wale watu hawakupokea ugeni ule, na ikakadiriwa kudongwa na nyoka kiongozi wa wale watu, wakaja kwa lile jeshi la Mtume rehma na amani ziwe juu yake wakitaka mwenye kumsomea kiongozi wao, Maswahaba wakawawekea sharti la malipo katika hilo, wale watu wakawapa Maswahaba kundi la mbuzi, kisha akaenda Swahaba mmoja kwa yule mgonjwa akamsomea Suratul Al-fatha, akasimama yule mgonjwa kana kwamba amefunguliwa kutoka kwenye kamba alokuwa amefungwa [Ameipokea Bukhar /2276/, na Muslimu/ 2201], hakika kisomo kiliathiri katika kumponesha Mgonjwa.

Kwa hiyo dua ina athari lakini sio katika kubadilisha yale aloyakadiria Mwenyezi Mungu, bali hilo limeandikwa kwa sababu yake, na kila kitu kwa Mwenyezi Mungu kinakuwa kwa makadirio

yake, na hivyo hivyo sababu zote zina taathira kwenye kile kitu zilicho kisababisha kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, kwa hiyo sababu zimeandikwa na visababishiwa pia vimeandikwa.

****

**Swali la 63: Je riziki na kuoa navyo vimeandikwa katika Lauhil Mahfudhi?**

**Jibu:** Kila kitu toka ameumba Mwenyezi Mungu kalamu mpaka siku ya Kiama hakika vyote hivyo vimeandikwa kwenye Lauhul Mahfudh, kwa sababu kitu cha kwanza alicho kiumba Mwenyezi Mungu ni kalamu kisha akaiambia: ((**Andika; ikasema: Ewe Mola wangu niandike kitu gani? Akasema: Andika vitu vyote vitakavyo tokea, ikandika kuanzia saa ile kila kitakacho tokea mpaka siku ya Kiama**)), [Ameipokea Abuu Daudi/4700/ na Tirmidhii /2155], Na imethibiti kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake  kuwa mtoto katika tumbo la mama yake itakapo pita kwake miezi minne, Mwenyezi Mungu humpelekea Malaika akampulizie roho, na andikiwe riziki yake na umri wake, na

matendo yake, atakuwa mwema au muovu. [Ameipokea Bukhar /3207, na Muslimu /2643].

Na riziki pia imeandikwa na imekadiriwa na imekadiriwa kwa sababu hazizidi wala hazipungui, na katika sababu ni Mwanadamu afanye kazi katika kutafuta riziki kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Yeye ndiye aliye idhalilisha ardhi kwa faida yenu, basi tembeeni katika pande zake,na kuleni katika riziki zake. Na kwake Yeye ndio kufufuliwa**], [Suratul Al-Mulk /15], na katika sababu pia ni kunganisha undugu,na kuwafanyia wema wazazi wawili, na pia kuunga undugu kwa watu wa karibu, hakika mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema: ((**Mwenye kutaka kukunjuliwa riziki yake, na zicheleweshwe athari zake zisifutike haraka basi aunge undugu**)), [Ameipokea Bukhari /2067].

Na katika sababu vilevile ni kumcha Mwenyezi Mungu kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Anaye mcha Mwenyezi Mungu humtengenezea nia ya kutokea**/2/ **Na humruzuku kwa sehemu asiyo itegemea**: 3], [Suratul Al-Talaq].

Wala usiseme: hakika riziki imeandikwa sito fanya sababu ambazo zitanipelekea kupata hiyo riziki, hakika huko ni katika kujishindisha, na halito kufaa katika dini yako na dunia yako amasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Mtu mjanja ni yule anaye ihesabu nafsi yake na akafanya yatakayo mfaa baada ya mauti na mwenye kushindwa ni yule ambaye nafsi yake hufuata matamanio yake na akatamani kwa Mwenyezi Mungu**

**matamanio yaa nafsi yake**)), [Ameipokea Tirmidhi /2459/, na Ibn Maaja /4260].

Kama ilivyo kuwa riziki imeandikwa na imekadiriwa na sababu zake hivyo hivyo kuoa kumeandikwa na kumekadiriwa, hakika imeandikwa kwa mume na mke kuwa ni mke au mume wa mwenzake, kwa Mwenyezi Mungu hakifichiki kitu katika mbingu na katika ardhi.

****

### Swali la 64: Ni ipi hukumu ya mwenye kukasirika na kuchukia pindi anapofikwa na matatizo?

**Jibu:** Watu katika hali ya kupatwa na matatizo wapo katika daraja nne:

**Daraja la kwanza**: Wenye kukasirika nao wamegawanyika:

**1**-Iwe anachukia kwa moyo kama vile kumchukia Mola wake na kupatwa na hasira kwa kile alicho kikadiria Mwenyezi Mungu kwake jambo hilo ni haramu, na linaweza kumpeleka mtu katika ukafiri amesema Mwenyezi Mungu: [**Na katika watu wapo wanao muabudu Mwenyezi Mungu kwa ukingoni. Ikimfika kheri hutulia kwayo, na ikimfika misukosuko hugeuza uso wake amepata khasara duniani na akhera**], [Suratul Al-Hajj: 11].

**2**-Iwe anachukia kwa ulimi kama kuomba maangamivu na mengine yanayo fanana na hayo, na hilo ni haramu.

**3-**Iwe ni kwa vitendo kama kujipiga katika mashavu, na kuchana nguo, na kujivuta nywele na kuzinyofoa na yanayo fanana na hayo. Yote hayo ni haramu inapingana na subra ambayo ni wajibu kwa mtu kuifanya.

**Daraja la pili**: Subra, nayo ni kama alivyo sema mshairi:

Subra ni kama mfano wa lilivyo jina lake ni chungu ladha yake lakini mwisho wake ni mtamu kuliko asali. Anaona kuwa hiki kitu ni kizito kwake lakini anavumilia, yeye anachukia kutokea kwake lakini Imani yake inamkinga na kukasirika, hakukuwa kutokea kwake na kuto tokea nia sawa kwake na hili ndio lililo la waibu, kwa sababu Mwenyezi Mungu ameamrisha kusubiri akasema: [**Na msubiri, hakika Mwenyezi Mungu yupo na wenye kusubiri**], [Suratul Al-Anfal: 46].

**Daraja la tatu**: Kuridhika, nayo ni Mwanadamu kuridhika kutokana na matatizo yalompata kiasi kwamba kuwepo kwa matatizo hayo na kuto kuwepo ni sawa, kule kupatikana kwake kusimtile uzito na wala asilichukulie hilo kwa uzito ulio pitiliza na hilo ni jambo lenye kupendeza si la waaJibu katika kauli iliyo na nguvu, na tofauti kati ya daraja hili na lilopita ipo wazi, kwasababu ku-

wepo kwa matatizo na kuto kuwepo kwake ni sawa katika daraja hili, ama lilopita matatizo kwake ni mazito yenye kumuelemeya lakini subra inatakikana kwa wakati huo.

**Daraja la nne**: Kushukuru, nalo ndio daraja la juu zaidi, nayo ni kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa lile lilompata katika matatizo, na ajue kuwa matatizo haya ni sababu ya kufutiwa madhambi na huenda ikawa ni sababu ya kuongezewa katika mema yake, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Hakuna msiba wowote unao mpata Muislamu isipokuwa Mwenyezi Mungu humfutia madhambi yake kwa msiba huo hata mwiba unao mchoma**)), [Ameipokea Bukhari/5640/, na Muslimu /2572].

****

**Swali la 65: Sheikh: Tunaomba kwa fadhila zako utuweke wazi maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((Hakuna Ghaduwa (maambukizi), wala Twiyara (kutiana mkosi) wala Al-Hammatu (ndege mwenye mkosi), wala Swafar (mwezi wa swafar kuwa una mkosi)), [Ameipokea Bukhar /5757/ na Muslimu /2220/ ]. Ni aina gani ya kukataza ilokuja katika Hadithi hii? Na tutaichukuaje Hadithi hii pamoja na ile inayo sema: ((Mkimbie mtu mwenye mbalanga kama unavyo mkimbia simba))? [Ameipokea Bukhar /5707].**

**Jibu:** (**Maambukizi**) ni kuhama maradhi kutoka kwa mgonjwa kwenda kwa mtu mzima, inaweza kuwa ni maradhi yenye kuonekana kwa macho au yasiyo onekana kama ya kitabia, kwa sababu hiyo ametuambia Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa rafiki mbaya ni kama mfua vyuma, ima akuchomee nguo zako au upate kutoka kwake harufu mbaya kwa hiyo maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake alipo sema: ((**Kuambukiza))** inakusanya maradhi yenye kuonekana na yasiyo onekana.

Na ((**Kutiana mkosi**)) ni mtu kukiona kitu flani au kusikia sauti flani kisha akasema: muda wa kuwa nimeona kitu hiki au nimekutana na kitu hiki au nimesikia sauti ya ndege huyu au mnyama huyu sitofanikiwa katika jambo langu hili.

Na Al-Hammu ((Ndege mwenye mkosi)) imetafsiriwa kwa

tafsiri mbili:-

**1**-Ni aina ya maradhi yanayo mpata mtu kisha huhamia kwa mwingine.

**2-**Ni aina ya ndege anaye julikana sana kwa warabu, wanadai waarabu kuwa akiuliwa mtu, ndege huyo huja kwa jamaa zake yule aliye uwawa na huanza kulia katika vichwa vyao mpaka watakapo lipiza kisasi kwa ndugu yao aliye uwawa, na kuna wengine huitakidi kuwa yule ndege ni roho ya yule aliye uwawa inakuja kwa sura ya ndege, nayo ni aina ya ndege inafanana na bundi au ndiye huyo huyo bundi, huwaudhi watu wa mtu aliye uliwa kwa kupiga kelele mpaka watakapo lipiza, naye ni ndege ambaye wanaitakidi kuwa anamkosi atakapo kuja katika nyumba fulani na akaanza kulia husema: hakika analia huyu kuashiria kuwa kuna mtu atakufa hapa, na hilo ni jambo ambalo sio sahihi na ni la batili kabisa.

Na **(Swafar)** imetafsiriwa kwa tafsiri zifuatazo:

**1**-Kuwa ni mwezi wa Swafar unaojulikana, walikuwa Waarabu wakiitakidi kuwa ni mwezi wenye mkosi.

**2-**Ni maradhi katika tumbo yanayo mpata ngamia, kisha yana hama kwenda kwa mwingine.

**3**-Ni mwezi wa Swafar (Mwezi wa pili katika miezi ya Kiislamu).

Na kauli yenye nguvu ni mwezi wa Swafar, ambao walikuwa wakitakidi kuwa ni mwezi wenye mkosi wakati wa ujahilia, na ukweli wa mambo ulivyo zama hazina athari yoyote, na katika makadirio ya Mwenyezi Mungu mwezi huo ni kama miezi mingine hukadiriwa ndani yake mambo ya kheri na mambo ya shari.

Kuna baadhi ya watu wakimaliza kazi zao siku ya tarehe ishirini na tano kwa mfano ya mwezi wa Swafar huhifadhi tarehe hiyo na husema: Imeisha katika tarehe ishirini na tano mwezi wa Swafar kwa kheri, Hii ni katika kutibu bidaa kwa bidaa, na ujinga kwa ujinga. Huo sio mwezi wa kheri wala wa shari.

Kwa sababu hiyo wamekataa baadhi ya wema walio tangulia Mwenyezi Mungu awarehemu kwa mwenye kusikia bundi analia kusema: **(( Iwe kheri akitaka Mwenyezi Mungu))** hukusemwi ,kheri wala shari bali yeye analia kama wanavyo lia ndege wengine.

Mambo haya manne aloyakataza Mtume  rehma na amani ziwe juu yake  yanaonesha ulazima wa kutegemea kwa Mwenyezi Mungu, na makusudio ya kweli, na Muislam asinyongeke yanapo mtokea mambo haya.

Na atakapo kuwa Muislam ameweka akili yake kwenye mam-

bo haya hatoacha kuwa katika mambo haya mawili:

**1**-Ima alipokee jambo hilo kwa kulifanya au kuliacha na itakuwa wakati huo ameyaweka mambo yake katika kitu ambacho hakina uhakika.

**2**-Asilipokee jambo hilo na wala asilijali, lakini itabaki katika nafsi yake aina flani ya simanzi au huzuni, na hili japo ni dogo kuliko la mwanzo lakini inampasa asiyakubali mambo hayo katika nafsi yake kabisaa, na awe ni mwenye kutengemea kwa Mwenyezi Mungu.

Kuna baadha ya watu hufungua msahafu kwa lengo la kuangalizia mambo yake kama afanye hicho kitu au asifanye, atakapo fungua Msahafu akakuta kumetajwa moto husema kufanya jambo hili kwa wakati huu sio vizuri, na atakapo fungua akakuta kumetajwa pepo husema kufanya jambo hili kwa wakati huu ni sahihi, mambo haya kwa hakika ni mfano wa mambo walokuwa wakifanya watu enzi za ujahili ambo walikuwa hawafanyi kitu mpaka waangalie ramli.

Na aina ya kukataa katika mambo haya mnne sio kukataa kuwa hayapo, kwa sababu yapo lakini ni kukataa kuwa yana athari kwa Mwanadamu, kwani mwenye kuathiri ni Mwenyezi Mungu peke yake, basi itakayo kuwa katika hizo ni sababu yenye kujulikana kisheria basi ni sababu sahihi, na itakayo kuwa katika hizo ni sa-

babu ya kudhani na ni sababu ya batili, inakuwa ni kukataa kuathiri kwake yenyewe na sababu yake pia, kuambukizana maradhi kupo, na inafahamisha kuwepo kwake maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Hawachanganywi mwenye wagonjwa na asio na wagonjwa**)) [Ameipokea Bukhari/5771/ na Muslimu /2221], yani maana yake: Hawachanganywi mwenye ngamia wenye maradhi na mwenye ngamia wasio na maradhi ili yasije yakahama maradhi.

Na maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Mkimbie mtu mwenye mbalanga kama unavyo mkimbia simba**)) [Umetangulia upokezi wake]. (Mbalanga): Ni maradhi mabaya yanayo enea kwa haraka sana na humharibu mwenye kupatwa na maradhi hayo,mpaka imesemwa: Hakika maradhi haya ni kama ugonjwa wa Tauni (kipindupindu)kuja amri kwa kumkimbia mwenye ugonjwa huu ili yasipatikane maambukizi, na ndani yake kuna uthibitisho kuwa ni wenye kuambukizwa na ni wenye kuathiri, lakini kuathiri kwake sio kuwa kila mwenye kuwa naye lazima apate bali ni jambo ambalo mpaka Mwenyezi Mungu akadirie, kuamrisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa mbali na mwenye mbalanga ni kwa sababu mwenye nao asimuambukize asokuwa nao, ni katika mlango wa kuepukana na sababu, na si katika mlango kuwa sababu inaathiri yenyewe kama yenyewe amesema Mwenyezi Mungu: [**Wala msitie mikono yenu katika maangamizo**], [Suratul Al-Baqar: 195]

Na wala haisemwi kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake anapinga kuambukizana ugonjwa; kwa sababu ni jambo ambalo hali halisi imelishuhudia na pia Hadithi zimeelezea.

***Iwapo kutasemwa**: Hakika Mtume rehma na amani ziwe juu yake wakati alipo sema: ((**Hakuna maambukizi**)) akasema mtu: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu unaonaje ngamia anakuwa na afya nzuri na mzima kabisa, anapo ingia ngamia mwenye maradhi na wale wengine pia wanapata maradhi? Akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Ni nani amemuambukiza Yule wa mwanzo**?)) [Umetangulia upokezi wake].

**Jibu**: Mtume rehma na amani ziwe juu yake ameashiria kwa maneno yake alipo sema**: ((Ni nani amemuambukuza Yule wa kwanza))** ya kuwa maradhi yamehama kutoka kwa yule mgonjwa kwenda kwa yule mzima kwa makadirio ya Mwenyezi Mungu, na yamekuja kwa yule wa kwanza bila kuambukizwa, bali kutoka kwa Mwenyezi Mungu Na kitu kinaweza kuwa na sababu maalumu au kiwe hakina sababu maalumu, maradhi ya ngamia wa mwanzo haijulikani sababu yake isipokuwa ni makadirio tu ya Mwenyezi Mungu, na yule wa pili ana sababu maalumu na lau kama angalitaka Mwenyezi Mungu asinge ambukizwa, na kwa ajili hiyo wakati mwingine ngamia anaweza kupatwa na maradhi hayo na yakaisha bila kufa, hivyo hivyo ugonjwa wa Tauni, Kipindupindu na maradhi mengine. Yenye kuambukiza yanaweza kuingia ndani ya nyumba yakawapata baadhi ya watu wakafa na wengine wakasalimika wale wasipatwe na hayo maradhi kabisaa, Mwanadamu anamtegemea Mwenyezi Mungu katika kila kitu, hakika imepokewa kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake: alikuja kwake mtu mwenye mbaranga akaushika mkono wake na akasema: ((**Kula**)) [Ameipokea Abu Daud /3925), na Tirmidhi /1817] Maana yake alimuambia kula katika chakula alicho kuwa akila Mtume rehma na amani ziwe juu yake, hilo linaonesha ni jinsi gani alivyo kuwa

na kutegemea kukubwa kwa Mwenyezi Mungu, kutegemea huku ni kwenye kushinda sababu ya maambukizi.

Na huu mkusanyiko ambao tumeutaja ni mkusanyiko mzuri katika kuzikusanya Hadithi zilizo elezea mas-ala haya, kwa sababu kuna

wengine wamedai kuwa baadhi ya Hadithi hizo ni mansokh madai hayo sio sahihi, kwa sababu katika sharti za naskhu (kufuta) ni kushindwa kuzikusanya pamoja, itakapo wezekana kuzikusanya ni lazima kuzikusanya kwa sababu kuna kuzifanyia kazi Hadithi zote mbili, na katika naskh ni kubatilisha moja katika hizo, na kuzifanyia kazi zote ni bora kuliko kuiacha moja, kwa sababu tutakuwa tumezizingatia zote mbili na tumezifanya kuwa ni Ushahidi.

****

**Swali la 66: Je kijicho kinaweza kumpata mtu? Na kikimpata kinatibiwa kwa namna gani? Na je kujikinga nacho kunapingana na kumtegemea Mwenyezi Mungu?**

**Jibu:** Rai yangu katika kijicho hakika hicho ni cha kweli na kimethibiti kisheria na kwa kuonekana amesema Mwenyezi Mungu: [**Na wale walio kufuru hukaribia kukutelezesha kwa macho yao**] [Suratul Al-Qalam 51], amesema Ibn Abas Mwenyezi Mungu awe radhi naye na wengine katika kutafsiri Aya hii:wanakudhuru kwa macho yao (Ameitoa Ibnu Jariri katika Tafsiri yake, [23/202], na anasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Kijicho ni**

**cha kweli na lau kama kuna kitu chenye kutangulia Qadar pindi mtakapo patwa nalo naweni** )), [Ameipokea Muslimu/ 2188].

Na katika hilo ni kama alivyo pokea Nasaai na Ibn Maaja Mwenyezi Mungu awarehemu, kuwa Ghamir Ibnu Rabii alipita kwa Sahli Ibnu hunaifa radha za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao naye akiwa anaoga akasema: (sikuwahi kuona kama leo..) hakukaa muda mrefu akapatwa na mafua au kuhara akaletwa kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake akaambiwa nenda kwa Sahal akasema: ((**Nani mnaye mtuhumu**)) wakasema Ghamir Ibn Rabiy, akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Anaweza kumuuwa mmoja wenu ndugu yake? pindi atakapoona mmoja wenu kwa ndugu yake kitu kinacho mpendeza basi na amuombee ndugu yake Baraka**)), [Ameipokea Ibnu Maaja /3509], kisha akaitisha maji akamuamrisha Ghamir atawadhe aoshe uso wake na mikono yake mpaka katika vifundo viwili, na magoti yake na ndani ya kikoi hichi na akamuamrisha ammwagie.

Na hali halisi inashuhudia hivyo wala haiwezekani kuipinga.

Na katika hali ya kutokea hilo hutumika matibabu ya Kisheria nayo ni:-

1-Kusomewa: Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Hakuna Ruqya isipokuwa katika kijicho au homa**)),

[ameipokea Bukhari/5705/, na Muslimu /220], na hakika alikuwa Jibrili Amani iwe juu yake akimfanyia Ruqya Mtume rehma na amani ziwe juu yake akisema: (**Kwa jina la Mwenyezi Mungu nakufanyia Ruqya, kutokana na kila kitu chenye kukuudhi, na shari ya kila nafsi, au kijicho cha kila hasidi Mwenyezi Mungu akuponyeshe, kwa jina la Mwenyezi Mungu nakufanyia Ruqya**)) [Umetangulia upokezi wake].

2-Kuoga au kunawa: Kama Mtume rehma na amani ziwe juu yake alivyo muamrisha Ghamiri bin Rabii katika Hadithi ilotangulia kisha ammwagie maji yule alopatwa.

Ama kuchukua mabaki yake yaliyo tokana na mkojo au choo kikubwa jambo hilo halina Ushahidi, na vile vile kuchukua athari yake ya unyayo au kitu chochote pia haifai, hakuna kitu ambacho kimepokelewa ni katika yale tulosema huko nyuma kuosha viungo vyake na ndani ya kikoi chake na inaweza kuwa mfano wa hivyo kama kofia yake au nguo zake, Mwenyezi Mungu ndiye mjuzi zaidi.

Na kujikinga na kijicho hakuna ubaya na wala halipingani na kumtegemea Mwenyezi Mungu, bali huko ndio kutegemea kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu Tawakul ni kumtengemea Mwenyezi Mungu pamoja na kufanya sababu ambazo Mwenyezi Mungu amezihalalisha na kuziamrisha. Hakika alikuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake akiwakinga Hasani na Husein na akisema: ((**Nakukingeni kwa maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyo**

**makamilifu kutokana na kila sheitwani na mkubwa wao, na kutokana kila kijicho**)) Na anasema: ((**Hivi ndivyo Ibrahimu alivyokuwa akiwakinga Is-haq na Ismail amani ya Mwenyezi Mungu iwe pamoja nao**)), [Ameipokea Bukhar /3371].

****

**Swali la 67: Je anahesabika kuwa ana udhuru mtu ambaye hajui mambo ya Aqida?**

**Jibu:** Ikhitilafu katika mas'ala kuwa na udhuru kwa mtu asiye jua katika Aqida ni kama walivyo khitilafiana katika mas'ala ya Fiqhi mas'ala ya kujitahidi, na huenda ikawa ikhitilafu ni ya kimaneno baadhi ya wakati kwa ajili ya kuitekeleza hukumu kwa mtu maalumu; maana yake ni kwamba: Wote wamekubaliana kuwa maneno haya ni ukafiri, au vitendo hivi ni ukafiri, au kuacha kitu hiki ni ukafiri, lakini je hukumu inakuwa mpaka kwa mtu huyu maalumu, kwa sababu imesimama kwake vitu ambavyo vinaweza kusababisha hukumu isisimamishwe kwake, au isisimamishwe kwa kuwa kuna vitu vimepungua au kumepatikana kizuizi kinacho zuiya hukumu isitekelezwe.

Kuwa mtu hajui kitu hiki ni ukafiri kumegawanyika katika sehemu mbili:

**1**-Awe mtu huyu ana dini isiyo kuwa ya Kiislamu, au hana dini yoyote na haikuwa ikipita katika akili yake kuwa dini ipo kinyume na analokuwa nayo, mtu huyu hupita kweke hukumu za kidunia zilizo wazi katika duni (huhukumiwa kuwa ni kafiri) na ama akhera jambo lake litakuwa kwa Mwenyezi Mungu akitaka atamuadhibu akitaka atamsamehe, na kauli yenye nguvu ni kuwa atapewa mtihani akhera kwa atakavyo taka Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu anajua kwa yale ambayo wengeyafanya, lakini sisi tunajua kuwa hatoingia motoni isipokuwa kwa dhambi kwa maneno ya Mwenyezi Mungu: [**Wala hamdhulumu Mola wako yoyote**], [Suratul Kahaf /49].

Hakika tumesema: (hupita kweke hukumu za kidunia zilizo wazi katika duni) nayo ni hukumu kuwa ni kafiri,Kwa sababu hayupo katika dini ya Kislamu kwa hiyo haiwezekani kupewa hukumu ya Kiislamu, na tumesema kauli yenye nguvu atapewa mtihani akhera, kwa sababu zimekuja Ushahidi nyingi amezitaja Ibnu Qayyim Mwenyezi Mungu amrehemu katika kitabu chake (Tariq Al-Hijiratain) katika maneno yake juu ya madhahabu ya nane kwa watoto wa washirikina chini ya maneno katika twabaka ya kumi na nne ((Tariq Al-Hijiratain uk: 842)).

**2-**Awe ni katika watu walio katika Uislamu lakini ameishi katika hali ya kukufuru na haikuwa ikipita katika akili yake kuwa

anakwenda kinyume na Uislamu, na wala hakumzindua yoyote kuhusu hilo huyu hupita kwake hukumu za Kiislamu zilizo wazi, ama akhera jambo lake litakuwa kwa Mwenyezi Mungu akitaka atamuadhibu akitaka atamsamehe, na hilo limeelezwa katika Kitabu na Sunna na maneno ya wanavyuona Mwenyezi Mungu awarehemu.

Katika Ushahidi za Qur`an: Maneno yake Mwenyezi Mungu aliposema: [**Wala sisi hatuadhibu mpaka tumpeleke Mtume**], [Suratul Al-Israa: 15], na maneno yake Mwenyezi Mungu: [**Na Mola wako Mlezi haangamizi miji mpaka ampeleke Mtume katika miji yake mikuu awasomee Ishara zetu.Wala hatuiangamizi miji mpaka watu wake wawe madhalimu**], [Suratul Qaswaswi: 59], na maneno yake: [**Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume**], [Suratul Nisaa: 165/], na maneno yake: [**Na hatukumtuma Mtume ila kwa ulimi wa watu wake ilia pate kuwabainishia. Basi Mwenyezi Mungu humuacha apotee amtakaye, na akamuongoza amtakaye],** [Suratu Ibrahim: 4]. Na maneno yake: [**Na haiwi kwa Mwenyezi Mungu kuwahesabu watu kuwa wamepotea baada ya kwisha waongoza mpaka awabainishie ya kujiepusha nayo**], [Suratul Tauba: 115], na maneno yake: [**Na hiki ni kitabu tulicho kiteremsha, kilicho barikiwa. Basi kifuateni,na mcheni Mwenyezi Mungu, ili mrehemewe**. **Msije mkasema: Hakika mataifa mawili kabla yetu yameteremshiwa Kitabu; na sisi tulikuwa hatuna khabari ya walio kuwa wakiyasoma**. **Au mkasema: Lau kuwa tumeteremshiwa sisi Kitabu tungelikuwa waongofu zaidi kuliko wao. Basi imekufikieni bayana kutoka kwa Mola wenu Mlezi na uongofu**

**na rehema]** [Suratul An'aam: 155-156], na nyingine zisizokuwa hizo katika Aya zenye kuonesha kuwa haisimami hoja isipokuwa baada ya kujua na kubainishiwa.

Ama katika Sunnah: Katika Sahihi Muslimu [1/134/] kutoka kwa Abu Huraira radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: ((**Naapa kwa Yule ambaye nafsi ya Mohammadi ipo mikononi mwake hato nisikia yoyote katika Umma huu awe Myahudi au Mnaswara kisha akafa na hukuamini kile nilicho tumilizwa kwacho isipokuwa atakuwa ni katika watu wa motoni**)), [Ameipokea Muslimu/153].

Ama maneno ya Wanavyuoni Mwenyezi Mungu awarehemu: Amesema Mwenyezi Mungu amrehemu katika [Al-Mughuniy 8/131]: ((Ikiwa ni katika watu wasio jua uwaJibu katika hilo kwa mfano wale wageni katika Uislamu, na alokulia katika mji usiokuwa wa Kiislamu, au ameishi vijijini mbali na mjini na ameishi mbali na Wanavyuoni hahukumiwi kuwa ni kafiri)).

Na amesema Sheikh Al-Islam Ibn Taymiya Mwenyezi Mungu amrehemu katika Al-Fatawa [3/229/ Al Majumuu libn Qasim]: ((Hakika mimi milele ni katika watu wakatazaji wakubwa kunasibiswa mtu maalumu katika ukafiri au uovu au maaswiya, isipokuwa itakapo julikana kuwa imesimama kwake Ushahidi za wazi ambazo mwenye kuzikhalifu huwa kafiri wakati flani au muovu wakati mwingine, au muasi wakati mwingine, na mimi narudia tena kusema hakika Mwenyezi Mungu ameusamehe Ummah huu

makosa yake, na hilo linaingia katika makosa ya mas'ala khabaria ya maneno, na mas'ala ya matendo, na hawakuacha kuwa wema walotangulia ni wenye kutofautiana katika mambo mengi kwenye mas-ala haya, na hakuna hata mmoja alomuambia mwenzake kuwa ni kafiri, au muovu au muasi)) mpaka alipo sema: ((na nilikuwa nikibainisha kuwa yale yalio nukuliwa kutoka kwa wema walotangulia na viongozi, kwa kuzungumza kwao kiujumla kwa kufurisha mwenye kusema hivi na hivi, hivyo pia ni haki lakini ni wajibu kutofautisha katika ya kuzungumza bila kumtaja yoyote na kuzungumza kwa kumtaja mtu maalumu)), mpaka akasema: ((Na kukufuru ni katika makemeo makubwa sana hasi ikiwa ni katika kukadhibisha yale alosema Mtume rehma na amani ziwe juu yake lakina mtu alosema anaweza kuwa mgeni katika Uislamu, au amekulia vijijini mbali na mjini hajui mambo hayo ya Uislamu, mfano wa huyu kakufuru kwa kupinga kile anacho kipinga mpaka isimamishwe hoja kwake kwa kubainishiwa haki, kwa sababu inaweza kuwa mtu huyu hakuwahi kusikia hizo Ushahidi au amezisikia lakini hazikuthibiti kwake, au mpingaji huyo ana mpingaji mwingine amempatia tafsiri nyingine ya kimakosa)), yameisha maneno yake.

Amesema Sheikh Muhammad bin Abdul Wahaab [1/56/ katika Al-Dar Sania]: ((Ama kuwakufurisha watu hakika mimi humkufurisha yule anaye jua dini ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake kisha baada ya kuijua akaituna, na akawakataza watu na dini hii, na akamfanyia uadui mwenye kushikamana nayo huyu ndio ambaye mimi humkufurisha)).

Na katika (Uk. 66): ((Na ama uongo na uzushi katika maneno yao kuwa mimi nawakufurisha watu kwa ujumla na tunalazimisha kuwahama yote hayo ni katika uongo na uzushi,ambao wa-

nawaaminisha watu uongo huo katika dini ya Mwenyezi Mungu na Mtume rehma na amani ziwe juu yake, ikiwa hatumkufurishi yule anaye abudu sanamu lililopo kwa Abdul qadir,na sanamu lililopo kwa Ahamed Al-Badawi na mfano wa wawili hao kwa sababu ya ujinga wao, na kukosekana wa kuwazindua, ni vipi tutamkufurisha yule ambaye hakumshirikisha Mwenyezi Mungu pindi atakapo kuwa hakutuhama wala hakutukufurisha wala hakutupiga vita)), mwisho wa maneno yake.

Ikiwa hivi ndivyo unavyo elekeza ushahidi wa Kitabu na Sunna na maneno ya wanavyuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, na hiyo ndio hekima ya Mwenyezi Mungu na upole wake, hato muadhibu yoyote mpaka amuonye kwanza, na akili sio kwamba hazitaki kuelewa mambo ambayo ni wajibu kumfanyia Mwenyezi Mungu katika haki zake, lau kama ingekuwa hazitaki basi kusingekuwa na haja ya kutumwa mitume.

Ilivyo asili kwa yule mwenye kujinasibisha na Uislamu abaki katika jina lake kuwa ni Muislamu mpaka upatikane uhakika wa kuondoka katika Uislamu kwa muJibu wa Ushahidi za kisheria, na wala haifai kufanya wepesi katika kukufurisha kwa sababu kuna makatazo mawili makubwa nayo ni:

**La kwanza**; Kuzua uongo kwa Mwenyezi Mungu katika hukumu na mwenye kuhukumiwa katika sifa ambazo amemsifia nazo.

Ama sifa ya kwanza ipo wazi, amemuhukumu mtu kuwa ni kafiri mtu ambaye Mwenyezi Mungu hakumkufurisha, basi huyo ni kama aloharamisha yale alohalalisha Mwenyezi Mungu, kwa sababu kuhukumu kuwa ni kafiri au sio kafiri kwa Mwenyezi Mungu ni kitu kimoja ni kama kuhukumu kitu kuwa haramu au sio haramu.

**Na la pili**; Kwa sababu amemsifia Muislamu kwa sifa ambazo zinapingana Amesema: kuwa yeye ni kafiri, pamoja ya kuwa yupo mbali na hilo, na huenda sifa hiyo ya ukafiri ikamrudia yeye mwenyewe, kwa sababu imethibiti katika (sahihi mbili) kutoka kwa Abdulallah  Ibnu Omar Mwenyezi Mungu awe radhi nao wote wawili, kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema: ((**Pindi atakapo mkufurisha mtu ndugu yake hakika itathibiti kwa mmoja katika wao**)), [Ameipokea Bukhari /6104/ na Muslim /60] na katika mapokezi mengine: **((Ikiwa ni kama alivyo sema basi itamthibitikia Yule aloambiwa, na isipokuwa kweli itamrudia mwenyewe**)), [Ameipokea Muslimu /60].

Na katika hilo kutoka katika Hadithi ya Abiy Dhari kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake  amesema: ((**Mwenye kumuita mtu kafiri, au akasema: wewe ni adui wa Mwenyezi Mungu, na sio kama alivyo sema basi jambo hilo litamrudia mwenyewe)),** [Ameipokea Muslimu /61].

Na maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake  katika Hadithi ya Ibnu Omar: ((**Ikiwa itakuwa ni kama alivyo sema**)), anakusudia katika hukumu ya Mwenyezi Mungu kuwa ni kafiri, na pia katika maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake

katika Hadithi ya Abiy Dhari: ((**Na hayupo hivyo**)), anakusudia katika hukumu Mwenyezi Mungu kuwa sio kafiri.

Na hili ndilo katazo la pili nakusudia: Kurudi sifa ya ukafiri kwake ikiwa ndugu yake yupo mbali na sifa hiyo, nalo ni katazo kubwa sana inahofiwa kuangukia humo, kwa sababu wengi wenye kufanya haraka kuwasifia Waislamu na sifa ya ukafiri akiwa anapendezeshwa na matendo yake akiwa anayadharau ya wenzake anakuwa ni mwenye kukusanya katika ya kupendezeshwa na matendo yake ambayo yanaweza kupelekea katika

kupomoka matendo hayo, na kibri ambacho hupelekea katika adhabu ya Mwenyezi Mungu katika moto kama ilivyo kuja katika Hadithi ambayo ameipokea Ahmad na Abu Daud Mwenyezi Mungu awarehemu kutoka kwa Abu Huraira radhi za Mwenyezi Mungu ziwe pamoja naye kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema: ((**Amesema Mwenyezi Mungu:Kibri ni nguo yangu, na utukufu ni nguo yangu ya chini (kikio) mwenye kunivua moja katika hizo nitamtupa katika moto**)), [Ameipokea Ahmad, Abu Daud na Ibnu Maaja].

Kitu cha lazima kabla ya kumhukumu mtu kwa ukafiri angalie mambo mawili:

1-Ushahidi katika Kitabu na Sunna kuwa je huyu mtu amekufuru ili asije akamzulia Mwenyezi Mungu uongo.

2-Kuafikiana huku hiyo kwa mtu maalumu kwa kiasi kwamba ziwe zimekamilika sharti za kukufurishwa na view vimeondoka vizuizi vya kukufurishwa.

Na katika sharti muhimu awe ni mwenye kujua jambo ambalo amelifanya ambalo linamlazimu kukufurishwa kwake kwa maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Na anaye mpinga Mtume baada ya kumdhihirikia uongofu,na akafuata njia isiyo kuwa ya Waumini, tutamuelekeza aliko elekea, na tutamuingiza katika Jahanamu.Na hayo ni marejeo mabaya**], [Suratul Al-Nisa: 115], imewekwa sharti ya kuadhibiwa kwa moto ni mtu kuwa na mashaka na Mtume rehma na amani ziwe juu yake baada ya kumbainikia uongofu.

***Lakini je:** Ni sharti awe anajua hukumu ya lile jambo alokwenda nalo kinyume kuwa linamkufurisha au nyingineyo, au inatosha awe ni mwenye kujua jambo hilo aloenda nalo hata kama atakuwa hajui hukumu yake katika jambo hilo?

***Jibu**: Inavyo onekana: la pili; kwa sababu kule kujua tu jambo alokwenda nalo kinyume inatosha kuhuhumiwa kwa mujibu wa jambo hilo, kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake amewajibisha kafara kwa mwenye kumuingilia mke wake mchana wa Ramadhani kwa kule kujua kwake kuwa amefanya kosa pamoja na kutokujua kwake kuwa ni ukafiri; kwa sababu zinaa kwa mtu alo oa mwenye kujua uharamu wa zinaa hupingwa mawe hata kama atakuwa hajui hukumu ya jambo hilo alolifanya.

Na katika vizuizi vya mtu kuwa kafiri ni kulazimishwa kukufuru amesema Mwenyezi Mungu: [**Anaye mkufuru Mwenyezi Mungu baada ya kuamini kwake, isipokuwa aliye lazimishwa na hali ya kuwa moyo wake umetulia juu ya Imani, lakini anaye kifungulia kifua chake kukataa-basi hao ghadhabu ya Mwenyezi Mungu ipo juu yao, na wao watapata adhabu kubwa**], [Suratul Nahli: 106].

Na katika vizuizi vya kukufuru ni fikra na makusudio yake yawe yamefungwa kwa kiasi kwamba hajui anasema nini kutokana na furaha au huzuni au hasira au hofu na mfano wa hayo, amesema Mwenyezi Mungu: [**Wala hapana juu yenu ubaya kwa mlio kosea, lakini upo ubaya katika yele ziliyo fanya nyoyo zenukwa kukusudia, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu**], [Suratul Ahzabu: 5], na katika [Sahihi Muslim /4/2104], kutoka kwa Anas bin Maalik Mwenyezi Mungu awe radhi naye kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu rehma na amani ziwe juu yake amesema: **((Mwenyezi Mungu huwa anakuwa na furaha zaidi kwa toba ya Mja wake wakati anapo tubia kwake kuliko mmoja wenu alikuwa katika kipando chake katika ardhi ambayo ni tupu, mara akamponyoka kutoka mikononi mwake na juu yake kulikuwa na chakula chake na kinywaji chake, akakata tama kumpata, akaenda katika kivuli cha mti akajilaza katika kivuli hali ya kuwa amekata tama kumpata mnyama wake, wakati yupo katika hali hiyo ghafla anamuona amesimama mbele yake, akaishika ile kamba yake, kisha akasema kutokana na kuzidiwa na furaha: Ewe Mola wangu Wewe ni Mja wangu, na mimi ni Mola wako, amekosea kutokana na furaha ilozidi**)), [Ameipokea Bukhari /6309/ na Muslimu /2747].

Na katika vizuizi pia iwe kwake kuna Shubha katika kutafsiri jambo lenye kukufurisha kwa kiasi kwamba anadhani kuwa yupo katika haki; kwa sababu atakapo kuwa hakufanya makusudi katika kosa na katika jambo alokosea anakuwa ameinga katika maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Wala hapana juu yenu ubaya kwa mlio kosea, lakini upo ubaya katika yele ziliyo fanya nyoyo zenu kwa kukusudia**], [Suratul Ahzabu: 5]. Kwa sababu hapo ndio mwisho wa juhudi zake anakuwa ni mwenye kuingia katika maneno yake Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Mwenyezi Mungu haikalifisha nafsi yoyote ila kwa kadri iwezavyo**], [Suratul Baqar: 286].

Amesema Mwenyezi Mungu amrehemu katika [Al-Mughuniy /8/131]: ((Ikiwa itakuwa halali kuwauwa na kuchukua mali zao watu ambao ni haramu kuwauwa pasina Shubha na Taawili basi hivyo hivyo hata ikiwa ni kwa Taawili kama vile kundi la Khawariji, hakika tumetaja kuwa wengi katika wana vyuoni hawakuwahukumu kuwa ni makafiri pamoja na kuwa wao wamehalalisha damu za Waislamu na mali zao, na kufanya kwao hivyo ni katika kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu)), mpaka aliposema: ((Hakika imejulikana kwa Madh-habu ya Khawariji kuwakufurisha wengi katika Maswahaba na walokuja baada yao na kuhalalisha damu zao na mali zao, na kuitakidi kwao kuwa kuwauwa hao ni kujikurubisha kwa Mola wao, pamoja na hayo yote hawakuwahukumu wana vyuoni kuwakufurisha kwa sababu ya

Taawili zao, na vile vile hutoka kila mwezi wa Muharamu kwa ajili ya kuadhimisha na kuhalalisha Taawili yao hii)). Na katika fatawa ya Sheikh Islamu Ibnu Taymiya Mwenyezi Mungu amrehemu [13/30 Majumuu Libnu Qasimu]: ((Na bidaa za Makhawariji ni miongoni mwa ufahamuji wao mbaya wa Qur`an, hawakukusudia kuipinga Qur`an, lakini wameifahamu kwa kile kitu ambacho haikuelekeza,wakadhani kuwa inawajibisha kuwakufurisha wenye madhambi makubwa)). Na katika (Uk. 210): ((Hakika Khawariji wameikhalifu Sunna ambayo Qur`an imeamrisha kuifuata, na wakawakufurisha Waumini ambao Qur`an imeamrisha kuwafanya marafiki.Wakawa wanafuata mambo yenye kufanana katika Qur`an wanayafanyia Taawili kwa isiyokuwa Taawili yake pasina wao kujua maana yake wale wale walio zama katika elimu, wala hawakufuata Sunnahh, na wala hawakurudi kwa Jamaa katika Waislamu ambao wameifahamu Qur`an)).

Na akasema vile vile Mwenyezi Mungu amrehemu [28/518/, katika Majumuu]: ((Hakika Maimamu wote wameafikiana juu ya kuwasema vibaya Khawariji na wakasema kuwa wamepotea,na hakika si vinginevyo walipo tofautiana ni kwenye kuwakufurisha katika kauli mbili zenye kujulikana)). Lakini yeye Mwenyezi Mungu amrehemu ametaja katika [/7/217/]: ((Hakika hukukuwa katika Maswahaba mwenye kuwakufurisha sio Ally Ibnu Abiy Twalibi wala wengine asio kuwa yeye, bali waliwahukumu kama wanavyo wahukumu Waislamu wengine walopotea kama zilivyo taja Athari kuwataja wao katika hilo na sio sehemu mmoja)).

Na katika [3/282], amesema: ((Na Khawariji waliotoka ambao aliamrisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake: kuwauwa na akawapiga Amirul-Muuminina Ally bin Abi Twalibi mmoja katika

Makhalifa waongofu, na wakaafikiana kuwapiga viongozo wote wa dini miongoni mwa Maswahaba, Matabiina, na wale walokuja baada yao, hakuwakufurisha Ally bin Abi Twalibi, na Saad bin Abi Waqaswa, wala wengine wasiokuwa wawili hao miongoni mwa Maswahaba, bali waliwafanya ni miongoni mwa Waislamu pamoja na kuwapiga kwao, na Ally hakuwapiga mpaka walipo mwaga damu pale Haramu, na wakazivamia mali za Waislamu, akawapiga kwa jili ya kuondoa dhulma yao na uasi wao, sio kwa sababu wao ni makafiri; kwa ajili hiyo hakuwateka wanawake wao na wala hakuchukua mali zao kama ghanima, pindi itakapo kuwa hawa jamaa umethibiti upotevu wao kwa ushahidi na kwa kukubaliana wana vyuoni hawakukufuru pamoja na kwamba Mwenyezi Mungu na Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake wameamrisha kupigwa vita, je itakuwa kwa makundi yenye kutofautiana ambao haki imewachanganya katika Mas'ala mazito na hakuna mjuzi wa mas-ala hayo zaidi ya wao? Si halali kwa yoyote katika makundi haya kumkufurisha mwenzake, na wala haiwi halali damu zao na mali zao, hata kama itakuwa ndani yake wana bidaa iliyo hakikiwa kuwa hii ni bidaa, je itakuwaje ikiwa anaye mkufurisha ni mtu wa bidaa pia,inaweza kuwa bidaa ya hawa ni kubwa, lakini mara nyingi watu hawa huwa ni wajinga kwa uhakika wa kitu wanacho tofautiana ndani yake)).

Mpaka alipo sema: ((Pindi itakapo kuwa Muislamu mwenye kufanya Taawili katika vita, au katika kukufurisha hakukufuru kwa hilo)). Mpaka aliposema katika (Uk. 288): ((Na hakika wametofautina wana vyuoni katika maneno ya Mwenyezi Mungu na Mtume rehma na amani ziwe juu yake je inathibiti hukumu hiyo kwa waja kabla ya kubalekhe katika sehemu tatu:

Katika Madh-habu ya Ahmad na wengine, nayo ndio sahihi iliyo fahamisha Qur`an katika maneno ya Mwenyezi Mungu aliposema: [**Wala Sisi hatutadhibu mpaka tumpeleke Mtume**], [Suratul Israa: 15], na maneno ya Mwenyezi Mungu: [**Mitume hao ni wabasiri na waonyaji, ili watu  wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuwaletea Mitume**], [Suratul Al-Nisaa: 165], na katika (Sahihi mbili) kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Hakuna yoyote ambaye udhuru unapendeza zaidi kwake kuliko Mwenyezi Mungu, na kwa sababu hio aliwatuma Mitume ili wawabashirie watu pepo na wawaonye na moto**)), [Ameipokea Bukhari /7416/, na Muslimu /1399].

**Na jambo tulolipata ni:** Mtu kuto kujua kitu ni udhuru kwa kile atakacho kisema,au kukufanya katika vitu ambavyo kuvisema au kuvifanya ni ukafiri, kama ambavyo huwa ni mwenye kusamehewa kwa kile atakacho kisema au kukufanya ambavyo huwa kusemwa kwake au kufanywa ni uovu, na hilo ni kwa Ushahidi kutoka katika Kitabu na Sunnah, na maneno ya wanavyuoni Mwenyezi Mungu awarehemu.

****

**Swali la 68: Ni ipi hukumu ya mwenye kuhukumu kwa kitu ambacho Mwenyezi Mungu hakukiteremsha?**

**Jibu:** Ninasema kuwa Mwenyezi Mungu ndie mwenye kutuafikisha na ninasema na ninamuomba uongofu na niwe ni mwenye kupatia: Hakika kuhukumu kwa kile alicho kiteremsha Mwenyezi Mungu ni katika Tauhid Rububiya; kwa sababu ni kupitisha hukumu ya Mwenyezi Mungu ambayo ndio usahihi wa ulezi wake, na ukamilifu wa Ufalme wake, na upangiliaje wake, kwa ajili hii amewaita Mwenyezi Mungu wale wenye kuhukumu kwa vile ambavyo hakuviteremsha ni Miungu wao kwa kule kuwafuata kwao amesema Mwenyezi Mungu: [**Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni miungu wao badala ya Mwenyezi Mungu, na pia Masihi bin Maryamu. Na wala hawakuamrishwa isipokuwa wamuabudu Mola mmoja, hapana Mola ila Yeye.Ametakasika na hayo wanayo mshirikisha nayo**], [Suratul Al-Tauba: 31], Mwenyezi Mungu amewaita wale wenye kuhukumu ni Miungu ,kwa sababu wamewafanya ni wenye kuweka sharia pamoja na Mwenyezi Mungu na akawaita wenye kufuata hizo hukumu waabuduji, kwa sababu wao wanawanyenyekea na wamewatii katika kuikhalifu hukumu ya Mwenyezi Mungu.

Hakika alisema Adiy Ibnu hatim Mwenyezi Mungu awe radhi naye kumuambia Mtume rehma na amani ziwe juu yake Hakika wao hawakuwaabudu wao; akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Hapana bali wao wamewaharamishia halali, na wakawahalalishia haramu na wakawafuata basi hiyo ndio**

**ibada yao kwao**)), [Ameipokea Tirmidhi /3095/].

Utakapo kuwa umelifahamu hilo jua ya kwamba yule ambaye atahukumu kwa kitu ambacho hakukiteremsha Mwenyezi Mungu na akataka iwe kuhukumu kwake kwa asokuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake hakika imekuja Aya ya kukataa Imani yake ya kuwa hana Imani, na kuna Aya za kumhukumu kwa ukafiri wake, udhwalimu wake na uovu wake.

**Ama kigawanyo cha kwanza:**

Mfano ni maneno ya Mwenyezi Mungu aliposema: [**Huwaoni wale wanao dai kwamba wameamini yale yalio teremshwa kwako na yale yalio teremshwa kabla yako, wanataka wakahukumiwe kwa njia ya upotofu, na hali wameamrishwa wakatae hayo! Na Sheitani anataka kuwapotezelea mbali**. **Na wanapo ambiwa: Njooni kwenye yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu Na njooni kwa Mtume utawaona wanafiki wanakukwepa kwa upinzani**. **Basi inakuwaje unapo wasibu msiba kwa sababu ya yale iliyo tanguliza mikono yao? Hapo tena hukujia wakiapa kwa Mwenyezi Mungu wakisema: Hatukutaka ila wema na mapatano. Hao ndio wale ambao Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo ndani ya nyoyo zao. Basi waachilie mbali, uwape mawaidha na uwaambie maneno ya kuathiri na kuingia katika nafsi zao**. **Na hatukumtuma Mtume yoyote ila atiiwe kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na lau pale walipo jidhulumu nafsi zao wangali kujia, wakamuomba Mwenyezi Mungu msamaha, na Mtume akawaombea msamaha, hapana shaka wangali mkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea**

**toba na Mwenye kurehemu**. **La!Hapana kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yake wanayo khitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utakayo itoa,na wanyenyekee kunyenyekea**], [Suratul Al-Nisaa: 60, 61, 62, 63, 64-65).

Amewasifu Mwenyezi Mungu hawa wenye kudai kuwa wana Imani na hali ya kuwa ni Wanafiki kwa sifa nazo ni:

1-Kuwa wao wanataka iwe kuhukumiwa kwao ni kwa Twaaghuti, na kila anaye kwenda kinyume na hukumu ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake Kwa sababu mwenye kwenda kinyume na hukumu za Mwenyezi Mungu basi huyo amepetuka na amefanya uadui na hukumu hizo na mwenye hukumu, na Kwake hurudishwa mambo yote; naye ni Mwenyezi Mungu mtukufu, amesema Mwenyezi Mungu: [**Fahamuni!Kuumba na amri ni zake.Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote**], [Suratul Araaf: 54].

**2**-Hakika wao wanapo itwa kwenye kile alicho teremsha Mwenyezi Mungu na kile alicho teremshiwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake hukataa na huzuiya watu pamoja na kuipa nyongo amri hiyo.

**3**-Hakika wao wanapo patwa na matatizo kwa yale walio yatanguliza kwa mikono yao, huja huku wakiapa kwamba wao

hawakukusudia isipokuwa wema, na hali hiyo ni kama hali ya wenye kukataa hukumu za Kiislamu na huhukumiwa kwa sharia za kikafiri zenye kwenda kinyume na sharia za Mwenyezi Mungu, wao hudai kuwa huo ndio wema na uzuri wenye kuafikiana na hali ya zama hizi.

Kisha Mwenyezi Mungu akawatahadharisha hawa wenye kudai kuwa wana Imani wenye kusifika kwa sifa hizo, kuwa Mwenyezi Mungu anajua yaliyo katika nyoyo zao na yale wanayo yaficha katika mambo ambayo yanakwenda kinyume na wanayo yasema, akamuamrisha Mtume wake awape mawaidha na aseme kuwaambia katika nafsi zao kuna maneno makubwa, kisha akabainisha hekima ya kuwatuma Mitume awe yeye ndiye mwenye kutiiwa na mwenye kufuatwa na sio mwingine katika watu hata kama atakuwa na fikra nzuri kiasi gani, kisha akaapa Mwenyezi Mungu kwa ulezi wake kwa Mtume wake ambao ni ulezi maalumu katika aina za ulezi ambao unakusanya ishara katika kuonesha usahihi wa utume wake rehma na amani ziwe juu yake na akaapia kwa kiapo chenye kutiliwa mkazo kuwa haiwi Imani ni nzuri isipokuwa kwa mambo matatu:

1-Iwe kuhukumiana kwa kila ikhtilafu ni kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake:

**2-**Nyoyo ziwe na furaha kwa hukumu yake,na wala zisiwe ni zenye uzito na kudhikika kwa hukumu ya Mtumerehma na amani ziwe juu yake:

**3-**Ipatikane kujisalimisha kwa kikamilifu kwa kukubali kile alicho kihukumu, na kulipitisha lile alilo lihukumu pasina kubadili chochote.

**Ama kigawanyo cha pili:**

Ni mfano wa maneno ya Mwenyezi Mungu aliposema: [**Na wasio hukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ni makafiri**], [Suratul Maida: 44], na maneno yake Mwenyezi Mungu: [**Na wasio hukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu**], [Suratul Maida /45/], na maneno yake Mwenyezi Mungu: [**Na wasio hukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio waovu**], [Suratul Maida: 47] na je hizi sifa tatu zinamuendea msifiwa mmoja? Kwa maana kuwa kila mwenye kuhukumu kwa asicho kiteremsha Mwenyezi Mungu basi huyo ni kafiri, dhalimu na muovu kwa sababu Mwenyezi Mungu amewasifu makafiri kwa sifa ya dhulma na uovu amesema Mwenyezi Mungu: [**Na makafiri wao ndio madhalimu**], [Suratul Baqar: 254], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Hakika wao wamemkufuru Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wakafa hali ya kuwa ni waovu**], [Suratul Tauba: 84], kila kafiri ni dhalimu na ni muovu, au sifa hizi zinakwenda kwa wenye kusifiwa kutokana na mwenye kuwa na sifa hizo na kuto hukumu kwa alicho kiteremsha Mwenyezi Mungu? Hii ndio ipo karibu kwangu, na Mwenyezi Mungu ndiye mjuzi zaidi.

***Tunasema**: Yule ambaye atahukumu kwa kile ambacho hakukiteremsha Mwenyezi Mungu kwa kuona hakina thamani au kuzarau au kwa kuitakidi kuwa hukumu isio ya Mwenyezi Mungu ni bora kuliko ya Mwenyezi Mungu, na inawafaa viumbe zaidi, basi huyo amekufuru kukufuru kunako mtoa mtu katika mila, na miongoni mwa hawa ni wale wanao wawekea watu sharia ambazo zinakwenda kinyume na sharia za Kiislamu ili hizo sharia ziwe ni njia ambayo watu wataifuata, na wao hawakuweka sharia hizo zenye kwenda kinyume na sharia za Kiislamu Isipokuwa wao wanaitakidi kuwa sharia hizo ni nzuri na zinawafaa zaidi viumbe, kwa sababu ni kitu kinajulikana kwa akili ya kimaumbile kuwa Mwanadamu hawezi kuacha njia akaenda kwenye njia nyingine inayo kwenda kinyume na hiyo isipokuwa atakuwa anaitakidi kuwa ile aloifuata ni bora kuliko ile aloiacha.

Na yule ambaye hata hukumu kwa kile alicho kiteresha Mwenyezi Mungu na hali yakuwa hakuichukia ile aloiteremsha Mwenyezi Mungu, wala hakuidharau, na wala hakuitakidi kuwa nyingine isiyo kuwa hiyo ni bora na inawafaa zaidi viumbe kuliko ya Mwenyezi Mungu, na si vinginevyo amehukumu kwa isiyo kuwa ya

Mwenyezi Mungu kwa kulazimishwa na yule mwenye kuhukumiwa, au amefanya hivyo kwa kulipiza kisasi na mfano wa hayo, basi huyu ni dhalimu sio kafiri, na zitatofautiana daraja za dhulma yake kutokana na kile atakacho tumia kuhukumia na zile vyenzo za kuhukumia.

Na Yule ambaye hata hukumu kwa kile alicho kiteresha Mwenyezi Mungu si kwa kuichukia ile aloiteremsha Mwenyezi Mungu, wala kuidharau, na wala kuitakidi kuwa nyingine isiyo kuwa hiyo ni bora na inawafaa zaidi viumbe kuliko ya Mwenyezi Mungu, hakika si vinginevyo amehukumu kwa kitu kingine ili amfurahishe yule mwenye kuhukumiwa, au kwa ajili ya kuchunga rushwa alopewa au kitu kingine kwa ajili ya malengo ya kidunia, basi huyu ni muovu na sio kafiri, na zitatofautiana daraja za uovu wake kutokana na kile atakacho kitumia katika hukumu hiyo au nyenzo atakazo zitumia.

Amesema Sheikh Islamu Ibnu Taymiya Mwenyezi Mungu amrehemu kwa wale walio wafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu wapo katika namna mbili:

1-Wawe wanajuwa kuwa wamebadili dini ya Mwenyezi Mungu kisha wawafuate pamoja na kubadili huko na wanaitakidi kuwa ni halali vile walivyo vihalalisha, na kuviharamisha vile alivyo vihalalisha Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kufuata viongozi wao pamoja na kujua kwao kuwa wameenda kinyume na dini ya Mitume hii ni kufuru, na hakika ameifanya Mwenyezi Mungu na Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa ni shirki.

**2**-Iwe itikadi yao na imani yao kwa kuhalalisha haramu,na kuharamisha halali ni yenye kuthibiti lakini wao wamewatwii katika kumuasi Mwenyezi Mungu kama anavyo fanya Muislamu katika

maaswi ambayo anaitakidi kuwa ni maaswi hawa wana hukumu kama ilivyo hukumu kwa watu wenye madhambi [Majuumuul Fataawa].

****

**Swali la 69: Ni ipi hukumu ya kuchinja kwa kujikurubisha kwa asiokuwa Mwenyezi Mungu? Na je inafaa kula kichinjwa hiki?**

**Jibu:** Kuchinja kwa asio kuwa Mwenyezi Mungu ni shirki kubwa; kwa sababu kuchinja ni ibada kama alivyo amrisha Mwenyezi Mungu katika maneno yake: [**Basi swali na uchinje kwa ajili ya Mola wako Mlezi**], [Suratul Kauthar: 2], na maneno yake Mwenyezi Mungu: [**Sema: Hakika Swala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote** 162 **Hana msirika wake. Na hayo ndiyo niliyo amrishwa, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu** 163], [Suratul An'aam], mwenye kuchinja kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu basi huyo ni mwenye kushirikisha shirki yenye kumtoa mtu katika mila ya Uislamu,ni sawasawa amechinja kwa ajili ya Malaika katika Malaika, au Mtume katika Mitume, au Nabii katika Manabii, au Khalifa katika Makhalifa, au Walii katika Mawalii, au kwa Mwanachuoni katika wana chuoni, yote hiyo

ni shirki kwa Mwenyezi Mungu na ni yenye kumtoa mtu katika Mila, kilicho waJibu kwa mtu ni kumuogopa Mwenyezi Mungu katika nafsi yake, na asiweke nafsi yake katika shirki hiyo ambayo Mwenyezi Mungu amesema kuielezea: [**Kwa hakika anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu hakika Mwenyezi Mungu atamharamishia pepo, na mahala pake ni motoni.Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru**], [Suratul Maida: 72].

Ama kula nyama ya vichinjwa hivi hakika hiyo nyama ni haramu, kwa sababu imechinjwa kwa ajili ya asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na kila kilicho chinjwa kwa ajili ya asiye kuwa Mwenyezi Mungu au kimechinjwa kwa ajili ya masanamu, hakika hivyo vyote ni haramu kama alivyo taja Mwenyezi Mungu hilo katika Suratul Al-Maida katika maneno yake: [**Mmeharamishiwa nyamafu, na damu, na nyama ya nguruwe, na nyama ya aliye chinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu,na aliye kufa kwa kunyongeka koo, na aliye kufa kwa kupigwa, na aliye kufa kwa kuanguka, na aliye kufa kwa kupigwa pembe, na aliye liwa na mnyama ila mkimdiriki kumchinja. Na pia ni haramu kula nyama ya aliye chinjiwa masanamu**], [Suratul Maida: 3].

Vichinjwa hivi ambavyo vimechinjwa kwa ajili ya asiye kuwa Mwenyezi Mungu ni katika vigawanyo vilivyo haramu ambavyo si halali kuvila.

****

**Swali la 70: Nini hukumu ya mwenye kufanya mzaha kwa maneno ambayo ndani yake kuna istihizai kwa Mwenyezi Mungu au Mtume rehma na amani ziwe juu yake au Dini?**

**Jibu**: Jambo hili la kufanya Istihizai kwa Mwenyezi Mungu, au Mtume rehma na amani ziwe juu yake au Kitabu cha Mwenyezi Mungu, au Dini yake, hata kama itakuwa ni kwa mzaha, au ikawa ni katika kuwachekesha watu; ni ukafiri na unafiki, na hali hiyo ndio kama ile ilitokea wakati wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa wale ambao walisema: ((Hatujaona mfano wa jamaa zetu hawa wanakula sana, na ni waongo sana, na niwaoga katika kukutana na maadui)), wakiwa wanakusudia Mtume rehma na amani ziwe juu yake na Maswahaba zake ikatereka kwao: [**Na ukiwauliza wanasema: Sisi tulikuwa tukipiga porojo na kucheza tu**], [Suratul Tauba: 65]; kwa sababu walikuja kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, wakisema: Hakika sisi tulikuwa tukizungumza mazungumzo ambayo yalikuwa yakitusaidia kukata masafa ya safari, wakati huo alikuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake akiwaambia kile alicho amrishwa na Mwenyezi Mungu awaambie: [**Sema: Mlikuwa mkimfanyia maskhara Mwenyezi Mungu na Ishara zake na Mtume wake**. **Msitoe udhuru; mmekwisha kufuru baada ya kuamini**], [Suratul Tauba: 65-66].

Basi upande wa Uungu, Utume, Wah'yi, na Dini ni upande wa kuheshimiwa sana, haifai kwa yoyote auchezee si kwa mzaha au kuchekesha, wala kwa kudharau, kwani kufanya hivyo ni ukafiri;

kwa sababu ina kumfanyia hiana Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na Vitabu vyake, na sheria yake, na ni juu ya mwenye kufanya hivyo atubie kwa Mwenyezi Mungukwa kile alicho kifanya; kwa sababu hiyo ni katika unafiki, basi ni juu yake kutubia kwa Mwenyezi Mungu, amtake masamaha, na ayafanye vizuri matendo yake, na aufanye moyo wake ni wenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na kumtukuza, kwa kumuogopa na kumpenda.

****

**Swali la 71: Ni ipi hukumu ya kuwaomba walioko ndani ya makaburi?**

**Jibu:** Dua imegawanyika katika sehemu mbili:

**Sehemu ya kwanza**: Dua kwa maana ya Ibada, kama vile Swala, Swaumu na mengineyo katika ibada, atakapo kuwa mtu ameswali, au amefunga basi hakika atakuwa ameumba Mola wake kwa vitendo amsamehe, na amuepushea na adhabu zake, na ampe mambo mazuri, na hilo limeelezwa kwenye maneno yake Mwenyezi Mungu aliposema: [**Na Mola wenu Mlezi anasema: Niombeni nitakuitikieni.Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia Jahannam wadhalilike**], [Suratul Ghaafir: 60], Mwenyezi Mungu katika Aya hii amejalia dua kuwa ni ibada, na mwenye kufanya ibada yoyote katika aina za ibada

kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu hakika amekufuru kukufuru kwenye kumtoa katika Mila ya Uislamu, lau kama mtu atarukuu au akasujudi kwa kitu chochote anacho kitukuza kama anavyo mtukuza Mwenyezi Mungu katika rukuu au sujudu atakuwa ni Mshirikina mwenye kutoka katika Uislamu, kwa ajili hii amekataza Mtume rehma na amani ziwe juu yake kumuinamia Mtu wakati wa kukutana ni kwa ajili ya kuzuiya Madhara ambayo yanaweka kujitokeza katika shiriki, aliulizwa kuhusu Mtu amekutana na ndugu yake anaweza kumuinamia? Akasema: ((**Hapana**)), [Ameipokea Tirmidhii /2728, na Ibnu Maaja / 3702].

Na wanayo fanya baadha  ya watu akikusalimia hukuinamia hilo ni kosa, ni lazima kwako kumbainishia hilo.

**Sehemu ya pili**: Dua kwa maana ya maombi, hii sio kwamba yote ni shiriki, bali kuna ufafanuzi:

1-Ikiwa mwenye kuombwa yupo hai na analiweza lile analo ombwa basi hiyo sio shiriki, kama vile unavyo weza kumuomba mtu kwa kusema (Naomba maji ya kunywa) kwa yule mwenye kuliweza hilo, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Mwenye kuwaomba basi mpeni**)), [Ameipokea Abu Daud /3702, nayo ipo katika Sahihi Bukhari /5173/ kwa maana hiyo, na pia katika Sahihi Muslimu /1429/], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Na wakati wa kugawanya wakihudhuria jamaa na mayatima na masikini, wapeni katika hiyo mali yaurithi**], [Suratul Nisaa: 8], ikiwa atanyoosha fakiri mkono wake akasema nipe,basi

inafaa kumpa, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**wapeni katika hiyo mali ya urithi**].

2-Ikiwa mwenye kuombwa ni maiti, hakika kumuomba yeye ni shiriki yenye kumtoa mtu katika mila ya Uisslamu.

Ni machukio yalioje katika baadhi ya miji ya Kiislamu kuna wenye kuitakidi kwa fulani alio zikwa ambaye amezikwa kisha mwili wake haukuliwa na ardhi au umeliwa ananufaisha au anadhuru au anaweza kuleta kizazi kwa yule ambaye hana watoto, na hii ni shiriki kubwa yenye kumtoa mtu katika Uislamu, na mtu kulifanya hili mara kwa mara ni baya zaidi kuliko kunywa pombe au zinaa au liwatwi, kwa sababu ni kurudia rudia katika ukafiri, na sio sawa na kurudia rudia katika uovu, tunamuomba Mwenyezi Mungu azitengeneze hali za Waislamu.

****

**Swali la 72: Mtu anataka msaada kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu, Anadai kuwa (ni walii wa Mwenyezi Mungu) ni zipi alama za mawalii wa Mwenyezi Mungu?**

**Jibu:** Alama za mawalii wa Mwenyezi Mungu amezibainisha Mwenyezi Mungu katika maneno yake aliposema: [**Jueni kuwa vipenzi wa Mwenyezi Mungu hawatakuwa na khofu wala hawata huzunika**. **Hao ni ambao wameamini na wakakawa wanamcha Mwenyezi Mungu**], [Suratu Yunus: 62-63], hizi ndizo alama za Mawalii wa Mwenyezi Mungu: Kumuamini Mwenyezi Mungu, na kumcha Mwenyezi Mungu ((Yule atakaye kuwa ni Muumini mwenye kumcha Mwenyezi Mungu, basi huyo ni walii wa Mwenyezi Mungu)).

Ama mwenye kushirikisha huyo sio Walii, bali ni adui wa Mwenyezi Mungu kama alivyo sema: [**Aliye kuwa adui na Mwenyezi Mungu na Malaika wake na Mitume wake na Jibrli na Mikail, basi hakika Mwenyezi Mungu ni adui wa makafiri**], [Suratul Baqara: 98], mwanadamu yoyote mwenye kutaka msaada kwa asiokuwa Mwenyezi Mungu kwa jambo ambalo haliwezi isipokuwa Mwenyezi Mungu hakika huyo ni mshirikina na ni kafiri, si Walii wa Mwenyezi Mungu hata kama yeye atadai hivyo, bali madai yake hayo bila kumpekesha Mwenyezi Mungu imani yake na uchaMungu wake ni vya uongo vinapingana na Uwalii.

Nasaha zangu kwa ndugu zangu Waislamu katika mambo haya wasidanganyike kwa hawa watu, na iwe marejeo yao katika hilo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na Hadithi sahihi za Mtume rehma na amani ziwe juu yake, mpaka yawe matarajio yao na mategemezi yao ni kwa Mwenyezi Mungu peke yake, waamini hilo katika nafsi zao na zipate utulivu.

Na hawa ambao wanajiita watukufu na wakati mwingine mawalii, lau kama utafikiria vizuri yale wanayo yafanya utakuta kuwa wapo mbali sana na huo Uwalii na Utukufu, lakini utamkuta walii wa kweli ni katika watu ambao hujiweka mbali na kujiita nafsi zao Mawalii na kujitukuza na kujikweza na mambo yanayo fanana na hayo, utamkuta ni muumini mwenye kumcha Mwenyezi Mungu, mwenye kijificha si mwenye kudhihirisha nafsi yake na wala hapendi kujitangaza, wala hapendi watu waje kwake kwa kuhofu na kutaraji, kule tu kuwa mwanadamu anataka watu wamtukuze na wamheshimu na awe ndio marejeo yao wanapo patwa na shida, hili kwa hakika linapingana na uchaMungu na linapingana na uwalii; na kwa sababu hii imekuja katika Hadithi kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kwa yule mwenye kutafuta elimu ili alumbane na wajinga, au ili watu wawe wakimgeukia kwa kumuangali basi, sehemu tunayo ikusudia katika Hadithi ni maneno yake alipo sema: ((**Ili watu wawe wakimgeukia kwa kumuangali)**), [Ameipokea Tirimidhii /2655, na Ibnu Maaja /253/], hawa ambao wanaitwa Mawalii na wanajaribu kugeuza nyuso za watu kwao kwa kuwaaminisha kwamba wao ni Mawalii, wao ni katika watu walio mbali na huo Uwalii.

Nasaha zangu kwa ndugu zangu Waislamu wasidanganyike na hawa watu na mfano wa hawa, na warudi kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah za Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na wafungamanishe matumaini yao na matarajio yao kwa Mwenyezi Mungu peke yake.

****

**Swali la 73: Ni nini uchawi na ni ipi hukumu ya kujifundisha?**

**Jibu:** Uchawi wamesema wanavyuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, katika Lugha ya Kiarabu (Ni kila kitu kipo kwa upole na kujificha sababu zake) kiasi kwamba unakuwa na athari zilizo jificha hawazioni watu.

Ama katika istwilaha wameeleza baadhi yao kuwa ni ((Ni Maazima Ruqiya na Vifundo vinaathiri katika nyoyo, akili na mwili, na wakati mwingine huiondoa akili, na huleta kupendana na kuchukiana, na humfarakanisha mtu na mkewe, na huufanya mwili kuwa mgonjwa, na huondoa kufikiria kwake)).

Na kujifundisha uchawi ni haramu, bali inakuwa ni kufuru ikiwa itampelekea katika kushirikisha kwa kupitia sheitwani; amesema Mwenyezi Mungu: [**Na wakafuata yale waliyo zua masheitwani kuuzulia ufalme wa Suleiman. Na wala Suleimani hakukufuru, bali masheitwani ndio walio kufuru wakiwafundisha watu uchawi, na yalioteremshwa kwa Malaika wawili Haaruta na Maaruta katika Baabil. Wala hao hawakuwafundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru. Wakajifunza kwa hao wawili yale ya kumfarikisha mtu na mkewe. Wala hawawezi kumdhuru ila kwa kutaka Mwenyezi**

**Mungu.Na wanajifunza yatakayo wadhuru wala hayawanufaishi. Na hakika wanajua kwamba aliye chagua haya hatakuwa na fungu lolote katika Akhera**], [Suratul Baqar: 102], kwa hivyo kujifundisha aina hii ya uchawi ni ukafiri, na kuutumia pia ni ukafiri na ni dhulumu na ni uadui kwa viumbe, kwa sababu hiyo huuliwa Mchawi ima kwa kuritadi au kwa hadi, na ikiwa uchawi wake upo katika upande ambao unamkufurisha basi atauliwa kwa kuritadi na kwa kukufuru, na ikiwa uchawi wake haufiki katika daraja ya kukufuru basi atauliwa kwa hadi kwa ajili ya kuondoa shari yake na maudhi yake kwa Waislamu.

****

**Swali la 74: Ni ipi hukumu ya kuwapatanisha mume na mke kwa uchawi?**

**Jibu:** Jambo hilo ni haramu halifai, na yale yanayo tokea pia kuwafarakanisha vilevile ni haramu, na inaweza kuwa ni kufuru na ni shiriki amesema Mwenyezi Mungu: [**Wala hao hawakuwafundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru. Nakajifunza kwa hao wawili yale ya kumfarikisha mtu na mkewe. Wala hawawezi kumdhuru ila kwa kutaka Mwenyezi Mungu. Na wanajifunza yatakayo wadhuru**

**wala hayawanufaishi. Na hakika wanajua kwamba aliye chagua haya hatakuwa na fungu lolote katika Akhera**], [Suratul Baqar: 102]

****

**Swali la 75: Ukuhani ni nini? Na ni ipi hukumu ya mwenye kumwendea kuhani?**

**Jibu:** Ukuhani ni kutafuta uhakika kwa mambo ambayo hayana msingi, na ilikuwa wakati wa ujahili wakifanya hivyo baadhi ya watu wakisaidiwa na masheitwani wakiende mbinguni kwa wizi kusikiliza maneno kisha wakirudi huwahadithia kile walicho kisikia, kisha makuhani hawa huchukua neno moja ambalo wameambiwa na hawa masheitwani wanaliongeza kwa yale watakayo taka kuyaongeza katika maneno, kisha wanawaeleza watu, pindi itakapo tokea kitu kimekwenda sawa na yale waloyasema;watu huwakubali na kuwafanya ndio marejeleo yao katika kuwahukumia katika yao yanapo tokea matatizo na katika kuwaelezea yale yatakayo kuwa katika siku zijazo, na kwa sababu hiyo tunasema: Kuhani ni yule ambaye anatoa habari ya mambo ya ghaibu ambayo yatatokea siku za mbeleni.

Na wale wenye kuwaendea makuhani wameganyika katika sehemu tatu:

1-Amuendee kuhani kisha amuulize lakini asimkubali kwa kile atakacho ambiwa, hii ni haramu, na adhabu ya mwenye kufanya hivyo ni kuto kukubaliwa swala zake kwa muda wa siku arobaini, kama ilivyo thibiti katika (Sahihi mbili) kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema: ((**Mwenye kumwendea mpiga ramli akamuuliza haito kubaliwa swala yake kwa siku arobaini au nyusiku arobaini**)) [Ameipokea Muslimu /2230/].

2-Amuendee kuhani kisha amuulize na amkubali kwa kile atakacho muambia, hii ni kufuru kwa Mwenyezi Mungu; kwa sababu amemswadikisha katika madai yake kuwa anajua mambi ya ghaibu, na kumswadikisha mwanadamu katika madai yake kuwa anajua mambo ya ghaibu ni kukadhibisha maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Sema: Hapana katika mbingu na ardhi ajuaye ya ghaibu isipo kuwa Mwenyezi Mungu**], [Suratul Namli: 65], kwa ajili hiyo imekuja katika Hadithi sahihi: ((**Mwenye kumwendea kuhani akamsadikisha kwa yale atakayo muambia hakika atakuwa amekufuru kile kilicho teremswa kwa Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake**)): [Ameipokuea Abu Daudi /3904/ na Tirimidhii /135 /na Ibnu Maaja /639/ na akaisahihisha Albani katika Al-Ir-waau /6817].

3- Amuendee kuhani kisha amtake ambainishie hali yake kwa watu, hili halina ubaya, na Ushahidi ya hilo hakika Mtumerehma

na amani ziwe juu yake alimjia Ibnu Swayad akamfichia yeye kitu Mtume rehma na amani ziwe juu yake katika nafsi yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake akamuuliza ameficha nini kwake? Akasema: Moshi akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Kuwa mbali hutoweza kuvunja vitimbi vyako**)), [Ameipokea Bukhar /1354/, na Muslimu /2930].

Hizi ni hali tatu za mwenye kumwendea kuhani:

1-Amuendee kisha amuulize bila kumswadikisha kwa yele atakayo muambia, na bila kukusudia kubainishiwa hali yake hii ni haramu, na adhabu ya mwenye kufanya hivyo haito kubaliwa swala zake kwa muda wa siku arobaini.

2-Amuendee kisha amuulize na amswadikishe kwa kile atakacho muambia hii ni kufuru kwa Mwenyezi Mungu ni juu ya mwanadamu mwenye kufanya hilo atubie kwa Mwenyezi Mungu na arudi kwake na asipo fanya hivyo mpaka akafa katika hali hiyo atakuwa emekufa katika ukafiri.

3-Amuendee kisha anamuuliza kwa lengo la kumpa mtihani ili awabainishie watu uongo wa huyu kuhani hili halina ubaya.

****

**Swali la 76: Ni ipi hukumu ya Ibada itakapo kuwa imechanganyika na Ria (kujionesha)?**

**Jibu**: Hukumu ya Ibada itakapo kuwa imechanganyika na Ria (kujionesha) Inasemwa: Ibada ikichanganyika na Ria inagawa-nyika katika sehemu tatu:

1-Iwe mwenye kuifanya ibada hiyo anachunga zaidi watu,kama aliosimama kuswali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, lakini anas-wali hali ya kuwa anachunga watu wamsifie katika swala yale jambo hili ni lenye kubatilisha ibada.

2-Iwe hiyo Ria ni yenye kuwa pamoja na ibada wakati wa kutendwa; kwa maana kwamba: Awe wakati anaanza ibada yake mwanzo ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kisha ikatokea Ria wakati ikifanya ibada hiyo, ibada hii itakuwa katika moja ya mam-bo mawili:

1-Isifungamane mwanzo wa ibada yake na mwisho wake, mwanzo wake ni sahihi lakini mwisho wake ni batili.

**Mfano wa hilo**: Mtu ana riyali mia moja anataka kuzitoa sa-daka akatoa sadaka hamsini kwa ikhlaswi, kisha ikampitia katika nafsi yake Ria katika hamsini iliobaki, hamsini ya kwanza ni sahi-

hi na imekubaliwa, na hamsini iliobaki ni sadaka batili kwa sababu ya kuchanganyika Ria na Ikhlasi.

2-Ifungamane mwanzo wa ibada yake na mwisho wake, mwanadamu wakati huo hawezi kuacha kuwa na moja katika mambo mawili:

**Jambo la kwanza**: Aondoshe Ria wala asikae nayo bali aiepuke na kuichukia,hakika hilo haliathiri kitu; amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Hakika Mwenyezi Mungu ameusamehe ummah wangu yale ambayo yamepita katika nafsi zao na hawakuyafanya wala hawakuyazungumza**)), [Ameipokea Bukhari /5269/ na Muslimu /127].

**Jambo la pili:** Atulie na Ria hii wala asiiondoshe, wakati huo itazibatilisha ibada zake zote; kwa sababu mwanzo wake umefungamana na mwisho wake.

**Mfano wa hilo**: Aanze swala yake kwa ikhlaswa kisha impitie Ria katika rakaa ya pili hapo itabatilika swala yote kwa sababu ya mafungamano ya mwanzo wake na mwisho wake.

**3-**Itokee Ria baada ya kumaliza ibada hakika hapo haito iathiri na wala haito ibatilisha kwa sababu imekamilika hali ya kuwa ni

sahihi haito haribika kwa kutokea Ria baada ya kumalizika kwake. Si katika Ria mtu akifurahi kuwa watu wanajua ibada zake, kwa sababu hilo limetokea baada ya kumaliza ibada, na pia sio katika Ria mtu akifurahi kwa yeye kufanya ibada kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu hilo ni katika Ushahidi za imani yake amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Mwenye kufurahishwa na mazuri yake na akakasirishwa na mabaya yake basi huyo ni Muumini**)), [Ameipokea Tirmidhi /2165], na hakika aliulizwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake: juu ya hilo akasema: ((**Hiyo ni bishara njema kwa Muumini**)), [Ameipokea Muslimu / 2742/].

****

## Swali la 77: Ni ipi hukumu ya kuapa kwa msahafu?

**Jibu:** Swali hili inatakiwa tujibu kwa urefu, na hilo ni kwa sababu kuapa kwa kitu kunaonesha kukiheshimu hicho ulicho kiapia utukuzo maalumu kwa yule mwenye kuapiwa, kwa sababu hii haifai kwa yoyote kuapa isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu na kwa moja katika majina yake, au kwa sifa katika sifa zake, mfano aseme: Naapa kwa Mwenyezi Mungu nitafanya, au naapa kwa Mola wa Al-Kaaba nitafanya, au kwa utukufu wa Mwenyezi Mungu

nitafanya, na zinazo fanana na hizo katika sifa zake Mwenyezi Mungu aliye tukuka.

Msahafu umekusanya maneno ya Mwenyezi Mungu, na maneno ya Mwenyezi Mungu ni katika sifa zake, nayo ni sifa ya dhati ya vitendo, kwa sababu kwa kuangalia katika asili yake na kwamba Mwenyezi Mungu hakuacha kuwa na hatoacha kuwa ni mwenye kusifiwa kwa sifa hiyo; kwa sababu maneno ni ukamilifu, hivyo yenyewe kwa upande huo ni katika sifa za dhati yake Mwenyezi Mungu, kwa sababu haachi na hatoacha kuwa ni mwenye kuzungumza na ni mfanyaji kwa lile analo litaka, na kwa kuangalia ule umoja wake inakuwa ni miongoni mwa sifa zake za kivitendo, kwa sababu yeye anaongea wakati wowote akitaka.

Amesema Mwenyezi Mungu: [**Hakika amri yake anapotaka kitu ni kukiambia tu: Kuwa na kinakuwa**], [Suratul Yasin: 82], katika Aya hii ameambatanisha maneno na kutaka, nayo ni Ushahidi ya kuwa maneno ya Mwenyezi Mungu yanaambatana na matakwa yake na kupenda kwake, na Ushahidi za hilo ni nyingi sana, na kwamba maneno ya Mwenyezi Mungu hutokea kwa lile linalo amuliwa na hekima zake, kwa hivyo tunajua ubatili wa maneno ya mwenye kusema: hakika maneno ya Mwenyezi Mungu ni ya (Azalii) ya muda mrefu, na wala haiwezekani kuwa ni ye-

nye kufuata matakwa yake, na kwamba hayo maneno ni maana ilosimama kwa nafsi yake, na sio kitu chenye kusikiwa ambacho anaweza kukisikia yule anaye ongeleshwa na Mwenyezi Mungu, hakika maneno haya ni batili, uhakika wake Kuwa mwenye kusema ameyafanya maneno ya Mwenyezi Mungu ni yenye kusikiwa na yameumbwa.

Hakika ametunga Sheikh Islam bin Taymiya Mwenyezi Mungu awe radhi naye kitabu kijulikanacho kwa jina (Tas-iniyatu) amebainisha ndani yake ubatili wa maneno haya katika njia tisini.

Pindi itakapo kuwa msahafu umekusanya maneno ya Mwenyezi Mungu, na maneno ya Mwenyezi Mungu ni katika sifa zake basi kwa hakika inafaa kuapa kwa kutumia msahafu, kwa kusema Mwanadamu: (Naapa kwa Msahafu) akiwa anakusudia kilichomo ndani yake katika maneno ya Mwenyezi Mungu, na hakika wamelitolea Ushahidi hilo wanavyuoni wa Hanabila Mwenyezi Mungu awarehemu (Al-Mughuni ibni Qudaama), pamoja na hivyo lakini kilicho bora ni mtu kuapa kwa kitu ambacho hakita leta ufumbufu kwa wenye kusikiliza wakidhani amekosea aape kwa jina la Mwenyezi Mungu, kwa kusema: (Mwenyezi Mungu,au naapa kwa Mola wa Al-Kaaba), au kwa kusema: (Naapa kwa Yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake), na viapo vinavyo fanana na hivyo ambavyo watu wengi wanavijua, na wala haviwaletei tabu, kwani hakika kuongea na watu kwa vitu ambavyo wanavijua na vinazituliza nyoyo zao ni kheri na ni bora zaidi, pindi itakapo kuwa kuapa kunakuwa ni kwa Mwenyezi Mungu na majina yake na sifa zake, kwa hakika haifai kwa yeyote kuapa kwa asio kuwa

Mwenyezi Mungu, awe Mtume au Malaika au Al-Kaaba, na kwa visivyo kuwa hivyo katika viumbe,amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Mwenye kutaka kuapa na aape kwa jina la Mwenyezi Mungu au anyamaze**)), [Ameipokea Bukhari /2679, na Muslimu /1646].

Na amesema tena Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Mwenye kuapa kwa asiokuwa Mwenyezi Mungu hakika amekufuru au ameshirikisha**)), [Ameipokea Abu Daud /3251), na Tirmidhi /1535/].

Pindi atakapo msikia mtu mwanadamu yoyote anaapa kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake au kwa uhai wa Mtume (rehma na amani ziwe juu yake, au kwa uhai wa mtu yoyote mwingine; basi naamkataze hilo, na ambainishiye kuwa jambo hilo ni haramu halifai, lakini iwe kumkataza kwake na kumbainishia kwake ni kwa hekima kiasi kwamba iwe ni kwa upole na kwa ulaini, na pia amuelekee mtu ambaye anataka kunasihiwa kwa jambo hilo la kharamu kwa sababu baadhi ya watu unawapata wivu wakati wa kuamrishwa na kukatazwa basi atakasirika na kuwa mwekundu uso wake na yatavimba mashavu yake, na huenda akahisi katika hali hiyo kwa anamkataza kwa ajili ya visasi sheitwani anaweza kuweka katika nafsi yake kasoro hiyo, na lau kama Mwanadamu atamuweka kila mtu katika sehemu yake na akalingania

kwa Mwenyezi Mungu kwa Hekima, ulaini na upole lingewapelekea hilo kwenye kukubali kwa haraka zaidi, na hakika imethibiti kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Hakika Mwenyezi Mungu hutoa katika upole kile ambacho hatoi katika ukali**)), [Ameipokea Bukhari /6024/, na Muslimu /2593].

Na wala halijifichi kwa wengi lile lilotokea kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake katika kisa chake na yule Aarabiyu ambaye alikuja msikitini, akakojoa sehemu katika ule msikiti, wakamkemea watu na wakampigia kelele, Mtume rehma na amani ziwe juu yake akawakataza hilo, alipo maliza kukojoa alimuita Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na akasema kumuambia: ((**Hakika huu msikiti haifai ndani yake chochote katika maudhi au uchafu,na hakika si vinginevyo Msikiti ni kwa ajili ya kumtukuza Mwenyezi Mungu na kumsabihi na kusoma Qur`an**)), au kama alivyo sema Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kisha akawaamrisha Maswahaba zake wamwage katika mkojo wake ndoo ya maji [Ameipkea Bukhari /219/, na Muslimu /285].

Kwa jambo hilo umeondoka uharibifu na imetwahirika sehemu ya msikiti, na yamepatikana makusudio kwa kumnasihi yule Aarabiyu aliokuwa hajui, na hivi ndivyo inatakiwa tuwe katika kuwalingania waja wa Mwenyezi Mungu katika dini ya Mwenyezi Mungu tuwe ni wenye kulingania kwa Mwenyezi Mungu kwa kutumia njia ambazo zipo ni nzuri katika kufikisha haki katika nyoyo za viumbe na kuwafanya wawe wema, Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuwafikisha.

****

**Swali la 78: Ni ipi hukumu ya kuapa kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake na kwa Al-Kaaba? Na kwa utukufu na dhima? Na maneno ya mtu kuapa kwa kusema: (Kwa dhima yangu)?**

**Jibu**: Kuapa kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake haifai, bali hiyo ni katika aina za shiriki, na vilevile kuapa kwa Al-Kaaba haifai, bali nayo pia ni katika aina za shirki; kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake na Al-Kaaba vyote viwili ni viumbwa, na kuapa kwa kiumbe wa aina yoyote ni shiriki.

Na vile vile kuapa kwa utukufu wa kitu Fulani haifai, pia kuapa kwa dhima, kwa maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake alipo sema: ((**Mwenye kuapa kwa asio kuwa Mwenyezi Mungu hakika amekufuru au ameshirikisha**)), [Umetangullia upokezi wake].

Na amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Wala msiape kwa baba zenu, mwenye kutaka kuapa na aape kwa Mwenyezi Mungu au anyamaze**)) [Ameipokea Bukhar /6108/ na Muslimu /1646/].

Lakini ni wajibu wetu tujue kuwa maneno ya mtu anapasema (Kwa dhima yangu) hakusudii kuapa kwa dhima, hakika inakusudiwa dhima ahadi, inamana hii ipo katika ahadi yangu na masu-

uliya yangu haya ndio makusudio kwa hilo, ama atakapo kusudia kiapo basi atakuwa ameapa kwa asio kuwa Mwenyezi Mungu na hilo halifai, lakini kinacho dhihiri kwangu ni kuwa watu hawakusudii kiapo lakini wanakusudia ahadi, kwani dhima Ni kwa maana ya ahadi.

****

**Swali la 79: Ni ipi hukumu ya mwenye kuabudu makaburi kwa kuyazunguka pembezoni mwake na kuwaomba walio katika makaburi hayo na kuwawekea nadhiri, na mambo mengine yasio kuwa hayo katika aina za ibada?**

**Jibu**: Swali hili ni swali muhimu sana, na jibu lake linahitaji kujibiwa kwa urefu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tunasema: hakika watu wa makaburi wamegawanyika katika sehemu mbili:

**1**-Watu ambao wamekufa katika Uislamu na watu wanawasifia kwa kheri walizo zifanya wakati wakiwa duniani, hawa hutarajiwa kwao kheri,

lakini wanahitaji kwa ndugu zao Waislamu wawaombe kwa

Mwenyezi Mungu msamaha na huingia katika maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Na wale walio kuja baada yao wanasema: Mola wetu Mlezi Tusamehe sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa Imani, wala usijalie ndini ya nyoyo zetu vifundo kwa walio amini.Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye kurehemu**], [Suratul Hashir: 109], na yeye kwa nafsi yake hawezi kumnufaisha yoyote kwa sababu yeye ni maiti na mfu hawezi kuondoa madhara katika nafsi yake wala kwa mwingine, na wala hawezi kuleta katika nafsi yake maufaa wala kwa mwingine, yeye anahitaji kunufaisha wengine walioko hai kwa kumuombea dua wala yeye si mwenye kuwanufaisha walio hai.

**2**-Kuna watu wa makaburi ambao matendo yao humpelekea mtu katika uovu, uovu ambao humtoa mtu katika Mila ya Kiislamu, kama wale ambao huitwa mawalii, na wanajua mambo ya ghaibu na huponyesha magonjwa, na wanaleta kheri na manufaa kwa sababu zisizo julikana kiakili wala kisheria,hawa ambao wamekufa katika ukafiri haifai kuwaombea wala kuwaonea huruma na hiyo ni kwa sababu ya maneno yake Mwenyezi Mungu aliposema: [**Haimpasi Nabii na wale walio amini kuwatakia msamahawashirikina, japo kuwa ni jamaa zao, baada ya kwisha bainika kuwa hao ni watu wa Motoni. Wala haikuwa Ibrahim kumtakia msamaha baba yake ila kwa sababu ya ahadi aliyo fanya naye. Lakini ilipo mbainikia kwamba yeye ni adui wa Mwenyezi Mungu alijiepusha naye. Hakika Ibrahim alikuwa mwingi wa kuomba, mnyenyekevu, mvumilivu}. [**Suratul Al-Tauba: 113-114].

Na wao hawamnufaishi yoyote wala hawamdhuru, wala haifai kwa yoyote kufungamana nao, na ikiwa itakadiriwa kuwa kuna mmoja ameona makarama yao, kwa mfano aoneshwe kuwa katika kaburi lake kuna nuru, au katika kaburi lake inatoka harufu nzuri, au yanayo fanana na hayo, hali ya kuwa wao wanajulikana kuwa wamekufa katika ukafiri hakika huo ni udanganyifu kutoka kwa Ibilisi ili awafitinishe hao watu na wenye hayo makaburi.

Hakika mimi ninawatahadharisha ndugu zangu Waislamu kufungamana na yoyote asiokuwa Mwenyezi Mungu hakika Mwenyezi Mungu ndiye ambaye katika mikono yake kuna ufalme wa mbingu na ardhi, na kwake hurudi mambo yote, wala hakuna mwenye kuJibu dua ya mwenye matatizo isipokuwa Mwenyezi Mungu, na wala hakuna mwenye kuondosha baya lolote isipokuwa Mwenyezi Mungu; amesema Mwenyezi Mungu: [**Na neema yoyote mlio nayo inatoka kwa Mwenyezi Mungu. Kisha yakikuguseni madhara manamuomba yeye**], [Suratul Nahli: 53].

Nasaha zangu nyingine pia Wasi muige katika dini yao na wala wasimfuate yoyote isipokuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, amesema Mwenyezi Mungu: [**Hakika nyinyi mna kiigizo kizuri kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana**], [Suratul Ahzaab: 21], na amesema Mwenyezi Mungu: [**Sema:Ikiwa mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi Mwenyezi Mungu atakupendeni**], [Suratul Al-Imran: 31].

Inampasa kila Muislamu apime matendo ya huyu anaye dai kuwa ni Walii kwa kutumia yale yaliokuja katika Kitabu na Sunnahh, ikiwa yataafikiana na Kitabu na Sunnahh hakika huyo hutarajiwa kuwa ni Walii katika mawalii wa Mwenyezi Mungu, na ikiwa itakwenda kinyume na Kitabu na Sunnah, basi huyo si katika Mawalii wa Mwenyezi Mungu, na hakika Mwenyezi Mungu ametaja katika Kitabu chake mizani ya usawa na uadilifu katika kumjua Walii wa Mwenyezi Mungu; pale alipo sema: [**Jueni kuwa vipenzivya Mwenyezi Mungu hawata kuwa na khofu wala hawatahuzunika**. **Hao ni ambao wameamini na wakawa wanamcha Mwenyezi Mungu**], [Suratu Yunus: 62-63], yule atakaye kuwa ni mwenye kumcha Mwenyezi Mungu basi huyo ni Walii wake, na yule ambaye hata kuwa na sifa hiyo basi huyo sio Walii katika Mawalii wa Mwenyezi Mungu, na yule ambaye atakuwa na baadhi ya Imani na uchaMungu atakuwa na kitu katika uwalii wa Mwenyezi Mungu, pamoja na hivyo hakika sisi hatuwezi kumhukumia mtu maalumu kwa kitu chochote, lakini sisi tunasema: kwa ujumla Kila aliye Muumini mwenye kumcha Mwenyezi Mungu anakuwa ni Walii katika Mawalii wa Mwenyezi Mungu.

Na ajue kuwa hakika Mwenyezi Mungu anaweza kumpa mtu mtihani kwa kitu kama hiki anaweza kufungamana mtu na makaburi akawa anamuomba yule mwenye lile kaburi, au akachukua mchanga wa kaburi lake akawa anataka baraka kwa mchanga huo, akawa anafanikiwa katika yale anayo yataka ikawa hiyo ni fitina ya Mwenyezi Mungu kwa mtu huyu; lakini sisi tunajua kuwa hili kaburi haliwezi kujibu dua ya mwenye kuomba na kuwa mchanga huu hauwezi kuwa ni sababu ya kuondosha madhara wala kuleta manufaa; tumelijua hilo kwenye maneno ya Mwenyezi Mun-

gu alipo sema: [**Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawata waitikia mpaka siku ya Kiama, na wala hawatambui maombi yao**. **Na watu watakapo kusanywa watakuwa maadui zao, na wataikataa Ibada yao**] [Suratul Ahqaf: 5-6], na amesema tena Mwenyezi Mungu: [**Na wale wanao waomba wasiokuwa Mwenyezi Mungu hawaumbi kitu, bali wao wameumbwa**. **ni wafu si hai, na wala hawajui watafufuliwa lini**], [Suratul Nahl: 20-21].

Na Aya kwa maana hii zipo nyingi zinaonesha kuwa kila mwenye kuombwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu hawezi kuJibu dua wala hanufaiki mwenye kuomba, lakini kinaweza kupatikana kile kiombwacho wakati wa kuomba asiye kuwa Mwenyezi Mungu ili iwe ni mtihani kwake.

***Tunasema**: Hakika kimepatikana hiki kitu wakati wa kuomba lakini sio kwa kuomba, na tofauti kati ya kupata kitu kwa kitu na kupata kitu wakati wa kitu, hakika sisi tunajua kujua kwa yakini kuwa kuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu sio sababu ya kuleta manufaa au kuondoa madhara, kwa Aya nyingi ambazo Mwenyezi Mungu amezitaja katika Kitabu chake, lakini kinaweza kutokea kitu wakati wa kuomba dua hiyo ili iwe ni fitna na mtihani, Mwenyezi Mungu anaweza kumjaribu mwanadamu kwa sababu ya maasi ili amjue yule ambaye ni mwenye kumuabudu Yeye, na yule ambaye huabudu matamanio yake, hivi hukuona kwa wale watu wa juma mosi miongoni mwa Mayahud wakati ambao Mwenyezi Mungu aliwaharamishia kuvua samaki siku ya juma mosi, akawajaribu Mwenyezi Mungu wakawa samaki wanakuja siku ya Juma

mosi kwa wingi wa ajabu, na siku isio ya juma mosi wakawa wana jificha, ikachukua muda mrefu hali hiyo, wakasema: ina kuwa vipi tunajiharamishia nafsi zetu hawa samaki, kisha wakafikiria wakakadiria wakaangalia wakasema: tuiweke mitego yetu siku ya Ijumaa, samaki wakinasa tunakuja kuwachukua siku ya juma pili, wakakifanya kitendo hiki ambacho ni mbinu za kuhalalisha alicho kiharamisha Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu akawageuza ni manyani wenye kupata hasara, amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: [**Na waulize khabari za mji uliokuwa kando ya bahari, wakivunja sabato(Juma mosi ya mapumzika). Samaki walikuwa wakiwajia juu juu siku ya mapumziko yao, na siku zisizo kuwa za mapumziko hawakuwa wakiwajia. Kwa namna hiyo tuliwajaribu kwa sababu walikuwa wakifanya upotovu**], [Suratul Aarafu: 163], na amesema Mwenyezi Mungu: **[Na hakika mlikwisha yajua ya wale miongoni mwenu walio ivunja sabato, (siku ya mapumziko, juma mosi) na tukawaambia: Kuweni manyani wadhalilifu**. **Kwa hivyo tukayafanya hayo kuwa onyo kwa wale walio kuwa katika zama zao na walio kuja baada yao, na mawaidha kwa wanao mcha Mwenyezi Mungu**], [Suratul Baqra: 65-66].

Anagalia ni namna gani alivyo wafanyia wepesi hao samaki katika siku zile ambazo walikatazwa kuwavua, lakini wao hawakusubiri wakafanya hila hii katika vitu alioviharamisha Mwenyezi Mungu.

Kisha angali yale yalio watokea Maswahaba wa Mtumerehma na amani ziwe juu yake  wakati ambao Mwenyezi Mungu aliwapa

mtihani hali ya kuwa wao wamehirimia Hijja kwa kuwinda vitu ambavyo vimeharamishwa kwa mwenye kuhirimia wakawa wanyama wanakuja karibu yao kiasi kwamba wanaweza kuwashika kwa mikono yao, lakini wao hawakuthubutu kushika chochote katika hivyo, anasema Mwenyezi Mungu: [**Enyi mlio muamini Mwenyezi Mungu! Atakujaribuni kidogo kwa wanyama wa kuwinda inayo wafikia mikono yenu, ili Mwenyezi Mungu amjue nani anaye mkhofu kwa ghaibu. Basi atakaye ruka mipaka baada ya hayo atapata adhabu kali**], [Suratul Maida: 94], vilikuwa viwindwa vipo sehemu ambazo wanaweza kuwashika kwa mikono yao na walikuwa wanaweza kuwapata ndege kwa kutumia mikuki kwa urahisi kabisa, lakini wao walimuogopa Mwenyezi Mungu, hakuna aliye tanguliza mkono wake kumshika mnyama yoyote.

Hivi ndivyo inavyo takiwa kwa mtu pindi atakapo rahisishiwa njia za kufanya mambo ya haramu amuogope Mwenyezi Mungu, na asije akafanya mambo hayo ya haramu aliokatazwa nayo, na ajue kuwa kufanyiwa wepesi sababu katika kuyafanya hayo ya haramu ni katika mlango wa mitihani basi naasubiri hakika mwisho mwema ni kwa wale wenye kusubiri.

****

**Swali la 80: TutawaJibu vipi wenye kuabudu makaburi ambao hutolea Ushahidi kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake amezikwa msikitini na watu wanaswali pale katika ule msikiti huko sio kuabudu kaburi?**

**Jibu:** Majibu ya swali hili yapo katika vigawanyo vifuatanyo:

**1**-Hakika Msikiti haukujengwa katika kaburi, bali ulijengwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake akiwa hai.

**2-**Hakika Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakuzikwa katika Msikiti mpaka isemwe huku ni kuwazika watu wema Msikitini, bali alizikwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake katika nyumba yake.

**3**-Hakika kuiingiza nyumba za Mtume rehma na amani ziwe juu yake ikiwemo ya Aisha Mwenyezi Mungu awe radhi naye kuwa ni katika Msikiti sio kwa kukubaliana Maswahaba Mwenyezi Mungu awe radhi nao, bali ni baada ya kuwa wengi katika wao wamekufa, na hilo lilikuwa tisini na nne Hijiria kwa kukadiria, hilo sio katika mas'ala ambayo waliyajuzisha Maswahaba; bali baadhi yao walilikataa hilo, na katika walio kataa ni Said bin Musayyibu Mwenyezi Mungu amrehemu.

**4**-Hakika kaburi lenyewe halipo Msikitini hata baada ya kuingizwa, kwa sababu lipo katika chumba chenye kujitegemea pembeni ya Msikiti, sio kwamba Msikiti umejengwa katika kaburi; kwa sababu hio ilifanywa sehemu hii ni yenye kuhifadhiwa na imezungushwa kuta tatu, na ukawekwa ukuta katika pembe yake kuzuiya muelekeo wa kibla, kwa maana kwamba ukuta umejengwa kwa pembe tatu ili mtu asiweze kulielekea wakati wa kuswali kwa sababu lipo mbali na muelekeo wa kibla, kwa hivyo hoja ya wenye kuabudu makaburi imebatilika.

****

### Swali la 81: Ni ipi hukumu ya kujengea makaburi?

**Jibu:** Kujengea makaburi ni haramu, hakika amekataza Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa sababu katika hilo kuna kuwatukuza wenye makaburi hayo [Ameipokea Muslimu /970/], kwamba kuyajengea ni njia ya kumpelekea mtu katika kuyaabudu na kuto kuya jengea ni kuzuiya kuyaabudu na kuya fanya ni miungu pamoja na Mwenyezi Mungu, kama ilivyo katika majengo mengi yaliyo jengwe kwenye makaburi, wamekuwa watu wakimshirikisha Mwenyezi Mungu na watu walioko kwenye makaburi hayo, wanawaomba walioko kwenye hayo makaburi pamoja na Mwenyezi Mungu, na kuwaomba walioko makaburini kutaka

wakuondoshee matatizo ulio kuwa nayo ni shirki kubwa na ni kuritadi kutoka katika Uislamu.

****

## Swali la 82: Ni ipi hukumu ya kuzika maiti msikitini?

**Jibu:** Kuzika Msikitini amekataza Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuifanya Misikiti kuwa makaburi, na amelaani mwenye kufanya hivyo naye wakati huo akiwa katika dakika zake za mwisho, na ameutahadharisha Ummah wake na akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa hilo ni katika vitendo vya Kiyahudi na Kinaswara [Ameipokea Bukhari / 1330/], kwa sababu hiyo ni njia ya kumpeleka mtu katika kumshirikisha Mwenyezi Mungu, kwa sababu kujenga Msikiti katika kaburi na kuwazika watu katika hiyo Misikiti ni njia ya kumpeleka mtu katika kumshirikisha Mwenyezi Mungu, kwa sababu watu wanaamini kuwa watu hawa waliozikwa katika Misikiti wananufaisha na wanadhuru, au wana kitu maalumu tofauti na watu wengine ambacho anaweza kukitumia kitu hicho kwenye kujikurubisha kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu, msingi wa Tauhid na Akida iliyo sahihi ni kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Na hakika Misikiti ni ya Mwenyezi Mungu, basi msiabudu yeyote pamoja Mwenyezi Mungu**], [Suratul Jinn: 18], inapasa kuwa Misikiti ni kwa ajili

ya Mwenyezi Mungu tu imeepukika na shiriki, huabudiwa ndani yake Mwenyezi Mungu peke yake asiye na msirika, hiki ndicho kilicho cha lazima kwa Muislamu.

****

**Swali la 83: Ni ipi hukumu ya kusafiri kwa ajili ya kuzuru kaburi la Mtume rehma na amani ziwe juu yake?**

**Jibu:** Kufunga safari kwa sababu ya kuzuru kaburi la yeyote haifai kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake anasema: ((**Haifungwi safari isipokuwa katika misikiti mitatu, msikiti mtukufu wa Makka, na msikiti wangu huu, na msikiti wa Aqswa**)), [Ameipokea Bukhar /1189/, na Muslimu /1397/].

Na makusudio ya hili ni kuwa haifungwi safari ya kwenda sehemu yeyote katika ardhi kwa sababu ya kufanya ibada isipokuwa katika sehemu hizo tatu; kwa sababu ndio sehemu maalumu ambazo hufungiwa safari ya kiibada, na zisiokuwa hizo katika sehemu hazifungiwi safari.

Ikwa ni hivyo basi kaburi la Mtume rehma na amani ziwe juu yake ,halifungiwi safari bali safari inafungwa kwenda katika msikiti wake, atakapo fipa hapo ni Sunnahh kwa wanaume kulizuru kaburi la Mtume rehma na amani ziwe juu yake, ama wanawake sio Sunna kwao kulizuru kaburi la Mtumerehma na amani ziwe juu yake .

****

**Swali la 84: Ni ipi hukumu ya kutaka Baraka kwenye makaburi na kuyazunguuka kwa makusudio ya kukidhiwa haja au kujikurubisha na ni ipi hukumu ya kuapa kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu?**

**Jibu:** Kutaka baraka katika makaburi ni haramu na ni aina katika aina za shiriki, kwa sababu ni kuthibitisha kuwa kuna athari inapatikana na Mwenyezi Mungu hakushusha katika hilo ushahidi, na haikuwa ni katika ada ya wema walio tangulia Mwenyezi Mungu awarehemu kutaka Baraka kwenye mfano wa vitu kama hivyo, inakuwa kwa upande huo ni bidaa pia, na atakapo itakidi mwenye kutaka Baraka kuwa mwenye kaburi lile ana athari au anaweza

kuondoa madhara au kuleta manufaa itakuwa hiyo ni shirki kubwa atakapo muomba amletee manufaa au amuondoshee madhara.

Na vile vile inakuwa ni katika shiriki kubwa atakapo muabudu mwenye kaburi kwa kurukuu na kusujudu au kwa kuchinja; kujikurubisha kwake na kumtukuza, amesema Mwenyezi Mungu: [**Na anaye muomba pamoja na Mwenyezi Mungu mwingine na hana ushahidi wa hili; Bila shaka hisabu yake iko kwa Mola wake Mlezi.Kwa hakika makafiri hawafanikiwi**], [Suratul Muuminun: 117], na amesema tena Allha: [**Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi naatende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi**], [Suratul Kahfi: 110], mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu siriki kubwa ni kafiri na atakaa motoni milele, na pepo kwake ni haramu; kwa maneno ya Mwenyezi Mungu aliposema: [**Kwani anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu hakika Mwenyezi Mungu atamharamisia pepo na mahala pake ni Motoni. Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru**], [Suratul Maida: 72].

Ama kuapa kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa mwenye kuapa anaitakidi kuwa chenye kuapiwa kina daraja kama alilo nalo Mwenyezi Mungu basi atakuwa ni mshirikina mwenye kushirikisha kwa shirki kubwa, na ikiwa haitakidi hivyo lakini iliingia katika moyo wake kukitukuza kile alicho kiapia, na haikumpelekea kukiapia pasina kuitakidi kuwa kina daraja kama alilo nalo Mwenyezi Mungu basi huyo ni mwenye kushirikisha shiriki ndogo, kwa maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, alipo

sema: ((**Mwenye kuapa kwa asiyo kuwa Mwenyezi Mungu hakika amekufuru au ameshirikisha**)) [Umetangulia upokezi wake].

Ni lazima kuwakemea kwa nguvu wale wenye kuomba Baraka katika makaburi au kuyaomba makaburi, au wenye kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na kumbainishia kuwa hawezi kumuokoa na adhabu ya Mwenyezi Mungu huyo anaye muomba,na maneno yao wanasema: ((hiki kitu tumechukua kwao)) hakika Ushahidi hii ni Ushahidi ya washirikina ambao waliwakadhibisha Mitume, na wakasema: [**Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhususi na sisi tunafuuta nyayo zao**] [Suratul Zuhurf: 23], akasema kuwaambia Mtume wa Mwenyezi Mungu: [**Hata nikikuleteeni yenye uwongofu bora kuliko mlio wakuta nayo baba zenu? Wakasema: Sisi tunayakataa tu hayo mliyo tumwa**], [Suratul Zuhurf: 24], akasema Mwenyezi Mungu**: [Basi tukawalipiza Angalia ulikuwaje mwisho wa walio kadhibisha],** **[**Suratul Zuhurf: 25]. Wala si halali kwa yeyote kutoa Ushahidi kwenye baatili yake kuwa aliwakuta baba zake wakifanya, au kwa kuwa ni ada ya kwao na mfano wa hayo, na kama atatolea ushahidi kwa hilo basi ushahidi wake ni batili mbele ya Mwenyezi Mungu haita mnufaisha wala kumsaidia na kitu chochote, ikiwa ni hivyo basi ni juu ya wale walio jaribiwa na vitu kama hivyo watubiye kwa Mwenyezi Mungu, na wafuate haki popote watakapo kuwa, na kwa hali yoyote, na sehemu yoyote, na wala isiwazuiye kukubali haki ada za watu wake, au lawama za watu wake wasio na

elimu, kwa hakika Muummini wa kweli ni yule ambaye haogopi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu lawama ya mwenye kulaumu, na wala hazuiwi na dini ya Mwenyezi Mungu kwa kizuizi cha aina yoyote.

Mwenyezi Mungu atupe Taufiq katika yale yote ambayo anayaridhia, na atukinge na yale yote ambayo yana makasiriko na adhabu zake.

****

**Swali la 85: Ni ipi hukumu ya kuvaa nguo ambayo ina picha ya Mnyama au Mwanadamu?**

**Jibu:** Haifai kwa Mwanadamu kuvaa nguo ambayo ina picha ya Mnyama au Mwanadamu, na pia haifai kuvaa kilemba au kitu chochote kinacho fanana na hivyo chenye picha ya Myama au Mwanadamu; na hilo ni kwa sababu imethibiti kutoka kwa Mtume

rehma na amani ziwe juu yake amesema: ((**Hakika Malaika hawaingii katika nyumba ambayo ina picha**)) [Ameipokea Bukhari /2105/na Muslimu /2104/].

Kwa ajili hiyo sioni haja kwa yoyote kuhifadhi mapicha kwa ajili ya ukumbusho kama wanavyo sema, na kwa yule ambaye anazo picha za ukumbusho kitu kilicho wajibu kwake ni aziharibu, ni sawa sawa ameziweka katika ukuta au ameziweka katika Albam au sehemu nyingine zisizo kuwa hizo; kwa sababu kubaki nazo kutapelekea kuzuiliwa Malaika kuingika katika nyumba zao, na hadithi hii ambayo nimeitaja hakika imethibiti kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, Mwenyezi Mungu ndiye mjuzi zaidi.

****

### Swali la 86: Ni ipi hukumu ya kutundika picha katika ukuta?

**Jibu:** Kutundika picha katika ukuta ni haramu, hata kama itakuwa kinacho onekana ni baadhi ya mwili au kichwa tu, na kusudio la kuitukuza lipo wazi na asili ya shirki ni ghuluu hii, kama

ilivyo kuja kutoka kwa Ibnu Abass Mwenyezi Mungu awe radhi naye amesema katika masanamu ya watu wa Nuhu ambayo walikuwa wakiyaabudu, hakika masanamu hayo yalikuwa ni majina ya watu wema walizipiga picha sura zao ili watu wawakumbuke, kisha zama zilivyo zidi kwenda wakawaabudu. [Ameipokea Bukhar / 4920/].

****

**Swali la 87: Ni ipi kuhumu ya kupiga picha kwa kutumia kamera za haraka?**

**Jibu:** Kuchukua picha kwa kamera za haraka ambazo hazihitaji kazi nyingi hilo halina ubaya; kwa sababu hilo haliingii katika picha, lakini kunabaki na swali la kujiuliza: Ni nini lengo la kupiga picha hizi? Ikwa lengo la kupigaa ni kuihifadhi tu kwa ajili ya ukumbusho itakuwa kupiga kwake ni haramu, na hilo ni kwa sababu vitu vinavyo pelekea katika jambo flani vina hukumu zake na makusudio yake, na kuhifadhi picha kwa ajili ya ukumbusho ni haramu; kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake ametupa khabari kuwa Malaika hawaingii katika nyumba ambayo

ina picha [Umetangulia upokezi wake] na hili linaonesha uharamu wa kuhifadhi picha katika majumba, ama kutundika picha katika ukuta hakika hilo ni haramu na halifai, na Malaika haingii katika nyumba yenye picha.

****

**Swali la 88: Ni vipi tutawajibu watu wa bidaa wanao toa Ushahidi katika bidaa zao kwa Hadithi: ((Mwenye kuanzisha katika Uislamu Sunna nzuri…)) [Ameipokea Muslimu /1017/].**

**Jibu:** Tunawajibu hao kwa kusema, Hakika ambaye amesema: ((**Mwenye kuanzisha katika Uislamu Sunna nzuri atakuwa na malipo yake na malipo ya mwenye kufanya Sunna hiyo**)). Na ndiye aliyesema: ((**Shikamaneni na Sunna zangu na Sunna za Makhalifa wangu waongofu baada yangu, na jiepusheni na mambo yenye kuzuka, kwani hakika kila chenye kuzuka ni bidaa na kila bidaa ni upotevu, na kila upotevu ni motoni**)) [Umetangulia upokezi wake].

Sababu ya Hadithi hii ni kuwa, Mtume rehma na amani ziwe juu yake: alikuwa akiwahimiza watu kutoa sadaka kwa watu ambao walikuja kwake wakiwa na shida ya chakula Mtume rehma na amani ziwe juu yake akawaita Maswahaba wake katika kuwachangia watu hawa, akaja mtu mmoja na kibubu kilicho jaa dhahabu akakiweka mbele ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Mwenye kuanzisha katika Uislamu Sunna nzuri atakuwa na malipo yake na malipo ya mwenye kufanya Sunnahh hiyo mpaka siku ya Kiama**)).

Tutakapo kuwa tumejua sababu ya Hadithi hii na tukaiweka katika maana ambayo imeelekezwa, itatubainikia kuwa makusudio ya Sunna ni Sunna katika kulifanyia kazi jambo flani, na sio Sunna ya kuweka jambo katika sharia ambalo halikuwekwa na sharia; kwa sababu kuweka jambo kuwa ni sharia haiwi isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake, na maana ya Hadithi mwenye kuanzisha Sunna ina maana: Ameanza kuifanyia kazi hiyo ya Sunna na watu wakamfuata katika kuitekeleza atakuwa na malipo yake ya kufanya na malipo ya mwenye kuifanyia kazi Sunna hiyo, hii ndio maana ya Hadithi, au huchukuliwa makusudio yake kwa ((Mwenye kuanzisha Sunnahh nzuri)) Mwenye kufanya njia ambayo itamfikisha katika ibada na watu wakamuiga katika njia hiyo, kama vile kutunga vitabu, kujenga Madrasa na yanayo fanana na hayo katika mambo ambayo yanakuwa ni njia katika kumfikisha mtu katika jambo lenye kutakiwa kisheria, atakapo lianzisha mtu jambo hili linalo pelekea katika jambo linalo takiwa Kisheria atakuwa ni mwenye kuingia katika Hadithi hii.

Na lau kama ingekuwa maana ya Hadithi kuwa anaweza mtu kuweka jambo katika sharia lile analo litaka, ingekuwa dini ya Kiislamu haikukamilika wakati wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake  na ingekuwa kila zama kuna sharia zake na njia zake, pindi atakapo dhani hivyo mwenye kufanya hiyo bidaa kwamba ni nzuri basi dhana yake itakuwa na makosa; kwa sababu dhana yake hiyo inapingana na maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, alipo sema: ((**Kila bidaa ni upotevu**)).

****

**Swali la 89: Ni ipi hukumu ya kusherehekea Maulidi ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake?**

**Jibu:** Kwanza: Usiku wa kuzaliwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, sio kwamba unajulikana kwa ushahidi wa kukata ambazo hauna mashaka,vbali baadhi ya wanawa vyuoni wa zama hizi wamehakikisha siku hiyo ilikuwa ni usiku wa tarehe tisa katika mwezi wa Rabii L-Awali, na sio usiku wa tarehe kumi na mbili Ikiwa ni hivyo basi kuifanya siku ya kusherekea ni tarehe kumi na mbili Hakuna asili kwa upande wa Kitarekhe (historiya).

**La pili:** Kwa upande wa Kisheria kusherekea maulidi ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakuna ushahidi pia, kwa sababu ingekuwa ni katika sharia ya Mwenyezi Mungu angeilifanya Mtume rehma na amani ziwe juu yake , au engeliufikishia Ummah wake,na kama engelifanya au kuufikisha kwa Ummah wake basi ingelazimika jambo hilo kuhifadhiwa ,kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema: [**Hakika Sisi ndio tulio teremsha ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutakao ulinda**], [Suratul Hijir: 9], kwa sababu, pindi itakapo kuwa si katika dini ya Mwenyezi Mungu,basi haifai kwetu kumuabudu nayo Mwenyezi Mungu na kujikurubisha kwake kwa jambo hilo, ikiwa Mwenyezi Mungu ameweka katika kumfikia Yeye kuna njia maalumu nayo ni ile aliokuja nayo Mtume rehma na amani ziwe juu yake, ikiwa ni hivyo ni vipi sisi tutaweza kuleta njia kutoka kwetu itakayo tufikisha kwa Mwenyezi Mungu hali ya kuwa sisi ni waja tu? Hii ni kwa upande wa haki za Mwenyezi Mungu tuweke sharia katika dini yake kitu ambacho hakikutoka kwake, kama ilivyo kufanya hivyo pia kunakusanya kukadhibisha maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Leo nimekukamilishieni dini yenu na nimekutimizieni neema zangu],** [Suratul Maida: 3].

***Tunasema**: Kusherekea huku ikiwa ni katika ukamilifu wa dini, basi hapana budi kuwa ulikuwepo kabla ya kufa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na iwapo kutakuwa si katika ukamilifu wa dini basi haiwezekani uwe katika dini kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema**:** [**Leo nimekukamilishieni dini yenu**]. Na mwenye kudai kuwa ni katika ukamilifu wa dini basi huyo atakuwa amezua kitu baada ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kwa sababu maneno yake yanakadhibisha Aya hii tukufu, na haku-

na shaka kuwa wale wanao sherekea Maulid ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, hakika wakakusudia kwa hilo kumtukuza Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na kudhihirisha mapenzi yao kwake, na zote hizo ni katika Ibada, kwa sababu kumpenda Mtume rehma na amani ziwe juu yake, ni Ibada, bali haiwi Imani ya Mtu ni kamili mpaka awe Mtume rehma na amani ziwe juu yake anapendeza zaidi kuliko nafsi yake na watoto wake na wazazi wake na watu wote kwa ujumla, na kumtukuza Mtume rehma na amani ziwe juu yake pia ni katika Ibada, pia kuonesha upole kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni katika Ibada kwa sababu katika hilo kuna kuipenda ndani yake sheria yake.

Kwa ajili hiyo: Kusherekea Maulid ya Mtumerehma na amani ziwe juu yake kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na kumtukuza Mtume wake ni Ibada, na pindi itakapo kuwa ni Ibada basi haifai milele kuzuliwa katika dini ya Mwenyezi Mungu kitu ambacho hakipo katika dini yake, kusherekea Maulidi ni bidaa na ni haramu, kisha hakika sisi tunasikia katika sherehe hizo kunapatikana maaovu makubwa sana ambayo sheria wala akili haiyakubali, na wao wanaghani kwa Kaswida ambazo kuna kupetuka mipaka ndani yake kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, mpaka wamemfanya Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni mkubwa kuliko Mwenyezi Mungu katika kaswida hizo.

Na jingine hakika sisi tunasikia kwa baadhi ya wenye kusherekea Maulidi Anapo soma msomaji kisa cha Maulid mpaka anapo fikia katika maneno yake: ((Amezaliwa Mtume)) husimama wote

kwa pamoja wakisema: Roho ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, imehudhuria tunasimama kuitukuza huu ni ujinga, kisha hakika si katika adabu wasimame kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake alikuwa akichukia kusimamiwa, na Maswahaba zake ambao ndio watu wenye kumpenda zaid Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuliko sisi na ndio wenye kumtukuza zaidi walikuwa hawamsimamii; kwa kile kilicho pokelewa kuwa alikuwa akichukia hilo [Ameipokea Tirmidh /2754] wakati huo Mtume alikuwa hai je kwa sasa vipi na hali ya kuwa Alisha fariki? Bidaa hii ilipatikana baada ya kupita Karne tatu zilizo bora, na yakapatikana mambo mengine ya uovu yanayo ambatana na hiyo Maulid ambayo yanaharibu asili ya dini, achilia mbali yale yanayo tokea katika kuchanganyikana Wanaume na Wanawake, na mambo mengine katika mambo maovu.

****

**Swali la 90: Ni ipi hukumu ya kusherehekea ile wanayo ita Sikukuu ya Mama?**

**Jibu:** Hakika kila Sikukuu ambayo inakwenda kinyume na Sikukuu za Kisheria zote hizo ni Sikukuu za uzushi zilizo zuliwa, na wala hazikuwa zikijulikana wakati wa Wema walio tangulia

Mwenyezi Mungu awarehemu, na huenda zikawa zimeanzishwa na wasio kuwa Waislamu, zinakuwa ni bidaa lakini pia ni kujifananisha na maadui wa Mwenyezi Mungu, na Sikukuu za Kisheria zinajulikana kwa Waislamu wote; nazo ni Idd Al-Fitir, Idd Al-Adhuha, na Idd ya kila wiki nayo ni siku ya Ijumaa, hakuna katika Uislamu Sikukuu zisizo kuwa hizo tatu, na kila Sikukuu zilizo zuliwa zisizo kuwa hizo hakika hizo ni zenye kurudishwa kwa aliye zizua na zinakuwa ni batili katika sharia ya Kiislamu, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Mwenye kuzua katika jambo letu hili kitu ambacho hakipo basi kitu hicho ni chenye kurudishwa**)) [Ameipokea Bukhar /2697/ na Muslimu /1718/] maana yake kinarudishwa kwake si chenye kukubaliwa mbele ya Mwenyezi Mungu, na katika mapokezi mengine: ((**Mwenye kufanya jambo halipo katika dini yetu basi jambo hilo ni lenye kurudishwa**)), [Ameipokea Muslimu /1718/].

Na litakapo kuwa lipo wazi hilo hakika haifai katika Sikukuu ambayo imetajwa na mwenye kuuliza inayoitwa (Sikukuu ya Mama) haifai kudhihirisha kitu katika vitu vinavyo dhihirishwa katika Sikukuu za Kisheria; kama vile kudhihirisha furaha,na kupeana zawadi na vitu vingine vinavyo fanana na hivyo, kilicho cha lazima kwa Muislam ni kujifaharisha kwa dini yake na kisha atosheke kwa kile alicho pewa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake katika dini hii Tukufu ambayo ameiridha Mwenyezi Mungu kwa waja wake asizidishwa kitu humo wala asipunguze.

Na kitu kingine ambacho anatakiwa Muislamu kuwa nacho pia asiwe mfuataji tu anafuata kila mlio, bali inatakiwa atengeneze utu wake kwa mujibu wa sheria za Mwenyezi Mungu mpaka awe ni mwenye kufuatwa si mwenye kufuata, na mpaka awe ni kiigizo chema na sio mwenye kuharibu jamii; kwa sababu sheria ya Mwenyezi Mungu imekamilika katika Nyanja zote kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Leo nimekukamilishieni dini yenu na nimekutimizieni neema zangu na nimekupendeleeni Uislamu uwe ndiyo dini yenu**], [Suratul Maida: 3].

Mama ana haki zaidi kuliko kufanyiwa sherehe siku moja kwa mwaka, bali Mama ana haki kwa watoto wake wamchunge na wamsaidie kwa kila usaidizi unao takiwa, na wamtii katika yale ambayo sio ya kumuasi Mwenyezi Mungu katika kila wakati na kila sehemu.

****

**Swali la 91: Ni ipi hukumu ya kusherehekea Sikukuu ya kuzaliwa watoto au Sikukuu ya kuowana?**

**Jibu:** Hakuna katika Uislamu Sikukuu isipokuwa siku ya Ijumaa Idd ya kila wiki, na Sikukuu ya siku ya kwanza katika mwezi wa Shawali Idd Al-Fitr, na siku ya kumi katika mwezi wa Dhul-Hijja Idd Al-Adh'ha, na inaweza kuitwa siku ya Arafa ni Idd kwa watu walio katika viwanja hivyo na siku tatu baada ya Idd Al-Adh'ha nazo ni Sikukuu zikiifuata Idd Al- Adh'ha.

Ama Sikukuu za kuzaliwa mtu au watoto, au siku walio oana na mfano wa hayo zote hizo hazipo katika Sheria nazo ni katika uzushi, zipo karibu sana na uzushi kuliko uhalali wake.

****

**Swali la 92: Mtu ameishi katika nyumba akapatwa na maradhi na yakamzidia matatizo mpaka ikapelekea yeye na familia yake kusema kuwa nyumba hii ina mkosi kwa sababu ya matatizo yaliyo wapata je inafaa kuihama hiyo nyumba kwa sababu hiyo?**

**Jibu:** Huenda ikawa katika baadhi ya majumba, au baadhi ya vipandwa, au baadhi ya wanawake wakawa na mikosi anayo ijalia Mwenyezi Mungu kwa hekma zake, na kinaambatana hicho kitu na; ima madhara, au kukosa manufaa fulani au mfano wa hayo, kwa hiyo inapo tokea hivyo hakuna ubaya kuiuza nyumba hiyo na kuhama kwenda katika nyumba nyingine huenda Mwenyezi Mungu akajaalia kheri katika hiyo nyingine atakayo hamia, hakika imepokewa kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema: ((**Mikosi ipo katika sehemu tatu:Nyumba, Mwanamke, na Farasi**)), [Ameipokea Bukhar /2857/ na Muslimu /2225], baadhi ya vipandwa vinakuwa na mikosi, na baadhi ya Wanawake wanakuwa na mikosi, na baadhi ya Majumba yanakuwa na mikosi, atakapo ona Mwanadamu hilo ajue kwamba hiyo ni katika makadirio ya Mwenyezi Mungu na kwamba Mwenyezi Mungu kwa hekima zake amekadiria hivyo; Basi ahame aende sehemu nyingine, Mwenyezi Mungu ndiye mjuzi zaidi.

****

**Swali la 93: Ni ipi hukumu ya Tawasuli?**

**Jibu:** Hili ni swali muhimu sana, ninapenda kurefusha kidogo majibu yake na ninasema:

**Tawasuli**: Ni mtu kufanya njia itakayo mfikisha katika makusudio yake, asili yake ni kutafuta kufikia katika lengo linalo kusudiwa.

Tawasuli imegawanyika katika vigawanyo viwili:

**Cha kwanza**: Tawasuli iliyo sahihi nayo ni: kufanya Tawasuli kwa njia zilizo sahihi zenye kufikisha katika kinacho tafutwa nayo ipo katika aina tofauti tofauti tutaje baadhi yake:

**Aina ya kwanza:** Kufanya Tawasuli kwa majina ya Mwenyezi Mungu na hiyo ipo katika namna mbili:

**1-**Iwe hiyo Tawasuli ni katika njia ya kiujumla sio kwa jina maalumu na mfano wake kama ilivyo kuja katika Hadithi ya Abdullah Ibnu Masuod Mwenyezi Mungu awe radhi naye katika dua yake amesema: ((**Ewe Mola hakika mimi ni mja wako, mtoto wa mja wako mtoto wa kijakazi wako, uso wangu upo katika mikono Yako, pitisha kwangu hukumu yako, nifanyie uadilifu Wako, ninakuomba Ewe Mwenyezi Mungu kwa jina ambalo ni lako umeita kwa jina hilo nafsi Yako, au umeliteremsha katika Kitabu chako, au umemfundisha yeyote katika viumbe wako, au umelifanya ni maalumu kwako katika elimu ya ghaibu ulokuwa nayo**…)). [Umetangulia upokezi wake], hapa amefanya Tawasuli kwa majina ya Mwenyezi Mungu kwa ujumla pale alipo sema: ((**ninakuomba Ewe Mwenyezi Mungu kwa**

**jina ambalo ni lako umeita kwa jina hilo nafsi Yako)).**

**2-**Iwe hiyo Tawasuli katika njia maalumu, nayo ni kufanya Mwanadamu Tawasuli kwa jina maalumu kwa haja maalumu inayo nasibiana na jina hilo, mfano kama ilivyo kuja katika Hadithi ya Abubakari Mwenyezi Mungu awe radhi naye wakati alipo taka kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake: dua atakayo iomba katika swala yake akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Sema Ewe Mola wangu hakika mimi nimeidhulumu nafsi yangu dhulma ambayo ni kubwa mno, na hakuna wa kunisamehe makosa yangu isipokuwa Wewe, nisamehe mimi msamaha utokao kwako, na unihurumie mimi hakika Wewe ni mwingi wa kusamehe na ni mwingi wa huruma**)) [Ameipokea Bukhar /834/, na Muslimu /2705/].

Ametaka kusamehewa na kuhurumiwa, na amefanya Tawasuli kwa Mwenyezi Mungu kwa kutumia majina mawili katika majina ya Mwenyezi Mungu yenye kunasibiana na Maombi yake nayo ni ((Al-Ghafuur na Al-Rahiim)).

Aina hii ya Tawasuli inaingia katika maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri basi muombeni kwa majina hayo**] [Suratul A'raaf: 180]; hakika maana ya dua hapa inakusanya dua ya kuomba na dua ya Ibada.

**Aina ya pili:** Kufanya Tawasuli kwa Mwenyezi Mungu kwa sifa zake, nayo pia ni kama kufanya Tawasuli kwa majina yake imegawanyika katika sehemu mbili:

**1**-Iwe hiyo Tawasuli ni yenye kuenea kama vile ukisema: ((Ewe Mwenyezi Mungu nakuomba kwa majina yako mazuri na kwa sifa zako zilizo juu)) kisha unataja kile unacho taka.

**2**-Iwe hiyo Tawasuli ni maalumu, kama vile kutawasali kwa Mwenyezi Mungu kwa sifa maalumu ambayo inaendana na matakwa yako, mfano wa hilo ni kama ilivyo kuja katika Hadithi**: ((Ewe Mola kwa kujua kwako mambo ya ghaibu, na kwa uwezo wako kwa viumbe, nibakishe kuwa hai muda wa kwamba unajua kuwa kwangu uhai ni bora kwangu, na unifishe muda wa kwamba unajua kufa kwangu ni bora kwangu**)), [Ameipokea Nasaai /1305/], hapa amefanya Tawasuli kwa Mwenyezi Mungu kwa sifa (Al-Elimu na Al-Qudra) nazo ni sifa zinazo nasibiana na kinacho takiwa.

Na katika hilo anaweza kutawasali kwa sifa ya kivitendo mfano: Ewe Mola Mteremshie Rehema Mohammad na watu wa Mohammad, kama ulivyo teremsha kwa Ibrahiim na watu wa Ibrahi.

**Aina ya tatu:** Atawasal Mwanadamu kwa Mwenyezi Mungu kwa kule kumuamini kwake Mwenyezi Mungu na Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake aseme: ((Ewe Mwenyezi Mungu

Mola wangu nimekuamini wewe, na nimemuamini mtume wako rehma na amani ziwe juu yake basi nisamehe mimi)) au asema: ((Ewe Mola wangu kwa kule kukuamini kwangu wewe na Mtume wako rehma na amani ziwe juu yake ninakuomba kitu flani na flani, na miongoni mwake ni maneno yake Mwenyezi Mungu alipo sema: [**Hakika katika kuumba mbingu na ardhi na kukhitalifiana usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili** 190. **Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala**] mpaka katika maneno yake: [**Mola wetu Mlezi! Hakika unaye mtia Motoni umemhizi; na walio dhulumu hawana wasaidizi** 192. **Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tumemsikia mwenye kuita akiitia katika Imani kwamba: Muaminini Mola wenu Mlezi, nasi tukaamini. Basi tusamehe madhambi yetu, na utufutie makosa yetu, na utufishe pamoja na watu wema** 194] [Suratul Al-Imran].

Katika Aya hii hawa watu walitawasali kwa Mwenyezi Mungu kwa kule kumuamini kwao Mwenyezi Mungu awasamehe madhambi yao, na awafutie makosa yao na awafufue pamoja na watu wema.

**Aina ya nne:** Atawasali Mwanadamu kwa Mwenyezi Mungu kwa matendo yake mazuri, na katika hilo ni kisa cha watu watatu ambao waliingia katika pango ili walale humo pangoni likajifunika kwa jiwe pale mlangoni sehemu ya kutokea na hawakuweza kulitoa, akatawasali kila mmoja katika wao kwa Mwenyezi Mungu kwa matendo mazuri aliyo yafanya, mmoja wao alitawasali kwa Mwenyezi Mungu kwa wema wake alio ufanya kwa wazazi

wake, na wapili kwa kujizuiya kwake na zinaa, na watatu kwa kutekeleza ahadi yake kwa wafanya kazi wake, akasema kila moja katika wao: ((Ewe Mola wangu ikiwa nilifanya vile kwa ajili yako basi tufanyie wepesi katika hili lililo tupata)) likaondoka jiwe [Ameipokea Bukhar 2215/, na Muslimu /2743/], hii ni Tawasuli kwa Mwenyezi Mungu kwa matendo mema.

**Aina ya tano:** Atawasli kwa Mwenyezi Mungu kwa kutaja hali yake, ina maana muombaji atawasali kwa Mwenyezi Mungu kwa kutaja hali yake na lile alilo kuwa nalo katika haja, na miongoni mwa hilo ni maneno ya Musa rehema na amani ziwe juu yake: [**Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ni mhitaji wa kheri utakayo niteremshia**], [Suratul Qaswas: 24], ametawasali kwa Mwenyezi Mungu kwa kutaja hali yake amteremshie kheri, na hilo linakaribiana na maneno ya zakaria rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: [**Akasema: Mola wangu mlezi! Mifupa yangu imedhoofika, na kichwa kinameremeta kwa mvi, wala Mola wangu Mlezi sikuwa mwenye bahati mbaya kwa kukuomba Wewe**] [Surat Maram: 4].

Aina hizi zote za Tawasuli zinafaa, kwa sababu ni sababu nzuri zinazo mpelekea mtu kwenye kupata anacho kikusudia.

**Aina ya sita:** Kutawasuli kwa Mwenyezi Mungu kwa dua ya Mtu mwema ambaye hutarajiwa dua yake itajibiwa, hakika Maswahaba walikuwa wanamuomba Mtume rehma na amani ziwe juu yake awaombee kwa Mwenyezi Mungu kwa dua ya pamoja, na

kwa dua maalumu, na katika ((Sahihi mbili)) kutoka katika Hadithi ya Anas Ibnu Maaliki Mwenyezi Mungu awe radhi naye kuwa Mtu mmoja aliingia Msikitini siku ya Ijumaa na Mtume rehma na amani ziwe juu yake akiwa anakhutubu akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu zimeangamia mali na njia zimekatika muombo Mwenyezi Mungu atuletee mvua, akanyanyua Mtume rehma na amani ziwe juu yake mikono yake akasema: ((**Ewe Mola wetu tuteremshie mvua**)), mara tatu hakushuka Mtume rehma na amani ziwe juu yake katika Minmbari yake isipokuwa matone ya Mvua alikuwa yakichirizika katika ndevu zake, ikaendelea mvua wiki nzima; na katika Ijumaa nyingine akaja yule Mtu au mwingine na Mtume rehma na amani ziwe juu yake akiwa anakhutubu akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu malizetu zimezama katika maji na majengo yamebomoka muombe Mwenyezi Mungu atuzuilie mvua; akainua Mtume rehma na amani ziwe juu yake mikono na akasema: ((**Ewe Mola tufanyie iwe ni yenye manufaa kwetu na sio yenye madhara kwetu**)), akiwa anaashiria upande wa mbinguni ikaondoka ile hali, mpaka watu wakatoka wakawa wanatembea katika jua [Ameipokea Bukhar, /933/ na Muslimu /897]. Kuna matukio mengi ambayo Maswahaba walimuomba Mtume rehma na amani ziwe juu yake Awaombee kwa Mwenyezi Mungu katika mambo maalumu, na katika hilo hakika Mtume rehma na amani ziwe juu yake alitaja kuwa katika Ummah wake kuna watu elfu sabini wataingia peponi bila kuhesabiwa wala adhabu, nao ni wale ambao hawafanyi Ruqiya isio kuwa ya Kisheria, wala hawaitibu mili yao kwa kuchoma sehemu yenye maradhi, na wala hawakadarii mikosi kwa kuona kitu Flani, na kwa Mola wao wanategemea, akasimama Ukasha Ibnu Muhasi akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu muombe Mwenyezi Mungu anijalie niwe katika hao akasema: ((**Wewe ni katika hao**)).

Hii pia ni katika Tawasuli inayo faa, nayo ni kutaka Mwanadamu kwa Mtu mwingine ambaye anatarajiwa kujibiwa dua zake amuombee kwa Mwenyezi Mungu, isipokuwa kitu ambacho kinahitajika, Awe mwenye kuomba anataka kwa dua hiyo manufaa katika nafsi yake na manufaa kwa ndugu yake ambaye ametaka amuombee dua, ili isije kuwa aliiombea nafsi yake tu; kwa sababu unapo taka kumunufaisha ndugu yako na kuinufaisha nafsi yako inakuwa hapo umemfanyia wema, kwani Mwanadamu anapo muombea ndugu yake katika moyo wake husema Mfalme wa Wafalme: ((**Nimeikubali na wewe una mfano wa ulicho muombea ndugu yako**)), na yeye wakati kwa dua hiyo anakuwa ni katika walofanya wema, na Mwenyezi Mungu anawapenda wenye kufanya wema.

**Kigawanyo cha pili**: Tawasuli isio kuwa sahihi, nayo ni:

Ni Mwanadamu kufanya Tawasuli kwa Mwenyezi Mungu kwa njia ambayo sio sahihi, ina maana Kwa njia ambayo haikuthibiti katika sheria kuwa ni njia ya Tawasuli, kwa sababu kufanya Tawasuli kwa njia hiyo ni katika upuzi na ni batili inayo kwenda kinyume na akili pamoja na Ushahidi; na miongoni mwa hizo atawasali Mwanadamu kwa Mwenyezi Mungu kwa dua ya maiti amtake huyu maiti, amuombee kwa Mwenyezi Mungu; kwa sababu hii sio njia sahihi iliyo thibiti Kisheria, bali ni katika ujinga wa Mwanadamu kumtaka maiti amuombee kwa Mwenyezi Mungu; kwa sababu maiti itakapo kufa mambo yake yote yamekatika, na wala haiwezekani kwa yeyote kumuomba baada ya kufa kwake, Hata Mtume rehma na amani ziwe juu yake haiwezekani kumuom-

bea yeyote baada ya kufa kwake, kwa sababu hiyo Maswahaba hawakufanya Tawasuli kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake baada ya kufa kwake, hakika watu wakati walipo patwa na ukame katika zama za Omar Mwenyezi Mungu awe radhi naye alisema: **((Ewe Mola wetu Mlezi hakika sisi tulikuwa tunatawasali kwako kwa kupitia Mtume wetu kisha unatuletea mvua, na hakika kwa sasa tunatawasali kwako kwa Ami ya Mtume wetu(rehma na amani ziwe juu yake:) basi tuteremshie mvua))** [Amepokea Bukhar /1010]. Akasimama Abas Mwenyezi Mungu awe radhi naye akamuomba Mwenyezi Mungu.

Lau kama kutaka dua kwa maiti inafaa na ni njia sahihi angelikuwa Omar na waliokuwa pamoja naye katika Maswahaba wakilitaka hilo kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa sababu kujibiwa dua ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kupo karibu zaidi kuliko kujibiwa dua ya Abas radhi ya Mwenyezi Mungu iwe pamoja naye

Kitu cha muhimu, kufanya Tawasuli kwa kutaka dua kwa maiti hiyo ni Tawasuli batili si halali na haifai kabisa.

Na miongoni mwa Tawasuli ambayo sio sahihi: Ni mtu kutawasali kwa Jaha ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na hilo ni kwa sababu Jaha ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake si yenye faida kwa muombaji kwa sababu haimfaidishi mtu isipokuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, ama kwa mwenye kuomba si yenye faida kwake, na hakika imetangulia kuwa Tawasuli ni kufanya njia nzuri ambayo inanufaisha, ni ipi faida yako wewe kule kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake mbele ya

Mwenyezi Mungu ana Jaha?! Ukitaka kufanya Tawasuli kwa njia ambayo ni sahihi basi sema: Ewe Mola wangu Mlezi kwa kukuamini wewe na Mtume wako, au kwa kumpenda kwangu Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na yanayo fanana na hayo hakika hiyo ndiyo Tawasuli iliyo sahihi yenye kunufaisha.

****

### Swali la 94: Ni nini Al-Walaa  Wal-Baraa?

**Jibu:** Al-Walaa  Wal-Baraa kwa Mwenyezi Mungu ni: kuwa mbali Mwanadamu na kila kitu ambacho Mwenyezi Mungu amekuwa mbali nacho kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Hakika nyinyi mna mfano mzuri kwenu kwa Ibrahimu na wale walio kuwa pamoja naye, walipo waambia watu wao: Hakika sisi tumejitenga nanyi na hayo mnayo yaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu. Tunakukataeni na umekwisha dhihiri uadui na chuki baina yetu na nyinyi mpaka  mtakapo muamini Mwenyezi Mungu peke yake**] [Suratul Mumtahina: 4], na ni  hii pamoja na Washirikina kama alivyo sema Mwenyezi Mungu:  [**Na ni tangazo kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa wote siku ya Hija Kubwa kwamba Mwenyezi Mungu na Mtume wake wako mbali na Washirikina**]

[Suratu Tauba: 3], ni lazima kwa kila Muumini kujiweka mbali na kila Mshirikina na Kafiri.

Na vile vile ni lazima kwa kila Muislamu kujiweka mbali na kila kitendo ambacho hakimridhishi Mwenyezi Mungu na Mtume wake hata kama hakita kuwa ni ukafiri, kama vile maovu na maaswi kama alivyo sema Mwenyezi Mungu**: [Lakini Mwenyezi Mungu amekupendezeeni Imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na amekufanyieni muuchukie ukafiri,na upotevu, na uasi. Hao ndio walio ongoka],** [Suratul Hujuraati: 7].

Pindi itakapo kuwa Muumini ana Imani na ana Maasia,tutampenda kwa Imani yake na tutamchukia kwa maasia yake, na hivyo ndivyo ilivyo katika maisha yetu, hakika unaweza ukachukua dawa yenye ladha mbaya lakini pamoja na kuichukia ladha yake mbaya hiyo unaipenda kwa sababu ina ponyo kwa maradhi yanayo kusumbua.

Kuna baadhi ya watu humchukia Muumini ambaye ni muasi kuliko anavyo mchukia kafiri, na hii ni katika ajabu, nayo ni kuigeuza uhalisia,

Kwa sababu kafiri ni adui wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake ni lazima kwetu tumchukie kwa mwiyo yetu yote amesema Mwenyezi Mungu**: [Enyi mlio amini! Msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa marafiki mkiwapa mapenzi, na hali wao wamekwisha ikataa haki iliyo kujieni wakamfukuza Mtume na nyinyi kwa sababu mnamua-**

**mini Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wenu.Mnapo toka kwa ajili ya jihadi katika njia yangu na kutafuta radhi zangu, mnafanya urafiki nao kwa siri, na Mimi najua mnayo yaficha na mnayo yadhihirisha. Na mwenye kufanya hayo kati yenu basi amepotea njia ya sawa]** [Suratul Mumtahina: 1]. Na amesema tena Mwenyezi Mungu**: [Enyi mlio amini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao. Na mwenye kufanya nao urafiki miongoni mwenu basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoizi watu wenye kudhulumu],** [Suratul Maida: 51]. Na hawa makafiri hawata ridhika na wewe mpaka ufuate mila yao na uiunge mkono dini yao amesema Mwenyezi Mungu**: [Mayahudi hawatakuwa radhi na wewe,wala Wakristo,mpaka ufuate mila zao],** [Suratul Baqar: 120], amesema tena Mwenyezi Mungu**: [Wengi miongoni mwa watu wa Kitabu wanatamani lau wenge kurudisheni nyinyi muwe makafiri baada ya kuamini kwenu],** [Suratul Baqar: 109], na hizi ni katika aina zote za Ukafi: uwe wa Kupinga, au Kukadhibisha, au Kushirikisha na nyinginezo.

Ama katika vitendo tunajiweka mbali na kila kitendo cha haramu, wala haifai kwetu sisi kufanya vitendo vya haramu wala kuvichukua, na Muumini mwenye kuasi tunakuwa mbali naye katika uasi wake, lakini tutakuwa naye na tutampenda kwa kiasi cha Imani alio kuwa nayo.

****

**Swali la 95: Ni ipi hukumu ya kusafiri kwenda katika miji ya kikafiri? Na ni ipi hukumu ya kusafiri kwa ajili ya kutalii?**

**Jibu:** Kusafiri kwenda katika miji ya kikafiri haifai isipokuwa kwa sharti tatu:

**1**-Awe mwenye kusafiri ana elimua ambayo ataweza kuondoa kwayo mambo ya Shubha.

**2**-Awe mwenye kusafiri ameshikamana na dini kisawasawa itakayo mzuiya na matamania.

**3-**Awe ni mwenye haja katika mji huo anao kusudia kwenda.

Ikiwa hazita timia sharti hizi basi itakuwa haifai kusafiri kwenda katika miji ya kikafiri kwa sababu ya fitna au kuogopea fitna inayo weza kutokea, lakini pia kuna kupoteza mali; kwa sababu Mwanadamu anatoa sana katika safari hizo.

Ama atakapo lazimika kwenda kwa sababu ya matibabu au ku-

soma elimu ambayo haipatikani katika nchi yake na akawa ana elimu na dini kama tulivyo sema huko nyuma basi hakuna ubaya kwake kwenda.

Na ama kusafiri kwa ajili ya kutalii katika nchi za kikafiri hii haina haja kwa sababu anaweza kwenda katika nchi za Kiislamu na akahifadhi familia yake na nembo za Kiislamu, na nchi yetu tunamshukuru Mwenyezi Mungu imekuwa ni nchi ya utalii katika baadhi ya sehemu anaweza kwenda huko na akamaliza likizo yake huko.

****

**Swali la 96: Sheikh: Mtu anafanya kazi na Makafiri ni kitu gani mnamuusia?**

**Jibu:** Tunamsihi huyu mtu ambaye anafanya kazi na Makafiri, atafute kazi nyingine, kwa sababu hakuna yeyote katika maadui wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake wenye uadui mkubwa kuliko wale wenye dini isiyo kuwa ya Kislamu, ikiwa itakuwa ni wepesi kwake kupata kazi nyingine hilo ndio bora, na kama itakuwa ni vigumu basi hapana ubaya kwa sababu yeye yupo katika kazi yake na wao wapo katika kazi yao, lakini kwa sharti isiwe katika moyo

wake mapenzi na kuwapenda na kuwa nao pamoja, na alazimiane na yale yalio kuja katika sheria kwa mfano mambo yanayo ambatana na kutoa salamu na kupokea salamu na mfano wa hayo, na vile vile pia wakifa asifuate majeneza yao wala asihudhuriye, wala asishirikiane nao katika sikukuu zao na wala asiwapongeze katika sikukuu hizo, pamoja na hivyo afanye juhudi kadri ya uwezo wake katika kuwalingania katika Uislamu.

****

**Swali la 97: Ni vipi tutaweza kupata faida katika vitu walivyo kuwa navyo Makafiri bila kuingia katika haramu? Na je Maslah Al-Mursala inaweza kuingia katika hilo?**

**Jibu:** Mambo wanayo yafanya maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui wetu ambao ni makafiri yamegawanyika katika sehemu tatu:

**1**-Ibada.

**2**-Ada au desturi.

**3**-Viwanda na ubunifu .

**Ama katika ibada:** Ni kitu kinajulikana kuwa haifai kwa Muislamu yeyote ajifananishe nao katika Ibada zao, na mwenye kujifananisha nao katika Ibada zao hakika huyo atakuwa yupo katika hatari kubwa ineweza kuwa hiyo ni sababu ya kumpelekea katika ukafiri na kutoka kwake katika Uislamu.

**Ama katika ada au desturi**: Kama vile mavazi na vinginevyo hakika ni haramu kujifananisha nao amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Mwenye kujifananisha na watu flani basi yeye ni katika wao)),** [Ameipokea Abu Daud /4031/].

**Ama katika viwanda na ubunifu**: Vitu ambavyo vina maslahi kwa wote hapana ubaya tujifundishe katika vile walivyo vitengeneza na tupate faida katika vitu hivyo, na hilo si katika kujifananisha nao, lakini ni katika kushirikiana katika vitu vyenye manufaa ambavyo hahesabiwi mwenye kufanya amejifananisha na makafiri.

**Ama maneno ya muulizaji**: ((Je Maslaha Al-Mursala inaweza kuingia katika hilo?)).

**Tunasema**: Hakika Maslaha Al-Mursala haitakikani ifanywe kuwa ni Ushahidi yenye kujitegemea, bali tunasema: Haya ni Maslaha Al-Mursala, ikiwa tutahakikisha kuwa ni Maslaha, na iwapo Sheria itashuhudia kuwa ni sahihi na kukubali, basi itakuwa ni katika Sheria, na kama Sheria itashuhudia kuwa ni baatili basi

itakuwa sio Maslaha Al-Mursala hata kama atadai mwenye kufanya kuwa ni Maslaha Al-Mursala.

Na iwapo itakuwa haipo haku wala kule basi itarudishwa katika asli yake, ikiwa ni katika Ibada basi asili ya Ibada zote ni haramu isipokuwa kwa ushahidi, na iwapo itakuwa si katika Ibada basi asili yake ni halali, na kwa hili inabainika kuwa Maslaha Al-Mursala sio katika ushahidi wenye kujitegemea.

****

**Swali la 98: Ni ipi hukumu ya kuingia wasiokuwa Waislamu katika Jazira Al-Arabiya?**

**Jibu:** Kuingia wasiokuwa Waislamu katika Jazira Al-Arabiya ninaogopea isije kuwa ni katika kumkhalifu Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kwa sababu imesihi kutoka Kwake katika [Sahihi Bukhar] hakika amesema katika maradhi yake: ((**Watoeni washirikina katika Jazira Al-Arabiya** )), [Ameipokea Bukhar /3053/ na Muslimu/1637/, na katika Sahihi Muslimu] amesema: ((**Naapa kwa Mwenyezi Mungu nitawatoa Mayahudi na Manaswara katika Jazira Al-Arabiya mpaka nisibakize humo isipokuwa Muislamu**)), [Ameipokea Muslimu /1767], Lakini ikiwa kuja kwao ni kwa sababu tuna haja nao kiasi kwamba hatukupata Muislamu atakae fanya haja hiyo kwa sharti wasipatiwe

ruhusa ya kuishi moja kwa moja.Tumesema: Inafaa, lakini ikiwa kuja kwao kutasababisha  ufisadi wa Kidini au Akida au Kitabia itakuwa ni haramu; kwa sababu ruhusa ikiambatana na uharibifu inakuwa haramu kama inavyo julikana.

Na katika uharibifu ambao unapatikana katika hilo ni kuogopewa kuangukia watu katika kuwapenda na kuridhika kwa kile walicho kuwa nacho miongoni mwa ukafiri na kuondoka wivu wa Kidini kwa kuchanganyika nao, na kwa Waislamu kuna kheri nyingi tunamshukuru Mwenyezi Mungu na zinatosha. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze na atuafukishe katika haki.

****

**Swali la 99: Sheikh: Baadhi ya watu Wanadai kuwa sababu ya kuchelewa Waislamu katika maendeleo ni kushikamana kwao na Dini yao. Na shubha yao katika hilo. Ni kuwa Wamagharibi walipo amua kuachaana na dini zote na wakajiweka mbali na kila dini matokeo yake wamefika pale walipo fika katika maendeleo, na huenda wakati mwingine wakaitilia nguvu shubha yao hiyo kwa vile walivyo kuwa navyo Wamagharibi miongoni mwa mvua nyingi na mazoa, ni ipi rai yenu ewe Sheikh?**

**Jibu:** Maneno hayo hayawezi kutoka isipokuwa kwa mtu ambaye ni dhaifu wa Imani, au aliyekosa Imani, mjinga wa Taarekhe, asio jua sababu za kunusuriwa, Ummah wa Kiislamu wakati ulipo kuwa umeshikamana na dini yao mwanzo mwa Uislamu ulikuwa na nguvu na uwezo na utawala katika kila nyaja za kimaisha, bali baadhi ya watu husema: hakika Magharibi hawakupata faida walio ipata katika elimu isipokuwa ile walio inakili kutoka kwa Waislamu mwanzo mwa Uislamu, lakini Ummah wa Kiislamu ulirudi yuma sana katika dini yao, na wakazua katika dini ya Mwenyezi Mungu ambayo hayakuwepo kiaqida, kimaneno na kivitendo, hilo likasababisha kuchelewa sana, na kurudi nyuma kukubwa sana, na sisi tunajua kwa hakika kwamba lau kama tutarudi katika yale waliokuwa nayo walio tutangulia, tungekuwa na nguvu na utukufu tungekuwa juu ya watu wote.

Kwa sababu hiyo wakati (Abu Sufiyani) radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake alipo msimulia (Hirakli) vile alivyo Mtume

(rehma na amani ziwe juu yake): na Maswahaba zake wakasema: ((Ikiwa unayo yasema ni kweli basi ipo siku huyo Mtume atavimiliki vyote vilivyo chini ya miguu yangu hii)).

Na alipo toka (Abu Sufiyani) na watu wake aliokuwa nao pale kwa Hirakli Akasema: ((Hakika Abi Kabsha ameamrishwa amri ambayo anaiogopa amri hiyo Mfalme wa Banii Asfar)).

Ama haya yanayo tokea katika Nchi za Kiarabu ya kuwa Makafiri wanaigia kwa sababu ya viwanda na mambo mengine, hakika dini yetu haikatai hilo, na lau kama tutaligeukia hilo kwa machukizo makubwa tutakuwa tumepoteza hili na lile, tutakuwa tumepoteza dini yetu na tumepoteza akhera yetu, na dini ya Kiislamu haipingi maendeleo haya, bali amesema Mwenyezi Mungu**: [Basi waandalieli nguvu kama muwezavyo, kwa Farasi walio fungwa tayari tayari, ili kuwatishia maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu],** [Suratul Anfaal: 60], na amesema tena Mwenyezi Mungu**: [Yeye ndiye aliye idhalilisha ardhi kwa faida yenu, basi tembeeni katika pande zake, na kuleni katika riziki zake],** [Suratul Mulk: 15] amesema tena Mwenyezi Mungu**: [Yeye ndiye aliye kuumbieni vyote vilivyo katika ardhi],** [Surat Baqara: 29]; na Aya nyingine zisizokuwa hizo ambazo zinatangaza matangazo ya wazi kuwa ni juu ya Mwanadamu achume na afanye kazi na anufaike, lakini sio kwa hesabu ya dini, Ummah huu tunao ishi nao ni Ummah wa Kikafiri katika asili, dini yake

ambayo unaidai ni dini ya baatili, dini hiyo na wale wapingaji wote wapo sawa hawana tofauti, Mwenyezi Mungu anasema**: [Na anaye fuata dini isio kuwa ya Uislamu haita kubaliwa kwake],** [Surat Al-Imran: 85].

Japo kuwa Ahalu Kitabi Mayahudi na Manaswara wao wana baadhi ya sifa ambazo wanatofautiana na wengine, lakina kwa akhera wao na wengini ni sawa, na kwa sababu hiyo aliapa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, ya kwamba hatomsikia yeyote katika Umma huu awe Myahudi au Mnaswara kisha asifuate yale aliokuja nayo isipokuwa atakuwa ni katika watu wa motoni, wao ni katika asili ya makafiri, ni sawa sawa wamejinasibisha katika Uyahudi au Unaswara, au hawakujinasibisha sehemu yeyote.

Ama wanayo yapata wao miongoni mwa Mvua na mengineyo,wao huyapata hayo kwa kujaribiwa na kutahiniwa na Mwenyezi Mungu, na mazuri yao yametangulia katika uhai wa kidunia, kama alivyo sema Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kumwambia Omar bin Khatwabi Mwenyezi Mungu awe radhi naye, wakati alipo muona Mtume rehma na amani ziwe juu yake, ameathiriwa katika ubavu wake na mkeka aliokuwa ameulalia, akalia Omar akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu Faaris na Ruum wanaishi katika hali wanayo ishi ya neema, na wewe upo katika hali hii.akasema: **((Ewe Omar hao ni watu ambao mazuri yao yametangulizwa katika uhai wa kidunia, hivi huridhiki wao wawe na dunia na sisi tuwe na akhera)),** [Ameipokea Bukhar /2468/, na Muslimu /1479].

Kisha wao ni mara nyingi tu hujiwa na ukame, matetemeko na vimbunga vyenye kuangamiza na hivyo ni vitu vinajulikana na hutangwazwa wakati wote katika Idhaa, na katika Magazeti na vituo vinginevyo vya matangazo.

Lakini mwenye fikira hizo ambazo amezitaja mulizaji ni kipofo, hakujua hali halisi, na hakujua uhakika wa mambo, na nasaha zangu kwake atubiye kwa Mwenyezi Mungu kutokana na fikra zake hizo kabla mauti hayajamjia, na kisha arudi kwa Mola wake, na kisha ajue kuwa hatuna nguvu sisi, wala utukufu,wala ushindi, isipokuwa tutakapo kuwa tumerudi katika Uislamu kurudi kwa kikweli kweli ambako kutaswadikiswa na maneno yetu na vitendo vyetu, na kisha ajue kuwa haya waliokuwa nayo Makafiri ni baatili sio ya kweli, na kwamba makazi yao ni motoni kama alivyo tuhabarisha hilo Mwenyezi Mungu katika Kitabu chake na kwa ulimi wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na hivi vitu ambavyo Mwenyezi Mungu amewapatia hawa Makafiri miongoni mwa neema hazikuwa hizo isipokuwa ni mtihani kwao na ni kutanguliziwa mazari yao, hii ni katika hekima ya Mwenyezi Mungu kuwa neemesha hawa Makafiri, na wao ni kama nilivyo sema hawakusalimika na majanga ambayo huwapata miongoni mwa Matetemeko, ukame,Vimbunga na Mafuriko na mengene yasio kuwa hayo, ninamuomba Mwenyezi Mungu amuongoze na ampe taufiq yule ambaye ana fikra kama za muulizaji, na amrudishe katika haki, na Mwenyezi Mungu atuoneshe wote haki katika dini yetu

****

**Swali la 100: Wanasema baadhi ya watu ya kwamba Hakika kuwa na maneno yalio sahihi sio jambo la muhimu muda wa kwamba moyo uko salama, ni yapi maelekezo yenu katika hilo?**

**Jibu:** Ikiwa atakusudia kusahihisha maneno kupitia lugha ya kiarabu hilo ni sahihi, hakika hilo sio muhimu kuwa maneno yanakuwa katika lugha ya kiarabu faswaha muda wa kwamba yanaeleweka na maana zake zipo salama.

Ama katika kusahihisha kwake atakapo kusudia kuacha maneno ambayo yanafafanua kuhusu kafiri na ushirikina, basi maneno yake sio sahihi bali kuyasahihisha ni muhimu, na wala haiwezekani tukamuambia mtu azunguze chochote anachotaka kwasababu niya yako ipo sahihi, bali tunasema: Maneno yamedhibitiwa kutokana na yale yaliyokuja katika Sheria ya Kiislamu.

****

**Swali la 101: Ni ipi hukumu ya maneno haya ((Mwenyezi Mungu azidumishe siku zako))?**

**Jibu**: Maneno ((Mwenyezi Mungu azidumishe siku zako)) ni katika kufanya dhulma katika dua; kwa sababu siku kudumu ni katika vitu ambavyo haviwezekani kutokea na maneno hayo yanapingana na maneno ya Mwenyezi Mungu alipo sema**: [Kila kilicho juu yake kitatoweka**. **Atabaki Mola wako Mlezi mwenye utukufu na ukarimu**], [Suratul Rahaman: 26-27]. Na maneno yake Mwenyezi Mungu aliposema**: [Nasi hatukumjalia Mwanadamu yeyote kabla yako kuwa na maisha ya milele. Basi ukifa wewe, wao wataishi milele],** [Suratul Ambiyaa: 34].

****

**Swali la 102: Baadhi ya watu wanapo omba dua huomba kwa Uso wa Mwenyezi Mungu wanasema: Nakuomba kwa Uso wa Mwenyezi Mungu kitu flani na flani ipi hukumu ya maneno haya?**

**Jibu:** Uso wa Mwenyezi Mungu ni mkubwa kwa kuutumia kwake Mwanadamu kuombea kitu katika dunia akafanya kuomba kwake ni kwa Uso wa Mwenyezi Mungu kwa kuujalia kama njia ya kupata yale anayo yakusudia, asifanye yeyote mfano wa maombi hayo; kwa maana kwamba asiseme: (Uso wa Mwenyezi Mungu uwe kwako) au (Ninakuomba kwa Uso wa Mwenyezi Mungu) au yanayo fanana na hayo miongoni mwa maneno haya.

****

**Swali la 103: Ni ipi hukumu ya mwenye kusema (Mwenyezi Mungu akurefushie kubaki kwako katika dunia) au (Mwenyezi Mungu akurefushie umri wako)?.**

**Jibu:** Haitakikani kusema hivyo kwa kuyaacha maneno ni yenye kuenea bila kuyawekea mipika katika kurefushiwa umri, kwa sababu kurefushiwa umri kunaweza kuwa kheri au inaweza kuwa ni shari kwake, hakika watu wabaya ni wale ambao umri wake umerefuka sana na matendo yake yakawa mabaya, na kwa sababu ya hilo lau kama atasema: Mwenyezi Mungu akurefushie katika kubaki kwako katika kumtii yeye na mfano wa maneno hayo; hapana ubaya.

****

**Swali la 104: Ni mara nyingi tunaona katika Ukuta maandishi yameandikwa jina tukufu la ((Mwenyezi Mungu)) na pembeni mwake kumeandikwa jina (Muhammad rehma na amani ziwe juu yake), au tunayakuta hayo kwenye vipande vya Karatasi, au Vitabu au katika Msahafu, Je kuwekwa sehemu hiyo ni sahihi?**

**Jibu:** Kuweka jina la (Mohammad) sehemu hiyo sio sahihi; kwa sababu kufanya hivyo kunamfanya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, ni mshirika wa Mwenyezi Mungu na wamelingana, na kama yeyote ataona maandishi hayo na yeye hawajui hao walio itiwa majina hayo ataamini kwa yakini kabisa wawili hao wapo sawa na wanafanana, ni lazima kuondosha jina la Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na ibaki inaonekana katika maandishi (Mwenyezi Mungu) peke yake, hakika neno hilo ni neno wanalo lisema Masufi na wanalifanya ni badala ya dhikir, wanasema: ((Mwenyezi Mungu Mwenyezi Mungu Mwenyezi Mungu)), na kwa sababu hiyo huondoshwa pia jina hilo, hakuna kuandika ((Mwenyezi Mungu )) wala ((Muhammad)) katika ukuta wala katika makaratasi wala kitu kingine chochote kisicho kuwa vitu hivyo.

****

**Swali la 105: Ni ipi hukumu ya maneno haya: ((Mwenyezi Mungu atauliza kuhusu hali yako))?**

**Jibu:** Maneno haya: ((Mwenyezi Mungu atauliza kuhusu hali yako)) hayafai; kwa sababu yana ashiria kuwa Mwenyezi Mungu hajui baadhi ya mambo kwa hiyo anahitaji kuuliza, na hili ni katika mambo yanayo julikana kuwa na uovu mkubwa, na msemaji katika hali ya kawaida hakusudii hivyo lakini maneno hayo yanaweza kufahamisha maana hiyo, au inaweza kuashiria katika maana hiyo, ikiwa ni hivyo basi kilicho cha lazima ni kuacha neno hilo, na kulibadili kwa kusema: ((Ninamuomba Mwenyezi Mungu akuhifadhi)), au: (( Akufanyie wepesi)) na mfano wa hayo.

****

**Swali la 106: Ni ipi hukumu ya kusema: ((Flani ni marehemu)) au ((Amehama kwenda kwenye rehema za Mwenyezi Mungu))?**

**Jibu:** Kusema ((Flani ni marehemu)) hapana ubaya kwa sababu maneno yao ((Marehemu)) ni katika mlango kwa kutaraji kurehemewa sio katika mlango wa kutoa habari kuwa amerehemewa, na itakapo kuwa ni katika mlango wa kutaraji basi hakuna ubaya.

Ama ((Amehama kwenda kwenye rehema za Mwenyezi Mungu)) na hilo pia inavyo nidhihirikia ni katika mlango wa kutaraji, na sio katika mlango wa kutoa habari; kwa sababu mfano wa maneno haya ni katika mambo ya ghaibu hatuwezi kuyahukumu moja kwa moja, na vile vile haifai kusema: ((Amehama kwenda kwa rafiki wa juu)).

****

**Swali la 107: Ni ipi hukumu ya maneno haya: ((Kwa jina la nchi, kwa jina la Taifa))?**

**Jibu:** Maneno haya ikiwa mwenye kusema anakusudia kwa maneno yake hayo Waarabu au anakusudia watu wa Nchi fulani hakuna ubaya, lakini

ikiwa makusudio yake ni kutaka Baraka na usaidizi basi hiyo ni aina katika aina za ushirikina, na hakika inaweza kuwa ni shirki kubwa kutokana na lile lililo kwenye moyo wa msemaji kwa kukitukuza kile alicho taka usaidizi kwake.

****

**Swali la 108: Ni ipi hukumu ya maneno ya watu wasiokuwa na elimu wanaposema: (Umetuletea Baraka kwetu) (Baraka imetutembelea)?**

**Jibu:** maneno ya watu wasiokuwa na elimu wanaposema: (Umetuletea baraka kwetu) haya hawakusudii kuyanasibisha kwa Mwenyezi Mungu, bali wana kusudia tumepata baraka kwa kuja kwetu (kututembelea), na baraka inafaa kuiegemeza kwa Mwanadamu, amesema Usaidu bin Hudhwair Mwenyezi Mungu awe radhi naye, wakati ilipo shuka Aya ya Tayamamu kwa sababu ya mkufu wa Aisha Mwenyezi Mungu awe radhi naye uliokuwa umempotea amesema: ((**Hii siyo ya kwanza katika baraka zenu enyi watu wa Abubakar**)), [Ameipokea Bukhari /334, na Muslimu /367].

Na kutafuta baraka hakuachi kuwa katika moja ya mambo mawili:

**1**-Iwe kutafuta baraka kwa kutumia jambo la kisheria linalo julikana kwa mfano Qur`an tukufu amesema Mwenyezi Mungu**: {Na hiki ni kitabu tulicho kiteremsha kilicho barikiwa}** (Suratul Al-An'aam: 92) na katika Baraka zake mwenye kuichukua hiyo Qur`an  na akaipigania utapatikana kwake Ufunguzi, na kwa Qur`an hiyo Mwenyezi Mungu ameuokoa Ummah mwingi kutoka kwenye Shirki, na katika baraka zake ni kuwa herufi moja ni kwa mwema kumi, na malipo hayo yanamtumzia Mwanadamu wakati wake na juhudi zake.

**2-** Iwe kutafuta baraka kwa kutumia jambo la hisiya linalo julikana kwa mfano elimu, mtu huyu ana elimu watu huchukua baraka katika Elimu yake na kulingania kwake katika kheri, amesema Usaidu bin Hudhwair ((Hii siyo ya kwanza katika baraka zenu enyi watu wa Abubakar)): hakika Mwenyezi Mungu anaweza akapitisha katika mikono ya baadhi ya watu mambo ya kheri ambayo hayapitishi katika mikono ya watu wengine.

Na kuna baraka za kudhani zilizo batili, mfano ni wanayo yadai waongo wenye kuwahadaa watu kwamba mtu flani ambaye ni maiti kuwa ni Walii na vitu hushuka kwa baraka yake, na vinavyo fanana na hivyo, hizo ni baraka za batili hazia athari yoyote, na anaweza kuwa Sheitwani ana athari katika hilo jambo lakini haihesabiwi kuwa ni athari za hissiya kwa sababu Sheitwani anamtu-

mikia huyu Sheikh inakuwa katika jambo hilo kuna ftina.

*Ama namna ya kujua kuwa hii ni katika baraka za batili au ni katika baraka sahihi:

*Hujulikana hilo kwa hali ya Mtu, ikiwa ni katika Mawalii wa Mwenyezi Mungu wamchao Mwenyezi Mungu wenye kufuata Sunna wenye kujiepusha na bidaa, hakika Mwenyezi Mungu anaweza kujalia katika mikono yake kheri na baraka zisizo patikana kwa watu wengine, ama atakapo kuwa ni mwenye kwenda kinyume na Kitabu na Sunna, na analingania watu katika batili hakika baraka zake ni kudhania na Sheitwani anaweza kuweka msaada katika batili yake.

****

**Swali la 109: Ni ipi hukumu ya maneno yao wanaposema: ((Qadari imeingilia kati)), au ((msaada wa Mwenyezi Mungu umeingilia kati))?**

**Jibu**: Maneno yao: ((Qadari imeingilia kati)) hayafai kwasababu yana maana kuwa Qadari imefanya uadui kwa kujiingiza na kuwa ni kama mwenye kujiingiza katika jambo lisilo muhusu, pamoja na kuwa Qadari ndio asili ni vipi inasemwa kuwa imeingilia katika jambo?! Lakini kilicho sahihi ni kusema: Lakini imeshuka hukumu na Qadari au Qadari imeshinda na mfano wake, na mfano wa hilo ni kusema: ((Msaada wa Mwenyezi Mungu umeingilia kati)) kilicho bora ni kubadili kwa kusema ((Umepatikana msaada wa Mwenyezi Mungu)).

****

**Swali la 110: Tunasikia na Tunasoma neno hili: ((Uhuru wa Kifikra)), Nayo ni kulingania katika Uhuru wa Kiitikadi, Mnasemaje juu ya hilo?**

**Jibu:** Tunasema katika hilo, kuwa yule ambaye anaruhusu Mwanadamu awe na uhuru katika Itikadi, ya kwamba aitakidi anacho kitaka katika dini hakika huyo ni kafiri, kwa sababu kila mwenye kuitakidi kwamba yeyote anaruhusiwa kuwa na dini isiyo kuwa dini ya Muhammad rehma na amani ziwe juu yake hakika huyo amemkufuru Mwenyezi Mungu na anatakiwa kutubia, iwapo atatubia sawa na asipo tubia itawajibika kwake kuuliwa.

Na hizi dini sio fikra, lakini ni Wah'yi kutoka kwa Mwenyezi Mungu aliouteremsha kwa Mitume wake ili waja wake waufuate, na neno hili (Fikra) ambalo hukusudiwa dini ni lazima liondoshwe kwenye Kamusi za Vitabu vya Kiislamu; kwa sababu inapelekea kwenye maana hii mbaya, nayo ni kusemwa Uislamu ni fikra, na Unaswara ni fikra, na Uyahudi ni fikra, hilo linapelekea kuwa hizi Sheria ni fikra tu za hapa ardhini anazichukua anaye zitaka katika watu, na uhakika wa mambo ni kuwa hizi dini za mbinguni ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu anazotakidi Mwanadamu kuwa ni Wahai kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuuabudu kwa Wahai huo ni Ibada, na wala haifai kuuta jina la ((Fikra)).

**Na ufupisho wa jibu hili ni:** Mwenye kuitakidi kwamba inafaa kwa yeyote kuwa na dini anayo itaka na kwamba yeye ni huru kwa kitu anacho taka kuabudu, hakika huyo amemkufuru Mwenyezi Mungu; kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema**: [Na anaye fuata dini isiokuwa Uislamu haitakubaliwa kwake],** [Suratu Al-Imran: 85], na amesema tena Mwenyezi Mungu: [**Bila shaka dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu**], [Suratu Al-Imran: 19], haifai kwa yeyote aitakidi kuwa dini nyingine isiyo kuwa ya Uislamu inaruhusiwa na inafaa kwa Mwanadamu kuabudu kwa dini hiyo, bali atakapo itakidi hivyo hakika Wanavyuoni wameweka wazi kuwa huyo ni kafiri ametoka katika Mila ya Uislamu.

****

**Swali la 111: Je inafaa kwa Mtu kumuambia Mufti ni ipi hukumu ya Uislamu katika jambo flani na flani? au ni ipi Rai ya Uislamu katika jambo flani?**

**Jibu:** Haitakiwi kusema: ((Ni ipi hukumu ya Uislamu katika jambo flani)) Au: ((Ni ipi Rai ya Uislamu katika jambo flani)): kwa sababu anaweza kukosea na haitokuwa hiyo aliyo isema ndiyo hukumu ya Uislamu, lakini kama itakuwa hukumu ni ushahidi wa wazi basi hakuna ubaya, mfano aseme: Ni ipi hukumu ya Uislamu katika kula mzoga? Tunasema: Hukumu ya Uislamu katika kula mzoga ni haramu.

****

**Swali la 112: Ni ipi hukumu ya kusema maneno haya: ((Zama zimetaka litokee jambo flani na flani)), na ((Qadari imetaka itokee kitu fulani na fulani))?**

**Jibu:** Maneno: ((Zama zimetaka litokee jambo fulani na fulani)) na ((Qadari imetaka itokee kitu fulani na fulani)) ni matamko mabaya, kwa sababu zama ni wakati, na wakati hauna matakwa yeyote, na ni hivyo hivyo Qadari haina matakwa yeyote, na hakika

si vingenevyo anaye taka kitu kiwe na kikawa ni Mwenyezi Mungu ndio; lau kama atasema Mwanadamu: ((Imehukumu Qadari ya Mwenyezi Mungu kitu fulani na kitu fulani)), hakuna ubaya kwa maneno hayo.

Ama matakwa haifai kuegemezwa katika Qudra; kwa sababu kutaka ni kupenda, na hakuna kutaka kwa sifa lakini kutaka ni kwa mwenye kusifiwa.

****

**Swali la 113: Ni nini hukumu ya Maneno haya: Fulani ni Shahidi?**

**Jibu**: Jibu la swali hilo ni kwamba, kumtolea ushahidi yeyote kuwa ni shahidi inakuwa katika namna mbili:

**1**-Kuwekewa mipaka kwa sifa maalum mfano kusemwe: Mwenye kuuliwa katika kupigania dini ya Mwenyezi Mungu huyo ni

shahidi, na mwenye kuuliwa akitetea mali yake huyo ni shahidi, na mwenye kufa kwa ugonjwa wa Tauni basi huyo ni shahidi na mfano wa hayo, hiyo inafaa kama ilivyo kuwa katika ushahidi, kwa sababu wewe unashuhudia kwa kitu ambacho amekitolea habari Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na ikiwa shahada ni kwa namna hiyo ni wajibu kukubali lile alilotuhabarisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake.

**2-**Ikiwa shahada itawekewa mipaka kwa mtu maalumu mfano kusemwe kwa mtu maalumu: Hakika huyu ni shahidi, hii haifai isipokuwa kwa yule aliye tajwa na Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kuwa ni shahidi, au Ummah umeafikiana kuwa kwa jambo hilo ni shahidi, hakika Imamu Bukhari ameweka mlango maalumu aliouita: ((Mlango ambao hakusemwi fulani ni shahidi)).

Amesema Al-Haafidhu katika: ((Al-Fat'h)) 6/90: ina maana ((Haifai kusema flani ni shahidi ukiwa na uhakika kabisa wa hilo isipokuwa ikiwa ni kwa njia ya Wah'yi, yani kuna Aya au Hadithi)), ni kama vile ameashiria kwenye Hadithi ya Omar kwamba alihutubia akasema: Mnasema katika kupigana kwenu vita: Fulani ni shahid, na amekufa fulani akiwa shahidi huenda akawa amemtia uzito wa bure mnyama wake, kaeni na kujua, msiseme maneno hayo, lakini semeni kama alivyo sema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((Mwenye kufa katika njia ya Mwenyezi Mungu au akauwawa basi huyo ni shahidi)).

Na hiyo ni Hadithi Hasan Ameitoa Ahmad na Said bin Mansour na wengine wasiokuwa wawili hao katika njia ya Muhammad bin Siirin kutoka kwa Abiy Jafaa kutoka kwa Omar)) yameisha maneno yake.

Kwa sababu kukitolea ushahidi kitu haiwi isipokuwa kwa kuwa na ujuzi na kitu hicho, na katika shrti za kuwa Mtu ni Shahidi ni kuwa alikuwa akipigana ili neno Mwenyezi Mungu liwe juu, nayo ni niya ya ndani hakuna njia ya kuijua, na kwa sababu hiyo amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake akiwa anaashiria katika hilo: ((**Mfano wa mwenye kupigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu Anamjua mwenye kupigana katika njia yake**)), [Ameipokea Bukhar /2787)/, na Muslim /1878].

Na akasema tena: ((**Naapa kwa Yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake, hazungumziwi yeyote katika kupigania njia ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu anamjuwa wa kuzungumziwa katika kupigania njia ya Mwenyezi Munguisipokuwa atakuja siku ya Kiama na mdomo wake unatoka damu, rangi ni rangi ya damu, na harufu yake ni harufu ya Miski**)), [Ameipokea Bukhar /2803/ na Muslimu /1876/].

Hadithi hizo mbili zimepokelewa na Bukhar kutoka katika Hadithi, Abu Hurayra Mwenyezi Mungu awe radhi naye.

Lakini kwa yule Mtu ambaye atakuwa dhahiri yake ni wema hakika sisi tunalitaraji hilo kwake, hatumshuhudilii kwa hilo wala hatumdhanii dhana mbaya, na kutaraji ni daraja kati ya daraja mbili, lakini sisi tutamfanyia katika dunia kwa hukumu zile ambazo hufanyiwa Mashahidi atakapokuwa  ameuliwa katika jihadi atazikwa na damu yake katika nguo zake pasna kuswaliwa, na akiwa ni katikaMashahidi wengine, hakika hao wataoshwa watavishwa sanda na wataswaliwa.

Kwa sababu lau kwamba tutamtolea ushahidi mtu maalumu kuwa ni shahidi italazimu katika hiyo shahada tutoe ushahidi wa pepo, na hilo ni kinyume na walio kuwa nayo Ahalu Sunna, kwa sababu wao walikuwa hawamshuhudilii yeyote kwa pepo isipokuwa yule aliye shuhudiliwa na Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa sifa maalumu au mtu maalum, na watu wengine wamesema inafaa kumsuhudilia kwa hilo kwa yule ambaye Ummah umeafikiana kwa kumsifia juu ya hilo, na katika hili ndio alilokwenda nalo Sheikh Islamu Ibnu Taymiyah Mwenyezi Mungu amrehemu.

Na kwa hili imebainika kuwa haifai kumshuhudilia mtu maalumu kuwa ni Shahidi isipokuwa kwa ushahidi wa Kitabu na Sunna au makubaliono ya Ummah juu ya hilo, lakini yule ambaye dhahiri yake ni wema hakika sisi tunataraji kwake hilo kama ilivyo tangulia, na kumjua zaidi ni kwa Muumba wake Mwenyezi Mungu.

****

**Swali la 114: Ni yapi maoni yenu katika kutumia neno: (Ghafla) au kushitukiza?**

**Jibu:** Maoni yangu kwenye neno hili ni kwamba hakuna ubaya kulitumia, na ni jambo linajulikana, na nina dhani kuna Hadithi imekuja kwa neno hilo, alitushitukiza Mtume rehma na amani ziwe juu yake  lakini hainijii Hadithi maalumu kwa sasa yenye neno hilo.

Na kitu kushtukiza au kutokea kwa ghafla kwa Mwanadamu ni kitu chenye kutokea; kwa sababu Mwanadamu hajui mambo ya ghaibu hakika kinaweza kumtokea kitu ambacho alikuwa hahisi kama kitatokea, na wala hakukuwa na utangulizi unao onesha kuwa kuna kitu flani kitatokea,wala hakuwa akitaraji kuwa kitatokea, kinatokea tu kwa ghafla.

Lakini kwa Mwenyezi Mungu hakuna kitu kinacho tokea kwa njia hiyo, hakika kila kitu kwake Mwenyezi Mungu kinajulikana, na kila kitu kwa Mwenyezi Mungu kinatokea kwakukadiriwa, kwake Mwenyezi Mungu hakitoke kitu kwa njia ya ghafla, lakini kwangu, kwako na kwa mwingine tunakutana na vitu hivyo bila ahadi navyo na bila kuvihisi na bila viashiria vya jambo hilo, hilo kwa mwanadamu huitwa: Ghafla au kushitukiza, na hakuna ubaya

ndani yake, ama katika matendo ya Mwenyezi Mungu hilo ni jambo lisilo wezekana na halifai.

****

**Swali la 115: Sheikh, Mwenyezi Mungu awalipe kheri, Ni yapi mawazo yenu kuhusu istilahi ya fikra ya Kiislamu? Na Mfikiriaji wa Kiislamu?**

**Jibu:** Neno (fikira ya Kiislamu) ni katika maneno ambayo watu hutahadharishwa nayo sana kwa sababu tutakuwa tumeufanya Uislamu kuwa ni mawazo ya watu ambayo mtu anauhuru wa kuyafata uu Kuwacha kuyafata na hili jambo ni hatari kubwa sana, huu msemo kuwa (fikra ya Kiislamu) wameulete maadui wa Uislamu nasi tukiwa hatufahamu.

**Kuhusu:** istalahi ya (Mwislamu mwenye kufikiria) sifahamu kama istilahi hiyo ina ubaya kwasababu ni kumsifu mwislamu wa kiume kuwa anafikiria na mwanaume wa kiislamu lazima afikirie.

****

**Swali la 116: Kuigawa Dini kunako mambo ya muhimu na mambo ya kawaida (mfano kufuga ndevu) hiyo ni sahihi?**

**Jibu**: Kuigawa dini kunako mambo ya muhimu na mambo ya kawaida kugawa hivo ni kosa na ni batili, mambo yote yanayo fungamana na Dini ni ya muhimu, na yote ni yenye manufaa kwa mja, na yote yana muweka karibu na Mwenyezi Mungu na hupata thawabu mtu akifanya jambo la Dini, na yote yanamfaa mtu kwa kuzidisha imani yake na kumuweka karibu na Mwenyezi Mungu, hata mavazi anayo yavaa namuonekano wake, hayo yote akiyafanya binaadamu kwa ajili ya kutafuta radhi ya Mwenyezi Mungu na kufuata Mafundisho ya Mtume wa Mwenyezi Mungu rehma na amani ziwe juu yake, mtu huyo hulipwa thawabu, na mambo ya kawaida kama tunavyojua ni kwamba hayana faida isipokuwa hutupwa, katika dini ya Uislamu na katika sheria ya Uislamu hakuna kitu hicho! Uislamu wote na sheria ya uislamu ni kiini mtu ananufaika nacho kama atafanya hilo jambo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na akafata mafuzo ya Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake, na wale wanao leta hiyo misemo wajifikirie vizuri katika jambo hilo ili wajue ukweli upo wapi na haki ipo wapi, kisha wafate haki na waache hii misemo, ukweli nikuwa dini ya uislamu ina mambo muhimu sana na mambo makubwa, kama nguzo tano za Uislamu amabazo Mtume Muhammad rehma

na amani ziwe juu yake amezifafanunua nguzo hizo, akasema: **((Uislam umejengwa juu ya mambo matano: la kwanza kutamka kwa ulimi na kukiri kwa moyo yakuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja hana mshirika, na kutamaka kwa ulimi na kukiri kwa moyo ya kuwa Muhammadi ni Mtume wake,la pili ni kusimamisha swala na kutoa zakka na kufunga Mwezi mtukufu wa Ramadhani na kwenda kufanya ibadi ya hija Makkah katika nyumba ya Mwenyezi Mungu)),** [7 / Swahihi Bukhary, /16/ Swahihi Muslimu]. Pia kuna mambo mengine yasio kuwa hayo lakini sio kuwa mamabo hayo ni maganda, hayamsaidi binadamu anayatupa na kuyaacha, bila kunufaika nayo.

**kuhusu ndevu**: Hakuna shaka kuwa kuacha ndevu ni ibada kwa sababu Mtume rehama na amani ziwe juu yake! Ameamrisha wanaume wache ndevu, na kila jambo alilo amrisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Ni ibada mtu akiifanya anakuwa karibu na Mwenyezi Mungu, kwa sababu ya kufata amri ya Mtume rahma na amani ziwe juu yake! Na hayo ndio mafunzo alio kuja nayo Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake! Pia ndio mafunzo walio kuja nayo mitume wengine walio kuja kabla ya Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu katika kisa cha Mussa na Haruna**: [Akasema ewe mwana wa mama yangu usinishike ndevu zangu wala kichwa change**], Surat Twaha: 94]. Na imethibiti kwa Mtume Muhammad rehma

na amani ziwe juu yake kuwa kuacha ndevu ni katika maumbile ambayo Mwenyezi Mungu amewaumba wanaadamu hivyo, pia kuacha ndevu ni ibada na sio tamaduni, wala sio maganda kama wanavyo dai baadhi ya watu.

****

**Swali la 117: Ni ipi hukumu ya kusema tumemzika katika maisha yake ya milele?**

**Jibu**: Mtu yoyote kusema kuwa tumemzikaa katika maisha yake ya milele, ni haramu kusema hivyo na hairuhusiwi kisheria kwasababu ukisema tumemzika katika maisha yake ya milele, maana yake kuwa kaburi ndio mwisho wa kila kitu, unakuwa umepinga kuwa hakuna kufufuliwa siku ya Qiyama, na hili jambo linajulikana kwa waislamu wote kuwa maisha ya kaburini sio maisha ya mwisho, na sio maisha ya milele, isipokuwa watu ambao hawaamini siku ya Qiyama, (siku ya mwisho) wanaamini kuwa maisha ya kaburini ndio maisha ya milele na ya mwisho, kuna muarabu mmoja alimsikia mwanaume mmoja anasoma maneno ya Mwenyezi Mungu Qur`ani: **[kumekushugulisheni kutafuta wingi, mpaka mje makaburini!**], [Surat Takathur: 1-2]. Akasema yule Mwarabu: ((**Naapa kwajina la Mwenyezi Mungu mtu alie kwenda kutembea sehemu hua haishi sehemu hiyo**)), anaetembea sehemu huondoka, ni lazima ya kuwa watu watafufuliwa siku ya Qiyama, (Siku ya mwisho)

kwa hivyo ni lazima kujiepusha kutumia lugha hiyo ya kuwa tumemzika hayo ndio maisha yake ya milele kwa sababu maisha ya mwisho ni mtu kuingia Peponi au kuingia motoni siku ya Qiyama, (siku ya mwisho).

****

## Swali la 118: Wakiristo kujiita kuwa ni wafuasi wa Yesu, na Yesu kuwa ni mkiristo, je ni sahihi?

**Jibu:** Hakuna shaka ya kuwa Wakiristo kujiita kuwa ni wafuasi wa Yesu baada ya kuja Mtume Muhammad rahma na amani ziwe juu yake na kujinasibisha kuwa wao ni wafuasi wa yesu sio sahihi, kama wangekuwa sahihi wange muamini Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake! Kwa kuwa kumuuamni Mtume Muhammad rahma na amani ziwe juu yake, ni kumuamini Issa bin Mariam rehma na amani ziwee juu yao! Amesema Mwenyezi Mungu mtukufu katika Qur`ani: [**Na Issa bin Mariyamu alipo sema: Enyi wana wa Israil! Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, ninae thibitisha yalio kuwa kbala yangu katika taurati na mwenye kubashiria kwa Mtume Atakae kuja baada yangu:jina lake ni Ahmad! Lakini alipo waletea hoja zilizo wazi walisema huu niuchawi ulio wazi], [**Surat Swaff: 6]. Hakubashiri Issa bin Mariyamu ya kuwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake! Ni kwa ajili watu wafate mafundisho alio kuja nayo

Muhammad, kubashiriwa Muhammad haya kuwa maneno ya upuuzi kutoka kwa Issa bin Mariam haiwezekani akabashiriwa mtu mwenye akili mbovu, Issa bin Mariyamu ni katika Mtume watano wakubwa alio wachagua Mwenyezi Mungu, naye Issa bin Mariam amewabashiria wana wa Israil kuWa huyo atakae kuja baada yangu ni Muhammad: **[Lakini alipo waletea hoja zilizo wazi walisema huu niuchawi ulio wazi],** kwa mujibu wa maneno ya Mwenyezi Mungu inaonyesha kuwa Mtume ambaye alibashiriwa na Issa bin Mariam ameisha kuja lakini walimpinga na wakasema kuwa ni mchawi wa wazi wazi, wakimpinga Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake! Watakuwa wamepinga utumee wa Issa bin Mariam, kwa kuwa Issa bin Mariam ndiye alie toa bishara ya kuja kwa Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake! Kwahiyo haifai kwa Wakiristo kujiita kuwa niwafuasi wa Yesu (Issa bin Mariam) kama ni kweli Wakiristo wanadai kuwa ni wafuwasi wa Yesu, Issa mtoto wa Mariam wange amini alicho kibashiri Issa bin Mariam, kwa kuwa Issa bin Mariam na wengine katika Mitume wa Mwenyezi Mungu amechukuwa ahadai kwao ya kuwa wamuamini Mtume Muhammad rehama na amani ziwe juu yake amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Pindi Mwenyezi Mungu alipo chukuwa ahadi kwa Manabii; kisha akakupeni Kitabu na hekima kisha akakujieni Mtume Mwenyewe kusadikisha mlio kuja nayo nijuu yenu kumuamini na kumsaidia, akasema jee mmekiri na mmekubali kushika agizo langu juu ya hayo? Wakasema: tumekubali akasema basi shuhudieni namimi ni pamoja nanyi katika kushuhudia**], [Surat Al-Imrani: 81]. Mtume ambae amekuja kuthibisha mamrisho walio kuja nayo Mitume walio tangulia, ni Mtume Muhammadi rehma na amani ziwee juu yake!, Amesema Mwenyezi

Mungu mtukufu katika Qur`ani: **[tumekuteremshia wewe, kwa haki, kitabu hichi kilicho sadikisha yalio kuwa kabla yake katika vitabu na kuyalinda, basi hukumu baina yao kwa aliyo yatelemsha Mwenyezi Mungu, wala usiafuate matanio yao ukaacha haki iliyokujia**], [Surat Maida: 48].

**Kwa kifupi nasema**: Wakiristo kujinasibisha kuwa ni wafwasi wa Issa bin Maraam (yesu) ni kujinasibisha kwa uongo kunako pingana na uhalisia kwa sababu Wakiristo wanapinga bishara aliyoitoa Issa bin Mariam rehma na amani za ziwe juu yake! Ambayo ni bishara ya kuja Mtume Muhammadi, Wakiristo kupinga bishara ya kuja kwa Mtume Muhammad ni kumpiga Yesu mwana wa Mariam.

****

**Swali la 119: Ni yapi mawazo yenu kuhusu neno hili, (La samaha LLah)?**

**Jibu:** Haifai mtu kusema la samaha LLah, kwa kuwa mtuu akisema hivyo huenda akadhaniwa kuwa yupo mtu mmoja anamlazimisha Mwenyezi Mungu kufanya kitu, Anasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Hakuna Mtuu Anauwezo wa kumlazimisha Mwenyezi Mungu**)). Amesema Mtume wa

Mwenyezi Mungu rehma na amani ziwee juu yake**: ((Asiseme mmoja wenu: awe Allah nisamehe ukitaka, Ewee Mwenyezi Mungu nihurumie ukitaka, isipokuwa akusudie kumuomba Mwenyezi Mungu na ajipendekeze kwa Mwenyezi Mungu hakika hakuna wakumuamuru Mwenyezi Mungu wala wakulifanya jambo kuwa kubwa jambo ambalo amelitoa Mwenyezi Mungu)), [6339/** Swahihi Bukhary, / 2679 / Swahihi Muslimu] Ni bora mtu kusema Mwenyezi Mungu hakupanga jambo hilo, (**La Qadara Allah**) kuliko kusema, La samaha Allah, kusema hivyo kuwa Mwenyezi Mungu hakulipanga ni bora kuliko kutuhumu mambo yasio faa kwa Mwenyezi Mungu.

****

**Swali la 120: Kuna baadhi ya watu, anapo fariki mtu, husema: [Ewe nafsi iliyo tua! Rejea kwa Mola wako ukiwa umeridhia na umemridhiwa] [Suratul-Fajir: 28, ni ipi hukumu ya kusema hivyo?.**

**Jibu**: Hairuhusiwi kusema hayo maneno kwa kumuashiria mtu maalum aliyefariki, kwa sababu kusema hivyo utakuwa unatoa ushahidi ya kuwa huyo marehemu anahizo sifa.

****

## MASWALI NA MAJIBU KUHUSU SWALA.

**Swali la 121: Ni ipi asili au chanzo cha kujisafisha kutokana na uchafu kama janaba au kinyesi?**

**Jibu:** Asili ya kujisafisha kwa mtu aliepatwa na uchafu wa hadathi (janaba au hedhi au nifasi) anatakiwa ajitwaharishe kwa kutumia maji yalio safi, na mtu akipatwa na uchafu huo hatokuwa safi hadi atumie maji katika kujisafisha, hata kama maji hayo yatakuwa ni masafi atayatumia hayo maji masafi, au yakiwa maji yamebadirika rangi kwa kuwekewa kitu kilicho safi ndani yake ambacho sio najisi, maji hayo inaruhusiwa kujitwaharisha kwa kutumia hayo maji, kwa kuwa kauli ya Wanawazuoni iliyo na nguvu: kuwa maji yakibadilika kwa kuweka kitu kilicho safi, maji hayo yataendeleaa kuitwa maji na kitu kilicho wekwa katika maji hayo hakita ondoa uhalisia wa maji hayo, hayo maji yatakuwa bado yapo safi unaweza kujisafisha kwa kutumia maji hayo, Au kusafisha maji mengine kwa kutumia maji hayo, kama mtu hato pata maji ya kujitwaharishia (kujisafisha) Au akahofu kuwa akitumia maji atapata madhara ya kiafya au atazidisha tatizo alilo nalo la maradhi, Mtu huyo atajitwaharisha kwa kutumia kutayamam (kutumia mchanga ulio safi) Atapiga mikono yake miwili kwenye mchanga juu ya ar-

dhi kisha atapakaa uso wake kwa kutumia viganja vya mikono yake miwili, kisha atapakaa kwenye mikono yake nyuma ya viganja kiganja cha kulia atapakaa kushoto na cha kushoto atapakaa kiganja cha mkono wa kulia,hii ni kuhusu kujisafisha kutokana na hadathi (Janaba au hedhi au nifasi).

Kujitwaharisha au kujisafisha kwa mtu alie patwa na uchafu wa kinyesi, kujisafisha kwakwe ni kutumia kitu chochote kinacho weza kuondoa huo uchafu ,kama kutumia maji, Au kitu kingine kinacho ondosha hicho kinyesi na sehemu hiyo ikabaki kuwa ni safi kwasababu inakausidiwa kuondosha kinyesi chenyewee, kikiondoka kwa maji au kitu kingine cha asili ya majimaji au kikawa kikavu kikaondosha najisi yote, kufanya hivyo kutakuwa kumesa fisha sehemu hiyo. Isipokuwa kwa mtu alie patwa na kinyesi cha mbwa, Ni lazima aoshe sehemu hiyo mara saba, mara moja kati ya hizo saba achanaganye na mchanaga. Huu ndio Utofauti wa kujitwaharisha na hadathi (janaba nk.) na kutwaharisha sehemu ilo patwa na kinyesi.

****

**Swali la 122: Je sehemu yenye najsi inaweza kusafika bila ya kutumia maji? kemiko zinazo safishia vyakula hivi zina twaharisha vyakula?**

**Jibu:** Kuondoa najsi haikusudiwi kuwa ni ibada, kusafisha sehemu yenye najsi: inakusudiwa kuondoa kiini cha uchafu kitu chochote kitakacho toa uchafu huo sehemu hiyo itabaki kuwa safi, akitumia maji au kitu kingine inazingatiwa kuwa sehemu hiyo imesafika.

Kauli iliyo na nguvu ambayo ameichagua Sheykhul Islamu bun Taymiyah rehma na amani zimuendee, kama sehemu yenye najsi itapatwa na jua au upepo najsi ikaondoka sehemu hiyo itakuwa safi, na itakuwa imetwaharika, kama alivyo sema, Sheykhul Islam bun Taymiyah: Sehemu iliyo patwa na uchafu, sehemu hiyo panakuwa pamenajisika, Na najsi ikiondoka sehemu hiyo inakuwa imetwaharika, kila kitu kinacho ondosha hicho najsi na alama ya najsi hicho- isipokuwa husamehewa ranga ya najsi iliyo shindikana kuondoka- hiyo sehemu itabaki kuwa safi; kwa misingi hiyo kemiko zinazo tumika kusafishia vyakula, vyakula vikisafika vinakuwa twahiri (safi) na kemiko hizo zinakuwa zimesafisha.

****

**Swali la 123: Ni ipi hukumu ya maji yalio badilika rangi kwa sababu ya kukaa muda mrefu?**

**Jibu:** Maji hayo ni safi, hata kama yatabadilika rangi, kwasababu hayakubadilika kwa kuwekewa kitu kingine, yamebadi-

lika kwa kukaa muda mrefu, kwahivyo inaruhusiwa kisheria kutawadha maji hayo na udhu utakuwa ni sahihi.

****

**Swali la 124: Ni ipi hekima ya Mwenyezi Mungu kuharamisha wanaume kuvaa dhahabu?**

**Jibu:** Fahamu ewe ulio uliza swali hili, pia afahamu kila mtu atakae soma swali hili na maJibu haya, kuwa sababu ya sheria za Mwenyezi Mungu kwa kila muumini, ni maneno ya Mwenyezi Mungu na maneno ya Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake! Amesema Mwenyezi mung: [**Haiwezekani kwa Muumini Mwanamume wala Muumini Mwanamke kuwa na khiyari katika jambo Mwenyezi Mungu na Mtume wanapo kata shauri katika jambo hilo**], [Surat Ahzab: 36].

Mtu yeyote atakaye tuliza swali kuhusu ulazima wa kufanya jambo au uharamu wa kuwacha kufanya jambo, ambalo hukumu yake imeelezwa katika kitabu cha Mwenyezi Mungu Qur`an, au katika hadithi, za Mtume Muhammad rehma na

amani ziwe juu yake! Tuna mJibu mtu huyo kwa sababu ya kuwa jambo ni lazima mtu kufanya au niharamu mtu kufanya kitu hicho, sababu ni maelezo ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na hii ni sababu tosha kwakila Muumin, kwasababu hiyo alivyo ulizwa Aisha Mke wa Mtume radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, kwanini wanawake wenye hedhi wakimaliza siku zao za hedhi wanalipa madeni ya swaumu ya mwezi wa Ramadhani? Na hawaliipi swala ambazo hawakuziswali walivyo kuwa na hedhi? AliJibu mke wa Mtume hivi: ((Tulikuwa **tukiwa katika hali ya hedhi, tunaamrishwa tulipe swaumu, na hatukuwamrishwa kulipa swala)),** [321/ Swahihi Bukhar, /335/ Sahihi Muslimu], kwa kuwa mamrisho yametoka kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hiyo ni sababu ya lazima kwa kila Muumin, lakini hakuna ubaya kama mtu atataka kujua sababu, Au akataka kujua hekma, katika mambo alio yahukumu Mwenyezi Mungu, kwa sababu kufanya hivyo kutamzidishia utulivu, pia atapata kujua kiini cha sheria ili apate kulinganisha hukumu za Mwenyezi Mungu na sababu zake, pia ataweze kuoanisha mambo ambayo yalio elekezwa na Mwenyezi Mungu kwa matamshi na mambo ambayo hakuyaeleza, kujifunza hekma ya sheriya ya Mwenyezi Mungu kuna faida tatu.

**Majibu ya swali**: **((Imethibiti kwa Mtume rehma na amani juu yake, amerahamisha kuvaa dhahabu kwa wanaume, na ameruhusu wanawake wavae dhahabu**)), [1720/ Al Tirmidhiy! /5148/ Nasaai] Kwa kuwa dhahabu ni katika vitu vyenye thamani anavyo jipamba mwanaadamu, dhahabu ni mapambo, na Mwanaume maumbile yake sio ya kujipamba, Mwanaume aliyekamili sio katika mapambo anakuwa kamili katika uanaume wake, na Mwanaume hana haja ya kujipamba kwa ajili ya mtu mwengine, tofauti na mwanamke, mwanamke anamapungufu anahitaji kuukamilisha uzuri wake, Anahitaji kujipamaba kwa mapambo ya thamani na mapambo ya aina mbali mbali, kufanya hivyo kunadumisha ndoa yake, kwa sababu hiyo sheria imeruhusu Mwanamke kujipamba kwa dhahabu, na sheria imekataza Mwanamume kujipamba kwa dhahabu, Amesema Mwenyezi Mungu: [**Ati alie lelewa katika mapambo na katika mabishano hawezi kusema kwa uwazi**], [Surat Zukhuruf: 18] Kwahiyo imefahamika hekma ya Mwenyezi Mungu! kuharamisha Wanaume kuvaa dhahabu.

Napenda kuwapa nasaha wanaume ambao wamepewa mtihani wa kujipamba kwa dhahabu, hakika Wanaume kujipamaba kwa dhahabu wanakuwa wamemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake Muhammadi, Na Wanaume hao wanakuwa Wamejifananisha na wanawake, Wanaume wanao vaa mikononi Mwao dhahabu Wanakuwa wamevaa makaa ya moto, kama alivyo sema Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake! Katikat kitabu: [Sahihi Muslim /2090] Wanaume Wanaovaa dhahabu watubuu kwa Mwenyezi Mungu waache kuvaa dhahabu! Kama wanataka kujipamba kwa fedha wajipambe kwa

kiwango ambacho sheria ya Mwenyezi Mungu imekiweka, Pia Wanaweza kujipamba kwa mapambo mengine yasio kuwa dhahabu, Wanaume wanaruhusiwa kuva pete za fedha! Na aina zingine za madini! kwasharti la kuwa Wasifanye israfu, (matumizi mabaya).

****

**Swali la 125: Ni ipi hukumu ya mtu kuweka meno ya dhahabu juu ya meno yake ya asili?**

**Jibu:** Meno yalio tengenezwa kwa dhahabu hairuhsiwi kwa Mwanaume kuyaweka juu ya meno yake ya asili, isipokuwa anaruhusiwa Mwanaume kuweka meno ya dhahabu juu ya meno yake ya asili kwa dharura, kwa sababu Mwanaume ni haramu kwake kuvaa dhahabu na kujipamba kwa dhahabu. Ama kuhusu Mwanamke, kama itakuwa ni tamaduni ya Wanawake kujipamba kwa kuweka meno ya dhahabu, hakuna ubaya nae akaweka hayo meno ya dhahabu, kama ndio itakuwa tamaduni yao ya kujipamba, kwa sharti Asijipambe kwa israfu! (matumizi yasio kuwa ya lazima) kwauthibisho wa kauli ya Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake: **((Mwenyezi Mungu ameruhusu Wanawake wa Uma wangu wajipambe kwa dhahabu na Hariri))**, [Al Tirmidhiy 1720].

Kama atafariki Mwanamke alie jipamba kwenye meno yake kwa dhahabu, Au akafariki Mwanaume alie weka dhahabu kwenye meno yake kwa dharura ya kisheria, meno hayo yataondolewa baada ya kufariki mtu huyo, kama kuyaondoa meno hayohakuta leta madhara kwenye muili wa marehemu, lakini kama kutasababisha kuukata mwili wa marehemu basi meno hayo watayachwa, kwa kuwa dhahabu inazingatiwa kuwa ni mali, na mali za marehemu baada ya kufariki zinarithiwa na familia yake, kuwacha dhahabu kwenye meno ya marehem na kumzika nayo nikupoteza mali ambayo nihaki ya warithi.

****

**Swali la 126: Ni ipi hukumu ya mtu kujisaidia haja ndogo sehemu wanayo tawadhia watu, jambo ambalo linapelekea kufunua sehemu zake za siri?**

**Jibu:** Hairusiwi binaadamu kufunua sehemu zake za siri kiasi ambacho watu watazionа sehemu za siri, watu ambao hawaruhusiwi kisheria kuona sehemu yake ya siri, mtu akifunua sehemu yake ya siri katika vyoo vilivyo andaliwa kwa ajili ya kutia udhu, na watu wakawa wanamuona mtu huyo anapata dhambi, na jambo hilo wamelieleza Wanachuoni wa kiisalam Mweneyezi Mungu awarehemu! Kuwa katika hali kama hiyo ni lazima atumie mawe au kitu kinge katika kujisafisha baada ya kumaliza kukidhi haja yake kuliko kutumia maji na kufunua sehemu

yake ya siri, aende sehemu ya mabali na watu akakidhi haja yake kisha atumie kijisafisha kwa vitu ambavyo sheria imeviruhusu, Apangushe sehemu iliyo toka haja yake kwa mawe mara tatu, au kitu kingine kilicho mfano wa jiwee, hadi sehemu hiyo isafike, mawe yawe matutu au zaidi ya matatu na haitoshi chini ya matatu, inamlazimu kufanya hivyo kwasababu kufunua sehemu yake ya siri wakati anajisafisha na watu wakamuona sehemu zake za siri jambo hilo ni haramu, kwa hivyo tunasema**:** Nilazima kuficha sehemu ya siri, hairuhusiwi kufunua sehemu yake ya siri mbele za watu kwa ajili ya kujisafisha, anatakiwa atafute sehemu ambayo hakuna Mtu anae muona hata mmoja .

****

**Swali la 127: Ni ipi hukumu ya mtu kukojoa akiwa amesimama?**

**Jibu**: Kukojoa mtuu akiwa amesimama inaruhusiwa kisheria, kwa masharati Mawili:

**1-**Awe na uhakika kuwa mkojo hautamrudia au cheche za mkojo hazito mpata.

**2-**Awe na uhakika kuwa hakuna mtu atakaemuona sehemu yake ya siri.

****

**Swali la 128: Ni ipi hukumu ya mtu kuingia chooni akiwa na Msahafu?**

**Jibu:** Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu wanasema: Hairuhisiwi kwa binadamu kuingia chooni akiwa na msahafu, kwa kuwa msahafu ni kitabu kitakatifu na kinacho heshimiwa, haifai kuingia nacho sehemu hiyo ya chooni. Mwenyezi Mungu ndio njuzi.

****

**Swali la 129: Ni ipi hukumu ya kuingia chooni ukiwa una karatasi limeandikwa jina la Mwenyezi Mungu?**

**Jibu:** Inaruhusiwa kuingia chooni Ukiwa na karatasi lilo andikwa jina la Mwenyezi Mungu, kama karatasi hiyo itakuwa ipo mfukoni na haionekani, hukumu ya karatasi hiyo itakuwa imejificha na imesitirika, pia yapo majina ya watu yanayo

karibiana na majina ya Mwenyezi mugu, kama jina la Abdul-allah na Abdul-Azizi, na Majina Mengine kama hayo.

****

**Swali la 130: Mtu anapo kuwa chooni vipi atasoma Bismillahi wakati wa kutia udhu?**

**Jibu:** Mtu akiwa chooni atasoma Bismillahi moyoni kwake, hato isoma kwa sauti, kwa kuwa kusoma bismilahi wakati wa kutia udhu au kukoga janaba sio jambo la lazima, hoja ya kuwa ni lazima kusoma bismillah wakati wakutia udhu na kuoga janaba hoja hiyo haina nguvu, Amesema mwana chuoni Imamu Ahmadi Ibun Hanbaali rahema na amani ziwe juu yake: **((Hakuna kauli iliyo sahihi kuwa Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake! Alikuwa Akisoma bismilahi wakati wakutia udhu))**, [Al Tirmidhiy /25] Amesema mwanawachuoni mwengine Ibun Qudaama mtunzi wa kitabu (Al-Mughuniy) Mwenyezi Mungu ameherem na Wanachuoni wengine kuwa kusoma bismilahi wakati wa kutia udhu ni Sunnah sio wajibu [Al-Mughuniy 146/145/1].

****

**Swali la 131: Ni ipi hukumu ya kuelekea kibla wakati wa kujisaidia haja ndogo au haja kubwa, au kuipa mgongo kibla?**

**Jibu:** Wametofautina Wanachuoni rehma na amani ziwee juu yao!, kauli nyingi, wapo Wanachuoni wamesema: kuwa Ni haramu mtu kuelekea kibla au kukipa mgongo kibla wakati anajisaidia haja kubwa au haja ndogo sehemu ya wazi isio kuwa ndani ya jengo, wakatoa ushahidi wa hadithi ya Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake! Amesimulia Abuu Ayubu Amesema: **((Msieelekee kibla mnapo kuwa mnajisaidia haja kubwa na mnapo kuwa mnajisaidia haja ndogo, wala Msikipe mgongo kibla mnapo kuwa mnajisaidia, isipokuwa elekeeni magaharibi au mashariki)) Amesema Abuu Ayubu rehama na amani ziwe juu yake: ((Tulikwenda Sham, tukakuta kunavyoo vimejengwe vikiwa vimeelekea upande wa Al-kaaba tukawa tunageuka kisha tunamuomba Msamaha Mwenyezi Mungu)),** [144/ Swahihi Bukhariy, /264/ Swahihi Muslimu], wakielewa kuwa hadithi ya Mtume imekataza kuelekea kibla wakati wa kujisaidia au kukipa mgongo kibla ni sehemu ya wazi na sio kwenye jengo, kama mtu atakuwa kwenye jengo anaruhusiwa kuelekea kibla au kukipa mgongo kibla anapo kuwa anajisaidia haja kubwa Au ndogo, kwa ushahidi wa hadithi ya Mtume Muhammad rehma na amani za ziwe ju yake amesimulia Abdul-allah Ibun Omari: ((**Kuwa nilipanda siku moja juu ya nyumba ya mke wa Mtume (Hafswa), Nikamuona Mtume wa Mwenyezi Mungu, Anajisaidia akiwa ameelekea Sham na akiwa ameipa mgongo Al-Kaaba)), [148/ Swahihu Bukhariy, /266/ Swahihi Muslimu]**.

**Wamesema baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu:** kuwa haifai mtu kuelekea kibla Au kukipa mgongo kibla anapokuwa anajisaidia haja ndogo Au haja kubwaa akiwa kwenye jengo au akiwa Sehemu ya wazi, haruhusiwi mtu huyo kueleke kibla, Au kukipa mgongo kibla, wametoa ushahidi wa hadithi alio isimulia Abu Ayubu, tulio ieleza hapo nyuma, wanachuoni hao wakatoa majibu ya hadithi alio isumilia Ibun Omari kama ifatavyo.

**1**-kuwa hadithi ya Ibun Omar rehma na amani ziwe ju yake! Nilipanda kwenye nyumba ya mke wa Mtume bi Hafswa, nikamuona Mtume Muhammadi anajisaidia haja akiwa amelekea shamu na ameipa mgongo Al-kaaba, hadithi hiyo ya Ibun Omari, ilikuwa kabla ya Mtume kukataza watu kuelekea kibla wanapo jisaidia haja ndogo Au haja kubwa Au kukipa mgongo kibla.

**2-** Hoja ya pili ni kuwa katazo hua linanguvu, na katazo linatoka kwenye asili, na jambo linalo toka kwenye asili huwa linapewa kipao mbele.

**3-**Hoja ya tatu kuwa hadithi ya Abii Ayubu rehma na amaniza ziwe juu yake! Ni ya matamshi na hadithi ya Ibun Omari ni ya kitendo na kitendo hakipingani na kauli au matamshi, kwakuwakitendo mtu Anaweza kufanya akiwa amesahau au akafanya kwa udhuru, au ikawa jambo hilo linaruhusiwa kulifanya mtu peke yake wafuwasi wake hawaruhusiwi kulifanya jambo hilo.

Hoja iliyo na nguvu kwaupande Wangu mimi, katika jambo hili, nikuwa ni haramu mtu kujisaidia haja kubwa Au haja ndogo akiwa Amelekea Al-kaaba, (kibla) Au ameiipa mgongo mtu huyo akiwa sehemu ya wazi kama jangwani nk, pia inaruhusiwa kuelekea upande wa kibla au kuipa mgongo kibla mtu anapokuwa anajisaidia haja ndogo au haja kubwa akiwa katika jengo au vyoo vilivyo jengewa, kwa kuwa katazo la kuelekea kibla wakati wa kujisaidia limehifadhiwa na halimuhusu mtu maalum, na katazo la mtu kuipa mgongo kibla kumehusishwa na kitendo na kukipa mgongo kibla kuna nafuu zaidi kuliko kukielekea kibla unapokuwa unajisaidia, na Mwenyezi Mungu ndio anaejua zaidi kwa hivyo imepatikana nafuu ya kuwa mtu akiwa kwenye jengo anaweza kuelekea lakini jambo lililo bora kama ataweza asikipe mgongo kibla hata kama atakuwa kwenye jengo.

****

**Swali la 132: Mtu akitokwa na upepo (ushuzi) hivi ni lazima kwa mtu huyo kujisafisha kwa kutumia maji?.**

**Jibu:** Mtu akitokwa na upepo (ushuzi) udhu wake unaharibika kwa uthibitisho wa maneno ya Mtume wa Mwenyezi Mungu rehma na amani ziwe juu yake: ((**Mtu akiwa kwenye swala akahisi kuwa kuna kitu kimetoka sehemu yake ya haja kubwa, asitoke kwenye swala hadi asikie sauti ya upepo**

**(shuzi) Au asikie harufu**)), [137/ Swahihi Bukhary, /361/ Swahihi Muslimu], lakini si lazima kwa mtu alie tokwa na upepo sehemu yake ya haja kubwa kujisafisha kwa maji, si lazima kuosha sehemu yake ya siri kwa sababu hakuna kitu kilicho toka kinacho mlazimu kuosha sehemu yake ya siri kwa hiyo mtu akitokwa na upepo udhu wake unaharibika inatosha kwake kutawadha, kuosha uso wake na kusukutua Na kupandisha maji puani, Na kuosha mikono yake Na kupaka maji kichwa chake na kupaka maji masikio Na kuosha miguu yake hadi kwenye vifundo vya miguu.

Napenda kuchukuwa nafasi hii kuwakumbusha mambo ambayo yanajificha kwa baadhi ya watu,Wapo baadhi ya watu wanakwenda kujisaidia haja kubwa au haja ndogo kisha wanajisafisha kwa maji, ikifika muda wa swala wakitaka kutia udhu, wanadhani kuwa ni lazima kwanza waende kujisafisha Sehemu zao za siri mara ya pili, hii sio sahihi, Mtu anapo osha sehemu yake ya siri baada ya kumaliza kujisaidia sehemu hiyo inakuwa imesafika, anapo taka kutawadha hana ulazima wakuwanza kuosha sehemu yake ya siri, makusudio ya kusafisha sehemu ya siri kwa maji au kusafisha kwa mawe au kitu kingine ni jambo la kisheria na lina masharti yake yanafahamika madhumuni ni kusafisha sehemu iliyo toka kinyesi, ukisafisha kinyesi hakirudi isipokuwa kama utajisaidia tena mara ya pili itakuwa lazimu uoshe tena.

****

**Swali la 133: Ni muda gani sheria inapendekeza kupiga mswaki? Na ni ipi hukumu yakupiga mswaki kwa mtu anae subiri swala muda ambao inatolewa khutba?**

**Jibu: M**uda ambao sheria imependekeza kupiga mswaki mtu atakapo amka kutoka usingizini, akitaka kuingia nyumbani kwake, wakati wa kutawadha, Na anapoa simama wakati wa-kutaka kuswali.

Sio vibaya mtu anae subiri Swala kupiga mswaki, lakini wakati wa khutuba asipige mswaki, akipiga mswaki wakati wakhutba itakuwa imemshughulisha kupiga mswaki na sio kusikiliza khutba, isipokuwa kama atakuwa anasinzia basi anaweza kupiga mswaki kwa ajili ya kuodosha usingizi.

****

**Swali la 134: Je ni lazima kusoma Bismilahi wakati wa kutawadha?**

**Jibu:** Mtu kusema Bismilahi wakati anaanza kutawadha sio lazima isipokuwa ni Sunna, hadithi iliyoelezea kusoma Bismillah wakati wa kuanza kutawadha kuna haja ya kuiangalia kwa kina.

**Amesema:** Imamu Ahmadi- Hili jambo linafahamika kwa Wanachuoni wote walio hifadhi hadithi za Mtume Muhammad **((Wakisema kuwa haikuthibiti kwenye maudhuii hadithi**)), [381/2/ kitabu Masaail Imammu Ahmadi/ Is'haqa Rahawiya], hadithi hiyo inabaki hivyo hivyo, hata kama kuthibiti kwa hadithi hiyo kunahitaji kuwangaliwa vizur, hatakiwi mtu kuwalazimisha watu kufanya jambo kuwa la lazima hali ya kuwa halikuthibiti kwa Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake! Kwa sababu hiyo naona kuwa kusoma Bismillahi wakati wa kuwanza kutawadha ni Sunnah, likini ambae itathibiti hadithi kwake ni lazima aseme kuwa ni lazima nayo ni kuleta bislillah ni waJibu kwa kauli ya Mtume: **((Hana udhu mtu ambae hakusoma bismilahi**)), [25/Al Tirmidhiy, /398/ Ibun Majah]. Usahihi wa hadithi hiyo inaonyesha kukataza kusihi na sio kukataza kukamilika kwa udhu.

****

**Swali la 135: Ni ipi hukumu ya kutahiri wanaume na wanawake?.**

**Jibu:** Wametofautiana Wanachuoni katika hukumu ya kutahiri, na kauli yenye usahihi zaidi ni kwamba ni wajibu kutahiri kwa wanaume na ni Sunnah kwa wanawake, na sababu ya kutofautisha hukumu ya kutahiri kwa wanaume na wanawake: Kutahiri kwa wanaume kuna maslahi yanayorudi katika sharti ya Swala ambayo ni twahara, kwasababu mwanaume akiwa hajatahiriwa mkojo unapotoka kwenye tupu ya mwanaume kuna mabaki ya mkojo yanayo jikusanya katika ile ngozi na inaweza kusababisha madhara ya kuchunika ngozi au kupata majeraha, au kila itakapo tikisika tupu yake basi mkojo hutoka na atakuwa ni mwenye najsi. Ama kutahiri kwa upande wa wanawake, hakika faida kubwa iliyopo ni kupunguza matamanio yake, na kufanya hivo kwa mwanamke ni kutaka ukamilifu wala siyo kwasababu ya kuondoa uchafu.

Wanachuoni wameweka masharti ya kutahiri Mtu anae tahiriwa awe na uhakika kuwa hato pata madhara ya kiafya kama atatahiriwa na hato poteza maisha yake kwa kutahiriwa kama mtu atahofia kuwa akitahiriwa anaweza kupoteza maisha au akitahiriwa atapata maradhi mtu huyo sio lazima kutahiriwa kwasababu ulazima wakutahiriwa unaondoka kama mtu hatokuwa na uwezo wakutahiriwa.

**Ushahid wa kuwatahiri wanaume**:

**1**-Zimepokelewa hadithi nyingi **((Kuwa Mtume Muhammad rehma na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, alitoa amri kwa waislam walio silimu kutoka kwenye ukafiri nakuigia katika dini ya kislamu, Watahiriwe))**, [356/ Abuu Daud]. Na asili ya amri huwa ni lazima kuifata.

**2-**Kutahiri nijambo linalo watofautisha Wakiristo na Waislamu, Waislamau walikuwa wanawafahamu ndugu zao waislamu wakati wa vita kati ya waislam na makafiri baada ya kumalizika vita kwenye kutahiri, wakimuona alie tahiriwa huyo anakuwa Mwislam na ambae hakutahiriwa huyo ni kafiri, wakasema**:** kutahiri ndio jambo litakalo tutofautishia kati ya mwislmu na asie kuwa muislamu, kama kutahiri ni jambo lino tofautisha kati ya Muislamu na kafiri basi kutahiri ni lazima ili ipatikane tofauti kati ya Muislamu na kafiri, pia imeharamishwa waislamu kujifananisha na makafiri kwa hadithi ya Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake anasema**: ((Mtu atakae jifananisha na watu huyo mtu atakuwa miongoni mwao**)), [4031/Abuu Daud].

**3-**Kutahiri Nikukata ngozi kwenye Mwili wa binaadam, na kukata mwili wa binaadamu niharamu na kutende cha haramu hakiwezi kuwa halali isipokuwa Kwa jambo hilo litakuwa na ulazima, kwahivyo kutahiri ni jambo la lazima.

**4-**Kumtahiri mtoto yatima anatakiwa kutoa ruhusa mlezi wake kwa kuwa kukata sehemu ya mwili wa yatima ni sawa na kumfanyia uadui na kuchukuwa mali ya huyo mtoto yatima, kwa kuwa anae mtahiri anahitaji malipo ya kutahiri, kama kutahiri sio lazima isinge faa kukata ngozi ya mwili wa mtoto yatima, na kuchukuwa mali ya mtoto yatima, kwa ajili ya kumlipa mtahiri, na huu ni ushahidi wa matendo ya wema walio tangulia, na kwa mtazamo wa wazi inatufahamisha kuwa kutahiriwa ni lazima kwa wanaume.

Kuhusu wanawake sio lazima kuwatahiri kama ilivyo kuwa ni lazima kwa Wanaume kutahiriwa, na hii ndio hoja iliyo na nguvu, kuna hadithi dhaifu: (( **Kutahiri wanaume ni Sunna, na kuwatahiri wanawake haipendezi-makuruhu)), k**ama hadithii hii ingeswihi ingetengenisha .

****

**Swali la 136: Kama mtu atakuwa na meno ya bandia (ya kutengeneza) je ni lazima kwa mtu huyo kuyatoa meno hayo wakati wa kusukutua mdomo anapotawadha?**

**Jibu:** Kama mtu atakuwa na meno ya kutengeneza yamepachikwa kwenye meno yake ya asili sio lazima kwa mtu huyo kuyatoa meno hayo wakati wa kusukutua mdomo anapokuwa

anatawadha, hukumu ya meno yalio pachikwa inafanana na mtu Alie vaa pete kwenye kidole chake, na mtu alie vaa pete sio lazima kuivua anapokuwa anatwadha, kilicho bora kwa mtu alie vaa pete wakati anatawadha aizungushe pete yake, na sio lazima kuizungusha pete hiyo, kwa sababu Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake alikuwa anavaa pete na haikupokelewa hadithi kuwa Mtume Muhammad alikuwa anaivua pete yake anapo taka kutawadha.

Jambo lipo wazi meno ya kutengeneza yalio bandikwa kwenye meno ya asili bila kuyatoa maji hayawezi kufika kwenye meno ya asili, lakini kuna watu wenye meno ya kutengeneza inakuwa vigumu kuyatoa hayo meno wakati wa kutawadhi kisha baada ya kutawadha ayarudishe.

****

**Swali la 137: Je ni lazima mtu akiwa anatawadha achukue maji mapya anapo osha masikio yake?**

**Jibu:** Sio lazima kwa mtu anae tawadha kuchukuwa maji mapya wakati anapo pangusa masikio yake, na haipendezi kuchukuwa maji mapya kwa ajili ya kupangusa masikio kwa kauli iliyo sahihi, kwa kuwa hadithi zilizo elezea sifa za udhu wa Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake hazikutaja kuwa Mtume Muhammad alikuwa anachukuwa maji kwa ajili ya kupangusa masikio, iliyo bora apanguse masikio yake kwa unyevunyevu wa maji ulio baki kwenye mikono yake wakati anapaka maji kichwa chake.

****

**Swali la 138: Ni ipi maana ya utaratibu wa kutawadha? Na ni yapi makusudio ya kufatanisha kuosha viugo wakati wakutawadha? Na ni ipi hukumu yake?**

**Jibu:** Utaratibu katika kutawadha maana yake ni mtu kuwanza kutawadhaa kwa kufata utaratibu alio upanga Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ameanza kutaja utaratibu wa kutawadha kwa kutaja kuosha uso, kisha kuosha mikono Miwili, kisha kupaka maji kichwani, kisha kuosha miguu miwili, Mwenyezi Mungu hakueleza kuosha viganja viwili vya mikono, kwa sababu kuosha viganja viwili kabla ya kuosha uso ni Sunnah na sio waJibu, huu ndio utaratibu wa kutawadha, tunatakiwa kutawadha kwa kuosha viungo vyetu kama alivyo panga Mwenyezi Mungu, Alivyo panga viungo vya kutawadha, kwa sababu Mtume Muhammadi alivyo hiji Makkah, alitoka

kwenda kwenye sehemu ya saayu alipo fika sehemu hiyo akasoma maneno ya Mwenyezi Mungu: [**Na hakika vilima vya safa na maruwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu**], [Suratul Baqara: 158] Akasema: ((**Naanza Alipo Anzia Mwenyezi Mungu)),** [1218 /Sahihi Muslimu] kaweka wazi kuwa amenza swafa kabala ya maruwa kwa kufata alivyo anza Mwenyezi Mungu.

Na kuhusu kufatanisha kuosha viungo wakati wa kutawadha, maana yake ni asipitishe muda mrefu kati ya kuosha kiungo na kiungo kingine, kwa mfano kama ataosha uso wake, kisha akataka aoshe mkino yake, lakini ukapiata muda mrefu hajaosha mikono, kuwafatanisha kuosha viungo kutakuwa kumeharibika, itamlazimu aanze tena kuosha uso ndio aoshe mikono yake, bila kupitisha muda mrefu kati ya kuosha uso na mikono, Mtume Muhammadi rahma na amani ziwe juu yake alimuona Mtu mmoja ametawadha na katika mguu wa mtu huyo kuna alama maji hayakufika sehemu hiyo, Mtume akasema kumwambia mtu yule: ((**Nenda ukatawadhe tena na utawadhe vizuri**)), [243/ Swahihi Muslimu], na katika upokezi wa hadithi nyingine ya Abi Dawud ((**Mtume alimuamrisha mtu yulee Atawadhe tena)),** [175/Abuu Daud] hadithi hizi zinatufahamisha kuwa kufatanisha kuosha viungo katika kutawadha ni sharti katika masharti ya kutawadha, kama mtu ataacha kufatanisha bila udhuru udhu wake hautakuwa sahihi, kutawadha ni ibada moja na ibada moja haifai kuitenganisha kwa mafungu.

**Kauli iliyo sahihi:** kutawadha kwa kufata utaratibu na kufatanisha kuosha viungo ni mambo ya lazima katika kutawadha.

****

**Swali la 139: Mtu akitawadha akasahau kuosha kiungo kimoja katika viungo vinavyo takiwa kuoshwa hukumu yake ni ipi?**

**Jibu: M**tu akitawadha akasahu kuosha kiungo katika viungo vinavyo takiwa kuoshwa, kama atakumbuka kabla ya kupita muda mrefu, ataosha kiungo hicho , kisha ataosha viungo vinavyo fatia, mfano**:** Mtu akiwa anatawadha akasahau kuosha mkono wake wa kushoto, akaosha mkono wa kulia kisha akapaka maji kichwani na masikioni na akaosha miguu yake miwili, alivyo malizia kuosha miguu yake miwili akakumbuka kuwa hakuosha mkono wake wa kushoto tunasema**:** kumuelekeza mtu huyo, anze kuosha mkono wake wa kushoto kisha apake maji kichwani na masikioni na aoshe miguu yake miwili, ni lazima kurudia kuosha miguu yake miwili na kupaka maji kichwa na masikio kwasababu ya kufata utaratibu kama alivyo upanga utaratibu huo Mwenyezi Mungu! Anasema Mwenyezi Mungu: **[Enyi mlio amini! mnapo simama kwa ajili ya swala**

**basi osheni nyuso zenu, na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na osheni miguu yeni mpaka vifundoni**], [Surat Maida: 6].

Kama atakumbuka baada ya kupita muda mrefu, anatakiwa arudie kutawadha upya, mfano akitawadha mtu akasahau kuosha mkono wake wa kushoto kisha akamaliza kutawadha udhu wake, akaondoka kwenda kufanya mambo yake, na ukapita muda mrefu, kisha akakumbuka kuwahakuosha mkono wake wakushoto alipokuwa anatawadha, ni lazima kwa mtu huyo kurudia kutawadha, kwa sababu kumekosekana kufatanisha kuosha viungo wakati wa kutadha na kufatanisha kuosha viungo wakati wakutawadha nisharti la kusihi udhu.

Fahamu kuwa kama mtu atatia shaka kuwa ameuosha mkono wake wakushoto au hajauosha, baada ya kumaliza kutawadha, au akatia shaka kuwa alisukutua mdomo wakati wakutia udhu, mtu huyo hatakiwi kuifata shaka, atendelela kuwa na udhu wake, na hakuna tatizo katika udhu wake, Pia kama atatia shaka baada ya kumaliza kuswali hato rudia ibada yake kwa kuwa shaka haina nafasi.

Kama mtu atafata shaka alio iweka kwenye ibada atakuwa amefungua mlango wa wasi wasi, kila Mtuu atakuwa hajiamini kwenye ibada yake, Mwenyezi mugu kwa rehma zake ametuwekea urahisi kuwa mtu akitia shaka baada ya kumaliza kufanya ibada shaka hiyo haina nafasi, lakini kama mtu akiwa na uhakika kuwa hakutawadha au akawa na uhakika kuwa alisahau kuosha

kiungo kimoja wakati anatawadha ni lazima mtu huyo kurudia hiyo ibada. Mwenyezi Mungu ndio anaye jua zaidi.

****

**Swali la 140: Je maji yakikatika wakati mtu anatwadha, kisha yakarudi hali ya kuwa viungo vimesha kauka ataanza upya kutawadha au ataendelea alipo kuwa amefikia?**

**Jibu:** Jambo hili hukumu yake inakuwa kwenye kufatanisha kuosha viungo wakati wa kutawadha, na kwa kuwa kufatanisha kuosha viungo ni sharti la kusihi udhu. Wanachuoni rehma na amani za Mwenyezi Mungu ziwaendee wana kauli mbli:

**Kauli ya kwanza:** kuwa kufatanisha kuosha viungo wakati wa kutawadha ni sharti la kusihi udhu, na udhu hausihi hadi sharti hilo likamilike, kama mtu atatenganisha kuosha kiungo kimoja na kiungo kingine udhu wake hauta sihi, na hii ndio kauli iliyo na nguvuu ambayo hoja zake zina nguvu, kwa sababu kutawadha ni ibada moja ni lazima iwee yenye kuungana na tunapo sema kuwa nilazima kufatanisha kuosha viungo ni jambo la lazima na ni sharati la kusihi udhu.

**Wamesema baadhi ya Wanachuoni**: kufatanisha kuosha viungo wakati wakutawadha mtu asichelewe kuosha kiungo hadi kiungo kilicho kabla ya kiungo hicho kikauke, isipokuwa kama atachelewa kuosha kiungo hicho kwa sababu inayo endana na mambo yanayo husu kutawadha, kama uchafu ulio ganda kwenye kiugo kinacho takiwa kuoshwa akawa anaondoa uchafu hadi kiungo kilicho kabla yake kika kauka, mtu huyo ataendelea na udhu wake sehemu alio kuwa amefikia hata kama atachelewa muda mrefu, kwa sabau kuchelewa kwake alikuwa anafanya jambo linalo husu kutawadha.

Kama atachelewa kuosha kiungo kwa sababu ya kukosekana maji, kama muulizaji wa swali hili alivyo uliza, baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, wanasema: kufatanisha kuosha viungo kutakuwa kumempita kwa hiyo atatakiwa anze kutawadha mara nyingine udhuu mpya.

Wanasema baadhi ya Wanachuoni wengine: kuwa hajapitwa na kufatanisha kuosha viungo kwa sababu jambo hilo hakuliweka yeye lipo njee ya uwezo wake na mtu huyo anakuwa bado anasubili akamilishe udhu wake, kwa hiyo maji yakirudi anaendelea pale pale alipo kuwa ameishia, hata kama viungo vyake vitakuwa vimekauka.

Baadhi ya Wanachuoni wanao sema kuwa ni lazima kufatanisha kuosha viungo na ni sharti la kusihi udhu, wanasema: kufatanisha kuosha viungo hakuwafikiani na kukauka viungo, kunaafikiana na desturi ya watu, desturi ya sehemu hiyo katika kuosha viungo ndio itafatwa, na desturi hiyo kama haipo sehemu hiyo haito fatwa, kwamfano: Watu ambao wanasubili maji yanapo kuwa yamekatika, watu hao wanakuwa na kazi ya kuleta maji au kutafuta maji, kwa baadh i ya watu hiyo sio sababu ya kuwa udhu wao wa Mwanzo walio kuwa wamenza kutawadha wanaonganisha udhu wao wa mwanzo na huu wapili bila kurudia, na hili jambo ndio ni bora yakija maji waendelea kutawadha pale walipo kuwa wameishia, isipokuwa kama utakuwa umepita muda mrefu sana, ambao utakuwa umenda kinyume na desturi yao, watanza kutawadha udhu mpya na jambo hili nijepesi.

****

**Swali la 141: Ni ipi hukumu ya udhu wa mtu alie weka kucha za kutengeneza (kucha za bandia )?**

**Jibu:** kucha za bandia ni plastiki zinazo wekwa kwenye kucha za mwanamke, na zinakuwa na ganda, hairuhusiwi kwa Mwanamke kuzitumia kucha hizo kama atakuwa anaswali,

kwa sababu kucha hizo zinazuiya maji kufika katika mwiili na kila kitu ambacho kinazuiya maji yasifike kwenye mwili wa mtu anaye tawadha au anae koga kitu hicho hakiruhusiwi kukivaa, amesema Mwenyezi Mungu: **[Na osheni nyuso zenu na mikono yenu],** [Surat Maida: 6].

Mwanamke akiva kwenye kucha zake kucha za kutendengeneza

(bandia) kucha hizo zinazuiya kufika maji kwenye mwili, hawezi kuwa ametwaharika akitawadha au akioga, atakuwa ameacha faradhi ya kutawadha na faradhi ya kuoga anapokuwa na janaba.

Kama mwanamke atakuwa haswali kwa sababu ya kisheria, kwa mfano mwanamke mwenye hedhi, anaruhusiwa kuweka hizo kucha za bandia kwa hayo masiku atakayo kuwa yupo kwenye siku za hedhi, lakini kama kuvaa hizo kucha za bandia ni katika mambo wanayo yafanya wanawake wa kikafiri, hairuhusiwi Mwanamke wa kiisalamu kuweka hizo kucha, kwa sababu sheria hairuhusu wanawake wa kiislamu kujifananisha na wanawake wa kikafiri.

Nimesikia kuwa kuna watu wametoa fat'wa (maelekezo) kuwa kuvaa kucha za bandia n isawa na kuvaa khofu, (viatu vinavyo funika migu) Anaruhusiwa mwanamke avae kucha za bandia kwa muda wa usiku na mchana kama hatokuwa safari, na mwanamke atakae kuwa yupo safari atavaa kucha hizo muda wa siku tatu, fatua hiyo (maelekezo) Sio sahihi sio kila kinacho sitiri mwili wa binaadamu hukumu yake inakuwa ya

khofu (viatu vinavyo funika miguu) Sheria imeruhusu kuvaa khofu na kufuta juu yake kwa haja (dhiki) kwa sababu miguu kuna haja ya kuipoza na kuihifadhi, kwa kuwa inagusa ardhi, na changarawe, na inapata baridi, na mambo mengine, ikaja sheria maalumu kuruhusu kufuta juu ya khofu, na wamechukuwa kiyasi kukisia na kupaka kwenye kilemba, na kukisia huku sio sahihi, kwa sababu kilemba huvaliwa kichwani, na kichwa faradhi yake ni nyepesi, faradhi ya kichwa wakati wakutawadha nikupaka, tofauti na mikono yenyewe huoshwa, faradhi ya mikono nikuiosha, kwa sababu hiyo Mtume Muhammadi hakuruhusu wanawake apake kwenye gloves, pamoja kuwa zimefunika mikono, ina tufahamisha kuwa hairuhusiwi mtu kukisiya kito chochote kitakacho ziwia kufika maji kwenye juu ya kilemba au juu ya khofu.

Ni lazima kwa kila Muislamu, atoe juhudi zake zote kutaka kuujua ukweli, na asitoe fat'wa (maelekezo) isipokuwa akiwa anafahamu kuwa Mweneyezi Mungu atamuuliza kuhusu hayo maelekezo alio yataoa, kwa kuwa mtu anakuwa anatoa maelekezo ya sheria ya Mwenyezi Mungu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze katika njia ya haki na njia iliyo nyoka.

****

## Swali la 142: Ni zipi sifa za udhu wa kisheria?

**Jibu**: Sifa za udhu wa kisheria zimegawanyika sehemu kuu mbili:

1-Sifa za lazima nazo hausihi udhu hadi sifa hizo zikamilike nazo zimeelezwa kwenye kauli ya Mwenyezi Mungu: **[Enyi mlio amini!mnapo simama kwa ajili ya swala basi osheni nyuso zenu,na mikono yenu mpaka kwenye vifundi, na pakeni vichwa vyenu, na osheni miguu yenu mpaka vifundoni**], [Surat Maida: 6].

Kuosha uso mara moja na kusukutua mdomo na kupandisha maji puani na kuyatoa, kuosha mikono miwili, kuwanzia kwenye incha za vidole hadi kwenye vifundo, inabidi watu wawe makini wakati wakutadha, wapo ambao hawafikishi maji kwenye viganja vya mikono wanapo kuwa wanatwadha, anaridhika na vile alivyo anza kuosha viganja mwanzo ikifikia wakati wakuosha mkono haoshi sehemu ya karibia na ncha za vidolee na hili nikosa katika kutawadha, na watu wengini wanajisahau, kuosha mkono kuwanzia kwenye ncha za vidole hadi kwenye vifundo, kisha atapaka maji kichwani mara moja, na masikioni kwa unyevunyevu wa maji yalio baki wakati wakupaka maji kichwani, kisha ataosha miguu miwili mkapa kwenye vifundo mara moja, hizi ndio sifa za lazima katika kutawadha.

2-Sifa ya pili katika sifa za kutawadha, ni sifa za Sunna, tunazielezea kama ifatavyo kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, kusoma bismillahi, wakati ananza kutawadha, kuosha vigan-

ya vya mikono mara tatu, kisha asukutue mdomo wake ,na apandishe maji puani kwake, kwa michoto mitatu kwa kutumia viganja vya mikono yake, kuosha uso mara tatu, kisha aoshe mikono yake miwili hadi kwenye vifundo mara tatu, atanza kuosha mkono wa kulia kisha atafatia mkono wa kushoto, kisha atapaka maji kichwani kwake mara moja, atapeleka mikono yake kuwanzia kwenye utosi hadi kufikia kwenye uchogo kisha atairudisha mikono yake sehemu ya utosi wake alipo anzia, kisha atapangusa masikio ataingiza kidole shahada kwenye matundu ya masikio yake mawili, atapitisha kidole gumba nyuma ya masikio kwa njee, kisha ataosha miguu yake hadi kwenye vifundo mara tatu atanza mguu wakulia kisha mguu wa kushoto, kisha atasema baada ya kumaliza: ((Ashhadu an la iLLah illa Allahu wahadau la shariykalahu, wa ashahadu anna Muhammadan Abduhu wa Rasuluhu, Allahuma ij-alaniy mina twabiyna wajaarani minal- mutatwahiriyna)), [Swahihi Muslimu /234]. Akifanya hivyo atafunguliwa milango Minane ya pepo aingie kupitia mlango atakao utaka, kama ilivyo thibiti hadithi ya Mtume Muhammadi rehma na amani ziwee juu yake! Aliyo isimulia Ibun Omar radhi za Mwenyezi Mungu zimuendee .

****

### Ujumbe Wa Maelekezo Namna Ya Kujisafisha Mgonjwa

**Amesema sheikh Mwenyezi Mungu amuhifadhi**:

Kila sifa njema zinamsatahiki Mwenyezi Mungu na Mwe-

nyezi Mungu ndio tunae muomba msaada na tunamuomba msamaha na tunarejea kwa Mwenyezi Mungu kwa kuwacha kufanya madhambi tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu kwa kutokana na shari tunazo zifanya na maovu tunayo yafanya, mtu akiongozwa na Mwenyezi Mungu kuifahamu haki na kufanya mambo mazuri, hakuna anaye weza kumpoteza, na Mwenyezi Mungu akimuacha mtu apotee hakuna anaye weza kumuongoza mtu huyo, natamka kwa ulimi na kuthibitisha kwa moyo kuwa hakuna Mungu anaestahiki kuwabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu mmoja peke yake hana mshirika, pia natamka kwa ulimi na kuthibitisha kwa moyo kuwa Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi mugu na ni mtumwa wake rehma na amani zimuendee yeye na familia yake na wafuasi wake na wema walio tangulia.

**Baada Ya Utangulizi Huu**:

Hii ni risala fupi inayo elezea, mambo ya lazima kwa mgonjwa , anapo taka kutawadha kwa jili ya kuswali na anavyo swali, hakika mgonjwa anasheria zake maalumu zinazo muhusu yeye anapo kuwa katika hali ya ugonjwa kwa kuwa sheria ya wislamu inalinda hali ya kila mmoja Mwenyezi Mungu amemtUma Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake!na dini ya hurUma nzuri, dini iliyo jengewa misingi ya wepesi na urahisi, amesema Mwenyezi Mungu : **[Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika dini]**, [Suratul Hajj: 78] Amesema pia: [**Mwenyezi Mungu anakutakieni, yalio mepesi,wala hakutakieni yalio mazito],** [Suratul-Baqarah: 185]. **[Basi mcheni Mwenyezi Mungu, muezavyo, na sikieni na tiini**,] [Surat Al

Taghabun: 16]. Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu rehma na amani ziwe juu yake: ((**Uislamu ni mwepsi**)), [39 /Sahihi Bukhary] Amesema pia: ((**Nikiwamrisha jambo lifanyeni kwa uwezo wenu**)), [7288 /Sahihi Bukhary /1337 /Sahihi Muslim], kwa mujibu wa ushahidi huu Mwenyezi munmgu amewarahisishia watu wenye udhuru katika ibada zao wafanye ibada zao kwa kulingana na hali zao, ili wanafaye ibada bila kupata shida, wala tabu, na kila sifa njema zinamsatahiki Mwenyezi Mungu .

### Vipi Atajisafisha Mgonjwa?

**1-** Ni lazima kwa mgonjwa ajisafishe kwa kutumia maji atawadhe kama atakuwa na uchafu mdogo, ambao sio lazima kwake kuoga, pia ni lazima kwa mgonjwa kuoga kama atakuwa na uchafu unao mlazimu kuoga uchafu mkubwa ( janaba, hedhi na nifasi).

**2-** Kama mgonjwa atakuwa hawezi kujisafisha kwa kutumia maji kwa sababu ya kushindwa kuyatumia maji, mfano mgonjwa ambaye yupo mahututi hawezi kuinuka au hawezi kutumia maji kwa sababu anahofia atazidisha ugonjwa au akahofia kuwa akitumia maji ugonjwa utachelewa kupona, mgonjwa huyo atatayamamu (atatumia mchanga).

**3-** Namna ya kutumia mchanga kwa ajili ya kutia udhu: Atapiga viganja vyake viwili juu ya mchanga ulio safi mara moja kisha atapaka uso wake wote kwa kutumia viganja hivyo kisha atapaka viganja vyake viwili kiganja cha mkono wa chakushoto kitapaka chakulia na chakulia kitapaka chakushoto.

**4-** Kama mgonjwa hatoweza kujisafisha Mwenyewee kwa kutumia maji basi atatwaharishwa na mtu mwengine, pia kama hato weza kutayamamu (kutumia mchanga) Atamtayamamisha na mtu mwengine, atapiga mtu huyo viganja vyake kwenye mchanga kisha atampaka mgonjwa uso wake na viganja vyake, mfano kama anagekuwa anamtawadhisha kwa kutumia maji.

**5-** Kama mtu atakuwa na madonda katika baadhi ya viungo vinavyo takiwa kuoshwa wakati wa kutawadha, ataosha viungo hivyo kwa kutumia maji, kama kuosha viungo hivyo vyenye majeraha kutamsababishia madhara, atapangusa juu yake na hato osha, ataurowesha mkono wake kwa kuutia maji kisha ataupitisha juu ya kiungo hicho chenye jeraha, kama kufanya hivyo kutakuwa kunamzidishia mardhi atatayamamu.

**6-** Mtu akiwa amefungwa ogo kwenye kiungo kinacho takiwa kuoshwa kama mkono au mguu mtu huyo atafuta kwa maji juu ya ogo hilo itakuwa sawa na kukiosha kiungo hicho na hato tayamamu kwa kuwa kufuta juu yake kunachukuwa nafasi ya kuosha.

**7-** Anarusiwa mtu kutayamamu kwenye ukuta wa nyumba au kitu kingine kilicho safi na chenye vumbi kama ukuta utakuwa umefutwa na kitu kingine kisichokuwa aridhi hairuhusiwi kutayamamu kwenye ukuta huo hadi uwee ukuta huo unavumbi.

**8-** Kama mtu atakuwa hawez i kutayamamu kwenye ardhi au kwenye ukuta au kitu kingine chenye vumbi inafaa kuweka udongo kwenye chombo au kitamba kisha tayamamu kwenye chombo hicho au kitamaba hicho.

**9-** Mtu akitayamamu kwa ajili ya kuswali akaendelea kuwa na udhu wake na haukuharibika hadi muda wa swala nyingine ukaingia ataswali kwa udhu wa mwanzo alio tayamamu na hato rudia kutayamamu mara ya pili, kwa sababu bado yupo na twahara na hakijamtokea kitu kinacho haribu udhu .

**10-** Ni lazima kwa mgonjwa ausafishe mwili wake kutokana na najisi, kama atakuwa hawezi kujisafisha, ataswali hivyo hivyo, aa swala yake ni sahihi na hato irudia swala hiyo.

**11-** Ni lazima kwa mgonjwa aswali kwenye nguo iliyo safi , kama nguo yake itachafuka kwa kupatwa na najisi, ni lazima aioshe nguo hiyo au abadilishe avae nguo nyingine, kama hato weza kufanya hivyo , ataswali kwenye nguo hiyo

hiyo yenye najisi aa swala yake itakuwa sahihi hato irudia.

**12-** Ni lazima kwa mgonjwa aswali sehemu iliyo safi kama sehemu hiyo ikichafuka kwa najisi ni lazima kupasafisha au kuweka kitu kingine kilicho safi, au wamtandikie kitu kingine kisafi kama haita wezekana ataswali hivyo hivyo na swala yake ni sahihi na hato irudia.

**13-** Haruhusiwi mgonjwa kuchelewesha swala hadi wakati wake ukatoka kwa sababu kuwa hawezi kutawadha, anatakiwa kutawadha kwa uwezo wake kisha aswali swala katika muda wake, hata kama kwenye nguo zake na sehemu alipo kutakuwa na najisi hawezi kuviondoa ataswali hivyo hivyo.

****

**Swali la 143: Ni ipi hukumu ya mtu kuvua soksi za miguu kila anapokuwa anatwadha akitia shaka ya kusihi udhu?.**

**Jibu: k**ufanya hivyo ni kinyume na mafunzo ya Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake! pia unakuwa umejifananisha na Marawafidhwa ambao hawaruhusu mtu kufuta juu ya khofu (viatu vinavyo valiwa miguuni vinafunika kote), na Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake! alimwambia Mughiyra alipo kuwa anataka kuvua khofu za Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Ziache mimi nimeziingiza (nimezivaa) baada ya kuwa nimetawadha**)) [206/ Sahihi Bukhry, /79/274/ Sahihi Muslim] Mtume rehma na amani ziwe juu yake akazifuta kwa juu.

****

**Swali la 144: Kukadiria muda wa kupangusa juu ya khofu mbili, unaanza muda gani?.**

**Jibu:** Mambo haya ni katika mambo muhimu sana ambayo watu wanatakiwa waelekezwe kwa hiyo nitajaribu kuJibu kwa kirefu kuliko ilivyo ulizwa insha-allah!.

**Tunasema:** Hakika kupangusa juu ya khofu mbili imethibit i kwenye kitabu cha Mwenyezi Mungu na imethibiti kwenye mafunzo ya Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake!.

Amesema Mwenyezi Mungu: [**Enyi mlio amini! Mnapo**

**simama kwa Ajili y swala basi osheni nyuso zenu, na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na osheni miguu yenu mpaka vifundoni**] [6/ Surat Maaida], kwenye maneno ya Mwenyezi mugu katika neno osheni miguu yenu mpaka vifundoni, limetiwa kasra, linakuwa limeungana na kauli ya pakeni vichwa vyenu, miguu inakuwa imeingia katika viungo vinavyo pakwa, pia ukisoma ibara ya osheni miguu yenu mpaka vifundoni kwa kutia fat-ha, inakuwa imeungana na ibara ya osheni nyuso zenu, miguu na yenyewe inatakiwa kuoshwa na sio kupakwa, kwa hiyo miguu inakuwa imechukuwa hukumu mbili unaweza kupaka kama unavyo paka kichwa au kuosha kama unavyo osha uso, hadithi za Mtume Muhammadi zimeweka wazi muda gani inafaa kupaka na muda gani inafa kuosha, hadithi zimeeleza kuWa inatakiwa kuosha miguu ikiwa upo wazi na kupaka miguu ikiwa imefunikwa na khofu.

Kuhusu hadithi za Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake zimethibiti nyingi na ni hadithi sahihi kuhusu kupaka juu ya khofu na Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu wamesema kuwa ushahidi wa kupaka kwenye khofu umethibi kwenye hadithi za Mtume hadithi sahihi,na kupata kwenye khofu kuna kuwa kwa mtu alie zivaa khofu akiwa na udhu kama atava khofu bila udhu ni bora kuzivua kisha aoshe miguu kwa hiyo wakati swahaba wa Mtume Mughiyra alivyo kuwa anataka kumvua khofu Mtume, Mtume alimwambaia ziache mimi nimezivaa nikwa naudhu.

## Masharti Ya Kupaka Juu Ya Khofu Mbili

**1- Sharti la kwanza**: Anatakiwa awe imevaa khofu (Viatu vinavyo funika miguu yake yote) baada ya kumaliza kujitwaharisha na uchafu mkubwa kama janaba hedhi nifasi na awe amejitwaharisha na uchafu mdogo kama mkojo nk , na awe ametawadha kama atavaa viatu vya khofu akiwa hana udhu kamili, hairuhusiwi kupaka juu ya khofu.

**2- Sharti la pili:** anatakiwa apake katika muda maalum, tutalielezea hapo mbele Mwenyezi Mungu akituwezesha.

**3- Sharti la tatu:** Anatakiwa apanguse juu ya khofu kama atakuwa na uchafu mdogo unao mlazimu kutawadha, kama atakuwa na uchafu mkubwa unao mlazimu kuoga ni lazima kwa mtu huyo avue viatu hivyo na akoge mwili mzima kwa hivyo hairuhusiwi mtu afute akiwa na janaba nk, kama ulivyo kuja ushidi katika hadithi ya swafuwani Ibun Ghaasaal radhi za Mwenyezi Mungu zimuendee amesema: **((Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake, alikuwa anatuamrisha tukiwa safarini tusivue viatu vyetu vya khofu kwa muda wa siku tatu, usiku na mchana, isipokuwa tukipatwa na janaba)),** [126/ Nasai /96/ Atirmidhiy/ 17/ Ibun Khuzayma.

Hayo ndio masharti matatu katika masharti ya kupaka maji juu ya viatu vya khofu.

**Kuhusu muda**: Muda wa kupaka juu ya khofu kwa mtu ambae sio msafiri atapaka usiku na mchana na kwa msafiri atapaka kwa muda wa siku tatu usiku na mchana na kwenye kupaka haziangaliwi idadi ya swala kinacho anagaliwa ni muda, Mtume Muhammadi rehama na amani ziwe juu yake amesema**:** kwa mtu asio safarini ni usiku na mchana na msafiri ni siku tatu usiku na mchana.

Kwa hiyo asio safiri atapaka ndani ya masaa ishirini na nne (24) na msafiri atapaka ndani ya masaa sabini na mbili ( 72)

## Kupaka Kunaanza Muda gani?

Muda wa kupaka unaanza punde tu atakapo paka mara ya kwanza na muda hauanzi kuhesabiwa anapo vaa viatu wala atakapo kuwa udhu umeharibika baada ya kuvaa khofu kwa sababu sheria imetumia ibara ya kupaka na kupaka hakuthibiti hadi kitendo cha kupaka kifanyike **((Apake mtu asio safarini ni usiku na mchana na msafiri apake kwa muda wa siku tatu)) [276/** Swahihu Muslim], ni lazima kupatikane kupaka ndio muda uanze kuhesabiwa na muda utaanza kuhesabiwa akipaka mara ya kwanza yakikamilika masaa ishirini na nne kuwanzia alivyo paka mara ya kwanza muda wake wakupaka utakuwa umeisha, hii ni kwa mtu ambaye sio msafiri, kwa msafiri yakipita masaa sabini na mbili baada ya kupaka mara ya kwanza muda wa kupaka utakuwa umeisha:

**Tuna kupa mfano uweze kuelewa vizuri**: Mwanaume akitawadha kwa ajili ya swala ya Al-fajiri, kisha baada ya kumaliza kutawadha akavaa viatu vya khofu, akawa na udhu wake haujaharibika hadi kufikia mchana akaswali swala ya adhuhuri kwa udhu alio tawadha Swala ya Al-fajiri ikafika swala ya alasiri akiwa bado anaudhu Akaswali pia swala ya Alasiri kwa udhu alio tawadha swala ya Al-fajiri, baada ya kumaliza kuswali alasiri, saa kumi na moja jioni akatawadha kwa ajili ya kuswali swala ya magharibi kisha akapaka kwenye viatu vyake vya khofu mtu huyo anaruhusa ya kupaka kwenye viatu vya khofu hadi kesho yake saa kumi na moja jioni,kama ikitokea kuwa amepaka maji kwenye viatu mara ya kwanza siku ya pili saa kumi na moja kasoro (4:45) akaendelea kuwa na udhu akaswali magharibi na ishaa atakuwa ameswali katika muda wa swala ya adhuhuri siku ya kwanza na atakuwa ameswali alasiri,na magharibi, na ishaa, na Al-fajir, siku ya pili, na adhuhuri na Alasiri magharibi na ishaa kwa hiyo atakuwa Ameswali swala nyingi kwa hivyo haizingatiwi idadi ya swala, kama wanavyo fahamu watu wengine kuwa kufuta kwenye viatu ni katika vipindi vitano vya swala, sheria imeweka kufuta kwa mtu asiye kuwa msafiri usiku na mchana masaa ( 24), muda unaanza baada ya kufuta mara ya kwanza na kwa mifano tuliyo ipiga umefahamu swala zilizo swaliwa.

Kwa mifano hii tuliyoieleza, umefahamu kuwa muda ikiisha hairuhusiwi kupaka juu ya khofu kama mtu atapaka baada ya kuisha muda udhu wake utakuwa ni batili, na kutawadha kwake kutakuwa hakujasihi, lakini kama atatawadha kabla ya kuisha muda kisha akapaka na udhu wake haukuharibika hata kama muda umekwisha atakuwa bado ana udhu wake unaendelea hadi utakapopaka kwa hiyo baadhi ya kauli kuwa udhu

unaharibika muda ukiisha hata kama haja tokewa na kitu kinacho haribu udhu kauli haina ushahidi, kuisha Maana ya muda ni haruhusiwi kupaka baada ya kuisha muda na siyo kuwa udhu wake unaharibika baada ya kuisha muda, hakuna ushahidi kuwa udhu unaharibika baada ya kuisha muda, tunasema: kwa kurudia kuutaja ushahidi ambao tumeelekeza hoja zetu mtu akitawadha udhu sahihi kwa muJibu wa sheria iliyo sahihi, hauwezi kusema kuwa udhu wake umeharibika isipokuwa kwa ushahidi wa kisheria uliyo sahihi na hakuna ushahidi kuwa kuisha muda udhu unakuwa umeharibika kwa hivyo atabaki kuwa na udhu hadi kitakapo patikana kinacho haribu udhu, ambacho kimethibiti katika Qur`an au Sun`na au Ijmai (Makubaliano ya Wanachuoni).

Kuhusu msafiri atapaka kwenye khofu kwa muda wa siku tatu usiku na mchana masaa sabini na mbil ( 72) muda unaanza baada ya kupaka mara ya kwanza kwa hivyo wameeleza Wanachuoni wa madhehebu ya hanbali Mwenyezi Mungu awarehemu kuwa kama mtu atavaa khofu na akawa sio msafiri kisha udhu wake ukaharibika kabla yakusafiri na hakutawadha kisha akasafiri akapaka akiwa safari mtu huyo atapaka siku tatu kama msafiri, na hili linatufahamisha udhaifu wa hoja ya kuwa muda unaanza baada ya kutengeka udhu akiwa amevaa khofu na sio baada ya kupaka.

Mambo ambayo yanaharibu udhu wa mtu aliye vaa khofu, kuisha muda wa kupaka na kuvua khofu, akivua khofu haruhusiwi kupaka tena kwenye khofu lakini udhu unakuwa bado upo mpaka utakapo haribika au mtu akivua khofu haruhusiwi kupaka, hadithi ya Swafuani bin Ghasaal radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! amesema: **((Ametuamrisha**

**Mtume rehma na amani za Mwenyezi Mungu, tusivue khofu zetu))** [276 /sahihi Muslim].

Inatufahamisha kuwa kuvua khofu kuna batilisha ruhusa ya kupaka, mtu akivua khofu baada ya kupaka haruhusiwi kupaka tena maana yake asiivae hiyo khofu kisha apake, isipokuwa akitawadha udhu mwengine ulio kamili na aoshe miguu yake.

Kuhusu udhu atakapo vua khofu udhu unaendelea kuwepo, udhu hauharibiki kwa kuvua khofu kwa kuwa mtu anaye paka anapopaka udhu unakuwa umekamilika kwa muJibu wa ushahidi wa kisheria, udhu wa mtu aliye paka hauezi kuharibikia isipokuwa kwa ushahidi wa kisheria na hakuna ushahidi unao thibitisha kuwa mtu akivua udhu unaharibika ushahidi uliopo ni kuwa mtu akivua haruhusiwi kupaka tena hadi atakapo tawadha udhu kamili na aoshe miguu yake mpaka vifundoni tunasema: Udhu utaendelea kuwepo kwa muuJibu wa sheria mpaka itakapo patikana ushahidi wa kisheria kuwa udhu unaharibika, kama haukupatikana ushahidi udhu utaendelea kuwepo na hauto haribika na hii ndio kauli iliyo na nguvu kwetu. Allah ndio Mjuzi.

****

**Swali la 145: Ni ipi hukumu ya kupaka juu ya soksi yenye tundu na soksi nyepesi?.**

**Jibu**: Inaruhusiwa kupaka juu ya soksi yenye tundu na soksi nyepesi ambayo inaonyesha rangi ya mwili, kwa kuwa kupaka juu ya soksi hakuna maana kuwa sehemu hiyo iwe imesitirika kwa sababu Mwanaume mwili wake sio uchi ya kuwa lazima aufunike makusudio niruhusa kwa wale ambao sheria imewawekea wepesi kiwango ambacho hatumlazimishi kuvua soksi au khofu wakati wakutawadha.

**Tunasema**: Inafaa kupaka juu ya soksi hizo tulizo zitaja hapo juu ndio sababu ambazo sheria imeweka jamabo hili kuwa ni halali kupaka, kama unavyo ona kuwa inalingana kupaka juu ya khofu na soksi zenye tundu na soksi zisizo na tundu soksi nyepesi na soksi nzito.

****

**Swali la 146: Ni ipi huhumu ya kupaka juu ya piopio (ogo)?.**

**Jibu**: Kwanza lazima mtu afahamu nini maana ya ogo?

**Ogo** ni kitu ambacho kina unga sehemu ilyo vunjika, na makusudio ya ogo kwa istilahi ya Wanachuoni**: ((Ogo ni kitu kinacho wekwa juu ya sehemu ilyo safi kwa haja))** Mfano kismenti kinacho wekwa juu ya sehemu iliyo vunjika au mtu amepata maumivu katika uti wamgongo na mamabo yanayo fanana na hayo, kupaka juu yake inafaa hata kwenye kuoga kama mtu atakuwa anakidonda kwenye mguu na mtu huyo akawa anahitaji kutawadha na bandeji juu ya kidonda anahitaji mtu huyo atapaka juu yake badala ya kuosha, na itakuwa hiyo ni twahara iliyo kamili kwa maana kama mtu ataondoa hilo ogo au bandeji baada ya kutawadha udhu wake utaendelea kuwepo mpaka utakapo haribika kwa sababu udhu wake ilikamilika kisheria, na kuondoa ogo hakuna ushahidi wa kisheria kuwa kunaharibu udhu pia hakuna ushahidi unao pinga kupaka juu ya ogo isipokuwa zipo hadithi dhaifu wamezielezea baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu amarehemu! wakasema: mkusanyiko wa hadithi hizo unazifanya kuwa ni hoja.

**Wapo Wanachuoni walio sema**: kwa udhaifu wake haiwezi kuwa hoja na wanzuoni walio sema hivyowametofautiana wapo wanao sema kuwa imepukutika kusafishwa sehemu iliyo fungwa ogo, kwa kuwa hawezi kupaosha.

**Wapo Wanachuoni wanao sema**: Atatayamamu sehemu hiyo na hato paka juu yake.

Kauli iliyo karibu na misingi ya kisheria na inayo toa mitazamo ya kuwangalia udhaifu wa hadithizilizo pokelewa kwenye jambo hilo nikuwa atapaka juu ya ogona kupaka huko kutatosheleza na hakuna haja ya kutayamamu **kwahivyotunasema**: Mtu akiwa na kidonda katika viungo vinavyo takiwa kuoshwa kuna daraja zake:

**1- Ki**donda kiwe kipo wazi na hapati madhara kuosha sehemu hiyo mtu huyo ni lazima kwake aoshe sehemu hiyo kama itakuwa katika viungo vinavyo takiwa kuoshwa.

**2-** Kidonda kiwe kipo wazi na anapata madhara kukiosha lakini hapati madhara kupaka juu yake daraja hii ni lazima kwa mtu huyo apake na asioshe.

**3-** Kidonda kikiwa wazi na anapata madhara kuosha sehemu hiyo pia anapata madhara kupaka hapo anatakiwa kutayamamu sehemu hiyo.

**4-** Kidonda kikiwa kimefunikwa kwa plasta au kitu kingine kama hicho na kukawa na haja ya kufunika sehemu hiyo daraji hii anatakiwa kupaka juu ya hiyo sitara na itakuwa imechukuwa nafasi ya kuosha na hato tayamamu.

****

**Swali la 147: Je ni lazima kukusanya kati ya kutayamamu na kupaka juu ya ogo?**

**Jibu:** Sio lazima mtu kukusanya kati ya kupaka na kutayamamu kufanya hivyo utakuwa umetawadha mara mbili katika kiungo kimoja na jambo hilo linapingana na kanuni za kisheria tunasema: Ni lazima kusafisha kiungo kwa kutumia kuosha au kupaka au kutayamamu ama kusema kuwa ni lazima mtu kutumia twahara mbili jambo hilo halina mtazamo katika sheria na Mwenyezi Mungu! Hakika Mwenyezi Mungu hamlazimishi mja wake kufanya ibada mara mbili kwa sababu moja.

****

**Swali la 148: Ni ipi hukumu ya mtu aliye tawadha akaosha mguu wake wa kulia, kisha akauingiza kwenye khofu au soksi, kisha akaosha mguu wakushoto akavaa khofu au soksi?**

**Jibu**: Mambo hayo yana kauli nyingi kwa Wanazunoni Mwenyezi Mungu awarehemu, wapo wanao sema: Ni lazima akamilishe udhu wake ndio avae khofu au soksi.

**Wapo nanaosema**: Inafaa mtu akiosha mguu wa kulia anaruhusiwa kuvaa khofu au soksi kisha aoshe mguu wa kushoto na avae khofu au soksi, kwa sababu hakuingiza mguu wa kulia isipokuwa baada ya kukamilisha kuosha na mguu wa kushoto pia anakubaliwa mtu huyo kuwa amevaa viatu baada ya kukamilisha kutawadha isipokuwa kuna hadithi ameielezea daar Al-Qutumiy na haakimu na wamesema : kuwa ni hadithi sahihi kuwa Mtume Muhammmad rehma na amani ziwe juu yake alisema: ((**Atakapo tawadha mmoja wanu, akavaa viatu vyake vya khofu**)) [781/ daarl-Qutuniy, /181/1/ haakimu, /279/1/ al-bayhaqiyu ], Hadithi Kauli ya Mtume: ((**Atakapo tawadha**)) inaunga mkono hoja ya kwanza kwa kuwa hakuosha na mguu wakushoto mtu huyo hawezi kukubaliwa kuwa ametwadha udhuu kamili na hiyo ndio hoja yenye ngunvu.

****

**Swali la 149: Mtu akiwa sio msafiri akapaka kisha akasafiri atapaka kama msafiri?.**

Jibu: Kama akiwa sio msafiri kisha akasafiri mtu huyo atapaka kama msafiri kwa kauli iliyo na nguvu wameelezea baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu kuwa mtu asio kuwa msafiri akipaka kisha akasafiri atakamilisha kupaka kama mtu ambaye sio msafiri lakini kauli iliyo na nguvu ni hiyo tulio ieleza kwa kuwa mtu huyo imebaki muda wa kupaka kwake kabla hajasafari kwa hiyo inakubalika kuwa yumo katika wasafiri, wanao takiwa kupaka siku tatu na ameeleza Imamu

Ahmadi Ibun Hanbaliy rehma na amani ziwe juu yake! kuwa amefuta kauli yake ya kwanza kuwa mtu huyo atapaka usiku na mchana asio kuwa msafiri ameeleza kauli hiyo katika kitabu [97/1/ Masaail Al-fiqihiya].

****

**Swali la 150: Mtu akiwa na shaka muda alio anza kupaka atafanyaje?**

**Jibu:** katika hali hiyo mtu atajengea kwenye uhakika mtu akitia shaka amepaka muda wa swala ya adhuhuri au alasili atachukuliwa kuwanza muda swala ya alasili kwa kuwa asili ni kuto kupaka na ushahidi wa hilo ni kanuni ya kisheria **((Asili hubaki kuwa vile vile))** na asili katika hili ni kuto kupaka.

Na Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake kuna mtu alimshatakia kuwa anahisi kuwa umetokwa na upepo sehemu yake ya haja kubwa akasema Mtume: ((**Asiondoke kwenye swala mpaka atakapo sikia sauti au atakapo sikia harufu**)) [137/ Sahihi Bukhary /361/ Sahihi Muslimu].

****

**Swali la 151: Mtu akipaka juu ya viatu vya kike vilivyo inuka kwa nyuma vilivyo funika vidole vya miguu kisha akavua akapaka juu ya soksi fupi hivi inaruhusiwa kupaka juu yake?.**

Jibu: Jambo linalo fahamika kwa wanzuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, mtu akipaka juu ya khofu mbili ya juu au ya chini hukumu inakuwa imefungana na jambo hilo na hatohamia kwenye ya pili wapo Wanachuoni wanaosema: kuwa hukumu inahamia kwenye ya pili kama inayo pakwa ni ya chini na muda ukawa bado upo na hii ndio kauli iliyo na nguvu kwa misingi hiyo kama mtu atatawadha akapaka juu ya soksi kisha akavaa soksi nyingine au viatu vya kike vilivyo inuka kwa nyuma na vimefunika vidole vya miguu na akapaka juu yake haina tatizo kufanya hivyo kwa kauli iliyo na nguvu kama muda wakupaka bado unaruhusu lakini huhesabiwa muda alio anza kupaka mara ya kwanza na sio alio paka mara ya pili.

****

**Swali la 152: Mtu akivua soksi fupi naye akiwa ametawadha kisha akazivaa kabla ya udhu wake hauja haribika hivi anaruhusiwa kupaka juu ya soksi hizo?.**

**Jibu**: Akivua soksi fupi alizo vaa kisha akazirudisha naye akiwa bado anaudhu wake jambo hilo limegwanyika sehemu kuu mbili:

1- Kama itakuwa udhu wake ndio wa kwanza yani haujaharibika udhu wake baada ya kuvaa soksi hakuna tatizo kama atarudisha soksi hizo na atapaka juu yake.

2- Kama atakuwa na udhu lakini ameisha futa juu ya hizo soksi, haruhusiwi mtu huyo akizivua azivae tena kisha afute juu yake, kwasababu ni lazima azivae akiwa ametawadha kwa kutumia maji na twahara yake ni ya kupaka ibara hiyo inafahamika katika maneno ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu! Lakini kama mtu yoyote akisema kuwa akirudisha soksi nae akiwa bado anatwahara hata kama ni twahara ya kupaka juu ya soksi anaruhusiwa kuendelea kupaka muda ukiwa bado unaruhusu kauli hii inanguvu, lakini sifahamu kama kuna mtu yoyote aliye sema kauli hii, ninacho kusudia kuwa mimi sijaona kauli ya mtu aliesema kauli hiyo kama yupo mWanachuoni aliye sema kauli hiyo, hiyo kauli kwangu ndio kauli sahihi, kwa sababu udhu wa mtu aliye paka ni udhuu kamili ilikuwa inatakiwa waseme: kama kupaka ni juu ya kitu alicho kivaa, twahara yake ni yakuosha basi apake juu ya alichoalicho kivaa, kwenye twahara ya kupaka lakini sijaona mtu hata mmoja alie sema kauli hiyo. Mwenyezi Mungu ndio mjuzi.

****

**Swali la 153: Mtu aliye paka juu ya khofu baada ya kuisha muda na akaswali kwa udhu huo hukumu yake ni ipi?.**

**Jibu**: Ukiisha muda wa kupaka juu ya khofu mbili, kisha mtu akaswali baada ya kuisha muda kama itakuwa udhu wake uliharibika baada ya kuisha muda wa kupaka, naye akapaka baada ya kuisha muda ni lazima kwa mtu huyo arudie kutawadha udhu kamili na aoshe miguu yake, na nilazima kurudia kuswali swala aliyo swali akiwa na udhi wa kupaka, kwa sababu hakuosha miguu yake miwili mpaka vifundoni, ameswali bila udhu ulio kamilika, kama muda wakupaka utaisha na akaendelea kuwa na udhu wake akaswali kwa udhu huo baada ya kuisha muda swala yake ni sahihi, kwa ababu kuisha muda wa kupaka hakuharibu udhu.

**Wamesema**: Baadhi ya Wanachuoni kuwa muda wakupaka ukiisha udhu unarahibika lakini kauli yao haina ushahidi kwa hivyo muda wa kupaka ukiisha mtu akendela kuwa na udhu wake baada ya kuisha muda hata kama ni siku nzima anaruhusa ya kuswali hata kama muda umekwisha, kwa sababu udhu wake umethibiti kwa muJibu wa sheria na hauto haribika isipokuwa kwa ushahidi wa sheria na hakuna hadithi ya Mtume

Muhammadi rehma na amani ziwe ju yake! inayo fahamisha kuwa kuisha muda wa kupaka kunaharibu udhu. Mwenyezi Mungu ndio mjuzi zaidi.

****

**Swali la 154: Ni vipi vitenguzi vya udhu?**

**Jibu**: Vitenguzi vya udhu ni katika mambo yaliyo na ikhtilafu kwa Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu! Lakini tuta eleza mambo ambayo yanaharibu udhu kwa muJibu wa ushahidi :

**1-** Kutoka kitu sehemu za siri mbele au nyuma kila kitacho toka sehemu ya siri ya binaadamu iwe mbele au nyuma udhu wa mtu huyo unaharibika ukiwa ni mkojo au kinyesi au madhii au manii au upepo (mchuzi) kila kitu kitakacho toka sehemu za siri mbele au myUma kinatengua udhu, haihitaji kuuliza, lakini kama yatatoka manii kwa matamanio hilo linafahamika kuwa ni lazima mtu aoge, yakitoka madhii kwa mwanaume ni lazima aoshe umee wake, kama atakuwa ni Mwanamke ataosha sehemu zake za siri, pia atatawadha.

**2-** Jambo la pili linalo tengua udhu, kulala usingizi mwingi, kama atalala usingizi ambao hatofahamu mambo yanayo jiri hata kama akitokwa na udhu usingizi huo unatengua udhu, kama atalala usingizi mwepesi ambao anajielewa hata kikimtokea kitu, usingzi huo hauharibu udhu, hakuna utofauti ya kulala mtu aliye lala chali au aliye lala akiwa amekaa na amegemea kitu au amelala bila kuegemea kitu, kinacho angaliwa ni ufahamu , kama atakuwa amelala usingizi ambao kikimtokea kitu anahisi, usingizi huo hauharibu udhu,kama utakuwa usingzi ambao kama kikimtokea kitu hato hisi, usingizi huo unaharibu udhu, ni lazima akatawadhe kwa kuwa usingizi sio katika vinavyo haribu udhu lakini hudhaniwa kuwa kimekutokea kitu kinacho haribu udhu ukiwa umelala, kama uchafu utajificha kiasi ambacho mtu hahisi uchafu huo hauharibu udhu.

Ushahidi wa hayo nikuwa usingizi kama usingzi hauharibu udhu,na usingzi mdogo hauharibu udhu, kama usingizi ungekuwa unaharibu udhu basi unge haribu usingzi mdogo na usingizi mwingi kama unavyo haribu udhu mkojo mdogo na mkojo mwingi.

**3-** Jambo la tatu linalo haribu udhu kula nyama ya ngamia mtu akila nyama ya ngamia dume au jike udhu wake unaharibika, akila nyama ya kupika au mbichi kwa sababu imethibiti kwa Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake! katika hadithi ya Jabiri bin Samratu Anasema: ((Aliulizwa Atume Muhammad rehma na amani ziwee juu yake: tutawadhe tukila nyama ya kondoo? akajibu Mtume ((**Mkitaka**)) akaulizwa: Tutawadhe tukila nyama ya ngamia ? akaJibu (( **ndio**)) [360/ Sahi-

hi Muslim], Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Amefanya kutawadha kwa mtu aliye kula nyama ya kondoo anakhiyari akitaka atatawadha asipo taka hato tawadha pia kwenye hadithi hiyo kuna ushahidi kuwa aliye kula nyama ya ngamia hana khiyari ni lazima atawadhe kwa hivyo ni lazima mtu aliye kula nyama ya ngamia atawadhe, ikiwa nyama ya kupika au mbichi, hakuna utofauti kati ya nyama nyekundu na isiyo kuwa nyekundu kunaharibu udhu hata kula utumbo, maini, moyo, mafuta, na vingine na viungo vyote vya ngamia vinaharibu udhu kwa kuwa Mtume hakutenganisha, na anafahamu kuwa watu wanakula vitu vyote hivyo kama hukumu ingekuwa inatofautiana Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake! Ange bainisha, mpaka watu walifahamu hilo, pia sisi hatufahamu katika sheria ya Kiislamu, myama ambayo hukumu yake inatofautina kwenye viungo vyake,ima mnyama atakuwa halali kuliwa au atakuwa ni haramu kuliwa kuhusu hivi vinaharibu udhu, na hivi haviharibu udhu au hivi hukumu yake ni hii na hivi hukumu yake ni hii hayo hatuyafahamu kwenye sheria ya Uislamu hayo yanajulikana kwenye sheria ya wayahudi kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Nawale walio fuata dini ya kiyahudi tumewaharamishia kila mwenye kucha na katika ng`ombe na kondoo na mbuzi tumewaharamishia mafuta yao isipokuwa kwaile iliyo beba migongo yao au matumbo yao, au iliyo gandamana na mifupa**], [Suratul An'aam: 146].

Kwa hivyo wamekubaliana wanachuoni! kuwa mafuta ya nguruwe (kiti moto) ni haramu pamoja ya kuwa Mwenyezi Mungu hakueleza kwenye Qur`an, Mwenyezi Mungu ameleza nyama tu amesema Mwenyezi Mungu: **[Mmeharamishiwa nyamafu na damu na nyama ya nguruwe na mnyama alie chinjwa si kwajina la Mwenyezi Mungu]** [Suraat Maaida:

3]. Sifahamu khilafu katika Wanachuoni ya kuwa mafuta ya nguruwe si haramu, kwa hivyo tunasema: nyama iliyo tajwa kwenye hadithi ya kutawadha kwa mtu aliye kula nyama ya ngamia yanaingia mafuta ya ngamia na utumbo supu na vitu vingine.

****

**Swali la 155: Je kumgusa mwanamke kunatengua udhu?.**

**Jibu: S**ahihi kumgusa mwanamke hakuharibu udhuu kabisa isipokuwa kama atatokwa na kitu sehemu ya siri udhu utaharibika ushahidi wa haya ni hadithi ya Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake: **((Aliwabusu baadhi ya wake zake, akaenda kuswali hakutawadha))** [179 /Abuu Daud / 86 / Atil-midhiy /170/ Nasaai / 502 / Ibun Majah], asili ni kuto kutenguka udhu hadi tupate ushahidi sahihi wawazi kuwa udhu unatenguka kwa kuwa mtu ametawadha kwa muuJibu wa sheria na udhu wake umekamilika kwa muJibu wa sheria hauwezi kutenguka udhu isipokuwa kwa ushahidi wa kisheria.

**Kama mtu atasema:** kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Au mkawagusa wanawake].**

**Jibu:** Makusudio katika kauli ya Mwenyezi Mungu au mkawagusa wanawake ina maana ya tendo la ndoa kama ilivyo sihi kwa Ibun Abasi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, kisha katika aya (ufunuo) umeelezea mgwanyiko wa twahara ya asili na twahara ya mbadala na kunamgawanyiko wa twahara ndogo na kubwa na mgawanyiko wa sababu ya twahara kubwa na ndogo amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: **[Enyi mlio amini mnapo simama kwa ajili ya swala osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu na osheni miguu yenu mpaka vifundoni**] [Surat maaida: 6]. Hii ni twahara ndogo ya kutumia maji ya asili, kisha akasema Mwenyezi Mungu: [**Na mkiwa na janaba basi ogeni],** hii ni twahara kubwa ya asili ya kutumia maji, kisha akasema Mwenyezi Mungu: **[Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini au mmoja wenu ametoka chooni au mmewagusa wanawake hamkupata maji basi tayamamuni**] kauli ya Mwenyezi Mungu: **[Tayamamuni**] hii ni badala na kauli ya Mwenyezi Mungu **[Au mmoja wenu ametoka chooni**] hii inaweka wazi sababu ndogo na kauli ya Mwenyezi Mungu: **[Au mmewagusa wanawake**] hii inawekawazi sababu kubwa.

Kama tutachukulia kuwa kugusa mwanamke ni kwa mkono na sio tendo la ndoa itakuwa kwenye kauli ya Mwenyezi Mungu! Ametaja sababu mbili za twahara ndogo na amekaa kimya kutaja sababu ya twahara kubwa pamoja yakuwa Mwenyezi Mungu Amesema: [**Na mkiwa na janaba basi ogeni**] nahii

itakuwa inapishana na ufasaha wa Qur`an pia Aya itakuwa inatufahamisha kuwa **[Au mkawaingia wanawake]** ili aya iwee imekusanya sababu mbili za kulazimsha kujitwaharisha sababu kubwa na sababu ndogo na twahara mbili ndogo ya kuosha viungo vine na kubwa yakuosha mwili mzima na twahara ya badala ambayo ni kutayamamukatika viungo viwili tu kwasababu hailingani na twahara ndogo na kubwa.

Kwa hivyo kauli iliyo na nguvu mtu akimgusa Mwanamke udhu wake hauharibiki kabisa hata kama atamgusa kwa matamanio au bila matamanio isipokuwa kikitoka kitu, na kikitoka ni lazima kukoga kwa mtu huyo kama yatakuwa yametoka manii itakuwa ni lazima kuosha uume wake na kutawadha kama yatakuwa yemetoka madhii.

****

**Swali la 156: Mwalimu ambae anafundisha wanafunzi Qur`an na hakuna maji sehemu ya madrasa hiyo wala sehemu ya karibu na madrasa, na Qur`an haruhusiwi kuishika isipokuwa mtu aliye twahara watafanyaje?.**

**Jibu:** Kama kwenye madrasa hiyo hakuna maji na karibu na madrasa hiyo hakuna maji mwalimu anatakiwa kuwambia wanafunzi waje wakiwa wametawadha kwasababu anatakiwa kuushika Msahafu mtu aliye safi kama ilivyo kuja kwenye hadithi ya Omar bin Hazmu radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, Mtume alimuandikia ujumbe ((**Asiishike Qur`an isipokuwa mtu aliye safi**)), [534/ Al-Muwatwaa ya Imamu maaliki]. Makusudio ya twahara kwenye ujumbe huo, mtu ambae hana uchafu kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu: katika Aya (ufunuo) iliyo elezea kutawadha na kuoga na kutayamamu: Amesema Mwenyezi Mungu: [**Hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika taabu: bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema yake juu yenu ili mpate kumshukuru!**] [Surati Maaida: 6] katika kauli yake Mwenyizi Mungu **[Bali anataka akutakaseni].** Imetufahamisha kuwa kabla ya kujisafisha anakuwa sio safi, kwa misingi hiyo haruhusiwi mtu yoyote kugusa msahafu isipokuwa akiwa yupo safi ametawadha.

Baadhi ya wanachuoni Mwenyezi Mungu awaheremu, wameruhusu kwa watoto wadogo kugusa Qur`an na kuibeba kwa dharura ya kufanya hivyo na kwa sababu wao hawana ufahamu wa kutawadha lakini jambo bora ni kuwaamuru wanafunzi watawadhe wakishika msahafu wawe na twahara.

**Kauli ya muulizaji:** kuwa Qur`an haishiki isipokuwa walio twahiri nadhani anataka kutoa ushahidi kuwa aya hiyo kuwa ni lazima kujitwaharisha kwa ajili ya kuugusa msahafu na aya hiyo haijakusudia hivyo makusudio ya kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Hapana wakigusae ila walio takaswa].** [Suratul Waq-

iaa: 79], kitabu maknun, maana yake ni ubao ulio hifadhiwa na kauli ya: walio takaswa ni malaika kama angekuwa anakusudia walio takaswa, angesema Mwenyezi Mungu! walio safi au walio safika na Mwenyezi Mungu hakuwasema hivyo.

Kwa hivyo hairuhusiwi kugusa msahafu isipokuwa mtu awe na twahara lakini ni kwa ushahidi wa hadithi ambayo tumeieleza hapo nyuma ndio inayo tufahamisha hivyo.

****

**Swali la 157: Ni mambo yapi yanayo mlazimu mtu kuoga?**

Jibu: Mambo yanayo mlazimu mtu kuoga:

**1** -Kutokwa na manii kwa matanio akiwa amelala au akiwa macho lakini kama atakuwa amelala ni lazima kuoga hata kama hato hisi matamanio kwa sababu mtu alielala yanaweza kutoka manii na asihisi matamanio yanapo kuwa yakimtoka manii kwa hivyo ni lazima kuoga kwa vyovyote itakavyo kuwa.

**2**-Tendo la ndoa Mwanaume akifanya tendo la ndoa na mke wake akaingiza uume wake kwenye uuke wa mke wake au

akazidisha kwenye kuingiza uume wake ni lazima kuoga kwa ushahidi wa kauli ya Mtume: **((Maji kwa maji))** [ 343/ Swahihu Muslimu], maana yake Mwanaume akifanya tendo landoa na mkewe hadi akafika kileleni ni lazima wakoge.

Kauli ya pili ya Mtume : **((Atakae kaa kati kati ya miguu minne, kisha akamuingilia ni lazima wakoge))** [ 291/ Sahihi Bukhary, /348 Sahihi Muslim], hata kama hakufika kileleni ni lazima akoge na mambo haya na kusudia kukutana kimwili bila kufika kileleni watu wengi hawafahamu hukumu yake kuna baadhi ya watu inapita weki nzima anakutana kimwili na mke wake bila kufika kileleni (kukojoa) na haogi kwa kuto kufahamu hili jambo la hatari sana, ni lazima mtu afahamu sheria aliyo itelemsha Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake, mtu akifanya tendo la ndoa na mke wake hata kama hakufika kileleni ni lazima aoge kwa ushahidi wahadithi tulio itaja hapo juu.

**3-**Katika mabo yanayo mlazimu mtu kuoga , ni kutoka damu ya hedhi au nifasi mwanamke anapo ingia katikia hedhi kisha damu ya hedhi ikakata ni lazima aoge Amesema Mwenyezi Mungu: [**Na wanakuliza juu ya hedhi. Waambie huo niuchafu basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi wala msiwaingilie mpaka watwaharike, wakisha twaharika basi waendeeni alivyo kuwamrisheni Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu hupenda wanao tubu na hupenda wanao jitakasa**], [Suratul Baqara: 222].

Na kwa kuwa Mtume **((Alimuaamur mwanamke mwenye tatizo la kutokwa na damu, akikaa kiasi cha muda wa hedhi yake akoge))** [228/ Sahihi Bukhary /333/ Sahihi Muslim]. Na

mwanamke Mwenye nifasi nikama Mwanamke mwenye hedhi, naye pia ni lazima kuoga sifa za kuoga hedhi na ni fasi ni kama sifa za kuoga janaba.

Baadhi ya Wanachuoni rehma za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao kuwa ni vizuri kwa mwanamke anaye koga hedhi au nifasi atumie mkunazi kwa kuwa mkunazi unasafisha vizuri na unatakatisha.

Wameelezea pia baadhi ya Wanachuuoni kuwa katika mambo yanayo lazimu kuoga kifo, wakitoa ushahidi wakauli ya Mtume rehma na mani ziwe juu yake! kuwambia Wanawake ambao wanawaosha mtoto wao: ((**Waoshani mara tatu, au mara tano, au mara saba, au zaidi ya hivyo , kama tukiona kuna haja ya kuzidisha))** [1253/ Sahihi Bukhary, 939/ Sahihi Muslim].

Na kauli ya Mtume katika kisa cha mtu alie kufa katika kipandwa chake akiwa amehirimia katika ibada ya hija katika viwanja vya Arafaa ((**Muosheni kwa kutumia maji na mkunazi,na mumvishe katika nguo yake**)) [ 1265/ Sahihi Bukhary, 12/7/ Sahihi Muslim] .

Wakasema Wanachuoni: Kifo ni sababu ya lazima ya kuoshwa lakini ulazima wakumuosha unakuwa kwa watu aliyo baki hai kwa kuwa mtu akiisha kufa mambo ya lazima kwake yanaanguka kwa sababu ya kifo kwa walio baki hai ni lazima

wawaoshe ndugu zao walio kufa, kwa sababu ya kutekeleza amri ya Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake!.

****

**Swali la 158: Hivi ni lazima kuoga kwa kuchezeana mke na mume bila ya kufanya tendo la ndoa au kumbusu?.**

**Jibu: S**io lazima kwa Mwanamume au Mwanamke kuoga kwa kuchezeana au busu isipokuwa kama manii yatatoka ni lzima kuoga kwa wote kama manii yata kuwa yamewatoka wote yakitoka kwa mmoja ni lazima akoge huyo yalio mtoka peke yake kama itakuwa nikuchezeana na mabusu kukumbatiana na manii haya kutoka sio lazima kuoga.

Kama watafanya tendo la ndoa ni lazima waoge hata kama hawakufika kileleni kwa uthibitisho wa maneno ya Mtume katika hadithi aliyo isimulia Abuu Hurayra **((Akikaa katika ya miguu yake minne kisha akamuingilia ni lazima kuoga))** [291 / Sahihi Bukhary, 348/ Sahihi Muslim] ((**Hata kama hakufika kileleni**)). Mambo haya wanawake wengi hawayafahamu wanadhani baadhi ya wanawake na baadhi ya wanaume kuwa kama watafanya tendo la ndoa kama hawakufika kileleni sio

lazima kuoga na huu niujinga mkubwa mtu aliye fanya tendo la ndoa ni lazima aoge kwa hali yoyote kama halikufanyika tendo la ndoa na manii hayakutoka sio lazima kuoga.

****

**Swali la 159: Mtu akiamka kutoka usingizini akakuta unyevu nyevu, je ni lazima kwa mtu huyo kuoga?.**

**Jibu:** Atakapo amka mtu akakuta unyevu nyevu kuna hali tatu:

**1-** Akiwa na uhakika kuwa huo unyevu nyevu ni manii ni lazima kuoga akikumbuka kuwa ameota au hata kama hakukumbuka.

**2-** Akiwa na uhakika kuwa huo unyevu nyevu sio manii sio lazima kwa mtu huyo kuoga isipokuwa ni lazima kuosha sehemu hiyo kwa sababu hukumu yake ni ya mkojo.

**3-** Akiwa hafahamu kuwa huo unyevu nyevu ni manii au sio manii ? Kuna naelezo yafuatayo:

**1**-kama atakumbuka kuwa aliota wakati alipokuwa amelala ataufanya unyevu nyevu huo kuwa ni manii ataoga kwa ushahidi wa hadithi ya Ummu salama, radhi za Mwenyezi Mugu ziwe juu yake alipo muuliza Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake! Kuhusu Mwanamke anaye ota njozi kama anavyo ota njozi Mwanaume ni lazima kuoga kwa mwanamke huyo? AkaJibu Mtume: ((**Ndio, kama Mwanamke huyo ataona maji)),** [130/ Sahihi Bukhary, 311/ Sahihi Muslim], imetufahamisha kuwa ni lazima kuoga kwa mtu aliye ota njozi na akaona unyevu neyevu.

**2**-kama hakuota nyozi yoyote lakini kabla ya kulala alikuwa anafikiria mambo ya tendo la ndoa huo unyevu nyevu itakuwa ni madhii.

Kama kabla ya kulala hakufikiria tendo la ndoa kuna khilafu katika jambo hilo:

Wapo Wanachuoni walio sema: Ni lazima kuoga kwa ajili ya kuondoa shaka.

Wapo wanao sema: Sio lazima kuoga kauli hiyo ndio sahihi kwa kuwa asili ni kuto kuwepo ulazima wakuoga jambo linabaki kwenye asiliyake mpaka upatikane ushahidi wa kuwa ni lazima kuoga.

****

**Swali la 160: Ni zipi hukumu za mtu mwenye janaba?.**

**Jibu:** Hukumu za mtu mwenye janaba ni:

**1-** Nirahamu kwa mwenye janaba kuswali swala ya faradhi na swala ya sun`na, hata swala ya jeneza (kumswalia maiti) Amesema Mwenyezi Mungu: **[Enyi mlio amni ,mnapo simama kwa jili ya swala basi osheni nyuso zenu,na mikono yenu mpaka vifundoni**]. Na kauli yake Mwenyezi Mungu **[Namkiwa na janaba basi ogeni**], Surat Maaida: 6] .

**2-** Mwenye janaba ni haramu kutufu ( kuzunguka) kwenye Al-kaaba, kwa sababu kutufu kwenye Al-kaaba na kukaa msikitini, amesema Mwenyezi Mungu: [**Enyi mlio amini! Msikaribie swala mkiwa mmelewa, mpaka myaelewe mnayo yasema, wala hali mnajanaba,isipokuwa mmo safarini, mpaka mkog**e], [Surat Nisaa: 43].

**3-** Ni haramu kwa mwenye janaba kugusa msahafu, kwa kauli ya Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake : ((**Asiguse Qur`an isipokuwa mtu alie na udhu**)) [534/ Al-Muwatwaa].

**4-** Ni haramu kwa mtu mwenye janaba kukaa msikitini, mpaka atawadhe amesema Mwenyezi Mungu: **[Enyi mlio amini! Msikaribie swala mkiwa mmelewa mpka muelewa mnayo**

**yasema wala hali mna janaba, isipokuwa mmo safarini mpka mkoge],** [Surat Nisaa: 43].

**5-** Ni haramu kwa mtu mwenye janaba kusoma Qur`an, mpaka akoge ((**kwa kuwa Mtume alikuwa anawafundisha maswahaba Qur`an, muda ambao alikuwa hana janaba**)) [229/ Abuu Daud, 146/ Atrmidhiy, 265/ Nasaai /594/ Ibun Majah ].

Hayo ndio mambo matano yanayo muhus u mtu mwenye janaba.

****

**Swali la 161: Ni zipi sifa za kuoga ?**

**Jibu:** Sifa za kuoga zimegawanyika sehemu mbili :

**1-** Sifa za lazima, nazo auroweshe mwili wake wote kwa maji, anatakiwa asukutue mdomo na apandinshe maji puani mwili wake ukienea maji kwa hali yoyote uchafu mkubwa utakuwa umeondoka na twahara inakuwa imekamilika, amesema Mwenyezi Mungu: [**Na mkiwa na janaba basi ogeni ]**, [Surat Maaida: 6].

Sifa kamili, nako ni kuoga kama alivyo oga Mtume, mtu akitaka kuoga janaba kwanza anaosha viganja vyake vya mikono, kisha anaosha sehemu zake za siri, na uchafu ulio ganda sehemu zake za siri anauondoa, kisha anatawadha udhu kamili, kama tulivyo elezea kwenye sifa za udhu kisha ataosha kichwa chake kwa kutumia maji mara tatu akiroweshe vizuri kisha aoge mwili mzima hizi ndio sifa za kuoga kamili.

** **

**Swali la 162: Mtu akioga josho kubwa kama janaba au hedhi au nifasi na hakusukutua mdomo wala hakupandisha maji puani jee kuoga kwakwe kumesihii?.**

**Jibu**: Hakusihii kuoga kwa mtu huyo mpaka aweke maji kinywani na puani kwakuwa Mwenyezi Mungu amesema: [**Na mkiwa na janaba basi ogeni**] Ni lazima kuoga mwili mzima na ndani ya mdomo na pua ni sehemu ya mwili ni lazima paoshwe kwa sababu hiyo Mtume Muhammad aliamrisha kuweka maji mdomoni na kuyazungusha na kupandisha maji puani wakati wakutawadha kwa kuwa pua na mdomo vinaingia kwenye kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Na osheni nyuso zenu ]** [6/ Suraat maaida] kwa kuwa vipo ndani ya uso na uso ni lazima uoshwe na kuosha uso kwenye twahara kubwa ni lazima pia itakuwa ni lazima kuweka waji mdomoni na kuyazungusha na kupandisha maji puani.

****

**Swali la 163: Mtu akiwa na udhuru wakutumia maji atafanyaje ili aweze kupata twahara?**

**Jibu:** Mtu akiwa na udhuru wa kutumia maji kwa sababu ya kukosekana kwa maji au kwa madhara atakayo yapata akitumia maji, mtu huyo ataacha kutumia maji na atatumia mchanga atapiga kwa mikono yake juu ya ardhi kisha apake juu ya uso wake kwa kutumia mikono yake miwili kisha apake mkono wa kushoto juu ya mkono wa kulia na wa kulia juu ya wa kushoto, lakini ni kwa uchafu mdogo.

Kuhusu kujisafisha kwa ajili ya uchafu ulio toka mtu hato tayamamu hata kama uchafu huo utakuwa kwenye mwili au nguo au kwenye ardhi kwa kuwa kutwaharisha uchafu ulio toka tumboni makusudio yake ni kuondoa najisi yenyewee haikusudiwi ibada na hakuna masharti kwa hivyo kama itaondoka hiyo najisi yenyewe bila mtu kukusudia kuiodosha shemu hiyo itakuwa imesafika, kwa mfano kama mvua itanyesha juu ya sehemu yenye najisi au nguo yenye najisi, najisi ikaondoka kwa sababu ya maji ya mvua sehemu iyo itakuwa imesafika au nguo hiyo itakuwa imetwaharika hata kama mtu atakuwa halifahamu hili ni tofauti na twahara ya uchafu unao takiwa kuoga inakuwa ni ibada kwa kuwa mtu akioga anakuwa karibu na Mwenyezi Mungu mtukufu! Ni lazima ipatikane niya ya kulifanya hilo.

****

**Swali la 164: Mtu akiamka na janaba wakati wa baridi kali anaruhusiwa kutayamamu?.**

**Jibu**: Atakaye kuwa na janaba ni lazima kwa mtu huyo kuoga kwa uthibitisho wa kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Na mkiwa na janaba basi ogeni**]. [Suraat Maaida: 6], kama itakuwa ni usiku wenye baridi kali mtu hawezi kuoga maji ya baridi ni lazima ayapashe mto maji hayo kama itawezekana kama haitowezekana kuyapasha moto kwasababu ya kukosa vya kupashia moto katika hali hiyo atatayamamu akiwa na janaba na ataswali kwa kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini au mmoja wenu ametoka chooni, au mmewagusa wanawake na hamkupata maji basi tayamamuni vumbi liliyo safi, mpake nyuso zenu na mikono yenu hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika taabu, bali anataka kukutakaseni nakutumiza neema yake juu yenu ili mpate kushukuru ],** [Suraati Maida: 6]. Mtu akitayamama, anapokuwa na janaba husafika na kubaki kuwa anatwahara mpaka takapo pata maji akipata maji ni lazima aoge kama ilivyo thibiti katika ((Sahihi Bukhary)), katika hadithi ya Imraani Ibun Huseyni radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! Hadithi ndefu katika sehemu ya hadithi hiyo kuwa Mtume Muhammad alimuona mtu mmoja amejitenga hakuswali na watu wengine akasema Mtume kumuliza mtu yule: ((**kwanini hauswali?** )) mtu huyo akajibu: nimepatwa na janaba na mimi sina maji akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Tumia mchanga unakutosha**)) kisha yakapatikana maji baada ya swala Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake! Akampa mtu yule maji na akasema kumwambia: ((**Oga mwenyewe**)), [344/ Sahihi Bukhary, 682/ Sahihi Muslim]. Tu-

mefahamu kwenye hadithi hiyo kuwa mtu akitayamamu kisha akipata maji ni lazima ajisafishe tena kwa kutumia maji ikiwa ni janaba hata kama sio janaba, mtu aliye tayamamu huwa yupo safi mpaka atakapo pata janaba nyingine au apate maji kwa hivyo mtu alie kuwa na janaba hatakwi kurudia rudia kutayamamu kwa kila muda wa swala, isipokuwa atakuwa ana tayamamu kila akipata janaba na akipatwa na uchafu mdogo.

****

**Swali la 165: Je ni sharti mtu akitaka kutayamamu atumie mchanga wenye vumbi? Na vipi katika kaulia ya Mwenyezi Mungu: [Na mpake nyuso zenu na mikono yenu] na neno hili katika kauli ya Mwenyezi Mungu: [minhu] ni ushahidi kuwa ni sharti kupaka vumbi kwenye uso na miko?.**

**Jibu**: kutayamamu kwa kutumia mchanga wenye vumbi sio sharti la kusihi kutayamamu kwa kauli iliyo na nguvu, isipokuwa akitayamamu juu ya ardhi yenye vumbi au isio kuwa na vumbi inafaa kwa hivyo kama mvua itakuwa imenyesha juu ya ardhi mtu atapiga mikono yake miwili juu ya ardhi na atapaka kwa mikono hiyo uso wake na viganja vya mikono yake kama ardhi itakuwa haina vumbi katika hali hiyo kwa kauli ya Mwenyezi Mungu: **[basi tayamamu vumbi liliyo safi, na mpake nyuso zenu na mikono yenu].** [Suraat Maida: 6], na kwa kuwa Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake,

alikuwa akisafiri na maswahaba zake sehemu ambazo hakuna mchanga na mvua zilikuwa zikinyesha na walikuwa wakitayamamu kama alivyo wamrisha Mwenyezi Mungu, kauli iliyo na nguvu mtu akitayamamu juu ya ardhi kutayamamu kwake ni sahihi ardhi ikiwa na vumbi au ikiwa haina vumbi kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: **[Nampake nyuso zenu na mikono yenu.]** Neno katika hio aya lina maana ya kiwango na halina maana ya sehemu, imethibiti kuwa Mtume Muhammadi: **((Alipuliza kwenye mikono yake alipo ipiga juu ya ardhi**)), [ 338 / Sahihi Bukhary, 368/ Sahihi Muslim].

****

**Swali la 166: Mgonjwa ambaye hawezi kupata mchanga anaruhusiwa kutayamamu juu ya ukuta wa nyumba, au juu ya tandiko?.**

**Jibu:** Ukuta wa nyumba ni udongo mzuri ikiwa ukuta utakuwa umejengwa kwa kutumia mawe au matofali au udongo inaruhusiwa kutayamamu juu ya ukuta huo, lakini kama utakuwa umewekewa mbao au umepakwa rangi kama kutakuwa na vumbi au mchanga juu ya ukuta huo inafaa kutayamamu na inakuwa sawa na mtu aliye tayamamu juu ya ardhi kwa kuwa mchanga ni kitu cha ardhini na kukiwa hakuna vumbi wala mchanga juu ya kuta hizo haifai kutayamamu juu ya ukuta huo.

Kuhusu tandiko tunasema: kama kutakuwa na vumbi anaruhusiwa kutayamamu juu yake na kama hakuna vumbi haruhusiwi kwa kuwa tandiko sio mchanga.

****

**Swali la 167: Ni ipi hukumu ya mkojo wa mtoto mdogo wakiume ukidondokea juu ya nguo?.**

**Jibu:** Kauli iliyo sahihi mkojo wa mtoto wakiume ambae chakula chake ni maziwa tu mkojo wake ni najisi ndogo nyepesi inatosha kumwagia maji juu yake maji yaenee sehemu yote uliopatwa na mkojo bila kusugua na kukamua kwa kuwa imethibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake!: ((**Alileteatewa mtoto mdogo wakiume akamuweka juu ya mapaja yake, mtoto akamkojolea, Mtume Muhammadi , akaomba maji akamwagia na hakupaosha))** [222/ Sahihi Bukhary, 286/ Sahihi Muslim].

Kuhusu mtoto wa kike ni lazima kuosha sehemu iliyo patwa na mkoja kwa kuwa asili ya mkojo ni najisi ni lazima kuosha umenyamubuliwa mkojo wa mtoto mdogo wakiume kwa sababu ya hadithi za Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake.

****

**Swali la 168: Mwanamke aliyevuka umri wa miaka khamsini anaona damu yake ya hedhi ikiwa na sifa inayo fahamika na mwanamke amevuka umri wamiaka khamsini anaona damu ya hedhi katika sifa isiyo fahamika anaona rangi ya kahawiya?.**

**Jibu:** Mwanamke ambaye anaona damu hiyo itakuwa ni hedhi sahihi kwa kauli iliyo na nguvu hakuna ukomo wa miaaka ya kutoka damu ya hedhi kwa hivyo zitathibiti hukumu za mwanamke mwenye hedhi kwa mtu huyo ataacha kuswali, kufunga,tendo la ndoa itamlazimu kuoga baada ya kukata damu na atatakiwa kulipa funga ya Ramadhan na mambo mengine.

Mwanamke ambaye anaona uchusichusi , au rangi ya kahawiya kama ataviona katika muda wake wa hedhi hiyo itakuwa ni hedhi ikiwa sio katika muda wake wa hedhi hiyo sio hedhi , ikiwa damu yake ni damu ya hedhi inayo fahamika lakini imewahi kutoka kabla ya siku zake au imechelewa kutoka, hilo halina tatizo damu zikianza kutoka itakuwa ni hedhi na zikikata atakoga na hii ndio kauli sahihi hakuna ukomo wa umiri wa kotokwa na damu ya hedhi lakini kwa madhehebu ya Imamu Ahmadi Ibun Hanbali Mwanamke hawezi kutoka hedhi baada ya kufikisha umri wa miaka zaidi ya khamsini mwanamke akitokwa na damu nyeusi inayo fahamika kuwa ni ya hedhi na katika siku zake hufunga na kuswali na haogi itakapo katika lakini kauli hii sio sahihi.

** * *

**Swali la 169: Damu inayo mtoka Mwanamke mwenye mimba damu hiyo ni ya hedhi?.**

**Jibu:** Mwanamke mwenye mimba haingii katika siku zake za hedhi, kama alivyo sema Imamu Ahmadi bin Hanbal**: ((Wanawake wenye mimba hujulikana kwa kuto kutoka damu ya hedhi)),** kama walivyo sema wanachuoni : Mwenyezi Mungu ameiumba damu ya hedhi kwa hekma, damu ya hedhi ni chakula cha mimba katika tumbo la mama mjamzito, mimba ikitunga damu ya hedhi inakata lakini baadhi ya wanawake wachache hutokeya ikaenaendela kutoka na akawa anaona siku zake kama ilivyo kuwa kabla haja beba mimba mwanamke huyo hukumu yake hiyo itakuwa damu ya hedhi iliyo sahihi kwa kuwa damu ya hedhi imeendelea na haikuwathirika kwa sababu ya mimba hedhi hiyo itakuwa inamziwia kufanya kila kitu ambacho haruhusiwi kukifanya mwenye hedhi, na n ilazima kufanya mambo yanayo mlazimu mwenye hedhi, na kuto kufanya mambo ambayo haruhusiwi kuyafanya mwenye hedhi.

**Kwa Ujumla:** Damu inayo mtoka mwenye mimba imegawanyika sehemu mbili:

**1-** Damu ya hedhi inayo endelea kutoka kama ilivyo kuwa inatoka kabla ya mimba, kwa kuwa huo ni ushahidi kuwa mimba haijaithiri chochote itakuwa hiyo ni damu ya hedhi.

**2-** Damu iliyo zuka kwa mwenye mimba kwa sabubu ya ajali au kubeba mzigo au kudondoka kutoka kwenye kitu, au mfano wa vitu kama hivyo hiyo damu sio hedhi huo ni mshipa wa irqi, uliyo njee ya fuko la uzazi huwa unatema damu kwa mwanamke akipata mshtuko, kwa hiyo ataendela kuswali na kufunga kwani yupo twahiri ( safi) .

****

**Swali la 170: Ni upi uchache wa siku za hedhi na ni upi wingi wake?.**

**Jibu:** Hedhi haina uchache wa masiku wala haina wingi wa masiku kwa kauli iliyo sahihi kwa kauli ya Mwenyezi Mungu: **[Na wanakuliza juu ya hedhi. Wambie huo niuchafu. Basi jitengeni na wanawake wakati wahedhi. Wala msiwakarbie mpaka watwaharike**], [Suratul Baqara: 222]. Mwenyezi Mungu hakuweka ukomo wa siku za hedhi isipokuwa ameweka ukomo wake ni kutwaharika, imetufahamisha kuwa sababu ya hukumu ni kuwepo na kuto kuwepo, hedhi ikiwepo hukumu inakuwepo , akitwaharika hukumu inaondoka, kisha kuweka idadi ya masiku ya hedhi hakuna ushahidi pamoja ya kuwa kunahaja ya kuliweka wazi kama kutokwa na hedhi kungekuwa na umri maalumu au muda maalumu kisheria jambo hilo lingewekwa wazi na Mwenyezi Mungu na Mtume wake Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake, kwa misingi hiyo Mwanamke akiona damu zinazo fahamika kwa Wanawake kuwa ni hedhi basi hiyo

damu itakuwa hedhi kweli, bila kukadiria muda maalumu, isipokuwa damu inayo endela kutoka kwa Mwanamke bila kukata au inakatika siku moja au siku mbili kwa Mwezi damu hiyo itakuwa damu ya ugonjwa.

****

**Swali la 171: Mwanamke aliye jisababishia kutokwa damu ya hedhi kwa matibabu na akaacha kuswali hivi atazilipa hizo swala?.**

**Jibu:** Hato lipa swala mwanamke ambaye amejisababishia kutokwa na damu ya hedhi kwa kuwa hedhi ni damu ambayo ikitoka hukumu inakuwepo kama vile angetumia dawa za kuzuia kutoka damu ya hedhi, ataswali na kufunga, na hato lipa siku alizo funga kwa sababu hayupo kwenye hedhi, hukumu yake inakuwepo hedhi ikiwepo na ispokuepo hakuna hukumu amesema Mwenyezi Mungu: **[Na wanakuliza juu ya hedhi wambie huo niuchafu**], [Suratul Baqara: 222]. Ukipatika huo uchafu hukumu yake inathibiti, na uchafu huo usipo patikana hukumu yake haithibiti.

****

**Swali la 172: Hivi anaruhusiwa Mwanamke mwenye hedhi kusoma Qur`an?.**

**Jibu**: Anaruhusiwa mwanamke mwenye hedhi kusoma Qur`an kwa haja, mfano akiwa ni mwalimu anasomesha Qur`an au Mwanafunzi anasoma Qur`an kwa ajili ya kujifunza, au mama anawafundisha watoto wake wadogo au wakubwa, muhimu kuwe kunahaja ya Mwanamke mwenye hedhi kusoma Qur`an, inafaa na hakuna shida pia kama atahofia kuwa atasahau akiwa amehifadhi, akawa anasoma kwa ajili ya kujikumbusha anaruhusiwa hata kama atakuwa kwenye hedhi.

Baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu! Wamesema : Anaruhusiwa Mwanamke mwenye hedhi kusoma Qur`an bila ya haja yoyote.

Wanesema: baadhi ya wanachuoni: Ni haramu kwa Mwanamke mwenye hedhi kusoma Qur`an, hata kama anahaja.

Kauli zote tatu, ambayo inatakiwa ni kuwa Mwanamke mwenye hedhi akiwa nahaja ya kusoma Qur`an kwa ajili ya kufundisha au kufundishwa au akahofia kusahau hakuna ubaya kwa mwanamke huyo kusoma Qur`an akiwa kwenye hedhi.

****

**Swali la 173: Ikichanganyika damu ya Mwanamke hakufahamu kati ya damu ya hedhi na damu ya ogonjwa, atafanyaje?.**

**Jibu:** Asili ya damu inayo mtoka Mwanamke ni damu ya hedhi mpaka ibainike kuwa ni damu ya ugonjwa kwa hivyo akiona damu ataendela kuzingatia kuwa ni hedhi mpaka itakapo mbainikia kuwa ni damu ya ogonjwa.

****

**Swali la 174: Mwanamke akingia katika siku zake za hedhi baada ya kuingia muda wa swala hukumu yake ni ipi? Na mwanamke akiingia kwenye hedhi atalipa swala?.**

**Jibu:** Ikitokea hedhi baada ya kuingia muda wa swala, kwa mfano againgia katika hedhi baada ya kukengeuka jua mchana kwa nusu saa Mwanamke huyo baada ya kUmalizika hedhi yake na kuoga atailipa hiyo swala ambayo muda wake umeingia akiwa yupo katika twahara, anasema: Mwenyezi Mungu: [**Hakika swala kwa waumini, ni faradhi iliyo wekewa nyakati maalum**]. [Suratu Nisaa: 103], hatolipa swala za wakati wa hedhi kwa kauli ya Mtume katika hadithi ndefu: ((**Si mkiingia kwenye hedhi hamswali na kufunga?**)). [304 /

Sahihi Bukhary].

Wamekubaliana Wanachuoni, Mwenyezi Mungu awarehemu, kuwa mwanamke halipi swala ambazo zimempita wakati akiwa kwenye hedhi.

Kama ataoga baada ya kukatika hedhi na ukawa umebaki muda wa kuweza kuswali rakaa moja au zaidi ya rakaa moja , ataswali katika muda huo ambao ameoga kwa uthibitisho wa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Atakae iwahi rakaa moja ya swala ya Alasiri kabla ya jua kuzama, huyo atakuwa ameidirki swala hiyo**)). [556/ Sahihi Bukhary, / 608/ Sahihi Muslim], mwanamke akitwaharaika muda wa alas iri au kabla ya jua kuzama au limebaki kidogo jua lizame, au wakati Wa kuchomoza jua kadiri ya kuswali rakaa moja , atatakiwa kuswali swala ya Al-fajiri na Alasiri.

****

**Swali la 175: Mwanamke ambaye alikuwa akiingia hedhi kwa muda wa siku sita kisha zikazidi siku zake za ada?.**

**Jibu:** Ikiwa ada ya mwanamke kuingia katika hedhi ni siku sita , kisha zikazidi akawa anaingia siku tisa au kumi au kumi na moja, Mwanamke huyo ataendelea kuwacha kuswali mpaka atakapo twaharika (oga) kwa kuwa Mtume Muhammad i rehma

na amani ziwe juu yake, hakuweka muda maalum wa masiku ya hedhi, Amesema Mwenyezi Mungu: [**Na wanakuliza juu ya hedhi waambiie huo ni uchafu]** [222/ Surat Al-Baqara], kwa mwanamke akiendelea kutokwa na damu atakuwa bado yupo katika hedhi mpaka atakapo twaharika na aoge kisha aswali, kama mwezi utakao fwata itapungua idadi ya siku zake kuliko mwezi ulio pita, akitwaharika ataoga hata idadi ya miezi hiyo itakuwa imepishana, muhimu ni kuwa mwanamke akiwa kwenye hedhi haswali hedhi ikiendana na ada yake au zikipishana, au ada yake ikizidi au ikipungua, akitwaharika anaoga kisha ataswali.

****

**Swali la 176: Mwanamke ameingia kwenye ada yake ya Mwezi akatwaharika akaoga baada ya kuswali siku tisa, ikarudi damu ya hedhi, ikaendelea kutoka siku tatu, naye hakuswali siku hizo tatu, kisha akatwaharika, Akaswali siku kumi na moja, ikatoka tena hedhi katika siku za ada yake alio kuwa anaingia kila Mwezi, mwanamke huyo atarudia kuswali swala za masiku matatu au inazingatiwa kuwa alikuwa kwenye hedhi?.**

**Jibu:** Muda wowote ikitoka damu hiyo itakuwa ni hedhi hata kama ikiwa itatoka muda mrefu kuliko hedhi iliyopita au ikatoka kidogo, Mwanamke akingia kwenye hedhi akatwa-

harika, baada ya siku tano au sita au kumi, ikarudi ada yake mara ya pili mwanamke huyo atacha kuswali, kwa kuwa yupo katika hedhi, kila atakapo kuwa anatwaharika kisha hedhi inarudi ni lazima aache kuswali lakini kama damu itaendela bila kukata, au inakatika muda kidogo kisha inaendela, huyo atakuwa anadamu ya ugonjwa kwahivyo atakuwa anaacha kuswali siku zake za hedhi tuu.

****

**Swali la 177: Ni ipi hukumu ya maji maji ya rangi ya njano yanayo mtoka mwanamke kabla ya kutokwa na hedhi kwa muda wa siku mbili?.**

**JIBU:** Kama utatoka uchafu wa maji maji ya njano kabla ya kuingia katika siku zake hiyo sio hedhi kwa ushahidi wa kauli ya Umu Atwiya radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! Amesema: ((**Tulikuwa hatuhesabu uchafu wa njano na maji maji kitu chchote**)) [326 /Swahihi Bukhary] katika hadithi nyingine **((Tulikuwa hatuhesabu ujano na maji maji ya uchafu baada ya kutwaharika kitu chochote**)), [308/ Abuu Daudi].

Kama huo uchafu wa njano utatoka kabla ya hedhi kisha kukawa na umbali kati ya kutoka hedhi na huo ujano, hiyo sio hedhi lakini Mwanmke akifahamu kuwa huo uchafu na unjano unao toka ni utangulizi wa kutoka hedhi basi hiyo itakuwa

ni hedhi atacha kuswali na mambo mengine ambayo haruhusiwi kufanya akiwa kwenye hedhi.

****

**Swali la 178: Ni ipi hukumu ya uchafu wa njano na kahawiya unao mtoka mwanamke sehemu za siri baada ya kuoga hedhi?.**

**Jibu**: Matatizo ya wanawake kuhusu hedhi ni jambo ambalo halina ukomo, kwa sababu ya kutumia madawa ya kuzuia mimba na kuzuia kuingia kwenye hedhi,watu wazamani hawakuwa wanafahamu matatizo hayo, lakini kauli sahihi kuwa matatizo bado yapo tokea kuepo kwa wanawake, lakini yamezidi kwa sababu hiyo, imefikia mtu hajui la kufanya kwa sababu ya matatizo hayo ,kuna kanuni kuwa :mwanamke akitwaharika akawa na uhakika kuwa hedhi imekata akajiridhisha na zikatokea alama za kukatika hedhi nako ni kutoka kaupinde kadogo keupe , (**Nayo ni maji meupe wanayafahamu wanawake**) . Ukitokea uchafu au matone ya damu au unyevu nyevu hivyo vyote sio hedhi, ataendelea kuswali Na kufunga na kufanya tendo landoa na mume wake kwa kuwa hayupo kwenye hedhi amesema Umu Atwiya : Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: ((**Tulikuwa hatuhesabu uchafu na ujano kitu chochote))** [Swahihu Bukhariy] Na amezidisha katika upokezi Abuu Daudi **((Baada ya kuoga** )) upokezi wake ni sahihi.

Kwa ushidi huo tunasema: kitacho tokea baada ya kupata uhakika kuwa ametwaharika na akaoga katika mambo tulio ya taja havidhuru twahara ya mwanamke na havimziwi kuwacha kuswali kufunga na kukutana kimwili na mume wake lakini ni lazima asiharakishe mpaka aone kuwa ametwaharika, kwa sababu baadhi ya wanawake damu ipikungua tu anawahi kuoga kabla hajapata uhakika kuwa imekata, wake wa Maswahaba Mwenyezi Mungu awarehemu walikuwa wanawatUma watu kwa mama wa Waislamu Aisha pamba ikiwa na uchafu wa njano njano, anasema: ((**Msiharakishe mpaka muone maji meupe yametoka** **))** [320 / Sahihi Bukhary, 59/1/ Maaliki ].

****

**Swali la 179: Ni ipi hukumu ya kutumia vidonge kwa ajili ya kuzuia damu ya hedhi?.**

**Jibu**: Mwanamke kutumia vidonge vya kuzuia damu ya hedhi isitoke kama hakuna madhara ya kiafya, anaruhusiwa kutumia vidonge hivyo, isipokuwa kwa sharti mume amruhusu kutumia vidonge hivyo, lakini kwa ni navyo fahamu vidonge vya kuzuia hedhi vinamadhara kwa mwanamke upande wa afya, kwa kuwa hedhi hutoka katika hali ya kawaida na kitu kinachotoka katika uhalisia wake kikizuiliwa kinaleta madhara kwenye mwili pia kutumia vidonge vya kuzuia hedhi kunasababisha mwanamke kuto kufahamu ada yake ya kutoka hedhi, kunasababisha mwanamke kuwa katika wasi wasi wa kuswali

na kukutana kimwili na mume wake na mambo mengine , kwa hivyo mimi sisemi kuwa ni haramu kutumia vidonge vya kuzuia hedhi, lakini sipendi mwanamke atumie hivyo vidonge kwa kuhofia kuidhuru afya yake.

**Nami ninasema**: Inatakiwa mwanamke aridhike na alivyo pangiwa na Mwenyezi Mungu! Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake aliingia kwa mama wa Waislamu Aisha radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake mwaka alio hiji, hija ya kuwaga , akamkuta Aisha analiya, na Aisha alikuwa amehirimia ibada ya Umra, Mtume akasema kumuliza Aisha: ((**Unatatizo gani? Umeingia kwenye hedhi? AkamJibu ndio, Akasema Mtume : hicho ni kitu Mwenyezi Mungu amewandikia mabinti wa Adamu**)) [294 / Sahihi Bukhary, 1211/120/ Sahihi Muslim] anacho takiwa mwanamke awe mvumilivu na atarajie malipo kwa Mwenyezi Mungu, akipatwa na udhuru wa kuwacha kuswali na kufunga kwa ajili ya hedhi, ibada za kufanya zipo nyingi, kumtaja Mwenyezi Mungu! na kumsifu, kumsabihi, kutoa sadaka, kuwafanyia wema watu kwa kauli na vitendo, na hizo ni ibada bora .

****

**Swali la 180: Mwanamke anae tokwa na damu ya uzazi (nifasi) ikizidi siku arubaini je anaruhusiwa kuswali na kufunga?.**

**Jibu**: Wanawake wanao endelea kutokwa na damu ya uzazi zaidi ya siku arubaini damu hiyo ikiwa haikubadilika, kama siku zilizo zidi arubaini (40) itakuwa zimeingia katika siku za hedhi ambazo alikuwa anaingia hedhi kabla ya kuingia kwenye nifasi hiyo itakuwa ni hedhi, kama itakuwa siku zilizo zidi arubaini hazikukutana na siku zake za mwezi, Wanachouni Mwenyezi Mungu awarehemu! wametofautiana:

**Wapo wanaosema:** Ataoga na ataswali na kufunga hata kama damu itakuwa inaendelaa kutoka,damu hiyo itakuwa ni damu ya ugonjwa, sio damu ya uzazi.

**Wapo wanaosema:** Ataendelea kuwacha kuswali na kufunga na mambo mengine ambayo haruhusiwi kuyafanya mpaka zitimie siku sitini, (60) kwa sababu wapo wanawake wanatokwa na damu ya uzazi kwa muda wa masiku sitini, (60) na jambo hili lipo kwa sasa, pia walikuepo wanawake ada yao ya damu ya uzazi ni masiku sitini, (60) kwa misingi hiyo mwanamke akiwa anatokwa na damu ya uzazi ikivuka siku arubaini (40) ataendela kuwa katika damu ya uzazi mpaka zifike siku sitini, kisha baada ya hapo ataendelea kukaa katika siku zake za he-

dhi zikiisha ataoga na kuswali, kwa sababu atakuwa anatokwa na damu ya ugonjwa.

****

**Swali la 181: Mwanamke akitwaharika kutokana na damu ya uzazi kabla ya kutimia siku arubaini, (40) anaruhusiwa kufanya tendo la ndoa na mume wake? Na kama damu itarudi baada ya kupita siku arubaini ni ipi hukumu ya damu hiyo?.**

**Jibu:** Wanawake walio katika hali ya nifasi, (Damu ya uzazi) hairuhusiwi waume zao kufanya nao tendo la ndoa, Mwanamke akitwaharika ikifika siku arubaini ni lazima mwanamke huyo aswali na swala yake itakuwa sahihi, na anaruhusiwa mume wake kufanya naye tendo la ndoa, amesema Mwenyezi Mungu kuhusu hedhi**: [Na wanakuliza juu ya hedhi waambie huo ni niuchafu,basi jitengeni na wanawake katika hali ya hedhi wala msiwaingilie mpaka watwaharike, wakisha twaharika basi waendeeni alivyo kuwamrisheni Mwenyezi Mungu**], [Suratul Baqara: 222].

Kwa kuwa uchafu upo nao ni damu, hairuhusiwi kufanya tendo la ndoa, akitwaharika inaruhusiwa kufanya tendo la ndoa, kama ilivyo kuwa ni lazima aswali, pia ni lazima kufanya yote ambayo alikuwa haruhusiwi alivyo kuwa kwenye damu ya uzazi, pia tendo la ndoa anaruhusiwa kufanya lakini ni bora asubilie damu isije kutoka tena kwa sababu ya kufanya tendo la ndoa,

mpaka zitimie siku arubaini (40), lakini kama watafanya tendo la ndoa kabla ya kufika siku arubaini hakuna ubaya.

Mwanamke akiona damu baada ya kupita siku arubaini na baada ya kutwaharika, hiyo itakuwa ni damu ya hedhi, sio damu ya nifasi (ya uzazi) damu ya hedhi inafahamika kwa wanawake akihisi imetoka itakuwa ni hedhi, kama itaenedelea bila kukata itakuwa ni damu ya ugonjwa, atarejea kwenye kawaida yake ya mwezi ,,atacha kuswali na kufunga na mambo mengine asio ruhusiwa akiwa katika hedhi, na siku ambazo damu zitaendelea kutoka zaidi ya siku zake za mwezi, ataoga na kuswali hata kama damu itaendelea kutoka. Mwenyezi Mungu ndio mjuzi.

****

**Swali la 182: Mwanamke ambae mimba imeharibika ya miezi mitatu, mwanamke huyo ataswali? Au ataacha kuswali?**

**Jibu**: Jamabo linalo fahamika kwa wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu! Ni kuwa mwanamke ambaye mimba yake imeharibika ikiwa na miezi mitatu, mwanamke huyo hato swali kwa kuwa ikiharibika mimba ambayo imeisha anza kuonyesha omba la binaadamu, damu itayo toka itakuwa ni damu ya nifasi (damu ya uzazi) kwa hivyo hato swali kwa ajili ya damu hiyo inayo mtoka.

Wamesema baadhi ya wanachouni: Mimba inaweza kutengeneza ombo la binaadamu zitakapo timia siku thamanini na moja, (81) na siku thamanini na moja ni chini ya miezi mitatu, ikithibiti kuwa mimba imeharibika ni ya miezi mitatu, damu itayo toka itakuwa ni damu ya nifasi (damu ya uzazi) kama itaharibika chini ya siku thamanini, damu itakayo toka ni damu chafu, hato acha kuswali kwa sababu ya damu hiyo. Huyu mulizaji inabidi ajitambue Mwenyewe, kama mimba imeharibika kabla ya siku themanini, atalipa swala alizo ziacha, kama atakuwa hafahamu idadi ya miezi itabidi akadirie, na ajitahidi na atalipa swala ambazo dhana yake imepelekea kuwa hakuziswali.

****

**Swali la 183: Mtu ambaye atakuwa anatokwa na damu zisizo kata, ataswali vipi? Na vipi atafunga swaumu?**

**Jibu:** Mfano: mwanamke ambaye anatokwa na damu, hukumu yake atacha kuswali na kufunga , kipindi cha siku zake za ada ya mwenzi, kabla haijatokea hiyo damu isio kata, kama ada yake anatokwa na hedhi mwanzo wa mwezi kwa muda wa siku sita, atakuwa anakaa kila mwanzo wa mwezi siku sita haswali na kufunga, zikiisha siku sita ataoga na ataswali na atafunga.

Namna ya kuswali mwanamke huyo na watu wamfano wake, ataosha sehemu zake za siri mpaka pasafike vizuri, kisha apafunge vizuri, atawadhe, aswali, atakuwa anafanya hivyo kila akitaka kuswali swala ya faradhi na swala za sun`naa abazo zipo njee ya muda wa swala za faradhi, kwa hali hii ya dharura anaruhusiwa kukusanya swala ya adhuhuri na swala ya alasili, au kinyume chake, swala ya magharibi na swala ya ishaa, au kinyume chake, mpaka awe amefanya ibada mbili kwa wakati mmoja kati ya swala ya adhuhuri na alasili, na kati ya magharibi na ishaa, na swala ya Al-fjiri peke yake, kinyume na badala ya kuswali mara tano ataswali mara tatu. Mwenyei Mungu ndio hukubali mambo.

****

**Swali la 184: Ni ipi hukumu ya swala? Na swala ni lazima kwa kwa mtu gani?.**

**Jibu:** Swala ni nguzo muhimu katika nguzo za Kiislamu, isipokuwa ni nguzo ya pili baada ya shahada mbili, swala ni nguzo inayo tendwa na viungo, na dio msingi wa Uislamu, kama ilivyo thibiti kwa Mtume Muhammadi herma na amani ziwe juu yake amesema: **((Msingi wa Uislamu ni swala))** [ 231 / 5 / Musnadi Imamu Ahmadi] Mwenyezi Mungu ameifaradhisha swala kwa Mtume wake Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake! sehemu tukufu alio fika mwanadamu, katika usiku bora, bila kupitia kwa mtu yoyote wala kupitia Malaika, Mwenyezi

Mungu ameifaradhisha swala kwa Mtume wake Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake swala khamsini kwa usiku na mchana lakini Mwenyezi Mungu aliwapunguzia waja wake mpaka zikafika swala tano kwa idadi ya swala khamsini katika mizani, jambo hili linatufahamisha umuhimu wa swala na mapenzi ya Mwenyezi Mungu kuipenda hiyo swala, inapendeza sana mwanaadamu kuutumia muda wake mwingi katika swala, swala imethibiti ulazima wake katika Qur`ani, na mafundisho sahihi ya Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake! Na makubaliano ya Waisalamu wote .

Thibitisho la ulazima wa swala katika Qur`aani, Amesema Mwenyezi Mungu: **[Na mnapo tulia basi simamisheni swala kama dasturi. Kwani hakika swala katika waumini ni faradhi ilo wekewa nyakati maalum**], [Surat Nisaa: 103].

Asema Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake kumwambia Muadhi bin Jabali, wakati Mtume alivyo mtUma kwenda Yemeni: ((**Wafundishe kuwa Mwenyezi Mungu ame-FarAdhisha juu yao swala tano siku zote usiku na mchana))** [1395/ Sahihi Bukhary, Sahihi Muslim / 19].

Wamekubaliana wanachuoni kuwa swala ni lazima wamesema wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu.

Mtu akipinga ulazima wa swala tano, au ulazima wa swala moja katika swala tano, Mtu huyo atakuwa kafiri ametoka kwe-nye Uislamu, ni halali kuuwawa na mali zake pia, isipokuwa mpaka akitubuu kwa Mwenyezi Mungu, kama hatokuwa mtu

alie silimu hafahamu alama za Uislamu chochote, huyo atakuwa na udhuru kwa kuwa hafahamu, kisha atafunzwa, kama ataendela kupiga ulazima wa swala baada ya kufunzwaa mtu huyo atakuwa kafiri.

Ni lazima kuswali kwa kila Muislamu aliye fikiya baleghe, mwenye akili tImamu, Mwanaume au Mwanamke.

Mwislamu kinyume chake ni kafiri, sio lazima kwa kafiri kuswali, kwa maana haimlazimu kafiri kuswali kwa muda ambao bado yupo katika ukafiri pia sio lazima kwa kafiri kulipa swala baada ya kusilimu kuingia katika Uislamu, lakini ataadhibiwa siku ya kiyama kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: **[Isokuwa watu wa kuliani, watakuwa katika mabustani wakiulizana wao kwa wao, juu ya watu wabaya, ni kipi kilicho kufikisheni katika moto? watasema: hatukuwa miongoni mwa walio kuwa wakiswali, wala hatukuwa tukiwalisha masikini. Na tulikuwa tukibobeya katika maasi pamoja na walio kuwa wakibobea. Na tulikuwa tukikadhibisha siku ya malipo.]** [Surat Mudathir: 46], kauli ya Mwenyezi Mungu**: [Hatukuwa miongoni mwa walio kuwa wakiswali]** Inatufahamisha kuwa wameadhibiwa kwa sababu ya kuwacha kuswali, na kupinga swala na siku ya malipo.

Mtu alie fikia baleghe, ni mtu ambaye amefikia kuona alama za kukuwa, kwa upande wa Mwanaume ni alama tatu (3) kwa Mwanamke ni alama nne (4):

**Ya kwanza**: Ni kutimiza umri wa miaka kumi na tano (15).

**Ya pili:** kutokwa na manii akiwa amelala au akiwa macho.

**Ya tatu**: kuota mavuzi pembeni ya sehemu za siri za mbele, hizi alama tatu zinapatikana kwa Mwanamke na Mwanaume.

**Inazidi alama ya nne:** kwa Mwanamke nayo ni hedhi, damu ya hedhi ni katika alama za kubaleghe.

Mwenye akili tImamu, kinyume chake ni mpungufu wa akili (Mwenda wazimu) ambaye hana akili katika hao wapo Wanaume watu wazima na Wanawake watu wazima ambao wamefikia kupoteza fahamu zao, watu hao sio lazima kwao kuswali, kwa kuwa hawana akili.

Wanawake wenye hedhi na nifasi, hawaruhusiwi kuswali kwa sababu ya hedhi, akingia kwenye hedhi au nifasi, basi kwa muda huo sio lazima kuswali, kwa hadithi ya Mtume Muhammadi rehma na amni ziwe juu yake kuhusu Mwanamke: ((**Hivi** m**kiwa na hedhi hamswali na hamfungi)),** [304/ Sahihi Bukhary].

****

**Swali la 185: Mtu aliye poteza kumbukumbu na mtu aliye zimia je watu hao wawili yana walazimikia mambo ya kisheria?**

**Jibu:** Mwenyezi Mungu amefaradhisha kwa binaadamu wafanye ibada kama mtu akuwa amefika hali ya kuwa ni lazima kwake kufanya hiyo ibada, kama akiwa na akili tImamu anafahamu mambo inakuwa ni lazima kwake kufanya ibada, kama takuwa hana akili tImamu sheria haimlazimishi kufanya ibada kwa hivyo sio lazima kwa mwenda wazimu na mtoto mdogo ambaye hajajitambua, wala mtoto ambaye hajafikia baleghe, na hiyo ni rehma ya Mwenyezi Mungu, pia na mfano wa mtu ambaye anapoteza kumbukumbu ambaye amepata tatizo la akili lakini haijafikia kiwango cha wenda wazimu, pia na mtu mzima ambaye amepoteza kumbu kumbu, sio lazima kwake kuswali na kufunga kwa kuwa mtu aliye poteza kumbukumbu anakuwa kama mtoto mdogo ambaye hajajitambua hakuna jambo linalo kuwa ni la lazima kwake.

Kuhusu mambo ya lazima kuhusu mali, ni lazima kweye mali yake kutolewa haki ya mali hata kama atakuwa amepoteza kumbukumbu.

Kwa mfano ni lazima zaka itolewe kwenye mali yake, pia ni lazima kwa msimamizi wa mali ya mtoto mdogo au msimamizi wa mali ya mwenda wazimu atowe zaka ya mali, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu: [**Chukuwa sadaka katika mali zao, uwatwaharishe na uwatakase kwazo ].** [Surat Tauwba: 103], na kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa Muadhi alivyo mtuma kwenda Yemeni**: ((Wafundishe kuwa Mwenyezi Mungu amewafaradhishia juu yao sadaka katika mali zao inachukuliwa kutoka kwa matajiri, wanapewa mafakiri))**.

[1395/ Sahihi Bukhary], kwa hivyo waJibu wa mali hauanguki kwa sababu ya kupoteza kumbukumbu, ama ibada ya mwili kama swala na twahara kufunga hivyo vinaanguka kwa mtu aliye poteza kumbukumbu kwa kuwa hana akili.

Mtu ambaye amepoteza akili kwa kuzimia kwa ajili ya maradhi au mfano wa maradhi, mtu huyo sio lazima kuswali, kwa kauli ya Wanachuoni walio wengi, Mwenyezi Mungu awarehemu, mtu akizimia kwa muda wa siku mbili hatolipa swala, kwa kuwa hana akili,na sio kuwa amelala, kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Mtu atakeye pitwa na swala kwa sababu ya kulala au akasahau , basi na aswali atakapo kumbuka**)), [597/ Sahihi Bukhary /684 Sahihi Muslim] kwa kuwa aliye lala anaufahamu kwa maana anaweza kuwamka akiamshwa, ama mtu ambaye amezimia hawezi kuwamaka akiamshwa, kama atakuwa amezimia bila sababu, kuhusu mtu ambaye amezimia kwa sababu yake mwenyewe,kwa mfano amezimia kwa kutumia madawa ya kulevya mtu huyo atalipa swala ambazo zimempita wakati amezimia. Mwenyezi Mungu ndio mjuzi.

****

**Swali la 186: Mwanaume ambaye anamiezi miwili hajitambui kwa chochote hakuswali wala hakufunga Ramadhani, mambo gani ya lazima kwake?**

**Jibu:** Sio lazima kwakwe kufanya kitu chochote kwa sababu hajitambui, lakini Mwenyezi Mungu akikadiria akajitambua ni lazima alipe funga ya Ramadhani, kama atakufa hatokuwa na dhambi, na hakuna jambo la lazima kwakwe, isipokuwa kama atakuwa katika watu wenye udhuru wa kuendelea kama watu wazima faradhi yake inakuwa kwa msimamizi wake, anatakiwa msimamizi wake awape chakula masikini kila siku katika Mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Kuhusu kulipa swala wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu wanakauli mbili:

**1-Kaulia ya kwanza:** Ni kauli ya jamuhuri ya wanachuoni: Hakuna kulipa **((kwa kuwa Ibn Omari radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake alizimia usiku na mchana, hakulipa swala zilizo mpita**)), [1861/ Daar Al-qutwuny].

2**-Kauli ya pili:** Ni juu yake kulipa nayo ni kauli ya madhehebu ya wanachuoni wa Hambali wanachuoni wa madhehebu hayo wa sasa, wameeleza hayo katika kitabu cha (10/3, Al-Inswaafu) kwa upokezi kutoka kwa Amar Ibn **Yaasiri (( kuwa alizimia siku tatu alivyo pata fahamu alilipa swala zilizo mpita ))** [ 455 /4 / Ibun Mundhir katika Al-ausatwu.] **Imehaririwa 24/02/ 1394 H.**

****

**Swali la 187: Je mtu anaruhusiwa kuchelewesha swala kwasababu ya sharti katika mashart ya swala kama mtu kushughulika na kutafuta maji?.**

**Jibu:** kauli iliyo shihihi hairuhusiwi kuchelesha swala kutoka kwenye wakati wake kwa hali yoyote, isipokuwa mtu akihofia wakati wa swala utapita naye haja pata shart la kusihi swala kama kuwa hajapata maji ya kutawadha ataswali kwa hali yoyote, hata kama atakuwa anatarijia kupata sharti hiyo kwa muda wa karibu, kwa kuli ya Mwenyezi Mungu: **[kwani hakika swala kwa waumini ni faradhi iliyo wekewa nyakati maalum**], [Surat Nisaa: 103]. Pia Mtume rehma na amani ziwe juu yake aliweka nyakati za swala, na jambo hili linatufahamisha ulazima wa kuswali katika nyakati zake kama ingeruhusiwa kusubili sharti mpaka nyakati zake zikapita, kusinge sihi kuwanzishwa kutayamamu, kwa sababu uwezekano wa kupata maji baada ya nyakati za swala upo, na hakuna totofauti wa kuchelewesha muda mrefu au muda mfupi, kwa kuwa vyote nikuitoa swala katika wakati wake, na fatuwa hii ndio uchaguzi wa Sheikh Islamu Ibun Taymiya Mwenyezi Mungu amrehemu! [57 / 22 / Majmuu fatawaa ].

****

**Swali la 188: Anae kesha usiku na haswali Al-fajir ila baada ya kutoka muda wake, hivi swala yake inakubaliwa? Na ni ipi hukumu ya swala zake zingine?.**

**Jibu:** Ama swala ya Al-fajir anayo ichelewesha na kuswali nje ya wakati wake naye anaweza kuiswali katika wakati wake maalumu alio upanga Mwenyezi Mungu, kwa kuwahi kulala mapema, hakika swala hiyo haikubaliwi, kwa kuwa mtu akicheleweshа swala pasina udhuru wa kisheria kisha akaswali baada ya kupita muda wake swala hiyo haikubaliwi, kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Atakae fanya jambo ambalo hatukuliamuru jambo hilo halikubaliwi**)) [1718/ Sahihi Muslim]. Mtu ambaye anachelewesha swala mpaka anaswali nje ya wakati wake kwa makusudi huyo atakuwa kafanya jambo ambalo hakuliamuru Mwenyezi Mungu na Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake jambo hilo halikubaliwi.

**Anaweza kusema**: Mimi nimelala na Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Amesema: ((**Atakae kuwa amelala wakati wa swala au amesahau na aiswali atakapo kumbuka hakuna kafara isipokuwa hiyo**)) [597/ Sahihi Bukhary, 684 / Sahihui Muslim].

**Tunasema**: kama inawezekana kulala mapema ili amke mapema au aweke alamu ya kumuamsha au amuusie mtu atakaye muamsha, kama atachelewa kuswali naye hakutia umuhimu huzingatiwa kafanya makusudi kuchelewesha swala

na kaiswali njee ya wakati wake kwa hivyo haito kubaliwa Swala zingine atakazo ziswali ndani ya wakati wake zitakubaliwa.

**Nami nachukuwa nafasi hii kusema:** Ni lazima kwa kila Mwislamu afanye ibada kwa Ajili ya Mwenyezi Mungu, kwa hali ambayo Mwenyezi Mungu ataridhia ,kwa kuwa tumeumbwa kwa ajili ya ibada na mtu hafahamu kifo kinaweza kuja ghafla akaenda kuishi katika maisha ya kaburini maisha ya malipo maisha ambayo hakuna tena kufanya matendo kama alivyo sema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Anapo fariki mwanaadamu matendo yake yote yana simama isipokuwa mambo matatu: sadaka inayo endelea, au elimu yenye manufa, au mtoto mwema anae muombea dua)),** [1631/ Sahihi Muslim].

****

**Swali la 189: Anaechelewesha swala ya Al-fajir mpaka muda wake ukatoka.**

**Jibu:** Hao wanaochelewesha swala ya Al-fajir mpaka muda wake unaisha wakiamini kuwa ni halali kufanya hivyo hakika jambo hilo ni kumkufuru Mwenyezi Mungu! Kwa sababu atakaye amini kuwa ni halali kuchelewesha swala bila udhuru

mtu huyo ni kaafiri,kwa sababu ya kupinga Qur`ani na mafundisho sahihu ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake!Na makubaliano ya Waislamu.

Akichelewesha swala lakini hasemi kuwa ni halali kuchelewesha swala, mtu huyo atakuwa ni muovu kwa kuchelewesha swala, kwa sababu yamemzidia matamanio yake au umemzidia usingizi, ajitahidi mtu atubu kwa Mwenyezi Mungu, na aache alio kuwa akiyafanya, milango ya toba ipo wazi , Amesema Mwenyezi Mungu: **[Sema: enyi waja wangu walio jidhulumu nafsi zao! Msikate tama na rehema za Mwenyezi Mungu. hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote hakika yeye ni Mwenye kusamehe Mwenye hurUmaa**], [Surat Zumar: 53]. Mtu anaye wafahamu wanao chelewesha swala awape nasaha na awaelekeze kufanya kheri wakitubuu itakuwa ni jambo zuri ,kama hawakutubu afikishe habari zao kwa viongozi wanao husika na jambo hilo, ili awe ametakasika na jambo hilo na viongozi wanao husika wamtie adabu mtu huyo na watiwe adabu watu mfano wa mtu huyo ambaye anaacha kuswali bila sababu au anaye chelewesha swala .Mwenyezi Mungu atuwafikishe kuswali kwa wakati.

****

**Swali la 190: Mwanaume alichumbia binti wa mtu walivyo ulizia tabiya ya mwanaume huyo wakaambiwa haswali muhusika akajibu Mwenyezi Mungu amuongoze hivi inaruhusiwa kumuozesha mtu huyo?.**

**Jibu:** Anaye chumbia ikiwa haswali jamaa huyo ni faasiq, (muovu) amemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake amepinga makubaliano ya Waislamu kuwa swala ya jamaa ni katika ibada bora, amesema Sheikh Islamu bin Taimiya Mwenyezi Mungu amrehemu: [222 /23 Majmuu Fatawaa] ((**Wamekubaliana wanachuoni kuwa swala ya jamaa ni katika ibada bora ya lazima, na ibada inayo mfanya mtu awe karibu na Mwenyezi Mungu! ni katika alama kubwa za Uislamu**)), hayo ni maneno ya sheikh Islamu bin Taimiya Mwenyezi Mungu marehemu! lakini uovu huo haumtoi kwenye Uislamu, anaruhusiwa kuoa mwanamke wa kislamu, lakini asioe mwanamke mwenye msimamo wa dini na mwenye tabia nzuri kuliko mwanaume huyo hata kama wanaa mali chache familia ya mwanamke na familia ya muowaji wana mali nyingi, kama ilivyo kuja katika hatidhi ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Akiwajia mwanaume ambaye mmeridhia dini yake na tabia yake waozeshieni , wakasema ewee mjumbe wa Mwenyezi Mungu! hata kama ni masikini? akasema: Atakapo kujieni mnae ridhia dini yake na tabia yake Waozesheni))** Mtume alisema **mara tatu**, [1085/ Atirmidhi, / 1967/ Ibun Majah,/ 175/2/ Al-Haakim] .

Imethibiti katika swahihi Bukhary na swahihi Muslim na katika vitabu vingine, hadithi ya Abuu Hurayra radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake!kuwa Mtume rahma na amani ziwe juu yake! Amesema: **((Mwanamke huolewa kwa mambo**

**manne: kwa mali zake na familia yake na kwa uzur wake na kwa dini yake, chagua mwenye dini utakuwa umepatia katika uchaguzi wako**)). [5090/ Sahihi Bukhary, / 1466 / Sahihi Muslim], kwa muJibu wa hadithi hizi mbili inatakiwa mtu awe na malengo na kupupia kwenye kuoa au kuolewa achague mwenye dini na tabia nzuri, na mzazi ambae anamuogopa Mwenyezi Mungu na anachukuwa jukumu lake la ulezi ajitahidi kufata maelekezo ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Kwa sababu ataulizwa siku ya kiyama, amesema Mwenyezi Mungu: **[Na siku atakapo waita na akasema: MliwaJibu nini Mitume?**] [Suratul Qaswaswi: 65]. Akasema: [**Na kwa yakini tutawauliza wale walio pelekewa ujumbe na pia tutawauliza hao wajumbe. Tena tutawasimulia kwa elimu: wala sisi hatuta kuwa mbali**], [Suratul- A'arafu: 6-7].

Kama anaye chumbia haswali kabisa, swala ya jamaa hata akiwa peke yake haswali, huyo ni kafiri ametoka kwenye Uislamu, ni lazima afanye toba, akikubali kufanya toba na akaswali Mwenyezi Mungu atamkubalia toba yake kama toba yake itakuwa ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kama hakukubali kufanya toba atauwawa na atakuwa ni kafiri aliye toka kwenye Uislamu kwa kuritadi, atazikwa kwenye makaburi yasio kuwa ya Waislamu bila kumuosha wala kumvalisha sanda, na ushaihidi kuwa mtu asiye swali ni kafiri ushahidi upo kwenye matini ya Qur`ani, na matini ya hadithi za Mtume rehma na amani ziwe juu yake:

Ushahid katika Qur`ani, kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Lakini wakaja baada yao walio wabaya, wakapoteza swalana wakafuata matamanio basi watakuja kuta malipo ya ubaya.**

**Isipokuwa walio tubu na wakatenda mema]**, [Surat Mariamu: 59]. kauli ya Mwenyezi Mungu: **[Isipokuwa walio tubu na wakatenda mema**] Ni ushahidi kuwa alivyo puuza kuswali na kufuata matamanio hakuwa muumini.

Amesema Mwenyezi Mungu! : **[Basi wakitubu na wakasimamisha swala na wakatoa zaka basi ni ndugu zenu katika dini]**. [Surat Tauwba: 11], inatufahamisha udugu wa dini unathibiti kwa kusimamisha swala na kutoa zaka, lakini hadithi za Mtume zinatufahamisha kuwa atakaye acha kutoa zakka hatokuwa kafari , kama atakuwa anakubali kuwa kutoa zakka ni lazima, lakini amekuwa bakhili kutoa zakka, imebaki kusimamaisha swala ni sharti la kuthibitisha udugu wa imani, na hili inapelekea kuwa kafiri atakaye acha kuswali na kuvunja udugu wa imani, na mtu huyo hawi muovu au ukafiri sio mtoa kwenye Uislamu anakuwa ni kafiri ukafiri unao mtoa kwenye Uislamu, kwa sababu mwislamu muovu au akafanya madhambi yanayo itwa kuwa ni ukafiri hakumtoi kwenye imani yake,kama alivyo sema Mwenyezi Mungu katika sulhu ya makundi mawiliya waumili wanao pigana: **[Hakika waumini ni ndugu basi patanisheni kati ya ndugu zenu**], [Suratul Hujraati: 10]. Hawakutoka kwenye imani yao wanao pigana pamoja kuwa kupigana waumini kwa waumini ni ukafiri, kama ilivyo thibiti katika hadithi za Mtume rehma na amani ziwe juu yake! hadithi aliyo ipokeya Imamu Bukhariy Mwenyezi Mungu amrehemu! Wameipokea na wengine kutoka kwa Ibun Masoud radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! Amesema: ((**Kutukanana Waislamu ni muovu na kupigana ni ukafiri))**, [48/ Sahihi Bukhary, /64 / Sahihi Muslim].

Ushahidi katika Sunna, juu ya ukafiri wa mtu anaye acha swala, mfano kauli ya Mtume rahma na amani ziwe juu yake: ((**Hakika kati ya mtu na ushirikina na ukafiri ni kuwacha swala)),** [ 82/ Sahihi Muslim].

Na amepokea hadithi Imamu Muslimu , rehma za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! kutoka kwa Jaabir bin Abdillah radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! kutoka kwa Mtume rahma na amani ziwe juu yake!, na kutoka kwa Burayda bin Haswiyb Amesema : Nilimsikia Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Akisema: **(( Ahadi iliyo kati yetu na wao ni swala atakaye acha swala amekufuru)**)[ 346 / 5 Imamu Ahmadi, /2621 / Atirmidhiy, / 463/ Al-Nasaai,/ 1079 / Ibun Majah.].

Hadithi hii imepokelewa na watu watano (5) Imamu Ahmadi na watuzi wa vitabu vya sunani, Mwenyezi Mungu awarehemu, imepokelewa hadithi kwa Ubaada bin Swaamit radhi za Mwenyezi Mungu ziwee juu yake: ((**Walimuunga mkono Mtume kuwa hataacha kumtii kingozi mpaka watakapo ona ukafiri wa wazi, mtakuwa kwa Mwenyezi Mungu mna hoja**)), [1709/ Sahihi Bukhary] Maana yake: Wasiache kuwatii viongozi ambao Mweyezi Mungu amewapa utawala, mpaka waone ukafiri wa wazi kwa kiongozi huyo, kwakuwa umelifahamu hilo, angalia katika hadithi aliyo ipokea Imamu Muslim Mwenyezi Mungu marehemu kutoka katika hadithi ya Umuu Salama radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake kuwa Mtume rehma za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake alisema: **((Watakuongozeni watawala ambao mwawakubali na wapo mtakao wapinga atakaye wafahamu atatakasika atakaye ona ni munkari atasalimika lakini atakaye ridhia na kuwafuata, wakasema: tupigane nao? Akajibu hapana kwa**

**muda ambao wanaswali**)), [1854/ Sahihi Muslim]. Tumefahamu katika hadithii kuwa kama hawato swali wapigwee vita na hadithi ya Ubada radhi ya Mwenyezi Mungu iwee juu yake, kuwa asiache kuwatii viongozi hao, ni bora kuliko kuwapiga vita, isipokuwa mpaka wakiona ukafiri wa wazi, kunahoja kwa Mwenyezi Mungu! Katika hadithi hizi mbili, pia kuna ushahidi kuwa kuwacha swala ni kufuru hoja ya wazi na ni hoja kubwa kwa Mwenyezi Mungu!.

Huo ndio ushahidi kutoka katika Qur`an na Sunna kuwa kuwacha swala ni ukafiri unao mtoa mtu kwenye dini, kama ilivyo elezwa waziwazi katika hadithi alio ipokeya Abuu Haatimu katika sunan yake, kutoka kwa Ubada Ibun Swaamiti radhi za Mwenyezi Mungu ziwee juu yake amesema: alituusia Mtume wa Mwenyezi Mungu: ((**Tusimshirikishe Mwenyezi Mungu na chochote na tusiache swala kwa makusudi atakaye acha swala makusudi ametoka kwenye dini))** [ 216/4 Majmuu zawaid ya twabraniy].

Kauli za maswahaba na wema walio tangulia radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wamesema: Omar Ibun Khatwabu radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake**: ((Sio mwislamu atakae acha swala)),** [**39 /** maliki, / 902 / 3 Ibun Abiy Shayba katika tariykh madinna].

Amesema Abdullah Ibun Shaqiyqi Mwenyezi Mungu amrehemu: ((**Maswahaba wa Mtume walikuwa hawaoni kitu ambacho ukikiacha ni kufru isipokuwa swala))**, [2622/ Atirmidhiy], hadithi hiyo ameipokea Tirmidhiy na Haakimu na wame sema kuwa ni sahihi kwa masharti yao.

Umethibiti ushahidi na uwelewa ushahidi unao fahamisha kuwa kuwacha swala ni ukafiri pia na ushahidi wa mtazamo ulio sahihi, Amesema: Imamu Ihmadi Ibun Hanbali Mwenyezi Mungu marehemu: **((Mtu anayeichukulia swala kuwa ni jambo jepesi, huwa anaidhalilisha na anaikejeli Uislamu, Na heshma ya Uislamu ni kwa kaqiri mtu anavyo iheshimu swala na mapenzi yao katiki Uislamu ni kwa kadri ya mapenzi yao katika Uislamu ))**. Amesema Ibunul Qayyimu Mwenyezi Mungu amrehemu: katika kitabu (Aswalatu) [Ukurasa / 400, katika mkusanyiko wa hadthi]: ((hawezi kuwacha swala kwa muda mrefu mtu ambae anaamini kuwa Mwenyezi Mungu ndio alio amrisha watu wa swali, haiwezekani katika hali ya ada na tabia awe mtu amaani kwa dhati kuwa Mwenyezi Mungu amefharadhisha swala kwakwe usiku na mchana swala tano na ataadhibiwa adhabu kali kwa kuwacha kuswali, halafu mtu huyo akaendelea kuwacha kuswali jambo hilo haliwezekani, anaye dumu kuwacha swala hana imani kuwa swala ni lazima kwake, hakika imani inamuamuru mwenye nayo, kama atakuwa moyoni kwakwe hana imani inayo muamuru kuswali mtu huyo hana imani ,nawala hauwezi kusema mtu ambaye hana uzowefi wala maarifa na hukumu ya moyo na matendo)). Mwisho wa nukuu maneno ya Ibnul Qayyimu Mweyezi Mungu amrehemu, amesema kweli katika maneno yake

haiwezekani kuacha swala pamoja na wepesi wake na urahisi wake na malipo yake yalivyo makubwa , na ataadhibiwa anaye acha swala kwa makusudi, kisha mtu huyo bado awe na imani kuwa swala ni lazima jambo hilo haliwezekani.

Tumefahamu kwenye matini ya Qur`an, na matini ya hadithi ,kuwa atakaye acha swala ni kafiri ukafiri unao mtoa kwenye dini ya kislamu kwa hivyo si halali kumuozesha Mwanamke wa kislamu kwa mwanaume asiye swali, kwa ushahidi ulio katika matini ya Qur`an na makubaliano ya Wanachuoni, Amesema Mwenyezi Mungu: [**Wala msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini na mjakazi muumini ni bora kuliko mshirikina hata akikupendezeni**], [Suratul Baqara: 221].

Amesema Mwenyezi Mungu: **[Mkiwa mnawajua kuwa ni waumini basi msiwarejeshe kwa makafiri. Wanawake hao sihalali kwa hao makafiri wala hao makafiri hawahalalishwi wanawake waumini**], [Suratul Muntahina: 10].

Wamekubalina waislamu kuwa kilicho tujulisha kwenye aya hizi mbili, ni uharamu wa mwanamke wa kislamu kuolewa na kafiri, kwa hivyo akimuozesha mwanamke mtu ambaye amepewa usimamzi wa binti au mzazi wake, kwa mwanaume asiye swali ndoa hiyo haiswihi na mwanamke huyo sio halali kwa Mwanaume huyo kwa kupitia ndoa hiyo kwaysababu ndoa hiyo haikufata sheria ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, imethibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema: ((**Atakae fanya ibada ambayo hatuku hatukuiamrisha ibada hiyo haikubaliwi**)) Atarudishiwa Mwenyewee.

Kama ndoa inavunjika kwa mume kuwacha swala, isipokuwa akitubu na akirudi kwenye Uislamu kwa kuswali,itakuwaje mtu anaye ozeshwa mara ya kwanza?!

**Majibu kwa ufupi:** Huyo anaye chumbia ambaye haswali, kama atakuwa haswali jamaa huyo ni muovu, hato toka kwenye Uislamu inaruhusiwa kuozeshwa, lakini asiozeshwee Mwanamke mwenye dini na tabia njema kuliko yeye.

Kama atakuwa haswali kabisaa swala ya jamaa au swala ya peke yake, huyo ni kafiri ameritadi ametoka kwenye Uislamu, hairuhusiwi kumuozesha binti wa kislamu, kwa hali yoyote, ispkuwa akitubu toba ya kweli, akiswali na akiwa na msimamo juu ya dini.

Kuhusu alicho kieleza mulizaji kuwa mzazi wa binti aliye chumbiwa aliulizia tabia za huyo aliye kuja kuchumbia kwakwe alivyo ambiwa tabia yake : Akasema Mwenyezi Mungu atamuongoza, hiyo dua ni ya muda wa baadae, na mambo ambayo hayajatokea anayafahamu Mwenyezi Mungu peke yake, na Mwenyezi Mungu ndio anaye endesha mambo yote, na sisi tuna zungumzia tunayo yafahamu katika wakati tulio nao, na hali ya huyo mchumba kwa sasa ni kafiri, hairuhusiwi kumuozesha binti wa kislamu, tunamuomba Mwenyezi Mungu amuogoze na amrudishe kwenye Uislamu mpaka apate kuoa mwanamke wa kislamu, na Mwenyezi Mungu ni muweza wa hayo.

MaJibu haya ameyaJibu na kuyandika kwa mkono wake mtu alie dhalili kwa Mwenyezi Mungu: Muhammadi Swaaleh Uthaymin , tareh /18/ Mwezi Dhul-Hija (Mfungo tatu) / Mwaka/ 1400/H.

****

**Swali la 191: Atafanya nini mume aliye amrisha familia yake kuswali lakini hawakumsikiliza ataendelea kuishi nao na kuchanganyika nao au aondeke nyumbani?**

**Jibu**: kama familia hiyo hawaswali kabisa hao ni makafiri wameritadi na wametoka kwenye Uislamu, haruhusiwi kuishi nao, lakini ni lazima kwake kuwapa nasaha na kuwaelekeza na kuwawaidhi na adumu kufanya hivyo huenda Mwenyezi Mungu akawaongoza, kwa sababu mtu kuwacha swala anakuwa kafiri, Mwenyezi Mungu! atulinde! anakuwa kafiri kwa ushahidi wa Qur`ani na hadithi na kauli za maswahaba radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao! Na kwa ushahidi wa mtazamo ulio sahihi. Hakika nimeuchunguza ushahidi wa wanaosema kuwa mtu akiacha swala sio kafiri, ushahidi huo una mambo makuu manne:

**1**-Kwanza hakuna ushahidi kuwa hawi kafiri.

**2**-Anakuwa na sifa ambazo haiwezekani kusema ameacha swala .

**3**-Anakuwa na fisa ya dharura ya kuwacha swala.

**4-**Au hadithi inagusa pande zote unaifanya kuwa ni mahussi kwa hadithi ya ukafiri kwa muacha swala.

Hakuna katika matini kuwa atakaye acha swala ni muumini au kuwa ataingia peponi au ataokoka na moto, hilo jambo linatupa shida kubadilisha maana ya hukumu ya anaye acha swala kuwa ni kafiri ukafiri wa kupinga neema ya Mwenyezi Mungu! au ni kafri lakini sio ukafiri unao mtoa kwenye Uislamu.

Tukisha fahamu kuwa anaye acha swala ni kafiri ukafiri wa kuritadi ukafiri wake unakuwa na hukumu ya walio ritadi hukumu hizo ni:

**1-**Haruhusiwi kuozeshwa , akifungiwa ndoa naye haswali ndoa hiyo ni batili na si halali kwakwe na huyo mke kwa kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Mkiwa mnawajua kuwa ni waumini basi msiwaresheje kwa makafiri wanawake hao si halali kwa hao makafiri, wala hao makafiri hawahalalishiwi wanawake waumini**], [Suratul Mumtahana: 10].

**2-**Akiacha swala baada ya kufungishwa ndoa, ndoa hiyo inavunjwa na si halali kwake huyo mume, kwa ushahidi tumeotoa katika aya iliyo pita hapo juu, kwa uchambuzi wa Wanachouni unao fahamika Mwenyezi Mungu awarehemu.

**3-**Mtu asiye swali akichinja si halali kula kichinjwa chake, kwa sababu ni haramu, kama atachinja myahudi au mkiristo kichinjwa chake ni halali kwa waislamu kula , na kichinjwa cha muacha swala ni uchafu kuliko cha myahudi na mkiristo.

**4-**Si halali kuingia Makkah au katika mipaka ya sehemu takatifu ya Makkah kwa kauli ya Mwenyezi Mungu**: [Enyi mlio amini! Hakika washirikina ni najsi, kwa hiyo wasiukaribie msikiti mtakatifu baada ya mwaka wao huu**], [Surat Tauwba: 28].

**5-**Akifa mtu wake wa karibu hana haki ya mirathi, hata kama atakufa baba akawa na mtoto asiye swali au akafa mtoto baba haswali au mtoto wa baba mdogo ambaye anamrithi mtoto wa baba mdogo kwa mbali kinyume na mwanae wa kuzaa, kwa kaul ya Mtume rehma na amani ziwee juu yake! Katika hadithi ya Osama : **(( Haruhusiwi mwislamu kumrithi kafiri, wala kafiri kumrithi mwislamu**.)) [6764/ Sahihi Bukhary, / 1614/ Sahihi Muslim]. Na kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Wapewe mirathi wahusika, kitacho baki ni bora kwa mwanaume**))**,** [6732/ Sahihi Bukhary, /1615/Sahihi Musilm] na mifano hii inahusu warithi wote.

**6**-Akifa haoshwi, hawekwi kwenye sanda, haswaliwi, hazikwi kwenye makaburi ya waislamu, chakufanya ni kumpeleka jangwani tunachimba shimo tunamfukia akiwa amevaa nguo zake, kwa kuwa hana heshma yoyote, kwa misingi hiyo sio halali kwa mtu yoyote anaye mfahamu mtu asiye swali akifa akampeleka kwa waislamu wamswalie.

**7-**Atafufuliwa siku ya Qiyama na Firauni na Haamana na Qaruni na Ubaya Ibun Khalafi, ushahid wa haya upo katika kitabu **[169/2, Musnadi wa Imamu Ahmadi],** hao ndio viongozi wa ukafiri, Mwenyezi Mungu atulinde! Mtu huyo hato ingia peponi, na si halali kwa yeyote katika familia yake kumuom-

bea dua ya rehma au msahamaha kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu ni kafiri, hastahiki kuombewa,kwa kauli ya Mwenyezi Mungu: **[Haimpasi nabii na wale walio amini kuwatakia msamaha washirikina japo kuwa ni jamaa zao, baada ya kwisha kubainika kuwa hao ni watu wa motoni]**, [Surat Tauwba: 113].

Jambo hili ni l ahatari sana, kwa masikitiko makubwa baadhi ya watu wanapuzia jambo hili, wanaishi majumbani na watu wasio swali. Mwenyezi Mungu ndio mjuzi**, Imehaririwa/ 6/2/1410/ H.**

****

**Swali la 192: Ni ipi hukumu ya mwanamke kuendelea kuishi na mume asiye swali na wamesha zaa watoto? Na ni ipi hukumu ya kumuozesha binti kwa Mwanaume asiye swali?.**

**Jibu**: Mwanamke akiozeshwa kwa mume asiye swali swala ya jamaa hata nyumbani haswali ndoa hiyo sio sahihi, kwa sababu asiye swali ni kafiri, kama ilivyo thibiti katika Qur`ani tukufu na hadithi za Mtume na kauli za maswahaba Mwenyezi Mungu awaridhie, kama alivyosema Abdallah bin Shaqiyq Mwenyezi Mungu amrehemu **((Walikuwa Maswahaba wa Mtume Mwenyezi Mungu awaridhie !hawaoni ibada ukiicha ni ukafiri isipokuwa swala))** na kafiri si halali kuoa mwanamke wa kiislamu kwa kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Mkiwa mnawajua kuwa ni waumini basi msiwaresheje kwa makafiri wanawake**

**hao si halali kwa hao makafiri, wala hao makafiri hawahalalishiwi wanawake waumini**], [Surat Al-Mumtahan: 10].

Ikitokea kuwacha swala baada ya ndoa kufungwa ndoa hiyo itavunjwa isipokuwa akitubu na akirejea kwenye Uislamu, baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu!wameweka sharti kuwa itakuwa baada ya kuisha eda , ikiisha eda sio halili kumrejea isipokuwa mpaka ifungwe ndoa nyingine, na mwanamke ajitenge na Mwanaume huyo asimpe nafasi katika mwili wake mpaka atubu na aswali, hata kama wamezaa watoto kwa sababu katika hali hiyo watoto hawatakiwi kuwa chini ya uwangaliza wa baba.

Kwa hivyo chukuwa tahadhari ndugu zangu waislamu kuwaozesha watoto zenu na watoto mnao wasimamia kwa wanaume wasio swali jambo hilo linahatari kubwa, hatakiwi kupendwa katika jambo hili mtu wako wakaribu wala rafiki. Namuomba Mwenyezi Munguatuongoze sisi sote, Mwenyezi Mungu ndio mjuzi. Namtakia rehma na amani Mtume wa Mwenyezi Mungu na familia yake na wafwasi wake. Imehaririwa 9/10/1414/H.

****

**Swali la 193: Atakae acha kuswali kwa makusudi kisha akatubu atalipa swala alizo ziacha?**

**Jibu:** Atakae acha kuswali kwa makusudi kisha akatubu kwa Mwenyezi Mungu na akarejea kwa Mwenyezi Mungu wametofautia Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu**. Je ni lazima kulipa swala alizo ziacha au hapana?** Wanachuoni wanakauli mbili:

Kauli ambayo naona inanguvu kwangu, Ni kauli aliyoichagua Sheykhul Isalamu bin Taymiya Mwenyezi Mungu marehemu, ameieleza katika katabu [Majumuul Fatawa: 21-18/22]. Mtu akiacha swala kwa makusudi mpaka ikatoka katika muda wake haimsaidi kuilipa, kwa sababu ibada zimepangiwa muda kwa hiyo ni lazima zifanyike katika muda wake, kama ilivyo kuwa haisihi ibada kufanya kabla ya muda wake pia haisihi kuifanya baada ya kupita muda wake, kwa sababu sheria za Mwenyezi Mungu ni lazima zizingatiwe, hii swala amefaradhishwa katika sheria kuwanzia muda kadhaa mpaka muda kadhaa muda huo ndio wakati wake, pia hairuhusiwi kuswali shehemu ambayo haikuwandaliwa kwa ajili ya swala , pia haifai kuswali muda ambao haukuwekwa na sheria kwa ajili ya swala, lakini mtu aliye acha swala kwa makusudi hato lipa hizo swala, anatakiwa azidishe toba na kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu na afanye matendo mema, na atarji kwa Mwenyezi Mungu amsamehe madhambi yake na amsamehe kwa kuwacha swala, Mwenyezi Mungu ndiye anaye toa taufiyki.

****

**Swali la 194: Ni mambo gani ya lazima kwa wazazi juu ya watoto wao wasio swali?.**

**Jibu:** Wakiwa watoto wao hawaswali, ni wajibu kwao wawalazimishe kuswali kwa kawaamrisha au kwa kipigo, atachukuwa hatua hizo kwa ushahidi wa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Na muwapige kwa kuwacha swala wakiwa na umri wa miaka kumi))**. [187/2/ Imamu Ahmadi, /496/495/ Abuu Daud,/ 5878/ Swahihul Jaami'].

Kama akiwapiga lakini haikusaidia atapeleka jambo hilo kwa wahusika wa serikali, namuomba Mwenyezi Mungu-awawafiqishe- ili wawalazimshe kutekeleza ibada hiyo, si halali kukaa kimya, kwa sababu utakuwa ameridhia uovu, kwa kuwa kuwacha swala ni ukafiri unao mtoa mtu kwenye Uislamu, Muacha swala ni kafiri ataishi mtoni milele, akifa hairuhusiwi kuoshwa pia hairuhusiwi kuswaliwa na waislamu pia hairuhusiwi kuzikwa katika makaburi ya waisalamu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amani.

****

**Swali la 195: Ni ipi hukumu ya kutoa adhana kwa wasafiri?.**

**Jibu:** Jambo hili wametofautiana Wanachuoni, na sahihi ni lazima kutoa adhana kwa wasafiri, kwa sababu Mtume rehma

na amani ziwe juu yake! Alisema kumwambia Maaliki Ibuni Huwaythir na maswahaba zake Mwenyezi Mungu awaridhie: ((**Ukifika muda wa swala basi na atoe adhana mmoja wenu)**), [628/ Sahihi Bukhary, / 674/ Sahihi Muslim]. Na wao walikuwa niwajumbe wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa watu wao, Na kwakuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakuwacha adhana wala iqama akiwa mjini au safarini, alikuwa ikitolewa adhana katika safari zake, alikuwa anamuamuru Bilali Mwenyezi Mungu amridhie atoe adhana.

****

**Swali la 196: Ni ipi hukumu ya adhana na iqama kwa mtu anaye swali peke yake?.**

**Jibu:** Adhana na iqama kwa mtu anaye swali peke yake ni sun`na, sio waaJibu kwa sababu hakuna anaye muita kwa kupitia adhana hiyo, lakini kwa kuwa adhana ni kumtaja Mwenyezi Mungu! Na kumtukuza, na kujiita mwenyewe katika swala na kufaulu, pia iqamaa ni sun`na , ushahid unao tujilisha kuwa adhana ni sun`na ni hadithi ya Uqubat Ibun Aamir radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake! Amesema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Reham na amani ziwe ju yake! Akisema: **((Anampenda Mungu wako mchunga kondoo juu ya kilele cha mli-**

**ma anatoa adhana kwa ajili ya swala, anasema Mwenyezi Mungu: muangalie mja wangu huyu anaadhini na kuqiymu kwa ajili ya swala ananiogopa mimi, hakika nimemsamehe mja wangu, nimemuingiza peponi)),** [157/145/4/ Imamu Ahmadi, /1203/ Abuu Daud, / 666/ Anasaai].

****

**Swali la 197: Mtu akikusanya Swala ya Adhuhuri na Alasiri hivi ataqimu kila Swala? Na je Swala za Sunna zina Iqaama?.**

**Jibu:** Kila swala moja utakuwa unaqimu, kama ilivyo thibti katika hadithi ya Jaabir Mwenyezi Mungu amrehme kwenye sifa za hijaa ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake yakuwa Mtume alikusanya swala alipokuwa Muzdalifa amesema Jabir: **((Ilikimiwa swala akaswali magharibi, kisha ikakimiwa akaswalia isha, na hakuleta tasbihi katikati ya swala hizo mbili)),** [1218/ Sahihi Muslim].

Kuhusu swala za sunna hazina iqama.

****

**Swali la 198: Neno (Aswalatu khayru mina naum) linatamkwa katika adhana ya kwanza au ya pili katika swala ya Al-fajir?.**

**Jibu**: Neno (Aswalatu khayru mina naum) linakuwa katika adhana ya kwanza kama ilivyo thibiti katika hadithi: **((Mkitoa adhana ya kwanza ya swala ya asubuhi sema: aswalatu khayru minal- naumi))**, [500/ Abuu Daud /, 633 / An Nasaai,]. Maan yake swala ni bora kuliko usingzi, inakuwa katika adhana ya kwanza siyo ya pili.

**Lakini ni lazima ufahamu ni ipi adhana ya kwanza iliyo kusudiwa katika hadithi**?

Adhana ya kwanza inakuwa baada ya kuingia muda wa swala, na adhana ya pili ni iqama, kwa sababu iqama inaitwa( adhana) Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake**!: ((kati ya kila adhana mbili kuna swala)),** [624/ Sahihi Bukhary, /838/ Sahihi Muslim]. Makusudio ya hadithi ni adhana na iqaama.

Katika (Sahihi Bukhary): imelezewa kuwa kiongozi wa waumini Othmani Ibuni Afaan radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! Alizidisha adhana ya tatu katika swala ya ijumaa.

Adhana ya kwanza ni ambayo aliamuamrisha Bilali radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! Aseme: (Aswalatu khayrun mina naum), ni adhana ya swala ya Al-fajiri.

Adhana kabla ya kuchomoza Al-fajir sio adhana kwa ajili ya swala ya Al-fajair, watu wanasikiliza adhana ya mwisho: Adhana ya kwanza ya swala ya Al-fajir, kwa ukweli hiyo adhan sio ya swala ya Al-fajir, kwa kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema ((**hakika Bilali anadhini usiku awamshe walio lala na warejee walio simama)),** [621/ Sahihi Bukhary, /1093/ Sahihi Muslim]. Maana ya hadithi kwa ajili ya aliye lala aamke kula daku na aliye simama kuswali ale daku.

Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Kumwambia Maliki Ibun Huwayrithi radhi za Mwenyezi Mungu ziwee juu yake: ((**Ikifika muda wa swala adhini mmoja wenu**)), inafahamika kuwa swala haiwadii mpaka Al-fajir ichomeze, adhana ya kabla ya kuchomoza Al-fajir sio adhana ya swala ya Alfajir.

Jambo hili ndio watu wengi wanalifanya , kauli ya (Aswalatu khayrun mina naum) katika adhana ya Al-fajiri hiyo ndio sahihi.

Ama walio sema kuwa makusudio ya adhana ya kwanza kwenye hadithi tulio itaja hapo juu , ni adhana kabla ya Al-fajir, hoja yao ni dhaifu .

Wamesema baadhi ya watu: ushahidi kuwa makusudio ni adhana inayo kuwa mwisho wa usiku kwa ajili ya kuswali swala ya sun`na, kuwa muadhini aseme: (Aswalatu khayrun mina naum) neno (khayru) linajulisha ubora .

**Tunasema**: Neno ( khayru) linatumika katika jambo la lazima , mfano kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Enyi mlio amin! Nikuon-**

**yesheni biashara itakayo kuokoeni na adhabu iliyo chungu?. Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na piganeni jihadi katika njia Mwenyezi Mungu kwa mali yenu na nafsi zenu, hayo ni bora kwenu, ikiwa nyinyi mnafahamu**], [Surat Swaff: 10-11]. Pamoja kuwa ni imani.

Amesema Mwenyezi Mungu katika swala ya ijumaa: **[Enyi mlio amini! Patakapo adhiniwa kwa ajili ya swala ya siku ya ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikir ya Mwenyezi Mungu, na wacheni biashara, hayo ni bora kwenu, laiti kama mnajua]**. [Suratul Jumaa: 9]. Neno ( kheyru ) linatumika kwenye jambo la lazima na jambo la sunna.

****

**Swali la 199: Je inasihi adhana ya kurikodi ( Recorder)?.**

**Jibu**: Adhana ya kurikodi sio halili, kwa kuwa adhana ni ibada, na ibada ni lazima iwe na niya.

****

**Swali la 200: Mtu akiingia msikitini na hali adhana ikiadhiniwa ni jambo lipi bora afanye?.**

**Jibu**: Ni bora amjibu muadhini kisha aombe dua baada ya adhana dua iliyo pokelewa katika hadithi sahihi za Mtume, kisha aswali tahiyatul Masjidi, isipokuwa baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu! Wamesema kama itakuwa siku ya ijumaa mtu akaingia msikitini na adhana ya pili ina adhiniwa mtu huyo aswali tahiyatu-lmasjidi kwa ajili apate muda wa kusikiliza khutba, wakatoa sababu kuwa kusikiliza khutba ni wajibu na kumjibu muadhini sio wajibu, na mtu kufanya wajibu ni bora kuliko kufanya lisilo kuwa la wajibu.

****

**Swali la 201: Imepokewa katika hadithi mtu aseme wakati anamfatisha muadhini (radhwitu billahi raban, wabil Islami diina, wabi Muhammadi rasula) ni muda gani mtu atasema hiyo nyiradi?.**

**Jibu:** Jambo linalo onekana lipo wazi katika hadithi Muadhini atakapo sema : Ashahadu an laa illah illa allah waa ashahadu ana muhammada rasulu allah, baada ya kujibu, utasema: radhwiytu billahi raban, wabil Islami diyna, wabi Muhammadi rasula, kwa sababu kwenye hadithi imeelezwa**: ((Atakae sema atakapo sikia muadhini: ashahadu an laa illah illa allah waa**

**ashahadu ana Muhammada rasulu allah, radhwiytu billahi raban, abil-islami diyna, wabi Muhammadi rasula))**, [386 / Sahihi Muslim], katika riway a nyingine: Atakae sema: **(Wanash'hadu**) ni ushahidi tosha kuwa atasema baada ya kauli ya muadhini: Ashahadu an laa illaha illa LLah, kwa sababu herufi ya wawu kwenye lugha ya kiarabu inaamaana ya kunganisha au kufatanisha kauli yake na kauli ya muadhini .

****

**Swali la 202: Ziada ya ( inaka laa tukhlifu miaadi) katika dua baada ya adhana ni sahihi?.**

**Jibu**: Ziada hiyo inakhilafu kwa Wanachuoni wahadithi Mwenyezi Mungu awarehemu, wapo Wanachuoni walio sema: ziada hiyo haikuthibiti katka hadithi za Mtume rehma na amani ziwe juu yake!, kwa sababu wapokezi wengi walio pokea hadithi hawakupokea neno hilo ,na haiwezekani wapokezi wa hadithi waliondoe neno hilo kwenye dua ya kumsifu Mwenyezi Mungu, na jambo likiwa hivyo hairuhusiwi kuliondoa kwa sababu neno hilo ni ibada.

Wapo Wanachuoni wanao sema: Upokezi wa ziada hiyo ni sahihi, na ziada hiyo husemwa na haipingani na riwaya yingine, miongoni mwa walio sahihisha upokezi wa riwaya hiyo ni Sheikh Abdul-azizi Ibun Bazi Mwenyezi Mungu amrehemu, [ma-

jmuu fatawa samaahat Ibun Bazi 336/10/] Akasema: upokezi wa riwaya hiyo ni sahihi ameipokea Bayhaqiyu Mwenyezi Mungu amrehemu kwa upokezi sahihi [528/ Abuu Daud].

****

**Swali la 203: Je mtu anatakiwa kumfatisha anaye qimu swala?**

**Jibu:** Kumfatisha anaye qimu swala amepokea hadithi Abuu Daud Mwenyezi Mungu amrehemu, lakini hadithi hiyo ni dhaifu hauwezi kusimamisha hoja kwa hadithi hiyo, kauli iliyo sahihi hakuna mkufata kwa nyiradi Anaye qimu swala

****

**Swali la 204: Tunawasikia baadhi ya watu baada ya kukimiwa swala wanasema: (Aqama LLah wa adaamaha) ni ipi hukumu yake?.**

**Jibu:** Imepokewa hadithi kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, alikuwa akisema baada ya kusema muadhini **((Qad qaamati swalaa**)). Anasema: ((**Aqama LLah wa adaamaha**)) [528/ Abuu Daud, /211/1 haafidh, na katika Tal-khiyswi, /258/1

/Al-Baany, katika , Al-Ir waai], lakini hadithi ni dhaifu haisimamishiwi hoja.

****

**Swali la 205: Ni muda gani bora kuswali? Je Mwanzo wake ndio bora?.**

**Jibu:** Swala iliyo kamili huswaliwa ndani ya wakati wa kisheria, amesema Mtume rehma na mani ziwe juu yake juu ya ulazima wa kuswali ndani ya wakati na ni jambo analo lipenda Mwenyezi Mungu! Amesema: ((S**wala kwa wakati wake**)) [527 / Sahihi Bukhary, /85 / Sahihi Muslim], na hakusema : ((S**wala mwanzo wa wakati))** kwa sababu swala zipo ambazo ni sunna kuzitanguliza na zipo ambazo ni sunna kuzicheleweshа, mfano swala ya ishaa ni Sunna kuichelewesha mpaka theluthi ya usiku, kwa hivyo kama mwanamke atakuwa nyumbani akauliza**: Ni ipi bora kwangu kuswali ishaa wanapo adhani au mwisho wa theluthi ya usiku?.**

**Tunasema:** Ni boraaicheleweshe swala hiyo ya ishaa mpaka teluthi ya usiku kwakuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alichelewa usiku mmoja mpaka wakasema maswahaba: Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu Wanawake na watoto wamelala, akatoka akawaswalisha Akasema: ((**Hakika huu ndio wakati wake kama sio kuwapa tabu Uma wangu.**)) [566/ Sa-

hihi Bukhary, /638 / Sahihi Muslim], iliyo bora kwa mwanamke akiwa nyumbani aicheleweshe .

Kama watu maalum watakuwa wapo safari, wakasema: tucheleshe swala au tuwahi kuswali?.

**Tunasema:** Ni bora waicheleweshe.

Piakama kundi la watu litatoka kwenda sehemu ya kupumzika ukawadia muda wa swala ya ishaa, hivi iliyo bora waicheleweshe swala au waitangulize?.

**Tunasema:** Ni bora waicheleweshe isipokuwa kama kuichelewesha kutawapa shida.

Swala zingine ni bora kuzitanguliza kwamaana kuiswali mwanzo wa wakati wake, isipokuwa kwa sababu, swala ya Alfajir inatangulizwa, swala ya adhuhuri, Alasili na magharibi pia, isipokuwa kama kutakuwa na sababu unaweza kuichelewesha.

Miongoni mwana sababu za kuchelewesha swala joto likizidi ni bora kuichelewesha swala ya adhuhuri mpaka ifikie muda wa kupoa joto, inakuwa karibu na swala ya alasili, kwa sababu joto linakuwa limeanza kupungua ikikaribia alasili, na joto likizidi ni bora kulipoza kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Litakapo zidi joto lipozeni kwa swala hakika joto kali ni mvuke wa jahanamu**.)) [536/ Sahihi Bukhary, / 715/ Sahihi Muslim].

Mtume rehma na amani ziwe juu yake alikuwa safari akasimama Bilali radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake ili atoe adhana, akasema Mtume kumwambia Bilali: **((ipoze**)) kisha aka-

simama ili atoe adhana, akasema tena Mtume kumwambia Bilali: **((ipoze**)) kisha akasimama ili atoe adhana,Mtume rehma na amani ziwee juu yake! Akamruhusu. [535/ Sahihi Bukhary /616/ Sahihi Muslim].

Miongoni mwa sababu za kuchelewesha swala ni kupatikana jamaa mwisho wa muda jamaa ambayo haipatikani mwanzo, katika hali hii kuchelwesha ni bora, kwa mfano umefika muda wa swala mtu yupo nje ya mji naye anafahamu kuwa atawahi kufika mjini na ataidiriki jamaa mwisho wa wakati, **hivi ni bora aswali muda ukifika au acheleweshe mpaka aiwahi jamaa?.**

**Tunasema:** Ni bora aicheleweshe mpaka aidiriki swala ya jamaa, isipokuwa tunasema Ni lazima kuichelewesha swala hiyo mpaka apate jamaa.

****

## Swali la 206: Mtu akiswali kabla ya kuingia muda bila kufahamu ni ipi hukumu yake?.

**JIBU: M**tu akiswali kabla ya wakati wa swala haiswihi, Amesema Mwenyezi Mungu: [**Hakika swala kwa waumini ni faradhi iliyo wekewa nyakati maalum**], [Surat Nisaa: 10] Ameweka wazi Mtume rahma na amani ziwe juu yake! Nyakati za swala katika kauli yake: **((wakati wa dhuhuri jua likikengeuka**)), nk. [612/ Sahihu Bukhary] kwa hivyo atakae swali kabla ya muda swala yake haikidhi kwa sababu ameiswali nje ya wakati

atalipwa thawabu za swala ya Sunnah, na ni lazima arudie kuswali baada ya kuingia muda. Mwenyezi Mungu ndio mjuzi.

****

**Swali la 207: Je inaruhusiwa kuto kufuata utaratibu kati ya swala na swala kwa mtu ambaye analipa swala zilizo mpita kwa kusahau au kuto kujua?**

**Jibu:** Jambo hilo wametofautiana Wanachuoni, na usahihi kufata utaratibu kunapukutika kwa kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Mola wetu! Usituchukulie tukisahau au tukikosea**], [Suratul Baqara: 287]. Amesema Mtume rahma na amani ziwe juu yake: ((**Wamesamehewa Uma wangu makosa ya kusahau au bahati mbaya**)), [2045 /Ibun Maajah.

** **

**Swali la 208: Mtu aliye ingia mskitini kwa ajili ya kuswali swala ya Ishaa kisha akakumbuka kuwa haja swali maghribi atafanyaje?**

**Jibu:** Mtu akiingia msikitini na swala inaqimiwa kisha akakumbuka kuwa haja swali Maghrib ataingia kuswali kwenye jamaa ya swala ya Ishaa kwania ya swala ya Maghrib, Imamu akisimama kwenye rakaa ya nne utakaa chini unamsubili Imamu

amalizie rakaa ya nne utoe naye salamu, pia unaruhusiwa kutoa salamu kisha ukasimama na kuendelea kuswali na Imamu, ukiwa umenuwiya swala ya isha, na hakuna tatizo kupishana niya kati ya Imamu na maama kwa kauli iliyo sahihi katika kauli za Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, ukiswali maghribi peke yake kisha ukaenda kuswali isha rakaa zilizo bakia na jamaa hakuna ubaya.

****

**Swali la 209: Ikinipita faradhi moja au zaidi kwa kusahau au usingizi, nitazilipa vipi swala zilizo nipita? Nitaanza kuswali iliyo pita kisha niswali iliyopo au kinyume chake?**

**Jibu:** Ataswali kwanza iliyo pita kisha ataswali iliyo katika wakati wake na hairuhusiwi kuichelewesha, jambo hili limeenea kwa wengi kuwa mtu ikimpita swala ya faradhi atailipa muda wa faradhi kama ile iliyo mpita siku ya pili, mfano mtu hakuswali Al-fajir basi haiswali mpaka aiswali na Al-fajiri ya kesho siku ya pili, na hili ni kosa, pia kunapingana na muongozo wa Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake! Muongozo wa kauli na vitendo:

**Mungozo wa kauli**: imethibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Amesema**: ((Atakae lala bila kuswali au akasahau, basi aswali atakapo kumbuka)),** hakusema: aiswali siku ya pili utakapo fika muda wake, isipokuwa alisema: ((**Basi aswali atakapo kumbuka**)).

Muongozo wa vitendo**:** ilivyo mpita swala siku ya khandaki aliiswali kabla ya swala iliyopo, umetufahamisha kuwa mtu atanza kuswali iliyo pita kisha ataswali iliyopo, lakini kama atasahau akatanguliza swala iliyopo kabla ya iliyo pita au akawa hafahamu swala yake ni sahihi, kwa sababu huo ni udhuru.

**Kwa kupitia nafasi hii napenda kusema:** hakika swala zinazo takiwa kulipwa zimegawanyika sehemu tatu:

**Sehemu ya kwanza:** Atalipwa udhuru ukiondoka, kwa maana udhuru wa kuchelewesha swala nazo ni swala tano, ukiondoka udhuru wa kuchelewesha ni lazima kulipa.

**Sehemu ya pili:** ikikupita hailipwi iliyo kupita lakini inalipwa badala yake, nayo ni swala ya ijumaa, mtu akimkuta Imamu ameisha inuka kutoka kwenye rukuu rakaa ya pili katika swala ya ijumaa mtu huyo ataswali adhuhuri, ataswali na Imamu akiwa na niya ya swala ya adhuhuri, pia akifika msikitini akakuta Imamu ameisha toa salamu ataswali adhuhuri, mtu ambaye atawahi rakaa ya pili ataswali ajumaa, kwa maana ataswali rakaa nyingine moja baada ya kutoa salamu Imamu, jambo hili watu wengi hawalifahamu, baadhi ya watu wanakuja msikitini siku ya ijumaa wanamkuta Imamu ameisha inuka kutoka kwenye rukuu ya rakaa ya pili, kisha mtu huyo anaswali rakaa mbili akidhani kuwa hiyo swala ni ya ijumaa na hili nikosa,

isipokuwa akija baada ya Imamu kuinuka kwenye rukuu ya rakaa ya pili mtu huyo hakuiwahi swala ya ijumaa kabisa ni lazima aswali adhuhuri, kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Atakae idiriki rakaa hakika ameidiriki swala)),** [570 /Sahihi Bukhary, /607/ Sahihi Muslim]. Tume fahamu katika hadithi atakaye diriki chini ya rakaa mtu huyo hakudiriki swala, na swala ya ijumaa inalipwa dhuhuri, kwa hivyo ni lazima kwa wanawake wanao swalia majumbani na wagonjwa ambao hawaendi kuswali ijumaa, ni laimza kuswali dhuhuri na wasi swali rakaa mbili za ijumaa,wakiswali rakaa mbili za ijumaa swala yao ni batili haikubaliwi.

**Sehemu ya tatu:** swala ikikupita hailipwi isipokuwa mpaka muda wake ule ule nayo ni swala ya iddi kama watu hawakufahamu kama ni sikuku ya iddi mpaka jua lika pinduka, Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu! Wanasema: wataiswali siku ya pili katika muda wake.

**K**ulipa swala kumegawanyika sehem tatu:

**1-**Swala inayo lipwa baada ya kuondoka udhuru, nazo ni swala tano, pia na swala ya witri, na sun`na zilizo wekewa muda maalum.

**2**-Swala inayo lipwa badala nayo ni swala ya ijumaa ikipita inalipwa dhuhuri.

**3-**Swala inayo lipwa yenyewee lakini katika muda wake siku ya pili, nayo ni swala ya iddi ikipita watu wakafahamu baada ya kupinduka jua wataiswali siku ya pili katika muda wake. Mwenyezi Mungu ndio anawafkisha .

****

**Swali la 210: Watu wengi wanaswali wakiwa wamevaa nguo nyepesi inayo onyesha rangi ya mwili, kwa chini amevaa suruali fupi haivuki kwenye mapaja isipokuwa kidogo mtu anaona mapaja kupitia muonekano wa nguo inayo onyesha, Ni ipi hukumu ya swala ya mtu huyo?**

**Jibu**: Hukumu ya swala ya watu hao ni hukumu ya mtu aliye swali bila nguo isipokuwa surual fupi, kwa kuwa nguo nyepesi inayo onyesha rangi ya mwili sio sitara kuepo kwake ni sawa na kuto kuwepo, kwa misingi hiyo swala ya mtu huyo sio sahihi kwa kauli sahihi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, kwasababu ni wajibu kwa wanaume wanao swali kusitiri sehemu iliyo kati ya kitovu na magoti na hicho ndio kiwango cha chini anacho takiwa kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu ya kumtaka ajisitiri amesema Mwenyezi Mungu: [**Enyi wanaadamu chukueni pambo lenu kwenye kila pahala wakati wa ibada**], [Suratul Aaraafu: 31], ni wajibu kati ya mambo mawili ima avae suruali inayo sitiri sehemu iliyo kati ya kitovu na magoti, au

avae juu ya suruali nguo nyingine fupi ambayo haionyeshi rangi ya mwili.

Na uvaaji ulio ulizwa kwenye swali ni jambo la hatari ni lazima watu tubu kwa Mwenyezi Mungu! Kwa kuwacha kuvaa mavazi hayo, Na wapupie kusitir miili yao wakati wa swala, tunamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze sisi na ndugu zetu katika mambo anayo yapenda na kuyaridhia Mwenyezi Mungu ni mkarimu Mwenye huruma.

****

**Swali la 211: Ni ipi hukumu ya mwanamke kuvaa nguo yenye mpasuo kwa mbele na ubavuni na nyuma, unayo inaoyesha sehemu ya miudi ya miguu, hoja yao ni kuwa wapo wanawake tu?**

**Jibu:** Jambo ambalo mimi naona mwanamke avae nguo ya kujisitiri, ameleza Sheykul Islam bin Taymiyah Mwenyezi Mungu marehemu [119/118/22/ Majmuu fatawa]. Wanawake wa zama za Mtume rehma na amani ziwe juu yake alikuwa wanavaa kanzu ambazo zinazo fika kwenye vifundo vya miguu miwili, na kwenye viganja vya mikono , hakuna shaka kuwa mpasuo au uwazi alio uashilia muulizaji ni uwazi unao onyesha muundi wa mguu na huenda uwazi huo ukawa mkubwa ukaonyesha zaidi ya muundi wa mguu, ni lazima kwa mwanamke awe na

aibu na abadu na avae mavazi yanayo usitiri mwili wake ili asingie kwenye kundi ambalo Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Amesema: **((Watu wa aina mbili ni watu wa motoni sijawahi kuwaona, watu wana bakora kama mikia ya ng`ombe wanawapiga watu kwa mikia hiyo, na wanawake wameva lakini wapo uchi, wanatembea kwa maringo, vichwa vyao ni kama nundu ya ngamia iliyo yumba hawato ingia peponi wala hawato pata harufu ya pepo, hakika harufu ya pepo inapatikana masafa marefu)).** [2128/ Sahihi Muslim].

****

**Swali la 212: Je inaruhusiwa kwa mwanamke kuswali akiwa amevaa niqabu au soksi za mikono?**

**Jibu:** Mwanamke anaye swalia nyumbani kwake, au sehemu ambayo wanaume hawamuoni isipokuwa wapo wanaume wasio ruhusiwa kumuoa atafunua uso wake na mikono ili uso na pua na mikono viguse ardhi au mswala atakapo sujudu.

Kama atakuwa anaswali lakini pembeni yake kuna wanaume ambao Wanaruhusiwa kumuoa pia ni lazima afunike uso, kwa sababu kufunika uso kwa mwanaume anaye ruhusiwa kumuoa ni wajibu, si halali kwa mwanamke huyo kufunua uso mbele ya mwanaume huyo, kama ilivyo elezea Qur`an na hadithi za Mtume rahma na amani ziwe juu yake na mtazamo ulio sahihi,

na akili sahihi ya muumini haipingi hilo.

Kuva soksi za mikono ni jambo ambalo lipo katika sheria, jambo hili lipo wazi ni katika mambo walio kuwa wakiyafanya wanawake wa maswahaba radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yo kwa ushahidi kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Alisema: ((**Asivae niqabu mwanamke aliye hirimia hija au umra, wala asivae soksi za mikono**)), [1838 / Sahihi Bukhary], hadithi hii inatufahamisha kuwa wanawake wa zama za Mtume walikuwa wanavaa soksi za mikono, kwa misingi hiyo sio vibaya mwanamke kuvaa soksi akiwa anaswali na pembeni kuna wanaume wanao ruhusiwa kumuoa, kuhusu kufukika uso atafunika akiwa amesimama au amekaa , akitaka kusujudu atafunua uso ili paji lake la uso liguse sehemu ya kusujudu.

****

**Swali la 213: Ni ipi hukumu ya mtu aliye swali akiwa amevaa nguo yenye najsi naye hafahamu?**

**Jibu**: Mtu akiswali akiwa amevaa nguo yenye najsi na hakufahamu kama nguo hiyo ina najsi au alikuwa anafahamu kama nguo hiyo inanajsi lakini hakukumbuka akakumbuka au akufahamu baada ya kumaliza kuswali swala yake ni sahihi na hato irudia swala hiyo, pia kama atafanya jambo la haramu kwa kuto kufahamu au kusahau, Amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: [**Mola wetu! Usituchukulie tukisahau au tukikosea], [**Suratul Baqara: 286], amesema Mwenyezi Mungu: **((hakika umefanya**)),

[126/ Sahihi Muslim], siku moja Mtume rahma na amani ziwe juu yake aliswali akiwa amevaa viatu na kwenye viatu vyake kulikuwa na uchafu alipo fika katikati ya swala alikuja malaika Jibril rehma za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! Akamwambia Mtume kuwa kwenye viatu vyako kuna uchafu Mtume akavivua naye akiwa anaswali [650/ Abu Daud], hakuwanza kuswali upya, inatufahamisha kuwa atakaye fahamu kuwa ana najsi wakati anaswali aiondoe najsi hiyo katikati ya swala na aendelee na swala kama ataweza kubaki akiwa amesitiri sehemu yake ya siri baada ya kuiondoa najsi hiyo, pia mtu aliye sahau akakumbuka akiwa kwenye swala ataiondoa nguo yenye najsi kama atabaki na nguo itakayomsitiri sehemu ya siri, kama atamaliza kuswali kisha akakumbuka baada ya kumaliza au akafahamu baada ya kumaliza kuswali, hato rudia na swala yake ni sahihi, kinyume na mtu alie sahau akaswali bila kutawadha au alikuwa ana udhuu ukaharibika akasahau kutawadha, kisha akaswali baada ya kumaliza kuswali akakumbuka kuwa hakutawadha, ni lazima atawadhe na arudie kuswali, pia kama atakuwa na janaba na hakufahamu, kwa mfano kama atakuwa amelala akaota alivyo amka asubihi akaswali bila kuoga kwa kuto kujua ilivyo fika mchana akaona kwenye nguo yake manii ya tokea usiku, ni lazima aoge na arudie kuswali.

Na utofauti kati mambo haya – nakusudia: mambo ya najsi- najis ni katika mambo ya kuwacha haramu, kutawadha na kuoga ni katika mambo ya kufanya yalio amrishwa, na kufanya mambo yalio amrishwa ni jambo la lazima mtu kulifanya , ibada haikamiliki isipokuwa kwa kulifanya jambo hilo, kuondoa najsi ni jambo ambalo halipo na swala haikamiliki isipokuwa kwa kukosekana jambo hilo, ikipatikana najsi wakati wa swala kwa kusahau au kuto kujua hakudhuru, kwa sababu halijampita

jambo ambalo linalo takiwa kuwepo katika swala. Mwenyezi Mungu ndio mjuzi.

****

**Swali la 214: Ni ipi adhabu ya mtu anaye vaa nguo ndefu inayo vuka vifundo vya miguu akivaa kwa maringo? Na ni ipi adhabu ya aliye vaa nguo ndefu bila maringo? Na vipi tuta wajibu wanao toa ushahidi wa kuruhusu kuvaa nguo ndefu kwa hoja ya hadithi ya Abuu bakar radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake?**

**Jibu:** Kuburuza nguo akikusudia maringo adhabu yake ni kuwa Mwenyezi Mungu hata muangalia siku ya kiyama wala hata msemesha, wala hata mtakasa, na atakuwa na adhabu kali. Asipo kusudia maringo adhabu yake ataadhibiwa sehemu iliyo zidi vifundo viwili vya miguu kwa moto, kwa kuwa Mtume rehama na amani ziwe juu yake anasema: **((Watu wa aina tatu Mwenyezi Mungu hata zungumza nao siku ya kiyama, wala hata wangalia, wala hata watakasa, wana adhabu kali: mburuza nguo,anaye toa kitu kisha anajisifu, anaye uza biashara kwa viapo vya uongo)**), [106/ Sahihi Muslim]. Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Atakaye buruza nguo kwa maringo Mwenyezi Mungu hata muangalia siku ya kiyama**)) [365/ Sahihi Bukhary, /2085/ Sahihi Muslim], hii ni kwa mtu aliye buruza ngo kwa maringo.

Ama mtu ambaye hakukusudia maringo imethibiti hadithi katika (Swahihi Bukhary na Swahihi Muslimu) kutoka kwa Abuu Hurayra radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake! Kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Amesema: **((Kilicho zidi chini ya vifundo viwili vya miguu katika nguo kitakuwa motoni**)), [5787/, Sahihi Bukhary] Mtume hakusema ni lazima kuwa na maringo, na hatuwezi kusema kuwa ni lazima kuwe na maringo kwa mujibu wa hadithi iliyo kabla ya hiyo, kwa kuwa Abaa Saidi Al-khudriy radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu rahema na amani ziwe juu yake: ((**Sio vibaya nguo ya muumini ikifika nusu ya muundi au alisema: si vibaya ikifika kati ya muundi na vifundo viwili, na kitakacho zidi kitaenda motoni, na atakaye buruza nguo yake kwa maringo Mwenyezi Mungu hata muangalia siku ya kiyama**)), [5/3/ Imamu Ahmadi, /4093/ Abuu Daud, /3573/ Ibun Majah, /9634/ Nasaai katika (Alkubra) / 217/2/ Maaliki].

Kweye hadithi kuna alama mbili tofauti, na adhabu mbili tofauti, ziki tofautiana hukumu na sababu haiwezeakani jambo likawa maalumu, kwa sababu kutakuwa kuna kupingana katika hukumu mbili na kwenye hadthi hizo mbili hazija pingana .

Kuhusu wanao toa hoja ya hadithi ya Abuu bakar radhi ya Mwenyezi Mungu iwee juu yake! Tumasema kumJibu: Hakuna hoja katika hadithi hiyo kwa pande mbili:

**Ya kwanza**: Hakika Abuu bakar radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake! Anasema**: ((Hakika ncha ya nguo yangu inatelemka lakini nachukuwa ahadi juu ya kuipandisha)),**

Abuu bakar radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake hakuishusha nguo yake kwa kupenda, isipokuwa inashuka kwa kuteleza, naye anaahidi kuto ishusha, wanao buruza nguo wanadai kuwa hakusudii maringo lakini wanashusha nguo zao kwa makusudi, tunasema kuwambia: Hakika mkikusudia kushusha nguo zeni mpaka chini ya vifundo viwili vya miguu bila maringo mtaadhibiwa kwa kile mlicho kishusha zidi vifundo viwili mtaadhibiwa kwa moto tu, na mkiburuza nguo zenu kwa maringo mtaadhibiwa kwa adhabu kubwa kuliko hiyo, Mwenyezi Mungu hato ongea nao siku ya kiyama, hato wangalia, hato watakasa, wanaadhabu kali.

**Ya pili**: Abuu bakar radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake alitakaswa na Mtume Muhammad rehma na mani ziwee juu yake, Mtume akatoa ushahidi kuwa Abuu bakar sio miongoni mwa wanao shusha nguo kwa maringo, hivi hao wanao shusha nguo yupo aliye pata utakaso na cheti kutoka kwa Mtume Muhammad kuwa sio katika watu wa maringo? Lakini shetani anawachezea watu wanataka wafate Aya zilizo shabihiyana na hadithi ili wapate utakaso wa wanayo ya fanya, Mwenyezi Mungu anamuongoza amtakae katika njia iliyo nyoka, na muomba Mwenyezi Mungu atupe muongozo na afya, imehaririwa /29 /6/ 1399 / Hjr.

****

**Swali la 215: Mtu akiswali na baada ya swala akakumbuka kuwa anauchafu mkubwa unao mlazimu kuoga?**

**Jibu:** Mtu yoyote akiswali bada ya swala akafahamu kuwa ameswali na uchafu mkubwa au mdogo, ni lazima ajitwaharishe kisha arudie kuswali, kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema**: ((Mwenyezi Mungu haukubali swala bila twahara)),** [242 / Sahihi muslim].

****

**Swali la 216: Mtu akitokwa na damu puani akiwa kwenye swala ni ipi hukumu yake? Hivi nguo yake inanajisika ikipatwa na damu inayo mtoka puani?**

**JIBU:** Damu inayo toka puani haiharibu udhu ikiwa nyingi au cheke, pia vyote vinavyo toka kwenye mwili kupitia njia isio kuwa ya mbele au nyuma udhu hauharibiki, mfano matapishi, na majimaji yanayo toka kwenye kidonda hayaharibu udhu yakiwa mengi au machache, kwa sababu haikuthibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, asili ni kuendelea kubaki twahara, hakika twahara imethibiti kwa muuJibu wa ushahidi wa sheria, kilicho thibiti kwa ushahidi wa kisheria hakiwezi kuondoka isipokuwa kwa ushahidi wa kisheria, hakuna ushaihidi kuwa kilicho toka katika mwili kupitia njia isiyo kuwa ya mbele au nyuma kina haribu udhu, kwa hivyo damu inayo toka puani na matapishi hayaharibu udhu hata ya kiwa mengi au machache, lakini kama itakuwa inakupa shida na ukawa hauna unyeyekevu katika swala sio vibaya ukatoka kwenye swala, pia

kama utahofia kuchafua msikiti ni lazima utoke ili usichafue msikiti kwa damu inayo kutoka, ama damu inayo kudondokea kwenye nguo nayo ni damu kidogo damu hiyo haiinajsi nguo.

****

**Swali la 217: Ni ipi hukumu ya kuswali katika msikiti wenye kaburi?**

**Jibu:** kuswali katika msikiti wenye kaburi kume gawanyika katika sehemu mbili:

**1-**Ni kuwa kaburi lilikuepo kabla ya kujenga msikiti, hali ambayo watajenga msikiti juu ya kabuli, ni lazima kuuhama msikiti huo na kuto kuswali ndani ya msikiti huo, na aliye ujenga msikiti huo aubomoe, kama hakuubomoa ni lazima kwa kiongozi wa waislamu aubomoe.

2-Ni kuwa msikiti ndio ulio anza kujengwa kabla ya kaburi, hali ambayo atazikwa mtu baada ya kujenga msikiti, ni lazima kulifukuwa kaburi, na kumtoa maiti, na kwenda kumzika kwenye makaburi ya watu wote.

Kuhusu kuswali katika msikiti huo inaruhusiwa kwa sharti kaburi lisiwe mbele ya anaye swali, kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake, alikataza kuswali mtu akiwa ameelekea makaburi.

Kuhusu kaburi la Mtume rehma na amani ziwe juu yake

ambalo lipo kushoto mwa msikiti wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, inafahamika kuwa msikiti wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake umejengwa kabla ya kufa kwa Mtume na haukujengwa kwenye kaburi, pia inafahamika kuwa Mtume hakuzikwa ndani ya msikiti alizikwa dani ya nyumba yake ambayo alikuwa imetengana na msikiti, katika utawala wa Walidi bin Abdul Maliki alimtumia barua kiongozi wake wa Madina Omar bin Abdul Aziz Mwenyezi Mungu amrehemu mwaka / **88 / H** , aubomoe msikiti wa Mtume na aunge vyumba vya wake wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake!viwe katika msikitini kwa maana msikiti utanuliwe, Omar bin Abdul Aziz akawakusanya watu wengi na Wanachuoni akawasomea barua ya kiongozi wa waislamu walidi jambo likawa gumu kwa watu wa Madina, wakasema: Tuuache msikiti kama ulivyo tutakuwa tunapata mazingatio, imeelezewa kuwa Saidi bin Musayabu rehma za Mwenyezi Mungu zimuendee alipinga kuingiza chumba cha Aisha katika sehemu ya Msikiti, [418 / 27/ Majmuu fatawa, / 415 / 12/ bidaaytu wahinhaya], Alikuwa anaogopa wasiufanye msikiti kuwa unakaburi, Omar bin Abdul Aziz akamuandikia ujumbe Walidi, kiongozi wa waislamu akamjibu Omar bin Abdul Aziz kuwa ni amri wafanye alivyo amrisha, akamlazimu Omar bin Abdul Aziz kufata amri ya kiongozi wa waislamu, Mpaka hapo umeona kuwa kaburi halikuwa kwenye msikiti, na halikujengwa msikitini, hakuna hoja kwa mtu anaye taka kuzika msikitini au kujengea kaburi, hakika imethibiti kwa Mtume rehma na amani ziwee juu yake kuwa Amesema: **((Mwenyezi Mungu amewalaani mayahudi na wakiristo wameya-**

**faya makaburi ya mitume wao kuwa ni misikiti**)), [435/ Sahihu Bukhary,/ 528/ Sahihi Muslim]. Aliyasema hayo alivyo kuwa anakaribia kufa akautahadharisha Uma wake kwa walio ya fanya mayahudi na Wakiristo.

Ummu Salama radhi ya Mwenyezi ziwe juu yake alivyo muhadithia Mtume kuwa aliona kwenye makanisa picha za watu za kuchonga katika ardhi ya uhabeshi akasema: ((**Picha hizo akifa mtu mwema au mja mwema wanajenga juu ya kaburi lake msikiti, hao ni watu waovu mbele ya Mwenyezi Mungu)**), [434/ Sahihu bukhariym /528 / Sahihi Muslim]. Imepokelewa hadithi kutoka kwa Ibun Mas'ud radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake kuwa Mtume Alisema: **((Hakika miongoni mwa watu waovu ni watu kitafika kiyama nao wako hai,na wale wanao yafana makaburi kuwa ni misikiti** )), [435/ 405/1/ Imamu Ahmadi]. Na waumini hawaridhii wafate njia ya Mayahudi na Wakiristo, wala hawardhii kuwa katika watu waovu. Imehaririwa / 7/ 4/ 1414 / H.

****

**Swali la 218: Ni ipi hukumu ya kuswali juu ya paa la choo? Ni ipi hukumu ya kuswali juu ya jengo linalo wekewa kinyesi cha wanyama?**

**JIBU:** Kuswali juu ya vyoo na mabafu ya kuogea tunayo ya fahamu sio vibaya, kwa sababu mabafu ya kuogea katika nchi yetu hayajengwi sehemu ya peke yake paa lake linakuwa ndio

paa la nyumba nzima, na kuswali katika majengo yanayo weka kinyesi cha wanyama sio vibaya kuswali juu ya jengo hilo kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwee juu yake: **((Imefanywa ardhi kwangu mimi kuwa ni msikiti na twahara**)) [438/ Sahihi Bukhary ]

****

**Swali la 219: Ni ipi hukumu ya wanao tembea na viatu ndani ya msikiti wa Makkah?**

**Jibu**: Kutembea na viatu katika msikiti mtukufu wa Makkah haitakiwi mtu kufanya hivyo, kwa kuwa wakiwachia watu kuingia na viatu wataingia na viatu vyenye uchafu na maji, na huenda wakauchafua msikiti kwa sababu ya uchafu wa viatu, jambo ambalo sheria imelikataza kama sheria imewaka wepesi kusiwe kunapatikana uharibifu ni lazima kulinda uhalibifu na kuuacha, kanuni wanayo penda kuisema Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, ((yakipingana manufaa au ya kulingana, au pamoja na kuyapa nguvu madhara hakika kuondoa madhara ni bora kuliko kuleta manufaa)), kwa misingi hiyo ndio sababu ilio mfanya Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake aache kubomoa Al-kaabaa, kwa ajili ya kuijenga upya kama alivyo kuwa ameijenga Na Nabii Ibrahimu rehma za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, lakini watu walivyo kuwa ni wapya kwenye Uiwislamu wametoka kwenye ukafiri aliacha

jambo hilo akihofia madhara akasema Mtume kumwambia Aisha radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake: **((Lau kama watu wako si wapya ninge bomoa Al-kaaba ,nikaijenga kwa msingi wa Ibrahimu, nikaweka milango miwili mlango watu wanaingia na mlango watu wanatoka)),** [1586/ Sahihi Bukhary, /1333/ Sahihi Muslim].

****

**Swali la 220: Mtu akiswali na baada ya swala akafahamu kuwa alikuwa amepinda kidogo kuelekea kibla mtu huyo atarudia kuswali?**

**Jibu**: Kupinda kidogo hakudhuru, na hii ni kwa mtu anaye swali sehemu isiyo kuwa ya msikiti mtukufu wa Makkah, kwa mtu aliye katika msikiti wa Makkah kibla yake ni kuielekea kaaba yenyewe anatakiwa aieleke Al Kaaba, wamesema Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu: Anae weza kuiona Al-kaaba ni lazima aielekee, kama atakuwa yupo ndani ya msikiti lakini akaelekea jiha ya Al-kaaba na hakuielekea Al Kaaba Atarudia kuswali kwa kuwa swala yake haikusihi, A mesema Mwenyezi Mungu: **[Basi elekeza uso wako upande wa msikiti mtakatifu na popote mtakapo kuwa zielekezeni nyuso zenu upande huo**] [Suratul Baqara: 144].

Mtu akiwa mbali na Al Kaaba hawezi kuiona- hata kama atakuwa yupo Makkah- ni lazima kwa mtu huyo kuelekea jiha ya Al Kaaba, wala hakudhuru kupinda kidogo, Amesema

Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (( **kati ya mashariki na magharibi kuna kibla ))** [344 / Atirmidhiy, / 1011/ Ibun Majah, / 225/1 / Mustadraki Al-Haakimu ]

Kwa kuwa watu wa Madina wanaelekea kusini, na kila kati ya mashariki na magharibi watu hao wanahaki ya kuelekea kibla, kwa mfano wanao swali wakiwa magharibi tunasema: kati ya kusini na kaskazini kuna kibla.

****

**Swali la 221: Watu wakiswali swala ya jamaa bila kuelekea kibla ni ipi hukumu ya swala hiyo?**

**JIBU**: Mambo hayo yana hali mbili:

**1-**Wakiwa sehemu ambayo hawawezi kufahamu kibla kipo upande gani, kwa mfano wakiwa safarini, na mbingu ikawa na mawingu, hawakupata muelekeo wa kufahamu jiha ya kibla wakiswali kwa kufanya juhudi za kujua jiha ya kibla ilipo, baada ya kuswali wakafahamu kuwa hawa kuelekea kibla hawata rudia kuswali, kwa kuwa wamemcha Mwenyezi Mungu kwa kadri ya uwezo wao, Amesema Mwenyezi Mungu: **[Basi mcheni Mwenyezi Mungu muezavyo**], [Suratu Taghaabun: 16]. Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Nikikuwam-**

**risheni amri ifanye kwa uwezavyo)**) [7288/ Sahihi Bukhary, / 1337/ Sahihi Muslim], amesema Mwenyezi Mungu kuhusu jambo hili: **[Na mashariki na magharibi ni za Mwenyezi Mungu kokote mnako elekea huko Mwenyezi Mungu yupo hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa na mjuzi**], [ 115/ Suratul Baqara: 115].

**2-**Wakiwa sehemu ambayo wanaweza kuliza jiha ya kibla,lakini wakapuzia kuliza , hali hii ni lazima walipe swala ambayo wameswali bila kuelekea kibla, hata kama wamefahamu kosa lao baada ya kupita muda wa swala au wakafahamu kabla ya kuisha muda wa swala,kwa kuwa wanamakosa na wamekosea jiha ya kibla,Hata kama hawakukusudia kupinda jiha ya Al-kaaba , lakini wamekosea kwa kupuuza na kudharau kuuliza jiha ya Al-kaaba, lakini ni lazima ufahamu kuwa kupinda kidogo jeha ya Al-kaaba hakuna madhara ya kusihi swala, kama mtu akipinda upande wa kulia kidogo au kushoto,kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa watu wa Madina, **((Kati ya mashariki na magharigi kuna kibla))** [344/ Atirmidhiy, / 1011/ Ibun Majah,/ 225/1 / Mustadraki Al-Haakimu.

**Kuna mambo nataka nikumbushe:**

Mtu akiwa ndani ya msikiti mtakatifu wa Makkah akawa anaiona Al Kaaba ni lazima aielekee kwa uso wake na macho yake na asieleke jiha ya Al Kaaba, kwa sababu akipinda kuielekea Al Kaaba yenyewee atakuwa hakuelekea kibla, Na ninawaona watu wengi katika msikiti mtukufu wa Makkah hawaielekei Al Kaaba yenyewee utakuta watu wanapanga swafu ndefu imenyoka, na tunafahamu kwa uhakika kuwa wengi kati ya hao hawakuele-

kea Al Kaaba yenyewee, na hili ni kosa kubwaa ni lazima kwa mwaislamu walitambue na wajitahadhari, na wasipendi, kwa sababu wakiswali katika hali hii wameswali bila kuelekea kibla.

****

## Swali la 222: Ni ipi hukumu ya kutamka niya?

**Jibu**: Amesema Mtume rahma na amani ziwe juu yake: **((Hakika kila amali ni kwa niya, hakika kila mtu atalipwa kwa niya yake**)), [1/ Sahihi Bukhary, /1907/ Sahihi Muslim], niya mahali pake ni moyoni haihitaji kuitamka, ukisimama kwenda kutwadha hiyo ni niya, haiwezekani kwa mtu mwenye akili ambaye hakulazimishwa kufanya jambo isipokuwa atakuwa amenuwiya, wamesema baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu: kama Mwenyezi Mungu ange tulazimisha kufanya mambo bila niya inge kuwa ametulazimisha kufanya mambo tusio yaweza.

Haikupokelewa hadithi kwa Mtume rehma na amani ziwee juu yake au Maswahaba walikuwa wakitamka niya, na wale tunao wasikia wakitamka niya watakuwa wanatamka kwa ujiga walio nao, au wanafata kauli za walio sema Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu wamesema: Inatakiwa niya itamkwe kwa ajili iende sambamba moyo na ulimi, lakini tunasema: kauli yao hii sio sahihi, kama jambo hili lingekuwa ni sheria au mafunzo ya

Uislamu Mtume rahma na amani ziwe juu yake ange libainisha jambo hilo kwa Uma wake, ima kwa kusema au kwa vitendo.

****

**Swali la 223: Ni ipi hukumu ya mtu kuswali faradhi nyuma ya anaye swali sun`na kama mtu anaye swali faradhi ya ishaa pamoja na wanao swali tarawehe?**

**Jibu**: Sio vibaya kuswali faradhi ya Ishaa nyuma ya Imamu anaye swalisha tarawehe, ameelezea Imamu Ahmadi Mwenyezi Mungu amarehemu [90 / Masaail Imamu Ahmad], akiwa ni msafiri akadiriki na Imamu mwanzo wa rakaa atatoa naye salamu, kama sio msafiri atakamilisha rakaa zilizo baki peke yake Imamu akitoa salamu.

****

**Swali la 224: Msafiri akimdiriki Imamu asio kuwa msafiri kwenye rakaa mbili za mwisho atatoa naye salamu kwa niya ya kupunguza?**

**Jibu**: Haruhusiwi msafiri akiwa anasalishwa na mtu asiye msafiri apunguze swala , kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Mlizo zidiriki mziswali zilizo wapita zikamilisheni))** [636 / Sahihi Bukhary, /602/ Sahihi Muslim], kwa hivyo msafiri akidiriki rakaa mbili nyuma ya Imamu asiye safari ni lazima aswali rakaa mbili baada ya Imamu kutoa salamu, haruhusiwi kutoa salamu na Imamu kupunguza rakaaa mbili. Mwenyezi Mungu ndio mjuzi.

****

**Swali la 225: Ni ipi hukumu ya kutembea kwa haraka kwenda kuwahi kuswali ?**

**Jibu:** Kutembea kwa haraka kwa ajili ya swala kumekatazwa, kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake ametuamrisha tutembee kwa utulivu na upole na ametukataza tusitembee kwa haraka, isipokuwa baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu! Wamesema: sio vibiya mtu kutembea kwa haraka ambako hakuonyeshi sura mbaya kama atakuwa anahofia kupitwa na rakaa mfano akiingia Msikitini akamkuta Imamu amerukuu akatembea kwa haraka, sio kama wanavyo fanya baadhi ya watu utamkuta anaenda kwenye swala anatembea kwa kishindo kikubwa, jambo hili limekatazwa, Mtume rehma na amani ziwe juu yake amrishwa kwenda kwa upole na utulivu na tusiende kwa haraka hii ndio bora hata kama mtu atapitwa

na rakaa kama alivyo sema Mtume rehma na amani ziwe juu yake katika hadithi tulio itaja hapo nyuma.

****

**Swali la 226: Hivi inaruhusiwa kutembea kwa haraka kwa ajili ya kuwahi rakaa na Imamu katika swala ya jamaa? Tupeni majibu naomba Mwenyezi Mungu awahifadhi.**

**Jibu:** Ukinguia msikitini na Imamu amerukuu usiende kwa haraka, na usiingie kwenye swala mpaka ufike kwenye swafu ya kwanza, kwa kuwa Mtume rehmana amani ziwe juu yake amesema kumwambia Abuu bakar radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake alivyo fanya hivyo**: ((Mwenyezi Mungu akuzidishie kupupia kuwahi swala lakini usirudie))**, [783/ Sahihi Bukhary].

****

**Swali la 227: Ni ipi hukumu ya mtu kusoma Qur`an ndani ya msikiti kwa sauti ya juu inayo washawishi watu wanao swali?**

**Jibu**: Hukumu ya kusoma Qur`an ndani ya msikitiki hali ambayo anawashawishi watu wengine wanao swali, au wanao soma darsa au anaye soma Qur`an kwasauti ya chini hukumu yake ni haramu, kwa sababu ya kufanya mambo yalio katazwa na Mtume rehma na amani ziwe juu yake amepokea hadithi Imamu Maliki katika kitabu chake [Al-Muwatwaa / 87/1 / 225/], kutoka kwa Bayadhu naye ni Fauwu Ibuni Omar radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alitoka akawakuta watu wakiswali wamepandisha sauti zao kwa kusoma, akasema: ((**Hakika anaye swali anaongea na mola wake azingatiye anayo ongeya naye, wala asi dhihirishe badhi yenu juu ya baadhi kwa kusoma Qur`ani**)), [ 1332/ Abuu Daud].

****

**Swali la 228: Baadhi ya watu wakingia msikitini karibu na muda wa kuqimu swala wanasimama wanusubiri Imamu aingie kuswalisha wanaacha kuswali tahiyatul Masjidi ni ipi hukumu ya kufanya hivyo?**

**Jibu**: Kama utakuwa umebaki muda mfupi swala ikimiwe na wakiswali tahiyatul Masjid hawawezi kuikamilisha sio vibaya kusimama kumsubili Imamu, kama watakuwa hawafahamu Imamu atakuja muda gani ni bora kuswali tahiyatu -masjidi, akija Imamu ikakimiwa swala na wewe upo kwenye rakaa ya kwanza utakata swala uende ukaswali faradhi, kama utakuwa upo kwenye rakaa ya pili utakamilisha lakini utaifanya rakaa hiyo ya pili nyepesi.

****

**Swali la 229: Tunawaona baadhi ya wanaume katika Msikiti mtukufu wa Makkah wanapanga swafu nyuma ya swafu ya wanawake katika swala za faradhi, je swala zao zinakubaliwa? Je Kuna maelekezo kwa watu hao?**

**Jibu**: Wanachuoni wanasema: Akiswali Mwanaume nyuma ya mwanamke hakuna ubaya, lakini ni kinyume na Sunna, kwa sababu Sunna wanawake wanakuwa nyuma ya wanaume, lakini kama mnavyo shuhudia katika msikiti mtukufu wa Makkah kuna kuwa na msongamani na dhiki wanakuja wanawake wanaweka

swafu, wanakuja wanaume baada yao wanaweka swafu nyuma yao, lakini anatakiwa mtu anaye swali ajitahidi kuliepuka hili kwa kadri ya uwezo wake, huenda ikatokea fitna kwa wanaume, mwanaume ajitahidi kuepuka kuswali nyuma ya wanawake, hata kama inaruhusiwa kwa walivyo sema Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, lakini tuna sema: ajitahidi mwanaume kujitenga na wanawake kwa kadri ya uwezo wake, na wanawake pia wajitahidi wasi swali maeneo ya karibu na wanaume.

****

**Swali la 230: Je inaruhusiwa kumtoa mtoto kwenye swafu ya swala?**

**Jibu**: Hairuhusiwi kumtoa mtoto kwenye swafu kwa kauli sahihi kwa hadithi ya Ibun Omar radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema: **((Asimsimamishe mwanaume mwanaume mwenzie mahali pake kisha akae yeye**)), [911/ Sahihi Bukhary, / 2177/ Sahihu Muslim], kufanya hivyo ni kuvunja haki ya mtoto, na kuonyongonyesha moyo wake, kumfanya aache kuswali, na kupandikiza chuki na roho mbaya katika moyo wa mtoto.

Tukisema inafaa kuwaweka watoto kwenye swafu ya mwisho

ili wajikusanye watoto wote katika swafu moja ukapatikana michezo katika swala, lakini sio vibaya kusimama nao kwenye swafu na kuwatenganisha tukifanya hivyo tutapunguza michezo.

****

**Swali la 231: Ni ipi hukumu ya kuswali kati ya nguzo mbili?**

**Jibu**: Kuswali kati ya nguzo mbili inaruhusiwa wakati wa dhiki kama itakuwa sio wakati wa dhiki asiswali kati ya nguzo mbili kwa kuwa inakata swafu**.** Imehaririwa /29/1/1419/H.

****

**Swali la 232: Ni ipi hukumu ya swafu ya wanawake? Je swafu ya shari kwa wanawake ni ya kwanza na ya kheri ni ya mwisho kwa ujumla, au ni katika hali ya kuto kuwepo sitara kati ya wanaume na mwanawake?**

**Jibu:** Makusudio kama watakuwa wanaume na wanawake katika sehemu moja swafu ya mwisho ni bora kwa wanawake kama alivyo sema Mtume rehma na amani ziwe juu yake:

**((Swafu bora kwa wanawake ni ya mwisho, swafu ya shari kwa wanawake ya mwanzo**)), [440/ Sahihi Muslim]. Imekuwa ya mwisho bora kwa sababu ya kuwa mbali na wanawume na ya kwanza imekuwa ya shari kwasababu inakuwa karibu na wanaume.

Kama watakuwa na sehemu yao maalum kama zilivyo katika sehemu nyingi za misikiti hakika swafu bora kwa wanawake niya kwanza kama ilivyo kwa wanaume.

****

**Swali la 233: Ni ipi hukumu ya swala ya mtu anaye swalia nje ya msikiti kama mtu anaye swali katika njia zilizo ungana na msikiti?**

**Jibu:** Kama msikiti ni mdogo hauwatoshi wanao swali mpaka swafu zikafika njiani na zikawa zimeungana hakuna ubaya, kama atakuwa wanaweza kumfata Imamu kwa kuwa hiyo ni dharura, imehaririwa /6/6/1413/H.

****

**Swali la 234: Ni jambo gani linalo angaliwa katika kupanga swafu? Inatakiwa mtu akutanishe kisigino cheke na kisigino cha mwenzie? Tupeni fatuwa Mwenyezi Mungu atawalipa.**

**Jibu**: Sahihi katika kupanga swafu ni kuelekeza visigno viwili kisigino kwa kisigino,sio ncha za vidole, kwa sababu mwili unakuwa sawa kwa kupitia visigino, vidole vya miguu na miguu vina tofautiana, yupo mwenye vidole virefu,na yupo mwenye vidole vifupi, hauwezi kudhibiti kuweka swafu sawa sawa isipokuwa kutumia visigino.

Kugusanisha visigino kwa visigino hakuna shaka jambo hilo limethibiti kwa Maswahaba radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yao walikuwa wanaweka sawa swa swafu kwa kukutanisha visigino kwa visigino, kwa maana kila mmoja anakutanisha kisigino chake na kisigino cha jirani yake ili upatikane kuelekeana na usawa wa swafu, makusudio sio mtu peke yake lakini pia ni kwa ajili ya mwengine kama walivyo sema Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu: ikikamilika swafu watu wakasimama inatakiwa kila mmoja akutanishe kisigino chake na kisigino cha jirani yake ili upatikane usawa, haina maana ulazima wa kukutanisha uwe ulazima kwakwe kwa swala zote.

Wapo wanao zidisha katika mambo haya baadhi ya watu wanakutanisha kisigino chake na cha mwenzake anaweka uwazi kati ya mguu wake na mguu wa mwenzie mpaka kuna kuwa

kati yake na jirani yake kwenye visigino kuna uwazi wanakuwa hawakufata Sunnah kwa kufanya hivyo, makusudio visigino viwe sawa sawa.

****

**Swali la 235: Je imethibiti kuinua mikono kwenye swali isipokuwa sehemu nne? Pia katika swala za Iddi mbili na swala ya jeneza?**

**Jibu:** Sehemu nne ambazo mtu anainua mikono ni lazima uzifahamu kwanza: Wakati wa takbira ya kuhirimia swala, wakati wa kurukuu, wakati wa kuinuka kutoka kwenye rukuu, wakati wa kusimama kutoka kwenye tahiyatu ya kwanza, hizo ndio sehemu ambazo imesihi hadithi ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, hadithi ya Ibun Omar radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake amesema**: ((Alikuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Anainua mikono yake anapo leta takbira kwa ajili ya swala, na anapo leta takbira wakati wa kwenda kurukuu, na anapo sema: ((Samia LLahu liman hamida**)) Anasema : ((**Alikuwa hafanyi hivyo akienda kusujudu))** [735/ Sahihi bukhariy / 390 / Sahihi Muslim].

Alikuwa Ibun Omar yupo makini kufatilia vitendo vya Mtume rehma na amani ziwe juu yake alimfatilia kwa vitendo akamuona anainua mikono kwenye takbira, na rukuu, na wakati wa kuinuka kutoka kwenye rukuu, na wakati wa kusimama ku-

toka kwenye tashahudi ya kwanza, (Tahiyatu ndogo) Akasema: ((Alikuwa hafanyi hivyo kwenye kusujudu)) Hatuwezi kusema hapo kuna kuthibisha na kukutaa, kilicho thibiti hutangulizwa kuliko ambacho hakikuthibiti kama ilivyo kuja kwenye hadithi ya Ibun Omar, na hadithi ya Ibun Omar ipo wazi inaweka msisitizo kuwa alikuwa hainui mikono isipokuwa sehemu nne, kitu ambacho amekiona ni kiunua mikono anapo rukuu na anapo inuka kutoka kwenye rukuu, kisha anasema hafanyi hivyo kwenye kusujudu, hivi tunasema alighafilika hakuwa makini? Haiwezekani hilo, kwasababu ameweka wazi kuwa hakuinua mikono wakati wa kusujudu bali alikuwa anainua wakati wa kurukuu na kutoka kwenye rukuu.

****

**Swali la 236: Maamuma akimkuta Imamu amerukuu ataleta takbira mbili?**

**Jibu**: Mtu akiingia msikitini akamkuta Imamu amerukuu kisha akaleta takbira ya kuhirimia swala anatakiwa arukuu harakaa kumfata Imamu, takbira ya rukuu ni Sunna na sio wajibu, akileta takbira ya kurukuu ni bora ,akiiacha hakuna ubaya, kisha baada ya hapo jambo hilo limegawanyika sehemu tatu:

**1-**Hali ya kwanza: Awe na yakini kuwa amefika kwenye rukuu kabla ya Imamu kuinuka kutoka kwenye rukuu, atakuwa ameiwahi rakaa, utaanguka ulazima wa kusoma surat Al-fatiha (Al-Hamdu).

**2-**Hali ya pili: Awe na yakini kuwa Imamu ameinuka kutoka kwenye rukuu naye hajafika kwenye rukuu,rakaa itakuwa imempita, ni waJibu kuilipa baada ya kutoa salamu Imamu.

**3-**Hali ya tatu: Ni kuwa na mashaka amemkuta Imamu kwenye rukuu au Imamu ameisha inuka kabla ya yeye kufika kwenye rukuu? Katika hali hii atafata dhana yake imeelekea wapi dhana atakayo iona kuwa inanguvu akiona kuwa alimuwahi Imamu bado yupo kwenye rukuu atakuwa ameiwahi rakaa,lakini akiona kuwa hakumuwahi Imamu basi rakaa itakuwa imempita, katika hali hii kama kuna kitu kitakuwa kimempita kwenye swala atasujusi sijida ya kusahau baada ya salamu,kama hakijampita kitu katika swala,kwa mfano rakaa aliokuwa anatilia shaka ni rakaa ya kwanza, dhana yake ikampeleka kuwa ameiwahi, hato sujudu sijda ya kusahau katika hali hiyo, kwa kuwa swala yake ipo sawa sawa na swala ya Imamu, na imamu hubeba sijida ya kusahau ya Maamuma kama Maamuma atakuwa hakuchelewa kwenye swala.

Kuna hali nyingine ya kutia shaka, ni mtu kuwa hana uhakika kuwa amemkuta Imamu kwenye rukuu bila kuwa na uhakika, katika hali hii anachukulia yakini nayo ni kuwa hakumuwahi Imamu kwenye rukuu, kwa sababu ndio asili, itakuwa rakaa hiyo imempita, atasujudi sijida ya kusahau kabla ya kutoa salamu.

Kuna mambo nataka nikumbushe kuhusu haya mambo ya kuwahi rakaa, wapo watu wengi wakiingia msikitini na Imamu amerukuu anaanza kujikohoza kwanguvu, na wengine huongea kusema: ((**Ina allah maa swaabirina**)), wengine hupiga miguu yao chini kwenye ardhi yote haya ni kinyume na Sunnah, (Mafundisho sahihi ya Mtume Muhammadi) kufanya hivyo nikum-

shawishi Imamu na Maamuma, wapo watu wakiingia msikitini na Imamu amerukuu wanatembea kwa haraka kuliko kubaya, Mtume rehma na amani amekataza hilo, Amesema **((Mkisikia swala inakimiwa nendeni kwenye swala kwa upole na utulivu, na msiendee kwa haraka, mlizo diriki mziswali, zilizo wapiti mzikamilishe))**, [636/ Sahihi Bukhary, /602 / Sahihi Muslim].

****

**Swali la 237: Ni ipi hukumu ya kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto juu ya kifua au moyo? Na ni ipi hukumu ya kuweka mikono miwili chini ya kitovu? Hivi kuna utofauti kati ya mwanamke na mwanaume katika hukumu hizo?**

**Jibu**: Hukumu ya kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto katika swala ni Sunna, kwa hadithi ya Sahli Ibun Saad radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake mesema: **((Watu walikuwa wanaamrishwa aweke mwanaume mkono wake wakulia juu ya mkono wakushoto katika swala))**, [740/ Sahihi Bukhary].

**Mikono inawekwa wapi?**

**Jibu:** Kauli iliyo karibu kwa Maswahaba kwenye jambo hilo mikono huwekwa juu ya kifua, kwa hadithi ya Wail Ibun Hujri radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake! Kuwa Mtume

rehma na amani ziwe juu yake: ((**Alikuwa anaweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto juu ya kifua**)), [479/ Ibun Khuzayma, /401/ Sahihi Muslim], Hadithii hii hata kama inasehemu ya udhaifu, lakini ipo karibu kwenye usahihi kuliko hadithi zingine.

Kuhusu kuweka mikono kwenye moyo upande wa kushoto jambo hilo ni lauzushi halina asili kwenye dini.

Kuhusu kuweka mikono chini ya kitovu imepokewa habari katika matendo ya maswahaba kuwa Ally Ibun Abii twalibi radhi za mwenyezi Mungu ziwe juu yake!alikuwa anaweka mikonoo chini ya kitovu lakini ni riwaya dhaifu, hadithi ya Wail Ibun Hajri radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! Inanguvu kuliko athari iliyo pokewa kuhusu Ally Ibun Abii Twalibi.

Hakuna utofauti wa hukumu kati ya mwanamke na mwanaumee, kwa kuwa asili ni kulingana Wanaume na wanawake kwenye hukumu, isipokuwa mpaka uje ushahidi wa kutenganisha hukumu kati ya mwanamke na mwanaume, sifahamu ushahidi sahihi unaotenganisha hukumu kati ya mwanamke na mwanaume katika sun`na hiyo.

****

**Swali la 238: Ni ipi hukumu ya kudhihirisha kusoma bismillah?**

**Jibu**: Kauli iliyo na nguvu haitakiwi kusoma bismillah kwa sauti kwenye swala, Sunna ni kusoma kwa siri, kwa kuwa bismillah sio aya katika Surat Al-fatiha, (Al-hamdu) lakini kama mtu ataisoma kwa sauti katika baadhi ya swala hakuna ubaya, wamesema baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu: inatakiwa isomwe kwa sauti baadhi ya nyakati, kwa kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake imepokewa hadithi kuwa alikuwa anaisoma kwa sauti **((Alikuwa akiidhihirisha**)), [904/ An Nasaai, /1788/ Ibun Hibani,/ 499/ Ibun Khuzayma].

Lakini iliyo thibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake **((Alikuwa haidhihirishi**)), [ 399/ Swahihi Muslimu].

Lakini kama itasomwa kwa ajili yamadhebu ya watu au kuwazowesha watu kuwa bismillah husomwa katka baadhi ya nyakati nadhani hakuna ubaya.

****

**Swali la 239: Ni ipi hukumu ya kusoma dua ya ufunguzi wa swala?**

**Jibu:** Kusoma dua ya ufunguzi wa swala ni Sunna sio wajibu, katika swala za faradhi hata katika swala za Sunna.

Anacho takiwa kukifanya mtu ni kusoma dua za ufunguzi wa swala tofauti tofauti kama ilivyo pokelewa katika hadithi za Mtume rehma na amani ziwe juu yake katika swala hii anasoma dua hii na katika swala nyingine anasoma dua ya ufunguzi

nyingine, ili apate kufata sunna ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake! kwa kusoma dua hizo za ufunguzi wa swala, kama atakuwa anaifahamu dua ya ufunguzi wa swala moja tu sio vibaya kusoma hiyo hiyo kila swala, kwa sababu Mtume alikuwa anasoma dua za ufunguzi wa swala tofauti tofauti, kwa ajili ya wepesi kwa wafwasi wake, pia nyiradi baada ya swala Mtume alikuwa anasoma nyiradi tofauti tofauti kwa faida mbili:

**1-**Mtu asiwe anasoma nyiradi aina moja kila siku, kwa sababu mtu akiwa anasoma nyiradi aina moja kila siku atakuwa anasoma kwa mazoea, hata akighafilika atajikuta anasoma tu hata bila kukusudia, kwa kuwa imekuwa ni ada yake kusoma nyiradi hizo, zikiwa nyiradi tofauti tofauti akawa leo anasoma hizi kesho anasoma zingine kwa kufanya hivyo moyo wake utakuwa unazingiatia, na itampelekea kuzingatia anayo ya soma na kuyafahamu.

2-kuwarahisisishia Uma wake kwa hali ambayo atasoma nyiradi baadae atasoma zingine kwa kulingana na munaasaba .

Kwa sababu ya faida hizi mbili baadhi ya ibada zimekuja kwa namna tofauti tofauti mfano dua ya ufunguzi wa swala tashahudi, (Tahiyatu) nyiradi baada ya swala.

****

**Swali la 240: Hivi ni sun`na kuitkia Aamin ?**

**Jibu**: Ndio, kuitkia Aamin ni Sunnah iliyo tiliwa mkazo, haswa anaposema Imamu aamin, kama ilivyo thibiti katika (Sahihi Bukhary na Sahihu Muslim), Hadithi ya Abi Hurayra radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kuwa Mtume rahma na amani ziwe juu yake amesema: **((Imamu akisema Aamin nanyi itikeni Aamni pamoja naye, ikiwafikiana kuitikia Aamin kwakwe na Malaik mtasamehewa madhambi yalio tangulia)), [**780/ Sahihi Bukhary, /410/ Sahihi Muslim].

Kuitikia Aamin kwa Imamu na Maamuma ni wakati mmoja, kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Akisema Imamu** [**Waladhwaaliin**], Semeni: Aamin)) [782/ Sahihi Bukhary, 410/ Sahihi Muslim].

****

**Swali la 241: Baadhi ya Maamuma inapo somwa: [Iyaka naabudu waiyaka nastaainu] wanasema: isataminna bi Ilah!, ni ipi hukumu ya kusema hivyo?**

**Jibu:** Jambo linalo takiwa katika haki ya Maamuma akaye kimya amsikilize Imamu wake, Imamu akimaliza kusoma Suratul Fatiha (Al-Hamdu) Imamu atasema Aamin, na Maamuma

naye atasema pamoja na Imamu Aamin, kuitikia Aamin kwa Maamuma inatosha kwake kutikia Aamin inachukuwa nafasi kwa kila kitu ambacho angesoma wakati Imamu anasoma Suratul Fatiha.

****

**Swali la 242: Ni ipi hukumu ya kusoma Suratul Fatiha (Alhamdu) kwenye swala?**

**JIBU**: Wametofautiana Wanachuoni katika kusoma Suratul Fatiha kauli nyingi:

**1-kauli ya kwanza:** kusoma Surat Suratul Fatiha sio lazima kwa Imamu wala Maamuma, wala anaye swali peke yake, wala katika swala za kusoma kwa sauti na ambazo hausomi kwa sauti, wakasema ni wajibu kusoma sehemu katika Qur`an, wakatoa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu katika Surati Muzamil: [Basi someni kilicho chepesi katika Qur`ani] Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Soma kilicho chepesi kwako katika Qur`an**)), [ 757/ Sahihi Bukhary, /397/ Sahihi Muslim].

**2-kauli ya pili:** kusoma Suratul Fatiha ni nguzo ya swala kwa Imamu, na Maamuma, na anaye swali peke yake, katika swala za kusoma kwa sauti na swala ambazo hazi somwi kwa sauti,na aliechelewa jamaa, na aliye wahi swala ya jamaa akanza pamoja na Imamu.

**3-kauli ya tatu:** kusoma Suratul Fatiha ni nguzo kwa Imamu

na anaye swali peke yake, na sio wajibu kwa Maamuma kabisa katika swala za kusoma kwa sauti na swala zinazo somwa kwa sauti.

**4-kauli ya nne:** kusoma Suratul Fatiha ni nguzo kwa Imamu na anaye swali peke yake katika swala za kusoma kwa sauti na zisizo somwa kwa sauti, na ni nguzo kwa Maamuma katika swala zakuto kusoma kwa sauti kinyume na swala zinazo somwa kwa sauti.

**Kauli iliyo na nguvu kwangu:** kusoma Suratul Fatiha ni nguzo kwa Imamu na Maamuma na anaye swali peke yake katika swala za kusoma kwa sauti na ambazo hazi somwi kwa sauti, isipokuwa aliye chelewa akimkuta Imamu yupo kwenye rukuu kusoma Suratul Fatiha kunaanguka kwa Maamuma katika hali hii, anatujulisha hilo hadithi ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake! **((Hana swala mtu ambaye hakusoma** Suratul Fatiha)), [756/ Sahihi Bukhary, / 394/ Sahihi Musilim]. Na kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake! ((A**takaye swali na hakusoma mama wa Qur`ani swala yake ni batili**)) [394/ Swahihi Muslim], pia inatufahamisha hadithi ya Ubada Ibun Swaamiti radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alimaliza kuswali subhi akasema kuwambia maswahaba zake radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao: **((Huenda mnasoma nyuma ya Imamu wenu?**)) Wakasema : Ndio iwe mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Akasema: **(( Msisome isipokuwa mama wa Qur`an, kwani swala haiswi kwa mtu ambaye hakusoma hiyo.))** [ 316/5/ Imamu Ahmadi, 823/ Abuu Daud, 311/Tirmidhy]. Ushahidi huu ni kwa swala zinazo somwa kwa sauti.

Kuhusu ushahidi : Wa aliye chelewa akamkuta Imamu yupo kwenye rukuu hato soma Suratul Fatiha ni hadithi ya Abuu bakar radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake alimkuta ameruku, akatembea kwa haraka akarukuu kabla ya kufika kwenye swafu, kisha akasogea akaingia kwenye swafu, Mtume rehma na amani ziwe juu yake alivyo maliza swala yake aliuliza aliye fanya hivyo, akasema Abu bakar mimi iwe mjumbe wa Mwenyezi Mungu, akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Mwenyezi Mungu akuzidishie pupa katika mambo ya khri lakini usirudie**)), [783 / Sahihi Bukhary] Mtume hakumuamrisha kurudia rakaa ambayo alifanya haraka ili isiimpite, kama inge kuwa ni lazima Mtume ange muamrisha kama alivyo muamrisha yule aliye swali bila kutulia katika swala arudiye kuswali, huu ni ushahidi wa mandiko.

**Ushahidi wa mtazamo tunasema:**

Mtu aliye chelewa hakuwahi kisimamo ambacho ndio shemu ya kusoma Suratul Fatiha, kwa kuwa hakuwahi basi imeanguka uwaJibu wa kusoma sura hiyo, kwa ushahidi mtu aliye katika mkono sio lazima kuosha kwenye mfupa ulio chini ya bega badala ya sehemu ya dhirai , isipokuwa hakuna ulazama wa kuosha kwa kuwa sehemu ya kuosha haipo, kwa hivyo ulazima wa kusoma Suratul Fatiha haupo kwa mtu aliye mkuta Imamu amerukuu,kwa kuwa hakuwahi kisimamo ambacho ndio sehemu ya kusoma Suratul Fatiha kusimama kuna kuwa sio lazima kwaysababu ya kumfata Imamu.

**Kauli hii ndio yenye nguvu kwangu na ndo sahihi,** kwa hadithi ya Ubada Ibun Swamiti radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake niliyo ieleza hapo nyuma- nayo Mtume alivyo maliza kuswali subuhi akawauliza manasoma nyuma ya Imamu wenu

wakajibu ndio akasema msisome zaidi ya surat al-fatiha, kama sio kauli hiyo ya Mtume isinge kuwa ni lazima kusoma surat al-fatiha kwa Maamuma katika swala zinazo somwa kwa sauti ndio kauli iliyo na nguvu,kwa kuwa anaye sikiliza Qur`ani ikisomwa anapata malipo kama anaye soma,kwa sababu hiyo amesema Mwenyezi Mungu kumwambia Musa rehma na amani ziwe juu yake**: [Hakika nimewaitikia maombi yenu]** pamoja kuwa aliye kuwa anaomba ni Mussa peke yake. Amesema Mwenyezi Mungu**: [Na Musa akasema: Mola wetu! Hakika wewe umempa Firauni na wakuu wake mapambo na mali katika maisha ya dunia, hivyo wanapoteza watu na njia yako, Mola wetu! yafutilie mbali mali yao na zifunge nyoyo zao, wasiamini mpaka waione adhabu chungu**], [Surat Yunus: 88]. Hivi Mwenyezi Mungu ameeleza kuwa haruna rehma na amani ziwe juu yake aliomba? Jawabu : hapana ,pamoja na hivyo amesema Mwenyezi Mungu: [**hakika nimewaitikia maombi yenu**] Wamesema Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu: kuelezea kuwa Musa alikuwa anaomba Haruna anaitikia Aamin.

Kuhusu hadithi ya Abuu Hurayrat radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake ambayo Amesema: ((**Atakaye kuwa Imamu kisomo cha Imamu kwake nikisomo**)) [339/ Imamu Ahmadi, /850/ Ibun Majah.] hadithi hii haisihi, kwa kuwa ni hadithi mursala kama alivyo sema Ibun Kathiri Mwenyezi Mungu amrehemu amesema hayo mwanzo wa tafsiri yake [109/1/ tafsiri Ibun Kathiri] pia hadithi hii hauezi kuitolea hoja, wale ambao wametoa hoja kupitia hadithi hiyo baadhi yao wanasema: Ni lazima kwa Maamuma kusoma katika swala zisizo somwa kwa sauti hawakusema kuwa kisomo cha Imamu kinatosha kwa Maamuma.

Mtu akisema:kama Imamu hakai kimya baada ya kumaliza kusoma surat al-fatiha ni muda gani Maamuma atasoma Suratul Fatiha?

**Tunasema:** Maamuma atasoma Suratul Fatiha wakati Imamu akiwa anasoma kwa sababu maswahaba walikuwa wanasoma na Mtume rehma na amani ziwe juu yake nae anasoma, Akasema Mtume: **((Msisome zaidi ya mama wa Qur`ani, kwani hana swala mtu ambaye hakuisoma**)), [316/5/ Imamu Ahmadi, / 823/ Abuu Daud/, 311/ Atirmidhiy] .

****

**Swali la 243: Ni muda gani Maamuma atasoma Suratul Fatiha (Alhamdu) katika swala atasoma wakati Imamu anasoma Suratul Fatiha au akiwa anasoma sura nyingine?**

**Jibu:** Ni bora Maamuma asome Suratul Fatiha baada ya kumaliza Imamu kusoma Suratul Fatiha, kwa kuwa kukaa kimya wakati kisomo cha nguzo ya swala , kama atasoma Suratul Fatiha na Imamu anasomaa Suratul Fatiha hatoweza Maamuma kumsikiliza Imamu wakati anasoma nguzo ya swala, na Maamuma kukaa kimyaa kusikiliza kisomo cha Imamu baada ya Suratul Fatiha ni Sunnah, ni bora Maamuma akaye kimya wakati Imamu anasoma Suratul Fatiha, kwa kuwa kusikiliza kisomo ambacho

ni nguzo ni muhimu kuliko kusikiliza kisomo cha sun`na, sehemu ya kwanza, ama sehemu ya pili, Imamu atakapo sema **[Wala dhwaalin]** na wewe haukumfata na kumsikiliza hautasema ((Aamin) na hapo utakuwa umetoka kwenye jamaa, iliyo bora ni kumsikiliza Imamu anapo soma Suratul Fatiha akimaliza ndio unasoma hata kama atakuwa anasoma sura nyingine.

****

**Swali la 244 : Vipi tutaweza kunyenyekea katika swala, na tunapo soma Qur`an katika swala na nje ya swala?**

**JIBU:** Unyenyekevu katika swala ni muhimu sana kama ubongo kwenye kichwa cha binaadamu, maana ya unyenyekevu ni kuhudhurisha moyo, na moyo wake asi uyumbishe kulia na kushoto kufiria mambo mengine wakati yupo ndani ya swala, mtu akihisi kuwa mawazo yamekuwa mengi mapaka hajijui kuwa yupo kwenye swali aombe kujilinda kwa Mwenyezi Mungu na shetwani aliye laaniwa kama ilivyo thibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, [68/2203/]. Hakuna shaka kuwa shetwani anafanya kila njia kuharibu ibada zote haswa ibada ya swala ambayo ndio ibada bora baada ya kutamka shahada mbili, shetwani humuendea mtu anaye swali anamwambia: kumbuka jambo fulani na jambo fulani, anakuwa anampa mawazo katika mambo yasio kuwa na faida, akimaliza kuswali tu mawazo yote hutoweka. Inatakiwa kila mtu aji-

tahidi anapo kuwa anaswali aelekee kwa Mwenyezi Mungu kwa moyo wake wote na ache mawazo ya dunia, na ikitokea amehisi mawazo ajilinde kwa Mwenyezi Mungu kutokana na shetwani aliye laaniwa, hata kama atakuwa amerukuu au yupo kwenye tahiyatu au amekaa kikao kidogo kati ya sijida mbili, au shemu nyingine katika swala.

Katika mambo yanoyo leta unyenyekevu ni mtu ahisi kuwa amesimama mbele ya Mwenyezi Mungu! Na kuwa yupo anaongea na Mwenyezi Mungu!.

****

**Swali la 245: Je kuna ushahidi kuwa Mtume alikuwa anakaa kimya baada ya kumaliza kusoma Suratul Fatiha na kusoma sura nyingine ?**

**JIBU**: Imamu kukaa kimya kati ya kusoma Suratul Fatiha na kusoma sura nyingine haikupokelewa hadithii kuwa Mtume alikuwa anakaa kimyaa kwa walivyo elezea baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu kuwa Imamu atakaa kimya kwa muda kidogo kiasi amabacho Maamuma atasoma Suratul Fatiha, Imamu atakaa kimya akivuta pumzi ya kuwanza kusoma sura nyingine, na Maamuma atatumia nafasi hiyo kusoma Suratul Fatiha, mpaka anze kusoma hata kama hato maliza kusoma

Maamuma atamalizia atakapo anza kusoma Imamu sura nyingine, kukaa kimya huko nikwa muda mfupi sana.

****

**Swali la 246: Mtu aliye chelewa rakaa moja ya swala ya Al-fajir, atakamilisha rakaa iliyo baki kwa kusoma kwa sauti au bila ya sauti?**

**Jibu**: Anakhiyari mtu huyo akita atasoma kwa sauti asipo taka hato soma kwa sauti, lakini ni bora asisome kwa sauti, kwa sababu inawezekana kuna watu pembeni yake wanalipa swala atawashawishi kwa kusoma kwake kwa sauti.

****

**Swali la 247: Nimesoma katika kitabu kimoja kinacho elezea swala ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake ya kwamba kuweka mikono juu ya kifua baada ya kutoka kwenye rukuu ni bidaa ya upotovu, ukweli ni upi?**

**Jibu**: Kwanza: mimi Napata shida kusema mtu huyo aliye sema hivyo amekhalifu Sunnah kwa kumwita mtu aliye fikia daraja ya kujitahidi kuwa ni mtu wa bidaa, watu wanao weka mikono yao juu ya vifua baada ya kurukuu wanafanya hivyo kwa ushahidi wa hadithi, watu kusema: Anaye weka mikono ni mzushi, kwa kuwa ametofautina na sisi katika mambo ya ijitihadi, neno hilo la kumwita mtu ni mzushi ni neno kubwa, na haitakiwi mtu amwite mwenzake (Ni mtu wa bidaa) katika mambo kama haya, kwa kuwa kunapeleka kuwaweka mabli watu wao kwa wao katika mambo ya ijitihadi ambayo haki huwa ni matarajio katika kauli hiyo, watu watatengeana katika mambo ambayo Mwenyezi Mungu ndio mjuzi.

**Ninasema:** kumwita aliye weka mkono juu ya kifua baada ya kuruku ni mzushi au amefanya bidaa: jambo hilo ni kubwa sana kwa binaadamu, hatakiwi awaite ndugu zake kwa sifa hiyo.

**Iliyo sahihi:** kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto baada ya kutoka kwenye rukuu ni Sunna, ushahidi ni hadithi ipo katika (Sahihi Bukhary) imepokewa kutoka kwa Sahal Ibun Saadi radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake amesema: **((Watu walikuwa wanaamrishwa waweke mkono wa kulia juu ya mkono wakushto kwenye swala)**), [740/ Sahihi Bukhary]. Ushahidi katika hadithi ni kufatanisha na kuelewaza mafungo tunasema; Mikono inawekwa wapi mtu akiwa amesujudu?

**Jibu**: Inawekwa juu ya ardhi.

**Tunasema:** mikono inawekwa wapi ukiwa umerukuu?

**Jibu:** juu ya magoti.

**Tunasema** : mikono unaweka wapi unapo kuwa umekaa?

**Jibu:** juu ya mapaja mawili, inabaki hali ya kusimama kabla ya kuruku na baada ya kurukuu inakuwa imo katika hadithi ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Amesema **(( Watu walikuwa wanamrishwa waweke mkono wa kulia juu ya mkono wakushto kwenye swala)**) [740/ Sahihi Bukhary] na huu ndio ukweli unao tujilisha Sunna ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake. Jibu la swali hili limegawanyika sehemu mbili:

**1-Sehemu ya kwanza:** Haifai kuzembea kuwaita watu ni watu wa bidaa katika mambo ambayo kuna fursa ya jitihada kwa Wanachuoni.

**2-Sehemu ya pili:** iliyo sahihi ni kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto baada ya kuinuka kutoka kwenye rukuu ni sun`na na sio bidaa, kwa ushahidi wa hadithi ambayo tumeitaja kwa kuwa hadithi imezingumzia sehemu zote inatakiwa kuweka mkono wakulia juu ua mkono wakushoto, na imenyambuliwa katika hali ya kurukuu, na kusujudu, na kukaa, kwa kuwa hadithi imekuja kwa sifa maalum ya kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wakushoto katika hali zote.

****

**Swali la 248: Baadhi ya watu wanazidisha neno: (Ashukri) baada ya kauli (Rabbana lakal-hamdu)) ni yapi mawazo yenu?**

**Jibu:** Hakuna shaka mtu kusoma nyiradi zilizo thibiti ni bora mtu akiinuka kutoka kwenye rukuu Aseme: ((Rabana walaka al-hamdu)) Asizidishe (Washukri) kwas ababu haikuthibi kwa Mtume alikuwa akizidisha neno hilo.

Nyiradhi zilizo thibiti kwenye hadithi za Mtumee baada ya kutoka kwenye rukuu ni :

**1-Rabana Walakal-hamdu.**

**2-Rabana Lakal-hamdu.**

**3-Allahuma Rabana lakal-hamdu.**

**4-Allahuma Rabana walakal-hamdu**.

Hizi ndio nyiradi zilizo thibiti kwa Mtume anatakiwa azisome hizo, lakini asizisome zote kwa mara moja, anasoma hii katika swala hii na nyingine katika swala nyingine, baadhi ya swala anasema ; Rabana walakal-hamdu, na swala nyingine anasema: Rabana lakal-hamdu, na nyingine anasema: allahuma Rabana lakal-hamdu, na nyingine anasema : Allahuma Rabana walakal-hamdu.

Ama neno shukri halikuthibi kwenye hadithi ni vizur kuliacha.

****

**Swali la 249: Mtu anaporomoka vipi kwenda kusujudu?**

**Jibu:** Kushuka kusujudu unatanguliza kwanza magoti , kisha viganja vya mikono miwili, kwa kuwa Mtume alikataza mtu kuporomoka kusujudu akafikia viganja vyake viwili vya mikono, Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake**:** **((Atakapo sujudu mmoja wenu asipige magoti kama anavyo piga magoti ngamia, na aweke mikono yake kabla ya magoti)),** [381/2/ Imamu Ahmadi, /840/ Abuu Daud, /1090/ An Nasaai.

Tutaelezea kuhusu hadithi hiyo katika sentesi ya kwanza **(( Asipige magoti kama anavyo piga magoti ngamia)),** katazo ni kwenye sifa ya kusujudu, kwa kuwa amezungumizia kwa herufi ya kafu na herufu ya kafu inamaana ya kufananisha,haina maana ya kiuongo ambacho mtu anaye kisujudia, kama ingekuwa anakusudia kiungo anacho kisujudia Angesema (Asipige magoti juu ya anayo ya piga magoti ngamia,) hapo tungesema: Usipige magoti, kwa kuwa ngamia anapiga magoti kwa magoti yake, lakini Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakusema: (asipige magoti juu ya anayo ya piga magoti ngamia) lakini amesema: (**Asipige magoti kama anavyo piga magoti** ) katazo lipo kwenye sifa sio kiungo ambacho anasujudia.

Amelezea mwanachuoni Ibun Qayimu rehma za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! Katika kitabu (Zaadi Al-miaadi) 215 /1 /Amesema kuwa mwisho wa hadithi hiyo imegeuzwa na mpokezi wa hadithi, miwsho wa hadithi**: ((Na aweke mikono yake kabla ya magoti))** amesema Ibun Qayimu: alio sahihi ni

(**Na awekee magoti yake kabla ya mikono**)), kwa kuwa akiweka mikono kabla ya magoti atakuwa amepiga magoti kama anavyo piga magoti ngamia, ngamia anavyo piga magoti huanzia mikono yake,na anaYe muona ngamia wakati anapiga magoti atatoa ushahidi wa haya maneno yangu.

Kwa hivyo kama tunataka kufata sahihi na tufate mwisho wa hadithi ni kubadilisha sentesi tunasema: (**Na aweke magoti yake kabla ya mikono**) kama ataweka mikono kabla ya magoti kama ilivyo kuja kwenye hadithi- Atapiga magoti kama anavyo piga magoti ngamia, itakuwa mwanzo wa hadithi na mwisho wake vinapingana.

Wametunga risala baadhi ya ndugu katika Uislamu ameiita risala hiyo: (Fat-hul-maabudu fiy wadhwai rukubatayin Qabla yadayin) -Maana yake ufunguzi wa kufanya ibada katika kuweka magoti mawili kabla ya mikono miwili katika kusujudu – Wamefafanua vizuri sana maswala hayo.

**Tunasema:** Sunna ambayo Mtume rehma na amani ziwe juu yake ametuamrisha katika kusujudu ni mtu aweke magoti yake mawili kabla ya mikono yake.

****

**Swali la 250: Ni ipi hukumu ya mtu kijinyosha zidi katikati ya kusujudu?**

**Jibu**: kujinyosha kuliko zidi katika hali ya kusujudu ni kinyume na sun`na,walio sifu swala ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakuna hata mmoja aliesema kuwa Mtume alikuwa anaunyosha mgogngo wake anapo kuwa kwenye sijida, wamesema alikuwa anaunyosha mgongo wake anapo kuwa kwenye rukuu, [498/ Sahihi Musilim]. Jamabo ambalo linafahamika kwenye kusujudu ainue tumbo lake lisishikane na mapaja tumbo liwe juu, sio anyoshe mgongo kama wanavyo fanya baadhi ya watu.

****

**Swali la 251: Je kunaushahidi kuwa alama inayo toka kwenye paji la uso kwa sababu ya kusujudi ni alama miongoni mwa alama za watu wema?**

**Jibu**: Hiyo sio alama ya watu wema, isipokuwa ni nuru inayo kuwa kwenye paji la uso, na inaenea kwenye kifua, na tabia njema na mambo mengine kama hayo, kuhusu alama inayo mtoka mtu kwa ajili ya kusujudi inaweza kutoka alama kwa mtu ambaye anaswali swala za faradhi tu na haswali swala za sunn`na kwa sababu ya ngozi yake kuwa nyepesi, na inaweza alama hiyo isitokee kwa mtu anaye swali sana na fardahi pia anarefusha sujudu.

****

**Swali la 252: Je imepokewa hadithi sahihi ya kutikisa kidole katika kikao kidogo kati ya sijida mbili?**

**Jibu**: Ndio, imepokewa hadithi katika (Sahihi Muslim) Hadithi ya Abdul-llah Ibun Omar radhi ya Mwenyezi Mungu iwe ju yake kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alikuwa akikaa katika swala kaelezea Ibun Omar kuwa alikuwa anaashiriya kwa kidole chake [580 / Sahihu Muslim], katika upokezi mwengine wa hadithii akikaa kwenye tashahudi [110 / 580 / Sahihu Muslim]. Tamko la hadithi ya kwanza linakusanya vikao vyote na tamko la hadithi ya pili ni tamko la kikao maalum, na kanuni kuwa kutaja tamko maalum katika jambo ambalo limetajwa katika jambo linalokusanya vitu vyote huwa hayapingani matamko hayo, kwa mfano: Mtu akimwambia mwenzie : wanafunzi wametunzwa, kisha akasema Muhammadi ametunzwa, na Muhammadi ni miongoni mwa wanafunzi , kusema hivyo haimanishi kuwa wanafunzi wengine hawakupewa zawadi, wameelezea Wanachuoni wa elimu ya Usulul-fqih Mwenyezi Mungu awarehemu! Kuhusu mambo haya na ameeleza mwanachuoni Sheikh Shingitwi Mwenyezi Mungu amrehemu katika kitabu (Adhuwau Al-Bayani ) [355 / 1].

Lakini kama angesema : Wanafunzi wametunzwa, kisha akasema : Hatunzwi mwanafuzi anaye lala darasani, kauli hii inakusudia watu maalum, kwa sababu kilicho tajwa mwazo ni tofauti na hukumu iliyo tajwa sehemu ya kujumwisha watu wote.

Kwenye hadithi kumetajwa jambo maalumu, amepokea ha-

dithi Imamu Ahmadi katika (Musanadi) kwa upokezi ambao amesema mtunzi wa kitabu ( Al-fatihu arabani) kuwa upokezi wa hadithi ni mzuri [ 147/3/ Al-fathu Rabaani]. Wamesema baadhi ya walio kuwa wakinyambua maana katika kitabu cha ( Zaadi Al-miaad) [ 231/1, zaadul-Miaad] Wamesema kuwa upokezi wake ni sahihi, **((kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alikuwa akikaa kati ya sijida mbili anakunja vidole vyake na anaashirya kwa kidole shahada))**, **Anaesema:** Haifai kutikisa kidole , tunamwambia : mkono wakulia utakuwa unafanya nini? **Akisema:** Anauweka juu ya paja tutamtaka ushahidi wa kunyosha mkono wakulia juu ya paja, na haikupokelewa hadithi kuwa Mtume alikuwa ananyosha mkono wake wakulia juu ya paja lake, kama angekuwa anaunyosha mkono wake maswahaba wangesema kama walivyo sema kuwa alikuwa ananyosha mkono wa kushoto juu ya paja la mguu wa kushoto.

****

**Swali la 253: Ni ipi hukumu ya kikao cha kupumzika katika swala?**

**Jibu**: Wanachuoni katika kuelezea kikao cha kupumzika wana kauli tatu:

1**-kauli ya kwanza**: Inapendeza kukaa kikao cha kupumzika.

**2-kauli ya pili:** Haipendezi kukaa kikao cha kupumzika kabisa .

**3-kauli ya tatu**: Inamchanganuo kati ya mtu ambaye anapata tabu kusimama moja kwa moja na mtu ambaye hapati tabu kusimama moja kwa moja, mtu ambaye hapati tabu kusimama moja kwa moja hato kaa kikao cha kupumzika, imelezwa katika kitabu (Al-Mughinii) [529/1/ chapa ya Daru Al-manara ] kauli hii inakusanya kati kauli mbili , imelezwa kuwa Aliy Ibun Ab twabili radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake: **((Hakika katika sun`na katika swala za faradhi atakapo shuka katika rakaa mbili za mwanzo asiege mikono yake juu ya ardhi isipokuwa akiwa mtu mzima asiye weza**)) Ameipokea Al-athrami Mwenyezi Mungu amrehemu, [200/3/, Ibun Mundhir kaikta Al-ausatwi,/ 214/2/ Al-Mughni], kisha akasema: Hadithi ya Maliki – akikusudia Ibun Huwayrithi, ((**kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alivyo inua kichwa chake kutoka katika sijida ya pili alikaa kisha akaegema mikono yake juu ya ardhi**)) [ 824 / Sahihi Bukhary.] tukio hilo linachukuliwa kuwa Mtume alikuwa ni dhaifu wa kusimama moja kwa moja kwa ajili ya utu uzima, Mtume alisema kuhusu hilo **((Mimi nimekuwa na mwili msi nitangulie kwenye kurukuu wala kusujudu))** [ 92/4/ Imamu Ahmadi, / 619/ Abuu Daud].

Kauli hii ndio naifata mimi, kwa sababu Maliki Ibun Huwaythir radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake!alifika kwa Mtume na Mtume anafanya maandalizi ya vita ya taabuwki , rejea kitabu ( Fatihu al-bari) [ 236/13] Mtume katika kipindi hicho amekuwa mtu mzima na ameishaanza kudhoofika, kama ilivyo kuja hadithi katika (Swahihi Muslimu ) [katika peji / 506/ Tahakiki ya Muhammad Fuadi Abdul-abaki] Imepokewa hadithi kwa Iisha radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake! Amesema: **((Alivyo kuwa na mwili na akawa mzito swala nyingi alikuwa anaswali amekaa))**[732/ Sahihi Muslim] alimuliza Abdul-allah

Ibun Shaqiyqi, kumuliza Aisha radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, hivi Mtume alikuwa anaswali amekaa? Akajibu Aisha **(( Ndio, baada ya kuchoshwa na mamabo ya watu))** [732/ Sahihi Muslim], Amesema Hafswa radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake: **((Sikumuona Mtume akiswali subhi akiwa amekaa mpaka kabla ya kufa kwake kwa mwaka mmoja au miwili** )) riwaya zote hizi zipo katika ((Sahihi Muslim)), inatufhamisha hadithi ya Maliki Ibun Huwayrithi kuwa Mtume alikuwa anaegemea mkono aliegemea kwa haja, na imepokea hadithi kutoka kwa Abdul-llah Ibun Buhayna radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake Hadithi ipo katika swahihu Bukhary **(( kuwa Mtume aliwaswalisha adhuhuri,akasimama kutoka katika rakaa mbili hakukaa))** kauli yake: **(( hakukaa))** ni kauli unayo jumwisha vikao vyote na hakusema alika kikao cha kupumzika, tunasema kikao kilicho kataliwa kwenye hadithi ni kikako cha tashahudi (tahiyatu) sio vikao vyote, Mwenyezi Mungu ndio mjuzi.

****

**Swali la 254: Ni ipi hukumu ya kutingisha kidole katika tashahudi (tahiyatu) kukitingisha kuwanzia mwanzo mpaka mwisho?**

**Jibu:** kutingisha kidole inakuwa wakati wa kusoma dua, sio katika tashahudi yote, ikiomba dua atatingisha kidole kama ilivyo thibiti katika hadithi**: ((Inakitingisha na anaomba dua))** [147/3/, Al-fathu Al-rabani] Amesema upokeza wa hadithi hii ni mzuri, mtu anaye omba dua anamuomba Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu yupo mbinguni, kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Mnadhani mko salama kwa alioko juu kuwa hatakudidimizeni kwenye ardhi na tahamaki inatikisika! Au mnadhani mko salama kwa alioko juu ya kuwa yeye hakupelekeeni kimbunga chenye changarawee? Mtajua vipi maonyo yangu],** [Suratul Mulki: 16-17]. Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu rehma na amani ziwe juu yake: **((Hamniamini name nimeaminiwa na aliye mbinguni** )) [4351 / Sahihi Bukhary, /1064/ Sahihu Muslim] Mwenyezi Mungu mtukufu yupo mbinguni juu ya kila kitu, ukimuomba Mwenyezi Mungu unaashiria kuwa yupo juu, imethiibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake aliwahutubia watu siku hija ya kuwaga **Akasema:**

**((Hivi nimefikisha**?)) wakasema Maswahaba: **ndio,** Akainua Mtume kidole chake kuelekeza mbinguni akawa anakielekeza na kuwashiria kwa watu akisema: ((**Mwenyezi Mungu shuhudia, Mwenyezi Mungu shuhudia , Mwenyezi Mungu shuhudia)**) [1218/ Sahihi musilm]. Alisema hivyo mara tatu, hadthi hii inatufahamisha kuwa Mwenyezi Mungu yupo mbinguni juu ya kila kitu, jambo hili lipo wazi hata kimaumbilee, na kiakili, na masikio, na makubaliano ya Wanachuoni, kwa hivyo kila mtu akiomba dua kwenye tashahudi unatakiwa kutingisha kidole shahada ukiashiria kwa kidole hicho kuwa Mwenyezi Mungu yupo mbinguni, ukimaliza kuomba dua utaacha kutingisha.

Sehemu ya dua kwenye tashahudi ni: Asalamu alaika ayuha an`nabiyu warahmatul-llah Wabarakatuh, Asalamu alaina waa-laa ibadii LLahi Swalihina, Allahuma swali alaa Muhammadi waali Muhammadi\, allahuma baariki Alaa Muhammadi waali Muhammad waali, audhu billah min adhabi jahanamu, wamin adhabu Al-qaburi, Wamin fitnati mahya Wal-mamati, Wamin fitnati Masihi Dajal.

Hizo ndio sehemu nane zinazo takiwa kutingisha kido-lee kukielekeza mbinguni, pia akiomba dua isiyo kuwa hiyo atatingisha kidole, kwa sababu ya kanuni hii kuwa anatakiwa kutingisha akiomba dua.

****

**Swali la 255: Je inatosha kusoma tashahud ya kwanza tu au mtu atazidisha dua?**

**Jibu:** Tashahudi ya kwanza katika swala ya rakaa nne au swala ya rakaa tatu atafupisha kama ifwatavyo atasoma: (Ata-hiyatu liLLah aswalawatu watwayibatu, asalamu alaika ayuha Nabii warahmatul-allah wabarakatuh, asalamu alaina waala iba-di LLahi swalihina, ashahadu an laa illah ila LLah, wa ashahadu anna Muhammmada rasulu Allah) [831/ Swahihi Bukhari, /402/ Sahihi Muslim] kusoma hivyo ndio bora lakini akizidisha aka-

soma: allah huma swali alaa Muhammad, walaa aali Muhammad, kama swalayta alaa Ibrahima wa alaali Ibrahima, innaka hamidu majidu, Allahuma baariki alaa Muhammad, wa alaa aali Muhammad, kama baarakta alaa Ibrahiyma, wa alaa ali Ibrahima, inaka hamidu majidu, [ 3370/3369/ Swahihi Bukhary, /405/ Sahihi Muslim].

Wapo Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu wamesema: ni bora mtuu kuzidisha na dua hiyo kuliko kufupisha, lakini mimi naona asome sehemu ya kwanza aridhike na hiyo, lakini kama atazidisha hakuna ubaya, haswa kama Imamu atarefusha kukaa kwenye tashahudi, Imamu akirefusha basi naye azidishe dua tulio itaja hapo juu .

****

**Swali la 256: Ni ipi hukumu ya mkao wa tawaruki (kukalia tako) katika swala? Mkao huo ni kwa wanawake na wanaume?**

**Jibu:** Mkao wa tawaruki katika swala ni sun`na katika tashahudi ya mwisho katika swala ambazo zina tashahudi mbili, kama swala ya magharibi, na swala ya ishaa, adhuhuri, alasiri, ama swala ambayo ina tashahudi moja swala hiyo haina mkao wa twaruki (kukalia tako) isipokuwa atakailia mguu.

Kuhusu wanawake na wanaume, mkao huo umethibiti kwa wanaume na wanawake, kwa sababu asili ni kulinga kati ya wa-

naume na wanawake katika hukumu na sheria, isipokuwa mpaka tuupate ushahidi wa kisheria unao julisha kuwa kwenye jambo hilo hawalingani mwanamke na mwanaume, hakuna ushahidi wakisheria kuwa mwanamke na mwanaume wanatofautiana katika mambo ya swala, isipokuwa mwanamke na mwanaume wanalingana kwa kila kitu .

****

**Swali la 257: Imamu anatoa salamu moja kuliani kwakwe je inatosha kutoa salamu moja? Tunaomba majibu, Mwenyezi Mungu atawalipa.**

**Jibu:** Wapo Wanachuoni wanao sema kuwa inaruhusiwa kutoa salamu moja tu, pia wapo Wanachuoni Wanaosema kuwa ni lazima Imamu atoe salamu mbili, wapo Wanachuoni wana sema salamu moja inaruhusiwa kwenye swala za Sunnah swala za faradhi hairuhusiwi kutoa salamu moja.

Mtu kutoka kwenye mashaka ni bora kutoa salamu mbili, kwa kuwa jambo hili la kutoa salamu mara mbili limepokelewa mara nyingi kuwa Mtume alikuwa akitoa salamu mara mbili mtu akitoa salamu mara mbili atakuwa ametoka kwenye wasiwasi na ndio imepokewa kweye riwaya nyingi, [582/ Sahihi Muslim].

Kama Imamu atatoa salamu moja upande wake wa kulia na Maamuma akaona hakupendezwa kupunguza salama moja Maamuma huyo anaruhusa ya kuongeza salamu ya pili jambo hili

halina ubaya, kama Imamu atatoa salamu mbili lakini Maamuma akataka atoe salamu moja ni lazima Maamuma atoe salamu ya pili kwa ajili ya kumfata Imamu.

****

**Swali la 258: Hivi iliyo bora Imamu aondoke sehemu alio swalia baada tu ya kumaliza swala au asubir kidogo?**

**Jibu:** Nibora kwa Imamu abaki amelekea kibla kiasi cha muda wa kusema astaghafiru LLah mara tatu, na aseme: Allah huma anta salamu, waminka salamu, tabaarakta ya Dhal-Jalali wal-ikirami, kisha ageukie upande wa Maamuma.

Ama kubaki Imamu baada ya kumaliza swala kama itakuwa kutoka kwakwe sehemu alipo inabidi kuwaruka watu na kuwaomba njia Maamuma ni bora asubiri mpaka Maamuma wakipungua ndio atoke kwa kuwa njia itakuwa imepatikana, lakini kama kutakuwa na njia anaweza kutoka mapema .

Kuhusa Maamuma ni bora asiondoke mpaka Imamu wake aondoke , kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Msinitangulie kuondoka**),) [426/ Sahihu Muslim], lakini Imamu akichelewa kugeuka upande wa kibla muda ambao sio

Sunnah kuelekea kibla muda mrefu Imamu kaendelea kuelekea kibla inaruhusiwa Maamuma kuondoka kabla ya Imamu kugeuka.

****

**Swali la 259: Ni ipi hukumu ya kupeana mikono baada ya swala na kuombeana dua (Taaqabbala LLah) ?**

**Jibu:**Hakuna ushahidi wa kupeana mikono baada ya swala wala kuwambina (Taqabbala LLah) jambo hilo halikuthibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake wala halikuthibiti kwa maswahaba kuwa walikuwa wanapeana mikono baada ya swala. Imehaririwa /20/5/1409/H.

****

**Swali la 260: Ni ipi hukumu ya kutumia tasbihi wakati wa kumtaja Mwenyezi Mungu?**

**Jibu**: Kutumia tasbihi inaruhusiwa, lakini ni bora kutumia vidole, kwa kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema: **((Mtajeni Mwenyezi Mungu kwa vidole kwani vitatamka**)),

[370/6/, Imamu Ahmadi katika musnadi, /1501/ Abuu Daud,/ 3583/ Al Tirmidhiy].

Kwa kuwa kubeba tasbihi huenda ikwa kuna kujionyesha kwa watu kuwa unamtaja sana Mwenyezi Mungu, na watu wengi wanao tumia tasbihi utamkuta anamtaja Mwenyezi Mungu lakini moyo wake haupo anamtaja Mwenyezi Mungu kwa tasbihi naye anatazama kulia na kushoto, kutumia vidole ni bora zaidi kuliko kutumia tasbihi.

****

**Swali la 261: Ni zipo nyiradi zilizo thibiti baada ya kutoa salamu kwenye swala?**

**Jibu:** Mwenyezi Mungu ameamrisha watu wamtaje baada ya swala, Amesema Mwenyezi Mungu**: [Mkisha swali basi mtajani Mwenyezi Mungu mkiwa mmesimama mmekaa na mnapo kuwa mmelala],** [Suratu Nnisaa: 103]. Na nyiradi alizo ziamrisha Mwenyezi Mungu amezibainisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Utasema ukisha toa salamu baada ya swala: Astaghafiru Allah- mara tatu- kisha utaendelea- Allahuma anta salamu, waminka salamu, tabaarakta ya Dhal-Jalali wal-ikraami, [591/ Sahihi Musilim], Utaendelea – laa Ilaha ila LLah wahdahu la shariyka lahu, lahul-mulku , walahul-hamdu, wahuwa alaa kuli shay in Qadiyru, Allahuma laa maaniu limaa

aatwayta, Wala muutwii limaa manaata, wala yanfau Dhal-Jaddi minkaal-Jaddu, [844/ Sahihi Bukhary, / 593/ Sahihi Muslim], Laa Ilaaha ila Allah, walaa naabudu ila iyyaahu, lahu Nniimati, walahul-fadhwili, walahu Thanaa wal-hasani, laa haula wala kuwwata ila biLLah, laa Ilaaha ila Allah, Walaa naabudu ila iyyahu, mukhliswiyna lahu Diyn walau karihal-kafiruuna, [ 594/ Sahihi Muslim].

Baada ya hapo unamtaja Mwenyezi Mungu! Kama ilivyo thibiti katika hadithi, unasema Subhana LLah mara thalathini na tatu. Al-hamdulillah , mara thalathini na tatu, Allahu akbar, mara thalathin na tatu, [843 Sahihi bukhar,/ 595/ Sahihi Muslim], kisha utasema kukamilisha mia moja: Laa Ilaha ila LLah wahdahu laa shariyka lahu, Lahul-mulku walahul-hamdu wa huwa alaa kuli shay in Qadiri [597/ Sahihi Muslim] Unaruhusiwa kusoma nyiradi hizo kwa mara moja au kwa mkato mkato, mfano: Subhana Allah, wal-hamdu liLLah, wa Allahu akbar, mara thalathini na tatu, Au ukasoma: Subhana Allah peke yake mara thalathini na tatu, ukimaliza unasoma: Al-hamduliLLah mara thalathini na tatu, kisha unasoma : Allahu Akbar , mara thalathini na tatu, atakamilisha kwa kusoma Laa Ilaha ila Allah wahdahu laa shariyka lahu, lahul-mulku, walahul-hamdu, wahuwa alaa kuli shay in Qadiyr.

Inaruhusiwa kusoma Subhana LLah, Al-hamdulillah, Allahu akibar, mara kumi kumi, badala ya kusoma mara thalathini na tatu, inatakiwa mtu asome: Subhana Allah, mara kumi, Al-hamdu liLLah, mara kumi, waLLahu akbar,mara kumi, utakuwa umekamilisha mara thalathini, hadithii zimethibitisha nyiradi hizo [5065 / Abuu Daud,/ 3410 / atirmidhiy,/ 1348/ Annasaai].

Pia imethibiti kwenye hadithi mtu aseme: Subhana LLah

, Wal-hamduli LLah walaa Ilaha ilaa LLah , waLLahu akbar, Atasoma mara ishirini na tano itakuwa imeenea idadi ya mia moja. [3413/ Atirmidhiy, / 1350/ Annasaai].

Nyiradi yoyote katika hizo tulizo ziorodhesha hapo juu inaruhusiwa kuzisoma, kwa sababu kanuni ya sheria inasema: ((**Ibada iliyo pokelewa kwa mapokezi tofauti ni sun`na kuifanya kwa kila aina ya upokezi ulio kuja muda huu unafanya hii na muda mwengine unafanya nyingine**)), kwa ajili mtu afanye sun`na zote alizo kuja nazo Mtume rehma na amani ziwe juu yake, nyiradi tulizo zitaja ni za swala tano: Al-fajir, Adhuhuri, Alasili, Magharibi , Ishaa, katika swala ya Al-fajir na Magharibi unasoma tahalili, kusoma Laa Ilaha ila LLah wahdahu laa shariyka lahu, lahul-mulku, walahul-hamdu, wahuwa alaa kuli shay in Qadiyr, mara kumi, pia utasoma **((Rabi ajirnii mina Nnaar**)), mara saba, utasoma baada ya swala ya magharibi na Al-fajir. Mwenyezi Mungu Atua fiqishe .

****

**Swali la 262 : Ni ipi hukumu ya kuinua mikono miwili na kuomba dua baada ya swala?**

**Jibu:** Haikuthibiti kuwa mtu akimaliza kuswali ainuwe mikono yake na kuomba dua, mtu akiwa anataka kuomba dua hakika dua bora ni dua anayo omba mtu akiwa kwenye swala,

ni bora kuomba dua kwenye swala kuliko kuomba baada ya kumaliza kuswali, jambo hili amelielekeza Mtume rehma na amani ziwe juu yake katika hadithi ya Abdul-llah Ibun Masoudi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake wakati alipo elezea kutoa tashahudi (tahiyatu) Akasema Mtume: **(( kisha achelewe katika kuomba dua anavyo taka))** [ 402/ Swahihi Bukhary].

Kuhusu wanayo yafanya watu wengi anapo maliza kuswali sun`na anainua mikono yake anaomba dua baadhi yao unaweza kusema hajaomba kitu, utamuona swala inakimiwa naye yupo katika tashahudi ya mwisho akitoa salamu anainua mikono yake juu kama anaomba – ilimradi ainue mikono kisha anaifuta mikono yake kwenye paji la uso, yote hayo ni watu kudhani jambo hilo linaasili kwenye dini ,jambo hilo halijathibiti, kudumu na kufanya jambo hilo linakuwa ni bidaa, ni jambo lauzushi kwa sababu halikuthibiti kwa Mtume na maswahaba.

****

**Swali la 263: Katika baadhi ya nchi baada ya swala za faradhi wanasoma Surt Al-fatiha, na nyiradi, na Ayatu Al-kurusiyu kwa sauti ya pamoja, ni ipi hukumu ya ibada hiyo?**

**Jibu**: Kusoma Suratul Fatiha na Ayatul- Al-kurusiyu na nyiradi baada ya swala kwa sauti ya pamoja jambo hilo ni bidaa (uzushi), jambo linalo fahamika kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake na Maswahaba zake walikuwa wanasoma nyiradi kwa sauti ya juu, lakini kila mmoja anamtaja Mwenyezi Mungu kivyake bila kushirikiana na mtu mwengine, kuinua sauti baada ya swala za faradhi ni sunna kama ilivyo thibiti katika (Sahihu Bukhary) imepokewa hadithi kwa Ibun Abasi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! Amesema: **((Ilikuwa kuinua sauti kwa nyiradi watu wanapo maliza kuswali faradhi))** [841/ Sahihi Bukhary, /583/ Sahihi Muslim].

Kuhusu kusoma Suratul Fatiha baada ya kumaliza swala kusoma kwa siri au kwa sauti sifahamu hadithi ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake iliyo pokelewa kuwa alikuwa akisoma Suratul Fatiha au Mwaswahaba walikuwa wakisoma, imethibiti katika hadithi Mtume alikuwa anasoma Ayatul-kurusiyu, Surat Ikhraswi, (kul huwa allahu ahadu) Mauwidhwatayn, Surat Al-Falaqi, na Surat Al-Naasi, hizo sura tatu na ayatu Al-kurusiyu ndio zilizo thibiti kuwa Mtume Alikuwa akisoma, [185/ ukursa/ Anasaii/,115 /3/ Imamu Ahmad].

****

**Swali la 264: Mtu akikhofia kuwa akienda msalani kujisaidia swala ya jamaa itampita, je ataswali jamaa akiwa amebana haja yake, au atajisaidia kwanza haja yake hata kama atachelewa swala ya jamaa?**

**Jibu:** Atajisaidi kwanza, hata kama swala ya jamaa itampita, kwa sababu huo ni udhuru, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Hakuna swala chakula kikiwa mezani, wala mtu aliye banwa na uchafu wa aina mbili**)), [570/ Sahihi Muslim].

****

**Swali la 265: Ni ipi hukumu ya kufumba macho mawili kwenye swala?**

**Jibu**: Ni karaha kufumba macho mawili kwenye swala, kwasababu ni kinyume na alivyo kuwa akifanya Mtume rehma na amani ziwe juu yake isipokuwa anaruhusiwa kufumba macho anapokuwa kwenye swala kwasababu, mfano mbele yake kama kutakuwa na mapambo kwenye ukuta au kwenye tandiko, au mbele yake kuna mwangaaza mkubwa wa taa unamchoma kwenye macho, jambo la muhimu kama atafumba kwa sasababu hakuna ubaya, kama atafumba bila sababu jambo hilo ni karaha, anayetaka kupata faida ya ziada arejee kitabu ((Zaadi Al-miaadi)) mtunzi Ibun Qayimu Mwenyezi Mungu amrehemu, [283/1/ zaadi almiaadi].

****

**Swali la 266: Je kunyosha nyosha vidole vya mikono ukiwa kwenye swala kwa kusahau kunaharibu swala?**

**Jibu**: Kunyosha vidole hakuharibu swala, lakini kuvinyosha vidole kutaleta ushawishi kwa mtu atakae kuwa anasikia sauti ya vidole jambo hilo lina kuwa na madhara kwa sababu utawashawishi watu kwenye swala zao, pia kuyosha vidole ni mchezo hatutakiwi kucheza kwenye swala.

**Nachukuwa nafasi hii kusema:** Kutingishika kwenye swala kumegawanyika sehemu tano: kutingishika kwa lazima, kutingishika ambako ni Sunna, kutingishika ambako ni karaha, kutingishika ambako ni haramu, kutingishika ambako kunaruhusiwa (Ruhsa).

**Kutingishika kwa lazima: Na**ko hupatikana kwa kufanya jambo la waJibu kwenye swala, mfano mtu akisimama kuswali kisha akakumbuka kuwa kwenye kilembea chake kuna najsi au viatu vyake, ni lazima avue kilemba hicho au viatu hivyo, kutingishika huku ni waJibu, ushahidi wa hayo: kuwa Mtume rehma na amani alimjia Jibril rehma za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! Mtume akiwa anaswali akamwambia kwenye viatu vyako kuna uchafu Mtume rehma na amani akavivua viatu vyake naye akiwa katikati ya swala akaendelea na swala, [650/ Abuu Daud, /786/ Ibun Khuzayma, /2185/], kutingishika huko ni lazima, unatakiwa utingishike kwa kufanya jambo la lazima kwenye swala, au kuwacha jambo la haramu.

**Kutingishika kwa Sunnah:** Ni jambo ambalo linakamilisha

swala, mfano kupiga hatua kwenda kwenye swafu ya mbele kukipatikana nafasi iliyo wazi kuziba nafasi iliyo wazi ni Sunnah.

**Kutingishika kwa karaha**: Ni kutingishika ambako hakuna haja, wala sio katika mambo yanayo kamilisha swala.

**Kutingishika kwa haramu**: Ni kutingishika kuliko kwingi kwa kufatana. mfano mtu anapokuwa amesimama kwenye swala anacheza cheza, na anapo rukuu acheza, na kwenye sujudu anacheza, akika anacheza mpaka anatoka kwenye muonekano kuwa yupo kwenye swala,harakati hizo ni haramu, kwa sababu zinaharibu swala.

**Kutingishika kwa halali:** Nako ni mtu akiwashwa mwili akaijiparua au uchafu ukamuingia kwenye macho akautoa, au mtu akamuaga kuwa anatoka naye anaswali akainua mkono akiwa anaswali harakati hizi ni halali.

****

**Swala la 267: Ni ipi hukumu ya kuweka kizuizi mbele ya mtu anaye swali? Na ni kipi kiwango cha kuweka kizuizi?**

**JIBU:** kuweka kizuizi mbele ya mtu anaye swali ni Sunna, lakini Maamuma sio Sunna aweke kizuizi atatosheka na kizuizi

alicho weka Imamu.

Kuwango cha kizuizi aliulizwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuhusu kiwango cha kuweka kiuizi Akasema**: ((Mfano wamgongo wa myama)), [** 499/ Sahihi Muslim].

Lakini hicho ni kiwango cha juu, inaruhusiwa kiwango cha chini ya hapo imethibit hadithi**: ((Akiswali mmoja wenu basi aweke ukingo hata kwa mshale))** 404/ Ahmadi,] imethibiti hadithi nyingine ambayo ameipokea Abuu Daud Mwenyezi Mungu amrehemu kwa upokezi mzuri: ((**Mtu ambaye hakupata kizuizi apige mstari)**) [698/ Abuu Daud,] Amesema: Al-hafidhu Ibun Hajar Mwenyezi Mungu amrehemu! Katika kitabu **((Bulughul Maraami**)) hakupatia mtu aliye sema kuwa hadithii hiyo ya Ibun Daud inaudhaifu, (Mudhitwaribu) hadithi hiyo haina tatizo ambalo haitakiwi kufanyiwa kazi, tunasema: Uchache wa kuweka kizuizi ni kupiga mstari na ukubwa wake ni sawa na urefu wa mgongo wa myama.

****

**Swali la 268: Ni ipi hukumu ya kupita mbele ya mtu anaye swali katika msikiti mtukufu wa Makkah kupita mbele yake ikiwa ni swala ya faradhi au Sunna Imamu au Maamuma?**

**Jibu:** Kupita mbele ya Maamuma anaye swali hakuna ubaya kama itakuwa katika Msikiti mtukufu wa Makkah na Misikiti mingine, kwa kuwa Ibun Abasi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake alikwenda kwa Mtume akamkuta na Mtume akiwaswalisha watu katika maeneo ya Mina na hakukuwa na kizuizi akapita katikati ya swafu naye amepanda punda anaye itwa atana, hakuna aliye mzuia wala kumkea baada ya swala, [ 76/ Sahihi Bukhary, / 504 Sahihi Muslim].

Kama mtu atakuwa ni Imamu au anaswali peke yake haifai kupita mbele yake ikiwa Msikiti mtukufu wa Makkah au Misikiti mingine kwa ushahidi wa kisheria, hakuna ushahidi kuwa Makkah mtu ndio anaruhusiwa kupita mbele ya mtu anaeswali kuwa haidhuru au mtu hapati madhambi.

****

**Swali la 269: Nipi hukumu ya kuweka vituliza joto vya umeme mbele ya wanaoswali je imethibiti tahadhari ya kisheria?**

**Jibu**: Sio vibaya kuweka vituliza joto kwenye kibla ya msikiti na mbele ya wanao swali, sifahamu tahadhari yoyote ya kisheiria juu ya jambo hilo.

****

**Swali la 270: Je inafaa kwa mtu anayeswali akisoma Aya inayo zungumzia habari za Pepo amuombe Mwenyezi Mungu Pepo na Aya ya Moto ajilinde kwa Mwenyezi Mungu kutokana na Moto? Je kuna utofauti kati ya maamuma na anaye swali peke yake?**

**Jibu:** Ndio, inaruhusiwa, na hakuna utofauti kati ya Imamu na Maamuma na anaye swali peke yake isipokuwa Maamuma inatakiwa asijishughulishe na mambo mengine akaye kimya awe anasikiliza kisomo cha Imamu wake.

****

**Swali la 271: Ni zipi sababu za kusujudi sijida ya kusahau?**

**Jibu:** Kusujudu kwa ajili ya kusahau kunasababu tatu:

**1-**kuzidisha kitu kwenye swala.

**2-**kupunguza kitu kwenye swala.

3-kuwa na mashaka umefanya kitu au haujafanya .

**Kuzidisha**: **Mfano:** Mtu akizidisha rukuu, au sujudu, au akazidisha kusimama au kukaa.

**Kupunguza: Mfano:** Mtu kupunguza nguzo ya swala, au jambo la waJibu katika ambayo ni waJibu katika swala.

**Kuwa nashaka:** Ni mtu kuwa anababaika, hajui ameswali rakaa ngapi, ameswali rakaa tatu, au nne.

Kuzidisha mtu akizidisha rukuu katika swala au akazidisha kusujudu, au kisimamo, au akazidisha kikao kwa makusudi swala yake inakuwa batili, kwa kuwa akizidisha kwa makusudi atakuwa ameswali kinyume na alivyo amrisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Atakaye fanya ibada ambayo hatukuiamuru ibada hiyo atarejeshewa**)), [1718/18, Sahihi Muslim].

Akizidisha kwa kusahau swala yake haibatiliki, lakini atasujudu sijida ya kusahahu baada ya salamu, ushahidi wa hayo hadithi ya Abuu Hurayra radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake wakati Mtume alipotoa salamu baada ya rakaa mbili katika swala za mchana, ima ilikuwa ni dhuhuri au alasiri, walipo mkumbusha aliswali rakaa mbili zilizo baki, kisha akasujudu sijida mbili za kusahau baada ya kutoa salamu, [482/ Sahihi Bukhary], na hadithi ya Ibun Masoud radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, Mtume aliwaswalisha swala ya dhuhuri rakaa tano walivyo geuka baada ya kutoa salamu, wakamwambia: Swala imezidishwa? Akasema: ((**kwanini mnauliza hivyo**)) wakasema: umeswali rakaa tano, akaweka miguu yake vizuri, akelekea kibla akasujudi sijida mbili kisha akatoa salamu. [404/ Sahihi Bukhary, /572/ Sahihi Muslim].

**Kupunguza**: Mtu akipunguza nguzo katika nguzo za swala haiepukani na hali hii: Ima awe mtu huyo amekumbuka kuwa kaacha nguzo kabla ya kufika kwenye sehemu yake katika rakaa

ya pili, ni lazima arudi ailete hiyo nguzo na kinacho fata baada ya nguzo hiyo.

Ima mtu huyo asikumbuke ila baada ya kufika kwenye sehemu yake katika rakaa ya ya pili, ikiwa hivyo rakaa ya pili itakuwa ni badala ya rakaa ya kwanza kwa kuwa rakaa ya kwanza ameacha nguzo, katika hali hizi mbili sijda ya kusahau inakuwa baada ya salamu.

**Mfano:** Mtu ameenda kusujudu kwenye rakaa ya kwanza akasujudi sijida moja akasahau sijida ya pili kisha akasimama bila kusujudi sijida ya pili, alivyo simama na akanza kusoma akakumbuka kuwa hakusujudu sijida ya pili wala hakukaa mkao mdogo kati ya sijida mbili , hapo atarudi chini atakaa mkao mdogo wa kati ya sijida mbili kisha atasujudu, ndipo atasimama na kuendelea na swala, atasujudu jisida ya kusahau baada ya salamu.

**Mfano:** Mtu ambaye hakukumbuka isipokuwa baada ya kufika sehemu hiyo kwenye rakaa ya pili, akisimama kutoka kwenye sijida ya kwanza kwenye rakaa ya kwanza na hakusujudu sijida ya pili wala hakukaa mkao wa kati ya sijida mbili, lakini hakukumbuka isipokuwa baada ya kukaa kati ya sijida mbili katika rakaa ya pili, katika hali hii rakaa ya pili ndio rakaa ya kwanza, atazidisha rakaa kwenye swala yake, atatoa salamu kisha atasujudu sijida ya kusahau.

**Kupunguza waJibu:** Akipunguza jambo la wajibu na akahama kutoka kwenye sehemu aliokuwa akaenda sehemu inayo fata Mfano: Akisahau kusema ((Subhana Rabbil-alaa)) hakukumbuka isipokuwa baada ya kuinuka kutoka kwenye sujudu, mtu huyo atakuwa ameacha jambo la wajibu katika mambo ambayo ni

waJibu katika swala ameacha kwa kusahau ataendelea na swala, atasujudu sijida ya kusahahu kabla ya kutoa salamu, kwa kuwa Mtume alivyo acha tashahudi ya kwanza (Tahiyatu) akaendelea na swala hakurudi akasujudi sijida ya kusahau kabla ya kutoa salamu [829/ Sahihi Bukhary, / 580/ Sahihi Muslim].

**Kutia shaka**: Ni mtu kuwa na wasi wasi amepunguza au amezidisha, **Mfano:** kuwa hana uhakika ameswali rakaa tatu au ameswali rakaa nne, hali hiyo ina hali mbili :

Ima apate uhakika kati ya hali hizo mbili kuwa amezidisha au amepunguza hapo atafata uhakika aliyo upata atakamilisha swala yake kwa kufata uhakika wake atasujudu jisida ya kusahau baada ya salamu, kama hakupata uhakika kati ya hali mbili kwa mfano hana uhakika ameswali rakaa mbili au rakaa tatu, atafata yaqini nayo ni kuwa ameswali rakaa mbili, yaqini itakuwa kwa idadi ya chini kisha atakamilisha swala atasujudu sijida kabla ya salamu.

**Mfano**: Mtu ameswali adhuhuri kisha akawa na shaka ameswali rakaa tatu au rakaa nne, akachagua kuwa ameswali tatu atamaliza rakaa ya nne kisha atatoa salamu, kisha atasujudu sijda ya kusahau.

**Hali mbili zikilingana:** Mtu akiswali swala ya dhuhur akawa na shaka hivi ameswali rakaa tatu, au nne, amefikiria hakupata uhakika kuwa ameswali tatu, au nne, atajengea yaqini nako ni idadi ndogo atajalia kuwa ameswali rakaa tatu kisha ataswali rakaa ya nne atasujudu sijida ya kusahau kabla ya salamu.

Hivyo umeelewa kuwa sijida ya kusahahu inakuwa kabla ya salamu mtu akiacha waJibu, au akiwa na mashaka kwenye idadi ya rakaa na haku hakupata uhakika kati wa mambo hayo mawili.

Sijida sahau inakuwa baada ya salamu akizidisha kwenye swala,au akiwa na mashaka na hakupata uhakika kati ya mambo hayo mawili.

* * * *

**Swali la 272: Imamu akizidisha rakaa na mimi sikumfuata nami nimechelewa hivi swala yangu ni sahihi? Ni ipi hukumu ya kuto kuacha kumfuata na nimezidisha rakaa?**

**Jibu:** Kauli sahihi ni kuwa swala yako ni sahihi, kwa kuwa swala yake imekamilika, na Imamu amezidisha mwenyewe, naye Imamu ana udhuru kwa kuwa amesahau, ama wewe kama ukisimama ukaswali rakaa baada ya rakaa zako kukamilika ungekuwa umezidisha rakaa, bila udhuru wowote na kuzidisha swala bila udhuru swala inakuwa batili**.** Imehaririwa 25/7/1407/H.

****

**Swali la 273: Mtu anaeswali swala za usiku, na swala za usiku ni rakaa mbili mbili, akasahau akasimama kuswali raka ya tatu atafanyaje?**

**Jibu:** Atarudi chini kwenye tashahudi (tahiyatu) kama hato rudi swala yake imebatilika, kwa kuwa amekusudia kuzidisha, ameelezea jambo hilo Imamu Ahmadi rehama za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, [395/1/ Al-Kashafu Al-Kinai], kuwa akisimama kwenye swala za usiku rakaa ya tatu ni kama amesimama rakaa ya tatu kwenye swala ya Al-fajiri, anakusudia Imamu Ahmadi kuwa kama hakurudi kwenye tashahudi akaendelea na rakaa ya tatu swala yake ni batili, lakini inanyambuliwa kwenye swala za usiku swala ya witiri, swala ya witiri inaruhusiwa kuzidisha zaidi ya rakaa mbili mtu ataswali tatu.

Kama mtu atanuwiya kuswali witiri kwa niya ya kuswali rakaa mbili kisha atoe salamu kisha aswali rakaa ya tatu, lakini akasahau akasimama kuswali rakaa ya tatu bila kutoa salamu kwenye rakaa ya pili, tunasema: Anaruhusiwa kukamilisha rakaa ya tatu kwa sababu inaruhusiwa witiri kuswali rakaa tatu kwa salamu moja.

****

**Swali la 274: Mtu anaswali akasimama kwenye rakaa ya pili hakukaa tashahudi ndogo, alivyo fika juu akakumbuka kuwa hakukaa kwenye tashahudi je mtu huyo atarud kwenye tashahudi? Na ni muda gani atasujudu sijida ya kusahau atasujudu baada ya salamu au kabla ya salamu?**

**Jibu:** Akiwa amesha simama hatorudi, kwa kuwa ameishahama kutoka kwenye tashahudi na kwenda kwenye nguzo ambayo inafata, ni karaha kurudi lakini akirudi swala yake haibatiliki, kwa kuwa hakufanya jambo la haramu, lakini ni lazima asujudu sijida ya kusahahu, itakuwa kabla ya salamu.

Wamesema baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu: Nilazima aendelee wala asirudi kwenye tashahudi na atasujudu sijida ya kusahau kwa kuwa amepunguza jambo la waJibu na sijida ya kusahau inakuwa kabla ya salamu.

****

**Swali la 275: Ni ipi hukumu ya swala ya witiri, je ni swala maalumu kwa mwezi wa Ramadhan?**

**Jibu:** Swala ya witiri ni sun`na iliyo tiliwa nguvu katika Mwezi wa Ramadhan na miezi mingine, Wesema Mwanachuoni Imamu Ahmad na Manazuoni wengine: **((Atakaye acha kuswali witiri mtu huyo ni muovu ushahidi wake haukubaliki)),** [266/1/ Masaail Al-Imamu Ahmadi] Swala ya witiri ni Sunna iliyo tiliwa mkazo haifai kwa mwislamu kuwacha kuiswali katika mwezi wa Ramadhan na miezi mingine, swala ya witiri ndio hukamilisha swala za usiku, Swala ya witiri sio kama wanavyo fahamu baadhi ya watu kuwa kunuti ndio swala ya witiri, kunuti ni kitu kingine na swala ya witiri ni kitu kingine, swala ya witiri ni swala inayo swaliwa mwisho kwa kuiswali rakaa moja au rakaa tatu, kwa hivyo swala ya witiri ni sun`na ndani ya mwezi wa Ramadhan na miezi mingine hatakiwi mwislamu kuwacha kuiswali.

****

**Swali la 276: Tunaomba kwa heshma zenu ufafanuzi wa Sunna ya dua ya kunuti, je kunuti ina dua malumu? Je ni sharti mtu akiomba dua ya kunuti katika swala ya witiri arefushe kuomba dua hiyo?**

**Jibu**: Dua ya kunuti ipo aliyo ifundisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake, limfundisha Hassani bin Ally bin Abii Twalibi : ((AllahUma ihdini fiyman hadayta, waafinii fiyman afayta)) [199/1/ Imamu Ahmadi, /1245/ Abuu Daud ,/ 464/ Atir-

midhiy], Mpaka mwisho wa dua ni mashuhuri dua hii, na Imamu anatakiwa aombe kwa dhamiri ya watu wengine asema ihdinaa kwa kuwa anajiombea yeye na walio nyuma yake, Akiomba dua inayofaa hakuna ubaya, lakini haitakiwi arefushe kiasi ambacho atawapa shida na tabu Maamuma, au atawachosha kwasababu ya dua ndefu kwa kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alimkasirikia Muadhi bin Jabal – Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake wakati alipo refusha swala alipo kuwa anawaswalisha jamaa zake akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake kumwambia Muadhi: ((**Umekuwa mfitinishaji wewe Muadhi**?!)) [705 / Sahihi Bukhary, / 465 / Sahihi Muslim].

****

**Swali la 277: Je ni Sunna kuinua mikono wakati wakuomba dua ya kunuti? Naomba ushahidi wa hilo?**

**Jibu:** Ndio, ni Sunna kuinua mikono wakati wakuomba dua kwenye kunuti, kwa kuwa kufanya hivyo imethibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Alikuwa anainua mikono kwenye kunuti wakati alivyo kunuti katika swala za faradhi wakati wa misiba 173/3 / Imamu Ahmadi], pia imethibiti kwa kiongozi wa Waislamu Omar Ibun Khatwabi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake aliinua mikono miwili kwenye kunuti ya swala ya witiri na Omari ni miongoni mwa viongizi tulio amrishwa kuwafata.

Kuinua mikono wakati wa dua ya kunuti ni sun`na, kwa Imamu na Maamuma au akiwa anaswali peke yake, kila akiomba dua kwenye kunuti ainue mikono.

****

**Swali la 278: Ni ipi hukumu ya dua ya kunuti katika swala za faradhi? Na ni ipi hukumu ya kunuti Waisalamu wakipatwa na balaa au misiba?**

**Jibu**: Kuomba dua kwenye kunuti sio jambo lenye asili kwenye sheria, na hatakiwi mtu kuwa anaomba dua ya kunuti kwenye swala za faradhi, lakini Imamu akikunuti mfuate Imamu kwenye kunuti kwa kuwa ukimukhalifu ni jambo la shari .

Waislamu wakipatwa na balaa au misibaa sio vibaya kuomba dua kwenye kunuti kuomba Allah aliondoe balaa hilo.

****

**Swali la 279: Ni ipi hukumu ya swala ya tarawehe, na ni ipi idadi ya rakaa za tarawehe?**

**JIBU**: Swala ya atarawehe ni Sunna , swala hiyo ameiswali Mtume rehma na amani ziwe juu yake katika ((Sahihi Bukhary na Sahihi Muslim)) Imepokewa hadithi ya Aisha radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kuwa Mtume rahma na amani ziwe juu yake aliswali msikitini usiku na watu wakaswali naye, kisha akaswali tarawehe siku inayofuata msikitini watu wakazidi kuwa wengi, ilipo kuwa siku ya tatu au ya nne watu wakajikusanya wengi kwa ajili ya kuswali tarawehe Mtume rehma na amani hakutoka nyumbani kwenda kuwaswalisha, ilipofika asubuhi akasema: **((Niliyona mlicho kifanya jana hakuna kilicho niziwia kutoka isipokuwa nimehofia swala ya tarawehe isifaradhishwe kwenu)), [**1129 / Sahihi Bukhary, / 761/ Sahihi Muslim].

**Kuhusu idadi ya rakaa**: Idadi yake ni rakaa kumi na moja, kama ilivyo thibiti katika (Sahihi Bukhary na Sahihi Muslim), katika hadithi ya Aisha radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake aliulizwa vipi Mtume alikuwa akiswali katika Mwezi wa Ramadhan? Akajibu bii Aisha: ((**Alikuwa hazidishi katika mwezi wa Ramadhan na miezi mingine rakaa kumi na moja))**, [1147/ Sahihi bukhari, 738/ Sahihi Muslim].

Mtu akiswali rakaa kumi na tatu sio vibaya, kwa kauli ya Ibun Abasi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: **((Zilikuwa swala za Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni rakaa kumi na tatu** )) anakusudia swala za usiku. Hadithi hii ameipokea Imamu Bukhary Mwenyezi Mungu amrehemu![ 1138/ Sahihi Bukhary,/ 764/ Sahihi Muslim].

Kuswali rakaa kumi na moja imethibiti kwa Omar Ibun Khatwabi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kama ilivyo katika kitabu ((Al-Muwatwaa)) imepokea kwa upokezi sahihi, [110/1,/280, ((Al-Muwatwaa].

Mtu akizidisha hapo hakuna ubaya, kwa ushahidi wa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Alipo ulizwa kuhusu swala za usiku Akasema: **((Mbili Mbili))**, [990/ Sahihi Bukhary, /145/ Sahihi Muslim], hakuweka ukomo wa kuswali usiku.

Na umepokelewa ushahidi mwingi kwa wema alio tangulia Mwenyezi Mungu awarehemu, swala za usiku zina upana, lakini iliyo bora na iliyo fupi ni aliokuja nayo Mtume rehma na amani ziwe juu yake, nazo ni rakaa kumi na mojaa au rakaa kumi na tatu.

Haikuthibiti kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alikuwa akiswali yeye au mmoja kati ya makhalifa wa Mtume kuswali rakaa ishirini na tatu, isipokuwa imethibiti kwa Omar radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake rakaa kumi na moja, Omar alimuamrisha Ubaya Ibun Kaabi Atamiym Al-Daryi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake awaswalishe watu rakaa kumi na moja [110/1,/280 Al Muwatwaa].

Na ushahidi huo ndio unao stahiki kwa Omar Ibun Khatwabai radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kuwa mwenendo wa Omar Ibun Khatwabi ndio mwenendo wa Mtume Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake.

Hatufahamu kuwa kunaswahaba aliye zidisha rakaa kumi na tatu, isipokuwa kinyume na hizo, na tumeisha onyesha ushahidi wa kauli ya Aisha radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, Mtume alikuwa hazidishi rakaa kumi na moja katika mwezi wa

Ramadhan na miezi mingine. Jambo ambalo wamekubaliana maswahaba Mwenyezi Mungu awaridhie hakuna shaka kuwa jambo hilo ni hoja, kwa sababu miongoni mwa maswahaba kuna makhalifa waongofu ambao Mtume ametuamrisha tuwafate, kwa kuwa ndio karne bora ya Umma huu .

Fahamu kuwa ikhtilafu juu ya idadi za rakaa za swala ya tarawehe na ikhtilafu ya mambo mengine ambayo wanachuoni wamejitahidi katika kupapatia ufumbuzi kupishana huko kwa ufahamu na uelewa hakutakiwi kuwa ndio chanzo cha Umma huu kugawanyika, ufahamu kuwa wema alio tangulia walitofautiana lakani hawakugawanyika, katika mambo haya hakuna ushahidi kuwa mtu anaziwiliwa kujitahidi, kauli iliyo bora ni kauli aliye sema mwana chuoni mmoja Mwenyezi Mungu amrehemu, mtu anauhuru wa kumukhalifu mtu katika mambo ya kujitahidi: Ukinipinga umenikubali kwa kuwa kila mmoja anaona ni lazima kufata alicho kiona kuwa ni haki. Namuomba Mwenyezi Mungu atupe sote taufiki ya kufanya anayo yapenda na kuyaridhia.

****

**Swali la 280: Ni ipi hukumu ya kusoma dua ya kukhitimisha Qur`an katika kisimamo cha mwezi wa Ramadhan?**

**Jibu**: Sifahamu ushahidi wowote wa kuhitimisha Qur`an usiku wa mwezi wa Ramadhani katika kiyamu na kuomba dua, siifahamu hadithi inayo thibitisha hilo Au maswahaba kuwa walikuwa wanafanya hilo, Lakini kilicho thibiti ni hadithi alio ipoke Anasi Ibun Maaliki radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: **((Alikuwa akithitimisha Qur`ani anakusanya familia yake anaomba dua))**, [27 / tafsiyri, Sunani Said Ibun Mansur], alikuwa akifanya hivyo njee ya Swala .

Kuhitimisha huko pamoja kuwa hakukuthibiti, lakini kuna asili kwenye Sunnah, lakini watu wanatoka majumbani haswa wanawake wanaelekea katika msikiti maalum kunakuwa na kuchanganyika kati ya wanawake na wanaume wakati watu wanatoka msikitini na jambo hili linafahamika kama tunavyo ona. Lakini baadhi ya Wanachuoni wamesema: Inapendeza Qur`an ikhitimishwe kwa duaa. Lakini kama Imamu angefanya kukhitmisha katika kisimamo cha mwisho

wa usiku na dua hiyo akasoma kwenye kunuti ya swala ya witiri ingekuwa hakuna ubaya, kwa kuwa kunuti ipo kisheria .

****

**Swali la 281: Je usiku wa chezo (Laylatul-Qadiri) huwa upo katika usiku mmoja maalum katika kila mwaka au usiku huo huwa unahama hama mwaka huu katika usiku huu na mwaka mwingine usiku mwengine?**

**Jibu:** Usiku wa cheo hakuna shaka kuwa unapatika ndani ya mwezi wa Ramadhan, kwa kauli ya Mwenyezi Mungu: **[Hakika sisi tumeiteremsha Qur`ani katika laylatul-Qadir**], [Suratul Qadr: 1] Mwenyezi Mungu ameweka wazi katika aya nyingine kuwa ametelemsha Qur`an katka mwezi wa Ramadhan, anasema: **[mwezi wa Ramadhan ambao imeteremshwa humo Qur`ani**] [185/ Surat Al-Baqara] Alikuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake !anakaa itikafu katika kumi la mwanzo la mwezi wa Ramadhan anaitafuta laylatu Al-Qadr, kisha akakaa itikafu katika kumi la pili,kisha akakaa katika kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhan [2016/ Sahihi Bukhary / 215/ Sahihi Muslim], kisha wakawa maswahaba wengi wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake idadi kubwa waliona kwenye ndoto kuwa usiku huo unakuwa katika siku saba za kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhan akasema Mtumee**: ((Naona kwenye Ndoto kawu inatokea sana katika siku saba za mwisho anaye taka kuitafuta basi aitafute katika siku hizo saba za mwisho))** [215/ Sahihi Bukhary, /1165/ Sahihi Muslim]. Huu ndio uchache wa muda ulio tajwa katika mwezi huo.

Tukichunguza ushahidi ulio tajwa kuhusu laylatu Qadr utunafahamu kuwa usiku huo huwa unahama kutoka kwenye usiku huu na kuwa kwenye usiku mwengine hauwi usiku mmoja kila mwaka, Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Alionyeshwa kwenye ndoto usiku wa laylat Qadr kuwa anasujudi asubuhi yake katika maji na udongo, na usiku huo ulikuwa ni siku ya ishirini na moja**)), [215/ Sahihi Bukhary, /1165/ Sahihi Muslim], amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake : **((Pupieni kuitafuta laylat Qadr katika kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhani)),** [2020/ Sahihi Bukhary, / 1169 / Sahihi Muslim]. Hadithi hii unatujulisha kuwa haipatikani siku hiyo katika

usiku maalum, kwa hivyo unakusanya ushahidi, mtu anakuwa katika kila usiku wa masiku kumi ya mwisho wa mwezi anaweza kuipata laylat Qadr, malipo ya usiku huo yanathibi kwa mtu aliye simama kuswali kwa imani na kutaraji malipo kwa Mwenyezi Mungu, mtu huyo akifahamu kuwa ameipata au hata asipo fahamu kuwa ameupata usiku huo, kwa kuwa Mtume Anasema: ((**Atakaye simama usikuwa wa laylatu Qadr kwa imani na kutaraji malipo kwa Mwenyezi Mungu atasamehewa madhambi yake aliyo yatangiliza**)) [37/ Sahihi Bukhary, /759/ Sahihi Muslim], Mtume hakusema kuwa akifahamu kuwa ameipata laylat Qadr, sio sharti kupata malipo ya usiku huo awe anafahamu kuwa ameupata usiku huo, lakini atakaye simama siku kimi za mwisho za mwezi wa Ramadhani siku zote akiwa na imani na kutarajia malipo kwa Mwenyezi Mungu! Tunasema: atakuwa ameupata usiku wa Laylatul Qadir, ikiwa mwanzo wa kumi la mwisho au katikati au mwisho.

****

**Swali la 282: Ni ipi hukumu ya Maamuma kubeba msahafu katika swala ya tarawehe ndani ya mwezi wa Ramadhan kwa hoja kuwa anamfata Imamu kwenye kisoma?**

**Jibu:** Kubeba msahafu kwa lengo hilo ni kinyume na Sunna, kwa mambo yafatayo:

**1-**kwanza kutampita kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto anapo kuwa amesimama.

**2-**kutapelekea kutingishika mara nyingi kusiko kuwa na sababu, katika kufungua msahafu na kuufunika, na kuweka kwenye kwapa au mfukoni nk.

**3-**Anaeswali anakuwa anashughulika na harakati hizo.

**4-**kutampita kutazama sehemu ya kusujudu, na Wanachuoni wengi wanasema kutazama sehemu ya kusujudi ni Sunna na ni bora.

**5-**Anaye fanya hivyo huenda akajisahahu kuwa yupo kwenye swala kama atakuwa hauhudhurishi moyo wake kuwa yupo kwenye swala, kinyume na akiwa mnyeyekevu ameweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto akiwa ameinamisha kichwa chake na macho yake sehemu ya kusujudu, kuwa hivyo kunamfanya azingatie kuwa anaswali na yupo nyuma ya Imamu.

****

**Swali la 273: Baadhi ya maimamu wa misikiti wanajaribu kuzivutia nyoyo za watu na kuwathiri kwa kubadilisha sauti zao muda mwengine wakati wanaswalisha tarawehe, nimesikia baadhi ya watu wanalikemea hilo, ni ipi kauli yenu juu ya jambo hilo? Namuomba Mwenyezi Mungu awahifadhi!.**

**Jibu:** Jambo ambalo mimi ninaona kama atafanya hivyo katika kiwango ambacho sheria inaruhusu hakuna ubaya, kwa ushahidi wa kauli ya Abuu Mussa Al-Ashary radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kumwambia Mtume Muhammadi rehma na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: **((Lau ningefahamu kuwa unasikiliza kisomo changu ninge kipendezesha kwa ajili yako)),** [3160/ Al-bazar, /7279/ Abuu Aliya, /7197/ Ibun Hiban/] Akasame ningeipamba sauti yangu na nikasoma vizuri, watu wakizifanya sauti zao kuwa nzuri. Au akasoma kwa namna ambayo nyoyo zitakuwa zinaigia huruma na kuzidisha imani mimi sioni kuwa kuna ubaya, lakini kuzidisha kiwango katika jambo hili isivuke kiwango cha maneno ya Qur`an kuyabadilisa lakini kama itakuwa kama swali lilivyo ulizwa naona kuwa itakuwa katika kuzidisha haitakiwi kufanya hivyo . Mweyezi Mungu ndio mjuzi.

****

**Swali la 284: Wanasema baadhi ya Wanachuoni: muda wa kuswali Sunna za kabla ya swala ya faradhi na Sunna za baada ya swala ya faradhi zinaswaliwa ukiingia muda wa swala ya faradhi na hauruhusiwi kuswali kwa kutoka muda wa swala ya fardhi, wanasema Wanachuoni wengine: Sunna ya kabliya inaisha muda wake kwa kuisha muda wa kulipa swala ni ipi kauli yenye nguvu?**

**JIBU:** Kauli yenye nguvu Sunna kabliya muda wake ni kuwanzia unapo ingia muda wa swala mpaka kuswali swala ya faradhi, Sunna za adhuhuri za kabla ya swala zina anza tokea muda wa adhana ya adhuhuri, kwa maana kuanzia kupinduka jua na unaisha muda wa Sunna hizo kwa kuswali kwa maana kuswali swala ya adhuhuri.

Sunna ya baada ya swala ya faradhi inayo itwa Sunna baadiya inaanza muda wake unapo isha muda wa swala ya faradhi na inaisha kwa kuisha muda wa swala ya faradhi.

Lakini mtu ukimpita muda wa kuswali Sunna ya kabliya bila kufanya kusudi utailipa Sunna hiyo ya kabliya baada ya swala ya faradhi, kama akiichelewesha kuswali bila udhuru haita msaidia kuilipa baada ya kuswali faradhi, kwa kuwa kauli sahihi kila ibada inamuda wake ukitoka muda wake bila udhuru ukiiswali baada ya kutoka muda haisihi wala haikubaliwi.

****

**Swali la 285: Ni ipi hukumu ya kulipa swala ya Sunna baada ya swala ya Al-fajir kwa mtu ambaye hakuweza kuiswali Sunna hiyo kabla ya swala? Je vina pingana kulipa Sunna baada ya Al-fajir na katazo la kuswali baada ya swala ya Al-fajir?**

**Jibu**: Kulipa Sunna baada ya swala ya Al-fajir hakuna ubaya kwa kauli iliyo na nguvu.

Wala haipingani na katazo la kuswali baada ya swala ya Al-fajir kwa kuwa katazo la kuswali baada ya swala ya Al-fajir ni swala ambayo haina sababu.

Lakini akiichelewesha kuilipa mpaka kufikia muda wa swala ya dhuhaa kama hato hofia kusahahu muda huo ni bora kwake kulipa Sunna iliyo mpita.

****

**Swali la 286: Mtu akingia msikitini kabla ya Adhana akaswali tahiyatul-masjidi, kisha muadhini akatoa Adhana je ataanza tena kuswali Sunna?**

**JIBU:** Ikiwa imetolewa adhana ya swala ya Al-fajir au adhuhuri akimaliza muadhini kutoa adhana inatakiwa naye anze kuswali Sunna za kabla ya swala ya Al-fajir, na rakaa nne kabla ya swala ya dhuhuri, ikiwa adhana itatolewa kwa ajili ya swala zingine pia ni Sunna kwa mtu huyo swali , kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((kati ya kila adhana mbili kuna swala**)), [627/ Sahihi Bukhary, /838 Sahihi Muslim].

****

**SWALI LA 287: Je mtu atalipa swala za Sunna za rawatibu?**

**Jibu:** Ndio, swala za Sunna za rawatibu muda wake ukiisha kwa kusahahu au kwa sababu ya usingizi mtu amelala mtu huyo atazilipa Sunna hizo, kwa ushahidi wa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Atakaye lala na hakuswali au akasahau na aswali atakapo kumbuka** )), [597/ Sahihi Bukhary, /684/ Sahihi Muslim] Aimepokewa hadithi kwa Umu salama radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kuwa Mtume alishughulishwa hakuswali rakaa mbili baada ya dhuhuri akazilipa baada ya swala ya alasiri .[1233/ Sahihi Bukhary, /834/ Sahihi Musilim], lakini akiiacha kwa makusudi mpaka muda wake ukapita swala hiyo hailipwi kwa kuwa Sunna za swala za rawatibu ni ibada

na ibada zinamuda wake mtu akifanya makusudi kuitoa katika muda wake haikubaliwi ibada hiyo.

****

**Swali la 288: Je kuna ushahidi wa mtu kubadili sehemu ya kuswalia Sunna baada ya kumaliza kuswali Faradhi?**

**Jibu**: Ndio, imepokewa hadithi ya Muaawiya radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! Amesema: **((Mtume rehma na amani ziwe juu yake ametuamrisha tusionganishe swala na swala mpaka tuonge au tutoke sehemu tulio swali swala ya kwanza**)) [ 833/ Sahihi Muslim] Wameelezea Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, kuwa inatakiwa kutenganisha kati ya swala ya faradhi na swala ya Sunna kwa kuongea au kuhama kwenda sehemu nyingine.

****

**Swali la 289: Mtu ikimpita Sunna ya swala ya Dhuha atailipa?**

**Jibu**: Swala ya dhuha ikipita muda wake hailipwi, kwa kuwa Sunna ya dhuha imepangwa hivyo, lakini Sunna za rawatibu kwa kuwa zinafata swala za faradhi ndio zinalipwa, pia imethibiti swala ya witiri **((Alikuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake ukimzidia usingizi au maradhi usiku huswali mchana rakaa kumi na mbili)).** [746/ Sahihi Muslim] Swala ya witiri inalipwa.

****

**Swali la 290: Hivi ni sharti kuwa na udhu ukitaka kusujudu sijida ya kisomo? Na ni yiradi gani sahihi unasoma ukiwa umesujudu?**

**Jibu:** Sijida ya kusoma Qur`an ni sijida ya kisheria inafahamika nayo ni mtu akiwa anasoma Qur`an akifika katika aya ya kusujudu ambayo inafahamika, akitaka kusujudu ataleta takbir (AllahAkbar) kisha atasujudu atasema kwenye sijida (Subhana Rabiyal-alaa)) au atasema: ((Subhaanaka Rabanaa wabihamdika, Allahuma ighfir lii)) au atasema: ((Allahuma laka sajadtu, wabika aamantu, walaka aslamtu, sajada wajihii liladhii khalakahu, wa swawarahu, washaka samuahu, wabaswarahu bihaulihi wakuwatihi, [1414 /Abuu Daud, /580/ Atirmidhy] au Atasema: ((Allahuma iktubu lii biha ajiraa, wahutwa anii biha wizraa, wajaalaha

lii indaka dhukhra, watakabalha min indika daawad )) [579/ Atirmidhiy], kisha atainuka bila kuleta takbir wala kutoa salamu, isipokuwa kama sijida itakuwa kwenye swala, mfano: mtu asome aya ambayo inasijida naye anaswali ni lazima alete takbira akienda kusujudu, na ni lazima alete takbira anapo inuka, kwa kuwa walio sifia swala ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Alikuwa akileta takbira anapo inama na kuinuka, [785/ Sahihi Bukhary, /392 / Sahihi Muslim] hiyo inakuwa kwenye takbira za kuinama kwa swala na kusujudu kwa kisomo. Ama wanavyo fanya baadhi ya watu kuwa wanaleta takbir wakienda kusujudu na wakiinuka kutoka kwenye sujudu hawaleti takbir sifahamu ushihidi katika mafunzo ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, wala sifahamu kauli za Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu.

**Kuhusu kauli ya muulizaji**: Hivi ni sharti kuwa na twahara ( udhu) wakati wa kusujudu kwa ajili ya kisomo?

Jambo hilo linakhilafu kwa Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu: Wapo Wanachuoni walio sema: kuwa ni lazima mtu awe na udhu.

Wapo Wanachuoni walio sema: kuwa sio sharti kuwa na udhu, alikuwa Ibun Omar radhi za Mwenyezi Mungu ziwee juu yake anasujudu bila kuwa na udhu. [1071/ Sahihi Bukhary, /4322/ Ibun Abii Shaybaa].

Lakini ninacho ona na kutoka kwenye mashaka asisujudu mpaka awe na udhu.

****

**Swali la 291: Ni muda gani mtu atasujudu kwa ajili ya kumshukuru Mwenyezi Mungu? Ni zipi sifa za kusujudu huko? Je ni sharti kwa anaye sujudu kwa ajili ya kushukuru awe na udhu?**

**Jibu:** Kusujudu kwa ajili ya kushukuru kuna kuwa wakati mtu aliye kuwa na matatizo yakiondoka matatizo hayo asujudu kwa ajili ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, au mtu akipata neema, kusujudu kwa mtu huyo kunakuwa kama kusjudu kwa anaye soma Qur`an nje ya swala, baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu wanasema: kuwa anatakiwa kuwa na udhu na ataleta takbira wakati wa kusujudu, baadhi ya Wanachuoni wengine wanasema: ni bora kuleta takbira tu kisha atasujudu ataomba dua hii akiwa kwenye kusujudu ((Subhana Rabii Al-alaa)).

****

**Swali la 292: Ni ipi hukumu ya swala ya istikhara? (kuomba maelekezo kwa Mwenyezi Mungu) Hivi mtu anaweza kusoma dua ya istikhara akiswali tahiyatu Al-masjidi au akiswali Sunna za kabla ya swala au baada ya swala?**

**Jibu:** Swala ya istikhara ni Sunna mtu akitaka kufanya jambo akawa hana ufumbuzi wa kufanya jambo hilo au kuwacha kulifanya.

Kuhusu mambo ambayo yapo wazi kuyafanya au kuwacha kufanya sio sheria kuswali istikhara, ndio maana Mtume rehma na amani ziwe juu yake alikuwa anafanya mambo mengi, alikuwa hafanyi isipokuwa baada ya dhiki, na haikupokewa hadithi kuwa alikuwa anaswali istikhara, kama atakuwa na pupa ya kutaka kuswali, au kutoa zaka, au kuwacha mambo ya haramu, nk. Au akawa na hamu ya kula, au kunywa, au kulala, haifai kuswali istikhara kwa ajili ya mambo hayo.

Hatakiwi kusoma dua ya istikhara akiswali tahiyatul- Masjidi-au Sunna za baada ya swala au kabla ya swala kwa kuwa hakunuwiya toka mwanzo, kwa kuwa hadithi ya kuswali istikhara ipo wazi akiswali bila kuwa na niya hatokuwa amefata maelekezo ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake.

Akinuwiya istikhara kabla ya tahiyatul-masjidi au swala za sun`na zinazo kuwa na swala ya faradhi kisha akaomba dua ya istikhara kwa mujubu wa hadithi kuwa inaruhusiwa, kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Aswali rakaa mbili zisizo kuwa za faradhi**)) [6382 / Sahihi Bukhary], Mtume hakuinyambua isipokuwa swala ya faradhi inakisiwa kuwa haifai, kwa kauli ya ((**Akipupia jambo aswali rakaa mbili))** inatijulisha kuwa hakuna sababu ya hizi rakaa mbili isipokuwa istikhara, na iliyo bora kwangu aswali rakaa mbilii zilizo jitegemea , Mwenyezi Mungu ndio mjuzi.

****

**Swali la 293: Ni ipi swala ya tasbihi?**

**Jibu**: Swala ya tasbihi haikuthibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, amesema Imamu Ahmadi Mwenyezi Mungu amrehemu kuhusu hadithi ya swala ya tasbi kuwa hadithi haisihi, na amesema sheikh Isalami Ibun Tayimya Mwenyezi Mungu amrehemu: **((Ni urongo, na amesema Ahmadi kwenye matini na maimamu na wafwasi wao kuipinga hadithi hiyo na Imamu Ahmadi hakuipenda, amaa Imamu Abuu Hanifa na Maaliki na Shafii hawakuisikia hadithi hiyo))** [405/2/ Al-Furuu /100-99/ Al-ikhiyaratu Abii Aliy] Maneno hayo ni ya Sheikh Islamu Ibun Taymiya alicho kisema ni ukweli, kama swala ingekuwa sahihi ingepokewa na maimamu kwa upokezi sahihi kwasababu ya ubora wake na kwa kuwa ingekuwa ni swala, lakini hatufahamu kuwa kuna ibada ambayo ni khiyari unafanya kila siku, au kwa weki mara moja, au kwa mwezi mara moja, au kwa mwaka, au kwa umri wako mara moja, hakika jambo ambalo lingekuwa geni kwa watu lazima ingepokewa habari yake, na habari yake ingeenea kwa kuwa ni jambo geni, kwa kuwa halikuwafahamika ni wazi kuwa halipo kwenye sheria kwa sababu hiyo hakupenda hata Imamu mmojo.

****

**Swali la 294: Ni ipi hukumu ya kuswali raaka mbili usiku wa ndoa wakati wa kukutana mke na mume?**

**Jibu**: kuswali rakaa mbili usiku wa kwanza kwa mtu alieoa waliswali baadhi ya maswahaba radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao [10460/ Muswanafu Abdul-Razaq, /8993 /Muujamu Al-kubra, liTwabrany], Lakini sifahamu Sunna hii usahihi wake kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, lakini jamabo ambalo linafahamika kuwa ni Sunna mwanaume amshike mke wake kwenye utosi amuombe kwa Allah kheri zinazo tokana na mwanamke huyo, na ajilinde kwa Mwenyezi Mungu kutokana na shari pia na shari zinazo tokana na mwanamke huyo, [2160/Abuu Daud, / 1918/ Ibun Majah], kama atakuwa anahofia kuwa mwanamke atamkimbia amshike kwenye utosi kama anataka kumsogelea kisha aombe dua kwa siri mwanamke huyo asimsikie, kwa kuwa baadhi ya wanawake wanaweza kushangaa ukisema kwenye dua :najilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na shari ya mwanamke huyo, Akasema: kwa hiyo mimi nina shari?.

****

**Swali la 295: Ni zipi nyakati zilizo katazwa mtu kuswali? Je swala ya tahiyatul Masjidi kabla ya swala ya magharibi inakuwa kabla ya adhana au baada ya adhana? Tupeni fatua Mwenyezi Mungu awalipe kheri.**

**Jibu:** Nyakati zilizo katazwa kuswali ni:

**1-Muda wa kwanza**: Ni kuwanzia baada ya swala ya Al-fajir

mpaka jua lichomoze na liinuke kiasi cha mkuki, muda wake ni ibaada ya jua kuchomoza ipite muda kama dakika kumi na tano au dakika ishrini na tano.

**2-Muda wa pili:** Ni kabla ya jua kukengeuka muda wake ni kabla ya kuingia wakati wa swala ya adhuhuri kama muda wa dakika kumi.

**3-Muda wa tatu:** Baada ya kuswali alasili mpaka jua lizame, nyakati hizi ndio zilizo katazwa kuswali.

Kuhusu kuswali tahiyat al-masjidi inaswaliwa kwa kila muda, ukiingia tu msikitini usikae mpaka uswali rakaa mbili, hata kama itakuwa katika nyakati zilizo katazwa.

Inatakiwa watu wafahamu kuwa kauli iliyo na nguvu katika kauli za Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu! Sunnah zote zenye sababu haziingii katika nyakati zilizo katazwa, isipokuwa huswaliwa hata kama ni katika nyakati zilizo katazwa, ukiingia msikitini baada ya swala ya Al-fajir swali rakaa mbili, ukiingia msikitini kabla ya jua kukengeuka swali rakaa mbili, ukiingia muda wowote iwe usiku au mchana usikae chini mpaka uswali rakaaa mbili.

****

### Swali la 296: Ni ipi hukumu ya swala ya jamaa?

**Jibu:** Hukumu ya swala ya jamaa wamekubaliana Wanachuoni

Mwenyezi Mungu awarehemu kuwa ni katika ibada tukufu, na ni ibada iliyo tiliwa mkazo, na ibada bora, hakika ameelezea Mwenyezi Mungu mtukufu katika Qur`an, na ameamrisha katika hali ya hofu, amesema Mwenyezi Mungu: **[Na unapo kuwa pamoja nao ukawaswalisha, basi kundi moja miongoni mwao wasimame pamoja na wewe na wachukue silaha zao, na watakapo maliza sijida zao, basi na warudi nyuma yenu, na lije kundi jingine ambalo halija swali, liswali pamoja na wewe nao wachukue hadhari yao na silaha zao, walio kufuru wanapenda mghafilike na silaha zenu na vifaa vyenu ili wakuvamieni mvamio wa mara moja wala sii vibaya kwenu mkiwa mnaona udhia kwa sababu ya mvua au mkawa wagonjwa mkaziweka silaha zenu na chukueni tahadhari yenu hakika Mwenyezi Mungu amewandalia makafiri adhabu yenye kudhalilisha],** [Suratu Nisaa: 102].

Katika Sunna za Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kuna hadithi nyingi sana zinazo tujulisha ulazima wa kuswali jamaa, mfano kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Nilikusudia niamuru swala ikimiwe, kisha niamuru mtu awaswalishe watu, kisha nitoke mimi na wanaume wakiwa wamebeba kuni niende kwa watu ambao hawakuswali jamaa nizichome nyumba zao kwa moto**)), [644/ Sahihi Bukhary,/ 651/ Sahihi Muslim] .

Na kauli ya Mtume rehma na amani ziwee juu yake**: ((Atakae sikia adhana na hakuenda swali jamaa mtu huyo hana swala isipokuwa kwa udhuru))** [551/ Abu Daud, / 551/793/ Ibun Majah], Na kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa mwanaume kipofu aliye kuja kwa Mtume kuomba ruhusa aswalie nyumbani Mtume akamuliza: **((Unasikia adhana?))** Akamjibu: ndio, akasema Mtume**: ((lazima uswali jamaa))** [653/

Swahihi Muslimu]. Amesema Ibun Masuod radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake**: ((Hakika tulikuwa maswahaba wa Mtume na Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Hakhalifu kuswali jamaa isipokuwa mnafiki tunaufhamu unafiki wake, au mgonjwa, alikuwa mtu analetwa amebebwa na wanaume wawili mpaka wanamsimamisha kwenye swafu))** [654/ Sahihi Muslim] .

.

Mtazamo sahihi unaonyesha kuwa kuswali jamaa ni lazima, hakika Uma wa kislamu ni Umma mmoja , na hauwezi ukakamilika umoja isipokuwa watu wakutane katika ibada na ibada iliyo tukufu na bora na iliyo tiliwa mkazo ni swala, ndio sababau imekuwa ni waJibu kwa Umma wa kiislamu kukusanyika kwa ajili ya swala.

Wametofautiana Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu baada ya kukubaliana kuwa swala ndio ibada tukufu na bora na iliyo tiliwa mkazo, wametofautiana kuwa kuswali jamaa ni sharti la kusihi swala? Au swala inasihi hata kama mtu hakuswali jamaa lakini anapata madhambi? Na ikhitilafu zingine.

Kauli sahihi: kuswali jamaa ni wajibu, sio sharti la kusihi swala, lakini atakaye acha kuswali jamaa atapata madhambi isipokuwa akiwa na udhuru wa kisheria, na ushahidi kuwa swala ya jamaa sio sharti la kusihi swala , Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema: **((Fadhila za swala ya jama juu ya swala ya mtu anaye swali peke yake))**, [645/ Sahihi Bukhary, 650/ Sahihi Mslim], na ubora wa swala ya jamaa ju ya swala ya mtu mmoja unajulisha kuwa mtu akiswali peke yake kuna ubora, kwa hivyo haiwezi kukawa na ubora wakati swala haikusihi.

Ni lazima kwa kila mwilsamu mwenye akili timamu mwanaume aliye baleghe aswali jamaa akiwa safari au hakusafiri.

****

**Swali la 297: Kundi la watu wanaoishi sehemu moja wanaruhusiwa kuswali jamaa katika nyumba hiyo au ni lazima watoke waende msikitini?**

**Jibu:** Ni lazima kwa kundi hilo la watu wanao ishi katika jengo moja waende kuswali msikitini, kila mtu ambaye yupo karibu na msikiti ni lazima aswali msiktini, hairuhusiwi kwa yeyote au kundi la watu kuswali nyumbani na msikiti upo karibu, kama msikiti utakuwa upo mbali kiasi ambacho hasikii adhana sio vibaya wakiswali jamaa kwenye nyumba hiyo wanao ishi, uzembe wa baadhi ya watu kuwacha kuswali jamaa ni kwa sababu ya kauli ya baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, walio sema kuwa makusudio ya jamaa ni watu wakusanyike hata kama sio msikitini, wakiswali jamaa hata kama ni katika majumba yao watakuwa wametekeleza wajibu.

Lakini iliyo sahihi ni lazima jamaa iwe msikitini kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Nilikusudia niamuru swala ikimiwe, kisha niamuru mtu awaswalishe watu, kisha nitoke mimi na wanaume wakiwa wamebeba kuni niende kwa watu ambao hawakuswali jamaa nizichome nyumba zao**

**kwa moto)),** [644/ Sahihi Bukhary, /651/ Sahihi Muslim]. pamoja kuwa watu hao inawezekana wameswali kwenye majumba yao au sehemu zao lakini Mtume amelikemea jambo hilo .

Ni lazima kwa kundi hilo linalo ishi katika jengo moja waswali jamaa msikitini isipokuwa kama msikiti utakuwa mbali nitabu kufika msikitini.

****

**Swali la 298: Ni lipi bora kwa mfanya kazi akisikia adhana awahi kwenda kwenye swala au asubiri amalizie baadhi ya kazi? Ni ipi hukumu ya kuswali Sunna zisizo kuwa za rawatibu?**

**Jibu**: Jambo bora kwa waislamu wote wawahi kwenda kwenye swala wanapo sikia adhana, kwa kuwa muadhini anasema**:** **((Hayya alaa swalaa))** njooni kwenye swala, mtu kuchelewa kwenda kwenye swala kutapelekea swala ya jamaa kumpita.

Kuhusu kuswali Sunna baada ya swala kama ni Sunna ambazo sio rawatibu (zinazo swaliwa baada ya swala za faradhi), hairuhusiwi kwa kuwa muda wake ni haki ya mtu mwengine kwa mujibu wa makubaliano ya ajira alio pewa, kuhusu swala za Sunna ambazo ni rawatibu sio vibaya kuswali, kwa kuwa zipo katika mambo ambayo yamezoweleka na wasimamizi wa

kazi wanaruhusu kuswali Sunna za baada ya swala. Mwenyezi Mungu ndio anaye toa taufiki.

****

**Swali la 299: Mtu akichelewa rakaa moja au mbili katika Swala ya jamaa wakati wakulipa rakaa zilizo mpita atasoma Suratul Fatiha na sura nyingine? Au atasoma Suratul Fatiha peke yake?**

**Jibu**: Rakaa anazozilipa Maamuma baada ya kutoa salamu Imamu huwa ni rakaa za mwisho, kwa hivyo hatosoma isipokuwa Suratul Fatiha kama itakuwa amechelewa rakaa mbili au rakaa moja kama swala ilikuwa ni ya rakaa nne au swala ya magharibi, kama atakuwa amechelewa katika swala ya Al-fajiri atasoma Suratul Fatiha na Sura nyingine baada ya kumaliza kusoma Suratul Fatiha kwa kuwa rakaa zote mbili za swala ya Al-fajir unasoma Suratul Fatiha na sura nyingine.

****

**Swali la 300: Mtu ameingia msikitni kamkuta Imamu yupo kwenye tahiyyaatu ya mwisho mtu huyo ataingia kwenye jamaa ya Imamu? Au atasubili jamaa nyingine ya pili?**

**Jibu:** Mtu akingiia akamkuta Imamu yupo kwenye tahiyy-aatu ya mwisho akiwa na uhakika kuwa jamaa nyingine ipo hato ingia kuswali na Imamu atasubili jama ya pili, lakini kama hatarajii kuwa kunajamaa ya pili aingie kuswali na Imamu, kwa kuwa kauli sahihi mtu hadiriki jamaa isipokuwa mpaka awahi rakaa, kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake**: ((Atakaye idiriki rakaa moja katka swala amediriki swala)),** [580/ Sahihi Bukhary, / 607/ Sahihi Muslim] kama ilivyo swala ya ijumaa mtu haidiriki isipokuwa kwa kudiriki rakaa moja basi na swala ya jamaa, akimkuta Imamu yupo katika tashahudi ya mwisho atakuwa hakudiriki jamaa, asubili mpaka aswali na jamaa anayo itarajia, kama atakuwa hataraji jamaa nyingine kuingia kuswali na Imamu kwenye tashahudi hiyo ni bora kuliko kuondoka .

****

## Swali la 301: Mtu atafanyaje kama atakuwa anaswali Sunna ikakimiwa swala ya faradhi?

**Jibu:** Iki kimiwa swala ya faradhi, na mtu ameanza kuswali Sunna, wapo Wanachuoni wanao sema: ni lazima kuikata swala ya Sunna kwa haraka, hata kama atakuwa kwenye tashahudi ya mwisho.

Wapo Wanachuoni wanaosema: hato ikata isipokuwa kama atahofia Imamu atatoa salamu kabla ya yeye kumuwahi Imamu na kudiriki takbira ya kuhirimia. Kauli hizi mbili zinapingana.

**Kauli ya kwanza**: Ikikimiwa swala aikate swala ya Sunnah hata kama upo kwenye tashahudi ya mwisho.

**Kauli ya pili**: Usikate swala isipokuwa ikabaki swala ya Imamu kiasi cha kuwahi takbira ya kuhirimia ndio ukate, kwa maana unaendela kuswali wala haukati mpaka ukiofu Imamu atatoa salamu kabla ya wewe haujamuwahi takbira ya kuhurimia.

Kauli hizi zina kinzana, kauli ya pili uendelee kuswali Sunna hata kama rakaa zote zitakupita, ilimradi uwahi takbira ya kuhirimia, kabla ya Imamu kutoa salamu, endelea na kuswali Sunna.

**Namimi nasema kauli ya kati na kati katika jambo hilo**: Iki kimiwa swala na wewe upo kwenye rakaa ya pili ikamilishe swala yako lakini ifanye nyepesi, iki kimiwa swala upo kwenye rakaa ya kwanza kata swala ukaswali faradhi, kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Atakaye diriki rakaa moja katika swala hakika ameidiriki swala**)), [580/ Sahihi Bukhary, /607/ Sahihi Muslim], ukiwa umeswali rakaa kabla ya kukimiwa swala umeipata rakaa kabla kizuizi.

Ukidiriki raka kabla ya kizuizi umeidiriki swala, swala itakuwa haija katazwa kwako, ikamilishe lakini nyepesi, kwa kuwa kupata sehemu ya faradhi ni bora kuliko kupata sehemu kwenye Sunna, kama utakuwa upo kwenye rakaa ya kwanza hakika hauwezi kudiriki muda wakuwahi swala, kwa kuwa Mtume amesema: ((**Atakaye diriki rakaa moja katika swala hakika ameidiriki swala**)), [580/ Sahihi Bukhary, / 607/

Sahihi Muslim] kwamisingi hiyo utaikata swala ya Sunna, kwa kauli ya Mtume: **((Iki kimiwa swala hakuna swala nyingine isipokuwa swala ya faradhi))** [710 / Swahihi Muslimu].

****

**Swali la 302: Maamuma akiingia kwenye swala baada ya Imamu kumaliza takbira ya kuhirimia na kusoma Suratul Fatiha, Maamuma akanza kusoma Suratul Fatiha lakini Imamu akarukuu kabla ya Maamuma kumaliza Suratul Fatiha, je Maamuma atarukuu na Imamu! Au atakamilisha Suratul Fatiha?**

**Jibu:** Maamuma akingia akamkuta Imamu anataka kurukuu,na Maamuma hakuweza kusoma Suratul Fatiha, kama atakuwa ameanza kusoma Suratul Fatiha lakini amebakisha aya mbili au tatu kukamulisha sura hiyo kwa hali ambayo anaweza kumuwahi Imamu akiwa amerukuu ni bora aikamilishe ndio arukuu, kama itakuwa imebaki sehemu kubwa kumaliza Suratul Fatiha, hali ambayo akisoma sura nzima hato muwahi Imamu kwenye rukuu anatakiwa arukuu na Imamu hata kama hakukamilisha kuisoma Suratul Fatiha.

****

**Swali la 303: Maamuma akimkuta Imamu amesujudu, atamsubiri Imamu ainuke au atamfata?**

**Jibu:** Iliyo bora ni kumfata Imamu kwenye sijida, au sehemu yoyote utakayo mkuta wala asimsubiri, kwa ujumla wa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Mtakazo zikuta mziswali**)), [636/ Sahihi Bukhary, /602/ Sahihi Muslim].

****

**Swali la 304: Mtu anaeswali nyuma ya Imamu katika swala ambazo anasoma kwa siri akimaliza kusoma Suratul Fatiha na sura nyingine kabla ya Imamu kurukuu, mtu huyo atakaa kimya?**

**Jibu**: Maamuma hatokaa kimya bada ya kumaliza kusoma Suratul Fatiha na sura nyingine baada ya Suratul Fatiha kama Imamu atakuwa haja rukuu, isipokuwa ataendelea kusoma mpaka Imamu arukuu, hata kama itakuwa ni rakaa mbili za mwisho zinazo kuwa baada ya tashahudi ya kwanza akimaliza kusoma Suratul Fatiha na Imamu hakurukuu Maamuma atasoma sura nyingine mpaka Imamu arukuu, kwa kuwa hakuna kukaa kimya kwenye swala isipokuwa wakati wa kumsikiliza Imamu akiwa anasoma.

****

**Swali la 305: Ni ipi hukumu ya Maamuma kumtangulia Imamu kwenye matendo ya swala?**

**Jibu**: Kumtangulia Imamu ni haramu, kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Haogopi yule ambaye anainua kichwa chake kabla ya Imamu kubadilishwa kichwa chake kama punda, au sura yake kuwa kama sura ya punda))**, [691/ Sahihi Bukhary, /427/ Sahihi Muslim]. Hilo ni kemeo kwa mtu anaye mtangulia Imamu, haliwezi kuja kemeo isipokuwa kufanya jambo la haramu, au kuwacha wajibu.

Imethibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa alisema: **((Amejaliwa Imamu ili akamilishe swala, akileta takbra nanyi leteni takbira, wala msilete takbra mpaka alete takbira, akirukuu mrukuu, wala msirukuu mpaka arukuu )),** [1114/ Sahihi Bukhary, / 411/ Sahihi Muslim, / 341/2/ Imamu Ahamdi].

**Nisema kuhusu munasaba huu**: Imamu na Maamuma wana hali nne:

**1-**Maamuma anaye mtangulia Imamu.

**2-**Mamuma anaye kwenda sambamba na Imamu.

**3-**Mamuma anaye mfata Imamu.

**4-**Mamuma Anaye chelewa kumfata Imamu.

**Anaye mtangulia Imamu**: Ni Maamuma anaye anza kufanya kitu kwenye swala kabla ya Imamu, kufanya hivyo ni haramu, kama atamtangulia Imamu katika takbra ya kuhirimia swala, atakuwa hajafunga swala kabisa, ni lazima arudiye kuswali.

**Anaye kwenda sambamba na Imamu**: Ni ambaye anakuwa yupo sawa sawa na Imamu anarukuu pamoja na Imamu na kusujudu pamoja naye na shuka pamoja naye, hadithi ya Mtume inaonyesha kufanya hivyo ni haramu kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Msirukuu mpaka arukuu))**.

Baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, wanaona kuwa ni karaha mtu kwenda sambamba na Imamu, na kuwa sio haramu, isipokuwa kwenye takbira ya kuhirimia swala akihirimia swala sambamaba na Imamu haja funga swala ni lazima arudie kuhirimia swala tena .

**Kumfata Imamu**: Ni kuleta matendo ya swala baada ya Imamu bila kuchelewa, na kufanya hivyo ndio jambo la kisheria linalo takiwa.

**Kuchelewa:** Ni mtu kuchelewa kumfata Imamu kuchelewa ambako kutamtoa katika kumfata Imamu kufanya hivyo ni kinyume na mafunzo ya sheria.

****

### Swali la 306: Je inasihi kuswali nyuma ya mtu muovu?

**Jibu**: Kuswali nyuma ya mwislamu hata kama anafanya baadhi ya maasi inaruhusiwa, na ndio kauli iliyo sahihi na yenye nguvu, lakini kuswali nyuma ya mtu mwema ni bora, kama mtu atakuwa anatumia vitu ambavyo ni vya ukafiri vinavyo mtoa

kwenye Uislamu hairuhusiwi kuswali nyuma yake, kwa kuwa swala ya mtu huyo sio sahihi, kama atakuwa sio mwislamu swala yake sio sahihi, ikiwa swala ya Imamu sio sahihi haiwezekani kumfata Imamu huyo, kwa kuwa unamfata asiye kuwa Imamu, unanuwiya kuwaogzwa na mtu asio kuwa Imamu.

****

**Swali la 307: Je inafaa kuswali faradhi nyuma ya anayeswali Sunna, na anaye swali Sunna nyuma ya anaye swali faradhi?**

**Jibu:** Inaruhusiwa, kama inavyo ruhusiwa kuswali Adhuhuri nyuma ya Imamu anaye swali Alasiri, na kuswali alasiri nyuma ya Imamu anaye swali adhuhuri, kwa kuwa kila mmoja kwa niya yake, amesema Imamu Ahmadi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake**: (Ukingia msikitini na Imamu anaswali tarawehe nawe haujaswali ishaa swali nyuma yake, wewe utakuwa unaswali faradhi naye anaswali Sunna),** [90/ Masail imau Ahmadi liabi Daud].

****

**Swali la 308: Kumetokea mjadala kati ya kundi la watu walio kuwa wanaswali akaingia mtu msikitini akiwa amechelewa akakuta swala imekimiwa na swafu imekamilika hakupata nafasi kwenye swafu, je inafaa kwa mtu huyo kumvute mtu mmoja katika swafu ya mbele ili waweke swafu ya pili nyuma wakiwa wawili, au aswali peke yake , au atafanyaje?**

**Jibu:** Mambo hayo yamegawanyika sehemu tatu: Mtu akikuta swafu imekamilika.

**1-**Ima aswali peke yake nyuma ya swafu.

**2-**Ima amvute mtu kwenye swafu ya mbele aswali naye kwenye swafu ya nyuma.

**3-**Au atangulie mbele aswali kwenye ubavu wa kulia wa Imamu.

Sifa hizi tatu akiingia kwenye swala, ima aache swala ya jamaa hiyo, ni jambo gani atachagua kwenye mambo hayo manne?

**Tunasema**: Anatakiwa kuchagua jambo moja katika mambo manne : Aweke swafu ya peke yake nyuma ya swafu aswali jamaa na Imamu, kwa sababu ni lazima kuswali jamaa , na kuswali kwenye swafu ni waJibu kwa hiyo zinakuwa waJibu mbili waJibu wa kuswali jamaa na kuwa kwenye swafu, ukipata udhuru wa waJibu mmoja nao ni kusimama kwenye swafu, umebaki waJibu mwengine wa kuswali jamaa, kwa hivyo tunasema: swali jamaa nyuma ya swafu upate ubora wa kuswali jamaa, na kuswali kwenye swafu katika hali hiyo sio lazima kwako,

kwa kuwa umeshindwa kupata nafasi, amesema Mwenyezi Mungu mtukufu**: [Basi mcheni Mwenyezi Mungu muwezavyo],** [Surat Taghaabun: 16]. Na ushahidi wa haya ni kuwa mwanamke anaruhusiwa kusimama nyuma ya swafu akiwa peke yake kama kutakuwa hakuna wanawake isipokuwa peke yake, kwa kuwa hana nafasi ya kisheria kwenye swafu ya wanaume, ilivyo patikana dharura ya kisheria katika swafu ya wanaumee ameswali peke yake.

Mwanaume ambaye amekuja msikitini na swafu imekamilika na hakupata nasafi katika swafu umeanguka ulazima wa kuwa kwenye swafu, ni lazima kwakwe kuswali jamaa, basi naaswali nyuma ya swafu, ama kumvuta mtu kutoka kwenye swafu ya mbele aswali naye, kufanya hivyo haitakiwi, kwakuwa kufanya hivyo kunasababisha mambo matutu:

**1-Jambo la kwanza:** Atasababisha kubaki nafasi katika swafu ya kwanza na kufanya hivyo ni kinyume na Bunna aliyo iamrisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake, Mtume ameamrisha kuziba mwanya kati ya swafu.

**2-Jambo la pili:** Utakuwa umemuhamisha mtu kutoka kwenye swafu bora kuja kwenye swafu ambayo haifikii ubora swafu aliyo kuwa,kufanya hivyo umemkosea.

**3-Jambo la tatu:** Utakuwa umemshawisha kwenye swala yake, kwa kuwa ukimvuta mtu kwenye swala ni lazima utamsababishia kutingishika kwa mwili na moyo kufanya hivyo utakuwa umemkosea pia.

kusimama na ImaMu, hili pia halitakiwi kwa kuwa ni lazima Imamu afahamike kwa Maamuma sehemu yeke, kama wanavyo fahamu kuwa Imamu lazima awatangulie kwa kauli

na vitendo, Imamu ataleta takbra kabla yao atarukuu kabla yao, inatakiwa awe anajulikana kwa wao.

Na huu ndio muongozo wa Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake kuwa Imamu anawatangulia Maamuma, kwa munasaba huo upo wazi kuwa anafahamika na amejitenga sehemu yake sehemu ambayo hatakiwi kujitenga isipokuwa Imamu kwenye swala.

**4-Sehemu ya nne**: Ni kuwacha kuswali jamaa, jambo hili halina nafasi kwa kuwa kuswali jamaa ni wajibu, na kukaa kwenye swafu ni waJibu, kimoja kikishindikana hakisababishi kingine kuto kuwepo.

****

**Swali la 309: Kuna Misikiti yenye ghorofa moja mpaka mbili wanao swali ghorofa ya pili hawawaoni wanao swali katika ghorofa ya chini, je swala zao ni sahihi?**

**Jibu:** Kwa kuwa Msikiti ni mmoja sio sharti waonane kama watakuwa wanasikia takbira ya Imamu.

Ameiandika muhmmadi swaleh uthaymini /25/8/1410/H.

****

**Swali la 310: Je Muislamu anaruhusiwa kuswali kwa kufuata swala inayo onyeshwa kwenye television moja kwa moja, au kwenye radio bila kumuona Imamu haswa kwa wanawake?**

**Jibu**: Hairuhusiwi kwa mtu kumfata Imamu katika swala kwa kupitia redio au televisioni, kwa kuwa swala ya jamaa inakusudiwa watu kukusanayika, ni lazima iwe sehemu moja, ziungane swafu baadhi kwa baaadhi, wala hairuhusiwi kuswali kufata redio au tv, kwa kuwa utakuwa haujapata makusudio, kama tukisema inafaa kuswali kwa kufata redio au television kila mmoja ata swali swala tano nyumbani kwakwe, na swala ya Ijumaa pia, nakufanya hivyo kunapingana na makusudio ya sheria ya kuswali jamaa na Ijumaa, kwa misingi hiyo haruhusiwi mwanamke au mtu mwengine kuswali akifata Imamu wa kwenye radio au televisioni.

****

<u>Bismillahi Al Rahmani Al Rahimu</u>.

Amesema Sheikh Mwenyezi Mungu amuhifadhi:

Ameuliza muulizaji

**Mgonjwa ataswali vipi?**

**Jibu:**

**1-Hali ya kwanza**: Ni lazima kwa mgonjwa kuswali faradhi akiwa amesimama, au ameinama, au ameegemea ukuta, au fimbo anayo hitaji kuegemea.

**2-Hali ya pili**: kama atakuwa hawezi kusimama ataswali akiwa amekaa, mkao mzuri akae amekunja miguu kwenye kusujudu na kurukuu.

**3-Hali ya tatu**: kama hato weza kuswali akiwa amekaa ataswali akiwa amelala ubavu amelekea kibla, na kuswali akiwa amelala ubavu wa kulia ni bora, kama haikuwezekana kuswali akiwa ameelekea kibla ataswali akiwa ameelekea sehemu yoyote na swala yake itakuwa sahihi, na hato irudia.

**4-Hali ya nne**: kama hato weza kuswali akiwa amelala ubavu ataswali amelala chali miguu yake imeeleka kibla, ni bora ainue kichwa chake kidogo ili aeleke kibla, kama hakuweza kuelekeza miguu yake kibla ataswali atakavyo kuwa, na hato irudia swala hiyo.

5-**Hali ya tano**: Ni lazima kwa mgonjwa arukuu na asujudu katika swala yake, kama hato weza atatumia kuwashiria kwa kichwa,na wakati wa kusujudu atainamisha kichwa zaidi kuliko kurukuu, akiweza kurukuu akashindwa kusujudu atarukuu , kwenye kusujudu atatumia kuwashiria, akiweza kusujudu akashindwa kurukuu atasujudi, ataashiria kwenye kurukuu.

6-**Hali ya sita**: kama hato weza kuwashiriya kwa kutumia kichwa katika kurukuu na kusujudu ataashiria kwa macho,atayafumba kidogo wakati wa kurukuu, atayafumba sana wakati wa kusujudu, kuhusu kuwashiria kwa kidole kama wa-

navyo fanya baadhi ya wagonjwa sio sahihi wala sifahamu kama kuna ushahidi kwenye Qur`ani na hadithi sahihi za Mtume, wala kauli za Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu.

**7-Hali ya saba**: Akiwa hawezi kuwashiria kwa kichwa wala kwa macho ataswali kwa moyo, ataleta takbira kwa myo kisha atasoma , atanuia kuruku, kusjudu, na kusimama , nakukaa kimoyo moyo, na mtu analipwa kwa alivyo nuwia.

**8-Hali ya nane**: Ni lazima kwa mgonjwa aswali kila swala kwa muda wake atafanya mambo ya lazima yanayo husu swala, ikiwa ni vigumu kwakwe kuswali kila swala katika muda wake anaruhusiwa kukusanya kati ya Adhuhuri na Alasiri, na kati ya Magharibi na Ishaa, au kukusanya kwa kuchelewesha anaichelewesha dhuhuri anaiswali na alasiri, magharibi anaiswali na isha, au anaitanguliza anaswali alasiri na adhuhuri na isha na magharibi ataswali kwa kuwangalia wepesi kwakwe, ama swala ya Al-fajir haikusanywi na swala iliyo kabla yake wala iliyo baada yake.

**9-Hali ya tisa**: Mgonjwa akiwa ni msafiri anatibiwa nje ya nchi yake au mji wake anaruhusiwa kupunguza swala ya rakaa nne ataswali Adhuhuri, Alasiri, Magharibi, Ishaa, ataziswala rakaa mbili mbili, mpaka atakapo rudi nchini kwakwe au katika mji wakwe muda ukiwa mrefu au mfupi.

****

**Swali la 311: Ni muda gani ambao ni lazima mtu kuswali ukiwa kwenye ndege? Na ni vipi mtu ataswali kwenye ndege swala ya Faradhi na swala ya Sunna?**

**Jibu:** Ni lazima kuswali ukiwa kwenye ndege muda wa swala ukiingia, lakini kama hatoweza kuswali kama anavyo swali akiwa aridhini asiswali swala ya faradhi akiwa kwenye ndege kama kunauwezekano wa ndege kushuka kabla ya muda wa swala kuisha, au kuisha muda ambao upo baada ya muda ambao anaruhusiwa kukusanya, mfano: kama ndege itaondoka jidah kabla ya kuzama jua, jua likazma naye akiwa angani hato swali magharibi mpaka ndege ishuke uwanajani, na ashuke kutoka kwenye ndege, akihofu kuwa muda wa magharigi utatoka atanuwiya kukusanaya kwa kuchelewesha kisha ataiswali magaharibi pamoja na swala ya al-ishaa atakapo shuka kwenye ndege, kama ndege itaendelea kuwa angani mpaka akahofia muda wa al-ishaa utatoka, na huwa ni nusu ya usiku ndio muda wa swala ya al-isha unaisha ataziswala zote mbili kabla ya muda kutoka akiwa kwenye ndege.

Namna ya kuswali faradhi ukiwa kwenye ndege atasimama akiwa amelekea kibla ataleta takibira, kisha atasoma Suratul Fatiha, ni Sunna kusoma kabla ya Suratul Fatiha dua ya ufunguzi wa swala, kisha atasoma baada ya Suratul Fatiha Sura nyingine, kisha atarukuu, kisha atainuka kutoka kwenye rukuu, kisha atasujudu kama hakuweza kusujudu atakaa, na atatumia kuwashiria kwenye kusujudu naye akiwa amekaa, atafanya hivyo mpaka amalize kuswali naye akiwa amelekea kibla.

Kuhusu kuswali Sunna ukiwa kwenye ndege ataswali aki-

wa amekaa kwenye kiti chake atatumia kuwashiria kwenye kusujud na kurukuu. Atainama sana kwenye kusujudu kulio kwenye kurukuu. Imehaririwa /22/4/1409/H.

****

**Swali la 312: Ni kipi kiwango cha masafa ya kupunguza swala? Je inaruhusiwa kukusanya bila kupunguza?**

**Jibu:** Umbali ambao unaruhusiwa kupunguza swala wameweka baadhi ya Wanachuoni ni umbali wa kilometa thamanini na tatu, wemeka baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu! Kuwa niumbali ambao watu husema kuwa hiyo ni safari hata kama haikufikia kilometa thamanini na tatu, na ambayo watu wanasema sio safari basi hiyo sio safari hata kama itafika kilometa mia moja.

Kauli hiyo ya mwisho ndio aliyoichagua Sheikhul Islamu Ibun Taymiya Mwenyezi Mungu amrehemu! [243/19/ Majmuu Al-Fatawa ] kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu hakuweka masafa malum ya kupunguza swala, pia Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakuweka masafa maalum. Amesema Anasi Ibun Maaliki radhi za Mwenyezi Mungu ziwe ju u yake**: ((Mtume alikuwa akitoka maili tatu au kilo meta sita anapunguza swala na anaswali rakaa mbili)),** [691 / Sahihi Muslim], kauli ya Sheikh Islamu Ibun Taymiya ndio kauli iliyo karibu na kupatia.

Hakuna ubaya kutofautiana ada ya watu, mtu anaweza kufata kauli ya kiwango cha masafa maalum ndio apunguze swala, kwa kuwa kauli hiyo wamesema baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, kwa kuwa jambo limedhibitiwa kurejea kwenda ada ndio kupatia.

**Je inaruhusiwa kukusanya itakapo ruhusiwa kupunguza?**

**Tunasema**: kukusanya hakufungamani na kupunguza, kukusanya kunafungamana na haja, mtu akiwa na haja ya kukusanya akiwa safari au asipo kuwa safari akusanye, kwa hivyo ndio maana watu wanakusanya swala mvua ikinyesha kama watu wataona tabu kurudi kuswali msikitini, pia watu wanakusanya kukiwa na baridi kali au upepo mkali watu wakiwa wanapata tabu kutoka kwenda msikitini pia anaruhusiwa kukusanya kama atahofia kupoteza mali yake au kupata madhara, nk.

Katika (Swahihi Muslimu) Imepokewa hadithi kwa Abdillahi Ibun Abasi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake! Amesema**: ((Alikusanya Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Kati ya magharibi na Al-ishaa, na kati ya adhuhuri na alasiri bila hofu wala mvua ))** [705/ Swahihi Muslimu]. Wakasema amekusudia nini? Akasema: amekusudia asiwape tabu Uma wake, asiwape tabu ya kukusanya swala.

Makusudio kila mtu akipata tabu anaruhusiwa kukusanya, kama atakuwa hana tabu asikusanye, lakini safari ni sehemu ya kupata tabu na dhiki kwa kuwacha kukusanya ,kwa misingi hiyo anaruhusiwa msafiri kukusanya akiwa amekula gadi kwenye safari au amekuwa mkazi, kama atakuwa amekula gadi katika

safari kukusanya ni bora, kama atakuwa amekuwa mkazi kuwacha kukusanya ni bora.

Imenyambuliwa kama mtu akiwa ni mkazi katika mji ambao unaswaliwa jamaa ni lazima kwa mtu huyo kuhudhuria jamaa, kwa hali hiyo hata punguza wala hata kusanya, lakini kama swala ya jamaa itampita atapunguza bila kukusanya, isipokuwa akihitaji kukusannya.

****

**Swali la 313: Mtu anaye safari kwenda Riyadhi kwa ajili ya masomo anakwenda jioni siku ya Ijumaa anarudi alasiri siku ya jumaa tatu, je anakuwa na hukumu ya msafiri katika swala na mambo mengine?**

**Jibu:** Huyo ni msafiri bila shaka, kwa kuwa mji anao kwenda kusoma sio mji anao ishi, pia hakunuwia kuishi katika mji anaoenda kusoma moja kwa moja, isipokuwa kuishi kwa kwe katika mji huo ni kwa malengo, lakini akiwa anaishi katika mji huo na kunaswaliwa jamaa, ni lazima anende akaswali jamaa, kuhusu yaliyo enea kwa baadhi ya watu kuwa msafiri haswali jamaa wala ijumaa, hayana asili wala ushahidi, kuswali jamaa ni waJibu kwa msafiri hata kama yupo vitani kama alivyo sema Mwenyezi Mungu**: [Na unapo kuwa pamoja nao ukawaswalisha basi kundi moja miongoni mwao wasimame pamoja nawewe],** **[**Surat Nisaa: 102]. Swala ya ijumaa ni waJibu kwa kila ataake sikia adhana, kwa kauli ya Mwenyezi Mungu**: [Enyi mlio amini**

**patakapo adhiniwa kwa ajili ya swala siku ya ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikir ya Mwenyezi Mungu]**. [Surtul Jumaa: 9], lakini swala ikikupita au ulikuwa upo mbali na msikiti, utaswali swala ya rakaa nne rakaa mbili.

****

**Swali la 314: Ni ipi hukumu ya kukusanya swala ya Alasiri katika swala ya Ijumaa? Je anaruhusiwa aliye njee ya mji kukusanya swala?**

**Jibu:** Haikusanywi swala ya alasiri na swala ya ijumaa, kwa kukosekana ushahidi kwenye Sunnah, haisihi kukisia ruhusa ya kukusanya adhuhuri kwa sababu kunautofauti mkubwa kati ya swala ya ijumaa na swala ya adhuhuri, asili kila swala inatakiwa iswaliwe katika muda wake isipokuwa kwa ushahidi unaoruhusu kukusanya.

Anaruhusiwa kukusanya aliye nje ya mji kama atakaa huko siku mbili au tatu kwa kuwa ni wasafiri, kama watakuwa kwenye vijiji vya karibu ambapo hauwezi kuwaita ni wasafiri hairuhusiwi kukusanya.

Naelezea hapa kukusanya adhuhuri na alasili, magharibi na Al-Ishaa, lakini haifai kukusanya swala ya Al-Jumaa na swala ya Alasiri hairuhusiwa kwa hali yoyote.

****

**Ujumbe:**

Sheikh Muhammadi Swalehe Uthaymini Mwenyezi Mungu mtukufu akuhifadhi.

Asalamu Alaykumu Warahmatul-Allah Wabarakatuhu.

Tumeona watu wamekuwa wanakusanya swala katika masiku yalio pita na tumeona watu wanafanya jambo la kukusanya swala ni jepesi, hivi kukusanya swala katika hali hii ya baridi inafaa? Mwenyezi Mungu awalipe thawabu.

**<u>Bismi LLahi Rahmani Rahim.</u>**

**Jibu:** Walaykum Salamu Warahmatul-Allah Wabarakatuh.

Sio ruhusa watu kufanya jambo la kukusanya swala kuwa ni jepesi, kwa kuwa mwenyezi Mungu Amesema: [**kwani haki-ka swala kwa waumini ni faradhi iliyo wekewa nyakati maalum**], [Surat Nisaa: 103]. Amesema Mwenyezi Mungu: **[Si-**

**mamisha swala jua linapo pinduka mpaka giza la usiku na Qur`ani ya al-fajir hakika Qur`ani ya al-fajir inashuhudiwa daima**]. [Suratul Israa: 78], ikiwa swala za faradhi zina nyakati zake hakika ni waJibu kuzitekeleza katika muda wake ulio pangwa kwa ajili ya swala hizo, kwa ujumla katika kauli ya Mwwenyezi Mungu**: [Simamisha swala jua linapo pinduka]** na Mtume rehma na amani ziwe juu yake amebainisha kwa kupambanua Akasema: **((Wakati wa adhuhuri jua linapo pinduka kikawa kivuli cha mtu mfano wake kwa urefu madamu haujaingia muda wa alasiri,na wakati wa alasiri nimpaka jua linapokuwa halijawa la njano, wakati wa magharibi ni muda ambao mawingu hayajazama, wakati wa al-ishai mpaka nusu ya usiku))** [612/ Sahihi Muslim].

Kwa kuwa Mtume amepanga nyakati kwa ufafanuzi hakika mtu kuswali wakati usio kuwa wake ni kuvunja mipaka ya Mwenyezi Mungu, **[Na watakao kiuka mipaka ya mwenyezi Mungu hao ndio madhalimu]**, [Suratul Baqarah: 229]. Atakaye swali kabla ya wakati akiwa anafahamu kwa makusudi mtu huyo anapata dhambi ni lazima kuirudia hiyo swala, kama atakuwa hafahamu hakukusudia hapati dhambi lakini ni lazima arudie, na hii inatokea kwa mtu aliye tanguliza kwa kukusanya bila sababu ya kisheria hakika swala alio itanguliza haisihi ni lazima airudie.

Na atakaye ichelewesha swala kwenye wakati wake akiwa anajua kwa makusudi bila udhuru mtu huyo anapata dhambi haikubaliwi swala yake kwa kauli iliyo na nguvu, jambo hili linapatikana kwa mtu anaye chelewesha swala bila sababu ya kisheria hakika swala iliyo cheleweshwa haikubaliwi kwa kauli iliyo na nguvu.

Ni wajibu kwa mwislamu amuogope Mwenyezi Mungu wala asione jambo hilo ni jepesi hakika jambo hilo ni kubwa sana na ni la hatari.

Kuhusu hadithi iliyo thibiti (Swahihu Muslimu) imepokewa kwa Ibun Abasi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: **((Kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, alikusanya kati ya swala ya Adhuhuri na Alasiri, na Magharibi na Ishaa,akiwa yupo Madina bila hofu wala mvua**)), [705/ Sahihi Muslim]. Hakuna ushahidi wakuzembea na kulifanya jambo hilo ni jepesi, kwa kuwa Ibun Abasi aliulizwa: kwanini alifanya vile? Wakikusudia Mtume? Akajibu Ibun Abasi: Alikusudia asiwape shida Umma wake)), [705/ Sahihi Muslim]. Huo ni ushahidi kuwa sababu inayo ruhusu kukusanya ni tabu inayo weza kumpa mtu kutekeleza swala katika wakati wake, mtu akipata shida kutekeleza swala katika muda wake inaruhusiwa kukusanya au ni Sunna kwakwe kukusanya, kama hakutakuwa na tabu ni lazima aswali katika muda wake kila swala.

Kwa misingi hiyo hairuhusiwi kukusanya kwa sababu ya biridi isipokuwa kama kutakuwa na baridi hiyo umekuja na upepo unawapa udhia watu kutoka kwenda msiktini, au baridi imekuja na theluji na barafu inawapa udhia watu .

Nasaha zangu kwa ndugu zangu Waislmu hasa maimamu wa misikiti wamche Mwenyezi Mungu katika jambo hilo, waombe msaada kwa Mwenyezi Mungu wa kutekeleza swala za faradhi kwa namna anayo iridhia Mwenyezi Mungu. Hayo ni maneno ya muandishi Muhammad Swaleh Uthaymini . /8 / 7 / 1413 / H.

****

**Swali la 315: Ni mambo gani yameruhusiwa katika safari?**

**Jibu:** Mambo yalio ruhusiwa safarini ni mambo manne:

**1-**Swala ya rakaa nne imeruhusiwa kuiswali rakaa mbili.

**2-**kula mchana wa mwezi wa Ramadhani, na kuzilipa siku hizo alizo kula baada ya Ramadhani.

**3-**kufuta juu ya viatu vya khofu kwa muda wa siku tatu usiku na mchana kuwanzia alivyo futa mara ya kwanza.

**4**-kuto swali swala za Sunnah za rawatibu za Dhuhur, Magharibi na Ishaa, ama swala ya Sunnah za rawatibu ya Alfajiri yenyewe inabaki na inaswaliwa vile vile na inapendekezwa kuiswali.

Msafiri anaswali swala za usiku, na Sunnah ya Alfajir, na rakaa mbili za dhuha na Sunnah baada ya kutawadha, na rakaa mbili za kuingia msikitini, rakaa mbili za kuwasili ukitoka safari, kwa kuwa ni sun`na mtu akitoka safari aanze kuingia msitini kabla ya kuingia nyumbani kwa kwe aswali rakaa mbili Msikitini [4418/ Sahihi Bukhary,/ 2769 / Sahihi Muslim] pia ibada zingine za swala za Sunna anatakiwa msafiri aziswali isipokuwa tulizo zitaja hapo nyuma nazo ni: sun`na zinazo swaliwa wakati wa faradhi ya adhuhuri na magharibi na Al-Ishai, kwa kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alikuwa haswali Sunna hizo akiwa safari.

****

**Swali la 316: Ni muda gani unanza saa ya kwanza siku ya Ijumaa?**

**Jibu:** Masaa alio yaeleza Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni masaa matano Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake**: ((Atakaye oga siku ya ijumaa kuoga kwa ajili ya janaba, kisha akaenda msikitni katika saa ya kwanza atakuwa kama ametoa ngamia, atakaye enda katika saa ya pili atakuwa sawa na aliye toa ng`mbe,atakaye enda katika saa ya tatu atakuwa kama ametoa kondoo atakaye enda katika saa ya nne atakuwa kama ametoa kuku atakaye enda katika saa ya tano atakuwa kama ametoa yai))** [881/ Sahihi Bukhary, / 850 / Sahihi Muslim] Mtume amegawa muda huo kuwanzia kuchomoza juu mpaka Imamu kuja msikitini ameugawa muda huo katika sehemu tano, inawezekana kugawa huko ni kwa saa moja moja muda ambao tunaufahamu, inaweza ikawa ni zaidi ya huo au ukawa ni muda chini ya saa moja, kwa kuwa nyakati zinabadilika, na masaa matano kuwanzia kuchomza jua mpaka kuja Imamu kwa ajili ya swala, wapo wanao sema muda huo unaanza baada ya kuchomza Al-fajir, lakini kauli ya kwanza ndio yenye nguvu, kwa kuwa kabla ya kuchomoza jua ni muda wa swala ya Alfajir.

****

**Swali la 317: Je inaruhusiwa mwislmu aswali nyumabni kwakwe swala ya ijumaa kama atakuwa anasikia sauti ya Imamu?**

**Jibu:** Hairuhusiwa kuswali swala ya ijumaa isipokuwa msikitini na waislamu wengine, lakini msikiti ukijaa swafu zikaungana mpaka barabarani sio vibaya kuswali barabarani kwa sababu ya dharura, kuhusu mtu kuswali nyumbani kwakwe au dukani kwake hairuhusiwi na sio halali kufanya hivyo, kwa kuwa makusudio ya swala ya ijumaa ni kukusanyika waisalmu kutoka kila sehemu wawe Umma mmoja kupatikane kuhurumiana na kufahamiana, na ipatikane elimu wasio jua wajifunze wanao jua wawafundishe wasio jua, kama tuta ruhusu kila mmoja tuka sema swali kupitia radio au swali ukiwa nyumbani ufate tu kipaza sauti kutakuwa hakuna faida ya kujenga misikiti na watu kuja kuswali misikitini hakuna faida, kwa kuwa kuswali majumbani kunapelekea kuwacha kuswali ijumaa na kuswali jamaa kama utafunguliwa mlango wa kuruhusu watu kuswalia nyumabni.

****

**Swali la 318: Je Mwanamke ataswali rakaa ngapi swala ya Ijumaa?**

**Jibu:** Mwanamke akiswali ijumaa na Imamu ataswali kama anavyo swali Imamu, kama ataswali nyumbani kwakwe ataswali Adhuhuri rakaa nne.

****

**Swali la 319: Atakaeswali Ijumaa ataswali na swala ya Adhuhuri?**

**Jibu:** Mtu akiswali swala ya Ijumaa hakika swala hiyo ya ijumaa ni lazima kwa muda huo, kwamana ni swala ya lazima ya wakati wa Adhuhuri- kwa hivyo hatoswali Adhuhuri, na kuswali Adhuhur baada ya kuswali Ijumaa ni katika uzushi, kwa kuwa hakufundishwa katika Qur`an wala mafunzo ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, ni lazima kuwakataza watu kuswali Adhuhuri baada ya Ijumaa, hata kama swala za Ijumaa zitaswaliwa nyingi, sio katika sheria mtu aswali adhuhuri baada ya swala ya Ijumaa, isipokuwa niuzushi unaotakiwa kukemewa, kwa kuwa Mwenyezi Mungu hakumlazimisha mtu mambo mawili ya wajibu katika wakati mmoja, isipokuwa amelazimishwa kuswali Ijumaa na mtu ameisha iswali.

Kuhusu walio sema kuwa ijumaa ziki swaliwa katika misikiti haifai, na ijumaa zikiwa nyingi ijumaa iliyo sahihi ni iliyo swaliwa katika msikiti wa mwanzo, na ikiwa hivyo Msikiti ulio tangulia kuswali Ijumaa utakuwa haujulikani kwa hivyo inapelekea kuwa swala za Ijumaa zote ni batili inabidi iswaliwe adhuhuri baada ya swala ya Ijumaa.

**Tunasema**: Ushahidi wa hayo mmeupata wapi? Uchambuzi huo mmeupata wapi? Je hoja yenu imejengewa juu ya mafunzo ya Mtume yalio sahihi na mtazamo sahihi?

**Jibu**: Hapana, isipokuwa tunasema : swala za ijumaa ziki swaliwa nyingi kwa haja ijumaa zote zilizo swaliwa ni sahihi, kwa akuli ya Mwenyezi Mungu**: [Basi mcheni Mwenyezi Mungu muezavyo]**, hivi mji ukipanuka ukawa mkubwa au msikiti ukawa hautoshii ijumaa zikawa nyingi kwa sababu ya haja watu hao wamemcha Mwenyezi Mungu kwa kadri ya uwezo wao, atakaye mcha Mwenyezi Mungu kwa kadri ya uwezo wake hakika atakuwa amefanya ambalo ni la waJibu kwakwe, vipi mtu aseme : ibada yake ni batili, na kuwa ni lazima alete badala ya ibada hiyo nayo ni swala ya adhuhuri badala ya swala ya ijumaa?!

Watu wakianzisha ijumaa nyingi katika maeneo tofauti bila haja yoyote hakuna shaka jambo hilo ni kunyume na mafunzo ya Mtume reham na amani ziwe juu yake, na ni kiyume na walivyo fanya makhalifa waongofu wanne, kufanya hivyo ni haramu kwa kauli ya Wanachuoni wengi Mwenyezi Mungu awarehemu, lakini pamoja na hivyo hatusemi: kuwa ibada yao sio sahihi, kwa sababu wanaohusika ni viongozi sio jambo linalo wahusu watu wote kwa kuwa viongozi ndio wanao toa idhini ya kuswaliwa ijumaa katika misikiti mingi bila haja, kwa hivyo tunasema: Nilazima kwa viongozi wanao simamiaa mambo ya Misikiti wasitoe idhini ya kuswaliwa Ijumaa katika misikiti mingi isipokuwa kukiwa na haja ya kufanya hivyo.

Kwa hivyo hakika sheria inamtazamo mkubwa kwenye kukusanyika watu katika ibada ili yapatikane mapezi na muungano na wajifunze wasio fahamu, na mambo mengi yasio kuwa hayo ambayo yanamasilahi makubwa na mengi, na mikusanyiko ya kisheria inakuwa katika wiki, au mwaka, au kila siku, kunakuwa katika mitaa Misikiti, kwa kuwa sheria kama ingewalazimisha watu wakusanyika kila siku sehemu moja jambo hilo linge kuwa na uzito kwa watu, kwa hivyo sheria imeweka wepesi imeweka kukusanyika kwa watu ni katika Misikiti yao, kila watu wa mtaa katika msikiti wao.

Mkusanyiko wa wiki ni siku ya Ijumaa, watu wanajikusanya kila wiki, kwa hivyo ndio maana ni Sunna swala ya Ijumaa iwe katika Msikiti mmoja na swala za Ijumaa zisiwe nyingi, kwa kuwa mkusanyiko wa wiki hauwadhuru wakikusanyika, na hauna tabu, na kuna masilahi makubwa, wanakusanyika watu nyuma ya Imamu mmoja khatwibu mmoja anatoa maelekezo kwa wote wanatawanyika wakiwa wamepewa mawaidha na mtu mmoja na wameswali pamoja.

Mkusanyiko wa mwaka ni mfano wa swala ya Idd huo ni mkusanyiko wa mwaka pia ni mkusanyiko wa nchi zote na miji yote, kwa hivyo haifai Misikiti ya kuswali swala za Idd iwe mingi isipokuwa kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo kama katika Misikiti ya Ijumaa.

****

**Swali la 320: Umefika muda wa swala ya Ijumaa na sisi tupo baharini tunafanya kazi, baada ya kuwadia muda wa adhana ya adhuhuri kwa nusu saa tukatoka baharini hivi inasihi na sisi tutoe adhana na tuswali Ijumaa?**

**Jibu:** Swala ya Ijumaa haisihi isipokuwa iswaliwe katika Misikiti ya kwenye miji na vitongoji, haisihi kwa kundi la watu wanao fanya kazi baharini au bara kuswali Ijumaa, kwa kuwa huo sio muongozo wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kuswali Ijumaa isipokuwa kwenye miji na vitongoji, hakika Mtume rehma na amani ziwe juu yake alikuwa anasafiri masiku mengi lakini alikuwa haswali Ijumaa, [1218/ Swahihi Muslim]. Nanyi sasa hivi mpo baharini hampo sehemu iliyo tulia, mnahama kuelekea kulia na kushoto na mnarudi katika miji yenu na mchi zenu jambo ambalo ni lazima kwenu ni kuswali adhuhuri na sio kuswali Ijumaa, pia mna ruhusa ya kupunguza swala ya rakaa nne mkaswali rakaa mbili.

****

**Swali la 321: Maamuma atafanyaje akifika Msikitini siku ya Ijumaa akimkuta Imamu yupo katika tahiyyatu ya mwisho, je atalipa rakaa nne au ataswali rakaa mbili?**

**Jibu:** Mtu akija siku ya Ijumaa akamkuta Imamu yupo kwenye tahiyatu ya mwisho mtu huyo swala ya ijumaa imempita, ataingia kuswali na Imamu lakini yeye ataswali Adhuhuri, kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake! **((Atakaye diriki raka katika swala basi amediriki swala))** [ 1580/ Sahihi Bukhary, /607/ Sahihi Muslim] kinacho fahamika kwenye hadithi hiyo atakaye diriki chini ya rakaa moja huyo haku diriki swala, pia imepokewa kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alisema: **(( Atakaye diriki rakaa moja katika swala ya ijumaa hakika ameidiriki**)) [557 / Al Nnasai ,/ 1123 / Ibun Majah], maana yake ameidiriki ijumaa akisimama akaswali rakaa ya pili.

****

**Swali la 322: Je Maamuma kuitikia aamin wakati Imamu anaomba dua baada ya khutba siku ya Ijumaa hivi ni uzushi?**

**Jibu:** Jambo hilo sio uzushi, kuitikia aamin wakati khatwibu anaomba dua kwenye khutba akianza kuwaombea waislamu ni vizuri kuitikia aamini wakati anaomba dua, lakini sio kwa sauti ya pamoja wala kwa sauti ya juu, inakuwa kila mmoja anaitikia peke yake na kw asauti ya chini, mpaka kusiwe na ushawishi, au sauti za juu, hakika huitikiwa aamin dua ya khatibu kwa siri na mtu mmoja mmoja .

****

**Swali la 323: Ni ipi hukumu ya kuinua mikono na Imamu anakhutubu siku ya Ijumaa?**

**Jibu**: Kuinua mikono na Imamu anakhutubu siku ya Ijumaa jambo hilo sio la kisheria, hakika walikemea maswahaba radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao kumkemea Bishri Ibun Marwani wakati alipo inua mikono yake katika khutba ya Ijumaa, [874 / Sahihi mslim] Lakini linanyambuliwa katika jambo hilo kuomba dua ya mvua hakika imethibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa aliinua mikono akimuomba Mwenyezi Mungu mvua na Mtume alikuwa kwenye khutuba ya ijumaa, watu wakainua mikoo yao pamoja na Mtume, [1029 / Sahihi Bukhary], kinyume na dua ya kuomba mvua haitakiwi kuinua mikono wakati wa dua kwenye khutba ya Ijumaa .

****

**Swali la 324: Ni ipi hukumu ya khutuba kwa lugha isio kuwa ya kiarabu?**

**Jibu:** Kauli iliyo sahihi katika mambo haya: Haifai kwa anaye hutubu siku ya ijumaa kuwahutubia watu kwa lugha wasio ifahamu watu walio hudhuria, kama watu hao sio waarabu wala hawafahamu lugha ya kiarabu atawahutubia kwa lugha yao kwa

kuwa kufanya hivyo ndio njia ya kuwafundisha, na makusudio ya khutuba nikufundisha watu sheria ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake na kuwapa mawaidha na kuwaelekeza anayo yataka Mwenyezi Mungu na Mtume wake, isipokuwa kama atasoma aya ya Qur`an ni lazima aisome kwa lugha ya kiarabu, kisha aitafsiri kwa lugha ya watu anao ongea nao, ushahidi kuwa anaye hutubia anatakiwa kuhutubia watu kwa lugha ya watu anao ongea nao ni kauli ya Mwenyezi Mungu! **[Na hatukumtuma Mtume isipokuwa kwa ulimi ( lugha) wa kaumi yake ili apate kuwabainishia]**, [Suratu Ibrahimu: 4]. Mwenyezi Mungu amebainisha kuwa njia ya kubainisha inakuwa kwa lugha ambayo wanaifahamu anao ongea nao.

****

**Swali la 325: Kuoga siku ya Ijumaa na kujipamaba kwa ajili ya siku hiyo ni kwa wanaume na wanawake? Ni ipi hukumu ya kuoga kabla ya Ijumaa kwa siku moja au siku mbili?**

**Jibu:** Hukumu hizi ni maalumu kwa wanaume kwa kuwa ndio wanao hudhuria swala ya Ijumaa, mwanaume ndio anatakiwa kujipamba siku ya Ijumaa akitaka kutoka kwenda Msikitini, kuhusu wanawake sio sheria wao kujipamaba katika jambo hilo, lakini kila biaadamu anatakiwa akiwa na uchafu kwenye mwili wake ajisafishe, kufanya hivyo ni jambo linalo sifiwa hatakiwi mtu kuwacha usafi.

Mtu kuoga kabla ya Ijumaa kwa siku moja au siku mbili haisaidii, kwa kuwa hadithi iliyo pokelewa katika jambo hilo inahusu siku ya Ijumaa, na muda wa kuoga ni kuwanzia kuchomoza Al-fajir mpaka kuswali Ijumaa, muda huo ndio wakuoga ambao unatakiwa mtu aoge, ama mtu kuoga kabla ya ijumaa kwa siku mbili haitoshi juu ya kuoga siku ya Ijumaa.

****

**Swali la 326: Mtu akingia Msikitini siku ya Ijumaa na muadhini anatoa adhana ya pili je ataswali tahiyatul Masjidi au atamfata muadhini kwa kujibu Adhana?**

**Jibu:** Wameleza baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu! Kuwa mtu akiingia msikitini siku ya ijumaa akasikia muadhini anatoa adhana ya pili ataswali tahiyatu Al-masjidi wala hato mfata muadhin kwenye adhana kwa kumjibu, atafanya hivyo ili apate muda wakumsikiliza khutuba, kwa kuwa kusikiliza khutuba ni lazima, na kujibu muadhini ni Sunna haiwezi kuziwia wajibu.

****

**Swali la 327: Ni yapi mawazo yenu kwa anaekata swafu na kuvuka kwenda mbele siku ya Ijumaa ?**

**JIBU:** Ni lazima kuwambia wanaopita kwenye swafu wakae chini lakini unawambia bila kuongea, unamvuta nguo au unamuashiria akae, iliyo bora jambo hilo alisimamie khatwibu mwenyewe kama alivyo kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake anafanya akimuona mtu anakata swafu na kuvuka kwenda mbele huku Mtume anahutubia siku ya ijumaa **Anasema: ((kaa chini hakika umewaudhi watu))** [1115/ Ibun Majah,/ 188/4 / Imamu Ahmadi] .

****

**Swali la 328: Ni ipi hukumu ya kumsalimia mtu na Imamu anahutubu, na ni ipi hukumu ya kurudisha salamu kwa aliye salimiwa?**

**Jibu:** Mtu akienda msikitni na Imamu anahutubia ataswali rakaa mbili nyepesi atakaa wala asimsalimie mtu yeyote, kumsalimia mtu hatika hali hiyo ni haramu kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema**: ((Ukisema kumwambia mwenzio: kaa kimya siku ya Ijumaa na Imamu anahutubu hakika umefanya mchezo))**, [934/ Sahihi Bukhary, /851/ Sahihi Muslim] Pia Amesema: **((Atakaye gusa gogoto hakika**

**amecheza )),** [857/ Swahihi Muslim]. Maana ya kucheza ni mtu kufanya jambo la upuuzi, na huenda jambo la upuzi alio lifanya litasababisha akose malipo ya ijumaa, kwa hivyo imethibiti katika hadithi: **((Atakaye cheza hana swala ya Ijumaa))**, [93/1/ Ahmadi,/ 1051/ Abuu Daud ].

Mtu akikusalimia kwa matamshi,usiseme kumjibu: Walaykum salamu, hata kama atasema kwa kutamka, kuhusu kukupa mkono hakuna ubaya, lakini ni bora kuto kukupa mkono, pamoja ya kuwa baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu! Wamesema: Anaruhusiwa kujibu salamu.

Lakini kauli sahihi: Hatakiwi kujibu salamu, kwa kuwa ni lazima kusikiliza hutuba unatangulizwa kuliko ulazima wa kujibu salamu, pia mwislamu katika hali hiyo hana haki ya kusalimia, kwa kuwa kusalimia kutawashughulisha watu kuto sikiliza mambo ambayo ni lazima kuyasikiliza.

**Sahihi:** Hato mjibu salamu wala hatakiwi kuanza kumsalimia mtu na Imamu anahutubu.

****

**Swali la 329: Ni ipi hukumu ya kupeana pongezi katika sikukuu ya Iddi? Je kuna maneno maalum ya kupeana pongezi ya iddi?**

**Jibu:** kupeana pongezi ya sikuku ya Iddi inaruhusiwa, na hakuna maneno maalum ya kupeana pongezi ya Iddi, isi-

pokuwa walivyo zowea watu kupeana pongezi inaruhusiwa, ila isiwe kwa lugha na vitendo vya madhambi hivyo haviruhusiwi.

****

**Swali la 330: Ni ipi hukumu ya swala ya Iddi?**

**Jibu:** Nionavyo mimi kuwa swala ya Iddi ni nguzo ya lazima, na hairuhusiwi kwa wanaume kuwacha kuiswali, isipokuwa ni lazima wahudhurie kuswali swala hiyo, kwa kuwa Mtume rehma na amani aliamrisha watu kuhudhuria kuiswali, isipokuwa ali waamur hata wanawake watumwa walio huru watoke kwenda kwenye swala ya Iddi, pia aliwaamuru wanawake walio katika hedhi watoke waende katika swala ya Iddi, lakini wajitenge na sehemu ya kuswalia, hii inatujulisha umuhimu wa swala ya Iddi, na hi ndio kauli niliyo isema : kuwa ndio yenye nguvu- na ndio kauli alio ichagua Sheikh Islamu Ibun Taymiya Mwenyezi Mungu amrehemu ! [ 183/24 / Majmuu fatawaa].

Lakini swala ya Iddi ni kama swala ya ijumaa ikikupita hailipwi kwa sababu hakuna ushahidi wa ulazima wa kuilipa, wala mtu hato swali, swala nyingine badala ya swala hiyo, kwa kuwa swala ya Ijumaa ikimpita mtu ni lazima aswali Adhuhuri kwa kuwa swala ya Ijumaa inaswaliwa katika wakati wa adhuhuri, kuhusu swala ya Iddi ikikupita hailipwi.

Nasaha zangu kwa ndugu zangu waislamu wamche Mwenyezi Mungu mtukufu, waende kuswali swala hii ambayo ime-

jaa kheri na dua, na watu kuonana, na kuungana waisalamu wote na kupendana, kama watu wataitwa kwenye jambo la starehe utawaona wanakwenda haraka, vipi watu wanakuwa wazito kwenda kuswali Iddi na aliye waita kwenda kuswali ni Mtume rehma na amani ziwe juu yake amewaita katika swala ambayo mtu anapata malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu wanapewa wanacho stahiki alicho waahidi mwenyezi Mungu, lakini ni lazima kwa wanawake wakitoka kwenda wajitenge na sehemu ya wanaume, wawe pembezoni mwa msikiti mbali na wanaume, wasitoke wakiwa wamejipamba na kupaka manukato, au hawakuvaa nguo za sitara, kwa saababu hiyo Mtume alipo amuru wanawake watoke kwenda kuswali Iddi walimuliza: Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu kama mmoja wetu hana jilbabi, Akasema: **((Amvalishe dada jilbabi lake))** [324/ Sahihi Bukhary, /890/ Sahihi Muslim] na jilbabi ni nguo inayo mfunika mwanamke au nguo inayo fanana na baibui, kwa hivyo inatujulisha kuwa ni lazima mwanamke atoke nyumbani akiwa amevaa jilbabi, kwa kuwa Mtume alivyo ulizwa mwanamke atoke na jilbabi hakusema atoke amevaa anavyo weza isipokuwa alisema: **((Amvalishe dada jilbabi lake)),** inatakiwa Imamu, nakusudia Imamu wa swala ya Iddi – Atakapo wahutubia wanaume awahutubie na wanawake kama wanawake watakuwa hawakusikia hutuba wakati anawahutubia wanaume, Lakini kama wanasikia hutuba ya wanaumee inatosha hakuna haja ya kuwahutubia na wanawake, lakini ni bora hutuba iwe na sehemu ya kuelezea hukumu maalum za wanawake na awape mawaidha wanawake na awakumbushe, kama alivyo

fanya Mtume rehma na amani ziwe juu yake! wakati alipo wahutubia wanaume katika swala ya Iddi kisha akawageukia wanawake akawapa mawaidha na akawakubusha, [979/ Sahihi Bukhary, /884/ Sahihi Muslim].

****

**Swali la 331: Ni ipi hukumu ya kuswali swala ya Iddi sehemu nyingi katika mji?**

**Jibu:** Kukiwa na haja ya watu kuswali katika sehemu nyingi hakuna ubaya, kama vile swala ya ijumaa kukiwa na haja ziswaliwe sehemu nyingi hakuna ubaya, kwa kuwa Mwenyezi Mungu Amesema: **[Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika dini],** [Suratul Hajj: 78]. Kama hatukusema inaruhusiwa watu kuswali katika sehemu tofauti tofaut ni lazima jambo hili litawanyima baadhi ya watu kuswali Al Jumaa na swala ya Iddi.

**Mfano:** Haja ya watu kuswali Iddi sehemu tofauti ni kupanuka mji watu wengine wanakuja kutoka nje ya mji kwenda upande wa mji sehemu ya pili.

Kama kutakuwa hakuna haja itaswaliwa sehemu moja tu.

****

**Swali la 332: Ni ipi namna ya kuswali swala za iddi mbili?**

**Jibu:** Namna ya kuswali swala za Iddi mbili ni kuja Imamu anawaswalisha watu rakaa mbili ataleta takbira ya kuhirimi swala katika rakaa ya kwanza, kisha ataleta baada ya takbira ya kuhirimia takbira sita, kisha atasoma Suratul Fatiha, na anatasoma Surat Qaf, katika rakaa ya pili akisimama atasimama akiwa analeta takbira akifika kwenye kusimama ataleta takbira mara tano, kisha atasoma Surat Suratul Fatiha kisha atasoma Suratul Qamar, hizi Sura mbili Mtume alikuwa anazisoma katika swala za Iddi mbili [891/ Swahihi Muslim], Akipenda atasoma katika rakaa ya kwanza sabhi, na rakaa ya pili hal-ataaka hadithu Al-Ghashiya [878/ Sahihi Muslim], Fahamu swala ya Iddi na ya al-ijumaa zinazo shirikiana katika swala sura mbili na zinapishana sura mbili, sura mbili ambazo zinashirikiana ni sabhi na Al-ghashiya, sura zinazo pishana katika swala hizo katika swala za Iddi mbili ni (Qaaf) na (Iqtarabat) katika swala ya Ijumaa unasoma Surat (Al-Jumua) na (Al-Munaafiquun) anatakiwa Imamu kufata Sunna kwa kusoma sura hizi mpaka waisalamu wazimfahamu wala wasimkemee kama itatokea, baada ya swala atahutubia, inatakiwa aungumzie kwenye sehemu ya hutuba yake jambo linalo wahusu wanawake awaamuru kufanya wanayo takiwa kufanya wanawake na awakataze mambo yasiyofaa inatakiwa khatibu afanye kama alivyo fanya Mtume rehma na amani ziwe juu yake.

****

**Swali la 333: Anasimama Imamu katika baadhi ya Miji siku ya Iddi kabla ya swala akileta takbira kwa kutumia kipaza sauti na Maamuma nao wanaleta takbira pamoja na Imamu, ni ipi hukumu ya kufanya hivyo?**

**Jibu:** Sifa alizo zitaja muulizaji kwenye swali lake sifa hizo hazikuthibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, wala kwa maswahaba radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao Sunna iliyo thibiti kila mmoja alete takbira peke yake.

****

**Swali la 334: Ni muda gani watu wanatakiwa kuwanza kuleta takbira za siku ya Iddi ? na ni zipi sifa zake?**

**Jibu:** Takbira za siku ya Iddi zinaanza kuwanzia kuzama jua siku ya mwisho ya Ramadhani mpaka atakapo kuja Imamu kwa ajili ya swala ya Iddi.

Sifa zake ni kusema: Allahu Akbar, Allahu Akbar, La Ilaaha ila Allah: Allahu Akbar, Allahu Akbar, WaliLLahi Al-hamdu. Au atasema: Allahu Akbar, Allahu Akbar: Allahu Akbar, La Ilaaha ila Allah: Allahu Akbar, Allahu Akbar, Allahu Akbar, WaliLLahil-hamdu.

Nakusudia ima alete takbira mara tatu au mara mbili vyote inaruhusiwa, lakini ni lazima katika alama hizo wanaume wata

dhihirisha takbra katika masoko na misikiti na majumbani, kuhusu wanawake ni bora kuleta takbra kwa siri siri.

****

**Swali la 335: Ni ipi hukumu ya swala ya kupatwa kwa mwezi na ni ipi swala ya kupatwa kwa jua?**

**Jibu:** Kuswali kwa ajili ya kupatwa kwa jua au mwezi ni sun`na iliyo tiliwa mkazo kwa mujibu wa muungano wa Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu na sio wajibu kuswali jua au mwenzi vikipatwa, hakuna shaka kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake ameamrisha watu kuswali jua au mwezi likipatwa, na Mtume aliswali na hiyo swala ni kubwa na tukufu ipo nje ya mtazamo wake,

Wamesema baadhi ya Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu kuwa ni lazima kuswali, wakesema kuwa itakuwa ni lazima kwa kila mtu au ni lazima kwa baadhi ya watu kwa maana wakiswali baadhi inatosha, wakatoa ushahidi wa amri ya Mtume kaamrisha watu wa swali [1044/ Sahihi Bukhary, /901/ Sahihi Muslim], Asili ya amri ni lazima ifanyike, pia amri imekutana na dhamiri inayo julisha umuhumu wa jambo hilo, kwa kuwa ni onyo kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa adhabu inayo inayo fungamana na sababu, kwa hivyo imekuwa ni wajibu kwa wajawanyeyekevu kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya hiyo adhabu ambayo imefungamana na sababu na Mwenyezi Mungu ameikemea watu waiache.

Hakuna shaka kuwa ushahidi huo unanguvu sana kwa mtazamo na ushahidi wa matendo ya watu wema walio tangulia, kwa kifupi itakuwa kuswali jua au mwezi vikipatwa ni faradhi kifaya, ambayo wakiswali baadhi ya watu inatosha kwa wengine, na hivi ndio mimi ninavyo ona lipo kwenye hukumu ya jambo hilo kuwa niya faradhi kifaya, lakini kauli ya mungano wa Wanachuoni, hawana ushahidi unao pelekea kuwa ni lazima kuswali isipokuwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Kumwambia mwanaume mmoja alipo muliza hivi kunaibada nyingine ya lazima kuwacha swala tano? Akasema Mtume**: ((Hapana, isipokuwa uswali Sunna)).** [47/ Sahihi Bukhary, /11/ Sahihi Muslim].

Kauli hiyo haikatazi kuwa hakuna swala nyingine ya lazima isipokuwa swala tano itakapo patikna sababu ya swala hiyo kuwa ni wajibu, inakuwa makusudio ya kukataa katika kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Hapana**)) kwa maana ya swala zilizo ratibiwa ambazo zinajirudia usiku na mchana.

Mchana na usiku, na ama swala zenye sababu maalumu; hadith hii haijapinga uwajibu wa swala hizo. Hitimisho la swali hili ni kwamba: swala ya kupatwa kwa jua ni waaJibu; ima kwa watu wote au kwa kufanya baadhi yao .

****

**Swali la 336: Ambaye imempita swala ya kupatwa kwa mwezi vipi anailipaje**

Jibu: mwenye kupitwa na swala ya kupatwa kwa mwezi au kushikwa kwa mwezi imethibiti kwa mtume rehema na amani ziwe juu yake kwamba yeye amesema: ((M**takapo sikia iqama iendeeni swala na jilazimisheni kuiyendea kwa utulivu na upole, wala msikimbie, sehemu mtakayo iwahi swalini na iliyo wapita itimizeni**)), Sahihi Bukhaar [636], na pia Sahihi Muslim [602]. Basi huyu ambae imempita rakaa katika swala ya kupatwa kwa mwezi na aitimize hiyo rakaa kwa namna aliyo iswali imamu au kama alivyo iswali imamu, kwa sababu mtume aliposema timizeni amekusudia swala zote hakutaja swala maalum. Na swali hili huwatatiza watu wengi, kuwa kama amepitwa na rukuu ya kwanza katika rakaa? analipa rakaa ambayo imempita yeye rukuu ya kwanza yote .

****

**Swali la 337: kugeuza kilemba katika dua baada ya swala ya kuomba mvua, je hugeuzwa wakati wa kuomba au hugeuzwa nyumbani kabla ya kutoka kwenda msikitini? na ni ipi hekma ya kugeuza kilelemba? nifahamisheni Allaah awabariki.**

**Jibu:** kugeuza kilemba wakati wa dua katika swala ya kuomba mvua, anaegeuza kilemba ni khatwibu anae khutubia waumini tu, kama walivyo sema wana wa chuoni Allah awarehemu. Na hikma katika hilo hupatikana faida tatu:

**Faida ya kwanza:** ni kumfuata na kumuiga Mtume rehema na amani ziwe juu yake.

**Faida ya pili**: kuwa na utulivu juu ya Allah kwamba hali itabadilika kutoka kwenye ukame na kuingia kwenye mavuno na starehe.

Faida ya tatu: ni ishara ya mtu kugeuza hali yake aliyo kuwa nayo ya kutokumuelekea Allaah na kumuasi, na kubadilika kwa kumuelekea Allaah na kudumu katika kumtii, kwa sababu ucha-Mungu huwa na maana ya vazi, na kilemba na mfano wake ni vazi, nikana kwamba amegeuka kutoka kwenye ubaya na kuwa mwema.

****

**Swali la 338: baadhi ya watu wanasema: lau msinge taka msaada kwa kuomba mvua inge nyesha tu, mnasemaje katika hili?.**

**Jibu:** mimi nasema: na ogopea kwa msemaji huyo khatari kubwa, hakika Allaah anasema: [**Amesema bwana wenu niomb-**

**eni nitawajibu**] [Surat Ghaafir: 60], Allaah ni mwenye kuhukumu na huenda akachelewesha malipo yake ili watu wafahamu ugumu wa ufakiri, na wafahamu kuwa hapana pakurejea isipo kuwa kwa Allaah, na anafanya maombi yao kuwa ni sababu ya kunyesha mvua, na pindi watakapo omba watu na isinyeshe mvua, basi Allah katika hilo kuna hekma kaiweka, hakika Allah ni mjuzi na nimwenye hekma sana na nimwenye huruma kwa waja wake na nafsi zao, kwani ni vitu vingi mtu anaviomba wala havipati, kisha anaomba hapati, kisha anaomba hapati, na amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Hujibiwa mmoja wenu muda wa kuwa hajafanya haraka; anasema: nimeomba sija jibiwa**)). Bukhaar [6340 ]; na pia ameipokea, Muslimu: [2735]. Na muda huo muombaji anaendelea na kuomba Dua - Allah atuhifadhi na kukata tama – pamoja na kwamba mtu hamuombi Allah kwa neno lolote isipo kuwa anapata thawabu kwa kuomba huko; kwa sababu Dua ni ibada, kwa hiyo mtu yoyote anae omba hupata faida kwa vile yuko ndani ya ibada, bali pia imekuja katika hadidh kutoka kwa mtume rehema na amani ziwe juu yake ya kwamba: ((**Mwenye kuomba hupata moja ya mambo matatu; ima ajibiwe, au angeuziwe kwenye jambo baya kubwa zaidi, na ima awekewe alicho kiomba mpaka siku ya kiama**)). [Imamu Ahmad [329 / 5], na tirmidhy: [3573 ]. Na mimi nazielekeza nasaha zangu kwa ndugu aliye sema maneno yale kwamba atubie kwa Allah, hakika alicho kisema ni dhambi kubwa inayo pingana na amri ya Allah mtukufu na ni maneno yenye kumghadhibisha Allah mtukufu.

****

**Swali la 339: Ni ipi rai yenu kwa mtu anayeusia kuwa akifa azikwe mahali Fulani, je ina paswa kutekeleza wasia huo?.**

**Jibu:** kwanza hapana budi kuulizwa kwanini achague sehemu hiyo? Huenda ikawa amechagua upande wa makaburi ya mawalii wa uwongo au upande wa makaburi ambayo anashirikishwa Allah mtukufu, au sababu nyinginezo zisizo kuwa hizo miongoni mwa sababu zilizo haramishwa, ikiwa ni kwa sababu hizo haipaswi kutekelezwa wasia wake, na atazikwa pamoja na waislam wengine ikiwa ni muislam .

Ikiwa kausia pasi na malengo hayo, bali kausia apelekwe kwenye mji wake aliyo ishi kwa hili hapana tatizo ukitekelezwa wasia wake ikiwa hakutatokea uharibifu wa mali, ikiwa hilo lita haribu mali kwamba hasafirishwi ila kwa kutumia pesa nyingi, kwa hapo hautekelezwi wasia wake na Ardhi ya Allaah ni moja, muda wakua Ardhi ni ya waislam .

****

**Swali la 340: Ni wakati gani inatakiwa kusomwa talakini?**

Jibu: Talakini husomwa wakati mtu anapo kufa na anapo karibia kufa , anafanyiwa talakini anae karibia kufa kwa kuambiwa aseme :

((**Laa Ilaaha ila LLah**)), kama alivyo fanya Mtume rehema na amani ziwe juu yake wakati alipo kufa baba yake mdogo Abii twaalib wakati anakaribia kufa akamuambia (Ewe baba mdogo, sema: ((**Laa Ilaaha ila LLah, tamko ambalo litakuwa ni hoja kwako mbele ya Allah**)) lakini Ami yake Abaa Twaalib -- Allah atulinde – hakusema hili na akafa katika shirki. Sahihi Bukhaary: (1360) na pia Muslim katika mlango dalili ya kuswihi uislamu wa mwenye kukaribia kufa.

Na ama talakini baada ya kufa hakika ni bidaa niuzushi kwa kuto thibiti hadith kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika hilo, lakini ambalo linapaswa kufanywa ni hadith aliyo ipokea Abuu daaud pindi alipo sema alikuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake akimaliza kumzika maiti husimama pembezoni mwa kaburi yake na kusema ((**Mtakieni msamaha ndugu yenu na mumuombee apate kauli thaabit kwani hakika yeye sasa hivi anaulizwa**)) Sahihi Bukhaar (1223) ama kusoma mbele ya kaburi au kufanya talakini katika kaburi hii ni bidaa imezuka haina asili kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake.

****

**Swali la 341: Ni ipi rai yenu kwa mtu ambae anach-elewesha kumzika maiti mpaka wafike au waje baadh ya ndugu waliyoko miji ya  mbali?.**

Jibu: Ambalo ni Sahihi katika sharia ya kiislamu ni kufanya haraka kumuandaa maiti na kumzika, kwa maneno ya mtume (rehema na amani ziwe juu yake  amesema: ((**Fanyeni haraka kumzika maiti, ikiwa ni miongoni mwa watu wema basi kuna kheri mnayo mharakishia aipate, na akiwa si katika wema basi ni shari mnayo jiwekea kwenye dhima yenu**)). Sahihi Bukhaar: (1315) na pia Sahihi Muslim (944). Wala haitakikani kuchelew-eshwa maiti kwa ajili ya kufika baadhi ya jamaa zake , isipokua ikitokea kucheleweshwa basi iwe muda mchache tu, lakini litaki-kanalo ni kufanyiwa haraka ndiyo bora zaidi, watakapo kuja hao jamaa wanaweza wakamswali katika kaburi lake  kama alivyo fan-ya Mtume rehma na amani iwe juu yake wakati alipo swali katika kaburi la mwanamke, mwanamke ambae alikuwa akishuhulikia msikiti, maswahaba walimzika na hawakumpa khabari  Mtume, akasema Mtume: ((N**ionyesheni kaburi lake**)) wakamfahamisha lilipo akamswalia.  Sahihi Bukhaar: (1337).

****

**Swali la 342: Kutangaza khabari za kifo kwa watu wake wa karibu na marafiki zake ili wakusanyike kwa ajili ya kumswalia maiti, je hili linaingia katika matangazo yaliyo katazwa kisheria au hii inafaa?.**

JIBU: Hili ni katika matangazo yanayofaa, na hili alitangaza Mtume rehema na amani ziwe juu yake: siku alipo kufa Najashi, na vile vile akasema Mtume kuhusu yule mwanamke alie kuwa akisimamia shukhuli za msikiti, walipo mzika maswahaba radh za Allah ziwe juu yao bila kumfahamisha Mtumerehema na amani ziwe juu yake, akasema Mtume: ((**Kwanini hamkunifahamisha**)) kwa hiyo kueneza khabari za kufa mtu kwa ajili ya kipatikana watu wengi watakao mswalia hapana vibaya kwa hilo; kwa kuwa hilo ni katika mambo ambayo yamepokewa na yana mifano katika Sunna, na hivyo hivyo kutoa khabari kwa jamaa zake wakaribu ni muhimu wakakusanyika kwa ajili ya kumswalia hapana tatizo.

****

**Swali la 343: Ni namna ipi ya sawasawa iliyo pokelewa kutoka kwa Mtume ikibainisha jinsi ya kuosha maiti?**

Jibu: Namna ya kisheria katika kuosha maiti ni kwamba mtu anaosha tupu ya maiti, kisha anafuatishia kumuosha mwili, ataanza na viungo vya udhu atamtia udhu isipokuwa asimuingizie maji

mdomoni kwake au puani, isipokuwa anachukua kitambaa anakiloanisha maji kisha anamsafisha puani na mdomoni kwa hicho kitambaa, kisha anaosha sehemu nyingine za mwili , na kumuosha ina kuwa ni kwakutumia sidiri

(**mkunaz**i ) na mkunazi ni maarufu – unachukuliwa majani yake kisha yanatwangwa halafu yanaingizwa katika maji kisha yana changanywa kwa mkono mpaka lina patikana povu, hala linachukuliwa povu anaoshwa nalo maiti kichwani na kwenye ndevu, na ataogeshwa sehemu nyingine na sidri iliyo baki, kwa kuwa sidri ina takasha sana, na josho la mwisho wanachanganya na kaafuur (**karafuu maiti**), na kaafuur ni manukato maarufu, wamesema wana wa chuoni Allah awarehemu : miongoni mwa faida za kaafuuri nikwamba hukausha mwili na inafukuza vidudu visimkaribie maiti .

Na ikiwa maiti ana uchafu mwingi, basi huoshwa zaidi ya mara moja; kwa neno la Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema kuwaambia wanawake ambao wana waogesha mabinti zao:

((**Muogesheni mara tatu, au mara tano, au zaidi ya mara hizo kama mtaona bado anastahili kuogeshwa**)) Sahihi Bukhaar (1253), na pia Sahihi Muslim (939). Kisha baada ya kumuogesha wanamkausha maji au kumfuta maji kisha anavishwa sanda yake.

****

**Swali la 344: Wakati mwingine katika ajali za magari na moto na kuvunjika yani kama kudondokewa na nyumba mtu huharibika au kupoteza baadhi ya viungo, na wakati mwingine kunapatikana vipande vidogo kama kipande cha mkono au kichwa, je ni sharia kuswalia viungo hivi? na je vinaoshwa?.**

Jibu: Viungo vyepesi kama vile mkono na mguu vitakapo kutwa au kuonekana na yule maiti mwenyewe ashaswaliwa basi havita swaliwa, mfano: lau tumemswalia maiti na tukamzika lakini hana mguu, kisha baadae tukaupata mguu wake basi tunauzika tu wala hatuuswalii kwakuwa maiti mwenyewe tushamswalia.

Ama itakapokuwa maiti hajapatikana yeye mwenyewe, isipokua kumepatikana kiungo chake chochote katika viungo vyake kama kichwa chake, au mguu wake, au mkono wake, basi viungo hivyo vilivyo patikana vinaoshwa na kuvishwa sanda kisha vina swaliwa baada ya hapo vinazikwa .

****

**Swali la 345: Mwanamke mimba yake imaharibika ikiwa na muda wa miezi sita, na alikua mwanamke huyo akifanya kazi ngumu na alikuwa akifunga ramadhani, na yeye huyo mwanamke ana shaka ya kuwa kufa kwa kiumbe alichokuwa amebeba tumbo na kikashindikana kuzaliwa salam ni kwa sababu ya zile kazi ngumu alizo-kuwa akifanya, pamoja na hilo nikwamba kiumbe hicho kimezikwa bila ya kuswaliwa, niipi hukmu ya kuacha kuswaliwa kiumbe hicho? na huyu mwanamke afanyeje ili aondoe shaka hii ya kudhani yeye ndiyo sababu ya kufa na kuharibika mimba? nifahamisheni .**

Jibu: Mimba ikiharibika na ishafikia miezi mine, basi kiumbe hicho kina paswa kuoshwa, na kuvishwa sanda, na kuswaliwa; kwa kuwa mimba ikifikisha miezi minne tiyari kiumbe kisha puz-iwa roho, kama inavyo fahamisha juu ya hilo hadith ya Abdallaah ibin Masuudi amesema: alituambia Mtume rehma na amani ziwe juu yake na yeye ni mwenye kusema ukweli mwenye kuamini-wa: Hakika mmoja wenu hukusanywa umbo lake katika tumbo la mama yake siku arubaini nakuwa ni tone la manii, kisha baada ya siku arubaini huwa pande la damu , kisha baada ya siku arubaini anakuwa pande la nyama, kisha hupelekwa malaika akalipuzia roho, (M**paka mwisho wa hadith**), Sahihi Bukhary: (3208), na pi Sahihi Muslim: 2643. hizi ni siku mia moja na ishirini: yani miezi minne, kwa hiyo ikiharibika au ikazaliwa kabla ya muda na mtoto akawa amefariki basi ataoshwa, na ata vishwa sanda, na ataswali-wa, na atafufuliwa siku ya kiama pamoja na watu wengine .

Ama ikiwa ni chini ya miezi minne basi hataoshwa wala kuvishwa sanda wala kuswaliwa, na atazikwa sehemu yoyote; kwa sababu ni pande la nyama tu na siyo Mtu.

Na hiyo iliyo haribika iliyotajwa kwenye swali imefikisha miezi sita, ni waaJibu aoshwe na avishwe sanda na aswaliwe, kwa hivyo kama walivyo sema katika swali kuwa hawakumswalia basi ni jukumu lao sasa hivi kumswalia kwenye kaburi lake ikiwa wanalifahamu lilipo, na kama hawalifahamu lilipo basi wamswalie swala ya aliye mbali, na inatosha kumswalia swala moja tu .

Ama kwa upande wa kuwa mama yake ana shaka ya kuwa mimba hiyo iliharibika kwa sababu yake hakika shaka hizo hazina faida yoyote kwake, wala hilo lisiishuhulishe akili yake, na ni viumbe vingi vinavyofia matumboni mwa mama zao, kwa hiyo hana lawama yoyote juu ya hilo, na achane na shaka hizo na wasiwasi ambao utazoofisha maisha yake tu. Allah ndio mjuzi zaidi.

****

**Swali la 346: ni ipi namna ya kuswali swala ya jeneza (maiti)?**

**Jibu**: Namna ya kuswali swala ya maiti: kwa mwanamume ni kuwekwa mbele ya imam na imamu atasimama upande wa kichwani kwa maiti, maiti awe ni mdogo au mkubwa ,anasimama upande wa kichani kisha ana toa bakbira ya kwanza (**Allah Akbar**), kisha anasoma Suratul fatiha (**Al hamdu**), na kama atasoma na Sura yoyote ndogo fupi sivibaya, bali wamesema baadhi ya wanachuoni kuwa hilo ni katika Sunna, kisha atatoa takbira ya pili (**Allah Akbar**) kisha atamswalia Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Allahmma swalli alaa Muhammad, wa alaa aali Muhammad, kamaa swallaita alaa Ibraahiima wa alaa aali Ibraahiima, innaka hamiidu majiidu , Allahmma baarik alaa Muhammad, wa alaa aali Muhammad, kamaa baarakta aIbraahiim wa alaa aali Ibraahiim, innaka hamiidu majiidu, kisha atatoa takbira ya tatu (**Allah Akbaru**) ataomba dua ambazo zimepokelewa kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na miongoni mwa dua hizo ni hii: ((**Allahmma ghfiri lihayinaa wa mayitinaa, wa shaahidnaa wa ghaaibinaa, wa swaghiirinaa wa kabiirinaa, wa dhakarinaa wa unthaanaa, Allahmma man ahayaitahu minnaa fa ahyihi alal islaam, wa man tawaffaitahu minnaa fatawaffahu alal iimaan**)), Sahihi Muslim: 368 / 2.

((**Allahmma ghifri lahuu, war hamhuu, wa aafihi, wa afu anhu, wa akrim nuzulahu, wa wasii madikhalahu, wa ghaslhu bil maai wathalji wal bardi, wa naqihi minal khatwaayaati kamaa yunaqqa thaubul abiyadhu minad danasi**)). Sahihi Muslim (963), ((**Allahmma laa taharimnaa ajrahu, walaa tudhwilunaa baadahuu, waghafri lanaa walahu** )), ameipokea Abuu

Daud: (3201) na pia Ibnu Maajah (1498 ). Na dua nyingine zisizo kuwa hizo miongoni mwa dua zilizo pokelewa kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kisha atatoa takbira ya nne (**Allah Akbaru**) wamesema baadhi ya wanawachuoni Allaah awarehemu: na atasema baada ya takbira ya nne: Rabbanaa aatinaa fiy dunia hasanat wafil aakhirati hasanat waqinaa adhaaba nnaari, na kama atatoa takbira ya tano si vibaya; kwa kuwa imethibiti kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake bali wakati mwingine inatakikana kufanya hivyo; yani: kutoa takbira ya tano kwa kuthibiti hilo kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, Sahihi Muslim (957).

Na ambalo limethibiti kutoka kwa Mtume inatakikana kwa Mtu alifanye kwa utaratibu ambao limepokelewa, atafanya hili mara hii na mara nyingine atafanya hili, ijapokuwa wengi wanazingatia takbira nne, kisha atatoa salamu moja upande wa kulia .

Ila kama maiti ni mwanamke imamam atasimama katika yake na safu za swala zitakuwa kama safu za swala ya mwanamume.

Zitakapo kusanyika maiti zaidi ya moja basi inatakikana ziwe ni zenye kupangiliwa, karibu ya imamu ziwe za wanaume waliyo balehe, kisha watoto wa kiume, kisha wanawake waliyo balehe, kisha watoto wa kike wadogo, kama hivi kwa utaratibu, na ama vichwa vyao vitawekwa hivi! vichwa vya wanaume vitakua usawa wa katikati ya mwili wa mwanamke ili imamu awe amesimama sehemu ambayo inapaswa asimame kisheria .

Na hapa natoa tahadhari: Watu wengi hudhani kuwa watu wanao beba jeneza wana simama sawa na imamu, bali wengine hudhani kuwa ni lazima mmoja au zaidi ya mmoja awe amesimama

na imamu, hili ni kosa; kwa sababu sunah ni kuwa imamu ndiye mwenye haki ya kutangulia mbele peke yake, na itakapo kuwa watu wanao beba jeneza hawana sehemu katika safu ya kwanza basi watasimama safu ya nyuma ya imamu yani kati ya safu ya kwanza na imamu - wao wanakuwa katikati.

****

**Swali la 347: Ni ipi hukumu ya kumswalia maiti ikiwa maiti huyo alikuwa haswali au inahisiwa kuwa haswali au haijulikani hali yake kuwa ana swali au haswali? je inajuzu kwa kiongozi kumswalia maiti huyo?**

**Jibu**: Ama ambae anafahamika kuwa haswali haijuzu kumswalia, hala haijuzu kwa jamaa zake kumpeleka kwa waislam ili wa mswalie; kwa kuwa yeye alikuwa ametoka katika uislam kwa kutokuswali, lililo waaJibu kwa waislam ni kumchimbia shimo sehemu yoyote ambayo sio katika makaburi ya waislam na kutupwa humo bila ya kuswaliwa; kwa sababu yeye hana utukufu wowote na atafufuliwa siku ya kiama akiwa pamoja na Firauni, na Haamaan, na Qaaruun ,

na Ubaiyi bin Khalafi. Ama ambaye haijulikani hali yake kwa waislamu kuwa ana swali au haswali, au wana shaka juu yake kuwa haswali, wana mswali, kwa kuwa asili yeye ni muislam mpaka ibainike kuwa si muislam, lakini hapana tatizo ikiwa watu wana mtilia shaka huyu maiti basi wakati wa kumuombea Dua atasema muombaji: ((**Allahumma inkaana muuminan faghfiri lahu warhamhu**)); kwa sababu kumbagua katika Dua ime tokea kwa wale wanao watuhumu wake zao kwa zinaa kisha hawakuleta mashahidi wanne, kwamba mwanamme anapo mlaani mkewe mbele ya kadhi anasema mara ya tano**:** [**Inna laanata LLahi alayhi inkaana minal kaadhibiina**] hakika laana ya Allah iwe juu yake akiwa ni mwenye kusema uwongo, na mwanamke nae atasema katika mara ya tano: [**Inna ghadhwaba LLahi alayhaa inkaana mina swaadiqiina**] hakika ghadhabu za Allah ziwe juu yake ikiwa mumewe anasema kweli.

****

**Swali la 348: Je swala ya maiti ina wakati maalum wa kuswaliwa? na je inajuzu kuzika usiku? na je swala ya maiti ina idadi ya watu maalumu wa kuswalia? na je yajuzu kuswaliwa makaburini na juu ya makaburi? (yani maiti ambaye ashazikwa ukamswalia akiwa ndani ya kaburi ina faa?) .**

**Jibu:** Swala ya maiti haina wakati maalumu, na mauti hayana wakati maalumu, wakati wowote atakapo kufa Mtu basi ataoshwa na kuvikwa sanda na kuswaliwa katika wakati wowote usiku au mchana, na atazikwa wakati wowote usiku au mchana, isipokuwa katika nyakati tatu haifai kuzika katika nyakati hizo nazo ni: wakati linapo chomoza jua mpaka lipande juu kiasi cha mkuki, na wakati likisimama mpaka lipinduke – yani: kabla ya kupinduka kwa mfano wa dakika kumi, na wakati jua linapo karibia kuzama mpaka lizame, na kuelekea kwake kuzama ni kuwa kati yake na kuzama ni kiasi cha mkuki, basi nyakati hizi tatu hairuhusiwi kuzika ndani yake, na makatazo ya kuzika ndani ya nyakati hizo kisheria ni haramu kuzika mida hiyo; kwa muJibu wa hadith aliyo ipokea uqubatu bi aamiri radh za Allaah ziwe juu yake kwamba yeye amesema: ((N**yakati tatu ametukataza Mtume wa Allaah rehema na amani ziwe juu yake: kuswali ndani ya nyakati hizo au kuwazika maiti wetu ndani ya nyakati hizo**)) (Sahihi Muslim : 831).

Na swala ya maiti haina idadi ya watu maalumu wa kuiswali bali hata kama ataiswali mtu mmoja basi imetosheleza .

Na inajuzu kuswaliwa makaburini, na kwa sababu hiyo wamechagua wana wa chuoni rehema za Allaah ziwe juu yao, kwamba swala ya Maiti inafaa kuswali makaburini kuliko swala ya kawaida haifai kuswaliwa makaburini, wakasema wana wa chuoni: kwamba inajuzu kuswali swala ya maiti makaburini, kama inavyo juzu kuswalia maiti ambaye ashazikwa tayari, na hakika imethibiti kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake yeye aliswali juu ya kaburi la mwanamke ambaye alikuwa akishuhulikia msikiti akafa usiku na maswahaba wakamzika, kisha Mtume akasema: ((**Nifahamisheni ilipo kaburi yake**)) akafahamishwa akamswalia.

****

**Swali la 349: Je ni sheria kumswalia maiti aliye mbali kwa hali yoyote ile? au kuna masharti maalumu yaliyo wekwa?**

Jibu: Kauli iliyo sahihi katika kauli za wana chuoni Allah awarehemu: ni kwamba swala ya maiti aliye mbali siyo sharia au lazima kuswali isipokuwa kwa yule maiti ambae hakuswaliwa,

Mfano kama Mtu amekufa katika mji ambao niwa kikafiri na hakuswaliwa na angalau Mtu mmoja, au alizama katika bahari au Mto au jangwa na maiti yake haikupatikana, hakika ina paswa kuswaliwa, ama ambae ameswaliwa basi siyo sheria au si lazima

kumswalia; kwa sababu hilo halikutokea katika Sunnahh isipokuwa katika kisa cha Najjaashi, na Najjaashy radhi za Allah ziwe juu yake hakushaliwa katika mji wake, kwa sababu hiyo Mtume rehema na amani ziwe juu yake akamswalia katika mji wa madina, na wamekufa watu wakubwa na waheshimiwa katika zama za Mtume na haikupokelewa kuwa Mtume aliwaswalia, na wakasema baadhi ya wanachuoni: Ambaye alikuwa na manufaa katika Dini kwa mali yake au kazi yake, au ilimu yake, anaswaliwa swala ya aliye mbali, na sihivyo haswaliwi swala ya aliye mbali. Na wakasema baadhi ya wana chuoni Allah awarehemu swala ya maiti aliye mbali inafaa kuswaliwa kwa namna yoyote, na kauli hii ni dhaifu.

****

**Swali la 350: Baadhi ya miji wanamzika maiti akiwa amelalia mgongo na mikono yake iko tumboni kwake ni njia ipi iliyo sahihi katika kumzika maiti?.**

Jibu: Namna iliyo sahihi ni maiti kuzikwa akiwa amelalia ubavu wake wa kulia uso wake ukiwa umeelekea kibla, kwani hakika Al Kaaba ni kibla cha waliyo hai na waliyo kufa, na kama ilivyo pia mwenye kulala analalia ubavu wa kulia, kama alivyo amrisha Mtume wa Allaah rehema na amani ziwe juu yake: **na vile vile maiti hulazwa upande wake wa kulia hakika kulala na kufa ni kitu kimoja**, (Sahihi Bukhaar 247) (Sahihi Muslim 2710).

Kama alivyo sema Mwenyezi Mungu mtukufu: [**Mwenyezi Mungu huzipokea roho zinapo kufa na. Na zile ambazo hazikufa wakati wa kulala kwake, Huzishika zilizo hukumiwa kufa, na huzirudisha nyingine mpaka ufike wakati uliyo wekwa, hakika katika hayo bila ya shaka zipo ishara kwa watu wanao fikiri** ]. (Suurat Zumari: 42).

Na akasema tena Allaah mtukufu: [**Na yeye ndiye anaye kufisheni usiku, na anakijua mlicho fanya mchana. Kisha yeye hukufufueni humo mchana ili muda uliyo wekwa utimizwe kisha kwake yeye ndiyo marejeo yenu na tena akuambieni mliyo kuwa mkiyafanya.**]

(Suurat An'am: 60).

Sheria katika kumzika maiti nikuwekwa au kulazwa upande wake wa kulia akiwa uso wake ameelekea kibla.

Huwenda alicho kiona muulizaji ilikuwa ni matokeo ya kuto kujua kwa huyo mwenye kusimamia jambo hilo, lakini mimi sijawahi kusoma kwa yoyote katika wanachuoni Allah awarehemu, akisema Maiti anawekwa kwa kulalia mgongo wake, na mikono yake ikawekwa tumboni kwake!

****

**Swali la 351: Nini hukumu ya kusoma Qur'an juu ya makaburi na kumuombea Maiti Dua kwenye kaburi lake, na mtu kujiombea mwenyewe akiwa kaburini?**

**Jibu**: Kusoma Qur'an makaburini ni Bidaa, na haikupokelewa kutoka kwa Mtume rehema na amani iwe juu yake, wala kutoka kwa Maswahaba radhi za Allah ziwe juu yao, na jambo likiwa halikupokelewa kutoka kwa Mtume wala kutoka kwa maswahaba, hakika haitakikani kisheria sisi kulizua jambo hilo kutoka kwenye nafsi zetu; kwa sababu Mtume amesema katika kuto kuswihi kwa jambo hilo, akasema: (**Hakika kila uzushi ni bidaa na kila bidaa ni upotevu na kila upotevu ni motoni**) – yani kila mwenye kuzua katika dini basi makazi yake yatakua motoni;

Jambo ambalo ni waajibu kwa waislam ni kufuata yale ambayo yamesha fanywa na maswahaba wa Mtume na wale waliyo fuatia maswahaba kwa wema, mpaka waislamu wawe katika kheri na uwongofu; kwa amabayo yamethibiti kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake hakika yeye amesema: ((**Bora ya maneno ni maneno ya Allah, na bora ya uwongofu niuwongofu wa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake**)).

Ama dua ya kuwaombea maiti ukiwa kaburini – hilo halina ubaya nijambo lina faa, atasimama Mtu kwenye kaburi na wanaomba yale ambayo yele ambayo yata wawia mepesi kuyaomba mfano wakisema: Allahmma ghifiri lahuu, Allahmma rihamhuu, Allahumma adikhil hul Jannata, Allahmma ifsah lahu fii qabrihi. na mfano wa hayo katika maombi .

Na ama kujiombea mtu yeye mwenyewe akiwa katika kaburi au makaburi- hili kama muombaji atakusudia kwenda kulifanyia makaburini, basi ni miongoni mwa uzushi yani bidaa; kwa sababu sharia haijataja mahali mahususi pa kuombea dua ila itakapokuja naswi- yani Aya au Hadith kulielezea jambo hilo, na kama haikuja dalili ya Aya na haikuja katika Sunna; Hakika hilo– na maanisha la kuweka au kuchagua sehemu mahususi ya Dua, kwa vyovyote ilivyo sehemu hiyo – itakuwa ni bidaa – yani uzushi .

****

**Swali la 352: Ni ipi hukumu ya kuzuru makaburi?, na kusoma Suratul Faatiha? Na ni ipi hukumu ya wanawake kuzuru makaburi? .**

**Jibu**: Kuzuru makaburi ni Sunna ameiamrisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake baada ya kuwa alikataza kuzuru makaburi, kama ilivyo thibiti hilo kutoka kwake Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akasema katika neno lake: ((**Nilikuwa nime wakatazeni kuzuru makaburi, nawapa khabari! yazuruni makaburi hakika hilo litawakumbusheni Akhera**)) hadith hii ameipokea imaamu Muslim Mungu amrehemu, kuzuru makaburi ni kwa ajili ya mazingatio na kupata mawaidha ni Sunna, hakika

Mtu anapo zuru hawa maiti katika makaburi yao, na hawa jana walikuwa nao juu ya mgongo wa Ardhi wakila kama wanavyo kula wengine, na wana kunywa kama wanavyo kunywa wengine, na wakisitarehe kwa Dunia yao na sasa wamekuwa rahani kwa matendo yao! Yakiwa ya kheri basi wana kheri na yakiwa ya shari basi wana shari, hakika hapanabudi kwa hawa waliyo enda kuzuru kupata mawaidha na kulainika nyoyo zao, na kumuelekea Allah Mtukufu kwa kuachana na maasi na na kushikamana na twaa ya Allah, na inatakikana kwa mwenye kuzuru makaburi aombe kwa vile alivyokua akiomba Mtume rehema na amani ziwe juu yake na akafundisha umati wake maombi haya ((**Assalaamu alaikum daaru qaumi muuminiina, ainnaa inshaAllah bikum laahikuuna, yarhamu Allahl mutaqaadimiina minnaa wal muta akhiriin** )), Swahihi Muslim (974-975 )

Nasialu LLaahu lanaa walakuml a'fiyata, Allahmma laa taharimnaa ajirahum, walaa taftinnaa ba a da hum, waghfirilaanaa walahum.

Na haikupokewa kutoka kwa Mtume kwamba yeye alikuwa akisoma faatiha anapo kwenda kuzuru makaburi, kwahiyo kusoma faatiha wakati wa kuzuru makaburi nikwenda kinyume cha sharia zitokazo kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake.

Ama wanawake kuzuru makaburi hilo ni haramu; kwa sababu Mtume amewalaani wanawake wenye kuzuru makaburi, na wenye kuyafanya ni misikiti (yani kuwa ni sehemu ya ibada) na wenye kuyawekea taa, siyo halali kwa mwanamke kwenda kuzuru makaburi, nah ii nipale atakapo toka nyumbani kwake moja kwa moja akikusudia kwenda makaburini kufanya ziara, lakini kama aliku-

wa ametoka anaenda safari zake nyingine na kwa bahati mbaya akapita makaburini bila ya kukusudia kuwa anaenda kuzuru hapo hakuna vibaya kwa mwanamke huyo kusimama na kuwatolea salamu watu waliyo zikwa hapo, atawatolea salamu ambayo Mtume rehema na amani ziwe juu yake amewafundisha umati wake, hapa itatofautishwa kati ya mwanamke aliye toka nyumbani kwake kwa ajili ya kwenda kuzuru tu, na mwanamke aliye pita makaburini tu bila kukusudia na akasimama akatoa salamu, mwanamke wa mwanzo alietoka kwa ajili ya kwenda kuzuru tu huyu amefanya kitu ambacho ni haramu, na kuisababishia nafsi yake ilaaniwe na Allaah mtukufu, ama mwanamke wa pili ambaye amepita kwa bahati mbaya huyu hana tatizo.

****

**Swali la 353: Kuna tabia katika baadh ya miji na tabia hiyo ni kwamba atakapo kufa maiti wanaweka kaseti za Qur'an kwa sauti kubwa katika ile nyumba ya marehem, nini hukumu ya jambo hili?**

**Jibu**: Bila ya shaka jambo hilo ni bidaa na upotevu, kwa sababu halikua katika zama za Mtume rehema na amani ziwe juu yake wala zama za maswahaba wake radh za Allah ziwe juu yao, na Qur'an hupunguza huzuni itakapo isoma Mtu yeye mwenyewe kati yake na nafsi yake, siyo atakapo isoma kwa kutumia spika ili aisikie kila Mtu hata wale ambao wako katika mambo yao ya kipuuzi wanaisikia katika upuuzi wao,  na mpaka wale ambao wanasikiliza miziki na vyombo vingine vya miziki na pumbao wanaisikia Qur'an, na wakati huo huo wana sikiliza miziki, kana kwamba wanaichezea Qur'an na kuicheza shere.

Kisha kukusanyika watu wa marehemu ili kuwasubiri wanaokuja kutoa pole pia ni katika mambo ambayo haya kuwa ya kijulikana katika zama za Mtume rehema na amani ziwe juu yake, mpaka baadhi ya wanachuoni Allaah awarehemu wamesema: jambo hilo ni bidaa; na kwa hili hatuja waona watu au jamaa wa maiti wakikusanyika kwa ajili ya kuwapokea wanaokuja kutoa pole bali walikuwa wakifunga milango yao, na wakikutana na mtu yoyote sokoni, au akaja yoyote katika watu wanao wafahamu bila ya kujiandaa kwa  ujio wake basi watamuandalia, na ama kukusanyika na kufungua milango kwa ajili ya kuwapokea watu, hakika hili halikuweko wakati wakati wa Mtume rehema na amani iwe juu yake, mpaka maswahaba walikuwa wakihesabu kuwa mkusanyiko kwa jamaa wa maiti, na kutengeneza kwao chakula ni katika moja ya maombolezo, na maombolezo kama inavyo fahamika ni miongoni mwa madhambi makubwa; kwa sababu Mtume rehema na amani ziwe juu yake: amemlaani mwenye kuombolezo na mwenye kusikiliza, na akasema: (Mwenye kuomboleza atakapo kufa na hakutubia kabla ya kufa kwake atasimamishwa siku ya qiyama na ana kanzu ya chuma, Allah atupe afya.

Nasaha zangu kwa ndungu zangu waislam: waache mambo hayayaliyo zushwa ; kwakuwa kuyaacha hayo nibora kwao wao mbele ya Allah Mtukufu, na nibora kwa upande wa Maiti pia; Kwa kuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ametuambia kuwa maiti anaadhibiwa kutokana na kiliyocha ndugu zake kumlilia yeye , na kwa maombolezo ya jamaa zake, ((**maana ya kuwa maiti anaadhibiwa**)) nikwamba yeye maiti anapata maumivu na uchungu kutokana na huku kuliya na kuomboleza kwa ndugu zake, ijapokuwa haadhibiwi mateso ya mwenye kufanya jambo; na kwakuwa Allaah mtukufu anasema: [**wala hatabeba mwenye kubeba mzigo wa mwenzie**]. (Surat An'aam: 164), na siyo lazima adhabu iwe ni kuteshwa tu, hivi huoni neno lake Mtume rehema na amani ziwe juu yake alipo sema: ((S**afari ni sehemu katika Adhabu**)), na sikwamba safarini kuna kuadhibiwa bali maumivu anayo yapata msafiji na kuchoka na tabu za njiani na mengine yanayo fanana na hayo hiyo inahesabika ni adhabu tosha, na miongoni mwa maneno ya watu wanasema: ((Y**ameniadhibu niliyo ya dhamiliya**)) pale atakapotwa na matatizo au huzuni kubwa.

Matokeo ya yote: Natoa nasaha kwa ndugu zangu kutokana na Ada au tabia kama hizi ambazo haziwazidishii kitu kwa Allah isipokuwa kuwaweka mbali na Allah, na hawawazidishii maiti wao isipokua Adhabu.

****

## FAT'WA ZINAZOHUSU ZAKA

### Swali la 354: Ni zipi sharti za kutoa Zaka?

**Jibu**: Sharti za kupasa kutoa zaka : kwanza ni Mtu awe Muislam, pili awe yuko huru siyo mtumwa, tatu aweni mwenye kumiliki kiwango ambacho kina tosha kutoa zaka na zaidi, nne kutimiza mwaka isipokuwa katika Muasharaati

**Ama Uislamu**: Ni kwamba kafiri hapaswi kutoa zaka, wala haikubaliwi hata akitoa kwa jina la zaka , ushahidi ni neno lake Allah Mtukufu :

[**Na hawakuzuiliwa kukubaliwa michango yao ila kwa kuwa walimkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala hawaji kwenye swala ila kwa uvivu, wala hawatoi michango ila nao wamechukia**]

[Surat Taubah: 54], lakini haimaanishi kuwa haipasi kwa kafiri wala haiswihi kwake kuwa yeye amesamehewa huko Akhera hapana, bali ata adhibiwa kwa ajili ya kutotoa zaka; kwa kauli yake Allah Mtukufu:

38. [**Kila nafsi imo rahanini kwa mabaya iliyo yachuma**]

39. [**Isipo kuwa watu wa kuliani**]

40. [**Hao watakuwa katika Mabustani, wawe wanaulizana**]

41[**Khabari za wakosefu**]

42. [**Ni nini kilicho kupelekeni Motoni**]

43.[**Waseme: Hatukuwa miongoni walio kuwa wakisali**]

44. [**Wala hatukuwa tukiwalisha masikini**]

45.[**Na tulikuwa tukizama pamoja na walio zama katika maovu**]

46.[**Na tulikuwa tukiikanusha siku ya malipo**].

47.[**Mpaka yakini ilipo tufikia**.] [Surat Mudathir], na hii ni dalili kuwa makafiri wataadhibiwa kwa baadhi ya vifungu vya uislam na hivyo ndivyo ilivyo .

**Ama kuwa huru**: Ni kwa sababu mtumwa mwenye kumilikiwa yeye hana mali; kwa kuwa mali yake niya bwana wake yani Yule anae mmiliki, Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Mwenye kuuza mtumwa mwenye mali basi mali yake niya alie muuza ila atakapo toa mashariti mnunuaji**)), kwa hiyo yeye simwenye kumiliki mali mpaka ipase kwake yeye kutoa zaka, na ikikadiriwa kuwa mtumwa ana anacho kimiliki basi umiliki wake mwisho unarudi kwa bwana wake; kwa sababu bwana wake anaweza kuchukua alicho nacho, na hivyo inakua umiliki wake haukutulizana kama umiliki wa mali kwa ambaye sio mtumwa.

**Na ama kumiliki kiwango**: Maana yake ni kuwa Mtu ana mali ambayo inafika kiwango ambacho sharia imekikadiria kutolewa zaka, na hii inatifautiana kutokana na mali yenyewe, itakapo kuwa Mtu hana kiwango ambacho kina pasa zaka basi yeye hatoi zaka;

kwa kuwa mali yake ni kidogo haiwezekani kugawanywa sawa.

Na kiwango katika mawaashi – yani wanyama wenye kufugwa kiasi cha kuanzia na chakuishilizia na wasiokuwa wanyama hoa ni kiasi cha kuanzia na kinacho zidi kitatolewa kulingana na hesabu yake.

**Na ama kupitiwa na mwaka**: Ni kwakuwa kupasa kwa zaka kwa mali ambayo haija zungukiwa na mwaka inalazimu matajiri kupata khasara au kukosa faida, kupasa kwake zaka kwa mali ambayo ni zaidi ya mwaka inalazimu madhara katika haki ya mtoaji zaka, ikawa ni hekma ya sharia kakadiria kiwango maalumu cha kutoa zaka na muda maalumu unao pasa kutoa zaka ni kuzunguka mwaka, katika kuunganisha mzunguko wa mwaka kwa kuweka haki ya matajiri, na haki za watoaji zaka.

Na kwa hali hii lau Mtu atakufa kwa mfano au ikaharibika mali yake kabla ya kutimia mwaka hupomoka kwake uwajibu wa kutoa zaka, ila imehusishwa kwake kutimia mwaka katika mambo matatu: biashara kuwa na faida, na matokeo yanayodhibitika, na mali zingine kama mazao na matunda.

Ima faida ya biashara asili yake ni kuzungukiwa na mwaka, na faida ya ujumla asili yake ni kuzungukiwa na mwaka, na ama mazoa na matunda kuzungukiwa kwake ni wakati wa kupatikana kwake yani – wakati wa kuvuna kama ni mazao au kuchuma kama ni matunda.

****

**Swali la 355: Ni namna gani ya kutoa Zaka ya mshahara wa mwisho wa mwezi?**

**Jibu**: vizuri katika hili ni kwamba inapotimia mwaka kutoka mshahara wa mwanzo aliopokea basi atatoa zaka kwa kile alichokuwa nacho chote, pesa ambayo imetimiza mwaka ataitolea zaka, na ambayo haija timiza mwaka atakua ameitanguliza zaka yake, na kuitanguliza zaka hapana neno, nah ii ni nyepesi kwake ikiwa anapatiliza kila mwezi kivyake, lakini kama ikiwa anautumia mshahara wa kila mwezi kabla ya kuingia mwezi mwingine hapaswi kutoa zaka; kwa kuwa moja ya masharti ya zaka ni mali itimize mwaka .

****

**Swali la 356: Inapasa kutoa Zaka katika mali ya mtoto na mwenda wazimu?**

**Jibu:** Katika jambo hili wametofautiana wana wa chuoni rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao: miongoni mwao kuna aliye sema: kutoa zaka katika mali ya motto na mwenda wazimu siyo wajibu, kwa kutizama kwamba haja kalifishwa na sharia katika

kutoa zaka, na inavyo julikana nikwamba mtoto na mwenda wazimu siyo katika ambao wame kalifishwa kisheria haipaswi kwao wao kutoa Zaka.

Na katika wana chuoni kuna anaesema: hakika zaka inapaswa kwa wawili hao - kauli hii ndiyo sahihi; kwa sababu zaka ni haki katika mali wala haitizamwi anae imiliki kuwa yukoje; kwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Chukua sadaka katika mali zao**]. Mwenyezi Mungu amejaalia sehemu ya kupasa zaka ni mali, na kwakauli yake Mtume rehema na amani ziwe juu yake kumuambia Muaadhi bin jabali radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake wakati alipo pelekwa Yemeni: ((**wafundishe ya kwamba Mwenyezi Mungu amefaradhisha juu yao zaka katika mali zao zinachukuliwakutoka kwa matajiri kisha zinatolewa kwamafakiri**)), na kwahili ni kwamba inapasa zaka katika mali ya Mtoto na mwenda wa zimu, na atakae simamia utoaji wake ni walii - yani baba - wa Mtoto au wa mwenda wazimu.

****

## Swali la 357: Ni ipi hukumu ya Zaka ya deni?

**Jibu**: Haipaswi kwa ambaye ana mdai mtu kutoa zaka hiyo pesa iliyoko kwa mdeni kabla hajaipewa; kwa kuwa haiko katika mikono yake, lakini ikiwa anaedai ni tajiri basi ni juu yake kuitolea zaka kila mwaka pesa hiyo au mali hiyo iliyoko kwa Mdeni, atakapo itolea zaka pamoja na mali yake basi ime muepuka dhimma, na asipo itolea zaka pesa hiyo iliyoko kwa mdeni pamoja na mali yake inampasa kutoa zaka wakati atakapo lipwa deni hilo, na atatoa zaka ya miaka yote iliyo pita, na hiyo ni kwa kuwa tajiri anauwezo wa kuitaka pesa hiy iliyoko kwa mdeni na akaipata, ameiyacha pesa hiyo kwa matakwa ya mdaiwa, Ama deni likiwa liko kwa masikini - yani anaedai ni masikini au ni tajiri lakini hana uwezo wa kuitaka pesa hiyo au mali hiyo na akaipata basi hapaswi kuitolea zaka kila mwaka, kwa sababu hana uwezo wakuipata pesa hiyo, kwani Mwenyezi Muangu Mtukufu anasema: [**Na akiwa (mdaiwa) ana shida, basi (mdai) angoje mpaka afarijike**.] [Suratul Baqara: 280], hana uwezo wa kuida mali hiyo na akaitumia hana juu yake zaka, lakini kuna baadhi ya wana wachuoni wana sema atakapo ichukua pesa hiyo ataanza kuihesabia mwaka upya; na wengine wao wamesema ataitolea zaka mwaka mmoja, na itakapo zungukiwa na mwaka vilevile ataitolea zaka na kauli hii inayo elemea kwenye ukweli Allah ndiyo Mjuzi zaidi .

****

**Swali la 358: Je Mtu aliye kufa na anadaiwa na hakuacha mali ya kuweza kulipa deni hilo inafaa kuchukua mali ya Zaka ili kumlipia deni hilo.?**

**Jibu**: Amesema ibnu barri na abuu ubaidi Allah awarehemu: kwamba Maiti halipiwi deni alilo acha kwa pesa ya zaka kwa mapatano ya wana wachuoni, lakini ukweli ni kwamba jambo hili wametofautiana wana wachuoni, lakini wana wachuoni waliyo wengi wamesema: Maiti halipiwi deni kutoka kwenya mali ya zaka; kwakuwa maiti ameshaondoka yuko Akhera, wala hapati unyonge na udhalili kwa deni alilo nalo kama matatizo wanayo kutana nayo walio hai, na kwakuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake hakuwa akilipa madeni ya waliyo kufa kwa kuchukua pesa ya zaka, lakini alikua akiwalipia mali zilizo kusanywa kutoka kwa makafiri wakati Allah alipo mfungulia, nahii inajulisha kwamba haiswihi kulipa deni la maiti kwa kutumia mali iliyo tolewa zaka.

Na kauli nyingine ni kwamba Aliye kufa kama alichukua mali za watu na anataka kuwalipa wenyewe basi Mwenyezi Mungu humlipia deni hilo kwa fadhila zake na utukufu wake, na ikiwa amechukua mali za watu ili azifanyie uharibifu basi amejichumia madhambi yeye mwenyewe, deni linabakia kwenye Dhimmah yake atalilita siku ya Qiyama; Na kwa upande wangu hii ndiyo kauli inayoendana na ukweli kwamba maiti analipiwa deni aliloliacha. Na inaweza kusemekana kuwa inatofautishwa kuwa waliyoko hai wanahitajia zaka kwa sababu ya ufakiri wao au kwa ajili ya kuzitumia wakiwa kwenye jihadi au gharama nyingine zisizo

kuwa hizo, na ikiwa waliyo hai hawahitajii, na katika hali ambayo wana hitajia waliyo hai basi kuna tangulizwa masilahi ya waliyo hai, na katika hali ambayo waliyo hai hawahitajii mali hapana vibaya tukalipa madeni ya waliyo kufa wale ambao wamekufa na hawakuacha mali, na huenda kauli hii ikawa ya kati na kati kati ya hizi kauli mbili .

****

### Swali la 359: Je inaswihi sadaka ya mwenye kudaiwa? Na nihaki gani anasamehewa katika haki za kisheria?

**Jibu**: Kutoa sadaka ni katika kutoa kuliko amrishwa kisheria na nikuwafanyia ihsaani waja wa Mwenyezi Mungu itakapo tolewa kwenye sehemu zake zinazo sitahiki, na Mtu anapata thawabu kwa kutoa sadaka na kila Mtu atakua kwenye kivuli cha sadaka yake siku ya kiama, na sadaka inakubaliwa itakapo timiza masharti yake iwe Mtu ana daiwa, au hakuwa na deni; na katika mashart ya sadaka ni iwe mtoaji kaitoa kwa ajili ya kutaka radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu na iwe imepatikana kwa kazi ya halali na ikatokezea katika sehemu yake; kwa mashart haya sadaka inakuwa ni yenye kukubaliwa kutokana na dalili za kisheria, wala siyo sharti kuwa Mtu anaetoa sadaka awe hana deni, lakini ikiwa deni lake linachukua kila alicho nacho katika mali, hakika siyo katika busara - wala katika Akili - atoe sadaka ambayo ni Sunna na siyo

lazima au waajibu - na akaacha deni ambalo ni wajibu kwaka na nilazima kwake kulilipa , uswahihu aanze jambo la wajibu na lazima kwake, kisha ndiyo atoe sadaka, na hili wametofautiana wanachuoni kwa ambae akitoa sadaka na ana deni ambalo ni kubwa lina enea mali yake yote akililipa, katika wanachuoni kuna waliyo sema: hakika haijuzu kwake kutoa sadaka; kwa sababu hali hiyo inamgharimu, na deni kubakia katika dhimmah yake kwa hali hii lazima kwake kuliilipa. Na katika wanachuoni kuna walio sema Inajuzu lakini kwa mtazamo tofauti na wa mwanzo.

Kwa kila hali ni kwamba haitakikani mwanadamu ambaye anadaiwa atoe vyote alivyo navyo kwa kutoa sadaka ila mpaka alipe dani kwa sababu deni ni wajibu kwake na sadaka ni suna, wajibu unatangulizwa kuliko Sunna.

Ama haki za kisheria amabazo husamehewa mtu mwenye deni mpaka alipe deni ni hizi: Kwanza ni Hija; Mtu mwenye deni hapaswi kwenda hija mpaka awe ashalipa deni lake .

Ama kutoa zaka wanachuoni wametofautiana kuwa je mwenye deni hapaswi kutoa zaka au ana paswa kutoa zaka? miongoni mwa wana wachuoni kuna wanaosema mwenye deni hapaswi kutoa zaka kiasi ambacho kinalingana na deni, iwe deni ni mali ya waziwazi inayoonekana na watu wote au mali amabayo haiyonekani.

Na katika wana wachuoni kuna wanao sema mwenye deni anatoa zaka kiasi ambacho kina lingana na deni analo daiwa bali pia anaweza kutoa zake kiasi chote ambacho anacho katika mali yake, ijapo kuwa deni linapunguza kiwango cha mali aliyo kuwa nayo.

Na miongoni mwa wanachuoni kuna waliosema kwa ufafanuzi ufuatao: Ikiwa mali yake ni katika mali zisizo onekana kama vile pesa na bidhaa za biashara basi haifai kutoa zaka kiasi ambacho kinalingana na deni, na ikiwa mali ni katika mali ambazo zinaonekana kama vile mifugo na mali ambazo zinatoka chini ya Ardhi basi anaweza kutoa zaka.

Na usahihi kwangu mimi ni kwamba: Inafaa kutoa zaka kwa hali yoyote iwe mali ni ambazo zinaonekana au zisizo onekana, na kila ambacho anakimiliki mikononi mwake ni mali ambayo inapasa kuitolea zaka basi ni juu yake kutoa zaka ya mali hiyo hata ikiwa anadaiwa, hii ni kwa sababu zaka nilazima kutolewa katika mali; kwa maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Chukua sadaka katika mali zao, uwa twaharishe na uwa takase kwazo na uwaombee rehma. Hakika maombi yako ni utulivu kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua**] [Surat Tauba: 103]. Na kwa maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake alipo Muambia Swahaba wake Muaadhi bin Jabal Allah amrehemu pindi alipo Mtuma kwenda yemen akamuambia: wafahamishe ya kwamba Mwenyezi Mungu amefaradhisha juu yao sadaka katika mali zao zinachukuliwa kutoka kwa matajiri wao na

kuprlekwa kwa masikini wao, na hadith hii iko katika kitabu cha imamu Bukhaar kwa tamko hili, na kwa dalili hizi Mbili Qur'an na Sunna ni ushahidi tosha kwamba, hakuna maingiliano kati ya kutoa zaka na kulipa deni, kwa sababu deni linapasa na nidhimmah kwa mwenye kudaiwa na zaka nayo inapasa kutolewa katika mali, kwahiyo kila kimoja katika hivi kinapasa au ni lazima katika sehemu yake bila kukihusisha kingine, hakuna mgongano wala muingiliano kati ya zaka na deni, deni litabaki kuwa ni dhimmah kwa anaedaiwa mpaka alilipe na zaka katika mali itatolewa kwa hali yoyote ile .

****

**Swali la 360: Kama Mtu hajatoa Zaka miaka minne analazimika kufanya nini?**

**Jibu**: Mtu huyu atakua ni mwenye kupata dhambi kwakuwa ameichelewesha zaka; kwa sababu mtu anatakikana atoe zaka haraka wala asiicheleweshe, kwa kuwa ni jambo la lazima, najambo la lazima nikulifanya haraka, kwa hiyo ni nijuu yake Mtu huyu atubie kwa Mwenyezi Mungu haraka sana kutokana na maasiya

hayo aliyo ya fanya ya kuto kutoa zaka mapema, na nijuu yake kuanza kutoa zaka zote zakila mwaka ambao hakutoa zaka, na hakuna mwaka ambao hatatoa zaka ya mali yake bali anatakiwa kufanya haraka kuitoa zaka yake ili madhambi yakuchelewesha kutoa kwake zaka yasizidi.

****

**Swali la 361: Je inatolewa Zaka mifugo ambayo uchungaji wake ni muda wa nusu ya mwaka?**

Jibu: Mifugo ambayo uchungaji wake ni nusu mwaka kwa ukamilifu haina zaka mifugo hiyo, nah ii ni kwa sababu zaka ya mifugo haipaswi ila itakapokuwa mifugo inachungwa kwa kulishwa majini yaliyo oteshwa na Mwenyezi Mungu katika ardhi kwa muda wa mwaka kamili au zaidi ya mwaka, Ama mifugo ambayo uchungwaji wake ni sehemu tu katika mwaka au nisu ya mwaka, mifugo hiyo haitolewi zaka ila itakapokuwa umfugaji kaifuga kwa ajili ya biashara, hiyo anaitolea zaka na hukumu yake inatolewa zaka ya bidhaa, na itakapokuwa kaifuga kwa ajili ya biashara basi

atatoa zaka kwa makadirio ya kila mwaka kuwa yanalingana na kiasi gani kisha kwenye hicho kiasi linatolewa fungu la kumi kiasi chake; yani - mbili na nusu katika kila mia moja ndiyo kima chake anacho toa.

****

**Swali la 362: Kabla ya miaka mitatu nimenunua nyumba na nje yake kuna mitende mitatu yenye matuma aina mbili na ina matunda mengi namshukuru Mwenyezi Mungu je kwa hali hii na paswa kutoa Zaka? kama jawabu ni ndiyo, na watu hawajui kabisa mimi ninauliza kutokana na hilo: Vipi nitafahamu kiwango cha kutoa Zaka na mimi nayapatia faida? Pili: ninawezaje kuigawanya Zaka? Na je itatolewa kila aina kivyake au hujumuishwa aina zote na kutolewa kama aina moja? Je inapasa kutoa pesa badala yake? Na nitafanyaje kwa miaka iliyo pita ambayo sikutoa Zaka?**

**JIBU**: Alicho kisema muulizaji ni kweli kabisa kuto kufahamika hukumu ya mitende hii ambayo inakua kwenye majumba kwa watu waliyo wengi, watu wangi wanakuwa na mitende saba, au mitende kumi, au zaidi au michache na matunda yake yanafikia

kiwango lakini watu hawafahamu kuwa matunda hayo yanatolewa zaka wanadhani zaka inakuwa kwenye mabustani tu, na zaka ya tende inakuwepo iwe mitende iko kwenye mabustani au majumbani; kwahiyo akiwa Mtu anamitende nyumbani baasi na amuite mtu mwenye uzoefu ampigie tathimini ya tende hizo au matunda aangarie je yanafikia kiwango cha kutoa zaka au hayajafikia? ikiwa inafikia kiwango cha zaka ni wajibu kwake kuitolea zaka lakini ataitoleaje na kasema yeye anaipatia faida? kama alivo sema muulizaji; kwa hali hii tende zitafanyiwa makadirio ya kima chake, na zinatolewa nusu fungu la kumi katika kima chake au thamani yake; nah ii inakuwa wepesi kwa anaemiliki tende hizo, na zitanufaisha kwa wenye kuhitajia - yani namaanisha kuwa akitoa hela katika hicho kiwango alicho pata, hela hiyo itawanufaisha wenye kuhitajia na kuifanyia makisio kwa pesa vilevile inakuwa wepesi kwa mmiliki wa tende hizo, na kiwango cha zaka nikutoa tano katika mia moja, wakati zaka ya mali katika mia moja unatoa mbili na nusu, lakini zaka hii ya tende unatoa tano katika mia moja; kwa sababu zaka yake ni zaka ya matunda, na siyo zaka ya biashara.

Ama kuhusu miaka iliyo pita ambayo hakutoa zaka kwa kutokujua basi atakadiria au kukisia katika nafsi yake, anadhani nikiasi gani kwa matunda ya miaka iliyo pita; na atatoa zaka yake muda huo akishajua baada ya kufanya makisiyo, na hatakuwa na madhambi kutokana na kuchelewesha zaka kwa miaka iliyo pita; kwa kuwa alikua hafahamu, lakini inamlazimu kulipa zaka za miaka iliyo pita.

****

**Swali la 363: NI kiwango gani cha kuweza kutoa zaka katika dhahabu na fedha? na pishi ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake ni sawa na kilo ngapi?**

**Jibu**: Kiwango cha kutoa zaka katika fedha na dhahabu ni mithkaala ishirini, ambayo ni sawa na glam. Ama kiwango cha fedha ni mithkaala mia moja na arobaini kwa dirhamu na fedha ya saudia ni Riyal khamsini na sita.

Ama kiasi cha pishi ya Mtume kwa kilo ni sawa na kilo mbili na glam arobaini za ngano kwa uzito.

****

**Swali la 364: Mtu ana watoto wa kike na amewapa mapambo ya thamani kama vile mikufu ya dhahabu heren pete bangiri na vinginevyo na mapambo hayo yakikusanywa yanafikia kiwango cha Zaka, lakini pambo moja moja peke yake halifikii kiwango cha Zaka, je yanakusanywa yote kisha ndiyo yatolewe zaka?**

**Jibu**: Ikiwa amewapa mapambo hayo kwa njia ya kuwaazima basi mapambo hayo yatakuwa ni yake inampasa ayakusanye yote, kama yanafikia kiwango cha Zaka basi atatoa Zaka yake, na ikiwa ame wapa watoto wake mapambo hayo yawe ni ya kwao moja kwa moja basi haipaswi kuyakusanya sababu kila pambo moja linajitegemea na kila moja linamilikiwa na mwingine; kwahiyo kama pambo moja litafikia kiwango cha Zaka atalitolea Zaka, na ikiwa halifikii kiwango basi halitolei Zaka.

****

**Swali la 365: Mtu atakapo toa Zaka akampa Mtu mwingine ambaye anasitahiki kupewa Zaka kisha Yule aliye pewa akaamua kumpa Yule aliyempa zawadi je aikubali zawadi hiyo?**

**Jibu**: Mtu atakapo toa Zaka yake kumpa Mtu ambae anasitahiki kupewa Zaka kisha yule aliye pewa akampa zawadi yule aliyempa Zaka hapana vibaya itakapo kuwa hawana makubaliano kwamba nitakupa Zaka kisha unipe zawadi, lakini lililo bora nikuto kuikubali hiyo zawadi.

****

**Swali la 366: Je inajuzu Mtu kutoa nguo au kitu kingine katika Zaka ya mali – yani alitakiwa atoe Zaka ya mali yake lakini akaona asitoe pesa bali atoe nguo au kitu kingine?**

**Jibu**: haijuzu kufanya hivyo.

****

**Swali la 367: Itakapo kuwa dhahabu pamoja na Almasi na mfano wake vipi itakadiriwa Zaka yake katika vitu hivyo?**

**Jibu**: Itakadiriwa au kukisiwa na watu wenye uzoefu mhusika ataenda na dhahabu yake kwa mfanya biashara wa Dhahabu au ili waitizame je inafikia kiwango cha kutoa zaka au haifikii kiwango? ikiwa haifikii kiwango cha zaka basi hatatoa zaka, isipo kuwa kama atakua na Dhahabu nyingine itakayo timiza kiwango cha kutoa zaka, itakisiwa kima au thamani ya Dhahabu ambayo imechanganyika pamoja na Alimasi, kisha Itatolewa zaka yake, nayo ni robo ya fungu la kumi.

****

**Swali la 368: Nini hukumu ya kutoa pesa ya Zaka ikajengea misikiti? Na fakiri ni Mtu wa namna gani?**

**Jibu**: Haijuzu kutoa Zaka isipo kuwa kwa watu aina nane ambao kawataja Mwenyezi Mungu Mtukufu; Na kwa sababu Mwenyezi Mungu kazitaja aina hizo za watu kwa msisitizo, amesema: [**Wa kupewa sadaka ni mafakiri, na masikini, na wanao zitumikia, na wa kutiwa nguvu nyoyo zao, na katika kukomboa watumwa, na wenye madeni, na katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na wasafiri. Huu ni waaJibu ulio faridhiwa na Mwe-**

**nyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima**.] (Surat Tauba: 60), haijuzu pesa ya zaka kuitoa kwa ajili ya kujenge misikiti, na kuitoa kwa ajili ya kufundishia ilimu yoyote na vinginevyo, sadaka zinazo kubalika ni bora zikatolewa kwa mambo yenye manufaa.

Na ama kuhusu fakiri: ni Yule ambaye ana sitahiki kupewa zaka, ambaye hapati mahitajio yake yanayo mtosha yeye na familia yake kwa muda wa mwaka kwa kutokana na zama alizopo na maeneo aliyopo, Huenda pesa kama riyali 1000 au laki moja katika wakati aliopo au zama alizopo pesa hiyo akiwa nayo anahesabika ni tajiri, na katika zama nyingine au maeneo mengine pesa hiyo akiwa nayo siyo tajiri; kwa ugumu wamaisha na mengineyo.

****

**Swali la 369: Je yanatolewa Zaka magari yaliyo wekwa kwa ajili ya kukodishwa na magari ya matumizi binafsi ambayo siyo ya kukodisha?**

**Jibu**: Magari yanayo kodishwa kwa kusafirisha watu au vitu, au magari ya mtu binafsi ambayo siyo ya kukodisha anatumia mtu mwenyewe, magari hayo yote hayatolewi zaka ila zaka inatolewa kwenye zile pesa zinazo patikana katika hiyo kazi ya kukodisha au kubeba - yani zaka inatolewa kwenye faida ya hiyo kazi ya kukodisha hayo magari, pesa hizo zitakapo fikia kiwango kinacho takikana kutoa zaka, au kuzikusanya na pesa nyingine ambazo anazo na zikawa zime zungukiwa na mwaka, na vile vile mali isi-

yo hamishika kama vile majumba au ardhi, mali hizo na majumba hayo hayatolewi zaka isipo kuwa zaka hutolewa kwenye zile kodi zinazo patikana.

****

**Swali la 370: ni nini hukumu ya zaka ya nyumba zinazo kodishwa?**

**Jibu**: Nyumba za kukodishwa zikiwa zime wekwa kwa ajili ya biashara na kunufaika basi zaka yake ni kile kiwango kinacho patikana katika kodi, ikizungukiwa na mwaka na mfungamano ya kupangishana ya kisha kamilika, ikiwa mapato haya timizi mwaka kuanzia wakati walipo funga mkataba basi nyumba hiyo haitolewi zaka, kwa mfano nyumba hii inapangishwa Alfu kumi 10,000 na mwenye nyumba anachukua alfu tano 5000 wakati ule wa makubaliano kisha anaitumia hiyo alfu tano, kisha ikifikia katikati ya mwaka anachukua alfu 5000 anaitumia kabla ya mwaka kuisha kwa mfano kama huu hatoi zaka; kwa kuwa mali hii haikutimiza mwaka, ama itakapo kuwa nyumba imeandaliwa kibiashara ili aiuzena kabla haja iuza wakati akisubiria ipande bei ilia pate

faida kubwa akaamua kuipangisha, basi kwa hali kama hiimmiliki ata paswa kutoa zaka kwa kiwango cha hiyo nyumba, na vile vile katika kodi yake ataitolea zaka ikitimiza mwaka kama maelezo yaliyo tangulia, itampasa kutoa zaka katika kiwango au kima cha hiyo nyumba; kwa sababu kaiyandaa kwa ajili ya biashara, kwa muda ambao ameoanga iwepo kwa ajili ya kuipatia faida, na hii ni katika kila kitu ambacho kimekusudia kwa ajili ya biashara na kukipatia faida basi kina kuwa na zaka; kwa maneno ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Hakika matendo yote yanazingatiwa niya, na hakika kila mtu kuna ambalo amelikusudia**)) (Sahihi Bukhaary (1), pia Muslimu], na huyu ambaye ana pesa au mali anacho taka ni kuchuma na amenuiya kwenye kiwango anacho pata kwenye nyuma hiyo na siyo nyumba yenyewe bali amelenga kile kinacho patikana, na kiwango chake ni dirhamu na pesa, na pesa zinatolewa zaka, basi huyu ambayeamekusudia nyumba hii iwe ya biashara na aipatie faida ina kuwa waJibu kwake yeye kutoa zaka katika kiwango au kima kinacho patikana katika kodi yake pindi tu ikizunguliwa na mwaka tangu siku walipo wekeana mkataba - yani kuanzia tarehe waliyo kabidhiana nyumba mpaka ikitimia mwaka anatoa zaka kwa ule mwaka.

****

**Swali la 371: Mtu kanunua aridhi ili aishi hapo na baada ya kupita miaka mitatu akakusudia kuifanyia biashara je ule muda uliopita atautolea Zaka?**

**Jibu**: Haipaswi kutoa zaka; kwa sababu miaka iliyo pita alikusudia kukaa, lakini kuanzia pale alipo nuiya kuifanyia biashara na aipatie faida aridh hiyo basi itaanza kufungamana na mzunguko wa mwaka, ikitimia mwaka kuanzia muda aliyo azimia kuifanyia biashara inapasa kwake kuitolea zaka.

****

**Swali la 372: Ni nini hukumu ya kutoa Zakatul Fitri katika masiku kumi ya mwanzo wa mwezi wa Ramadhan.**

**Jibu**: Zakatul Fitri, imeitwa Fitri kukwa inamafungamano na siku ya kufungua; kwa kuwa fitri ndiyo sababu kuu iliyo ifanya iitwe Zakatul fitri; basi haitangulizwi Zaka hiyo, ubora ni kutolewa siku ya Iddi kabla ya swala ya iddi, lakini pia inajuzu na kufaa

kutangulizwa kabla ya Iddi kwa siku moja au mbili, kwa kutokana na wepesi wa Yule mwenye kutoa na mwenye kupokea, ama kutoa kabla ya hapo kauli iliyo swahihu katika kauli za wana wachuoni Allaah awarehemu ni kwamba haijuzu kuitoa Zakatul Fitri siku za mwanzo wa ramadhani, kwa hiyo kuna nyakati mbili za kutoa Zakatul Fitri: wakati ambao inajuzu kutolewa nao ni kuitoa siku moja kabla ya Iddi au siku mbili kabla ya Iddi, na wakati mwingine ni wakati ambao ni bora zaidi kuitoa Zakatul Fitri nao: ni kuitoa Zakatul Fitri siku ile ya Iddi kabla ya swala ya Iddi, Ama kuicheleweshaMpaka baada ya swala ya Iddi haifai ni haramu, wala haihesabiki katika Zakatul Fitri; kwa ushahidi wa hadith ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Mwenye kuitoa kabla ya swala basi hiyo ni zaka yenye kukubaliwa, na mwenye kuitoa baada ya swala basi hiyo ni sadaka miongoni mwa sadaka**)); [hadith hii kaipokea abuu daudi: (1510) Isipokua kama mtu hajui siku ya Iddi kwa mfano Mtu akiwa anakaa kijijini na hakujua siku ya Iddi ila kwa kuchelewa au kwa sababu nyingine mfano wa hiyo basi hapana vibaya kuitoa baada ya Iddi, na itahesabiwa ni Zakatul Fitri.

****

**Swali la 373: Je inajuzu kuzidisha kiwango cha Zakatul Fitri kwa niya ya kutoa sadaka?**

**Jibu**: Ndiyo; inafaa Mtu kuzidisha katika Zakatul Fitri na kile kilicho zidi aka nuiya kuwa ni sadaka ya waaJibu, na katika hii ndiyo wafanyayo baadhi ya watu zama hizi anakuwa na zaka kumi za Fitri kwa mfano na ana nunua mfuko wa mcheleambao ni zaidi ya zaka kumi za Fitri na kisha anatoa mchele wote kwa ajili yake, na kwa ajili ya watu wake wa nyumbani, nah ii inafaa atakapo kuwa na uhakika wa kwamba huu mfuko wa mchele unafikia kiasi ambacho kinafaa kutoa fitri na zaidi; kwa kuwa pishi la Fitri siyo lazima isipo kuwa ni kwa kutaka kujua kiwango tu, tuki fahamu kuwa kiwango chenye uhakika kwa huu mfuko wa mchele na akatoa kumpa faqiri basi sivibaya.

****

**Swali la 374: Wanasema baadhi ya wanachuoni: kwamba haijuzu kutoa Zakatul Fitri mchele, hali ya kuwa aina za vyakula vilivyo chaguliwa kisheria vipo?.**

**Jibu**: Wamesema baadhi ya wana wa chuoni Allah awarehemu, wamesema: itakapo kuwa aina tano nazo ni: nayo ni ngano, na tende, ngano na tende na zabibu na maziwa ya unga; itakapo kua aina hizi zipo basi Zakatul Fitri inafaa kutoa aina hizi haifai

kutolewa aina nyingine, na kauli hii ya wana chuoni ina khitalifiana na kauli ya wanao sema kwamba: Zakatul Fitri inafaa kutolewa aina hizi na aina nyingine hata pesa  hizi ni pande mbili zinazo pishana .

Sahihi ni kwamba: zaka ya Fitri inafaa kutolewa kwenye vyakula vya wanadamu, nah ii ni kwasababu Abaa saidi al khudriy radhi za Allah ziwe juu yake kama ilivyo thibiti kutoka kwake katika kitabu cha  ((Sahihi Bukhary)) anasema: **((Tulikua katika zama za Mtume rehema na amani ziwe juu yake tukiitoa zaka ya Fitri pishi katika chakula, na wakati huo chakula chetu kilikua ni Tende, na Ngano  na Zabibu, na Maziwa ya unga**)), [Sahihi Bukhary: 1510],  na wala haikutajwa Buru, wala sifahamu kuwa burru ilitajwa katika Zakatul Fitri katika hadith Sahihi iliyo wazi, lakini hakuna shaka kuwa burru pia inatosheleza, kisha  hadith ya ibinu abasi radhi za Allah ziwe juu yake amesema:

((**Amefaradhisha Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake, zaka ya Fitri kwa ajili ya kutwaharisha swaumu kutokana na upuuzi na maneno ya kijinga, na pia kuwalisha masikini**)), [hiki ni kipande katika hadith ya ibnu Abasi] na uswahihu ni kwamba chakula cha wanaadamu kina tosheleza kutoa Fitri hata kisiwe miongoni mwa aina tano ambazo zilizo tajwa na wanachuoni wa Fiqihi Allah awarehemu; kwa sababu aina hizo tano za vyakula - kama zilivyo tajwa hapo mwanzo na kuashiriwa zili kuwa ni aina nne ambazo moja wapo ilikuwa ni chakula cha watu walicho kuwa wakikitumia zama za Tume rehema na amani

ziwe juu yake; kwa hiyo inajuzu kutoa zaka ya Fitri Mchele, bali naona Mchele ni bora kuliko chakula kingine katika zama zetu hizi; kwakuwa ndiyo chakula chenye gharama ndogo na kinacho penda na watu, pamoja na hili mambo yana tofautiana inaweza ikawa katika upande wa vijijini baadhi ya watu wanapenda tende mtu akatoa zaka ya Fitri Tende ,na katika sehemu nyingine wanapenda zabibu Mtu akatoa zaka ya Fitri Zabibu, na vile vile maziwa ya unga na vyakula vingine visivyo kuwa hivyo, lililo bora ni kwamba katika kila watu wana chakula wanacho kipenda na ambacho kinafaa zaidi kwao wao.

****

**Swali la 375: Ameulizwa Shekh: ambaye ana thuluthiya ambayo niya maiti na ana pesa za mayatima je hizo zinatolewa zaka?**

**Akajibu shekh kwa kusema**: Ama thuluthi amabayo niya maiti haina zaka - yani haitolewi zaka ndani yake, kwa sababu haina mmiliki, isipokuwa ame wekwa kwa ajili ya mambo ya kheri,

Na ama pesa za mayatima hizo zina paswa kutolewa zaka ndani yake, Zaka hiyo ataitoa Msimamizi wa mayatima hao kwa niyaba yao, kwa kuwa kauli iliyo sahihi katika kauli za wanachuoni Allah awarehemu ni kwamba Zaka ya Fitri haina mashariti ya kusema Mtoaji awe amebaleghe au au awe na Akili; kwa sababu zaka ni wajibu kutolewa katika Mali.

****

**Swali la 376: Je gari la Mtu binafsi ambalo siyo la biashara je linatolewa zaka?**

**Jibu**: Gari hilo halitolewi zaka, na kila kitu anacho tumia Mtu kwa matumizi yake Binafsi havitolewi Zaka, (**Isipikuwa vipambo kama Dhahabu na Fedha hivi vinatolewa zaka kutokana na ufafanuzi uliyo pita rejea swali no 364**), lakini gari binafsi au kipando chochote, au mashine ya shambani, au vitu vingine visivyo kuwa hivyo havina zaka; Kwa kauli ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema: ((**Hana muislamu kwa Mtumwa wake au farasi wake sadaka**)). [Sahihi Bukhaary 1463; na Sahihi Muslim: 982] .

****

**Swali la 377: Mtu atakapo toa zaka yake kumpa anae sitahiki kupewa zaka je Mtoaji huyo anasitahiki kumuambia anaempa kuwa hii ni zaka?**

**JIBU**: Mtu atakapotoa zaka yake kumpa anaesitahiki kupewa, ikiwa huyoanae pewa anakataa zaka na haikubali kabisa basi inapaswa kwa mwenye kutoa zaka amuambie Yule anae mpa kuwa hii ni zaka, ili alifahamu hilo akitaka akatae kupokea, na akitaka apokeaa, na kama ni kawaida yake kupokea zaka basi linalo takikana asimuambie; kwa kuwa kumuambia kuwa ni zaka ndani yake kuna kitu kama masimbulizi, na hakika amesema Allaah subhaanahu wa taala: [**Enyi mlio amini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi**]. (Surat Baqarah 264).

****

**Swali la 378: Nini hukmu ya kuipeleka Zaka sehemu nyingine na kuacha sehemu ambapo inafaa kutolewa?**

**Jibu**: Inajuzu kwa mtu kuitoa zaka yake kwenye mji na kuipeleka mji mwingine itakapokuwa kuna manufaa kufanya hivyo, Mtu atakapo kuwa ana ndugu zake wakaribu wanao sitahiki kupewa zaka na wako mji mwingine siyo mji anao ishi yeye na akaamua kuwatumia zaka hiyo basi hakuna ubaya katika hilo, na vile vile kama kwenye mji aliopo maisha ya watu wa hapo ni ya juu wana jiweza na akaamua kuipeleka zaka yake kwenye mji ambao watu

wake ni mafakiri zaidi basi hilo pia nijambo linafaa halina tatizo, ima itakapo hakuna manufaa yoyote kuitoa zaka mji aliyopo na kuipeleka mji mwingine basi asiipeleke.

****

**Swali la 379: Ambaye yuko Makkah na familia yake iko mji wa Riyadh je atawatolea Zakatul Fitri Katika Mji wa Makkah? Hii ni kwa mfano, unaweza pigia mfano huu miji mingine**

**Jibu**: Inajuzu kwa Mtu aitolee familia yake Zakatul Fitri, itakapo kuwa familia hiyo hayuko nayo katika Mji mmoja, Itakapo kuwa yeye yuko Mji wa Makkah na familia iko Mji wa Riyadh basi inajuzu kuwa tolea zaka ya Fitri katika Mji wa Makkah, Lakini lililo bora ni kuitoa zaka ya Fitri katika sehemu aliyopo; Iddi itakapo mkuta yuko Mji wa Makkah ataitoa zaka ya Fitri katika Mji wa Makkah, na akiwa yuko Mji wa Riyadh ataitolea Mji wa Riyadh, Na itakapokuwa baadh ya familia iko Makkah na wengine wako Riyadh, basi ambao wako Riyadh wataitolea Riyadh, na ambao wako Makkah wataitolea Makkah; kwa sababu Zakatul Fitri inafuata na Mtoaji.

****

**Swali la 380: Je ubora ni kumpa zaka Mtu anae daiwa ili alipe deni lake au ubora ni Yule Mtu anae taka kutoa zaka aende kwa Yule anae dai na amlipie mdaiwa deni lake?**

**Jibu**: Hali zina tofautiana; akiwa huyu Mtu anae daiwa ni mkweli juu ya kulipa deni lake na aepukane na dhima yake, nani muaminifu wa kutekeleza kwa kile atakacho pewa kwa ajili ya kulipa deni basi tutampa aende akalipe mwenyewe deni lake; kwa kuwa hii ni sitara kwake na kumuepusha aibu inayo mbele za wale Watu wanao mdai.

Ama atakapokua huyo anae daiwa ni Mtu mharibifu wa pesa, na lau tuna mpa pesa kwa ajili ya kulipa deni lake hata lipa deni badala yake ataenda kununua mavitu yasiyo kuwa na umuhimu wowote, basi tusimpe na sisi ndiyo twende kwa anae mdai, na tumuulize: ni kiasi gani unamdai fulani? kisha tunampa na kumuambia deni lake tunamlipia kiasi chote au nusu yake.

****

**Swali la 381: Je kila anaenyoosha Mkono wake akiomba Zaka anasitahiki kupewa?**

**Jibu**: Hapana siyo kila mwenye kunyoosha Mkono wake kuomba zaka anasitahiki kupewa zaka; kwa sababu watu wengine wanaomba pesa lakini ni matahiri, na Mtu wa namna hii atakuja siku ya kiama hali ya kuwa uso wake umenyofolewa nyama - Mungu Atuhifadhi,

Atakuja siku ya kiyama siku ambayo mifupa na uso wake vitatoa ushahidi uliyo wazi kabisa - Mungu atukinge, na akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Mwenye kuwaomba watu mali zao ili awe na pesa nyingi hakika sivinginevyo anaomba kaa la moto basi apunguze kuomba au azidishe**)) (Sahihi Muslim 1041).

Kwa munaasaba huu tuna watahadharisha wale watu ambao wanawaomba watu kwa kutaka kujiongezea fedha ili hali wao ni matajiri, bali pia tuna mtahadharisha kila mtu anae kubali kuchukua zaka na ili hali yeye siyo mtu wa kupewa zaka hahitajii , na nina muambia: hakika wewe utakapo chukua zaka na wewe siyo mtu wa kupewa zaka elewa unakula pesa ya dhulma ambayo siyo haki yako – na Mwenyezi Mungu atulinde, na nijuu ya Mtu kumcha Mwenyezi Mungu mtukufu, na amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Mwenye kukinahiMwenyezim Mungu humtosheleza na mwenye kujizuia Mwenyezi Mungu humzuia**)), (Sahihi Bukhary: 1427 na pia Sahihi Muslim: 1053].

Lakini Mtu akikunyooshea mkono wake kwa kukuomba na

unaamini kuwa yeye ni katika watu wanao sitahiki zaka na ukampa basi zaka yako imetosheleza na kukubalika, na unaondokana na dhima, na kama itakubainikia kuwa mtu huyo siyo katika watu wanao sitahiki zaka basi zaka hairudishi, na ushahidi juu ya hilo ni kisa cha Mwanamume ambae ametoa sadaka ya mali mara ya kwanzaakampa mwanamke mzinifu ikawa watu wanazungumza kumetolewa sadaka usiku akapewa mwanamke mzinifu; yule mwana mume akasema: Alhamduli LLah, kisha akatoa sadaka usiku wa pili, sadaka ikaangukia kwa mwizi wakawa watu wanaongea usiku kumetolewa sadaka kwa mwizi, kisha akatoa sadaka usiku wa tatu akampa tajiri; watu wakawa wanaongea: usiku kumetolewa sadaka kwa tajiri; akasema yule Mwanamume Alhamduli LLah, kwa Mzinifu, kwa mwizi, na kwa tajiri; Akaambiwa: Hakika sadaka yako imekubaliwa, ama mzinifu huenda akajizuia kwa kile ulichompa akaachana na zinaa, Ama Mwizi huenda akakinahi akajizuia na wizi, Ama tajiri huenda akapata mazingatio akatoa sadaka , [Sahihi Bukhary: 1421; na pia Sahihi Muslimu: 1022 ], tizama ndugu yangu ni kiasi gani niya safi inakua na athari .

Kwa hiyo utakapompa ambae amekuomba na ukagundua kuwa uliye mpa ni tajiri, umempa ukidhani ni fakiri basi hakuna haja ya kurudisha zaka.

****

**Swali la 382: Mtu tajiri ametuma Zaka yake kwa mtu na akasema: zigawanye kwa unavyo ona wewe, je huyu wakili anakuwa ni miongoni mwa wenye kuitumikia zaka na anasitahiki kupata katika zaka hiyo?**

**Jibu**: Huyu wakili siyo katika watumishi wa zaka, na wala hasitahiki kitu katika zaka hiyo; kwa sababu huyu ni wakili wa mtu maalumu, na hii ndiyo siri iliyopo katika hili Mwenyezi Mungu anajua zaidi katika msemo wa Qur'an pale aliposema: na wanao zitumikia kwakua hii inaonyesha kuwa uongozi kwa maana ya kuisimamia zaka zote; kwahiyo ambae amesimamia kugawa zaka ya mtu mmoja anaefahamika hahisabiki kuwa ni miongini mwa wasimamizi wa zaka.

****

**Swali la 383: Mtu ni Mdhaifu wa imani je anapewa Zaka kwa ajili ya kuikuza imani yake japokuwa siyo Muheshimiwa katika jamaa zake?**

**Jibu**: Jambo hili wametofautiana wana wachuoni Mungu awarehenu, na kauli iliyo sahihi kwangu mimi: Ni kwamba hapana vibaya akipewa kwa ajili ya kumfanyia mazoea katika Uislamu kwa kuipa nguvu na kuikuza imani yake - na ijapokua anapewa kwa sifa yay eye kama yeye na siyo kiongozi au muheshimiwa katika jamaa zake - kwa neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Na wenye kutiwa nguvu nyoyo zao**], na itakapo kuwa imejuzu kumpa fakiri kutokana na haja zake za kimwili, basi kumpa huyu mnyonge wa imani kwa ajili ya kumpa nguvu na kuikuza imani yake ni bora zaidi; kwa sababu kuikuza imani ya Mtu ni muhimu kuliko mahitajio ya kiwiliwili .

****

**Swali la 384: Ni nini hukmu ya kutoa Zaka ukampa mwanafunzi?**

**Jibu**: Mwanafunzi ambaye ameacha mambo yote na kushikamana na kutafuta elimu ya sharia ya kiisilam ajapokua anauwezo wa tafuta inafaa kupewa zaka; kwa sababu kutafuta ilimu ya kisharia ni moja katika aina za jihadi katika njia ya Allah, Allah mtukufu ameijaalia jihadi katika njia yake iwe ni upande miongoni mwa pande ambazo zinasitahiki zaka Anasema Allah Mtukufu: [**Wakupewa sadaka ni mafakir, na masikini, na wanao zitu-**

**mikia, na wakutiwa nguvu nyoyo zao, na katika kukomboa watumwa, na wenye madeni, na katika njia ya Mwenyezi Mungu, na wasafiri, huu ni wajibu uliyo faradhishwa na Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni mwenye kujua mwenye hikima**]. Ima ikiwa mwanafuzi yuko kwa ajili ya kutafuta elimu ya kidunia tu yeye hapewi zaka, na tunamuambia wewe sasa hivi unaishuhulikia dunia, unaweza ukajichumia kwa kazi za kidunia hatukupi zaka.

Lakini lau tumepata mtu anaeweza kuchuma kwa ajili ya kula, na kunywa, na kupangisha pa kukaa, lakini ikawa anahitaji kuoa na hana cha kuolea je huyu inafaa tumuozeshe kwa pesa ya zaka? Jibu lake ni ndiyo inafaa tumuozeshe kwa pesa za zaka , na apewe mahali kamili.

kama atahoji mwenye kuhoji akasema nikwa mtizamo gani wakusema fakiri inafaa kumuozesha kwa pesa ya zaka na alikua anapewa vingi?

**Tuna wajibu kusema:** kwakuwa haja ya Mtu kuoa ni dharura zaidi na inawezekana katika baadhi ya wakati ikawa kama kuhitajia kula na kunywa; na kwasababu hiyo wana wachuoni Allah awarehemu wamesema: inajuzu kwa yule ambaye anauwezo wa kumlisha Mtu na kumpa mahitajio mengine ya lazima inafaa kumuozeshapia ikiwa mali yake inatosheleza kufanya hivyo, ni juu yake baba kumuozesha Mwanae anapo hitajia kuoa ikiwa mtoto hana cha kuolea, lakini nimesikia baadhi ya mababa wamesahau waJibu wao na kusau hali za watoto wao, mtoto anapo muambia baba yake anataka kuoa, baba anamuambia mwanae: Owa kwaku-

tumia pesa ya mfuko wako, hii siyo sahihi, ni haramu kwa baba kufanya hivyo kama anao uwezo wa kumuozesha mwanae, na mwanae siku ya kiama atashitakia kama hakumuozesha na alikua na uwezo wa kumuozesha.

**Na kuna suala jengine**: Ikiwa mtu ana watoto wengi wengine wameshafikia umri wa kuoa na akawaozesha na wengine ni wadogo, je inajuzu kwa mtu huyu kutoa wasia katika mali yake kuwa waje waozeshwe watoto wake wadogo wakikua kwa sababu aliwapa aliwaozesha watoto wake wakubwa?

**Jibu**: Haijuzu kwa mtu kama amewaozesha watoto wake wakubwa kuwa aache wasia kuwa watoto wake wadogo wakikua wapewe mahali, lililo wajibu kwake ni mtoto akifikia umri wa kuoa amuozeshe, ama kuusia kwamba baada ya kufa kwake watoto waozeshwe na pesa alizo acha hii ni haramu haifai; na ushahidi wa hilo ni maneno yake Mtume rehema na Amani ziwe juu yake: ((**Hakika Mwenyezi Mungu amempa kila mwenye haki haki yake, hapa usia kwa mrithi**)) [ameipokea Imamu Ahmad 5 / 267; na Abuu Daud: 2870; na Ibnu Maaja: 2713]

****

**Swali la 385: Je inajuzu kutoa Zaka kuwapa wanaopigana jihadi?**

**Jibu**: Hakika Mwenyezi Mungu amejaalia miongoni mwa aina za wanao pewa Zaka ni Mujaahidina wanaopigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, kwahiyo inajuzu kuwapa mujaahidiina pesa ya Zaka, lakini swali ni kwamba ni kina nani hao mujaahidina wanao pigana katika nji ya Mwenyezi Mungu? Mujaahidina wanao pigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, ame wabainisha Mtume wa Mwenyezi Mungu rehema na amani ziwe juu yake wakati alipo ulizwa kuhusu mtu shujaa anaye pigana, na anapigana kwa kuhami, na anapigana ili apate cheo chake, ni yupi katka hao yuko katika njia ya Mwenyezi Mungu? Mtume akatupa mizani na kipimo cha kumjua nani anapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu akasema: ((**Mwenye kupigana kwa ajili ya kulipandisha jina la Allaah niyo liwe juu basi huyo ndiyo yuko katika njia ya Mwenyezi Mungu**)) kwakila mwenye kupigana kwa lengo hilo la kulinyanyua tamko la mwenyezi Mungu liwe juu na kuhukumu kwa sharia ya Mwenyezi Mungu, na kuiyeneza Dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika miji ya makafiri hakika yeye yuko katika njia ya Mwenyezi Mungu; na anapewa Zaka, ima atapewa pesa imsaidie kwenye jihadi, ima kununuliwe vifaa vya maandalizi ya vita.

****

**Swali la 386: Je kutoa pesa ya Zaka ikajengea misikiti pia ni katika kuifuata kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: [Na katika njia ya Mwenyezi Mungu] katika kubainisha watu wanao stahiki kupewa Zaka?**

**Jibu**: Kujenga misikiti hakuingii katika kauli aliyo itaoa Mwenyezi Mungu isemayo: [**katika njia ya Mwenyezi Mungu**] kwa sababu tafsiri ambayo wameitafsiri wafasiri Mungu awarehema: makusudio ya kauli ya Mwenyezi Mungu kusema na katika njia ya Mwenyezi Mungu: makusudia ni kupigana jihadi kwa njia ya mwenyezi Mungu; kwa kua tunge sema: makusudio ya kusema katika njia za Mwenyezi Mungu ni njia zote za kheri isingekua katika kauli yake Mwenyezi Mungu: [**Na hakika sivinginevyo wakupewa sadaka ni mafakiri**]; faida inayo patikana hapa ni kwamba hukumu hii ya kutoa sadaka kuwapa mafakiri imekuja kwa njia ya msisitizo kuonyesha kuwa alicho taja Mwenyezi Mungu kuwa zaka igawanywe kwa mafakiri nikuonyesha kuwa vingine visivyo kuwa hivyo vilivyo tajwa katika aya haifai kutoa zaka kuziingiza kwenye mambo mengine ambayo siyo yaliyo tajwa; Kisha kama tutapitisha kuwa zaka inaweza kujengea misikiti na njia nyingine za kheri tutakuwa tumeikengeusha kheri; sababu watu wengi wameelemewa na ubakhili, watakapo ona kwamba kujenga misikiti na kwamba njia za kheri inawezekana ikahamishwa zaka basi watazigeuzia Zaka zao huko kwenye njia nyingine za kheri, na masikini na mafakiri bado watakua wakiendelea kuhitaji milele .

****

**Swali la 387: Nini hukumu ya kutoa Zaka na kuwapa watu wako wa karibu au ndugu zako?.**

**Jibu**: Msingi wa kuhukumu katika hili ni kwamba kila Mtu wa karibu ambae mahitaji yake anayapata kwa huyo mwenye kutoa Zaka, haijuzu kutoa Zaka kumpa yeye ambaye ndiyo amekua sababu ya kutoa Zaka kumpa yeye, ama akiwa ndugu ambaye hapaswi kumpa mahitajio yake ya kumlea kama vile kaka akiwa ana watoto, kwani kaka akiwa ana watoto haipasi kwa kaka yake kumlisha na kumpa mahitajio yake kwa kuzingatia kuwa hawezi kumrithi kwa kuwa ana watoto, basi katika hali hii inajuzu kutoa Zaka kumpa ndugu yake kama atakua ni miongoni mwa watu wanaositahiki kupewa Zaka, na vilevile wakiwa ni watu wakaribu ambao hawahitajii Zaka katika mahitajio yao lakini wakawa wana madeni basi inajuzu kuwalipia madeni yao hata kama niwatu wakaribu kwa baba, au watoto wa kiume, au watoto wa kike, au baba wadogo au baba wakubwa; muda wakua hayo madeni ambalo wanadaiwa siyo sababu ya kupunguza katika mahitajio.

Mifano ya hilo: Mtu Mtoto wake alikua anaendesha gari na akapata ajali na Mtoto huyo akalazimishwa alipe ghalama ya ile gari aliyo igonga au aliyo gongana nayo, na Mtoto akawa hana pesa yakuweza kulipia ghalama za gari hiyo, basi inajuzu au inafaa kwa baba kumlipia mwanae ghalama za gari hiyo kutoka kwenye zaka yake - yani: katika Zaka ya baba; kwakuwa hiyo aliyo ighalamia haikuwa sababu yake ni matumizi, bali nijambo ambalo limembidi halina mafungamano au makubaliano, na kama hivyo

kila ambaye ametoa zaka kumpa mtu wake wa karibu ambaye mtoaji Zaka hawezi kutoa pesa yake pasi na sababu ya Zaka ikiwa nihivyo basi inajuzu kumpa Zaka .

****

**Swali la 388: Je utoaji Zaka na sadaka umuhimu wake ni kwa ajili ya mwezi wa Ramadhan tu?**

**Jibu**: Utoaji Zaka na sadaka nisiku zote unahitajika siyo kwa ajili ya mwezi wa ramadhani tu, bali nijambo linalo takikana na ni sharia kutolewa kila muda wowote, na zaka inapashwa kwa Mtu aitoe pindi tu mali yake inapo timiza mwaka na siyo asubirie Ramadhani, ila itakapokuwa Ramadhani iko karibu kwa mfano mzunguko wa mwaka katika biashara yake ni mwezi wa shaaban akaamua kusubiri iingie Ramadhani hili halina tatizo mana nim karibu, ama ikiwa Mzunguko wa mwaka ni katika mwezi wa Muharram kwa mfano hapo haijuzu kuichelewesha zaka mpaka Mwezi wa Ramadhan, lakini inajuzu na kufaa kuitanguliza zaka yake katika ramadhani kabla ya Muharram wala sio vibaya kufanya hivyo, ama kuichelewesha zaka ukapita ule wakati wake wa kisheria uliyo wekwa hii haijuzu wala haifai kabisa; kwakuwa umuhimu wake na ulazima wake uliyo wekwa na sharia umefungamana na muda huo basi inapashwa kutolewa zaka wakati un-

apoingia muda huo ambao ndiyo sababu ya kutoa zaka na haijuzu kabisa kuichelewesha zaka kuiepusha na wakati huo; Kisha nikwamba Mtu hana dhamana kwamba akichelewesha kutoa zaka ata bakia kuwa hai mpaka huo wakati aliyopanga kutoa zaka hiyo, mana anaweza akafa na akajikuta anakufa na dhimma hiyo, kwa kuwa wanao mrithi wanaweza wasifahamu kuwa anadhima hilo, sababu hii na sababu nyinginezo nyingi amabazo inahofiwa kama Mtu atazembea katika kutoa zaka yake baadae iakamuwia vigumu na akashindwa kutoa zaka yake.

Ama sadaka: sadaka haina muda maalumu, siku zote za mwaka ni wakati wakuweza kutoa sadaka, lakini watu wanachagua na kupendelea kutoa sadaka zao katika mwezi wa Ramadhan; kwa sababu ni wakati bora; wakati uliyo mzuri zaidi na uliyo bora zaidi, na alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu rehema na amani ziwe juu yake ni mtoaji zaidi kuliko watu wengini na nimtoaji zaidi kwa yale ambayo yanakuwa katika ramadhan wakati anapokutana na malaika Jibril na anamfundisha Qur'an, Sahihi bukhary katika mlango uliyo itwa vipi ulianza wahai: 6, na Sahihi Muslim: 23008), lakini inapaswa tufahamu kuwa ubora wa zaka au sadaka katika Ramadhan ni ubora amabao una mafungamano na wakati, itakapo kuwa hakuna malipo mengine ya ziada basi katika wakati huu ni bora kutoa sadaka kuliko wakati mwingine, ama itakapokuwa kuna malipo mengine ya ziada kutokana na ubora wa kutoa sadaka katika wakati huo, kwa mfano: ikiwa mafakiri wana shida zaidi ya kupewa msaada au sadaka katika mwezi wa Ramadhani kuliko wakati mwengine ambao siyo wa ramadhani hakika haifai kuichelewesha sadaka mpaka ramadhani, bali linalo takikana nikutizama muda au zama ambazo zina faa na zina manufaa zaidi kwa masikini na mafakiri, nikutoa sadaka wakati huo kwakuwa wanahitajia zaidi, na mara nyingi masikini kipindi

ambacho siyo cha ramadhani wanakuwa masikini zaidi na wenye shida zaidi kuliko wakati wa ramadhani, hii ni kwasababu wakati wa ramadhani  sadaka zinatolewa kwa wingi kwahiyo masikini na mafakiri unawakuta wametosheka kwa zile sadaka wanazo pewa, lakini kwenye miezi mingineya mwaka wanakuwa mafakiri zaidi, kwa sababu watu hawatoi sadaka, kwahiyo watu inawabidi kuchunga sana katika maswala haya wasitazame zaidi manufaa ya muda au wakati wakaacha kutizama ubora na ulazima uliyopo kwenye jambo lenyewe na wakatanguliza ubora wa wakati kuliko kila kitu.

****

**Swali la 389: Je Swadakatun jaaria (Sadaka yenye kuendelea): ni ile ambayo aliitoa Mtu katika uhai wake au ni ile ambayo wametoa ndugu zake kwa ajili yake baada ya yeye kufa?**

**Jibu**: Uwazi uliopo katika kauli ya Mtume rehema na amani iwe juu yake alipo sema: ((**Isipokua sadaka yenye kuendelea**)); [Sahihi Muslim: 1631].  yaani - alikusudia maiti mwenyewe na siyo ile ambayo wameitoa watoto wake baada ya yeye kufa; kwa kua ambayo yanafanywa na Mtoto ameyaweka wazi Mtume rehema na amani ziwe juu yake pale alipo sema: ((**Mtoto mwema**

**anae muombea**)); Maiti ikiwa alitoa usia wa kuwa kitu Fulani kiwe ni sadaka au alitoa waqfu kitu chochote basi kwake kitu hicho kinakua ni sadakatu jaaria yani - sadaka yenye kuendelea, basi kitu hicho atanufaika nayo baada ya kufa kwake; na vile vile ilimu aliyo ifundisha inakua ni miongoni mwa mambo yanayo ya chumia thawabu, na vilevile Mtoto atakapo muombea mzazi wake; kwahiyo kama tutaulizwa: je ubora ni kuswali rakaa mbili kwa ajili ya mzazi wangu, au ubora nikuswali mimi mwenyewe rakaa mbili kisha nika muombea mzazi wangu katika rakaa mbili hizo?

Tutamjibu kuwa: bora ni kuswali rakaa mbili kwa ajili yako, na kisha unamuombea mzazi wako , kwa kuwa hili ndiyo alilo tuelekeza Mtume rehema na amani iwe juu yake pale aliposema: ((**Au mtoto mwema atakae muombea** )); na mtume hakusema: aswali rakaa mbili kwa ajili mzazi wake au afanye amali nyingine.

****

**Swali la 390: Je inajuzu kwa mwanamke ajitolee sadaka kwenye mali ya mume wake au amtolee Mtu mwingine katika jamaa zake? yani - jamaa wa mwanamke.**

**Jibu**: Inavyofahamika ni kwamba mali ya mwanamume ni ya mwanamume, haifai kwa Mtu yoyote atoe sadaka katika mali ya Mtu yoyote isipokua kwa ruhsa yake huyo mwenye mali, Mwanamume akimpa ruhsa mke wake ajitolee sadaka, au amtolee yoyote anaemtaka hakuna vibaya kwa kuwa ameruhusiwa na mwenye mali, kama hakumpa idhni au ruhsa haijuzu na haifai kwa mwanamke atoe sadaka ya chochote katika mali hiyo ya mumewe; kwa sababu mume ni mali yake na sihalali kwa Mtu yoyote Muislam kutumia mali ya mtu mwingine isipokua Mtu akiitoa mali hiyo kwa mapenzi ya nafsi yake.

****

**Swali la 391: Mtu masikini anachukua zaka kutoka kwa rafiki yake tajiri kwa madai kuwa sadaka hiyo ataigawa kwa watu kisha anaichukua yeye; je nini hukmu ya kufanya jambo hilo?**

**Jibu**: jambo hili ni haramu kwake kulifanya, na ni kukosa uaminifu; kwa sababu rafiki yake anampa kwa kumuwakilisha ili atoe kwa wengine, na yeye anajichukulia mwenyewe, wamesema wana wachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu: kwamba wakili alietumwa haifai ajitolee sadaka yeye mwenyewe katika mali aliyo pewa akaigawe , linalotakikanani Mtu awe muwazi kwa Mwenzie

kuwa anacho kichukua kutoka kwake ana chukua yeye, akimruhusa sawa, na asipo mruhusu basi hilyo ni dhamani; yani-anakua na dhamana ya kulipa sadaka hizo kwa ajili ya kutekeleza zile zaka alizokua amezikusudia mwenzie .

Kwahiyo hapa napenda niwa tahadharishe baadhi ya watu kwa mambo wanayo yafanya kwa kuto kufahamu kwao,  mambo nayo: ni kwamba mtu ni masikini baadae Mwenyezi Mungu ana mjaalia utajiri na huku watu wanaendelea kumpa sadaka zao wakijua kuwa bado ni masikini, kisha anazipokea, najingine ni kwamba kuna watu wanachukua sadaka na wanazila kisha wanasema: mimi sijawaomba watu wanipe, bali hii ni rizki kaniletea Mungu; hii ni haramu kabisa; Kwa kua aliye mtajirisha Mwenyezi Mungu amemharamishia kuchukua kitu chochote katika zaka.

Na miongoni mwa Watu kuna kuna wanaochukua zaka za watu kisha wanazigawa kwa watu wengine bila ya kupewa idhini na wenye zaka zao hili pia ni haramu na sihalali kwake kuigawa zaka hiyo, ni haramu kwake kufanya hivyo, na inampasa alipe zaka hiyo kwa mwenyewe ikiwa hakumruhusu kutoa zaka hiyo.

****

****

## Swali la 392: Nini hekma ya kufaradhishwa kwa Swaumu ?

**Jibu**: Tukisoma kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu inayo sema :

[**Enyi mlio amini! mmelazimishwa kufunga, kama walivyo andikiwa waliyo kuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu**]

(Surat Baqara: 183), tumefahamu ni ipi hikma ya kufaradhishwa kufunga swaumu na hikma yenyewe ni kumcha Mwenyezi Mungu na kufanya ibada kwa ajili yake, na kumcha ni kuacha yale aliyo ya haramisha, na kufanya yaliyo amrishwa na amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Amabaye haachi maneno ya uwongo na kuutumia na ujinga hapana haja kwa mwenyezi Mungu kwa mtu huyo kuacha chakula chake na kinywaji chake**)); [Sahihi Bukhary: 1903], kwahiyo awe na uhakika Yule aliye Funga kutekeleza wajib na vile vile kujiepusha na mambo yaliyo haramishwa kwa kuongea na kutenda, na asiwasengenye watu, wala asiseme uwongo, wala asieneze maneno ya uwongo kwa watu, wala asiuze biashara za haramu, na ajiepushe na mambo yote yaliyo haramishwa, na Mtu atakapo fanya hivyo kuacha mambo ya haramu na kufanya mambo mema mwezi mzima basi

nafsi yake huenda ikawa katika muelekeo uliyo nyooka mwaka mzima.

Lakini kwa masikitiko makubwa ni kwamba wafungaji wengi hawatofautishi kati ya masiku ya swaumu zao na masiku wanayo kula mchana ambayo siyo masiku ya kufunga, wao wanabakia katika mazoea yao ambayo walikua nayo kwa kuacha mambo ya wajibu, na kufanya mambo ya haramu, wala hahisi kwamba ana utulivu wa swaumu; na vitendo hivi haviharibu swaumu lakini vinapunguza malipo yake, na huenda wakati wa kulinganisha matendo hayo maovu na swaumu ukakuta zinapotea thawabu za swaumu yake.

****

**Swali la 393: Kuna mwenye kutangaza kuunganisha machimbuko yote ya mwezi kuwa yafuate makkah kwa lengo la kuukusanya umma katika kuingia mwezi mtukufu wa Ramadhan na miezi mingine nini rai yenu katika hili?**

**Jibu**: Hili ukilitizama kwa upande wa kutizamia mwezi kwa vipimo vya watu wa anga ni jambo ambalo haliwezekani; kwasababu machimbuko ya mwezi kama alivyo sema Ibnu Taymiyah Mwenyezi Mungu amrehemu katika kitabu chake kiitwa-

cho Fataawal Kubra: machimboko ya mwezi yana tofautiana kwa makubaliano ya watu wenye kufahamu  ilimu hii, na kama machimbuko ya mwezi yana tofautiana basi kwakuangaria dalili na mtizamo ni kufanya kila mji au nchi kuwa na hukmu yake .

Ama dalili za athari; amesema Mwenyezi Mungu [**Atakae ushudia Mwezi miongoni mwenu basi afunge**] [Surat Baqara: 185], na kama ikikadiriwa kuwa watu katika sehemu ya mbali hawakuuona mwezi - yani mwezi muandamo, na watu wa makkah wame uona mwezi; viti itaelekezwa kauli katika aya hii kwa yule ambae hakuona mwezi?! na amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((F**ungeni kwa kuonekana mwezi na fungueni kwa kuonekana mwezi**)) wanachuoni wa hadith wamekubanliaa katika hadith hii  (Sahihi Bukhaary: 1909 na Sahihi Muslim: 1081).

Kwahadith hii watakapo uona mwezi watu wa makkah kwa mfano vipi tuta walazimisha watu wa pakstani na waliyo nyuma ya paksitani kuwa na wao wafunge, pamoja yakua tunafahamu kwamba mwezi haukuchomoza katika upande wao, na mtume rehema na amani ziwe juu yake: ameiweka mafungamano ya swaumu na kuona mwezi.

Ama dalili ya kimtizamo ni makisiyo yaliyo swahihu ambayo yako wazi, sisi tunafahamu ya kuwa alfajiri inachomoza katika upande wa mashariki kabla ya upande wa magharibi, ikichomoza alfajiri katika upande wa mashariki je sisi inapashwa tujizuilie na kula na kunywa na kwetu niusiku? Jawabu: ni hapana; na likizama jua katika upande wa mashariki lakini sisi kwetu ni mchana je inajuzu kwetu sisi tufungue? Jibu ni: hapana; kwa hiyo mwezi ni kama jua; mwezi machimbuko yake yanakua nikwa mwezi , na jua machimbuko yake niya siku; na ambaye amesema: [**Mme halalishiwa usiku wa swaumu kuingiliana na wake zenu. Wao ni**

**vazi kwenu na nyinyi ni vazi kwao. Mwenyezi Mungu anajua kwamba mlikua mkizikhini nafsi zenu .kwa hiyo amekukubalieni toba yenu na ame kusameheni. Basi sasa changanyikeni nao na takeni alio kuandikieni Mwenyezi Mungu. Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku. Kisha timizeni swaumu mpaka usiku. Wala msichanganyike nao .na hali mnakaa itikafu msikitini. Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu , Baasi Msiikaribie. Namna hivi Mwenyezi Mungu ana bainisha ishara zake kwa watu ili wapate kumcha**] na ndiyo huyo aliyesema:

[**Atake shuhudia mwezi miongoni mwenu basi afunge**] kwa kuzingatia dalili zote: nikufanya kila sehemu pawe na hukumu yake tu kwa yale yanayo husiyana na kufunga na kufungua, udhibiti wa hili ni hisiya amabazo Mungu katika kitabu chake na kupitia mtume wake Muhammad katika Sunna zake nazo ni kuushuhudia mwezi na jua, na waoshudia jua au alfajiri.

****

**Swali la 394: Atakapo safari mfungaji kutoka katika mji wake na kwenda mji mwingine na ikatangazwa katika mji aliyo toka kuwa mwezi wa kufungua umeonekana je anafungua kwa kuwafuata wale wa mji aliotoka? pia ifahamike kuwa mji huu wa pili aliyo fikia mwezi hauja onekana?**

**Jibu**: Mtu atakapo safari kutoka mji wa kiislamu kwenda kwenye mji wa kiislam kisha mji huu aliyo kwenda wakachelewa kufungua basi anabaki na swaumu yake mpaka hao wenye mji wafungue; kwakua swaumu ni siku wanao funga watu, na kufungua ni siku wanayo fungua watu, na adhuha ni siku watu wanayokuwa kwenye chinja watu, nah ii kama atazidisha siku moja au zaidi hakuna tatizo sababu ni kama ambaye amesafiri kwenda kwenye mji amabao jua lake linachelewa kuzama , inaweza kuzidi siku kwa kawaida kama masaa mawili , au matatu , au zaidi, na kwakua alipotoka kwenda mji wa pili mwezi ulikua hauja zaliwa, na Mtume ameamrisha tusifunge ila kwa kuonekana mwezi na vile vile akasema ((**Fungueni kwa kuonekana mwezi**)).

Na kinyume chake mfano amesafiri kutoka kwenye mji ambao umechelewa kuandama mwezi na kwenda kwenye mji ambao mwezi umewahi kuandama basi atakula pamoja nao, na atalipa swaumu atakazo ziwacha au zilizo mpita, kama itampita siku

moja atailipa siku moja na zikimpita siku mbili basi atalipa siku mbili, na tumesema analipa kwakua mwezi haiwezekani upungue iwe ni siku ishirini na tisa, au uzidi zaidi ya siku thelathini, na tulimuambia afungue japo hazijatimia siku ishirini na tisa; kwakua mwezi wa shauwali umeonekana, na ukionekana hapana budi kufungua, na ulipokua umepungua chini ya siku ishirini na tisa; ni kwakua mwezi haiwezekani upungue zaidi ya siku ishirini na tisa, umelazimika kutimiza siku ishirini na tisa, kinyume na suala la mwanzo huwezi fungua mpaka uone mwezi, ukito uona basi wewe unakua bado uko ndani ya ramadhani - sasa utafungua je; ni lazima ufunge, na kama mwezi utazidi basi ni kama kuzidisha masaa Fulani katika siku.

****

**Swali la 395: Ni ipi rai yenu kwa Mtu ambaye kazi zake ni Ngumu na swaumu kwake ikawa ni ngumu; Je afungue?**

**Jibu**: Ambaye anaona kuwa afungue kwa ajili ya kazi hii ni haramu haifai, na kama itakua haiwezekani kwake kufunga na ku-

fanya kazi pamoja basi ni bora achukue likizo au apumzike kazi hiyo katika ramadhani ili afunge kwanza kwa sababu swaumu ya ramadhani ni nguzo miongini mwa nguzo za uislam haifai kuipuuza .

****

**Swali la 396: Msichana mdogo ameingia katika hedhi na alikua akifunga wakati akiwa kwenye hedhi kwa kuto kufahamu; anapaswa kufanya nini?**

**Jibu**: Anapaswa kuzilipa swaumu ambazo alikua akizifunga wakati yuko kwenye damu ya hedhi; kwa sababu swaumu katika siku za hedhi haikubaliwi wala haiswihi hata kama alikua hajui; kwa sababu kulipa hakuna mpaka kuwa mpaka muda Fulani ni mwisho wa kulipa.

Na kuna suala jingine kinyume cha suala hili: Mwanamke imemjia hedhi na ni mdogo, akaona aibu kumuambia mama yake au mlezi wake na akawa hafungi, huyu inampasa kulipa mwezi ambao hakuufunga kwa sababu mwanamke anapo balehe anaingia katika mambo ya sharia na akifanya baya anapata dhambi na akifanya jema anapata thawabu; na hedhi ni moja katika alama za balehe .

****

**Swali la 397: Mtu aliacha swaumu ya Ramadhan kwa ajili ya kutafuta maisha na maisha ya wale waliyo chini yake katika kizazi chake nini hukmu yake?.**

**Jibu**: Huyu Mtu alie acha kufunga kwa ajili ya kutafuta maisha yake naya watoto wake, ikiwa kitendo hicho ni kwa mtizamo wa kudhani kua yeye ni kama alivyo ruhusiwa mgonjwa kufungua, inaruhusiwa kwa yule ambae hawezi kuishi ila kwa kufungua, basi huyu mwenye mtizamo huu analipa ramadhani akiwa yuko hai au afungiwe akiwa amekufa, na akito mfungia mzazi wake au msimamizi wake basi wanalishwa masikini kwa niaba yake kwa kila siku masikini mmoja.

Ama atakapo acha kufunga pasi na kuweka wazi basi kauli iliyo swahihu katika kauli za wana wachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu

Ni kwamba: kila ibada na wakati maalumu mtu akikusudia kutoifanya katika wakati wake bila ya udhuru wowote hakika hilo halikubaliki kwake, na anatakiwa kufanya amali njema , na kufanya Sunnah kwa wingi na kutaka msamaha, na ushahidi wa hilo ni kauli yake Mtume rehrma na amani ziwe juu yake katika yale yaliyo swihi kutoka kwake: ((**Mwenye kufanya jambo lolote ambalo si katika dini yetu basi jambo hilo nilenye kurudishwa**)), ibada yenye wakati maalumu haifanywi kabla ya wakati wake, na vile vile haikubaliki kufanywa baada ya wakati wake; Ama itakapo kuwa kuna udhuru kama kuto kufahamu na kusahau, basi hakika Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema: ((**Mwenye kulala wakati wa swala au akaisahau basi ataiswali**

**atakapo kumbuka, hatatoa kafara ila hilo la kuswali**)) pamoja na kwamba kutokufahamu kuna kuwa na ufafanuzi, ila hapa siyo sehemu yake ya kuelezea hilo.

****

### Swali la 398: Ni nyuzuru gani zinazo ruhusu Mtu kuacha kufunga?.

**Jibu**: Nyuzuru ambazo zinamruhusu mtu kuacha kufunga: ni maradhi, na safari, kama ilivyo kuja katika Qu'rani; na miongoni mwa nyuzuru: Ni mwanamke akiwa Mja mzito akiwa anamuogopea kiumbe kilichoko tumboni kwake au kujiogopea yeye mwenyewe na Mwanamke anae nyonyesha anaeogopa kama akifunga atakua hana nguvu za kunyonyeshea au anaogopa mwanae atakosa maziwa ya kutosha, na vile vile kama Mtu atahitajia kufungua kwa ajili anataka kumuokoa mtu mwenye matatizo kwa mfano mtua anazama katika maji au hatari yoyote ambayo hawezi kutoa msaada ila awe amefungu basi anaweza kufungua kwa ajili ya kutoa msaada huo, na vile vile kama Mtu anahitajika kufungua ilia pate nguvu akiwa kwenye jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, hiyo pia ni sababo ya kumfanya yeye kuto kufunga; kwa sababu Mtume rehema na amani ziwe juu yake alisema kuwaambia maswahaba wake siku ya vita vya Fat-hi: ((**Hakika nyinyi mtakutana na**

**maadui kesho, na kufungua kutawafanya muwe na nguvu zaidi basi fungueni**)) (Sahihi Muslim: 314), ikipatikana sababu inayo ruhusu kufungua, na Mtu akafungua basi halazimiki kujizuiya na kuto kula mchana huo au siku hiyo, na kama ikikadiriwa kuwa Mtu amefungua kwa ajili ya kumuokoa Mtu asie kuwa na hatia akiwa ana angamia basi ataendelea kuwa hakufunga na kuendele kula kwa siku nzima tangu alipo muokoa huyo aliye kuwa akizama; kwa kuwa amefungua kwa sababu ambayo imekubaliwa kisheria hailazimu kumuambia amefungua lakini asiwe ana kula kwa kuwa watu wamefunga; na imeharamishwa kula mchana, kwakua kuacha kufunga kaacha kisheria, na kauli iliyo swahihu katika hili ni kwamba ataendelea kula kwa siku hiyio nzima: na kama ni mgonjwa amepona mchana na alikua hakufunga basi anaendelea kula wala hailazimu kuwa ajizuie na kula, na kama ni msafiri amefika safari yake mchana na alikuwa hakufunga pia haimlazimu kujizuia na kula bali ataendelea kula sehemu ya mchana iliyo baki, na vile vile kama mwanamke alikuwa kwenye hedhi na ikakatika katikati ya mchana akajitwaharisha pia ataendelea kula mchana uliyo baki, kwa sababu hawa wote wame fungua kwa sababu ambazo zina kubalika kisheria, na ndiyo mana siku hiyo ikawa halali kwake yeye kula na hakuna uharamu wowote, na hii ni tofauti na kwamba lau itathibitika kuwa umeingia mwezi wa ramadhani mchana basi inalazimu kujizuia na kutokula mchana uliyo baki, na tofauti kati ya mambo haya mawili la kuacha kufunga kwa sababu za kisheria na kuacha kufunga kwa kutokufahamu kabla ya hapo kuwa mwezi umeandama ni kwamba: utakapo patikana ushahidi wa kuwa mwezi umethibiti katikati ya mchana basi niwajibu kujizuia na kula, lakini kabla yahapo niwenye udhuru wa kuto kujua, kwa hiyo kama wangekua wanafahamu kuwa leo ni ramadhani inge walazimu kujizuilia na kula, Ama wale watu wengine tuliyo

wataja wameruhusiwa kufungua pamoja na kua wanafahamu kua wako kwenye ramadhani, kwahiyo wana tofauti zilizo wazi kabisa.

****

**Swali la 399: Mtu amelala usiku wa kwanza katika Ramadhan kabla ya kuthibitika kuonekana kwa mwezi, na hakulala na nia ya swaumu, baada ya kupambazuka akafahamu kuwa ni Ramadhan, atafanya nini katika hali kama hii? Na je atailipa siku hiyo?**

**Jibu**: Mtu huyu ambae amelala usiku wa kwanza na hakulala na niya ya swaumu, kisha akaamka akafahamu kuwa yumo kwenye ramadhani, inampasa kujizuilia na kula na itampasa kulipa siku hiyo kwa mapatano ya wana wachuoni Allaah awarehemu , na hakuna kauli iliyo pinga kauli hiyo ya wana chuoni, isipokua shekh ibin taimiya yeye alisema: hakika nia inafuatana na kufahamu na huyu hakufahamu, yeye anaudhuru katika hilo, hakuacha kulala na nia baada ya kufahamu, bali alikua hajui , na asiye jua ana udhuru, kwahiyo akijizuilia na kula tangu alipo fahamu kuwa yuko kwenye ramadhani swaumu yake ni swahihu , wala hatalipa,

Ama kauli ya jopu la wanachuoni wamesema : inamlazimu ku-

jizuilia na kula, na inamlazimu kulipa, na wakasema kwa sababu nusu au baadhi ya mchana imempita bila ya kuwa na nia ya kufunga, na kwa mtizamo wangu mimi ni kwamba aje kuilipa siku hiyo.

****

**Swali la 400: Mtu Atakapo fungua kwa udhuru wa kisheria kisha ule udhuru ukaondoka katikati ya mchana je atajizuilia na kula katika sehemu ya mchana iliyobaki?**

**Jibu**: haimlazimu yeye kujizuilia na kula, kwa sababu huyu mtu ameruhusiwa siku hiyo kufungua kutokana na dalili za kisheria, sharia imetoa ruhusa kwa yule aliye shikika na tatizo kama ugonjwa na mengine tuliyo yataja akapewa nafasi ya kufungua kwa kunywa dawa na akafungua akala kwahiyo siku hiyo sihaki yake kufunga bali atakuja kuilipa, kumlazimisha kuwa ajizuilie na kula, ni kujizuia kusiko na faida yoyote, kwahiyo ikiwa mtu huyu hapati faida yoyote kwa kujizuia kwake hatumlazimishi kufanya hivyo.

Mifano ya swala hilo: Mtu ameona mtu mwingine ana zaka katika maji, akasema: nikinywa maji nitaweza kumuokoa na nikito kunywa maji sitoweza kumuokoa, akanywa na akamuokoa, atakula na atakunywa mchana uliyo baki; kwakua Mtu huyu siku hii haikua siku yake aliyo ruhusiwa kufunga kisheria, haimlaz-

imu yeye kujizuilia na kula, na lau kuna Mtu ni mgonjwa; je tutamuambia kuwa usile mpaka usikie njaa na usinywe mpaka usikie kiu? kwa maana ya kuwa usile wala usinywe isipokua kwa kutizama dharura iliyo mfanya asifunge, hatuwezi kumuambia hivyo, kwakua ameruhusiwa na sharia afungue, kwa kila mwenye kufungua katika ramadhani ni kwa muJibu wa sharia haimlazimu kujizuilia  na kinyume chake, mwenye kufungua pasi na udhuru wa kisheria inamlazimu kujizuilia, kwa kuwa hana ruhsa ya kufungua, kwani amevunja heshima ya siku hii pasi na idhini ya sharia, hivyo itamlazimu yeye kujizuilia na kula siku hiyo na atakuja ilipa pia Mwenyezi Mungu ndiyo Mjuzi zaidi.

****

**Swali la 401: Mwanamke amepatwa na maradhi ya kuota uvimbe tumboni, madaktari wakamkataza kufunga hukumu yake nini?**

**Jibu**: Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Mwezi wa Ramadhan ambao imeteremshwa humo Qu'rani kuwa ni uwongofu kwa watu, nani hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi. Basi atakae ushuhudia mwezi katika nyinyi naafunge. Na mwenye kuwa Mgonjwa au aliyoko safarini basi atatimiza hesabu ya kufunga katika masiku mengine. Na Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyomazito**] [Surat Baqara: 185] Mtu akiwa ni mgonjwa ugonjwa

ambao hautarajiwi kupona kwake, basi kila siku atamlisha masikini, na jinsi ya kumlisha ni hivi: ni kuwagaiya mchele, na iliyo bora ni kuwapa na kitoweo nyama au kingine kisicho kua nyama, au awaalike masikini katika cha kula cha usiku, au cha mchana, hii ndiyo hukumu ya mgonjwa ambae ugonjwa wake hautarajiwi kupona yani ni wamaisha hadi kufa kwake, na huyu mwanamke aliye mtaja muulizaji ni miongoni mwa wagonjwa wa namna hiyo, kwa hiyo inampasa amlishe masikini kila siku.

****

**Swali la 402: Ni wakati gani inakua swala ya msafiri na inakuwaje? Na vipi atafunga swaumu?**

**Jibu**: Swala ya msafiri ni rakaa mbili ina anzia wakati akishatika kwenye mji wake mpaka atakapo rudi; kwa kauli ya Aisha radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake amesema: ((**Mwanzo wa kufaradhishwa swala ilifaradhishwa rakaa mbili, ikawa swala ya msafiri na kutimiza kwa asie kuwamsafiri**)), na katika mapokezi mengine: ((**Na ikazidishwa katika swala ya aliyoko mjini yani ambae siyo msafiri)),** (Sahihi Bukhary: 1090, na Sahihi Muslim: 680), na akasema Anasi bin Maaliki radhi Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: ((**Tulitoka pamoja na Mtume rehema na amani ziwe juu yake: tulitoka Madina kuelekea Makkah Akaswali Rakaa**

**mbili mbili mpaka tulipo Rudi madina**)) [hadith hii kaipokea Bukhari: 1081, na Muslim: 693]

Lakini Msafiri atakapo swali pamoja na Imamu atatimiza rakaa nne, iwe ameanza swala na Imamu au awe amechelewa baadhi ya rakaa; kwa maelezo kamili ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema :

((**Mtakapo isikia Iqama basi iyendeeni swala kwa upole na utulivu , wala msiikimbilie, sehemu mtakayo ipata swalini, na sehemu mtakayo ikosa itimizeni**)), yani - mkienda kuswali msikimbie muende taratibu ,ukimkuta imamu kwenye rakaa yoyote mfuate, akishatoa salamu mmalizie rakaa zilizo wapita ambazo hamkuswali na imamu…. Na kauli hii ya mtume inajumuisha Wasafiri na wote ambao wanaswali nyuma ya Imamu, Na aliulizwa Ibinu Abaasi Allaah amrehemu: hajaacha Msafiri kuswali rakaa Mbili akiwa peke yake na kuswali rakaa nne akitimiza kwa mkazi wa mji? akasema : ((**Hiyo ndiyo Sunna**)).

Na swala ya jamaa haipomoki kwa msafiri; Kwa kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ameiyamrisha hata katika vita ni lazima kuswali jamaa, Amesema: [**Na unapokua pamoja nao, ukawasalisha, basi kundi mmoja kiongoni mwao wasimame pamoja na wewe na wachukue silaha zao. Na watakapo maliza sijida zao basin a warudi nyuma yenu, na lije kundi linguine ambalo halijaSali, lisali pamoja na wewe…**] [Surat Nnisaa: 102]; kwa hii Msafiri atakapo kuwa katika mji ambao siyo mji

wake basi nilazima kwake kuhudhuria swala ya jamaa msikitini endapo anaisikia adhana, isipokuwa kama yuko mbali na msikiti na haisikii adhana, au anachelea kuupoteza msaada wake aliyo nao au jamaa zakea liyo ongozana nao; hii ni kutokana na dalili zilizo wazi zinazo zinazo onyesha na kulazimisha kuswali jamaa kwa kila ambaye anaisikia adhana na iqama popote alipo kama hapana kizuizi cha yeye kutoka kwenda msikitini.

Ama kuswali swala za Sunna: Msafiri anaswali swala zote za Sunna isipo kuwa swala za kabliya na baadiya za swala ya Adhuhuri, na Alasiri, Na Ishaa; na anaruhusiwa kuswali swala ya witri, na swala ya usiku, na swala ya dhuha, na suna za swala ya asubuhi, na nyingine zisizo kuwa hizo katika swala za Sunnahh ambazo siyo kabliya na baadiya isipokua zile ambazo zimetajwa.

Ama kukusanya swala: Ikiwa Msafiri bado yuko safarini kama vile akiwa kwenye kipando kama vile gari au vyombo vingine vya kusafiria au kwa mguu lakini hajafika aendako, basi bora kwake ni kukusanya swala, akusanye Adhuhuri na Alasiri, Magharibi na Ishaa, Ima aswali jamuu takdiim au jamu taakhiir, kuswali jamuu takdiim, yani - aswali adhuhuri na Alasiri wakati wa Adhuhuri, hii ndiyo maana ya jamuu Tak'diim . Au aswali jamuu taakhiir, yani aswali Adhuhuri na Alasiri kwenye wakati wa Alasiri hii ndiyo maana ya jamuu ta akhiiri - yani kukusanya na kuchelewesha, ataswali kulingana na hali ambayo ni nyepesi kwake, kwa hali yoyote itakayo muwia nyepesi basi hiyo ni bora kwake.

Na kama amefika aendako bora ni kuto kukusanya, na kama atakusanya pia hakuna tatizo; kwa kuthibiti mambo yote mawili au hali zote mbili kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake.

Ama swaumu ya Msafiri katika Mwezi wa Ramadhan, iliyo bora kwa Msafiri ni kufunga, na kama ataacha kufunga akiwa safarini pia hakuna tatizo, na atalipa siku ambazo ameacha kufunga, Ikiwa kufungua ni wepesi kwake basi kufungua ni bora; Kwakua Mwenyezi Mungu Mtukufu anapenda kufuatwa fursa au ruhusa alizo zitoa, Na sifa njema niza Mwenyezi Mungu bwana wa viumbe.

****

**Swali la 303: Nini hukumu ya msafiri kufunga pamoja na kuwa kunaugumu katika safari yake?.**

**Jibu**: Swaumu ikimuwia nzito uzito ambao unavumilika basin ni makuruhu kufunga; Kwa sababu Mtume Rehema na amani ziwe juu yake Alimuona Mwanamme Amewekewa kivuli, na watu wamekusanyika pembezoni mwake Akasema Mtume: ((**Ni nini hii**? **watu wakasema: Amefunga, Akasema Mtume: Si katika wema kufunga safarini**)) (hadith ameipokea Bukhary katika kitabu cha Swaumu hadith no 1946. Na Muslim katika kitabu sw-

aumu: 1115) Ima swaumu ikimuwia nzito sana ni waJibu kwake kutokufunga akiwa safarini; kwa kua Mtume rehema na amani ziwe juu yake, kipindi ilipo pewa mashitaka kuwa Watu swaumu imewawia Nzito alifungua, kisha Akaambiwa: Baadhi ya watu wamefunga, Mtume akasema: ((**Hao wamefanya maasi Hao wamefanya maasi**)) (Sahihi Muslim: 1114).

Ama ambae swaumu haimuwii nzito akiwa safarini basi bora kwake ni kufunga kwa ajili ya kumfuata Mtume rehema na amani ziwe juu yake: Alivyo kuwa akifunga, kama alivyo sema Abuu Daudi Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: ((**Tulikuwa pamoja na Mtume rehrma na amani ziwae juu yake katika Ramadhani katika joto kali, Hakuna aliye funga katika sisi isipokua Mtume na Abdullaahi bin rawaaha**)) (Sahihi Bukhary: 1945; na Muslim: 1122).

****

### Swali la 404: Ni ipi hukumu ya msafiri kufunga pamoja na kuwa swaumu siyo nzito kwa mfungaji katika zama za sasa zilizoenea vyombo vya kisasa vya kusafiria?

**Jibu**: Msafiri ana weza kufunga na asifunge; Kwa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo: [**Na atakae kuwa mgonjwa miongoni mwenu au yumo safarini basi atomize hisabu katika**

**siku nyingine**] (Surat Baqara: 185), na walikua maswahaba Allah awarehemu wanasafiri pamoja na Mtume rehema na amani ziwe juu yake, miongoni Mwa maswahaba kuna waliyo funga, na miongoni mwao kuna ambao hawakufunga, na aliye funga hamdharau ambaye haja funga, na alikuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake anafunga akiwa safarini, Amesema Ibin Daudi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

((**Tulisafiri pamoja na Mtume katika joto kali, na hakuna katika sisi aliye funga isipokua Mtume rehema na amani ziwe juu yake na Abdallahi bin rawaaha**)).

Desturi kwa msafiri nikwamba yeye anachagua kati ya kufunga na kuto kufunga, lakini ikiwa swaumu haimsumbui akiwa safarini basi bora kwake ni kufunga; kwa sababu kwenye kufunga kuna faida tatu:

**Faida ya kwanza**: ni kumfuata au kumuiga Mtume rehema na amani ziwe juu yake.

**Faida ya pili**: Ni wepesi, swaumu ina muwia mtu nyepesi wakati akifunga na watu pamoja kuliko akija kufunga peke yake.

**Faida ya tatu**: dhima au deni lina muepuka kwa haraka.

Swaumu ikimuwia nzito basi asifunge, kwani siyo katika wema kufunga safarini katika hali ngumu kama hiyo, Kwa kua Mtume rehema na amani ziwe juu yake alimuona Mtu amewekewa kivuli na watu wamemzunguka Mtume akauliza akasema: **((Ni nini hii**)) watu wakamjibu wakasema: Amefunga, Akasema Mtume: ((S**i wema kufunga safarini**)). Hadithi hii inakua ni yenye kuenea kwa kila ambaye akifunga anakua katika hali mbaya kama ya huyu mwanaume ambaye swaumu ilikua nzito kwake.

Na mpaka hapa tunasema: Safari katika zama zetu hizi ni nyepesi - kama alivyo sema muulizaji - mara nyingi swaumu kufunga zama hizi siyo tabu, Ikiwa swaumu haiwi nzito basi bora ni kufunga.

****

**Swali la 405: Msafiri atakapofika Makkah akiwa kafunga je anaruhusiwa kufungua ili apate nguvu za kufanyia ibada ya Ummrah?**

**Jibu**: Tunasema: Mtume aliingia Makkah Mwezi ishirini katika ramadhani katika Mwaka wa fat'hi, Na alikua hajafunga, na akawa ana swali rakaa mbili katika watu wa makkah, na anawaambia watu wa makkah: ((**Enyi watu wa makkah! Timizeni swala, kwani hakika sisi tuko safarini**)), na imethibiti katika kitabu cha swahihi Bukhaary: kwamba: hakika Mtume rehema na amani ziwe juu yake: alikuwa amefungua sehemu iliyo baki katika mwezi ; kwakua yeye alikua safarini, (Sahihi Bukhary: 4275, Sahihi Muslim: 1113).

Safari ya mwenye kwenda kufanya ummarah haikatiki kwa yeye kuingia makkah, wala halazimiki kujizuilia na kula kama ameingia makkah hajafunga, na huenda watu wengine wakaendelea na swaumu zao hata wakiwa safarini, kwa mtizamo wa kwamba kufunga ukiwa safarini hakuna ugumu kwa watu kutokana na zama zetu hizi, Mtu akaendelea na swaumu yake akiwa safarini, kisha anafika makkaha yuko hoi amechoka, huku akijiuliza nafsini mwake, je! Niendelee na swaumu yangu, na nifanye ummara baada ya kufuturu, au nifungue ili niitekeleze ibada ya Ummrah haraka nitakapo fika makkah?

Sisi tuna muambia kutokana na hali hii: Bora ni ufungue na utekeleze haraka ibada yako ya ummrah pindi tu uingiapo makkah na wewe ukiwa umechangamka; Kwakua Sunna ya mwenye kuingia makkah kwa ajili ya kutekeleza ibada ni afanye haraka kwenda msikitini kutekeleza ibada hii ya ummrah, kwa kua Mtume rehema na amani ziwe juu yake: alikua akiingia Makkah kwa ajili ya ibada basi hukumbilia Msikitini, mpaka mnyama wake alikua akizunguka zunguka maeneo ya msikitini, na anaingia Msikitini ili atekeleze ibada yake ambayo alishaikusudia kuifanya, kwa wewe mwenye kutaka kufanya Ummrah utafungua mchana ili utekeleze ibada yako ya ummrah ukiwa mchangamfu, pia bora kubaki swaumu, kisha wakati ukifuturu usiku unatekeleza ummarah yako, ((**Na imethibiti kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kwamba yeye alifunga wakati yuko katika safari yake alipokua anaenda katika vita vya fat'hi, wakamjia watu waka muambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hakika watu imewawia nzito swaumu, na wao wanakusubiri wewe kitu gani utafanya, na huo ulikua ni wakati wa Alasiri, akaagizia maji Mtume rehema na amani ziwe juu yake: akayanywa, na watu wakisubiria, Mtume akafungua katikati ya safari yake rehema na amani ziwe juu yake, bali alifungua mwisho wa siku**)), (Sahihi Muslim: 1114], yote haya aliyafanya Mtume ili abainishe na kuweka wazi kwa umma wa kiislamu kuwa jambo hilo lina faa, kwahiyo kuwalasimisha watu wafunge wakiwa safarini pamoja na tabu au uzito wa swaumu hii bila shaka ni kuenda kinyume na Sunna, na nisehemu ya kuitekeleza kauli ya Mtume isemayo ((**Siyo katika wema kufunga katika safari**)).

****

**Swali la 406: Je inajuzu kwa mwanamke mwenye kunyonyesha afungue, na niwakati gani atalipa? na je anawalisha masikini?**

**Jibu**: Mwanamke mwenye kunyonyesha akiwa anaogopa kufunga kwa ajili ya mtoto wake, kwamba akifungua maziwa yatapungua na motto atadhurika; basi ata fungua ataacha kufunga, lakini atalipa baadae kwakua yeye anafanana na mgonjwa ambaye amemtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Basi atakae ushuhudia mwezi katika nyinyi naafunge. Na mwenye kuwa Mgonjwa au aliyoko safarini basi atatimiza hesabu ya kufunga katika masiku mengine. Na Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyomazito**] [Surat Baqara: 185] kwa hiyo wakati wowote kikiondoka kile kizuizi au alicho kua akikiogopea atalipa Imai we ni wakati wa Baridi mchana mfupi na anga liko daridi, au ikiwa siyo wakati wa baridi basi atalipa mwaka unaofuatia, lakini haijuzu kwake kuwalisha masikini labda ikiwa ile hali au hilo tatizo linaendelea halitarajiwi kumalizika kama niugonjwa hautarajiwi kupona, tatizo au ugonjwa wa aina hii ndiyo mtu anatakiwa kuwalisha masiki badala ya kufunga.

****

**Swali la 407: Aliyefunga atakapo maliza mchana wake kwa kulala kutokana njaa kali na kiu, je hilo linafanya swaumu yake isiswihi?.**

**Jibu**: Hii haiyathiri katika kuswihi swaumu yake, na kutokana na hilo anapata malipo zaidi ; kwa ushahidi wa kauli ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake alipo muambia Aisha mkewe radh za Mwenyezi Mungu Ziwe juu yake: alimuambia: ((**Malipo yako ni kutokana na fungu lako**)) Sahihi Bukhary: 1787 na Sahihi Muslim: 1211) kila Mtu anavyo zidi kupata tabu katika kumtwii Mwenyezi Mungu yanazidi malipo yake, na anaweza kujifanyia yanayo punguza makali ya swaumu kama vile kujimwagia maji ya baridi, na kukaa sehemu yenye baridi.

****

**Swali la 408: Je inahitaji kutia nia kila siku katika mwezi mtukufu wa Ramadhan au inatosha nia mara moja tu kwa mwezi mzima?**

**Jibu**: Inatosha nia moja tu mwanzo wa Ramadhan; kwa kuan mfungaji asipo nuiya kila siku usiku inakua asha fanya hivyo katika mwanzo wa mwezi, lakini kama itatokea aka katisha swaumu

akaacha kufunga katikati ya mwezi kwa kusafiri, au kwa kuumwa, au likamtokea lolote akawaacha kufunga, basi atakapo anza kufunga tena inambidi kuchukua niya tena; kwa sababu aliyacha kufunga alipo safari au alipo umwa.

****

**Swali la 409: Mwenye kunuiya kufungua pasina kula au kunywa, Je hilo linamfanya awe amefungua kwa kukusudia?**

**Jibu**: Inavyo julikana ni kwamba swaumu ni mkusanyiko wa niya na kuacha yaan - kuacha yote yaliyo katazwa kwa mfungaji, Mtu ananuiya swaumu yake kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuacha yale yote yaliyo katazwa, kwa hiyo atakapo kusudia moyoni kuwa naacha kufunga basi nikweli swaumu inabatilika na kuharibika, anakua simwenye kufunga, lakini ikiwa swaumu hiyo ni katika Ramadhan, basi hatakula au kunywa atajizuiya kutokula mpaka jua lizame; hii nikwa sababu kila ambae anafungua katika Ramadhan bila ya sababu ya kisheria au udhuru wa kisheria basi nilazima ajizuilie na kula na kunywa kisha atakuja ilipa swaumu hiyo.

Ama akiwa hakunuiya kutoka moyoni kuwa naacha kufunga lakini akawa na kigegezi yani - anasema niendelee kufunga au nifungue, hili wana wachuoni Allah awarehemu: wametofautiana hukumu yake.

Miongoni mwao kuna aliye sema: swaumu yake ina batilika (Inaharibika); sababu kigegezi kinaashiria kuwa hajakua na niya wala haja azimia kufunga.

Na miongoni mwao kuna waliosema: swaumu haibatilika (**hai-haribiki**) kwa sababu asili ya niya nikubakia kwa mfungaji mpaka pale atakato azimia moyoni moja kwa moja kuwa hana niya ya kufunga kabisa, siyo kuwa na kigegezi, kwahiyo kauli hizo mbili za wanawachuni kauli swahihu ni hii ya pili kuwa hafungui kwa kuwa na kigegezi tu, bali mpaka apitishe niya moja kuwa sifungi. Allahu a'alamu - Mungu Ndiyo mjuzi zaidi.

****

**Swali la 410: Ni ipi hukumu ya anae kula au kunywa kwa kusahau? Na nini analazimika yule aliye muona?**

**Jibu**: Aliye kula au kunywa kwa kusahau swaumu yake ni swahihu, lakini anapo kumbuka nilazima aache kula au kunywa,

hata kama tonge liko kinywani mwake au hicho kinywaji kiko kinywani mwake basi ni lazima akiteme na ahakikishe hamezi chochote katika chakula hicho au kinywaji hicho baada ya kukumbuka kuwa amefunga; Na dalili ama ushahidi wa kuwa swaumu yake ni swahihu ni kauli ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake alipo sema: ((**Mwenye kusahau akala au akanywa na hali yakuwa amefunga basi na aitimize swaumu yake hakika amemlisha Mwenyezi Mungu na kumywesha**)) [Sahihi Bukhary: 1933 na Sahihi Muslim: 1155].

Kwa sababu Mtu hapatilizwi anapo fanya yale ambayo yamekatazwa ikiwa kayafanya kwa kusahau; kwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu (ombeni): [**Mola wetu! usituchukulie tukisahau au tukikosea**], (Surat Baqara: 286). Na akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Hakika nimesha fanya**].

Ama kwa upande wa yule aliye muona kuwa fulani amefunga lakini mbona ana kula! Ni wajibu wake kumkumbusha; kwakua hili ni katika kuubadilisha munkari au kuondoa munkari kwani hakika amesema Mtume rehema na amaniziwe juu yake: ((Mwenye kuona Munkari miongoni mwenu basi na uondoe kwa mkono wake, asipoweza basi auondoe kwa ulimi wake, akitoweza basi auondoe kwa moyo wake)) makusudio ya kuondoa kwa ulimi yani kukemea kusema acha hilo halifai na kwa moyo ni kulichukia lile jambo linalo fanyika [Sahihi Muslim: 49] na hapana shaka ya kwamba kula au kunywa kwa ambae amefunga ni miongoni mwa munkari, lakini munkari huu husamehewa katika hali ya kusahau kwa sababu kusahau hakuchukuliwi kisheria, ama yule aliye

amemuona mwenzie anakula au ana kunywa na hali anajua kuwa amefunga basi hana udhuru wa kuto kumuambia aache munkari huo au jambo hilo baya nilazima amuonye.

****

**Swali la 411: Ni ipi hukmu ya kutia wanja kwa mtu aliyefunga?**

**Jibu**: Hakuna tatizo kwa aliye funga kupaka wanja, na kuweka tone kwenye macho yake, na kuweka tone kwenye masikio yake hata kama atasikia ladha kwenye koo lake hatafungua; (kwakua siyo kitu cha kula wala kunywewa, wala hakiwi katika maana ya kula na kunywa; na dalili nikwamba kuliko katazwa ni kula na kunywa, kwahiyo vingine haviingii kwenye maana ya orodha ya kula na kunywa), na kauli hii tuliyotaja ni pendekezo la Sheykhul Islaam bin Taymiyah Allah amrehemu, na kauli hii ni saahihi kabisa. [Maneno haya yako kwenye kitabu cha mkusanyiko wa fatua 25/ 233- 234].

Ama kama ataweka tone katika pua yake na likaingia mpaka ndani atafungua akiwa kafanya hivyo kwa kukusudia; kwa ushahidi ni kauli ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Balighesha maji wakati wa kutawadha isipokua ukiwa umefunga** )). (kubalighisha maji ni kuyatia mdomoni na kuyachezesha kooni

wakati wa kutawadha), [hadith hii ameipokea Abuu Daud mlango wa istinthaari hadith no 142, na Tirmidhy hadith no 37, na Al Nnasaai hadith no 87, na Ibunu Maajah na hadith no 407].

****

**Swali la 412: Ni ipi hukumu ya kupiga mswaki na kujitia manukato kwa mtu aliyefunga?**

**Jibu**: Kupiga mswaki kwa aliye funga ni Sunna wakati wa mwanzo wa mchana na mwisho wa mchana; kwa ushahidi wa kauli ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake ((**Kupiga mswaki ni kujitwaharisha mdomo Mwenyezi Mungu anaridhia**)) [ameipokea Bukhaary kittabu Swiyaam hadith no. 1934, na Ahmadi 6 / 47 na Al Nnasaai no. 5], na pia kauli yake: ((**Lau sikuuonea uzito umati wangu aamrisha kupiga mswaki katika kila swala** )). [Ameipokea Bukhary kitaab Siwaak hadith no. 887, na Muslim, kitaab Twahara hadith no. 252], ama kupaka manukato vilevile ni jambo linafaa katika mwanzo wa mchana na mwisho wake iwe ni manukato ya kupuliza au yakufukiza kama udi au ya kupaka au mengine yoyote yasiyo kuwa hayo, ila haijuzu kuyaingiza puani; kwa sababu udi au ubani au chochote cha kufukiza kuna vitu ambavyo vinaoneka ukiviingiza puani vikifika ndani vitaendelea mpaka kwenye… Na kwasababu hii akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake kumuambia Laqiitwi bin sabrat radhi za mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

**((Balighisha (kuyafikisha ndani kabisa) maji katika kuyapitisha puani isipokua ukiwa umefunga))**.

****

**Swali la 413: Ni mambo gani yanayo haribu swaumu?**

**Jibu**: Yanayo haribu swaumu ni yale yanayo funguza nayo ni:

1-Kufanya mapenzi , yani – kukutana kimwili mke na mume.

2-Kula.

3-Kunywa.

4-Kutokwa na manii kwa kutamani.

5-Kufanya kitu ambacho kina maana ya kula au kunywa.

6-Kujitapisha kwa makusudi.

7-Kutokwa na Damu kwa kupiga chuku.

8-Kutokwa na damu ya hedhi au kutokwa na damu ya nifasi (nifasi ni damu inayomtoka mwanamke baada ya kuzaa).

Ushahidi wa kula na kunywa na kufanya tendo la ndoa; ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

[**Basi sasa changanyikeni nao na takeni aliyo kuandikieni Mwenyezi Mungu. Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa Alfajiri katika weusi wa usiku. kisha timizeni swaumu mpaka usiku**]. [Surat Baqara: 187].

Ama dalili ya kutokwa na manii kwa matamanio; ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu katika hadith Qudus inayo elezea kufunga: ((**Ana acha chakula chake na kinywaji chake na matamanio yake kwa ajili yangu**)), [ameipokea Muslim katika Swiyam hadith no. 1151].

Na pia kauli yake Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Katika tupu ya mmoja wenu kuna sadaka** )) Maswahaba wakasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu; Anayaendea mmo-

ja wetu matamanio yake na anakua na malipo? akasema Mtume: ((**Mnaonaje lau atayaweka kwenye haramu – anakua na madhambi – basi na vile vile atakapo yaweka katika halali anakua na malipo**)) [ameipokea Muslim kitabu Zakat hadith no. 1006]. Na ambayo yanawekwa hakika si kitu kingine bali ni manii yenye kuruka, na kwasababu hiyo ikawa kauli swahihu ni kwamba Madhii hayaharibu swaumu hata yakitoka kwa matamanio au yakatoka madhii kwa kutomasana tomasana bila kufanya tendo la ndoa.

Na jambo la tano ni lile ambalo linakua katika maana ya kula na kunywa: Ni sindano, sindano ambazo ukichomwa basi huhitajii kuwa au kunywa; napia kuwekewa drip ambalo linaondoa njaa na kukufanya uwe umeshiba au huisikii njaa kabisa; vitu hivi ijapo kua siyo chakula wala maji lakini vinachukua sehemu ya chakula kwavile mtumiaji anatosheka na kutokuhitajia kula au kunywa, kwa sababu kitu chochote kinacho kua mfano wa kitu basi kinakua na hukmu ya kile kitu chenyewe; Na ndiyo mana kwa kutumia sindano hizo mwili unabaki kwenye hali yakua umekula na kutoisikia njaa.

Ama kutumia au kuchoma sindano ambazo hazina maana ya kula au kunywa, sindano hizi hazifunguzi kama Mtu atachomwa sindano hizo popote iwe kwenye makalio au mikononi au sehemu yoyote katika mwili wake hata fungua.

Na jambo la sita ni kutapika kwa makusudi: Ni mtu kujitapisha kilichoko tumboni mwake mpaka kitoke mdomoni mwake ,

Amesema mtume rehema na amani ziwe juu yake : ((**Mwenye kujitapisha kwa makusudi basi alipe, na ambae matapishi yatamshinda nguvu basi hatalipa**)) ameipokea Ibin Daud kitaab swiyam hadith no. 2380, na Trimidhy hadith no. 720], yani – mtu akitumia kidole au kituchochote akakiingiza mdomoni ili ajitapishe au kutumia mbinu nyingine ili atapike huyu hana swaumu na atakuja kuilipa swaumu hiyo, tofauti na Mtu ambae amekaa tu au amelala ghafla tapishi likamjia pasi na kutarajia au kukusudia huyu atasukutua na kuhakikisha hamezi maji au chochote wakati anatapika na atakamilisha swaumu yake hatalipa, na hikma katika jambo hilo ni kwamba Mtu atakapo tapika tumbo lake litakua tupu halina chakula, na mwili unahitaji kitu ambacho kitaziba nafasi ya kilicho toka; kwa ajili ya jambo hili tunasema: ikiwa swaumu niya wajibu (faradh) basi haifai mtu kujitapisha; kwakua akijitapisha ameharibu swaumu yake ya waajibu.

Na Jambo la saba ni: Ni kutokwa na damu kwa kupiga chuku: Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Amefungua mwenye kupiga chuku na mwenye kupigwa** )). [Ameipokea Bukhaary kitaab swaum hadith no. 1937, na Trimidhy hadith no. 774 ].

Jambo la nane ni: ni kutokwa na damu ya hedhi au damu ya nifasi; Kauli ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika kumuelezea Mwanamke: akasema Mtume: ((**Si nikwamba akitokwa na hedhi haswali na hafungi**)) [ ameipokea Bukhary kitabu haidh hadith no. 304, na Muslim kitabu Imaan hadith no. 79]

hakika wamepatana wana wa chuoni yakwamba swaumu haiswihi kwa mwenye hedhi na vile vile mwenye nifasi.

Mambo haya yenye kuharibu swaumu hayaharibu swaumu mpaka yatimize masharti matatu, yani swaumu itaharibika ikiwa mtu anayajua mambo haya matatu.

**1-Ni kufahamu**: Mtu akiwa anafahamu kuwa jambo hili haliruhusiwi nikiwa nimefunga.

**2-Ni kukumbuka**: yani hakusahau wakati anafanya jambo hilo bali alikua anafanya huku anaufahamu kuwa jambo hili hali-fai litaniharibia swaumu .

**3-Ni kufanya kwa makusudi:** Aliye funga na akafanya mambo ambayo yamekatazwa swaumu yake itaharibika ikiwa anafahamu mashariti haya matatu.

**Sharti la kwanza**: Ni mtu kufanya akiwa anajua hukmu za kisheria napia anafahamu kuwa yuko kwenye wakati Fulani kwa mfano awe anafahamu kuwa yuko kwenye ramadhani na amefunga, kisha akaamua kula na anafahamu kuwa muda wa kufungua haujafika huyu swaumu yake inaharibika, kinyume kama alikua hafahamu hukmu ya jambo hilo kisheria au hafahamu kuwa yuko kwenye wakati gani kwa mfano hafahamu kuwa muda wa kufun-

gua hauja fika yeye akadhani umefika na akafungua basi swaumu yake itakua sahihi kwasababu kafanya hivyo kwa kuto kujua; kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

[**Mola wetu! usituchukulie tukisahau au tukikosea**] Na akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu [**Hakika nimesha fanya**]. Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Wala hakuna lawama juu yenu kwa mlivyo kosea. Lakini mna lawama katika yale ziliyo fanya nyoyo zenu kwa makusudi**] [Suratul Ahzaab: 5]. Na dalili mbili hizi zinakusanya hayo yote.

Na pia kwa kuthibiti Sunna katiika hilo hasa katika swaumu, Katika kitabu cha sahihi Bukhary, hadith ya Adiyyi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: kwamba yeye Adiyyi alifunga kisha akaweka chini ya Mto wake wa kulalia kamba mbili ambazo hutumika kwa kumfumga mikono ya ngamia anapo piga magoti - kamba alizo weka moja ilikua ni nyeupe na nyingine ilikua na nyeusi, akawa anakula na kunywa mpaka ilipo mdhihirikia kamba nyeupe na nyekundu, kisha ndiyo akaacha kula na kuanza swaumu, kesho kulipo kucha alienda kwa mtume wa Mwenyezi Mungu rehema na amani ziwe juu yake, akamuambia hilo alilo fanya usiku, Mtume akambainishia na kumfahamisha ya kwamba makusudio ya kamba nyeupe na nyeusi zilizo tajwa katika aya siyo kamba hizi zinazo fahamika, isipokua makusudio ya kamba nyeupe ni ule weupe wa mchana, na kamba nyeusi ni ule weusi wa usiku, (yani - mna ruhsa ya kula na kunywa mpaka itakapofikia usiku unaanza kutoeka giza la usiku linaanza kupotea na kuanza kuona hali

ya mwanga kujulisha kwamba kunakaribia kucha, hali ikishafikia hapo hamruhusiwi kula tena) Mtume baada ya kumfahamu huyu bwana na kufahamu aliyo ya fanya na akamfahamisha usawa ni upi, lakini hakumuambia alipe swaumu hiyo; kwa vile alikua hafahamu hukmu, aliyo yafanya alifanya kwa kudhani hiyo ndiyo maana halisi ya aya katika Qur'an tukufu.

Na ama kutokufahamu wakati , katika kitabu cha ((Sahihi Bukhary)) kutoka kwa As'maa bint Abi bakari radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao, amesema As'maa: ((**Tulifungua katika zama za Mtume rehema na amani ziwe juu yake, katika siku ya mawingu kisha baadae likachomoza jua**)), (yani - siku hiyo anga ilikua imejaa mawingu kiasi kwamba hawakufahamu kuwa jua halija zama wakaanza kula, kutahamaki baadae wanaliona jua lakini wakawa washafungua tayari). Na Mtume hakuwaamrisha kulipa swaumu hiyo, lau ingekua kunaulazima wa kulipa siku hiyo Mtume angewaamrisha kuwa siku hiyo wailipe, na lau ange waamrisha basi khabari hiyo ingeufikia umah wa kiislam; Mwenyezi Mungu anasema: [**Hakika sisi ndiyo tuliyo teremsha ukumbusho huu, na hakika sisi ndiyo tutakao ulinda**]. [Surat Hijir: 5], kwakua hatukuletewa hadith ya kuwa walilipa, imefahamika kuwa Mtume hakuwaamrisha na ikafahamika kuwa haikua waajib, Mfano wa hili: lau Mtu ataamka kutoka usingizini akadhani kuwa ni usiku akala na akanywa, kisha baadae akafahamu kuwa alikula au alikunywa baada ya alfajiri basi hata lipa kwa kuwa alikua hajui kuwa kumeshakucha.

**Sharti la pili**: Ni kuwa anakumbuka, na kinyume chake ni kusahau, lau atakula au atakunywa hali yakuwa ni mwenye kusahau, basi swaumu yake itakua ni swahihu wala hatalipa; kwa ushahidi

wa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Mola wetu! usituchukulie tukisahau au tukikosea** ] Na akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: **[Hakika nimesha fanya**]; Na kwa hadith ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake ((**Mwenye kusahau na yeye amefunga akala au akanywa basi na atimize swaumu yake, hakika sivinginevyo amemlisha Mwenyezi Mungu na akamnywesha**)).

**Sharti la tatu**: Ni kukusudia: Ni mtu kuchagua kuwa nifanye jambo hili linalo funguza, Ikiwa hakulichagua kulifanya basi swaumu yake ni swahihu, iwe kalifanya kwa kutenzwa nguvu (kulazimishwa au hakulazimishwa; kutokana na kauli ya Mwenyezi Mungu kwa anae lazimishwa kukufuru: [**Anaye mkataa Mwenyezi Mungu baada ya kuamini kwake - Isipokuwa aliye lazimishwa na hali ya kuwa moyo wake umetua juu ya imani, lakini aliye kifungulia kifua chaka kukataa - basi hao ghadhabu ya Mwenyezi Mungu ipo juu yao, na wao watapata adhabu kubwa**] [Surat Nnahli: 106], yani - aliye lazimishwa kumkataa Mwenyezi Mungu, basi anakua haja mkataa kwakua kalazimishwa, isipokua yule ambae ameamua mwenyewe kumkataa Mwenyezi Mungu huyo ndiye aliekufuru, ikiwa hukmu ya kukufuru husamehewa ikiwa ni kwa kulazimishwa basi hukmu ya jambo ambalo siyo la kukufuru ni bora zaidi kusamehewa, na kwa hadith aliyo pokewa kutoka kwa mtume rehema na amani ziwe juu yake Amesema ((Hakika Mwenyezi Mungu amesamehe kwenye umati wangu kukosea, na kusahau, nayale wanayo lazimishwa)), [hadith kaipokea Ibnu Maajah kitaab Twalaqa hadith no. 2045], na kwa hili lau vumbi lita ruka likaingia kwenye pua ya aliye funga na aliye funga akaihisi ile ladha ya lile vumbi katika koo lake na likashuka mpaka tumboni kwake basi hatafungua kwa fumbi hilo;

kwa sababu hakukusudia vumbi hilo limuingie, na vil vile kama atalazimishwa kufungua na akafungua kwa kule kulazimishwa basi swaumu yake ni sahihi; kwasababu hakuchagua kufungua bali kalazimishwa kufanya hivyo, na vile vile lau ataota anafanya tendo la ndoa na akashusha manii na hali yakua yeye amelala basi swaumu yake ni swahihu; kwa sababu aliye lala hawezi kukusudia kitu bali inatokea tu, na vile vile lau mwanamke atalazimishwa na mumewe kufanya tendo la ndoa mchana wa Ramadhan na mwanamke huyo amefunga na mwanamume huyo kweli akamuingilia mkewe basi mwanamke huyo swaumu yake ni sahihi; kwa sababu yeye hajachagua kufanya mapenzi mida hiyo wala haja penda.

Na hapa kuna suala inapasa lifahamike: nalo ni hili: Lau mwanamume atafungua kwa ajili ya kufanya tendo la ndoa katika mchana wa Ramadhan na swaumu kwake ni waajib na lazima basi kwa ajili ya tendo hilo yanamlazimu mambo matano:

**Jambo la kwanza**: Anapata dhambi.

**Jambo la pili:** Anapaswa kujizuilia na kula na kunywa kwa mchana wote uliyo baki.

**Jambo la tatu:** Swaumu hiyo imeharibika hakufunga.

**Jambo la nne:** Ni kulipa swaumu hiyo.

**Jambo la tano:** Ni kutoa kafara.

Na hakuna tofauti ya kuwa anajua au hajui kuwa tendo hilo halifai katika mchana wa Ramadhan, yani - Mwanaume atakapo fanya tendo la ndoa katika swaumu ya Ramadhan na swaumu kwake ni waajibu, lakini alikua hajui kuwa inamlazimu yeye kutoa kafara, basi zinamlazimu yeye hukumu tulizo taja hapo juu kwa mwenye kufanya tendo hilo, kwa sababu yeye amekusudia kuiharibu swaumu, na kwa kukusudia kwake huko zinamlazimu hukumu juu yake; bali katika hadith ya Abii Hurairah kwamba mwanamume mmoja alikuja kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake; Akasema kumuambia Mtume: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu mimi nimeangamia, Mtume akasema ((**Ni kipi kilicho kuangamiza**)) akasema nimemuingilia mke wangu katika mchana wa Ramadhan na mimi nimefunga, Mtume akamua mrisha atoe kafara na hali yakua Mwenamume huyu alikua hajui kuwa anapaswa kutoa kafara au hapana, na ((**Tulipo sema swaumu ni waJibu juu yake**)) ni kwa kuchunga yule ambae atamuingilia mkewe katika ramadhani na amefunga na yeye yuko safarini kwa mfano, basi huyu haimlazimi yeye kutoa kafara, yeye atalipa tu bila ya kutoa kafara, mfano: mtu akiwa amesafiri na mkewe katika mwezi wa Ramadhani na wote wawili wamefunga, kisha akamuingilia mkewe, basi hatatoa kafara, na hiyo nikwa sababu msafiri atakapo anza kufunga haimlazimu yeye kuitimiza swaumu hiyo akitaka ataitimiza, na akitaka atafungua kisha atalipa, yani - msafiri anaweza kuanza kufunga lakini ikafikia muda akaamua kufungua kutokana na safari yake.

****

**Swali la 414: Ni ipi hukumu ya kutumia dawa ya pumu ya kupuliza mdomoni kwa aliye funga, je inafunguza?**

**Jibu**: Dawa hii ya kupuliza kwa mwenye pumu haifiki tumboni, kwahiyo hapana tatizo kuitumia ukiwa umefunga, wala hutafungua kwa kutumia dawa hiyo; kwa sababu kama tulivyo sema haifiki tumboni, kwa kua ni kitu ambacho kinaruka na kinaondoka kama upepo, wala hakuna chembe yoyote inafika tumboni, inafaa kuitumia na wewe umefunga, na wala swaumu yako haita haribika kwa hilo.

****

## Swali la 415: Je matapishi yana funguza?

**Jibu**: Mtu atakapo tapika kwa makusudi anafungua, na akitapika bila ya kukusudia hafungui, na dalili ya hilo ni hadith aliyo ipokea Abuu Huraira kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema:

((**Ambaye yatamshinda nguvu matapishi hatalipa, na mwenye kujitapisha kwa makusudi na alipe**)).

Matapishi yakikushinda hutafungua, Mtu atakapo hisi kuwa tumbo lake linavuruga na kwamba vitatoka vilivyomo tumboni tunamuambia: asivizuie kutoka wala asivivute ili vitoke kwasababu ukijitapisha umefungua, na ukizuia utapata madhara, yaache yakitoka basi na kutaka kwako haita kudhuru wala hutafungua kwa hilo.

****

**Swali la 416: kutokwa na damu katika meno kwa aliye funga kunafunguza?**

**Jibu**: Damu ambayo inatoka katika meno haina madhara kwenye swaumu, lakini kuwe na tahadhari ya kuimeza vyovyote itakavyo wezekama, na vile vile lau zitatoa kamasi pua zake na akajizuia kuzimeza, hakika hakuna tatizo katika hilo, wala hatalipa, yani - damu inayotoka kwenye meno ajitahidi asiimeze na vile vile kamasi au kohozi kama likifikia mdomoni aliteme asilimeze akifanya hivyo swaumu yake haina tatizo.

****

**Swali la 417: Atakapo twaharika mwanamke kutokan na hedhi kabla ya Alfajiri na akaoga baada ya kuchomoza alfajiri ni ipi hukumu ya swaumu yake?**

**Jibu**: Swaumu yake ni sahihi atakapo kuwa na yakini ya kutwaharika kwake kabla ya kuchomoza alfajiri; Muhimu ni kuwa na yakini kuwa ametwaharika; kwa kuwa baadhi ya wanawake hudhani kuwa ametwaharika kumbe haja thaharika; na kwasababu hiiwanawake walikua wakienda na pamba kwa Aisha radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: wanamuonyesha alama za kuwa wametwaharika, Aisha anawaambia: ((**Hapana subirini mpaka muone maji meupe**)), mwanamke ni juu yake kufanya

subra mpaka awe na yakini kuwa ametwaharika (**kutwaharika ni ile damu kukatika na ikawa haitoki tena**), atakapo twaharika ananuiya swaumu hata kama hajaoga mpaka baada ya alfajiri, lakini pia anatakiwa aangarie muda wa swala ya alfajiri afanye haraka kuoga ili aiswali swala ya alfajiri katika wakati wake.

Kuna baadhi ya wanawake wanatwaharika baada ya alifajiri, au kabla ya alfajiri lakini anachelewesha kuoga mpaka baada ya kuchomoza jua kwa hoja ya kwamba anataka ajitwaharishe vizuri zaidi, na hili ni kosa katika ramadhani na miezi mingine; kwakuwa lililo wajibu juu yake ni kufanya haraka kuonga ili aiwahi sala ya alfajiri katika wakati wake, na anaweza kufanya ufupiliza kuoga katika josho la waajib ili akatekeleze sala, na baadae kama anataka ajizidishie twahara na usafi mpaka baada ya kuchomoza jua hakuna tatizo juu ya hilo na swaumu yake ni sahihi, Ikiwa Mtu anajanaba na hakuoga mpaka baada ya alfajiri na yeye amefunga pia hakuna tatizo katika hilo, kwa kua Imethibiti kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake; kwamba yeye inamdiriki alfajiri naye anajaba kwa tendo alilofanya na mkewe na anafunga anaoga baada ya kuchimbuka alfajiri . Allah ni mjuzi zaidi.

****

**Swali la 418: Ni ipi hukumu ya kung'oa jino kwa aliye funga je kunafunguza?**

**Jibu**: Damu inayo toka wakati wa kung'olewa jino haifunguzi kwa sababu haina madhara kama ilivyo damu ya kupiga chuku - kwahiyo hafungui kwa kung'oa jino.

****

**Swali la 419: Ni ipi hukmu ya kutoa Damu kwa ajili ya kupimwa kwa Mtu aliye funga je kunafunguza?**

**Jibu**: Hakufunguzi kutoa damu ili afanyiwe vipimo, kwasababu ni damu chache haina madhara mwilini kama madhara ya kupiga chuku, asili ni kubakia kwa swaumu, swaumu haiharibiki mpaka zipatikane dalili za kisheria za kukataza, na hakuna dalili kwamba aliyefunga anafungua kwa kutoa damu hii chache ya vipimo, ama damu ikiwa nyingi anafungua kwa mfano akijitolea damu kwa ajili ya kumsaidia mgonjwa anae ihitaji kuongezewa damu, damu kama hii anafungua kwasababu nikama damu ya kupiga chuku,

kwa hiyo ikiwa mtu amefunga swaumu ya waajib haifai kujitolea kutoa damu, labda asubiri mpaka magharibi akifungua ndiyo atoe, na kama itakua damu yake inahitajika sana hakuna wakutoa damu ila huyu aliye funga, basi hakuna tatizo atatoa damu kisha atafungua atakula na atakunywa ili arudishe nguvu, kisha atailipa siku hii aliyo fungua.

****

**Swali la 420: Aliye funga akijitoa manii kwa kutumia mkono (au kupiga punyeto kama wasemavyo) je anafungua kwa sababu hiyo? Na je analazimika kutoa kafara?**

**Jibu**: Aliye funga akijitoa manii kwa kutumia mkono anafungua, na nilazima kulipa siku hiyo aliyo fanya jambo hilo, na hatatoa kafara; kwa sababu hakufanya tendo landoa, aliye fanya tendo la ndoa ndiyo analipa pamoja na kafara, na ni juu yake kutubia kwaajili ya tendo hilo alilofanya.

****

**Swali la 421: Ni ipi hukumu ya kunusa manukato kwa aliye funga?**

**Jibu**: Kunusa manukato kwa aliye funga hakuna tatizo, iwe ni manukato ya kufukiza kama vile udi au manukato ya mafuta, lakini kama ni manukato ya kufukiza basi asivute moshi wake, kwasababu moshi ni kitu kinacho onekana, unaweza kuingia mpaka ndani ya tumbo, akawa amefungua, lakini mafukato mengineyo kama ya mafuta au ya maji hayana tatizo na wala hatafungua ikiwa atayanusa kawaida bila kuingiza puani.

****

**Swali la 422: Ni ipi tofauti ya kunusa kitu kinacho fukizwa kama udi, na tone kwa kua kunusa hakufunguzi tofauti na tone linafunguza tofauti ya viwili hivi ni ipi?**

**Jibu**: Tofauti iliyopo kati ya vitu hivyo viwili ni kwamba mwenye kuvuta moshi anaweza akakusudia moshi uingie mpaka ndani, ama mwenye kuweka tone anakua hakukusudia tone hilo

lifike mpaka ndali isipokua amekusudia aweke kwenye mianzio ya pua yake tu.

****

**Swali la 423: NI ipi hukumu ya kuweka tone puani na jichoni kwa aliye funga?**

**Jibu**: kuweka tone puani likaingia mpaka ndani tumboni linafunguza

Kama ilivyo kuja katika hadith ya lakiitwa bin swabra alipo ambiwa na Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Baleghisha wakati wakupandisha maji pua ni isipokua ukiwa umefunga**)) haijuzu kwa liye funga aweke tone ambalo litafika mpaka ndani ya tumbo lake, ama kuweka tone ambalo haliingii mpaka ndani hilo ni tone linalo wekwa puani halifunguzi.

Na ama tone linalo wekwa kwenye jicho , mfano wake nikama kupaka wanja, na vile vile tone linalo wekwa puani hakika matone hayo yote hayafunguzi; kwa kuwa siyo kitu kilicho husishwa na sehemu hizo, na jicho siyo sehemu ya kulia chakula au ya kunywea maji na vile vile sikio ni miongoni mwa matundu yaliyoko katika mwili, wanachuoni wameelezea Allah awarehemu: kwamba

lau mtu atakanyaga kitu chochote  kwa mguu wake kisha akasikia ladha ya kile kitu alicho kanyaga kooni basi hatafungua; kwa sababu mguu siyosehemu inayotumika kwa kulia chakula, na kupaka wanja au kuweka tone katika jicho au tone la sikio siyo vinavyo funguza hata kama tone hilo alilo weka ataisikia ladha yake kooni, na mfano wa hili vilevile lau mfungaji atapaka mafuta kwa ajili ya tiba kama dawa ya kuchua, au akapaka mafuta yoyote ambayo siyo kwa ajili ya dawa basi pia hakuna madhara, na vilevile lau atabanwa na kifua au mapafu kama vile pumu na akatumia dawa zile fakupuliza maarufu zinazo julikana kwa ajili ya kumfanyia wepesi kupumua, pia hata fungua kwa kupuliza dawa hiyo mdomoni, kwasababu dawa hiyo haifiki kwenye utumbo au tumboni, kwahiyo haiwi ni kula au kunywa.

****

**Swali la 424: Atakae kuwa usingizini akaota na hali amefunga je swaumu yake itaswihi?**

**Jibu**: Ndiyo; swaumu yake ni sahihi kwani kuota hakuharibu swaumu; kwa kuwa siyo khiyari ya Mtu, amesamehewa akiwa amelala, na kwakupitia swali hili nitawazindua baadhi ya watu waliyo wengi katika zama zetu hizi, watu hao ni wale wanaopenda

kukesha katika nyusiku za Ramadhan, na hutokea wakakesha katika jambo au mamboa ambayo hayawamanufaishi wala hayawadhuru, kisha ikifika mchana, mchana wote wanautumia kwa kulala; jambo hili siyo zuri halitakikani, bali ambalo lina takikana ni Mtu kuifanya swaumu yake ni sehemu ya kufanya twaa na kumtaja Mwenyezi Mungu na kusoma Qur'an na mambo mengine mengi yanayo mkurubisha kwa Allah Mtukufu.

****

**Swali la 425: Ni ipi hukumu ya kujimiminia maji ya baridi kwa ajili ya kujipoza kwa aliye funga?**

**Jibu**: kujipoza kwa aliye funga inafaa hakuna tatizo, kwani Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikua akijimiminia maji kichwani kwa ajili ya kupunguza makali joto, au kiu hali yakua amefunga, na alikua Ibin umar radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake; akizitotesha nguo zake kwa maji na hali yakua amefunga kwa ajili ya kupunguza makali joto, au kiu na huo umajimaji uliyoko kwenye nguo hauathiri chochote katika swaumu; kwa kuwa siyo kwamba ni maji yanayofika tumboni.

****

**Swali la 426: Atakapo sukutua aliyefunga , au kupandisha maji puani na maji yakaingia mpaka ndani ya pua je kufanya hivyo kunafunguza?**

**Jibu**: Atakapo sukutua aliye funga, au kupandisha maji puani na maji yakaingia mpaka ndani ya pua yake hafungui; kwakua hajakusudia kufanya hivyo, Amesema Allaah Mtukufu: [**Wala hakuna lawama juu yenu kwa mlivyo kosea . Lakini mna lawama katika yale ziliyo fanya nyoyo zenu kwa makusudi**] . [Suratul Ahzaab: 5].

****

**Swali la 427: Ni ipi hukumu ya kutumia mafuta mazuri kama vile marashi kwa aliye funga?**

**Jibu**: Hapana vibaya akitumia katika mchana wa Ramadhan, au kuyaweka puani na kuyavutia ndani , ila manukato ya kufukiza kama vile udi au ubani asiuvute; kwa kuwa unakitu kinacho onekana kinachoweza kufika ndani tumboni na kitu hicho ni moshi.

****

**Swali la 428: Je kutokwa na damu puani kunafunguza?**

**Jibu:** kutokwa na damu puani hakufunguzi hatakama ni nyingi kwa kuwa ikimtoka siyo hiyari yake**.**

****

**Swali la 429: Tunaona baadhi ya kalenda katika mwezi wa Ramadhan zimewekwa kipengele kinacho sema (kujizuilia) na huko kujizuilia inakua ni kabla ya swala ya alfajiri kama dakika kumi, au robo saa, je jambo hili lina asili katika Sunna au ni miongoni mwa bida'a na uzushi?**

**Jibu**: Hili ni miongoni mwa bida'a na uzushi, halina asili katika Sunna, isipokua Sunna iko kinyume na jambo hilo; kwa sababu Allah Mtukufu amesema katika kitabu chake kitukufu:

[**Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe aw Alfajiri katika weusi wa usiku**] [Surat Baqara: 187].

Na amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Hakika bilali anaadhini usiku, basi kuleni na kunyweni mpaka muisikie adhana ya Ummu Maktuum kwakua yeye haadhini**

**mpaka ichomoze Alfajiri**)), [hadith hii iko katika Sahihi Bukhary katika kitabu cha Swaumu hadith no. 1918, na Sahihi muslim katika kitabu Swaumu hadith no. 1092], huku kujizuiya ambako wamekutengeneza baadhi ya watu ni kuzidisha kile alicho kifaradhisha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwahiyo ni baatili, na hiyo ni kuchupa mipaka katika dini ya Allah, na amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Wameangamia wenye kuchupa mipaka, wameangamia wenye kuchupa mipaka, wameangamia wenye kuchupa mipaka** )). [Hadith hii iko katika Sahihi Musilm katabu Ilim hadith no. 2670].

****

**Swali la 430: Mwenye kuchwewa na jua akiwa uwanja wa Ndege na muadhini aka adhini kisha akafungua na baada ya ndege kupaa akaona jua je anajizulia na kula?**

**Jibu**: Huyu hajizuilii; kwakua wakati wa kufuturu umefika na yeye alikua yuko aridhini; kwakua limezama jua alipokua yuko aridhini, Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Utakapo ingia usiku kutokea hapo na ukapita mchana kutokea hapo na likazama jua basi amefuturu aliye kuwa amefunga**)) [hadith iko katika Sahihi Bukhary kitabu Swaum no. 1941, na katika Sahihi Muslim no. 1101], yani - popote utakapo ondoka mchana na ukaingia usiku basi huo ndiyo muda wa kufungua, itakapo kuwa amefungua yule ambae limemchwea jua na yeye yuko airpot au uwanja wa ndege hapo ndiyo imeishia siku

yake, na itakapo isha siku yake haimlazimu yeye kujizuilia na kula au kunywa nk. Isipokuwa anasubiri siku inayo fuata ili aanze tena swaumu nyingine.

Kwa hiyo jua lilipo zama alipo kuwa uwanja wa ndege hapo ndiyo amepata ruhsa ya kufungua kisheriya wala hahitajii tena kufunga hata kama ataliona jua akiwa angani .

****

**Swali la 431: Ni ipi hukmu ya kumeza makohozi au makamasi kwa mtu aliyefunga?**

**Jibu**: Makohozi au makamasi kama yakiishia kooni na hayakufika mdomoni ama kinywani hayafunguzi, lakini kama yamefika kinywani kisha akayarudisha ndani na akayameza; wanachuoni wamegawanyika mafungu mawili katika kulijibu hilo: baadhi yao wamesema huyo alie meza amefungua kwa kuwa makohozi au makamasi yamefika kinywani na hakuyatema akayameza ni kama alie kula au kunywa.

Na wengine wakasema hajafungua nikama alie meza mate tu,

kwa sababu mate haya batilishi swaumu hata kama atayakusanya kinywani na akayameza swaumu yake haiharibiki.

Na wanachuoni wakipishana kauli katika jambo basi tunatakiwa kurudi katika Qur'an na hadith za mtume, tunapokua na shaka katika jambo kuwa je linafunguza au halifunguzi? nikubaki kwenye asili ya kuwa swaumu ipo na haiharibiki, kwa hiyo alie meza kamasi au kohozi hafungui.

Ambalo ni muhimu ni mtu kujiepusha na kutavuta makamasi na makohozi ili yafike kinywani kwake, na vizuri yanapofika mdomoni ayateme iwe amefunga au hajafunga, lakini kusema kuwa yanafunguza basi jambo hilo linahitaji dalili vile vile itakua ni ushahidi kwa Mwanadamu mbele ya Allah Mtukufu katika kusema swaumu inaharibika.

****

### Swali la 432: Je swaumu inaharibika kwa kuonja chakula bila ya kukimeza?

**Jibu**: Swaumu haibatiliki kwa kuonja chakula akiwa hatakimeza lakini jambo hili usilifanye mpaka pale inapotokea kwamba kuna haja ya kuonja, na katika hali hii ya kuonja kama kitu kitapita

kwa bahati mbaya ukakimeza bila ya kukusudia kukimeza basi swaumu yako haiharibiki.

****

**Swali la 433: Je Mtu kuongea maneno ya haramu katika mchana wa Ramadhan anaharibu Swaumu?**

**Jibu**: Tukisoma maneno la Allah Mtukufu linalo sema: [**Enyi mliyo amini! Mmelazimishwa kufunga, kama walivyo andikiwa waliyo kuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu**] [Surat Baqara: 183]. Tumeifahamu hikma ya kulazimishwa kufunga kuwa ni kumcha na kumuabudu Allah Mtukufu, na kumcha ni kuacha mambo yaliyo haramishwa na kufanya mambo yaliyo amrishwa, na kuacha yaliyo katazwa na kutahadharishwa, amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ((**Ambae hata acha maneno ya uzushi, na kuyafanyia kazi, na ujinga; hakuna haja kwa mwenyezi Mungu katika kuacha chakula chake na kinywaji chake**)) kwa hiyo ina takikana kwa mfungaji kuhakikisha anajiepusha na yale yaliyo haramishwa miongoni mwa maneno na matendo, wala asiwafedheheshe watu kwa kutaja aibu zao, wala asiseme uongo, wala asiwasengenye watu, wala asiuze biashara haramu, na ajiepushe na yote yaliyo haramishwa, kwani mtu atakapo simama kuacha yaliyo haramishwa na akafanya yaliyo amrishwa mwezi mzima hakika nafsi yake itakaa katika njia ya sawasawa na itarekebika mwaka mzima.

Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba watu wengi wanaofunga hawatofautishi kati ya siku za swaumu zao na siku zao za kula mchana, wanakua bado wako kwenye kawaida yao waliyo izoea ya kuongea mambo ya haramu kama vile uongo, na mengineyo, bila ya kuhisi utulivu wa swaumu, vitendo hivi havi batilishi swaumu, lakini vinapunguza malipo na thawabu za swaumu , na huenda vikilinganishwa vitendo hivyo viovu na swaumu basi ukakuta vitendo hivyo vina poteza thawabu za swaumu.

****

**Swali la 434: Ni upi ushahidi wa uongo? na je unabatilisha Swaumu?**

**Jibu**: Ushahidi wa uongo ni miongoni mwa madhambi makubwa, nao ni Mtu kutoa ushahidi kwa jambo ambalo halifahamu, au ufahamu wake ni tofauti, wala halibatilishi swaumu lakini linapunguza malipo ya swaumu.

****

**Swali la 435: Ni zipi adabu za Swaumu?**

**Jibu:** Adabubu za swaumu ni kuambatana na kumcha Mwenyezi Mungu Kwa vitendo au amri zake na kujiepusha na makatazo yake; kwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: [**Enyi mliyo amini! Mmelazimishwa kufunga kama walivyo andikiwa waliyo kuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu**]. (Surat Baqara: 183 ), na kwa kauli ya Mtume Rehma na amani ziwe juu yake amesema: ((**Ambae hataacha maneno ya uzushi na kuufanyia kazi, haina haja kwa Mwenyezi Mungu Mtu huyo kuacha chakula chake na kinywaji chake**)). Na miongoni mwa adabu za swaumu ni kutoa sadaka kwa wingi, na kufanya mambo mema, na watu kuwafanyia ihisaani, hasa hasa katika Ramadhan **(Kwani mtume wa Mwenyezi Mungu alikua ni mbora wa watu, na alikua ni mbora wa watu zaidi inapo kuwa katika Ramadhani pale anapokutana na Jibriilu akifundiswa Qur'an**) (Sahihi Bukhary 1902).

Na miongoni mwa adabu za swaumu ni Mtu kujiepusha na mambo ambayo Mwenyezi Mungu ameyaharamisha kuyasema uwongo, na kutuna, na kufanya khiyana, na udanganyifu na kutizama mambo yaliyo haramishwa, na kusikiliza mambo ambayo ni haramu, na mengine yasiyo kuwa hayo katika mambo ambayo ni haramu, mambo ambayo niharamu kwa mfungaji na kwa ambae hakufunga, lakini mambo hayo kwa mfungaji yametiliwa mkazo zaidi kuyaacha.

Na miongoni mwa adabu za swaumu vile vile ni: kula daku, achelewe kula daku; kwa kauli ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema: ((K**uleni daku hakika katika kula daku kuna Barka**)) (Sahihi Bukhary 1923, na katika Sahihi Muslim 1095).

Na vile vile katika adabu za swaumu ni kufungua na kitu cha umajimaji , akikosa afungue kwa tende na akikosa afungue kwa maji, na vile vile kufanya haraka wakati wa kufungua wakati wa kuwa na uhakika wa jua kuzama, kwa maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: **((Watu hawatoacha kuwa katika heri muda wakua wanafanya harakakufungua**))

[Sahihi Bukhary kitabu Swaumu mlango wa kufanya haraka kufungua 1957, na katika Sahihi Muslim kitabu Swaumu mlango wa ubora wa kula Daku 1098].

****

**Swali la 436: Je kuna Dua zilizo pokelewa za kusomwa wakati wa kufungua? na je mfungaji anapo isikia Adhana amfuatishe muadhini kwanza au aendelee na kufuturu?**

**Jibu**: Hakika kusoma dua wakati wa kufungua ni wakati mzuri wa kukubaliwa Dua; kwa sababu ni mwisho wa ibada, kwa kuwa Mwanadamu wakati wa kufungua nafsi yake ni dhaifu sana, na moyo unapo kuwa mpole unakua karibu zaidi na kutubia na kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na Dua zilizo pokelewa ni: ((**Allaahumma laka swumtu wa alaa rizikuka aftwartu**)) Ewe mola wangu wa haki kwako wewe nimefunga na nimefungua kwa riziki yako, na katika Dua vile vile ni kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake wakati alipo fungua akasema:

((**Dhahaba dhwamau, wabtallatil uruuk wathabbatal ajiru inshaa Allah**)), [ameipokea Abuu Daud kitaabu Swaumu hadith no. 2357], Imeondoka kiu na imeroa mishipa na malipo yamethibiti akitaka Mwenyezi Mungu; na hadithi mbili hizi japo kuwa zinaudhaifu ndani yake lakina baadh ya wanachuoni Allaah awarehemu wamezisahihisha, na kwa hali yoyote utakapo omba kwa dua hizo, au au kwa Dua nyingine ambazo zimekujia moyoni mwako wakati wa kufungua zinakubaliwa.

Ama Mtu kumfuatishia Muadhini na wakati anafungua hii ni sharia hatamsubiri muadhini amalize bali atafungua na muadhini ana adhini kwa kuwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Mtakapo msikia Muadhini semeni mfano wa anayosema Muadhini**)) [ameipokea Bukhary kitabu cha Adhan hadith no. 611], maneno haya yamekusanya kumjibu muadhini kwa hali zote silazima umsubiri amalize ndiyo ufungue.

****

**Swali la 437: Ni upi ushauri wenu kwa mwenye kutaka kufunga swaumu ya sittatu shawwaali na ana Swaumu ya kulipa ya Ramadhan?.**

**Jibu**: Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Mwenye kufunga Ramadhan, kisha akafuatishia siku sita za mwezi wa Shawwaali amekua kama aliye funga mwaka mzima**)).

**Mfano:** Mtu kafunga Ramadhan siku ishirini na nne 24, na amebakiza siku sita, atakapo funga siku sita za mwezi wa shawwaali kabla ya kufunga siku sita alizo acha za Ramadhan haitwi kwamba amefunga Ramadhani, kisha akafuatishia masiku sita ya mwezi wa shawwaali; na pia hatumuiti kuwa kafunga Ramadhan

kamili ila atakapo ifunga mwanzo mpaka mwisho, kwa maana hiyo hayathibiti malipo ya kufunga siku sita za mwezi wa shawwaali kwa yule ambae anadaiwa Ramadhan, na suala hili siyo kwamba linamalumbano kwa wanachuoni katika kupitisha kufaa Sunna kwa Yule aliye na deni la kufunga; kwakuwa tofauti haziko kwenye siku sita, siku sita huwa zinaifuatia Ramadhan na haiwezekani kuthibiti malipo ya swaumu ya sita isipokua kwa yule ambaye amekamilisha Ramadhan kwanza, kama unadeni la Ramadhan ni kulilipa kwanza kisha ndiyo ufunge sita.

****

**Swali la 438: Mgomjwa amefungua katika mwezi wa Ramadhan na baada ya siku nne tangu kuingia mwezi akafa, je analipiwa Ramadhan?**

**Jibu**: Kama hayo maradhi yamemvamia ghafla na yakaendelea mpaka akafa basi hata lipiwa; kwasababu Allah Mtukufu amesema: [**Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini basi atimize hisabu katika siku nyingine**]. [Surat Baqara: 185], ambalo lilikuwa ni lazima kwake nikuja kufunga katika masiku mengine kwa maana alipe akisha pona, sasa kama amekufa kabla ya kulipa imepomoka kwake swaumu yani - siyo wajibu kwake na hatolipiwa; kwa kuwa hakufanikiwa kufika wakati ambao alitakiwa alipe swaumu,

kwahiyo yeye anakua kama aliye kufa katika mwezi wa shaabani, haimlazimu swaumu ya mwezi wa Ramadhan ambayo inakuja haijafika, ama kama ni ugonjwa ambao hautarajiwi kupona basi kawaida anapaswa kulisha masikini kila siku.

****

**Swali la 439: Mtu ana deni la swaumu moja ya Ramadhan iliyo pita na hakuilipa mpaka imeingia Ramadhan nyingine anafanyaje?**

**Jibu**: Allah Mtukufu anasema: [**Basi atakae kuwa mjini katika mwezi huu naafunge. Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini basi atimize hisabu katika siku nyingine**], [Surat Baqara: 185]. Mtu huyu aliyefungua kutokana na udhuru wa kisheria ni juu yake kulipa kwa kuifuata kauli hiyo ya Mwenyezi Mungu mtukufu, na inampasa kuilipa katika mwaka huo, asicheleweshe mpaka baada ya Ramadhani nyingine; kutokana na kauli ya Aisha mke wa mtume radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake amesema: ((**Ilikua ninakua na Swaumu kutoka ramadhani sikuweza kuilipa isipokua katika mwezi wa shaabani** )). Maneno haya ya bibi Aisha kuwa siwezi kuilipa ila katika shaabani ni dalili kuwa hapana budi kulipa swaumu kabla ya kuingia ramadhani nyingine, lakini itakapo tokea kuto kulipa mpaka ikaingia ramadhani nyingine basi

nijuu yake kutaka istighfaari na msamaha kwa Mwenyezi Mungu mtukufu na kutubia kwake, pia ajutie kwa kitendo hicho alicho kifanya, kisha ailipe siku hiyo; kwa sababu kuchelewesha kwake haiwi sababu ya kutokulipa, atailipa siku hiyo hata kama ni baada ya ramadhani ya pili. Mwenyezi Mungu nimwenye kuafikisha.

****

**Swali la 440: NI njia ipi bora ya kufunga Swaumu ya sita katika mwezi wa Shawwaali?**

**Jibu**: Ubora ni kufunga sita baada ya iddi tu unaunganisha na iwe kwa kufunga mfululizo kama walivyo eleza Wanachuonirehma na amani ziwe juu yao; kwa sababu utaratibu huo ni bora zaidi katika kuhakikisha kufuata Sunnahh kama alivyo eleza mtume: ((**Kisha akaifuatishia**)); yani baada ya ramadhani tu inafuatia sita hiyo ni bora katika kuipupia kheri; lengo nikufanya haraka ya vitendo na kuitumia nafasi iliyopo - na inatakikana kwa Mja kuyaendea mambo yake yote kwa haraka pindi tu anapogundua ukweli ndani yake.

****

**Swali la 441: Je inafaa kwa Mwanadamu kuchagua siku za kufunga katika Mwezi wa shawwaali, au siku hizi zina muda maalumu? na je atakapofunga muislam kwake inakua ni faradh yaani inakua lazima kwake kufunga kila mwaka?**

**JIBU**: Imethibiti kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake Amesema: ((Mwenye kufunga Ramadhan kisha akaifuatishia siku sita za mwezi wa Shawwaali anakua kama aliyefunga mwaka mzima)), na hizi siku sita hazina siku maalum, isipokua muumini anachagua mwenyewe katika miezi yote, akitaka atazifunga mwanzo wa mwezi, na akitaka atazifunga katikati ya mwezi, na akitaka atazifunga mwishoni mwa mwezi, na akitaka atazifunga kwa kuzigawanya, yani - afunge mbili mbili au tatu tatu kwa vile atakavyo weza, jambo hili lina nafasi pana Alhamduli LLah, kisha akizifunga siku sita hizo baadhi ya miaka, na kama ataziacha baadhi ya miaka pia hakuna tatizo; kwasababu ni Sunna na siyo faradhi.

****

**SWALI LA 442: Ni ipi hukmu ya kufunga siku ya A'shuraa?**

**Jibu**: Wakati mtume alipofika katika mji wa madina aliwakuta mayahudi wanafunga siku ya kumi katika Mwezi wa Muharram, akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwaambia mayahudi: ((**Mimi nina haki zaidi kwa mussa kuliko nyinyi**)) Mtume akazifunga siku kumi katika mwezi wa Muharram na aka amrisha zifungwe, [Sahihi Bukhary kitabu swaumu mlango wa aashuuraa 2004 na katika Sahihi Muslim 1130]. Na katika hadith aliyo ipokea Ibinu Abbasi Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - katika hadith ambayo wameafikiana juu ya usahihi wake - kwamba Mtume rehma na amani ziwe juu yake alifunga siku ya A'shuraa na aka amrisha ifungwe; na aliulizwa kuhusu ubora wake akasema: ((**Nataraji kwa Mwenyezi Mungu kufutiwa Madhambi ya Mwaka wa kabla yake**)) Isipokua baada ya hilo Mtume aliamrisha kutofautiana na mayahudi kwa kuamrisha A'shuraa ifungwe kuanzia siku ya kabla yake nayo ni siku ya tisa, na siku baadayake nayo ni siku ya kumi na moja. Na kufutana na hayo, lilo bora ni afunge siku ya kumi nan a kuongezea siku iliyo kabla yake, au siku baada yake; na kuongeza siku ya tisa ni bora kuliko siku ya kumi na moja.

Inatakikana kwako ewe ndugu yangu muislam - kuifunga siku ya A'shuraa na vilevile siku ya tisa - yani ufunge siku ya tisa naya kumi katika mwezi wa Muharram.

* * * *

**Swali la 443: Ni ipi hukmu ya kufunga katika Mwezi wa Shaban?**

**Jibu**: Kufunga katika mwezi wa shaabani ni Sunna na kufunga kwa wingi katika mwezi huo ni Sunna; kwa kauli yake Aisha radhi za mwenyezi Mungu ziwe juu yake: ((**Sikumuona akifunga sana isipokua katika mwezi wa shaabani**)), [Sahihi Bukhary kitabu Swaumu mlango wa Swaumu ya Shaban no. 1989, na katika Sahihi Muslim mlango wa Swaumu ya Mtume no. 1156], yani Aisha anasema hajamuona Mtume kufunga kwa wingi kama anavyo funga katika mwezi wa shaaban, inatakikana kufunga kwa wingi katika Mwezi wa shaabani kutokana na hadith hii ya Mtume. Na wamesema Wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu: Swaumu katika Mwezi wa shaabani ni kama vile Sunna zinazo swaliwa kabla na baada ya swala katika swala za faradh, pia inakua ni kama vile kitangulizi kwa ajili ya mwezi wa ramadhani, yani - kufunga shaabani nikama vile kuswali rakaa mmbili kabla ya swala , na vile vile kufunga siku sita katika mwezi wa shawwaali nikama vile kuswali baada ya swala, na kufunga katika mwezi wa shaabani kuna faida nyingine zisizokua hizo nazo ni: kuituliza Nafsi na kuiyandaa kwa ajili ya kufunga Ramadhan, ili swaumu iwe nyepesi kuitekeleza.

****

**Swali la 444: Ikiwa mtu amejiwekea kawaida anafunga siku moja na siku nyingine inayo fuata hafungi na ikatokea siku ambayo anataka kufunga ikawa ni siku ya ijumaa, Je inafaa afunge siku hiyo au haifai?**

**Jibu**: Ndiyo inafaa kufunga: ikiwa Mtu anafunga siku moja na siku inayo fuatia hafungi, anaweza kufunga siku ya Ijumaa, au Jumamosi, au Jumapili, au siku nyingine yoyote katika masiku, ikiwa siku hiyo haitakutana na siku ambazo zimeharamishwa kufunga, ikiwa swaumu hiyo itakutana na siku ambazo zimeharamishwa kufunga, inampasa asifunge katika siku hiyo, kwa mfano kama itatokea Mtu anafunga baadhi ya siku na baadhi ya siku hafungi ikawa siku ambayo hakufunga ni siku ya Alkhamisi na siku anayotaka kufunga ni Ijumaa basi hakuna tatizo akifunga siku hiyo ya Ijumaa, kwasababu hakufunga kuikusudia siku ya Ijumaa bali siku ya Ijumaa imeingiliana na siku ya swaumu yake, Ama itakapo kutana siku anayofunga na siku ambazo zimeharamishwa kufunga, basi inampasa kuacha kufunga siku hiyo, kwa mfano kama siku anayo funga itakutana na siku ya Iddi al - adhuha, au ikakutana na siku za tashriiki wakati wa hijjah, na kama ni mwanamke anafunga kwa mpangilio huo kufunga siku na kuacha kufunga siku inayo fuatia, kisha ikamjia hedhi basi hatafunga kwa kuwa siku yake ya kufunga imeingiliana na siku ambayo haruhusiwi kufunga katika siku hiyo.

**Swali la 445: Ni ipi funga ya kuunganisha?**

**Jibu:** Funga ya kuunganisha ni mtu kufunga au kujizuiya kula na kunywa na kufanya mambo yote yanayo haribu funga kwa muda wa siku mbili anafunga siku mbili za kufuatana bila kufungua, hakika mtume rehma na amani! Amekataza kufunga hiyo, amesema:

((**Anaetaka kuunganisha basi na aunganishe mpaka muda wa kula dakuu**)) [Sahihi Bukhary /1963]. Kuunganisha mpaka muda wa kula daku ni ruhusaa sio jambo la sheria, Mtume rehma na amani ziwe juu yake amehimiza kuwahi kufuturu aliposema: ((**Watu huwa wapo kwenye kheri wakiwahi kufuturu**)), [Sahihi Bukhary/1923, na Sahihi Muslim /1095]. Lakini wameruhusiwa kuunganisha mpaka muda wa kula daku tu na wasizidishe hapo, maswahaba walivyo sema kumwambia mtume rehma na amani ziwe juu yake, kwanini wewe unaonganisha fungaa? Mtume rehma na amani ziwe juu yake aliwajibu kuwa: ((**Umbile langu sio kama maumbile yenu**)) [Sahihi Bukhary /1922, na Sahihi Muslim /1102].

****

**Swali la 446: Ni ipi sababu ya kisheria ya kukataza kufunga swaumu ya Sunna siku ya ijumaa peke yake bila ya kutanguliza siku kabala au baada yake? Je katazo la kufunga siku ya ijumaa lina muhusu na mtu anaefunga kwa jili ya kulipa deni la swamu?**

**Jibu**: Imethibiti hadithi kutoka kwa mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Msii husishe siku ya ijumaa kwa kufunga swaumu wala kusimama kuswali usiku wake**)), [Sahihi Muslim /1144]. Hekma kwenye katazo la kuifanya siku ya Ijumaa kuwa siku maalumu kwa kufunga swaumu ni kwasababu siku ya ijumaa ni sikukuu ya wiki, pia siku ya Ijumaa ni miongoni mwa masiku matatu ya sikukuu za kisheria katika Uislamu, siku kuu za Kiislamu ni tatu sikukuu ya Iddi Al-Fitir inakuwa baada ya kumaliza mfungo wa ramadahani na sikukuu ya Iddi Al-Adhuhaa (sikukuu ya kuchinja) na sikukuu ya wiki nayo ni siku ya Ijumaa, kwa sababu hiyo sheria imekataza kuifanya kuwa ni siku maalumu kwa kufanya ibada ya funga, kwa kuwa wanaume wanatakiwa suku ya ijumaa waende kuswali misikitini na washugulike na kuomba dua na kumtaja Mwenyezi Mungu, siku ya ijumaa inafanana na siku ya arafaa siku hiyo ya arafaa sheriya haimruhusu kufunga mtu ambae yuko katika viwanja vya arafa katika mji mtukatifu wa Makkah anatakiwa ale katika mchana wa siku ya arafa, kwakuwa anae fanya ibada ya Hijjah anakuwa ameshughiliswa na ibada na kuomba dua na kumtaja Mwenyezi Mungu, pia inafahamika kuwa kunakuwa na msongamano wa ibada ambazo inawezekana baadhi ya ibada ukazichelewesha kuzifanya pia kuna kuwa na ibada huwezi kuzichelewesha kuzifanya katika siku hiyo.

Mtu akisema: Hakika inafaa sikukuu ya wiki inaonyesha mtu kufunga swaumu siku ya Ijumaa ni haramu kwa kuwa siku ya ijuma inachukuwa hukumu ya sikukuu ya iddi mbili iddi ya Al-Fitir na iddi Al-Adhuha, na haifai kuibagua sikukuu ya siku ya ijumaa.

Tunasema: Siku ya ijumaa inatofautiana na sikukuu mbili za iddi kwa kuwa sikukuu ya Ijumaa inajirudia mara nne ndani ya mwezi mmoja, kwa sababu hiyo katazo la kuwacha kufunga swaumu siku ya ijuma sio katazo la kuharamisha, pia sikukuu mbili za iddi zina maana nyingine, ambayo haipatikani katika siku ya ijumaa.

Kuhusu mtu kufunga siku moja kabla ya siku ya Ijumaa au kufunga siku baada ya siku ya Ijumaa kufunga huko hakumaanishi kuwa umeifanya siku ya Ijumaa kuwa ni siku maalumu kwa kufanya ibada ya funga, kwa kuwa kufunga siku moja kabla ya ijuma nayo ni siku ya Al-khamisi au kufunga siku baada yake nayo ni siku ya Jumamosi.

Kuhusu swali lilivyo ulizwa: Hivi katazo ni malumu kwa funga za Sunna au hata kwa mtu anae lipa deni la ibada ya funga?.

Katazo kwenye ushahidi unaonyesha ni kwenye funga za Sunna na mtu anae lipa deni la funga, kuwa ni karaha kuifanya siku ya ijumaa kuwa siku maalumu kwa ibada ya funga hata kama itakuwa funga ni ya Faradhi au ya Sunna, Lakini kama atakuwa anaetaka kulipa deni ni mfanya kazi siku yake

ya mapumziko ni Ijumaa tu na hawezi kulipa deni la funga isipokuwa siku ya Ijumaa anayo kuwa yupo kwenye mapumziko katika hali hiyo sio karaha kulipa deni la funga siku ya Ijumaa kwa sababu anahitaji kuilipa siku hiyo.

****

**Swali la 447: Mtu akiiharibu ibada yake ya funga ya Sunna je atapata dhambi? kama ataiharibu ibada hiyo kwa kufanya tendo la ndoa je anatakiwa kulipa kafara?**

**Jibu**: Mtu akifunga ibada ya Sunna kisha akafungua kwa kula au kunywa au kufanya tendo la ndoa na mke wake au mume wake hato pata dhambi kwa kuwa ibada yoyote ya Sunna mtu akiianza kuifanya sio lazima kuikamilisha isipokuwa ibada ya Hijja na Umrah lakini iliyo bora mtu aikamilishe ibada yake, Kwa misingi hiyo sio lazima kwa mtu huyo kulipa kafara kwa kufanya tendo la ndoa mchana akiwa amefunga Sunna kwakuwa sio lazima kuikamilisha ibada hiyo ya funga.

Kama itakuwa ni ibada ya funga ya faradhi akafaya tendo la ndoa na mke wake kitendo hicho hakiruhusiwi kisheriya kwa kuwa ibada ya funga ya faradhi hairuhusiwi kuikatisha isipokuwa kwa dharura, hato toa kafara isipokuwa kama atafanya tendo la ndoa mchana wa mwezi wa ramadhani na mtu huyo ni lazima kwake kufunga.

Kuwa makini na kauli yetu (Akiwa ni miongoni mwa wanao takiwa kufunga) kwa mfano mwanaume akiwa yupo safarini na mke wake wakafanya tendo la ndoa wakiwa safarini katka mchana wa mwezi wa ramadhani hawapati dhambi kwa kufanya tendo hilo la ndoa na hawatakiwi kulipa kafara isipokuwa wanatakiwa kuilipa siku hiyo badaa ya kumalizika mwezi wa Ramadhan.

****

**Swali la 448: Ni ipi hukumu ya kukaa itikafu? Je inaruhusiwa aliye kaa itikafu kutoka nje ya msikiti kwa ajili ya kukidhi haja zake na kutoka kwa ajili ya kula, au kutoka kwa ajili ya kupata matibabu? Ni zipi Sunna za itikafu? Na Mtume alikaa vipi itikafu?**

**Jibu**: Itikafu ni mtu kukaa msikitini kwa niya ya kufanya ibada na kumtii Mwenyezi Mungu, kukaa itikafu ni Sunna kwa mtu ambae napupia kutafuta usiku wa cheo (laylatul qadri) katika mwezi wa ramadhani, Ameelizea ibada hiyo Mwenyezi Mungu katika Qur`an: **{Wala msichangayike nao na hali mnakaa itikafu msikitini}**, [Suratul Baqara: 187]. Na imethibiti hadithi katika Swahihi Bukhari na Swahihi Muslimu na katika vitabu vingine kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alikaa itikafu pia Maswaahaba zake walikaa itikafu wakiwa na Mtume Ibada ya itikafu ikaendelea kuwa ipo kisheriya haikufutwa kisheriya kwa mujibu wa hadithi iliyopo katika Sahihi

Bukhary na Sahihi Muslim, kuwa Aisha radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake amesema: ((M**tume alikuwa anakaa itikafu katika makumi ya mwisho ya mwezi wa remadhani mpaka alivyo fariki Mtume wa Mwenyezi Mungu kisha wake zake mtume walikaa itikafu baada ya kufa mtume**)), [Sahihi Bukhary /2026, na Sahihi Muslim /1172]. Katika Sahihi Muslim imepokewa hadithi kutoka kwa Said Al-Khidry radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kuwa Mtume alikaa itikafu katika kumi la mwanzo katika mwezi wa Ramadhan kisha akakaa katika kumi la katikati kisha Mtume akasema: ((**Mimi nimekaa katika kumi la kwanza kwajili ya kutafuta usiku wa cheo (Laylatul Qadir) kisha nimekaa itikafu katika kumi la katikati kisha nimejiwa nikaambia: Usiku wa cheo unapatikana katika kumi la mwisho atakae taka kati yenu kukaa itikafu basi na akae**)), [Sahihi Bukhary /2027], na Watu wakakaa itikafu pamoja na Mtume.

Amesema Imamu Ahmadi bin Hambali radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: Sifahamu mwachuoni yeyote aliye sema kuwa itikafu sio Sunna.

Kwa misingi hiyo kukaa itikafu ni Sunna kwa ushahidi wa matini ya Qur`an na hadithi na makubaliano ya Wanachuoni.

Sehemu inayo takiwa kukaa itikafu ni katika misikiti ambayo huswaliwa swala za jamaa katika nchi yoyote au mji wowote kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu [**Na hali mnakaa itikafu msikitini**], Iliyo bora iwe ni kwenye msikiti unao swaliwa ijumaa ili asipate shida ya kwenda kuswali ijumaa kwenye msikiti mwengine kama atakaa kwenye msikiti usio swaliwa ijumaa sio vibaya lakini ajitahidi kuwahi kwenda katika msikitini siku ya ijumaa.

Anatakiwa kwa aliyekaa itikafu ajishughulishe na kufanya ibada kuswali na kusoma Qur`ani na kumtaja Mwenyezi Mungu kwa kuleta nyiradi kwakuwa hayo ndio makusudio ya kukaa itikafu pia sio vibaya kama atazungumza na marafiki zake kwa muda mfupi hasa kama watazungumza mambo yenye faida.

Niharamu mtu aliye kaa itikafu kufanya tendo la ndoa au kuchezeana kimapenzi au kutomasana tomasana yote mawili ni haramu akiwa katika itikaafu.

Kuhusu kutoka msikini kwa mtu aliye kaa itikafu wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu jambo hili la kutoka msikitini kwa aliye kaa itikafu wame ligawa sehemu kuu tatu:

**Sehemu ya kwanza:** Anaruhusiwa kutoka, Ni kutoka kwa kufanya jambo ambalo ni lazima atoke kwa mujibu wa sheriya au kimaumbile, kama mtu kutoka kwenda kuswali ijuma kwa mtu aliye kaa itikafu katika msikiti usio swaliwa ijumaa, au mtu kutoka nje ya msikiti kwa ajili ya kwenda kula na kunywa kama atakuwa hana mtu wakumletea chakula na kutoka nje ya msikiti kwa ajili ya kutawadha na kuoga jambo ambalo ni lazima pia kwenda kujisaidia haja kubwa au ndogo.

**Sehemu ya pili**: kutoka nje ya msikti kwa ajili ya kufanya ibada ambayo ni lazima yeye kuifanya kama kwenda kumtembelea mgonjwa na kwenda kumzika mwislamu mwenzake isipokuwa kama ata jiwekea masharti kuwa hato toka basi hairuhusiwi kutoka, Lakini kama hakujiwekea mashariti anaruhusiwa kutoka.

**Sehemu ya tatu:** Ni kutoka kwa ajili ya kufanya jambo ambalo hairuhusiwi kwa mtu aliye kaa itikafu kulifanya kama mtu kutoka kwenda nyumbani kwake bila sababu au kwenda kununua vitu bila ya kuwa na hajaa ya msingi au kwenda nyum-

bani kwake kufanya tendo la ndoa na mke wake nk. Yote hayo haruhusiwi kuyafanya pia haruhusiwi kuweka mashariti katika kufanya hayo pia hata kama hakuweka sharti haruhusiwi kuyafanya. Mwenyezi Mungu ndio mjuzi .

****

**Swali la 449: Akifanya ibada ya Hijja mtu amabae haswali wala hafungi mwezi wa Ramadhan, ni ipi hukumu ya Hijja hiyo? Je mtu atalipa ibada alizoacha baada ya kutubia kwa Mwenyezi Mungu?**

**Jibu:** Kuacha swala ni kitendo cha kikafiri kinacho mtoa mtu kwenye uwislamu kitendo hicho cha kuwacha swala kinamlazimu mtu akifa aishi milele katika moto kwa ushahidi wa Qur`an na hadithi na kauli za watu wema waliyo tangulia, kwa misingi hiyo mtu ambae haswali siyo halali kwa mtu huyo kuingia katika mji mtakatifu wa Makkah, kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu:

[**Enyi mlio amini hakika washirikina ni najsi kwa hivyo wasiukaribie msikiti mtakatifu baada ya mwaka wao huu**], [Surat Tawba: 28 ].

Kufanya ibada ya Hijjah mtu akiwa haswali ibada hiyo haifai wala haikubaliwi kwakuwa ameingia kwenye ukafiri kwa kuwacha swala na kafiri haiswihi ibada yake, Kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Na hawakuziwiliwa kukubaliwa michango yao ila kwa kuwa walimkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake wala hawaji kwenye swala ila kwa uvivu wala hawatoi michango ila nao wanachukia**], [Surat Tawba: 54]. Kuhusu ibada alizo acha kuzifanya sio lazima kuzilipa, kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Wambie wale waliyo kufuru wakikoma watasamehewa yalio kwisha pita**],

[Suratul Anfaal: 38].

Atakae kuwa amefanya hivyo basi atubu kwa Mwenyezi Mungu toba ya kweli na aendelee kufanya ibada na Mambo yanayo mridhisha Mwenyezi Mungu na azidishe kuomba msamaha na toba na kufanya mambo mema, hakika Amesema Mwenyezi Mungu: [**Sema: Enyi waja wangu waliyo jidhulumu nafsi zao msikate tamaa na rehma za Mwenyezi Mungu hakika Mwenyezi Mungu husamehee dhambi zote hakika yeye ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu**], [Surat Zumar: 53]. Aya hii imeteremka ikielezea habari za wanao tubu kwa Mwenyezi Mungu, kila dhambi ambayo mjaa anatubu kwa Mwenyezi Mungu hata kama ni shirki Mwenyezi Mungu anakubali toba yake na Mwenyezi Mungu ndio anae ongoza watu katika njia iliyo nyooka.

****

**Swali la 450: Maranyingi tunaona baadhi ya waislamu hasa vijana wanapuzia kufanya ibada ya Hijja wanasema tutafanya tu, ni ipi hukumu ya jambo hilo? Na mnatupa nasaha gani? Mara nyingine tunawaona wazazi wanawazuilia vijana wao wa kiume kwenda kufanya ibada ya Hijja kwa madai kuwa wanahofia kuwa bado ni wadogo pamoja na kuwa wamekamilisha masharti ya kutekeleza ibada hiyo, ni ipi hukumu ya mzazi huyo? Na ni ipi hukumu ya watoto kuwatii wazazi katika jambo hilo? Naomba Mwenyezi Mungu awalipe kheri dunia na akhera.**

**Jibu**: Inafahamika kuwa ibada ya Hijjah ni katika nguzo tano za uwislamu na uwislamu wa mtu hauwezi kukamilika isipokuwa mpaka afanye ibada ya hijja kama atakuwa amekamilisha mashart yanayo mfanya kuwa Hijja ni lazima kwakwe hairuhusiwi kwa mtu ambae amekamilisha mashart ya kuwa Hijjah ni wajibu kwake acheleweshe ibada hiyo kwakuwa Mwenyezi Mungu mtukufu ame muamrisha Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake kuifanya ibada hiyo kwa haraka, pia mwanaadamu hafahamu yatakayo tokea baadae huenda akafilisika au akapata maradhi au kifo.

Hairuhusiwi kwa wazazi wa kiume au wakike kuwaziwia watoto zao wa kiume kwenda kufanya ibada ya hijja, vijana hao watakapo kamilisha masharti na vijana hao wakiongozana na marafiki zao waaminfu kweye dini na tabia wanatakiwa waende wakakamilishe ibada hiyo.

Pia hairuhusiwi kwa watoto wa kiume kumtii mzazi wake wa kiume au wakike atakapo mzuilia kwenda kufanya ibada ya hijja pale itakapo kuwa ni lazima kwa vijana hao kufanya ibada hiyo ya Hijja, kwa sababu hakuna ruhusa ya kumtii kiumbe yeyote katika jambo la kumuasi Mwenyezi Mungu, Isipokuwa kama wazazi watatoa hoja za kisheriya za kuwaziwia watoto hao wasiende kufanya ibada hiyo ya hijja kwa hali hiyo watoto waanatakiwa kuchelewesha ibada hiyo mpaka hizo sababu za kuichelewesha ibada hiyo zitakapo ondoka.

Namuomba Mwenyezi Mungu atuafikishe kufanya mambo yote yenye kheri na manufaa.

****

**Swali la 451: Mtu anae daiwa (mwenye deni) ni lazima kwake kwenda kufanya ibada ya Hijja?**

**Jibu**: Atakae kuwa na deni linalo zidi mali zake mtu huyo sio wajibu kwakwe kwenda Makkah kufanya ibada ya hijja kwa kuwa Mwenyezi Mungu ameifanya ibada hiyo kuwa ni wajibu kwa mtu mwenye uwezo, amesema Mwenyezi Mungu: [**Na kwajili ya Mwenyezi Mungu ime wawajibikia watu wahiji kwenye nyumba hiyo kwa Yule mwenye uwezo njia ipo wazi**], [Surat Al-Imran: 97]. Mtu Mwenye deni linalo zidi mali zake huyo hana uwezo wa kwenda kufanya ibada ya Hi-

jja, kwa misingi hiyo anatakiwa alipe deni analo daiwa, kama Mwenyezi Mungu atamuwekea wepesi atakwenda kufanya ibada hiyo ya Hijja mwaka mwengine.

Kama deni litakuwa ni ndogo kuliko mali alizo nazo kiasi chakuwa anaweza kwenda hijja baada ya kulipa deni, anatakiwa kulipa deni kisha aende kufanya ibada ya Hijja, hata kama itakuwa ni Hijja ya faradhi au Hijja ya Sunna, lakini kama itakuwa ni Hijja ya Faradhi ni lazima aifanye kwa haraka, ama kwenda kufanya ibada ya Hijja isio kuwa ya faradhi anakhiyari akitaka atafanya ibada hiyo ya Sunna asipo taka ata acha kuifanya na hatopata dhambi.

****

**Swali la 452: Mwenye kumtafuta mtu amuhijie mama yake kisha akafahamu kuwa mtu aliye pewa kumuhijia mama yake amepewa uwakala wa hijja nyingi ni ipi hukumu ya hilo? Tunaomba majbu, Naomba Mwenyezi Mungu awasamehe madhambi yenu.**

**Jibu**: Inatakiwa mtu awe makini katika mambo yake na asimpe mtu kumfanyia kitu isipokuwa mtu ambaye ana muamini katika dini yake na muaminfu mwenye elimu katika jambo ambalo anampa alifanye kumuwakilisha, kama utataka kumpa

mtu amuhijie baba yako au mama yako aliye fariki ni lazima uchague mtu unae muamini kwenye elimu na dini yake, kwa sababu watu wengi hawana elimu ya ibada ya Hijja kuzifahamu hukumu za Hijja, hawatekelezi ibada ya Hijja kama inavyo takiwa, hata kama watakuwa ni waaminifu Lakini wanadhani kuwa hiyo ibada ni wajibu kwao, kwa misingi hiyo wanakosea sana mfano wa watu hao haifai kuwapa kufanya ibada ya hijja kwa niaba ya aliyefariki kwa sababu wanamapungufu kwenye elimu yao, pia kuna watu wana elimu lakini sio waaminifu utamkuta hatekelezi anayo yasema au anayo yafanya katika ibada ya hijja kwa sababu ya udhaifu wake katika dini yake, mfano wa mtu huyo haitakiwi kumpa amuakilishe katika kutekeleza ibada ya hijja, Mtu ambae anataka kumpa mtu afanye ibada ya hijja kwa niaba achague mtu bora kielimu na dini ili mtu huyo afanye ibada hiyo katika namna inayo takiwa.

Na mtu huyu ambae Ameuliza kuwa alimpa mtu amuhijjie mzazi wake kisha akasikia kuwa mtu huyo alichukuwa Hijja za watu wengi jambo hili inabidi lichunguzwe, huenda mtu huyo alizipokea Hijja hizo kwa niaba ya watu wengine na watu wengine ndio watakao zitekeleza ibada hizo za Hijja alizo zipokea, yeye akafanya ibada ya huyo aliye pewa amafanyie ibada kwa niaba, lakini inaruhusiwa mtu kufanya hivyo? Hivi inaruhusiwa mtu atafute watu wa kuwa wakilisha watu katika kufanya ibada ya hijja au umrah, kisha yeye aliye pokea ibada hizo hafanyi lakini wanamuakilisha watu wengine?

Tunasema kukujibu kuwa: Kufaya hivyo haifai na sio halali, kufanya hivyo ni katika njia ya kula mali kwa batili, wapo watu wanavuka mipaka katika jambo hili utamkuta anachukuwa hijja nyingi na ummra nyingi, na kukubali kuwa yeye ndio ata-

fanya, lakini anawakilishwa kufanya ibada hizo na watu wengine tofauti anawapakiwango kidogo cha pesa kuliko wanacho kiridhia hao wanao muakilisha na kiwango kidogo kuliko alicho pokea kutoka kwa wahusika, anachuma mali kwa njia ya batili, anawapa watu walio fanya ibada hiyo kiwango kidogo cha pesa wasicho kiridhia wanao fanya ibada hiyo ya hijja na umrah, Inatakiwa mtu wamuogope Mwenyezi Mungu kwenye mambo ya ndungu zao na wamuogope Mwenyezi Mungu katika nafsi zao, kwakuwa kuchukuwa mali hiyo unakuwa umechukuwa bila ya haki, pia ukiaminiwa na ndungu zako kuwa wewe ndio utafanya ibada ya Hijjah au umrah hairuhusiwi kumpa mtu mwengine akuwakilishe katika kufanya ibada hiyo, kwakuwa huyo mtu mwengine inawezekana hato ridhia kumpa afanye ibada hiyo ya Hijja au ya umrah.

****

**Swali la 453: Mtu ambae umri wake ni mkubwa, amehirimia ibada ya Umrah (kunuwia) alivyo fika katika nyumba ya Mwenyezi Mungu Makkah ameshindwa kufanya ibada hiyo ya Umrah atafanyaje?**

**Jibu**: Ataendelea kubaki katika ihirami yake mpaka atakapo changamka, isipokuwa kama atakuwa ameweka sharti wakati ana hirimia (kutia nia) kuwa nikipata pingamizi lolote likanizuilia kutimiza ibada yangu, basi ibada yangu itaishia sehumu hiyo nilipo pata tatizo, mtu huyo atakuwa ametoka kwenye ibada

hiyo wala hato takiwa kulipia fidia yoyote, Hato fanya ibada ya umrah wala hato tufu twawafu ya kuwaga, (Kuzunguka Al-Kaaba) kama hakusema hivyo na hatarajii nimuda gani tatizo hilo litaondoka, basi mtu huyo atajitoa kwenye ibada hiyo badala yake atatoa fidia ya kichinja kama atakuwa na uwezo, kwakuwa Mwenyezi Mungu anasema: [**Na timizeni Hijjah na Umrah kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na ikiwa mkizuiwa basi (chinjeni) waanyama walio wepesi kupatikana wala msinyoe vichwa vyenu mpaka wanyama hao wafike Machinjioni**] [Suratul Baqara: 196]. Pia mtume rehma na amani ziwe juu yake alivyo zuiwiliwa na makafiri kufanya ibada ya Umrah katika sehumu ya hudaibiya alichinja mnyama wake akajitoa kwenye ibada hiyo, [Sahihi Bukary 1809].

****

**Swali la 454: Mtu akihiji kwa niaba ya mtu mwengine kwa ujira na ikabaki pesa nyingine kwenye ujira alio pewa hivi ataichukuwa pesa hiyo?**

**Jibu**: Mtu akipokea pesa ili ahiji kwa kutumia pesa hiyo na pesa ikawa nyingi kuliko matumizi ya anae hiji, sio lazima kwa mtu huyo kurudisha pesa hiyo kwa aliyempa Isipokuwa yule aliyempa kama alisema kumwambia: (Hiji kutokana na sehemu ya pesa hiyo) na hakusema: (Hiji kwa pesa hiyo), kisema: (Hiji kutokana na sehemu ya pesa hiyo) hakika pesa itakayo zidi kwenye matumizi ni lazima airejeshe kwa mwenyewe, kama

akitaka atampa na akitaka atachukuwa pesa yake, lakini kama atasema: (Hiji kwa pesa hiyo) Mtu huyo sio lazima kurejesha chochote katika pesa hiyo, isipokuwa kama mtu aliye mpa pesa hiyo hafahamu mambo ya gharama za Hijjah akadhani kuwa Hijjah inahitaji matumizi makubwa akampa pesa kulingana na ufahamu wake, katika hali hiyo ni lazima amuweke wazi, amwambie: nimehiji kwa gharama kadha na kadha pesa uliyo nipa ni nyingi kuliko gharama nilizo zitumia, katika hali hiyo akimruhusu kuzitumia na akasamehe hakuna ubaya kwa mtu huyo kuzitumia.

****

**Swali la 455: Mtoto akifanya ibada ya Umrah kwa ajili ya baba yake aliye fariki anaruhusiwa ajiombe dua Mwenyewee?**

**Jibu**: Anarusiwa ajiombee dua mwenyewe katika ibada hiyo ya Umrah, pia inaruhusiwa amuombee dua baba yake na waislamu wote anao wataka, kwa kuwa makusudio afanye vitendo vya ibada ya Umrah kwa aliye mkusudia. Kuhusu kuomba dua sio nguzo katika ibada hiyo wala sio sharti kwa hivyo anaruhusiwa kujiombea dua mwenyewe, na anaruhusiwa kumuombea dua yule aliye mkusudia kumfayia ibada hiyo na waislamu wote.

****

**Swali la 456: Ni ipi hukumu ya kufanya ibada ya Umrah au Hijjah kwa niaba ya mtu mwengine?**

**Jibu**: Mtu kufanya ibada ya kwa niaba ya mtu kumegawanyika sehemu kuu mbili:

**Sehemu ya kwanza:** Amuwakilishe kwenye ibada ya faradhi (ya lazima).

**Sehemu ya pili**: Nikufanya ibada ya Sunna kwa niaba ya mtu mwengine.

Kama itakuwa ni ibada ya faradhi hairuhusiwi mtu mwengine amuwakilishe kwenye kutekeleza ibada ya Hijjah au Umrah, Isipokuwa kama atakuwa mtu huyo hawezi kufika Mwenyewee katika nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu ilio Makahh, kwa sababu ya maradhi ya kudumu mabayo hatarajii kupona, au uzee nk. Kama atakuwa na maradhi nayo tarajia kupona basi atasubili mpaka Mwenyezi Mungu amponye, Na atatekeleza ibada hiyo ya Hijjah Mwenyewee kama atakuwa hana jambo amabalo litakalo Mziwia kufanya ibada ya Hijjah, bali anaweza kufanya ibada hiyo Mwenyewee, mtu huyo sio halali amuakilishe mtu mwengine katika kutekeleza ibada hiyo, kwa kuwa inatakiwa yeye Mwenywee ndio aitekeleze ibada hiyo, amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: [**Na kwajili ya Mwenyezi Mungu imewajibika watu wahiji kwenye nyumba hiyo kwa Yule Mwenye uwezo njia ya kwendea**], [Surat Al-Imran: 97]. Ibada inakusudiwa mtu aitekeleze yeye Mwenyewe ili ikamilikee kwake kufanya ibada na kuyenyekea kwa Mwenyezi Mungu, na jambo hili linafahamika kuwa anae wakilishwa hua haya patikani hayo mambo makubwa ambayo ibada ineanzishwa

kwa ajili ya mambo hayo.

Kama itakuwa anae wakilishwa ameisha tekeleza faradhi ya Hijja akataka mtu amuakilishe katika ibada ya Hijjah au umrah, Wanachuoni wametofautina:

Wapo waliyo sema kuwa inaruhusiwa, na wapo waliyo sema kuwa hairuhusiwi.

Na hoja ilio karibu kwangu ni kuwa haifai, na kuwa hairuhusiwi kwa mtu yoyote amuwakilishe mtu ahiji kwa niaba yake au fanye ibada ya umrah kwa niaba yake kama itakuwa ni ibada ya Sunna, kwa kuwa asili katika ibada mtu aifanye Mwenywe, kama ilivyo kuwa haifai mtu awakilishwe na mtu Mwengine kwenye ibada ya funga ya ramadhani, pamoja na kuwa mtu akifa na anadaiwa deni la funga ya faradhi ya Ramadahan atatakiwa amfungie walii yake, pia katika ibada ya Hijjah kama atakufa akiwa haja hiji atamuhijia walii wake, ibada ya Hijjah hua inatakiwa aifanye mtu mwenyewe na siyo ibada ya kipesa inayo mnufaisha mwengine, kama ibada itakuwa ni ya kutumia mwili haifai kuifanya mtu mwengine mpaka mtu aifanye mwenyewe, isipokuwa kama kutakuwa na ushahidi katika mafunzo ya mtume rehma na amani ziwe juu yake, na haikuthibiti katika hadithi za mtume kuwa mtu anaruhusiwa akamhijie mtu mwengine ibada ya Umrah kwa ushahidi wa riwaya mbili alizo zipokea imamu ahmadi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake nakusudia kuwa haifai kumuakilisha mtu mwengine katika Hijjah ya Sunna au ibada ya umrah , akiwa na uwezo au hata kama hana uwezo, na sisi tunapo sema kauli hii kwakuwa tunawahizima matajiri wano weza kwenda kufanya ibada ya Hijjah wao wenyewe waende na wasisubirie kuwakilishwa, kwakuwa baadhi ya watu inapita miaka mingi lakini hawaendi Makkah

kufanya ibada ya Hijjah wakitegemea kuwa watawakilishwa na watu wengine kuwahijia kila mwaka, inawapita sababu ya kufaradhiswa iabada ya Hijjah kwa kutegemea kuwakilshwa na watu wengine kuwafanyia ibada hiyo ya Hijjah.

****

**Swali la 457: Je inaruhusiwa kufanya ibada ya Umrah kumfanyia mtu aliye fariki?**

**Jibu**: Inaruhusiwa kumfanyia ibada ya Umrah mtu aliye fariki kama inavyo ruhusiwa kumfanyia Hijjah mtu aliye fariki, pia kumfanyia twawafu inaruhusiwa (kuzunguka al-kaaba) pia inaruhusiwa kumfanyia mtu aliye fariki ibada zote nzuri na njema, amesema Imamu Ahmadi rehama na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kila ibada mtu akifanya kisha akaweka thawabu zake kwa lie fariki au aliye hai mwislamu zinammnufaisha, lakini kumuombea dua maiti nibora kuliko kumpa zawadi ya thawabu ushahidi wa kauli yangu hii ni kau ya mtume rehma na amni ziwe juu yake: ((**Akifariki mwaana adamu ibada zake zote zinakatika isipokuwa mambo matatu: sadaka inayo endelea kuwapata malipo au elimu yenye manufaa au mtoto mwema anae muombea dua**)), [1631/ Sahihi Muslim] ushahidi katika hadithi hii ni kuwa mtu hakusema: ((**Au mtoto mwema anae fanya ibada kwa ajili ya babake au anasoma au anaswali au anafanya ibada ya umrah au anafunga**)), au kauli inayo fanan na hiyo pamoja kuwa hadithi inaelezea matendo,

mtume ameelezea matendo ambayo yanakatika baada ya kufariki, kama ingekuwa kinacho takiwa kwa mwanaadamu afanye ibada kwa aliji ya baba yake au kwa ajili ya mama yake, mtume anage sema: ((**Au mtoto mwema nae fanaya ibada kwa ajili ya mzazi wake**)), lakini kama mtu atafanya ibada kisha akampa zawadi kwa mtu yoyote katika waislamu inafaa kufanya hivyo.

****

**Swali la 458: Mwanamke akienda kufanya ibada ya Hijjah bila kuwa na mtu amabe hawezi kumuoa (Mahrim) je Hijjah yake ni sahihi? Na vipi mtoto wa kume ambae anajitambua anahesabiwa kuwa ni mahram (Ambae haruhusiwi kumuoa mwanamke)? Na nimasharti gani kwa mahram?**

**Jibu**: Hijjah yake ni sahihi, lakini kitendo cha kusafiri bila kuwa na mtu ambae ni mahram kwake jambo hilo ni haramu na amemuasi mtume wa Mwenyezi Mungu rehma na amaniziwe juu yake, hakika Mtume rehma na amani amesema: ((**Asisafiri mwanamke isipokuwa awe na mtu ambae haruhusiwi kumuoa**)) [1862/ Sahihi Bukhary, 1341/ Sahihi Muslim].

Na mtoto mdogo wa kiume amabe haja fikia baleghe, hakuhirimia ibada hiyo, kwakuwa yeye mwenyewee anahitaji usimamizi na uangalizi, na mtu huyo hatakiwa kuwa ndio muangalizi wa mtu mwengine na hatakiwi kuwa walii wa mtu mwengine.

Kuhusu mashart ya mahrami ni lazima awe mwislamu mwanaume aliye fikia baleghe, awe na akili timamu, kama atakuwa hana sifa hizo basi huyo sio mahram.

Najambo hili linatia huzuni sana nalo ni: Kuzembea kwa baadhi ya wanawake kusafiri kwa ndege bila kuwa na mahrami wake, hakika wanawake hao wanapuzia sana jambo hilo, utamkuta mwanamke anasafiri kwa ndegee akiwa pekeake, wanatoa hoja kuwa mahrami anampeleka hadi uwanja wa ndege kisha mahrami mwengine atampokea uwanja wa ngede huko anako kwenda na wanasema kuwa kwenye ndege kunaa amani.

Hiyo sababu sio sahihi, kwakuwa mahrami anae mpeleka uwanja wa ndegee hamfikishi hadi kwenye ndege isipokuwa namuacha kwenye ukumbi wa wasafir kwa ajili ya kusubilia ndege, huenda ndege ikachelewa kuondoka akabaki huyo mwanamke amepotea.

Hunda ndege ikaruka ikashindika kutuwa sehemu ambayo intakiwa itue kwa ajili ya sababu za hali ya hewa, ndege ikatuwa sehemu nyingine akapotea huyo mwanamke. Na huenda akafika katika uwanja wa ndege asipokelewe na huyo mahrami ambae alitakiwa kuja kumpokea kwa sababu ya maradhi au kapitiwa na usingizi au ajali ya gari ambayo itasababisha asifike uwanjani kumpokea au mambo mengine kama hayo.

Kama mambo yote hayo hayakutokea na ndege ikafika katika muda wake halisi na kamkuta mahrami wake amekuja kumpokea, Lakini nani atake kaa pembeni ya mwanamke huyo kwnye ndege? Huenda akawa jirani yake mwanaume ambae hamuogopi Mwenyezi Mungu wana hawahurumi waja wa Mwenyezi Mungu kanaza kumwambia mabo ya kipuzi na mwanamke

huyo akaningia kwenye fitna ya kapatika mambo ya haramu kama inavyo fahamika.

Nilazima kwa wanawake wamuogope Mwenyezi Mungu mtukufu wala wasisafiri isipokuwa wawee na mahrami zao, Pia ni lazima kwa wano wasimamia wa wanawake miongoni mwa wanaume amabo Mwenyezi Mungu amewapa usimamizi kwa waanawake wamuogope Mwenyezi Mungu mtukufu, wala wasivuke mipaka katika maharimi zao wala wasiiondoshe uwislamu wa wanawake hao na aibu zao, Hakika mtu ataulizwa siku ya kiama juu ya familia yake, kwa Mwenyezi Mungu ameifanya hiyo kuwa ni amana juu yao, amesema Mwenyezi Mungu: [**Enyi mlio amini zikingeni nafsi zenu na ahli zenu na moto ambao kuni zake ni watu na mawe wanausimamia malaika wakali wenye nguvu hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa anayo wamirisha na wanatenda wanayo amrishwa**], [Surat Tahrim: 6].

****

**Swali la 459: Mwanamke anasema: Nanuwiya kutekeleza ibada ya Umrah katika mwezi mtukufu wa Ramadhan lakini nitakwenda kufanya ibada hiyo nikiwa na dada yangu pamoja na mume wake na mzazi wangu wa kike je ninaruhusiwa?**

**Jibu**: Hairuhusiwi kwenda nao kwa ajili ya kufanya ibada ya Umrah kwa kuwa mume wa dada yako siyo maharam kwako na imethibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake hadithi alio ipokea ibun abasi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake amesema: Nilimsikia Mtume anahutubia, Akasema: ((**Asikae sehemu ya kujitenga mwanamke na mwanaume isipokuwa awe na mahrami wala asisafiri mwanamke isipokuwa awe na mahrami**)). Akasimama mtu mmoja akasema : Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hakika mke wangu ametoka kwa ajili ya kwenda kufanya ibada ya Hijjah Nami jina langu limeandikwa kuwa nitakuwa katika vita kadha na kadha , Akasema mtume rehama na amani ziwe juu yake: ((**Nenda ukahiji na mke wako**)), [1862/ Sahihi Bukhary, 1341 Sahihi Muslim]. Mtume hakumuliza hivi mke wako yupo na wanawake wengine? Hivi mke wako ni kijana au mzee? Hivi kuna amani au hakuna amani? Na mambo haya kama mwanamke ataacha kwenda kufanya ibada ya umrah kwa sabbu hana mahrami mwanamke huyo hapati madhambi, hata kama alikuwa hajawahi kufanya umrah kabla, kwa kuwa miongoni mwa masharti ya uwajibu wa ibada ya umrah na Hijjah ni mwanamke awe na mahrami (mwanaume ambae haruhusiwi kumuoa).

****

**Swali la 460: Ni ipi mipaka ya Hijjah ya nyakati?**

**Jibu**: Mipaka ya Hijjah ya nyakati inaanza kwa kuingia mfungo mosi inaisha Ima kwa kuisha masiku kumi ya Dhul-Hijjah mfungo tatu au siku ya sikukuu ya Iddi al-adhuha ama kuisha mwezi wa Dhul-Hijjah mfungo tatu, na kauili hiyo ndio sahihi kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Hijjah ni miezi maalumu**], [Suratul Baqara: 197]. Na maana ya muda huo wa miezi hiyo ndio muda inafanyika ibada ya Hijjah katika miezi hiyo mitatu na haifanyii katika siku miongoni mwa siku hizo kwakuwa Hijjah inamasiku yake maalumu, isipokuwa ibada ya kutufu na saayi (Swafaa na Mar'wa) tukisema kuwa mwezi wa Dhul-Hijjah wote ni wakati wa kufanya ibada ya Hijjah, kwahivyo anaruhusiwa mtu kuichelewesha twawafu ya ifadhwa na say ya ibada ya Hijjah mpaka siku ya mwisho ya mwezi wa dhul-Hijjah (mfungo tatu) Wala haruhusiwi kuchelesha zaidi ya hapo, isipokuwa kwa udhuru kama mwanamke akitokwa na damu ya nifasi kabla ya kutufu twawafu ya ifadhwa damu ya nifasi ikaendelea kutoka mpaka mwezi wa Dhul-Hijjah ukaisha mwanamke huyo anakuwa na udhuru wa kuchelewesha twawafu ya ifadhwa, hiyo ndio mipaka ya nyakati za ibada ya Hijjah .

Kuhusu ibada ya umrah haina mipaka ya nyakati, unaruhusiwa kuifanya ibada hiyo muda wowote katika masiku ya mwaka, lakini kuifanya katika mwezi wa Ramadhani malipo yake yanalingana kama mtu aliye fanya ibada ya Hijjah, katika miezi ya Hijjah mtume rehma na amani ziwe juu yake alifanya ibada zake zote za umrah katika nyakati hizo, umrah ya hudaybiya ilikuwa katika mwezi wa Dhul-Qaada (mfungo pili)

na Umrah alio kuja kulipa ilikuwa Dhul-Qaada ( mfungo pili) na umrah alio ifanya na ibada ya Hijjah ilikuwa katika miezi ya Hijjah huenda kutakuwa na mambo maalumu na ubora katika miezi hiyo, kwa sababu Mtume rahama na amani ziwe juu yake alichagua kufanya ibada ya Umrah katika miezi hiyo.

****

**Swali la 461: Ni ipi hukumu ya kuhirimia ibada ya Hijjah kabla ya kuingia mipaka ya nyakati?**

**Jibu**: Wazuoni Mwenyezi Mungu awarehemu wametofautiana katika kuhirimia ibada ya Hijjah kabla ya kuingia muda wake:

Wapo wanachuoni Walio sema: Hakika mtu kuingia katika ibada ya Hijjah kabla ya muda wake, mtu huyo anakuwa ameingai kwenye ibada hiyo na anaendelea kuwa kwenye ibada, isipokuwa ni karaha kuhirimia ibada ya Hijjah kabla ya kuigia miezi ya Hijjah.

Wapo wanachuoni walio sema: Hakika anae hirimia ibada ya Hijjah kabla ya miezi yake ibada hiyo inakuwa haijafungamana inakuwa ibada ya umrah, kwa maana ibada alio hirimia

Hijjah inabadilika kuwa umrah, kwakuwa umrah kama alivyo sema mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Umeingia kwenye ibada ya Hijjah**)), [1241/ Sahihi Muslim] Mtume rehma na amani ziwe juu yake aliita ibada ya Umrah kuwa ni Hijjah ndogo, kama ilivyo thibiti katika hadithi ya Ibun Omar hazmi hadithi mursala [6559/ Ibun Hibaani /2723/ Adar Al-Qutniy]. Hadithi hiyo watu watu wameikubali na wameipokea.

****

**Swali la 462: Ni ipi mipaka anayopitia mwenye kwenda kufanya ibada ya Hijjah (miikati)?**

**Jibu**: Mipaka imegawanyika sehemu kuu tano:

**1-Sehemu ya kwanza ni:** Dhul-Khulayfah.

**2-Sehemu ya pili ni:** Al-Juhfah.

**3-Sehemu ya tatu ni:** Yalamlam.

**4-Sehemu ya nne ni:** Qarnul Manaazil.

**5-Sehemu ya tano ni:** Dhaatu Irqi.

Kuhusu Dhul-khuyalfa: Ni sehemu amabyo kwasasa inaitwa

Abiyar Ally ni kijiji kilicho katika mji wa madina, kina umbali na mji wa Makkah Kilo meta (450) na ndio mpaka ulio wa mbali kufika Makkah, na mpaka huo wanautumia watu wa madina na watu walio kusudia kwenda Makkah wakanza kupita madina.

Kuhusu Al-Juhfa: Ni kijiji cha zamani kipo katika njia ya watu wa shamu walio kuwa wanakusudia kwenda Makkah kijiji hicho kina umbali wa kufika Makkah Kilo meta (135) Kijiji hicho kimeharibika watu wamekuwa wakihirimia ibada za umrah na Hijjah katika sehemu inaitwa rabiyghi.

Kuhusu Yalamlamu: Nao ni mlima au sehemu ipo njiani walio kuwa wakipita watu wa Yemeni wakienda Makkah, kwasasa kijiji hicho kinaitwa Al-Sudayatu, umbali wa kutoka wenye kijijihicho na kufika Makkah ni kilo meta (90).

Kuhusu Qarnul Manaazil: Ni mlima ulio katika njia wa watu wa najidi walio kuwa wanakwenda Makkah, kwasasa panaitwa Saylil-Kabiyr, ubali wa kutoka hapo mpaka kufiika Makkah ni.

Kuhusu Dhaatu Irqi: Ni sehemu ipo katika njia ya watu wa Iraqi walio kuwa wanakwenda Makkah, umbali wa kutoka hapo mpaka kufika Makkha ni kilo meta ( 90)

Kuhusu sehemu nne, Ambazo ni Dhul-hulayfa, Al-Juhfa, na Yalamlam, na Qarnul-Manaazil, sehemu hizo aliziweka Mtume rehma na amani ziwe juu yake, [1524/ Swahihi Bukhary, /1181/ Swahihi Muslimu]. Kuhusu sehemu ya Dhaat Irqi hakika aliyeweka mtume rehma na amani ziwe juu yake! Kama walivyo pokea hadithi watu wa vitabu vya Sunna katika hadithi ya aisha radhi za mwenyezi Mungu ziwe juu yake, pia imethibiti kwa omra

radhi za mwenyezi Mungu ziwe juu yake kuwa aliweka mpka wa watu wa mji wa kufa ulipo Iraq na watu wa mji wa basra, walivyo kuja watu wa miji hiyo kwa omar wakasema: Ewee kiongozi wa waislamu hakika mtume rehma na amani aliweka kwa watu wa najdi mapaka wao ni Qarn, na sisi kupita hukoo tunapata shidaa kwa kuwacha njia yetu, akasema omar radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake anagaliye sehemu mtakayo kuwa mpo sawasawa na mpaka huo wa Qarni kwa kupitia kwenye njia yenu [1531 / Sahihi Bukhary]. Kwahivyo imethibiti kwa mtume rehma na mani ziwe juu yake! Na jambo lipo wazi, hata kama halikutihibit kwa mtume, limethibiti kwa omar ibun khatwabi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, nae ni mmoja kati ya Makhalifa waongofu ambao tumeamrishwa kuwafuata, jambo ambalo tuna elezea katika hukumu ya Mwenyezi Mungu katika mambo mengi, katika hayo ni kuwa ikithibiti kuwa mtume ndio alio weka mpaka huo, au akawa omar ndio alio weka atakuwa amefata qiyaasi kwakuwa mtu akipita katika mipaka hiyo ni lazima ahirimie katika sehemu za mipaka hiyo (kunuwiya ibada) akaiwa yupo sehemu ilipo sawasawa na mpaka anakuwa sawa na mtu alio sehemu ya mpaka anakuwa sawa na mtu aliye pita katika mpaka, katika matendo ya omar ibun khatwabi kuna faida kubwa katika zama zetu hizi, faida zenyewe kama mtu atakuwa anakwenda Makkah kwa ajili ya Hijjah au umrah kwa usafir wa ndege ni lazima kwa mtu huyo akifika katika sehemu inayo kuwa sawa na mipaka akiwa bado yupo angani anatakiwa kuhirimia akiwa yupo hukohuko angani wala sio halali kuchelewesha kuhirimia ibada hiyo ya Hijjah au umrah mpaka afike Jiddah Kama wanavyo fanya baadhi ya

watu wengi, hakika kuwa sehemu sawasawa na mpaka hakuna utofauti aliye aridhini na aliye angani au baharani, kwahiyo wanatakiwa wahirimie wanao tumia njia ya maji wakiwa kwenye usawa wa mkapa wa yalamlam au mpaka wa rabiygha watahirimia wakifika usawa wa mipaka hiyo miwili.

****

**Swali la 463: Ni ipi hukumu ya mtu aliye vuka mipaka ya Makkah bila kuhirimia?**

**Jibu**: Atakayevuka katika mipaka bila kuhirmia jambo hilo limegawanyika sehemu mbili:

Ima atakuwa anakusudia kuwenda kufanya ibada ya Hijjah au umrah katika hali hiyo ni lazima arudi kwenye mipaka ndio ahirimie ibada anayo itaka ima umrah au Hijjah, kama hakufanya hivyo atakuwa ameacha jambo la waJibu katika mambo ya ibada ya Hijjah, itamlazimu atoe fidia ya kijichijwa katika mji wa Makkah na atawagawiye mafaqiri wa Makkah ,kwa kauli ya wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu.

Kuhusu mtu aliye vuka mipaka nae hakukusudia ibada ya Hijjah au umrah mtu huyo hato lipia fidia yoyote. Hata kama atakuwa amekaa muda mrefu au muda mfupi, kama tunge mlazimisha kuhirimia katika mipaka wakati anapita ingekuwa ni lazima kwa mtu uyo kufanya ibada ya Hijjah au umrah na ingekuwa nia lazima kwakwe kufanya ibada hiyo zaid ya mara

moja, na imethibiti kwa mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa ibada ya Hijjah sio lazima kwa umri wake wote anaoishi mtu isipokuwa mara moja katika umri wake wote [1337/ Sahihi Muslim]. Na mtu kuzidisha zaidi ya mara moja inakuwa ni Sunna, na kauli hii ndio kauli sahihi katika kauli za wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu, mtu akivuka mipaka bila kuhirimia kwa maana mtu uyo akiwa hakukusudia ibada ya Hijjah au umrah mtu huyo hato toa fidia yoyote wala sio lazima kurudi kuhirimia kwenye mipaka.

****

**Swali la 464: Niya ya kuingia katika ibada ya Hijjah au Umrah hivi inatamkwa wakati wa kuleta nyiradi za labayka?**

**Jibu**: Kusema talbiya, ni mtu kusema: labayka umrah, kama mtu atakuwa anakusudia ibada ya Umrah, na atasema labayka, ama niya hairuhusiwi kuitamka, asiseme kwa mfano Mweneyezi Mungu mimi nakusudia ibada ya Hijjah au ibada ya Umrah, kusema hivyo haikuthibiti kwa mtume rehma na mani ziwe juu yake.

****

**Swali la 465: Ni vipi atahirimia mtu anakwenda Makkha kwa kutumia njia ya anga (ndege)?**

**Jibu**: Kuhirimia (kunuwiya) kwa mtu ambae anakwenda Makkah kwa ajili ya ibada kwa usafiri wa ndege, ni lazima akifika usawa wa mpaka ahirimie, kwa misingi hiyo anatakiwa ajiandae kwa kuoga atakapo kuwa anatoka nyumbani kwakwe kisha avae nguo ya ihramu kabla hajafika kwenye mipaka, wakati atakapofika kwenye mipaka atahirimia, kutia niya ya kuingia kwenye ibada wala asicheleweshe kutia niya kwa kuwa ndege inapita sehemu hiyo kwa haraka, kwa muda wa dakika moja ndege inaweza kuwa imekata masafa marefu, na jambo hili watu wengi wanajisahau unawaona watu wengi hawajiandai wanapo tangaza wafanyakazi wa ndege kuwa wamefika kwenye mipaka ndio unaona watu wanakwenda kuvua nguo zao kisha wanavaa ihram na kufanya hivyo ni mapungufu makubwaa kwa wafanyakazi wa ndege kwa vile wanavyo anza kutangaza, bora wange kuwa wana wambia watu wajiandae kabala ya kufika kwenye mipaka kwa muda wa robo saa nk. Na kwa kazi hiyo watashughulishwa sana kwakuwa wakiwambia watu kabla ya muda huo watakuwa wamewapa watu muda wa kubadili mavazi yao na kujiandaa, lakini kwa hali hiyo ni lazima kwa anaetaka kuhirimia awe makini, pindi atakapo tangaza mfanya kazi wa ndege kuwa umebaki muda kama wa robo saa angaliye saa yake mpaka utakapo pita muda wa robo saa au kabla ya kufika robo sana kwa dakika mbili au dakika tatu, atasema labayka na kuitaja ibada anayo ikusudia.

****

**Swali la 466: Ni ipi hukumu ya mtu aliyevuka mipaka ya Makkah bila kuhirimia nae akiwa anakusudia kwenda kufanya ibada ya Umrah?**

**Jibu**: Jambo ambalo ni lazima kwa mtu ambae anataka kufanya ibada ya Hijjah au Umrah na akapita kwenye mipaka asivukee kwenye mipaka mpaka ahirimie akiwa kwenye mipaka kwakuwa Mtume rehma na mani ziwe juu yake amesema: ((**Wahirimie ibada ya Hijjah au umrah watu wa madina katika mpaka wa dhiy al-hulayfa**)) [1525/ Sahihi Bukhary, /1182/ Sahihi Muslim]. Na tamko wahirimie linamaana ya amri, kwa hivyo ni lazima kwa mtu anae taka kufanya ibada ya Hijjah au Umrah atakapo fika kwenye mipaka ahirimie akiwa yupo kwenye mipaka, wala asivuke mipka bila kuhirimia, akivuka kwenye miapaka bila kuhirimia ni lazima arudi kwenye mipaka ahirimie akiwa kwenye mipaka, akirudi akahirimia kwenye mipaka hato toa fidia, lakini akihirimia sehemu alipo na hakurudi kwenye mipaka wamesema wanachuoni. Mwenyezi Mungu awarehemu anatakiwa atoe fidia ya myama achinjwee myama huyo na nyama wagawiwee mafaqiri wa maji wa Makkah.

****

## UJUMBE

### Vipi Mtu Ataswali Akiwa Katika Ndege Na Vipi Atahirimia Ibada Ya Hijjah Au Umrah?

Bismi LLahi Rahmani Rahim, Kila sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe wote, pia na mtakia rehma na amani Mtume wetu Muhammad yeye na familia yake na Maswahaba zake wote kwa ujumla.

**Sehemu ya kwanza:** Vipi mtu ataswali akiwa kwenye ndege?.

1-Ataswali swala ya Sunna akiwa kwenye ndege akiwa amekaa kwenye kiti chake sehemu yoyote ndege itakapo kuwa imeleekea na atakuwa anaashiria kwenye kurukuu na kusujudu na kwenye kusujudu atakuwa anaimana zaidi kuliko kurukuu.

2-Hataswali swala ya faradhi akiwa kwenye ndege isipokuwa mpaka ikiwezekana ndege kuelekea kibla muda wote atakao kuwa anaswali, pia kukawa na uwezekano wa kurukuu na kusujudu na kusimama na kukaa.

3-Kama itakuwa haiwezekani kupatikana hayo basi ataichelewesha swala mpaka atakapo shuka uwanaja wa ndege ataswali aridhini, akihofia kuwa muda wa swala utatoka basi ataichelewesha swala hiyo mpaka muda wa pili ikiwa ni katika swala ambazo inaruhusiwa kuzikusanya kama swala ya Adhuhuri na Alasiri na swala ya Magharibi na Al-Ishaa kama atahofia muda wa pili utaisha akiwa bado hajafika uwanja wa ndege

ataziswali akiwa kwenye ndege kabla ya muda wake haujaisha na atafanya masharti na nguzo na mambo ya wajibu atakayo weza kuyafanya.

Kwamfano: kama ndege itaondoka kabla ya kuzama jua na jua likazama mtu yupo angani, mtu huyo hato swali Magharibi mpaka ashuke uwanja wa ndege akishuka aridhini ndio aswali, kama atahofia muda wa swala ya Magharibi utapita basi ataicheleweshа swala ya Magharibi mpaka muda wa swala ya Al-Ishaa ataziswali pamoja kwa kuzikusanya kwa kuchelewesha, kama atahofia muda wa swala ya Ishaa utaisha nae bado hajafika na muda wa swala ya Al-Ishaa mwisho wake ni nusu ya usiku , basi ataziswali pamoja akiwa kwenye ndege kabla ya muda wake haujaisha.

4-Namna ya kuswali faradhi mtu akiwa kwenye ndege atasimama na anaelekea kibla ataleta takbira atasoma Suratul-fat'ha na dua ya ufunguzi wa swala inayo somwa kabla ya Suratul-fat'ha au atasoma bada ya Suratul-fat'ha Sura nyingine au Aya zingine kwenye Qur`an, kisha atarukuu kisha atainuka kutoka kwenye rukuu na atatulia kidogo akiwa amesimama kisha atasujudu kisha atainuka kutoka kwenye kusujudu na atatulia akiwa amekaa kisha atasujudu mara ya pili kisha atafanya hivyo mpaka swala yake itakapo kamilika, kama haikuwezekana kusujudu atakaa kisha ataashiria kwenye kusujudu akiwa amekaa, hata kama hakufahamu kibla kipo wapi au hakuwambiwa na mtu mwaminifu upande wa kibla ilipo, atajitahidi Mwenyewee kujua kibla kipo upnande gani kisha ataswali sehemu yoyote jitihada zake zitakuwa zimeelekea.

5-Swala ya mtu anae safiri akiwa kwenye ndege inakuwa ni rakaa mbili kama swala itakuwa ni ya rakaa nne, swala yake

inakuwa kama swala ya wasafiri wengine.

**Sehemu ya pili:** Vipi atahirimia ibada ya Hijjah na Umrah mtu aliye kwenda Makkah kwa kutumia ndege?

1-Atakoga nyumbani kwake kisha atabaki amevaa nguo zake za kawaida, au akitaka atavaa nguo ya ihram.

2-Ndege ikikaribia kufika usawa wa mpika atavaa nguo ya ihram, kama atakuwa hakuivaa kabla.

3-Ndege ikifika usawa wa mpaka atanuwia kuingia katika ibada , na ataleta talbiya ya ibada alio ikusudia, ikiwa ni Hijjah au Umrah.

4-kama atahirimia kabla ya kufika kwenye mipka kwa ajili ya kuhofia asije kupita kwenye mipaka kabla ya kunuwia kwa kusahau hakuna ubaya kufanya hivyo.

****

**Swali la 467 : Mtu aliye safiri kutoka katika nchi yake au mji wake akaenda jiddah kisha akataka afanye ibada ya umrah hivi atahirimia akiwa jiddah?**

**Jibu**: Jibu linasehemu mbili :

1-Nimtu kusafili kwenda Jiddah bila kuwa na niya ya kufanya ibada ya umrah, isipokuwa zimemjia fikra za kwenda

kufanya ibada ya umrah akiwa yupo Jiddah mtu huyo atahirimia ibada ya umrah akiwa yupo hapo hapo Jiddah na hakuna ubaya kufanya hivyo kwa ushahidi wa hadithi ya ibun abassi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao alivyo elezea mipaka ya Makkah akasema: ((**Atakae kuwa yupo sehemu ya ndani ya mipaka atahirimia sehemu alipo mpaka watu wa Makkah watahirimia Makkah**)), [1524/ Sahihi Bukhary].

2-Nikuwa mtu amesafili kutoka katika nchi yake au mji wake kwa nia ya kufanya ibada ya umrah mtu huyo ni lazima ahirimie kwenye mipaka ambayo amepita, wala hairuhusiwii ahirimie akiwa yupo Jiddah kwakuwa atakuwa ameisha vuka mipaka, na imethibiti kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa aliweka mipaka akasema: ((Mipaka hiyo niya watu wa miji hiyo na watu walio kujaa kupitiaa njia hiyo wasio kuwa wa kazi wa miji hiyo kwa anae kusudia kufanya ibada ya Hijjah na Umrah)), [1529/ Sahihi Bukhary].

Atakae hirimia akiwa yupo Jiddah na akaenda Makkah, wanasema wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu kuwa anatakiwa kutoa fidiaa ya kichinjwaa atakitoa kichinjwa hicho katika mjii wa Makkah, Atato sadaka kuwapa mafukara na ibada yake ya Umrah itakuwa ni sahihi, kama hakuhirimia tokea yupo Jiddah baada tu ya kufika Jiddah h nae akiwa anadhamira ya kwenda kufanya ibada ya umrah kbla hajafika Jiddah, anatakiwa arudi kwenye mipaka ahirimie akiwa yupo kwenye mipaka na hato toa fidia yoyote.

****

**Swali la 468: Ni ipi hukumu ya mtu aliyehirimia ibada ya Hijjah au Umrah kuoga baada ya kuvaa ihram?**

**Jibu**: Kuoga baada ya kuvaa nguo ya ihram sio vibaya kwa kuwa imethibiti hilo kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake anaruhusiwa kuoga mara moja au mara mbili hakuna ubaya, akini ni lazima kuoga atakapo kuwa amelala akaota anafanya tendo la ndoa hali ya kuwa amehirimia ibada anatakiwa aonge janaba, kuhusu kuoga wakati wa kuhirimia ibada ni Sunna.

****

**Swali la 469: Ni ipi hukumu ya kumuhijia mtu aliyefariki kama atakuwa ni babu yake na mtu huyo ameishahiji Hijjah yake?**

**Jibu**: Hakuna ubaya mtu kumuhijia babu yake ambae amefariki hajahiji, imethibiti katika hadithi za mtume rehma na amani ziwe juu yake.

****

**Swali la 470: Je mtu aliyehirimia ibada ya Hijjah au Umrah anatakiwa kuswali swala maalumu?**

**Jibu**: Mtu aliye hirimia ibada ya Hijjah au Umrah hana swala maalumu, lakini mtu akifika kwenye mipaka na muda wa swala ya faradhi umekaribia ilio bora acheleweshe kuhirimiaa mpaka aswali swala ya faradhi kisha ndio ahirimie, kama atafika kwenye mipaka muda amabao sio wa swala ya faradhi, jambo hilo kama linavyo fahamika ataoga kama mtu anavyo oga mwenye janaba kisha atajipamba na atavaa mavazi yake ya ihram kima itakuwa ni muda wa swala ya dhuhaa akita kuswalii swala hiyo ya dhuhaa ataswali, au akitaka kuswali Sunna ya udhuu kama itakuwa muda huo sio wa swala ya dhuhaa kisha ndio ahirimie baada ya kumaliza kuswali kufanya hivyo ndio bora, hakuna swala maalumu kwa mtu aliye hirimia ibada ya Hijjah au Umrah, hakika haikupokelewa hadithi kwa mtume rehma na amani ziwe juu yake.

****

**Swali la 471: Mtu aliyehirimia ibada ya Umrah katika miezi ya Hijjah kisha akasafiri kutoka Makkah kwenda Madina akahirimia ibada ya Hijjah sehemu inayo itwa Abyaar Ally, je mtu huyo atakuwa amefanya ibada ya tamatui? (Hijjah na Umrah).**

**Jibu**: Kwa kuwa mtu huyo wakati anakwenda Makkah kufanya ibada ya Umrah katika miezi ya Hijjah na amekusudia kuwa atafanya ibada ya Hijjah katika mwaka huo mtu huyo atakuwa amefanya ibada ya tamatui, kwa kuwa kusafiri kwakwe ni kati ya ibada ya Umrah na Hijjah hakubatilishi ibada ya tamatui isipokuwa kama atarejea kwenda katika nchi yake, akaanzisha safari ya kutoka nchini kwake na kwenda kufanya ibada ya Hijjah ibada ya tamatui itakuwa imebatilika, kwakuwa atakuwa amefanya ibada mbili kila ibada itakuwa na safari yake inajitegemea , na mtu aliye kwenda madina baada ya kutekeleza ibada ya Umrah kisha akahirimia ibada ya Hijjah sehemu inayo itwa abyaari alliyi, Ni lazima mtu huyo achinje myama kwa ajili ya ibada ya tamatui, kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Basi Mwenye kujisitarehesha kwa kufanya Umrah kisha ndio ahiji basi achinje mnyama atakae muiya mwepesi**] [Suratul Baqara: 196].

****

**Swali la 472: Mtu aliyehirimia ibada ya Umrah katika mwezi wa shawaal (mfunguo mosi) akaikamilisha ibada yake, Na mtu huyo hakukusudia kufanya ibada ya Hijjah, kisha mambo ya kawa mepesi kwa kufanya ibada ya Hijjah, je mtu huyo akifanya ibada ya Hijjah atakuwa amefanya tamatui?**

**Jibu**: Mtu huyo hakufanya ibada ya tamatui (Hijjah na Umrah), wala sio lazima kwake kuchinja.

****

**Swali la 473: Ni zipi nyiradi za talbiya ambazo zimesihi kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake? Na ni muda gani mtu ataacha kuleta talbiya katika ibada ya Hijjah na ibada ya Umrah?**

**Jibu**: Nyiradi za talbiya zilizo thibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni kusema: ((**Labayka Allahumma labayka, labayka laa shariyka lakaa labayka, inal-hamda waniimata laka wal-Mulku laa shariika laka**)), [476/2 Imamu Ahmadi, /2752/ Al-Nasaai/2920/ Ibun Majah]. Na mtu ataacha kuleta talbya kwa anae fanya ibada ya Umrah atakapo anza kufanya twawafu (kuzunguka Al-Kaaba) Kwa anae fanya ibada ya Hijjah ataacha kuleta talbiya atakapo anza kupiga mawe katika kikuta cha Jamaraat siku ya sikukuu ya iddi, kwa ushahidi wa hadithi aliyo ipokea Tirmidhiy radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake katika hadithi ya ibun abasi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao amepokea hadithi kuwa: ((**Alikuwa anaacha kulete talbiya katika ibada ya umrah anapo nyoosha mkono kwenye jiwe**)), [1817/ Abuu Daudi, /1919/ Tirmidhiy], hadithi hii ameisahihisha Tirmidhiy lakni kwenye hadithi hii yupo Muhammad Ibun Abdul Rahman Ibun Abii Layliy wanachuoni wengi wa hadhithii wamesema kuwa ni mdhaifu katika fani ya hadith,

imepokewa hadithi kutoka kwa ibun abasi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yo kuwa Osama radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake alikuwa amepakizwa na Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwenye kipandwa cha Mtume rehma na amani ziwe juu yake kutoka Arafa kwenda Muzdalifa kisha Mtume akampakiza Al fadhili radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kutoka Muzdalifa kuelekea Mina wote hao wawili wamesema: ((**Mtume aliyendelea kuleta talbya mpaka alivyo piga mawe kwenye vikuta**)), hadithii hii ipo katika Sahihi Bukhury na Sahihi Muslim [1670/1669 Sahihi Bukhary, / 1281/1280 Sahihi Muslimu]. Na kwa upokezi wa Imamu Maaliki radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, ataacha kuelete talbya mtu anae fanya ibada ya Umrah atakapo fika maeneo matakatifu wa Makkah, pia kuna kauli kuwa ataacha kuleta talbya atakapo fika jirani na Msikiti mtakatifu wa Makkha, Maana ya kusema: ((**Labayka**)): Nimeitikia wito wako.

****

**Swali la 474: Je inaruhusiwa kwa mtu aliyehirimia ibada ya Hijjah au Umrah kuchana nywele?**

**Jibu**: Mtu aliye hirimia ibada ya Hijjah au Umrah haifai kuchana Nywele, inatakiwa kwa mtu aliye hirimia ibada hizo awe na nywele timu timu zenye vumbi, lakini sio vibaya kuziosha nywele zake, kuhusu kuchana nywele hakika makusudio yake ni kudondosha baadhi ya Nywele, lakini nywele za mtu aliye hir-

imia ibada ya Hijjah au Umrah zikikatika bila yeye kukusudia ima kwa kujikuna au kusugua nk. Hakuna ubaya kama zita katika kwa njia hiyo kwakuwa hakukusudiaa kuziondoa, Na fahamu kuwa mambo yote ambayo ni haramu kuyafanya mtu aliye hirimia ibada ya Hijjah au Umrah akiyafanya bila kukusudia au kwa kusahau au kwa bahati mbaya hakuna ubaya, kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu: [**wala sio lawama juu yenu kwa mliyo kosea lakini ipo lawama katika yale ziliyo fanya nyoyo zenu kwa makusudi na Mwemyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu**], [Suratul Ahzab: 5]. Pia amesema Mwenyezi Mungu: [**Mola wetu! usituchukulie tukisahau au tukikosea**], [Suratul Baqara: 286].

Kuhusu uwindaji wa wanyama kwa mtu aliye hirimia ibada ya Hijjah ni katika mambo ambayo ni haramu kufanya mtu aliye katika ibada hiyo, Amesema Mwenyezi Mungu: [**Enyi mlio amini msiue wanyama wa kuwinda nanyi mmehirimia katika Hijjah na miongoni mwenu atakae wauwa makusudi basi malipo yake yatakuwa kwa kuchinja kilicho sawa na alicho kiuwa katika mifugo kama wanavyo hukumu wa adilifu wawili miongoni mwenu ].** [Suratul Maaida: 95], na sehemu ya ushahidi muhimu kwenye kauli ya Mwenyezi Mungu (makusudi) inatufahamisha kuwa atakae uwa mnyama bila kukusudia hatakiwi kulipa, na hiki ndiyo kizuizi kinacho endana na hukumu, kwa kuwa anaye fanya jambo kwa makusudi ndio anae takiwa kulipa ama anaye fanya kwa bahati mbaya hatakiwi kulipa kwa ushahidi unao fahamika katika dini hii ya kiislamu dini amabyo inasamehe mambo na dini yenye wepesi, kwa misingi hiyo tunasema: Mambo yote amabyo ni haramu

mtu kuyafanya akiwa amehirimiaa ibada ya Hijjah akiyafanya kwa kusahau au kwa kuto kujua mtu huyo hakuna hukumu inayo mtaka afanye kitu, kwa maana hato kuwa na ulazima wa kulipa fidia wala ibada yake haito haribika, Mambo ambayo yanaharibu ibada ya Hijjah ni kutenda tendo la ndoa tendo hilo linaharibu ibada kwa ushahidi wa kisheriya ambao tumeuelezea.

****

**Swali la 475: Mtu aliyehirimia ibada ya Hijjah au Umrah akapunguza sehemu ya nywele zake bila kujua na akamaliza kufanya ibada hiyo, ni jambo gani anatakiwa kufanya?**

**Jibu**: Huyo aliyepunguza nywele bila kufahamu kuwa ni haramu kupunguza nywele kwa aliye hirimia ni haramu, kisha akamaliza kufanya ibada hiyo, hato takiwa kulipia fidia yoyote baada ya kumaliza ibada hiyo, kwasababu amepunguza nywele bila kujua, kinacho takiwa akamilishe kwenye kupunguza nywele zake.

Namimi kupitia nafasi hii napenda kuwapa nasaha ndugu zangu, kuwa atakae taka kufanya ibada asiifanye mpaka ajifunze sheriya zake na mipaka yake ambayo Mwenyezi Mungu ameiweka, ili mtu huyo asije kufanya jambo ambalo litaitia dosari ibada yake, kwa kauli ya Mwenyezi Mungu mtukufu kumuawambia Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake:

[**Sema: hii ndiyo njia yangu ninawalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa elimu mimi na waliyo nifuata na ametakasika Mwenyezi Mungu wala mimi si katika washirikina**.] [Surat Yusuf: 108]. Na kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Sema: Je watakuwa sawa wale wanao jua na wale wasio jua? hakika wao kumbuka ni watu wenye akili**], [Surat Zumar: 9]. Mtu kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa elimu akiwa anafahamu mipaka ya Mwenyezi Mungu katika ibada anayo ifanya, nibora sana kuliko anae fanya ibada akiwa ni mjinga bali anafanya ibada kwa kuwafata watu wanavyo fanya, wakifanya jambo na yeye anafanya wakiacha kufanya na yeye hafanyi.

****

**Swali la 476: Mtu akingia Makkah bila kuhirimia ibada kwa sababu ya kuogopa katazo la viongozi, baada ya kufika Makkah ndipo akahirimia ibada ya Hijjah, je Hijjah yake ni sahihi? Tupeni maelekezo Mwenyezi Mungu atawalipa kheri nyinyi na waislamu wote.**

**Jibu**: Kuhusu ibada ya Hijjah aliyo ifanya ni sahihi, lakini kitendo cheke ni haramu kwa sehemu mbili:

**Sehemu ya kwanza:** Ni kuvuka mipaka ya Mweneyezi Mungu kwa kuwacha kuhirimia ibada ya Hijjah akiwa yupo kwenye mipaka.

**Sehemu ya pili:** Na kupinga amri ya kiongozi wa dini, viongozi amabao tumeamrishwa tuwatii katika mambo ambayo sio ya kumuasi Mwenyezi Mungu. Kwa misingi hiyo anatakiwa atubu sana kwa Mwenyezi Mungu na amuombe sana msamaha Mwenyezi Mungu kwa aliyo yafanya, pia anatakiwa kutoa fidia atachinja mnyama akiwa yupo Makkah na nyama awagawie mafaqiri wa Makkah, kwa sababu ya kuwacha kuhirimia ibada ya Hijjah akiwa kwenye mipaka, Kwa ushahidi wa kauli za wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu wamesema: ni lazima kutoa fidia kwa mtu aliye acha kufanya jambo la lazima katika ibada ya Hijjah au Umrah mtu huyo ni lazima atoe fidia ya kichinjwa.

****

**Swali la 477: Mtu aliyehirimia ibada ya Tamatui (Hijjah na Umrah) kisha akarudi nchini kwake, akapanga safari nyinginee kwa ajili ya Hijjah akitokea nchini kwakwe, je mtu huyo atakuwa amefanya ibada ya ifradi (Hijjah bila umrah)?**

**Jibu**: Ndio, aliyehirimia ibada ya Tamatui akarudi nchini kwake au mji wake kisha akanza safari nyingine kwa ajili ya Hijjah mtu huyo atakuwa amefanya ibada ya ifradi (Hijjah bila Umrah) kwa kuwa itakuwa imekatika ibada ya Umrah na Hijjah kwakuwa amerudi kwenye familia yake, na kuwanza safari nyingine, maana yake ameanza safari mpya kwa ajili ya Hij-

jah kwa hivyo Hijjah inakuwa Hijjah inajitegemea, kwahivyo sio lazima kutoa fidia ya kichinjwa kwa ajili ya ibada ya tamatui, Lakini kama atarudi katika nchi yake au mji wake kwa ajili ya kukwepa kuchinja, ulazima wa kuchinja bado upo palepale kwakuwa amefanya hila ya kuodosha wajibu na haujaondoka, (tahalluli) kama ilivyo kuwa mtu akijiondoa kwenye ibada (tahaluli) sio kuwa ulazima wa kulipia fidia utakuwa umeondoka kwa kufanya kwakwe tahaluli.

****

**Swali la 478: Ni ipi hukumu ya mtu kujifunika kwa mwamvuli akiwa amehirimia ibada ya Hijjah au Umrah au mtu kujifunga mkanda kiunoni pamoja na kuwa anafahamu kuwa vyote hivyo vimeshonwa?**

**Jibu**: Kubeba mwamvuli kichwani kwa ajili ya kujifunika na kuziwia joto hakuna ubaya na sheriya haizuii kufanya hivyo, pia haliingii kwenye katazo la mtume rehma na amani ziwe juu yake! Kuwa alikataza kufunika kichwa kwa mwanaume, [1543 Sahihi Bukhary /1177/ Sahihi Muslim], kwakuwa kutumia mwamvuli sio kufunika kichwa isipokuwa ni kujikinga na joto na jua, Pia imethibi hadithi katika swahihu bukhary na swahihu muslimu kuwa mtume rehma na amani ziwe juu yake alikuwa na osama ibun zaaydi na bilali radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao kuwa mmoja wao alikuwa ameshika kamba ya mnyama wa mtume akimkokota na mwengine ameinua guo

akimkinga mtume asipatwe na joto mpaka mtume alivyo fika kwenye kikuta akapiga mawe, pia kwenye upokezi wa hadithi nyingine, kuwa mmoja wao ameinua nguo juu ya kichwa cha Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa ajili ya jua, [1298/ Sahihi Muslim]. Huu ni ushahidi kuwa mtume rehma na amani ziwe juu yake alijikinga kwa nguo nae akiwa amehirimia ibada ya Hijjah na kabla ya kujitoa kwenye ibada hiyo (tahaluli ).

Kuhusu mtu kufunga mkanda juu ya kikoi hakuna ubaya kufunga mkanda, na kuhusu kauli ya muulizaji kuwa: ((**Mkanda unamashono**)) Kauli hii imejengewa kwenye ufahamu wa makosa kwa baadhi ya watu, baadhi ya watu wanadhani kuwa maana ya kauli ya wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu: ((**Ni haramu kwa mtu aliye hirimia ibada ya Hijjah kuvaa nguo yenye mshono au iliyoshonwa**)), wamedhani baadhi ya watu kuwa nikuvaa chenye mashono, na sio hivyo, makusudio ya wanachuoni Mweneyzi Mungu awarehemu kuvaa chenye mashono ni kilicho tenegenezwa kwa mashono na kikawa na ukubwa wa kuenea kwenye kiungo, na kukivaa katika hali amabyo imezoeweleka kama kanzu au suruali na flana na vinginevyo, na sio kuwa wanachuoni wamekusudia chenye mashono, kwa hivyo kama mtu atakuwa mehirimia akiwa amevaa kikoi chenye viraka au kilemba chenye viraka hakuna ubaya kuvaa hivyo kama atakuwa amezishonea pamoja.

****

**Swali la 479: Mtu ambaye amepata matatizo ya kupooza hawezi kuvaa nguo ya ihrami atafanyaje?**

**Jibu**: Mtu Akiwa hawezi kuvaa nguo ya ihram mtu huyo atavaa nguo yoyote ambayo ataweza kuvaa katika mavazi mengine yasiyo kuwa nguo hiyo ya ihram, na wanachuoni Mwenyezi Mungu awarehemu wamesema kuwa ima mtu huyo atachinja akiwa Makkah mbuzi kisha nyama atawagawia mafaqiri wa Makkah au awalishe chakula masikini sita kila masikini nusu ya pishi (kibaba) au atafunga siku tatu, Hayo ndio waliyo sema Wanachuoni kwa kukisia kwa mtu aliye nyoa nywele za kichwa, Kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu: [**Atakaye kuwa ni mgonjwa au anavya kumuudhi kichwani mwake basi atoe fidia kwa kufunga au kwa kutoa sadaka au kuchinja wanyama**], [Suratul Baqara: 196], yani - akiwa na matatizo ambayo hawezi pitisha kiwembe kichwani kwake. Na mtume rehma na amani ziwe juu yake ameweka ufafanuzi wa kufunga na sadaka kama tulivyo eleza.

****

**Swali la 480: Ni ipi hukumu ya mtu aliyefanya tendo la ndoa nae akiwa amehirimia ibada ya Hijjah bila ya kujuaa kuwa ni haramu?**

**Jibu**: Jambo ambalo linafahamika kuwa kufanya tendo la ndoa kwa aliye hirimia ibada ya Hijjah ni haramu, na pia ni jambo kubwa la haramu katika mambo ambayo hatakiwi mtu

aliye hirimia ibada ya Hijjah kuyafanya, amesema Mwenyezi Mungu: [**Hijjah ni Miezi Maalumu na anaye kusudia kufanya Hijjah katika miezi hiyo basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu na asibishane katika Hijjah**], [Suratul Baqara: 197]. Na makusudio ya kusema vitendo vichafu ni tendo la ndoa ndiyo lililo kusudiwa na mambo anayo yafanya mtu kabala ya tendo la ndoa, Kufanya tendo la ndoa ni katika mambo makubwa ambayo ni haramu kuyafanya akiwa amehirimia ibada ya Hijjah, Mtu akifanya tendo la ndoa katika msimu wa Hijjah ima atakuwa ame fanya tendo hilo kabla ya tahaluli ya kwanza (kuhalalika kufanya yalokua yamekatazwa), au baada ya tahaluli ya Kwanza kama atakuwa amefanya tendo la ndoa kabla ya tahaluli ya kwanza, mtu huyo aliye fanya tendo hilo yatamtokea mambo ya fuatayo kuhusiana na ibada yake:

**Jambo la kwanza:** Ibada yake itaharibika kwa hali ambayo haito kuwa ni ibada ya Sunna wala ibada ya faradhi.

**jambo la pili:** Atapata madhambi.

**Jambo la tatu:** Itaendelea kuwa ni lazima kuifanya ibada hiyo, maana yake pamoja kuwa ibada hiyo imeharibika ataendela na ibada na ataikamilisha na ibada hiyo itakuwa imeharibika lakini itakuwa kama ibada sahihi kwa hukumu zake kwa ujumla.

**Jambo la nne:** Ina mlazimu kuja kulipa ibada hiyo mwaka ujao, Hata kama itakuwa ibada ya Hijjah ni Hijjah ya faradhi (lazima) Au anafanya ibada ya Hijjah ya Sunna, kama itakuwa ni Hijjah ya faradhi kuhusu kulipa ibada hiyo jambo lipo wazi, Kwakuwa Hijjah ambayo amefanya tendo la ndoa hakuwa Mwenye kuhiji (haikusihi) kama akiwa amefanya Hijjah ya Sunna hakika Hijjah ya Sunna ni lazima aendelee na ibada yake ya

Hijjah, Kwa kauli ya Mwenyezi Mungu: [ **Na timizeni Hijjah na Umrah kwa ajili ya Mwenyezi Mungu**] [Suratul Baqar: 196]. Mwenyezi Mungu ameiita Hijjah kuwa ukamilifu wa Hijjah ni ukamilifu wake, amesema Mwenyezi Mungu: [**Hijjah ni miezi malumu na anaekusudia kufanya Hijjah katika miezi hiyo**], [Suratul Baqara: 197]. Kwa misingi hiyo tumesema: Ni lazima kwa mtu huyo ailipe ibada hiyo ya Hijjah iliyo haribika hata kama ibada hiyo ya Hijjah ikiwa ni ya faradhi au Hijjah ya Sunna.

**Jambo la tano:** Inatikiwa kwa mtu huyo achinje mnyama kwa ajili ya kulipia kafara ya kitendo chake cha kufanya tendo la ndoa akiwa kwenye ibada ya Hijjah, na nyama awagawia mafaqiri wa mji wa Makkah, Hata kama atachinja kondoo saba hakuna ubaya, hii ndio hukumu ya mtu aliye fanya tendo la ndoa kabla ya tahaluli ya kwanza (kujitoa kwenye ibada).

Kama atakuwa amefanya tendo la ndoa baada ya tahaluli ya kwanza (kujitoa kwenye ibada) mtu huyo atapata madhambi tu na Ihiram yake (niya yake) itakuwa imeharibika, na atatakiwa kuchinja mbuzi na atawagawia mafaqiri wa Makkah au awalishe chakula masikini sita kila masikini nusu pishi (kibaba) cha ngano au chakula kingine, au afunge siku tatu, Atachagua kufanya jambo moja katika mambo hayo matatu, yani - ima Achinje au alishe masikini au Afunge. Na anatakiwa ahirimie tena aende kwenye mpaka wa karibu ahirimie ibada kisha atufu twawafu ya ifadhwa (nguzo) Akiwa amehirimia, hivyo ndivyo walivyosema Wanachuoni Mwenyezi Mungu Awarehemu.

**Mtu akiuliza:** Ni muda gani mtu anakuwa kwenye tahaluli ya kwanza?

**Tunamjibu:** Tahaluli ya kwanza inakuwa baada ya kupiga mawe kwenye vikuta siku ya sikukuu, na kunyoa au kupunguza, mtu akitupa mawe kwenye vikuta siku ya sikukuu akanyoa au akapunguza anakuwa amefanya tahaluli ya kwanza (kujitoa kwenye ibada) Mtu huyo anaruhusiwa kufanya kila jambo ambalo lilikuwa ni haramu kufanya kwa mtu aliye hirimnia ibada ya Hijjah Isipokuwa kufanya tendo la ndoa, tendo hilo litaendelea kuwa haramu kwake, amesema Aisha radhi za Mweneyzi Mungu ziwe juu yake: ((**Nilikuwa nampamba mtume rehma na amani ziwe juu yake! Kwa ajili ya kuhirimia ibada kabla ya mtume kuhirimia Na alivyo kuwa amejitoa kwenye ibada kabla ya kutufu kwenye nyumba ya Mwenyezi Mungu**)), [1539/ Sahihi Bukhary, /1189 Sahihi Muslim]. Na hadithii hii inatufahamisha kuwa tahaluli inafatiwa na twawafu (kuzunguka Al-Kaaba) na inatufahamisha kuwa kunyoa inakuwa kabla ya kutahaluli, kama tulivyo sema hapo nyuma, Kuwa tahaluli ya kwanza inakuwa baada ya kupiga mawee kwenye vikuta siku ya iddi pamoja na kunyoa au kupunguza nywele, kufanya tendo la ndoa ambalo tumeeleza hapo nyuma inatakiwa mambo ma tano ambayo tume yaeleza hapo nyuma, na tendo la ndoa ambalo linakuwa baada ya tahaluli, yanapatika mambo ambayo tume yaeleza kuwa atapata madhambi na kuhirimia kwakwe ibada kutakuwa kumeharibika, pia ni lazima atoe fidia ya kichinja au kuwalisha chakula au kufunga swaumu anaruhusiwa kufungia Makkah au sehemu nyingine pia anaruhusiwa kufunga siku hizo kwa kuzifatanisha au kuziachanisha.

Kama mtu atakuwa ni mjinga, Kwa maana hafahamu kuwa jambo hilo ni haramu, Mtu huyo hatakiwi kufanya chochote hata kama atakuwa amefanya kabla ya tahaluli ya kwanza au baada ya tahaluli, kwakuwa Mwenyezi Mungu Amesema: [**Mola wetu usituchukulie tukisahau au tukikosea**] [Suratul Baqara]. Hakika amesema Mwenyezi Mungu ((umefanya)) Amesema Mwenyezi Mungu: [**wala si lawama juu yenu kwa mlivyo kosea, lakini ipo lawama katika yale zilizo fanya nyoyo zenu kwa makusudi na mwenyezi Mungu ni mwenye kusamehe na mwenye huruma**], [Suratul Ahzaab: 5].

**Mtu akisema:** Kama mtu atakuwa anafahamu kuwa kufanya tendo la ndoa ni haramu kwa mtu aliye hirimia ibada ya Hijjah, Lakini hakudhani kuwa kuwa akifanya tendo la ndoa hukumu zake ndio hizo, hivi mtu huyo atakuwa kwenye udhuru kuwa hakufahamu?

**Jibu:** Hakika huo sio udhuru kwakuwa udhuru ni mtu kuwa hafahamu hukumu ya jambo hilo ni haramu, ama kuwa hafahamu kuwa akifanya tendo hilo hakufahamu kuwa hukumu yake ndio hiyo huo sio udhuru, Kwa hivyo kama mtu aliye katika ndoa anafahamu kuwa zinaa ni haramu na mtu huyo amebelehe na anaakili timamu mtu huyo anakuwa amekamilisha masharti ya kuwa amehifadhika mtu huyo akizini anatakiwa kupigwa mawe, lau akisema: Mimi sikufahamu kuwa adhabu yake ni kupigwa mawe kama ningefahamu kuwa adhabu yake ni kupigwa mawe nisinge fanya, tunasema: Huo sio udhuru ni lazima apigwe mawe hata kama hafahamu adhabu ya zinaa ndio hiyo, Kwa misingi hiyo alikuja mwanaume moja kwa mtume rehma na amani ziwe juu yake mwanaume ambae amefanya tendo

la ndoa na mke wake mchana wa Ramdhan akimuomba mtume fatuwa (maelekezo) kuwa mambo gani ni lazima kwakwe afanye, mtume rehma na amani ziwe juu yake alimwambi ni lazima utoe kafara pamoja na kuwa alivyo tenda tendo la ndoa alikuwa hafahamu mambo ambayo yana mlazimu, imetufahamisha kuwa mtu akifanya ujeuli wa kufanya maovu na akavunja mipaka ya Mwenyezi Mungu mtu huyo anapata athari za maasi hayo hata kama hakuwa anafahamu athari za maasi hayo wakati alipo kuwa anafanya maasi.

****

**Swali la 481: Mwanamke aliyehirimia ibada ya Hijjah atajisitri vipi? Je ni sharti kufunika na kufunua stara amabyo ipo usoni kwake?**

**Jibu**: Mwanamke aliyehirimia ibada ya Hijjah akipita sehemu walipo wanaume au wanaume wakipata sehemu walipo wanawake na wanaume, Ni lazima kwa mwanamke huyo afunike uso wake kama walivyo kuwa wakifunika nyuso wake za maswahaba rehma na amani ziwe juu yao kwahali hiyo hakuna fidia kwa mwanamke huyo kwa kuto kufunika uso wake kwakuwa ameamrishwa kufunika, jambo hilo haliwi ni haramu.

Wala sio sharti ashike kitu alicho funika uso wake, lakini kama atashika uso wake au alicho funika kwenye uso wake hakuna ubaya, ni lazima kwa mwanamke afunike uso wake kwa muda ambao atakuwa yupo sehemu waliyopo wanaume kama ataingia kwenye hema au akawa yupo kwake atafunua uso wake kwakuwa jambo ambalo lianatakiwa kwa mwanamke kwenye Hijjah afunue uso wake.

****

**Swali la 482 : Mwanamke ambaye yupo katika ibada ya Hijjah akaingia katika hedhi kabla ya kutufu (kuzunguka Al-kaaba) kwa ajli ya kuaga ni ipi hukumu yake?**

**Jibu**: Hukumu ya jambo hilo ni kwamba Mwanamke akitufu twawafu ya ifadhwa (ya nguzo) kisha akaingia kwenye hedhi baada ya kukamilisha ibada ya Hijjah na haikubaki kwake isipokuwa twawafu ya kuaga basi mwanamke huyo amesemehewa twawafu hiyo kwa sababu hiyo ya kutokwa na hedhi , Kwa ushahidi wa hadithi ya Ibun Abasi radhi za Mweneyzi Mungu ziwe juu yao, amesema: ((**Wame amrishwa watu waliyo katika ibada ya Hijjah jambo lao la mwisho iwe ni kutufu, isipokuwa wamefanyiwa wepesi wanawake waliyo kwenye hedh**i)), [1756 / Sahihi Bukhary, /1328/ Sahihi Muslim]. Na alivyo ambiwa mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa Swafiya bint Huyayyi amepata hedhi na alikuwa swafiya ameisha tufu twawafu

ya ifadhwa (nguzo) Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake akasema mtume rehama na amani ziwe juu yake: ((**Anzisheni msafara**)) [1757/ Sahihi Bukhary, /1211/ Sahihi Muslim]. Na Swafiya hakufanya twawaafu ya kuaga .

Kuhusu twawafu ya ifadhwa (yanguzo) hiyo haruhusiwi mtu mwenye hedhi kuiacha mwanamke huyo ataendela kubaki Makkahh mpaka atakapo twaharika na atufu twawafu ya ifadhwa (nguzo) au mwanamke huyo asafiri kwenda nchini kwake au katika mji wake akiwa amehirimia ibada hiyo akitwaharika atarudu Makkah kwa ajili ya kutufu twawafu ya ifadhwa , pia katika hali hiyo ni vizuri akiwa anarudi kufanya twawafu ya ifadhwa anze kufanya ibada ya umrah kwanza kisha atufu twawafu ya umrah aende swafa na maruwa kisha anyoe au apunguze, kisha ndio atufu twawafu ya ifadhwa aliyo iyacha, kama mwanamke huyo hato kuwa na uwezo wa kurudi basi atafanya kwa hali yoyote kuweka sehemu inayo toka hedhi kitu ambacho kinazuia hedhi isitoke na asichafue msikiti kwa hedhi hiyo kisha atafanya twawafu ya ifadhwa kwa dharura, na hii ndio kauli ilio na nguvu.

****

**Swali la 483: Mwanamke Amehirimia ibada akiwa na mume wake hali ya kuwa mwanamke huyo yupo katika hedhi, na alivyo twaharika akafanya ibada ya Umrah bila ya kuwa na mahram wake, kisha akaona damu bada ya kumaliza ibada ya Umrah ni ipi hukumu yake? Tunaomba majibu Mwenyezi Mungu awalipe kheri.**

**Jibu**: Tunasema: Hakika huyu mwanamke kwa inavyo onekana alikaa Makkah akiwa na maharam wake, pia alikuwa amehirimia ibada akiwa kwenye mipaka hali ya kuwa yupo kwenye hedhi, na kuhirimia kwake ibada akiwa kwenye hali ya hedhi ni sahihi, kwakuwa mtume rehma na amani ziwe juu yake wakati alipo ulizwa na asmaa bint umaysi radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao, naye akiwa katipa mpaka wa Dhul-Hulayfa alisema mwanamke huyo: Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu mimi nimengia kwenye hedhi, Akasema mtume wa Mwenyezi Mungu: ((O**ga na ujifunge na guo kisha uhirimie ibada**)) [ 1218/ Swahihi Muslimu].

Lakini damu kurejea rejea kunaleta tatizo kuwa twahara aliyo iyona mara ya kwanza ni twahara kweli? Tunasema: kama atakuwa ameona twahara ya yaqini (uhakika) ibada ya Umrah ya mwanamke huyo itakuwa ni sahihi kama atakuwa na mashaka basi arudie kufanya umrah mara nyingine, lakini siyo kurudia ibada yaUmrah uende kwenye mipaka na kisha uhirimie mara ya pili, bali ninacho kikusudia arudie kutufu na kwenda saayi na kupunguza nywele.

****

**Swali la 484: Mwanamke ambaye yupo kwenye ibada ya Hijjah akaingia kwenye hedhi kabla ya kutufu twawafu ya ifadhwa (nguzo), na anaishi nje ya Saudi Arabia ukawadia muda wa kusafiri na hawezi kuchelewesha safari, na akisafiri hana uwezo wa kurudi Saudi Arabia kwa mara nyingine atafanyaje? Tunaomba maJibu Mwenyezi Mungu awalipe kheri .**

**Jibu**: Kama hali hiyo itakuwa kama ilivyoelezwa katika swali: Kuwa mwanamke aliye katika ibada ya Hijjah hajatufu twawafu ya ifadhwa (nguzo) akaingia kwenye hedhi na kukawa na dharura ya kuwa yeye hawezi kubaki Makkah au hana uwezo wa kurudi tena Makkah lau kama angesafiri kabla ya kutufu, katika hali hii inaruhusiwa kwa mwanamke huyo afanye moja kati ya mambo mawili:

1-Ima atumie sindao inayo kata damu ya hedhi isitoke kisha atufu kama kutakuwa hakuna madhara ya kiafya akitumia sindano hiyo.

2-Au ajifunge vizur sehemu zake za siri kiasi ambacho atazuiya damu isichilizike na kudondoka msikitini na atatufu kwa dharura, nahii ndio kauli ilio na nguvu ambayo ameielezea Sheykhul Isalaam bin Taymiyah Mwenyezi Mungu amrehemu. [245/ Majmuul-Fatawa].

1-Ima ataendelea kuwa kwenye ihram yake, wala haitakuwa halali kwa mume wake kukutana nae kimwili, pia haitaruhusiwa kufungishwa ndoa kama atakuwa mwanamke ambae hajaolewa.

2- Au atachukuwa hukumu ya mtu aliyepatwa na matatizo jiani kama kuzuiliwa, atachinja kwa ajili ya fidia na baada ya kuchinja atakuwa ametoka kwenye ihram yake, akifanya hivyo hato zingatiwa kuwa amefanya ibada ya Hijjah.

Na mambo yote mawili ni magumu, jambo la kwanza ni kuendelea kuwa yupo kwenye ihram na jambo la pili ni kama Hijjah inakuwa imempita mwanamke huyo, kwahivyo kauli yenye nguvu ni kauli ya Sheykhul Isalaam bin Taymiyah Mwenyezi Mungu amrehemu anasema ikitokea mfano wa jambo hilo inakuwa ni dharura Na amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: [**Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika dini**], [Suratul Hajj: 78]. Pia amesema Mwenyezi Mungu: [**Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo** mazito], [Suratul Baqara: 185 ].

Kama mwanamke huyo itawezekana asafiri kisha arudi Makkah baada ya kutwaharika hakuna ubaya kusafiri atakapo twaharika atarudi na atatufu twawafu ya ifadhwa (ya nguzo) twawafu ya Hijjah, na muda wote huo mwanamke huyo hato ruhusiwa kufanya tendo la ndoa na mume wake, kwasababu mwanamke huyo hajafanya tahaluli ya pili (kujitoa kwenye ibada).

****

**Swali la 485: Mwanamke aliyehirimia ibada ya Umrah kisha akaingia katika hedhi akaondoka Makkah bila kutekeleza ibada ya Umrah anatakiwa kufanya jambo gani?**

**Jibu**: Mwanamke akihirimia ibada ya Umrah baada ya kuhirimia akatokwa na damu ya hedhi hakika kuhirimia kwakwe ibada hiyo hakujaharibika ataendelea kuwa katika ihramu yake, na mwanamke huyu aliyehirimia ibada ya Umrah na akaondoka Makkah na hakutufu na hakufanya saay huyo bado yupo kwenye ibada yake ya Umrah ni lazima arudi Makkah akatufu na kufanya saay pamoja na kupunguza nywele hapo ndio atakuwa amejitoa kwenye ihram yake, pia inatakiwa kwa mwanamke huyo ajiepushe kufanya mambo yote ambayo ni haramu kuyafanya mtu aliye hirimia kujipamba na kukata nywele au kukata kucha na asifanye tendo la ndoa na mume wake kama atakuwa ameolewa mpaka akaikamlishe ibada yake ya Umrah, Isipokuwa kama mwanamke huyo alihofia wakati anahirimia ibada yake kuwa anaweza kuingia kwenye hedhi, akaweka sharti kuwa popote litakapo mtokea tatizo hilo ndiyo atakua amefaya tahaluli, hatofanya jambo lolote kama atakuwa amejitoa kwenye tahaluli.

****

**Swali la 486: Je inaruhusiwa kwa mwanamke aliyehirimia ibada ya Hijjah au Umrah kubadilisha nguo aliyo ivaa wakati anahirimia ibada hiyo? Je nguo aliyoivaa mtu aliyehirimia inamuhusu yeye peke yake?**

**Jibu**: Inaruhusiwa kwa mwanamke aliye hirimia kubadilisha nguo nyingine ikiwa ni kwa haja au bila haja sheriya inamruhusu, lakini kwa sharti nguo atakayo badili isiwe nguo ambayo itakuwa haimsitiri vizuri mwili wake na isiwe nguo inayo washawishi wanaume, kwa misingi hiyo kama atakuwa anataka kubadili nguo hakuna shida kwa mwanamke huyo kubadilisha.

Mtu aliye hirimia ibada hana nguo inayo muhusu, kwa upande wa mwanamke anaruhusiwa kuvaa nguo anayo itaka isipokuwa haruhusiwi kuvaa niqabu wala asivae soksi za mikono, maana ya niqabu ni kitamba kinacho wekwa juu ya uso kinakuwa na matundu mawili sehemu ya macho, na kuhusu soksi maana yake ni soksi wanazo zivaa wanawake kwenye mikono na waziita soksi fupi za mikono.

Kuhusu mwanaume yeye ana mavazi yake maalumu akiwa amehirimia ibada ya Umrah au ya Hijjah nguo niyo ni kikoi na nguo juu anayo jifunika nayo na hafuniki kickwa, haruhusiwi kuvaa kanzu wala suruali wala kilemba cha kichwa wala asivae kanzu yenye koffia kwa nyuma wala nguo nyepesi.

****

**Swali la 487: Je anaruhusiwa mwanamke aliyehirimia ibada ya Hijjah au Umrah kuvaa soksi mbili za mikono au kuvaa soksi za miguu?**

**Jibu**: Kuhusu kuvaa soksi za miguu hakuna ubaya kwa mwanamke huyo.

Kuhusu kuvaa soksi mbili za mikono hakika Mtume rehma na amani ziwe juu yake alikataza akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuhusu mwanamke aliye hirimia: ((**Asivae soksimbili za mikono**)), [1838/ Sahihi Muslim].

****

**Swali la 488: Mwanamke aliyepita kwenye mipaka akiwa katika hedhi kisha akahirimia ibada yake akiwa kwenye mipaka akafika Makkah akachelewesha ibada ya Umrah mpaka akatwaharika ni ipi hukumu ya ibada yake?**

**Jibu**: Ibada yake ya Umrah ni sahihi hata kama ataichelewesha kwa muda wa siku mbili au siku moja, lakini nisharti awe ametwaharika na hedhi, kwa sababu mwanamke mwenye hedhi haruhusiwi kutufu kwenye Al-Kaaba, Kwa sababu alipo patwa na hedhi aisha radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake nae alikuwa amefika Makkah akiwa amehirimia ibada ya umrah, Mtume rehma na amani ziwe juu yake alisema kum-

wambia: ((**Hirimia ibada ya Hijjah na fanya anayo yafanya mwenye kuhiji isipokuwa usitufu kwenye Al-Kaaba**)), [305/ Sahihi Bukhary, /1211/ Sahihi Muslim]. Pia wakati Swafiya alivyo patwa na hedhi alisema Mtume rehma na amani ziwe juu yake akasema: ((**Mmemzuia yeye asiondoke?**)), [305/ Sahihi Bukhary, /1211/ Sahihi Muslim], Mtume alidhani kuwa swafiya hajatufu twawafu ya ifadhwa, wakasema kumwambia mtume rehma na amani ziwe juu yake Hakika ameisha fanya twawafu ya ifadhwa (ya nguzo) akasema mtume: ((**Ondokeni**)). [1757/ Swahihi Bukhary, /1211/ Swahihi Muslimu]. Mwanamke mwenye hedhi haruhusiwi kutufu kwenye Al-qaaba akifika Makkah akiwa kwenye hedhi ni lazima kusuburi mpka atwaharike kisha ndio atufu kwenye Al-qaaba kama akitokwa na hedhi baada ya kutufu twawafu ya Umrah lakini kabla ya kufanya saayi atakamlisha ibada yake ya Umrah wala hato toa fidia yoyote, kama ikija hedhi bada ya kufanya saayi sio lazima kwakwe kutufu twawafu ya kuwaga kwakuwa twawafu ya kuwaga hatakiwi kuifanya mwanamke mwenye hedhi.

****

**Swali la 489: Mwanamke amehirimia Hijjah akiwa Miiqati na hali ya kuwa yuko katika hedhi, kisha akatwaharika akiwa Makkahh na akavua nguo zake ni ipi hukumu yake?**

**Jibu:** Mwanamke huyo anaruhusiwa kubadili nguo nyingine, na atavaa nguo zozote anazotaka, muda wa kuwa nguo hizo ni katika nguo zinazo ruhusiwa Kisheria, na vile vile Mwanaume anaruhusiwa kubadili nguo zake za Ihramu kwa kuchukua nyingene.

****

**Swali la 490: Ni ipi hukumu ya Mwanamke kufunika uso wake kwa niqabu katika Hijjah, hakika nilikuwa nimesoma Hadithi yenye maana hii ((Havai niqabu Mwanamke aliye hirimia Hijjah wala asivae gloves)), na nikasoma maneno mengine ya Aisha radhi za Allah ziwe juu yake anasema: ((Tulikuwa tunapo kuwa na Wanaume tunafunika nyuso zetu tunapo wapita tunafunua)) (Ameipokea Al-Bazari (234/18) na Ibnu Maaja (2935), ni vipi tutazikusanya kauli mbili hizi?**

**Jibu:** Lililo sahihi katika hili ni lile lililoelekezwa katika Hadithi, na amekataza Mtume rehma na amani ziwe juu yake: kwa Mwanamke aliye hirimia kuvaa niqabu, na Mwanamke aliye hirimia Hijjah amekatazwa moja kwa moja kuvaa niqabu ni Iwe amepita kwa Wanaume ambao siyo maharim zake au hakupita, kwa hilo ni haramu kwa Mwanamke aliye hirimia kuvaa niqabu awe katika ibada ya Hijjah au katika ibada ya Umra.

Na niqabu ijulikanayo kwa Wanawake ni kufunika uso wake kwa kitu ambacho kinakuwa na matundu katika macho yake.

Na ama Hadithi ya Aisha haipingani na katazo la kuvaa niqabu, na hili ni kwa sababu katika Hadithi ya Aisha hakuna maneno ndani yake ya kusema Wanawake waliku wa waki vaa niqabu, lakini walikuwa wakifunika vyuso zao bila niqabu, na hilo ni jambo ambalo hapana budi kwa wanawake wanapo pita kwa wanaume, hakika ni waJibu juu yao kusitiri vyuso zao; kwa sababu kusitiri uso mbele ya wanaume wa pembeni ni jambo la lazima; na kwa sababu hiyo tunasema: Kuvaa niqabu kwa Mwanamke aliye hirimia ni haramu moja kwa moja, ama kusitiri uso wake kilicho bora ni kufungua lakini wakipita Wanaume karibu yake ni wajibu kufunika uso wake, lakini kufunika kwa kitu kingine kisicho kuwa niqabu.

****

**Swali la 491: Mwenye kufanya kitu katika vitu vilivyo katazwa kwa aliye hirimia ima kwa kusahau au kwa kuto kujua ni ipi hukumu yake?**

**Jibu:** Atakapo fanya kitu katika vitu vilivyo katazwa kwa mwenye kuhirimia baada ya kuvaa ihramu yake na yeye bado hajafunga niya Hijjah halazimiki kitu chochote; Kwa sababu mazingatio ni kwa nia sio kwa kuvaa nguo za Ihramu, lakini pindi atakapo kuwa amenuiya kungia katika Ibada atakapo fanya kitu katika

vitu vilivyo katazwa kwa kusahau au kwa kuto kujua halazimiki kitu chochote, lakini ni wajibu kwake unapo ondoka tu ule udhuru kama ni kwa kusahau basi amekumbuka kama ni kwa kuto kujua basi amejua anatakiwa kuondosha au kujiweka mbali na kile kitu kilicho katazwa.

**Mfano wa hili**: Lau kama Mwanaume amesahau akavaa kanzu hali ya kuwa amehirimia, halazimiki kitu chochote, lakini akikumbuka tu inampasa kuvua hiyo nguo, vile vile kama atasahau akawa hajavua suruali, kisha akakumbuka baada ya kunuiya, hakika inampasa kuvua haraka na wala halazimiki kitu chichote, na hivyo hivyo kama akiwa hajui hakika halazimiki kitu chochote, na mfano wake: Mtu amevaa T-Sheti ndani anadhani kuvaa T-Sheti ndani kwa mtu aliyo hirimia sio tatizo, hakika huyo haimlazimu kitu chochote, lakini itakapo mbainikia kuwa amevaa T-Sheti na kuvaa nguo hiyo ni haramu kwa mtu aliye hirimiya basi ni lazima kuivua.

Na msingi wa pamoja katika hili ni kwamba: Mambo yote yaliyo katazwa kwa aliye hirimiya Hijjah atakapo yafanya Mwanadamu kwa kusahau, au kuto kujua, au kwa kulazimishwa haimlazimu kitu chochote, amesema Allah**: [Mola wetu Mlezi Usituchukulie tukisahau au tukikosea]**. (Suratul Baqar: 286), akasema Allah: ((**Hakika nimesha fanya**)) na amesema Allah: [**Wala hapana ubaya juu yenu kwa mlivyo kosea.Lakini ipo lawama katika yale ziliyo fanya nyoyo zenu kwa makusudi. Na Allah ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu]**, (Suratul Ahzaab 5), na maneno ya Allah kuhusiana na kuwinda nayo ni katika vitu vilivyo katazwa kwa mtu aliye hirimia**: [Na miongoni mwenu atakaye muuwa makusudi]**. (Suratul Maida: 95), na wala hakuna tofauti katika hilo baina ya kuwa kitu kilicho katazwa ni mavazi au manukato au kitu kingine katika vitu vilivyo katazwa, au kwa

mwenye kuuwa kiwindwa au akanyoa nywele na mfano wake, japo kuwa baadhi ya wanachuoni wametofautisha kati ya hiki na hiki, lakini kilicho sahihi ni kuto kutofautisha; kwa sababu hivi nimiongoni vitu vilivyo katazwa ambavyo anasamehewa Mwanadamu kwa kutojua au kusahau au kulazimishwa.

****

**Swali la 492: Mtu amehiji ikatokea baadhi ya makosa katika utekelezaji wake wa Ibada hiyo akalazimika kutoa kafara lakini hakuwa na kitu cha kutoa akiwa Makkah, na akasafiri kwenda katika Nchi yake, je atatoa kile kilicho mlazimu akiwa katika Nchi yake au ni lazima kinachotolewa akitoe akiwa Makkah? Na ikiwa ni lazima iwe Makkah, je inafaa kumuwakilisha mtu kwa ajili ya kumtolea kafara hiyo?**

**Jibu:** Kwanza hapana budi tujue ni kitu gani hicho ambacho kimetokea: Ikiwa ameacha wajibu kuna fidia inatakiwa achinje akiwa Makkah; kwasababu hilo linaambatana na ibada ya Hijjah, na wala haitofaa sehemu nyingine isiyo kuwa Makkah.

Na ikiwa amefanya mambo ambayo yamekatazwa kwa mwenye kuhirimia Hijjah, hakika inatakiwa afanye moja kati ya mambo matatu:

Ima kuwalisha masikini sita, na inakuwa ni Makkah au katika

sehemu ambayo amefanya kosa hilo, au kufunga siku tatu, na katika hali hii atafunga siku tatu akiwa Makkah au sehemu nyingine.

Isipokuwa itakapo kuwa kitu alicho kifanya ni kumuingilia mkewe kabla ya tahaluli ya kwanza katika Hijjah, hakika kilicho wajibu kwake ni ngamia au ng'ombe atamchinja sehemu aliyofanya jambo hilo au Makkah, kisha anaigawa nyama yake kwa masikini, au awe amewinda mnyama hakika kilicho wajibu ni kuchinja manyama anaye fanana na yule aliye muwinda, au kulisha masikini, au kufunga, ikiwa ni kufunga basi atafunga akiwa sehemu yoyote au nchi yoyote, na ikiwa ni kulisha masikini au kuchinja mnyama basi hivyo atavifanyia Makkah Anasema Allah Mtukufu**: [Mnyama huyo apelekwe kwenye Al-Kaaba]** (Suratul Maida: 95), ni lazima achinjiwe pale, na inafaa kumuwakilisha mtu mwingine amfanyie; kwa sababu Mtuma rehma na amani ziwe juu yake alimuwakilisha Ally Radhi za Allah ziwe juu yake katika kuchinja vile vilivyo baki katika wanyama. (Ameipokea Bukhary (4352) na Muslim (1218) ).

****

### Swali la 493: Je inafaa kutanguliza Saayi kabla ya Twawafu?

**Jibu:** Ama kuhusiana na kutanguliza Saayi ya Hijjah kabla ya twawaful ifadha hilo linafaa; kwasababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake alisimama siku ya kuchinja wanyama watu wakawa wanamuuliza, kwa kusema: Nimefanya Saayi kabla ya kutufu; akasema: ((**Hakuna tatizo**)) (Ameipokea Bukhar (1734)

na Muslim (1307)); yule atakaye kuwa amefanya Hijjah ya Tamatuu akatanguliza Saayi katika Haji juu ya twawafu, au amefanya Hijjah ya Ifraadi au Qirani na hakuwa amefanya Saayi pamoja na twawafu Al-Qudumu akaitanguliza Saayi juu ya twawafu; jambo hilo halina ubaya; kwa maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake alipo sema: (Hakuna tatizo).

****

**Swali la 494: Ni ipi hukumu ya kukaririsha Umra katika Ramadhan? Na je kuna muda maalumu kati ya Umra mbili?**

**Jibu**: Kukaririsha Umrah katika Ramadhan ni katika Bidaa; kwa sababu kuzikaririsha katika mwezi mmoja ni kinyume na walivyo fanya wema waliyo tangulia Allah awarehemu; mpaka Sheykhul Islaam Ibn Taymiyah ametaja katika (Fatawa (270/26), kuwa ni makuruhu kukaririsha Umra na kuzidisha, kwa kuafikiana na wema waliyo tangulia, na hasa mwenye kuikaririsha katika Ramadhan, na jambo hilo kama lingekuwa ni jambo lenye kupendeza wengekuwa limefanywa na wema waliyo tangulia wao walikua ni wenye kupupia juu ya hilo na wenge lifanya kwa wingi, huyu hapa Mtume rehma na amani ziwe juu yake mwenye kumcha Allah kuliko watu wote, na ni mwenye kupenda kheri zaidi kuliko watu wote alikaa Makkah mwaka ule wa fathu siku kumi na tisa anapunguza swala na hakufanya Umrah, na huyu hapa Aisha Radhi za Allah ziwe juu yake wakati alipo mlalamikia Mtume rehma

na amani ziwe juu yake ili afanye Umrah Mtume rehma na amani ziwe juu yake alimuamrisha kaka yake Abdul Rahamani Ibnu Abubakari Allah awe radhi nao atoke naye pale Makkah waende sehemu ya kuhirimia ili afanye Umra, lakini Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakumuelekeza Abdul Rahaman afanye Umrah, lau kama ingekuwa hilo linaruhusiwa ange muelekeza Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na lau kama hilo lingekuwa linajulikana kwa Maswahaba basi angelifanya Abdul Rahama kwa sababu alitoka mpaka sehemu ya kuhirimia na hakufanya hivyo.

Ama kuhusu muda maalumu ulio wekwa kati ya Umrah mbili amesema Imamu Ahmed Allah amrehemu: ((Anasubiri mpaka kichwa chake kiwe cheusi)).

****

**Swali la 495: Ni ipi hukumu iwapo swala itakimiwa swala wakati wa kutufu? Je akimaliza kuswali ataanza upya kutufu? kama hatoanza atamalizia sehemu gani?**

**Jibu:** Itakapo kimiwa swala na mtu akawa anatufu ni sawa sawa ni twawafu ya Umrah au twawafu ya Haji, au ni twawafu ya Sunna hakika yeye ataondoka kwenye twawafu yake kisha atakwenda kuswali, kisha atarudi na kukamilisha twawafu yake, na wala haanzi upya, bali atakamilisha katika sehemu ile aliokuwa ameishia kabla ya kusimama, na wala hakuna haja ya kuanza

mzunguko upya; kwa sababu ile iliyo tangulia ilijengwa katika msingi sahihi kwa idhini ya Kisheria haiwezekani kuwa ni batili isipokuwa kwa dalili ya Kisheria.

****

**Swali la 496: Mwenye kufanya Umra atakapo fanya Saayi kabla ya Twawafu, ni kitu gani kinamlazimu?**

**Jibu:** Atakapo fanya Saayi mwenye kufanya Umra kabla ya twawafu kisha akatufu hakika yeye hatorudia isipokuwa Saayi tu; na hilo ni kwa sababu mpangilio baina ya twawafu na Saayi ni lazima;kwani Mtume rehma na amani ziwe juu yakealipangili hivyo na akasema: ((**Chukueni kwangu Ibada yenu ya Hijjah**)). (Ameipokea Bukhary (83) na Muslimu (1297), na tutakapo chukua kwake Mtume rehma na amani ziwe juu yake Ibada hiyo ya Hijjah tutaanza na twawafu kwanza kisha tunakwenda kwenye Saayi, lakini lau kama atasema: Mimi nimechoka kufanya Saayi kwanza, tutasema: Atalipwa kwa kuchoka kwake lakini hatuto muachia kufanya makosa.

Na wamesema baadhi ya taabiina na baadhi ya wanachuoni Allah awarehemu kuwa atakapo fanya Saayi kabla ya twawafu katika ibada ya Umra kwa kusahau, au kuto kujua halazimiki kitu chochote, kama ilivyo katika Hijjah.

****

**Swali la 497: Ni nini Idhitwibaau? na ni wakati gani ina fanywa?**

**Jibu:** Idhitwibau ni mtu kufunua bega lake la kulia na kuiweka pembe ya nguo ya upande wa bega la kushoto. Nayo hufanywa wakati wa kutekeleza a ibada twawaaful Qudumu, ama nyingenezo haifanywi.

****

**Swali la 498: Je inafaa kufanya Sunna ya Saayi?**

**JIBU:** Haifai kufanya Sunna ya Saayi; kwasababu Saayi ime wekwa katika Ibada ya Hijjah au Umra; amesema Allah**: [Hakika vilima vya Swafa na Marua ni katika alama za Allah . Basi anaye hiji kwenye nyumba hiyo au akafanya Umra, si kosa kwake kuvizunguka. Na anaye jitendea mwenyewe kheri basi bila shaka Allah ni Mwenye shukurani na Mjuzi]** (Suratul Al-Baqara: 158 ).

****

**Swali la 499: Mwenye kuacha Twawaaful ifaadhwah kwa kuto kujua ni kitugani kinamlazimu?**

**Jibu:** Twawaaful ifaadhwah ni nguzo katika nguzo za Hijjah haitimii Hijjah isipokuwa kwayo, atakapo iacha mtu hakika Hijjah yake itakuwa haija kamilika, ni lazima ailete, itamlazimu kuifanya hata kama atakuwa Alisha rudi katika Nchi yake italazimika kurudi kuja kuifanya, na katika hali hiyo muda wa kuwa hajatufu twawafu ya Ifadhwa haifai kwake kustarehe na mke wake; kwa sababu hakutahaluli tahaluli ya pili (kuhalalika kwa mara ya pili), kwa sababu haiwi tahaluli ya pili isipokuwa baada ya twawaful ifaadhwah, na Saayi ikiwa alikuwa amefanya Tamatuu, au Qirani au Ifradi, na hakuwa amefanya Saayi pamoja na Twawaaful Qudumu.

****

**Swali la 500: Nimeona baadhi ya watu wanao tufu wanatumia nguvu kuwapeleka wake zao katika kulibusu jiwe jeusi, ni kipi kilicho bora kulibusu jiwe au kujiweka mbali na msongamano pamoja na wanaume?**

**Jibu:** Ikiwa huyu muulizaji ameona jambo la ajabu kama hili mimi nimeona jambo la ajabu kuliko hilo, nimemuona mtu alisimama kabla ya kutoa salamu ili awahi akalibusu jiwe, anabatilisha swala yake ya faradhi aliofaradhishiwa ambayo ni moja kati ya nguzo za Kiislamu ili afanye jambo hilo ambalo sio la wajibu, na pia halikuwekwa katika sharia isipokuwa likiambatana na

twawafu, na hii ni kwa sababu ya ujinga wa watu; kulibusu jiwe na kulinyooshea mkono sio Sunna isipokuwa katika twawafu, mimi sijui kama kulibusu tu peke yake bila twawafu ni katika Sunna, na mimi nasema katika sehemu hii sijui, na ninataraji kwa mwenye elimu kinyume na nijuavyo anifikishie, Allah amlipe kila la kheri.

Kwa hivyo hiyo ni katika Sunna za twawafu, kisha haitakuwa ni katika Sunna isipokuwa ikiwa hakuna katika hilo maudhi sio katika twawafu au katika kitu kingine, pindi itakapo kuwa kuna maudhi katika twawafu au kingine; hakika sisi tutahamia kwenye daraja la pili ambalo ametuwekea sharia Mtume rehma na amani ziwe juu yake ambayo ni mtu aligusa kwa mkono wake kisha aubusu mkono wake, na ikiwa daraja hilo pia kama haliwezekani isipokuwa kwa maudhi na uzito, hakika tutahamia daraja la tatu ambalo ametuwekea Mtume rehma na amani ziwe juu yakenalo ni kuashiria kwa mkono, tunaashiria kwa mko wetu mmoja wa kuliya na sio yote miwili, tunaashiria tu na hatuibusu, hivi ndivo ilivyo kuwa Sunna ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake.

Ikiwa jambo baya na gumu kama alivyo eleza muulizaji kuwa mtu anatumia nguvu kumuingiza mwanamke na huenda akawa mwanamke ni mja mzito, au kikongwe, Au ni binti mdogo asiye weza kusukumana na watu, anaweza kumletea matatizo makubwa, hayo yote ni katika mambo yenye kuchukiza, kwa sababu yanasababisha madhara kwa watu wake na kubanana na wanaume, na yote hayo ni katika mambo yaliyo kati ya uharamu na umakuruhu;ni juu ya mtu asifanye hivyo muda wa kuwa jambo ni pana katika nafsi yake, wala asifanye tashdidi Allah asije akamshadidia.

****

**Swali la 501: Mwanamke amehiji pamoja na mumewe Hijjah ya Tamatuu, walipo fika mzunguko wa sita wa Twawafu ya Umra mume wake akasema: huo ni mzunguko wa saba na akashikilia msimamo wake huo, je kwa huyu mwanamke atalazimika kufanya kitu chochote?**

**Jibu:** Ikiwa yeye mwanake anauhakika wapo katika mzunguko wa sita, na kuwa yeye hajakamilisha twawafu hakika Umra yake itakuwa haijakamilika; kwa sababu twawafu ni nguzo katika nguzo za Umra haiwezekani kutimia Umra isipokuwa kwayo, pindi atakapo kuwa amehirimia Hijjah baada ya hapo atakuwa na Hijjah ya Qirani; kwa sababu yeye ameingiza Hijjah katika Umra kabla ya kuisha kwake, na iwapo itatokea kwake shaka baada ya kuona mume wake ameshikilia msimamo wake kuwa huu ni mzunguko wa saba hakika wakati huo hawajibiki kitu chochote; kwa sababu itakapo tokea kwake shaka, na mume wake ana uhakika, hakika yeye atarudi kwenye kauli ya mume wake, Allah ndiye mjuzi zaidi.

**Swali la 502: Pindi itakapokuwa mwenye kufanya Hijjah au Umra hajui isipokuwa kiasi kidogo katika dua je anaweza kusoma katika vitabu vya dua akiwa katika Twawafu yake au Saayi na sehemu nyingine katika sehemu za Ibada?**

**Jibu:** Hakika mwenye kuhiji au kufanya Umrah zinamtosha dua chache alokuwa nazo ambazo anazijua; kwa sababu dua ambazo anazijua ataziomba hali ya kuwa anajua maana yake, na atamuomba Allah haja yake humo, lakini atakapo chukua kitabu au kuna anaye soma yeye anaitikia kitu ambacho hakijui hakika hilo halimnufaishi, na watu wengi hufuata wenye kutufu kile wanacho sema, hali ya kuwa wao hawajui maana ya anacho kisemwa, na watu wengi huchukua hivi vitabu na kuvisoma hali ya kuwa hajui maana yake, na katika hivyo kuna ambavyo vimepangiliwa katika kila mzunguko kuna dua maalumu hiyo ni katika mambo ya ushushi, haifai kwa Muislamu kuvitumia kwa sababu ni upotevu, na Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakuweka kwa Umma wake dua maalumu kwa kila mzunguko, hakika yeye alisema: ((**Hakika imefanywa kutufu katika nyumba, na katika Swafa na Marua, na kurusha mawe, kwa ajili ya kumtaja Allah)),** (Ameipokea Abuu Daud 1888) na Tirmidhiy (902) na Ahmad (75/6).

Pindi itakapo kuwa hivyo hakika kitu cha wajibu kwa Muumini kujitahadharisha na vitabu hivyo, na amuombe Allah haja yake ambayo anaitaka, na amtaje Allah kwa kitu ambacho anakiweza, na kwa kitu ambacho anakifahamu hilo ni bora kwake kuliko kutumia vitabu hivi ambavyo huenda asijue maana yake, bali anaweza kuwa asiyajue maneno yake achilia mbali maana yake.

****

**Swali la 503: Je kuna dua maalumu kwa ajili ya ibada ya Hijjah na Umrah katika Twawafu na Saayi na sehemu nyingine?**

**Jibu:** Hakuna dua maalumu katika ibada ya Hijjah na Umrah bali ataomba Mtu dua anayo ipenda katika dua anazo zifahamu, lakini atakapo chukua zilizo thibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yakehilo ni bora zaidi, mfano: Dua kati ya Rukunil Yamani na Hajaril As'wadi: ((**Ewe Mola wetu Mlezi tupe katika dunia mambo mema na katika akhera mambo mema na utukinge na adhabu ya moto**)) (Ameipokea Ahamadi 411/3) na Abu Daud 1892) ).

Na vile vile zilizo thibiti katika siku ya Arafa, na dhikiri zilizo thibiti katika Swafa na Mar'wa na zinazo fanana na hizo, kitu anacho kijua katika Sunnahh anatakiwa akiseme, na kitu ambacho hakijui akiache kinatosha kile kilichoko katika kichwa chake katika vile anavyo vijua, na dua hizo sio wajibu bali ni kwa yule anaye taka.

Na kwa mnasaba wa swali hili nataka kusema: Hakika vile vilivyo andikwa kwa ajili ya Ibada ambavyo vipo katika mikono ya Mahujaji na wenye kufanya Umrah miongoni mwa dua maalumu kwa kila mzunguko wa twawafu ninasema: Hakika hiyo ni katika Bidaa, na ndani yake kuna maovu ambayo yanajulikana, hakika hawa ambao wanasoma wanadhani kuwa ni amri iliokuja kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake.

Kisha wanaitakidi kuwa wanafanya Ibada kwa maneno yale maalumu,kisha wao wanayasemo yale maneno na wala hawajui

makusudio yake, kisha wao wamefanya katika kila mzungoko dua maalumu, anapo maliza dua kabala ya kumaliza mzinguko hunyamaza katika sehemu iliobaki ya mzunguko, na akimaliza mzunguko kabla ya kumaliza dua huitaka ile dua na akaiacha, hata kama atakuwa alifika kwenye neno ((Ewe Mola)) haombi tena anacho kitaka bali huiacha,yote hayo ni katika madhara ambayo yanapatikana katika Bidaa hii, na vile vile vingine katika Ibada hii ni kuomba dua wanapo fika Makamu Ibrahim,hakika hili halikuthibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yakekuwa aliomba pale Makamu Ibarahim, hakika alisoma alipo fika pale (Ameipokea Ahmadi (320 /2), Abu Daudi (1905), Tirimidhi (856), Nasaayi (2939) na Ibnu Maaja ( 3074 ))**: [Na alipo kuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia]** (Suratul Al-Baqara 125).

Na aliswali nyuma yake rakaa mbili, ama hizi dua wanazo ziomba hapo na wanawasumbua kwazo wenye kuswali pale hakika hizo ni munkari kwa namna mbili:

1-Hazikuthibiti kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yakekwa hiyo ni Bidaa.

2-Hakika wao wanawaudhi kwa dua hizo wenye kuswali, ambao huswali nyuma ya Makamu Ibrahim .

Na kuna mambo mengi yanayo patikana katika Ibada hizi ya uzushi,ima iwe katika namna ya kutenda au katika wakati, au katika sehemu ya kufanyia Ibada hizi.

Tunamuomba Allah atuongoze.

****

**Swali la 504: Mtu baada ya kumaliza Ibada yake ya Umra amekuta katika nguo zake za Ihramu najisi ni ipi hukumu yake?**

**Jibu:** Atakapo tufu mtu na akafanya Saayi,na baada ya hapo akakuta katika nguo zake najsi, hakika twawafu yake ni sahihi na Saayi yake (kuzunguka baina ya Swafaa na Mar'wa) ni sahihi na Umrah yake ni sahihi; na hilo ni kwa sababu itakapo kuwa katika nguo zake kuna najsi na hakujua,au alikuwa anajua lakini amesahau kuiosha, na akaswali na ile nguo hakika swala yake ni sahihi, na ni hivyo hivyo kama atatufu na nguo hii hakika twawafu yake itakuwa sahihi; na dalili ya hilo ni maneno ya Allah aliposema**:** **[Mola wetu Mlezi!Usituchukulie tukisahau au tukikosea]** (Suratul Baqara: 286), na hii ni dalili yenye kukusanya inazingatiwa kuwa ni msingi mkubwa katika misingi ya sharia , na kuna dalili maalumu katika mas-ala haya; nayo ni:

Mtume rehma na amani ziwe juu yakealiswali siku moja na Maswahaba zake na ilikuwa ni katika Sunna zake rehma na amani ziwe juu yakekuswali na viatu vyake, akavua viatu vyake, watu nao wakavua viatu vyao, alipo maliza swala yake akasema: (**Mnajambo gani**) wakasema: Tumekuona ewe Mtume wa Allah umevua viatu vyako nasi tukavua viatu vyetu, akasema: ((**Hakika Jibrili alinijia ananiambia kuwa katika viatu vyangu kuna uchafu)**). (Ameipokea Abu Daud (650)), ina maana najsi,na hakuanza upya Mtume rehma na amani ziwe juu yakeswala yake, pamoja ya kuwa mwanzo mwa swala yake alikuwa amevaa viatu vyenye najsi, linafahamisha hilo kuwa mwenye kuswali na nguo yenye najsi kwa kusahau au kwa kuto kujua hakika swala yake ni sahihi.

***Na hapa kuna mas'ala:** Atakapo kula mtu nyama ya Ngamia na akasimama kuswali na hakutawadha kwa kudhani kuwa amekula nyama ya mbuzi je atarudia swala yake akikumbuka?

(Haya mas-ala ni kwa wenye kusema mtu alikila nyama ya Ngamia udhu wake umetenguka,ni madhahabu ya Ahmad)

***Tunasema:** Hakika yeye atarudia swala yake baada ya kutawadha.

***Atakapo sema mwenye kusema:** Kwanini mmesema kwa yule alioswali na nguo ya najsi kwa kuto kujua harudii, na huyu aliokula nyama ya Ngamia kwa kuto jua arudiye?

***Tunasema:** Kwa sababu tuna msingi wenye faida na muhimu na ni: ((Hakika vitu vilivyo amrishwa havipomoki kwa kuto kujua na kusahau, na vitu vilivyo katazwa vinapomaka kwa kuto kujua na kusahau)), na dalili ya Msingi huu ni maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Mwenye kulala juu ya swala au akasahau basi aiswali atakapo kumbuka**)) (Umetangulia utangulizi wake); na Mtume rehma na amani ziwe juu yake alipo toa salamu katika rakaa mbili katika moja ya swala zake za usiku na akawa amesahau sehemu ya swala yake aliikamilisha wakati alipo kumbuka, hii ni dalili kuwa vitu vilivyo amrishwa havipomoki kwa kusahau; kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yakeameamrisha mwenye kusahau swala aiswali atakapo kumbuka, na haikupomoka kwa kusahau kwake, hivyo hivyo alikamilisha swala yake kile alicho kisahau hakikupomoka kwa kusahau.

Na dalili kuwa vitu vilivyo amrishwa havipomoki kwa kuto jua, mtu mmoja alikuja akaswali swala ambayo ilikuwa haina utulivu ndani yake,kisha akaja kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yakeakamsalimia akasema kumuambia: **((Rudi ukaswali hakika wewe hukuswali**)) akarudia mara tatu hali ya kuwa anaswali ki-

sha anakuja kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yakena Mtume anamrudisha huku akimuambia: ((**Rudi ukaswali hakika wewe hukuswali** )) (Ameipokea Bukhary (757) na Muslim (397)), mpaka alipo mfundisha Mtume rehma na amani ziwe juu yakena akaswali swala iliyo sahihi, huyu mtu aliacha waJibu kwa kuto kujua ; kwa sababu alisema: ((Naapa kwa yule ambaye amekutuma kwa haki siwezi kuswali vizuri zaidi ya hivi nifundishe)), lau kama ingelikuwa waJibu unapomoka kwa kuto kujua basi Mtume rehma na amani ziwe juu yakeanagalimuacha yule mtu,na huu ni msingi muhimu wenye faida kwa wenye kutafua selimu.

****

**Swali la 505: Je ile alama ya nyayo iliyopo pale Makamu Ibrahimu ndio alama yenyewe ya miguu ya Ibrahim rehema na amani ziwe juu yake au hapana?**

**Jibu:** Hapana shaka kuwa Makamu Ibrahimu ipo, na sehemu ambayo imejengewa kwa vioo ndio Makamu Ibrahimu, lakini shimo lililopo ndani yake hainidhihirikii kuwa ndio alama za nyayo zake mbili; kwasababu kinacho julikana katika upande wa kitarekhe ni kuwa alama za nyayo zake zilisha futika tangu muda mrefu, lakini ilichimbwa sehemu hii kwa ajili ya kuweka alama tu, na haiwezekani tuseme kwa uhakika kuwa lile shimo ndio sehemu ya miguu ya Ibrahimu rehema za Allah ziwe juu yake.

Na kwa kunasibiana na hilo nataka nitoe uzindushi katika jambo moja nalo ni kuwa baadhi ya wenye kufanya Umrah na Mahujaji huwa wanasimama pale Makamu Ibrahimu, na wanaomba kwa

dua ambazo hazikupokelewa kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake,na wakati mwingine huomba dua hizo kwa sauti ya juu,wanakuwa wanawasumbua wale ambao wanaswali rakaa mbili za twawafu pale Makamu Ibrahim, ile sio sehemu ya kuomba dua bali Sunnahh ni kuswali rakaa mbili nyuma yake, kisha baada ya kumaliza atasimama wakati huohuo ili awaachie wenzeke ambao wanataka kuswali rakaa mbili za twawafu.

****

**Swali la 506: Je inafaa kujifuta kwa ile nguo iliyofunika Al Kaaba kwa ajili ya kutafuta baraka?**

**Jibu:** Kujifuta kwa nguo ya Al-Kaaba kwa kutafuta Baraka ni katika mambo ya uzushi; kwa sababu hilo halikupokelewa kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, na wakati alipotufu Muawiya Ibnu Sufiyani Al-Kaaba radhi za Allah ziwe juu yakena akawa anazifuta nguzo zote za Al-Kaaba, Ibnu Abas alimkataza jambo hilo, akamjibu Muawiya ((Hukuna kitu chochote katika Al-Kaaba kinafaa kuachwa)), Ibnu Abasi akamJibu kwa kusema: ((Hakika mna kiigizo kizuri kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, hakika nilimuona Mtume rehma na amani ziwe juu yakeakifuta nguzo mbili za yamani)) (Ameipokea Bukhari (1608).

Nguzo mbili anazo kusudia ni nguzo ya kwenye Hajari asuwadi na rukuni Al-Yamani, na hii ni dalili ya kuwa tunatakiwa

tuiguse Al-Kaaba na nguzo zake kama ilivyo kuja katika Sunnahh za Mtume rehma na amani ziwe juu yakekwa sababu hicho ndicho kiigizo chema kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, ama sehemu iliyo kati ya jiwe jeusi na mlango hakika pale imethibiti kuwa Maswahaba walisimama pale wakaomba, Allah ndiye mjuzi zaidi.

****

**Swali la 507: Ni ipi hukumu ya kunyoa au kupunguza katika Umrah? na ni kipi kilicho bora kati ya kunyoa na kupunguza?**

**Jibu:** Kunyoa au kupunguza kwa mtu aliofanya Umrah ni wajibu; kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake alipo kuja Makkah katika Hijjah ya kuaga alitufu na akafanya saayi na akaamrisha kila ambaye hajaswaga wanyama wa hadiyi apunguze kisha ahalalike kwa yale yaliyo kuwa haramu kwa mwenye kuhirimia, alipo waamrisha wapunguze hilo linaonesha ni lazima kupunguza; na pia linaonesha juu ya hilo kuwa Mtume

rehma na amani ziwe juu yakealiwaamrisha Maswahaba zake wakati walipo zuiliwa na makafiri kuingia Makkah katika vita vya Hudaibiya wanyoe, mpaka Mtume rehma na amani ziwe juu yakealikasirika walipo kuwa wanasitasita kunyoa. (Ameipokea Bukhar (273).

Ama kuhusu ni kipi kilicho bora kati ya kunyoa na kupunguza?

Kilicho bora ni kunyoa isipokuwa aliyo kusudia kufanya Hijj-

ah ya Tamatuu ambaye ameingia Makkah kwa kuchelewa, hakika kilicho bora kwa huyu ni kupunguza ili atunze nywele zake kwa ajili ya kuja kunyoa kwa ajili ya Hijjah.

****

**Swali la 508: Mtu amehiji Hijjah ya Tamatuu, akatufu na akafanya saayi kwa ajili ya Umrah na akavaa nguo zake za kawaida, hakunyoa wala kupunguza akauliza baada ya Hijjah akaambiwa alikosea, analazimika kufanya nini?**

**Jibu:** Mtu huyo atakuwa ameacha waajibu katika waajibu wa Umrah, nao ni kunyoa au kupunguza, na kwa mujibu wa Wanazuoni atalazimika kuchinja mnyama pale Makkah, kisha aigawe kwa masikini wa Makkah, na yeye atabaki katika Tamatuu yake na Umrah yake itakuwa sahihi.

****

**Swali la 509: Mwenye kuhirimia Hijjah ya Tamatuu na hakunyoa wala kupunguza katika Umrah yake na akakamilisha Ibada ya Hijjah; anatakiwa afanye nini?**

**Jibu:** Huyo mwenye kuhiji atakuwa ameacha wajibu katika wajibu wa Umrah, kwa sababu kunyoa au kupunguza ni katika wajibu wa Umrah, na suala la kuacha wajibu kwa wanachuoni atalazimika kuchinja mnyama Makkah kisha anaigawa kwa mafukara wa Makkah; kwa sababu hiyo tunasema kwa huyu Haji: Kwa muJibu wa maneno ya wanachuoni ni lazima uchinje mnyama kisha ugawe nyama yake kwa mafukara wa Makkah, ukifanya hivyo itakuwa Umra yake na Hijjah yake imekamilika, na kama atakuwa yupo nje ya Makkah hakika atatakiwa kumuwakilisha Mtu atakaye mchinjia fidia yake Makkah, Allah ndiye mjuzi.

****

**Swali la 510: Mtu amefanya Hijjah ya Tamatuu na hakupata mnyama wa kumchinja akafunga siku tatu akiwa Hijjah na hakufunga siku saba zilizo baki, na ikapita miaka mitatu, atafanya nini?**

**Jibu:** Itamlazimu kufunga zile siku saba zilizo baki katika siku kumi. Tunamuomba Allah msaada kwa kila jambo.

****

**Swali la 511: Mtu amefanya Umrah kisha hakunyoa akiwa Makkah amekwenda kunyoa akiwa katika nchi yake ni ipi hukumu yake?**

**Jibu:** Wanasema wana chuoni Allah awarehemu: Hakika kunyoa kichwa hakuhusiani na sehemu maalumu, pindi mtu atakapo nyoa Makkah au akanyoa nje ya Makkahh hakuna tatizo, lakini kunyoa katika Umrah ndio kutakako mfanya mtu iwe halali kwake kufanya yele aliyo kuwa ameharamishiwa wakati amehirimia, pia atatakiwa kwake baada ya kunyoa twawafu ya kuaga Umrah ipo hivi taratibu zake:

Kuhirimia, kutufu,kufanya sayi, kunyoa au kupunguza, na kufanya twawafu ya kuagapindi atakapo kaa mtu baada ya kufanya Umrah, ama atakapo ondoka mara tu baada ya kumaliza ibada yake ya Umrah basi hatafanya Wadaa, kwa sababu hiyo hapana budi kunyoa au kupunguza nywele zake akiwa Makkahh ikiwa anataka kubakia hapo kwa muda flani; kwa sababu atafanya baada ya Umrah twawafu ya kuaga, ama atakapo tufu kisha akafanya Saayi muda huo huo akatoka kurudi katika nchi yake basi hapana ubaya kwake kunyoa au kupunguza akiwa katika nchi yake, lakini atabaki katika nguo zake za Ihramu mpaka atakapo nyoa au kupunguza.

****

**Swali la 512: Mwenye kuhirimia Umrah hali yakuwa anakusudia kufanya Hijjah ya Tamatuu, kisha akaamua asihiji katika mwaka huo je inamlazimu kitu chochote?**

**Jibu:** Halazimiki kitu chochote; kwasababu mwenye kufanya Hijjah ya Tamatui atakapo hirimia Umrah kisha akaikamilisha kisha ikampitikia kabla ya kuhirimia Hijjah kuwa asihiji halazimiki kitu chochote, isipokuwa kama aliweka nadhiri kuwa atahiji katika mwaka huu basi atalazimika kutekeleza nadhiri yake, lakini ikiwa bila nadhiri basi hapana ubaya juu yake pindi atakapo acha Hijjah baada ya kutekeleza Ibada ya Umrah.

****

**Swali la 513: Mtu amehirimia Hijjah ya Tamatuu na akafanya Umrah na hakujihalalisha katika ihramu yake ya Umrah mpaka alipo chinja mnyama wake lakini amefanya hilo kwa kuto jua analazimika kufanya nini? Je Hijjah yake itakuwa sahihi?**

**Jibu:** Mtu ni lazima ajue kuwa atakapo hirimia Hijjah ya Tamatuu, hakika yeye atakapotufu na akafanya saayi, akanyoa au kupunguza nywele zake anakuwa ametoka katika kuhirimia, kila kitu kilicho kuwa haramu kwake kinakuwa ni halali, hili ndilo la waaJibu, pindi atakapo endelea katika ihramu yake ikiwa alikuwa amenuiya Hijjah kabla hajaanza kutufu twawafu ya Umrah hilo

halina ubaya kwake; kwa sababu katika hali hiyo atakuwa amefanya Hijjah ya Qirani, na yule mnyama wake ni kwa sababu ya Hijjah ya Qirani.

Ikiwa alikuwa amebaki katika niya ya Umrah mpaka akatufu na akafanya saayi, hakika wengi katika wanachuoni Allah awarehemu wanasema: Hakika kuhirimia kwake Hijjah sio sahihi; kwa sababu haiswihi kuingiza Hijjah katika Umrah baada ya kuanza kutufu.

Na baadhi ya wanachuoni Allah awarehemu wanaona jambo hilo halina ubaya, muda wa kwamba hajui, kitu ninacho kiona mimi hakika yeye halazimiki kitu chochote na Hijjah yake ni sahihi akipenda Allah.

****

**Swali la 514: Watu walikuwa wanaelekea Muzdalifa wakapotea njia walipo fika sehemu wakasimama wakaswali Magharibi na Ishaa saa saba ya usiku wakaendelea na safari yao mpaka walipo ingia Muzdalifa wakati wa adhana ya Alfajiri wakaswali Alfajiri hapo Muzdalifa, je watalazimika kufanya kitu chochote kwa kutolala pale Muzdalifa?**

**Jibu:** Watu hawa hawalazimika kitu chochote; kwasababu wameipata swala ya Alfajiri Muzdalifa wakati walipoingia hali ya kuwa kunaadhiniwa, na wame swali pale hali ya kuwa bado kuna

giza lake, hakika imethibiti kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa amesema: ((**Mwenye kuipata swala yetu hii, na akasimama nasi mpaka tukaondoka pamoja , na alikuwa amesimama kabla ya hapo Arafa iwe usiku au mchana hakika Hijjah yake itakuwa imekamilika**)) (Ameipokea Abu Daud (1950), Tirmidhii (891), Nasaaiyi (3041), na Ibnu Maaja (3016), lakini hao walikosea pale walipo chelewesha swala mpaka baada ya nusu ya usiku; kwa sababu wakati wa swala ya Ishaa ni mpaka katika nusu ya usiku, kama lilivyo thibiti hilo katika (Sahihi Muslim) kutoka katika Hadithi ya Abdillah Ibnu Al-Aswi radhi ya Allah iwe juu yake, kutoka kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake.

****

**Swali la 515: Mwanamke ameondoka Muzdalifa mwisho wa usiku, akamtaka mtoto wake akamrushie mawe pamoja ya kuwa mwenyewe anaweza kwenda kurusha, je ni ipi hukumu ya jambo hilo?**

**Jibu:** Kurusha mawe ni katika Ibada za Hijjah; kwasababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake ameliamrisha hilo na akalifanya mwenyewe kwa nafsi yake, na akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake ((**Hakika si vinginevyo imewekwa Twawafu katika nyumba na Swafa na Marua, na kurusha Mawe kwa sababu ya kumtaja Allah**)) (Umetangulia upokezi wake), hiyo ni

Ibada ambayo Mwanadamu hujikurubisha nayo kwa Mola wake, nayo ni Ibada kwa sababu Mwanadamu husimama na kurusha mawe katika sehemu hiyo hali ya kuwa ni kumuabudu Allah, na kumtaja Allah,kwa hiyo kurusha mawe kumejengwa juu ya msingi wa Ibada; kwa ajili hiyo inatakiwa Mwanadamu wakati anarusha awe mnyenyekevu kwa Allah, kwa hali yoyote itakayo kuwa, yatakapo kuwa yametokea mazungumzo katika kuwahi kurusha katika mwanzoni mwa wakati wake au kuchelewesha mwishoni mwa wakati wake - lakini pindi atakapo chelewesha akarusha kwa utulivu na kwa unyenyekevu basi inakuwa kuchelewesha kwake ni bora; kwa sababu ubora huu unafungamana na Ibada yenyewe, na kitu kinacho fungamana na Ibada yenyewe hutangulizwa kuliko kinacho fungamana na wakati wa Ibada au sehemu ya Ibada, na kwa sababu hii amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Hakuna swala chakula kinapo kuwa tayari wala hali ya kuwa yeye anazuiya vichafu viwili**)) (Umetangulia upokezi wake); anaweza Mwanadamu kuchelewesha swala kutoka mwanzo mwa wakati wake kwa sababu ya kukidhi haja, au kwa sababu ya chakula kilicho tayari.

Kwa hiyo: Yatakapo kuwa mambo ni kati ya kurusha mawe katika mwanzo mwa wakati wake, lakini kutokana na uzito na msongamano mkubwa uliopo, na kupupia katika usalama wa maisha, na katika kuchelewesha kurusha mpaka mwisho mwa wakati wake hata kama ni usiku ukarusha kwa utulivu na kwa unyenyekevu inakuwa kuchelewesha ni bora zaidi, na kwa sababu hiyo aliruhusu Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa wale walio madhaifu miongoni mwao kuondoka Muzdalifa mwishoni mwa usiku, ili wasije wakapatwa na usumbufu wa msongamano ambao hutokea pindi watu wanapo ondoka baada ya alfajiri (Ameipokea Bukhary ( 1681) na Muslim (1290).

Pindi litakapo kuwa lipo wazi hilo hakika haifai kwa Mwanadamu kuwakilishwa na yeyote katika kurusha mawe kwa maneno ya Allah aliposema: [**Na kamilisheni Hijjah na Umra kwa ajili ya Allah**], na wala hakuna tofauti katika hilo kati ya Mwanaume na Mwanamke, na hakika kurusha mawe ni katika Ibada, na kwamba haifai kwa mwenye kuweza awe Mwanaume au Mwanamke awakilishwe na mtu mwingine hali ya kuwa anaweza kurusha mwenyewe, hakika hapo inampasa kurusha mwenyewe kwa ajili ya nafsi yake, isipokuwa kwa mgonjwa Mwanamke au Mwanaume, au mjamzito inaogopewa mimba yake, basi kwa dharura hizo mwenye kuwa nazo anaweza kurushiwa.

Ama mas-ala yalio tokea kwa Mwanamke huyu ambaye ametajwa kwamba hajarusha pamoja ya kuwa alikuwa na uwezo wa kurusha, kitu ninacho kiona ni yeye kuchinja mnyama na kugawa nyama yake kwa watu wa Makkah kwa ajili ya fidia kwa kuacha kwake waaJibu katika waaJibu wa Hijjah .

****

**Swali la 516: Mtu mwenye kuhiji amerusha mawe Jamaratul Al-Akaba kwa upande wa mashariki na jiwe halikuangukia kwenye lile shimo na siku hiyo ni siku ya kumi na tatu je inamlazimu kurudia kurusha yote?**

**Jibu:** Haimlazimu kurudia yote bali itamlazimu kurudia yale aliyo kosea tu, kwa sababu hiyo atarudia kurusha katika Jamaratul Al-Akaba tu, atarusha kama inavyo takiwa, na wala yale mawe

aliorusha kwa upande wa mashariki hayato tosheleza ikiwa yata kuwa haya kuangukia katika shimo, ambapo ndio sehemu ya kurushiwa, kwa ajili hiyo kama atarusha katika daraja kwa upande wa mashariki itatosheleza kwa sababu yataangukia katika shimo.

****

**Swali la 517: Itakapo kuwa wakati wa kurusha jiwe moja au mawili katika yale mawe saba hayakufika sehemu inayo takiwa kufika na zimepita siku mbili au tatu je atarudia kurusha yale ambayo alikosea? Na iwapo itamlazimu je atarudia na yaliyo fuata baada ya yale aliyo kosea?**

**Jibu:** Itakapo tokea kuwa hakurusha jiwe moja au mawili katika mawe yanyao rushwa, au kwa uwazi zaidi tunasema atakapo rusha kijiwe kimoja au viwili katika moja ya sehemu za kurusha mawe, hakika wana chuoni wanasema pindi itakapo kuwa ni ile sehemu ya kurusha ya mwisho basi atakamilisha kile kilicho pungua tu, wala haita mlazimu kurudia yale yalio pita, na ikiwa sio katika ile sehemu ya mwisho ya kurusha, basi atakamilisha kilicho pungua na atarusha yanayo rushwa baada ya hapo.

**Na kilicho sahihi kwangu**: Hakika yeye atakamilisha yale mapungufu moja kwa moja, wala haimlazimu kurudia kurusha yaliyo baada yake, na hilo ni kwa sababu kufanya kwa mpangilio huondoka kwa kuto kujua, au kwa kusahau, na huyu mtu amerusha mara ya pili naye akiwa haamini kuwa anakitu katika vitu vilivyo kuwa kabla yake yeye yupo kati ya kuto kujua na kusahau, na wakati huo tutasema kumuambia: kile kilicho pungua katika kurusha basi rusha, wala haikulazimu kurusha yale yalio kuwa baada ya hapo.

Na kabla sijamalizia Jibu ninapenda kutoa uzindushi kwamba ile sehemu ya kurusha yanapo kusanyika mawe sio kwamba ile nguzo ndio inayo kusudiwa tu katika kurusha, lau kama mtu atarusha na kijiwe chake hakikuipata nguzo kikaangukia katika ile shimo basi kurusha kwake ni sahihi, Allah ndiyo mjuzi zaidi.

****

**Swali la 518: Kunasemwa: Haifai kurusha jiwe ambalo limesha rushwa je hiyo ni sahihi? Na ni ipi dalili ya shutma hiyo? Allah akulipeni pamoja na Waislamu wote kheri.**

**Jibu:** Hiyo sio sahihi; kwasababu ambao wamesema haifai kurusha kijiwe ambacho kimerushwa wametoa sababu tatu:

1-Wamesema: Jiwe ambalo limesharushwa limekuwa ni kama maji yalio tumika katika kujitwaharisha twahara ya wajibu, na maji yalio tumika katika kujitwaharisha twahara ya wajibu yana kuwa ni twahara yasio twaharisha.

2-Jiwe ambalo limesha rushwa ni kama mtumwa ambaye amesha achwa huru, hakika hafai kuacha huru tena katika kafara au kitu kingine ambacho kitamlazimu kuacha mtumwa huru.

3-Kusema kuwa inafaa kurusha kijiwe ambacho kimesha rushwa kauli hiyo inajuzisha Mahujaji wote kurusha jiwe moja, yani anachukua huyu anarusha mpaka yanakamilika saba, kisha anachukua mwingin anarusha mpaka yanakamilika saba.

Hizi sababu tatu ukizizingatia vizuri ni dhaifu sana.

**Ama sababu ya kwanza**: Hakika sisi tunasema tunakataa hukumu katika asili, ambayo ni maji yaliyo tumika katika twahara ya wajibu yanakuwa ni twahara yasio twaharisha; kwa sababu hakuna dalili juu ya hilo, na wala haiwezekani kuyaondoa maji katika sifa yake ya asili ambayo ni twahara isipokuwa kwa dalili, kwa hivyo maji yalio tumika katika twahara ya wajibu ni twahara nan i yenye kutwaharisha, pindi itakapo kuwa imeondoka hukumu katika asili ilio pimiwa kwayo huondoka hukumu katika tawi.

**Ama sababu ya pili**: Nayo ni kulinganisha kijiwe kilicho tumika kwa kurusha na mtumwa alio achwa huru, hakika huko ni kulinganisha vitu viwili visivyo fanana, hakika mtumwa atakapo acha huru hawi mtumwa tena anakuwa hafai kutolewa kafara sehemu ambayo inahitajika kutolewa kafara kwa mtumwa, ni kinyume na jiwe likirushwa hakika bado linabaki kuwa ni jiwe hata kama

limerushwa, haiondoki ile maana ambayo ilisababisha liwe linafaa kurushwa, na kwa ajili hiyo lau kama mtumwa aliye achwa huru atakuwa mtumwa kwa mara nyingine kwasababu za Kisheria inafaa kuachwa huru mara ya pili.

**Ama sababu ya tatu**: Ambayo ni kulazimu Mahujaji kurusha jiwe moja tunasema: Ikiwa itawezekana hilo basi na liwe, lakini hilo haliwezekani, na wala mtu hawezi kufanya hivyo hali ya kuwa mawe yamejaa kila sehemu.

Kwa sababu hiyo pindi litakapo anguka jiwe moja au zaidi mkononi mwako pale katika sehemu ya kurushia mawe chukua jiwe jingine kwa mtu yeyote aliyoko karibu yako, kisha lirushe na hata kama unahisi mwenzio amelitumia au hakulitumia.

****

**Swali la 519: Je inafaa kwa mwenye kuhiji kutanguliza Saayi ya haji juu ya Twawafu Al-Ifadhwa?**

**Jibu:** Ikiwa mwenye kuhiji amefanya Hijjah ya Ifradi au Qirani hakika hiyo inafaa kutanguliza Saayi juu ya Twawafu Al-Ifadhwa, na ataifanya hiyo Saayi baada ya Twawaaful Qudumu kama alivyo fanya Mtume rehma na amani ziwe juu yake na Maswahaba zake ambao waliswaga wanyama (walienda na wanyama).

Ama atakapo kuwa ni mwenye kufanya Hijjah ya Tamatuu hakika yeye inamlazimu kufanya Saayi mbili, ya kwanza wakati

wa kufika kwake Makkah nayo ni ya Umrah atatufu, na atafanya Saayi na atapunguza, na ya pili ni kwa ajili ya Hijjah.

Na iliyo bora ni kuwa baada ya Twawafu Al-Ifadhwa; kwasababu Saayi huwa inaifuata Twawafu, na iwapo atatanguliza Saayi juu ya Twawafu hakuna tatizo katika kauli yenye nguvu; kwasababu Mtume rehma na amani ziwe juu yakealiulizwa akaambiwa: Nimefanya Saayi kabla ya kutufu akasema: ((Hakuna tatizo)) (Umetangulia upokezi wake).

Mwenye kuhiji anafanya  siku ya Idd Ibada tano kwa mpangilio: Kurusha mawe kwenye  Jamaratu Al-Akaba, kisha kuchinja, kisha kunyoa au kupunguza, kisha kufanya Twawafu katika Al-Kaaba, kisha kufanya Saayi katika Swafa na Marua, isipokuwa mwenye kufanya Hijjah  ya Qirani au Ifradi ambaye alifanya Saayi baada ya Twawafu Ya Quduumu (ya kufika )  hana Saayi nyingine, kilicho bora ni kupangilia kama nilivyo eleza, na iwapo itatokea akatanguliza kimoja juu ya kingine  hapana tatizo na hii ni katika rehema za Allah na kutufanyia wepesi, sifa zote nzuri anastahiki Allah Mlezi wa viumbe wote.

****

**Swali la 520: Ni wakati gani kurusha mawe Jamaratul Aqaba kunaisha ili mtu azingatiwe amerusha katika wakati wake, na ni wakati gani unazingatiwa kuwa amerushwa kwa kulipa yani amerusha nje ya wakati?**

**Jibu:** Ama kurusha mawe kwenye Jamaratul Aqaba siku ya Iddi hakika kunaishia baada ya kuchomoza alfajiri ya tarehe kumi na moja, na inaanza mwisho wa usiku wa siku ya kuchinja kwa wale madhaifu na mfano wa haoambao hawawezi kusongamana na watu, ama kurusha katika masiku ya Tashiriki wana anza kurusha baada ya zawali ,na kunaisha kwa kuchomoza alfajiri katika usiku ambao unaielekea siku inayo fuata, isipokuwa itakapo kuwa ni siku ya mwisho katika masiku ya Tashriki, basi usiku hakuna kurusha nao ni usiku wa tarehe kumi na nne; kwa sababu siku za Tashiriki zimekwisha kwa kuzama jua, pamoja na hivyo kurusha mchana ni bora isipokuwa katika wakati huu kwa kuwa mahujaji ni wengi, na huwa kunatokea kuto kujaliana baadhi yao na wengine, na pindi mtu atakapo ogopea nafsi yake kuangamia, au kupata madhara, au kupata tabu; hakika huyo anaweza kuacha kurusha mchana akasubiri kwenda kurusha usiku na wala hakuna tatizo kwake, lakini lililo bora ni kurusha mchana na wala asirushe usiku isipokuwa kwa dharura.

Ama maneno ya muuliza kuwa anarusha (kulipa) hakika hiyo haiwi kulipa isipokuwa akichelewa mpaka likachomoza jua katika siku inayo fuata.

****

**Swali la 521: Je inafaa kutanguliza Saayi kabla ya Twawafu hasahasa siku ya Idd?**

**Jibu:** Lililo sahihi ni kuwa hakuna tofauti kati ya siku ya Idd na siku nyingine katika kufaa kutanguliza Saayi juu ya twawafu hata kama itakuwa ni baada ya siku ya Idd; kwasababu ya hadithi wakati aliposema mtu mmoja kumuambia Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Nimefanya Saayi kabla sijatufu, akasema: ((**Hakuna tatizo**)) (Umetangulia upokezi wa hadithi hii), pindi itakapo kuwa Hadithi ni yenye kueneya hakika inakuwa hakuna tofauti kati ya kulifanya hilo siku ya Idd au baada yake.

****

**Swali la 522: Atakapo tufu mtu analazimika pia kufanya Saayi lakini akatoka bila kufanya Saayi kisha akaambiwa baada ya kutoka kuwa hakufanya Saayi, je atafanya Saayi tu au atalazimika arudie na Twawafu?**

**Jibu:** Mtu atakapo tufu hali ya kuwa anaamini kuwa analazimika kufanya Saayi, kisha akatoka akaambiwa kuwa ana Saayi hajaifanya hakika huyo ataleta Saayi tu, wala hakuna haja ya kurudia twawaafu, na hilo ni kwa sababu sio sharti kufuatanisha kati ya twawaafu na Saayi.

Hata tukijalia kuwa Mtu huyu aliacha kwa makusudi, yani ameichelewesha Saayi baada ya kufanya twawaafu kwa makusudi, hakuna tatizo kwake, lakini kilicho bora ni iwe Saayi ni yenye kufuatana na twawaafu.

****

**Swali la 523: Ni ipi rai yenu kwa yule ambaye akishamaliza ibada ya umra anapunguza nywele baadhi ya sehemu katika kichwa na sio kichwa kizima?**

**Jibu:** Ninacho kiona kwa huyu hakika hajakamilisha kupunguza kwake, na hakika kitu kilicho wajibu kwake ni avue nguo zake kisha avae ihramu kisha apunguze kupunguza kuliko sahihi, kisha baada ya hapo kila kilicho kuwa ni haramu kwa ajili ya kuhirimia kitakuwa halali.

Na mimi kwa mnasaba huu nataka kutoa uzindushi kuwa ni wajibu kwa kila Muumini anaye taka kumuabudu Allah kwa Ibada yeyote inamlazimu aijue mipaka ambayo Allah ameiteremsha kwa Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake katika Ibada hiyo, ili amuabudu Allah kwa ujuzi sio kwa ujinga, amesema Allah kumuambia Mtume wake rehma na amani ziwe juu yake: [**Sema: Hii ndio njia yangu ninailingania kwa Allah kwa kujua mimi na wanao nifuata**] (Suratul Yusuf: 108) lau kama Mtu atataka kusafiri kutoka Makkah kwenda Madina hawezi kutoka mpaka aulizie kwanza usafiri na hali ya njia ipoje hizi ni njia ambazo tunaziona kwa nini isiwe pia katika njia ambazo hatuzioni ambazo ndizo zinazo tufikisha kwa Allah?!

Na kupunguza: Ni kunyoa baadhi ya nywele katika kichwa chote, na kilicho bora katika kupunguza atamie mashine kwa sababu yenyewe inaenea kichwa kizima, japo kuwa inafaa kupunguza na mkasi, lakini kwa sharti apite katika kichwa kizima, kama vile ambavyo katika udhu anapitisha kichwa kizima hivyo hivyo katika kunyoa, Allah ndiye mjuzi zaidi.

****

**Swali la 524: Ni upi wakati wa kurusha mawe?**

**Jibu:** Wakati wa kwenda jamarati kwa ajili ya kwenda kurusha mawe na kwenda kwenye Al-Akaba katika siku ya Idd kwa wale watu wenye kuweza ni kuanzia kuchomoza jua siku ya Idd, na kwa wengine wenye udhaifu ambao hawawezi kusongamana na watu kama vile Wanawake na Watoto wakati wao wa kuanza kurusha ni mwisho wa usiku, alikuwa Asmaa binti Abubakar Radhi za Allah ziwe juu yake akichunga kuzama kwa mwezi usiku wa siku ya Idd utakapo zama tu huondoka Muzdalifa kuelekea Minna na anakwenda kurusha mawe (Ameipokea Bukhary (1679) na Muslim (1291).

Ama mwisho wake ni kuzama jua siku ya Iddi, na kama kutakuwa na msongamano au ikawa yupo mbali na Jamarati na akapenda acheleweshe mpaka usiku nyingine hapana ubaya kwa hilo, lakini asicheleweshe mpaka alfajiri ikachomoza siku ya kumi na moja.

Ama kuhusiana na kurusha mawe katika masiku ya Tashriki nayo ni tarehe kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tatu, hakika kuanza kurusha kunakuwa ni baada ya (zawali) nao ni mchana wakati wa kuingia muda wa swala ya adhuhuri na unaendelea mpaka usiku, na pindi itakapo kuwa kuna uzito wa msongamano na mengineyo basi hakuna ubaya akirusha usiku mpaka wakati wa kuchomoza alfajiri,

Na wala haifai kurusha katika siku za tarehe kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tatu kabla ya zawali; kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yakehakurusha isipokuwa baada ya zawali, na akasema kuwaambia watu: ((**Chukueni kutoka kwangu ibada zenu**) (Umetangulia upokezi wake), kule kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yakeamecheleweshа kurusha mawe

mpaka katika wakati huu pamoja ya kwamba walikuwa katika joto kali na ameacha kwenda kurusha asubuhi pamoja na kwamba asubuhi kuna hali ya hewa nzuri na kuna wepesi, hiyo ni dalili ya kuwa haifai kurusha kabla ya wakati huo, na inafahamisha juu ya hilo pia kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yakealikuwa akirusha wakati wa kupondoka kwa jua kabla hajaswali adhuhuri (Ameipokea Muslim (1291).

Na hii pia ni dalili kuwa haifai kurusha kabla ya zawali, kama si hivyo ingelikuwa kabla ya zawali ni bora ili aswali swala ya adhuhuri katika mwanzo mwa wakati wake; kwa sababu swala mwanzo mwa wakati wake ni bora.

**Tulicho kipata**: Ni kuwa dalili zinaonesha kuwa kurusha katika siku za tashriiki haifai kabla ya zawali.

****

## Swali la 525: Mtu amepatwa na maradhi siku ya Arafa ikawa hakulala Mina na hakurusha mawe na hakutufu Twawaaful Ifaadhwa anatakiwa afanye nini?

**Jibu:** Itakapo kuwa Mtu huyu ambaye ameugua siku ya Arafa maradhi ambayo hawezi kukamilisha Ibada kwa sababu ya maradhi hayo, na alikuwa ameweka sharti mwanzo mwa Ihramu yake: ((Ikiwa nitazuiliwa na chenye kunizuiya basi kuhalalika kwangu ni hapo nilipo zuiliwa)) hakika atahalalika na wala hatolazimika kitu chochote, lakini ikiwa hiyo ni Hijjah yake ya faradhi hakika atatakiwa kuja kuhiji tena mwaka mwingine, ikiwa alikuwa hajaweka

sharti, hakika yeye pindi atakapo kuwa hakuweza kukamilisha Hijjah  yake anaweza kuhalalika lakini ni waJibu kwake kuchinja mnyama kwa maneno ya Allah aliposema: [**Na timizeni Hijjah na Umra kwa ajili ya Allah na ikiwa mkizuiwa basi (chinjeni) wanyama walio wepesi kupatikana**]. (Suratul Baqara: 196), na maneno ya Allah aliposema: [ **ikiwa mtazuiwa**] iliyo sahihi: Hakika hiyo inakusanya kuzuiwa na au kwa kitu chochote kingine.

Na maana ya kuzuiwa: Ni maadui kumzuiwa  muisilamu kukamilisha Ibada yake ya Hijjah.

Na kwa sababu hiyo atajihalalisha kisha atachinja mnyama, na wala hana kitu kingine তপেপুবগতজপ্র hicho, isipokuwa kama alikuwa hajatekeleza Hijjah  ya faradhi basi atatakiwa kuja kuhiji mwaka unao fuata.

Ama ikiwa huyu mgonjwa ameendelea katika Hijjah yake mpaka akasimama Muzdalifa lakini hakulala Mina, na hakurusha mawe hakika katika hali hiyo itakuwa Hijjah  yake ni sahihi lakini itamlazimu kuchinja mnyama kwa kila wajibu alio acha, kwa huyu itamlazimu kuchinja wanyama wawili mmoja kwa ajili kuto kulala Mina na wapili kwa ajili ya kuto kurusha mawe.

Na ama Twawaaful Ifadhwa itabaki na atatufu Allah atakapo mponyesha; kwa sababu Twawaaful Ifadhwa mwisho wake kwa kauli yenye  nguvu ni mwisho wa mwezi wa dhulhijjah  na ikiwa ni kwa udhuru basi mpaka uishe udhuru wake.

****

**Swali la 526: Mwenye kulala nje ya Muzdalifa kwa kutokujua mipaka yake atalazimika kufanya nini?**

**Jibu:** Kwa muJibu wa wanachuoni Allah awarehemu inamuwajibikia kuchinja mbuzi kisha aigawe kwa mafukara wa Makkah; kwasababu ameacha waJibu katika waJibu Hijjah.

Na kwa munasaba huu ninataka kuwa kuwambusha ndungu zangu Mahujaji wawe makini na mipaka ya sehemu za Ibada kama Arafa na Muzdalifa, hakika watu wengi pale Arafa huwa wanakaa nje ya mipaka yake, na wanabaki huko huko nje mpaka jua linazama, kisha wanaondoka hali ya kuwa hawajaingia Arafa, na hawa wote wanapo ondoka bila kuingia Arafa hakika huondoka bila Hijjah, kwa hiyo inampasa kila mmoja kuchunga mipaka ya Arafa na kuijua ili asikae nje mipika hiyo.

****

**Swali la 527: Mtu aliye hiji Hijjah ya Ifradi na akafanya Saayi baada ya Twawaaful Quduum, je itatakiwa kufanya tena Saayi baada ya Twawaful Ifaadhwa?**

**Jibu:** Hanatena Saayi baada ya Twawaful Ifaadhwa, mtu alio fanya Hijjah ya Ifradi pindi atakapotufu Twawaaful Quduum na akafanya Saayi baada ya Twawaaful Quduum, hakika hii Saayi ndio Saayi ya Hijjah hatakiwi kuirudia tema mara nyingine baada ya Twawaaful Ifaadhwa.

****

**Swali la 528: Je inatosha Twawaafu moja na Saayi moja kwa mtu mwenye kufanya Hijjah ya Qirani?**

**Jibu:** Pindi atakapo hiji Mtu Hijjah ya Qirani hakika yeye inamtosha Twawafu ya Hijjah na Saayi ya Hijjah na Umrah kwa pamoja, na inakuwa Twawaaful Quduum Sunna, kama atataka atatanguliza Saayi baada ya Twawaaful Quduum kama alivyo fanya Mtume rehma na amani ziwe juu yakena akitaka ataicheleweshampaka siku ya Idd baada ya Twawaafil Ifadhwa, lakini kutanguliza kwake ni bora; kwa ajili ndivyo alivyo fanya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, itakapo fika siku ya Idd hakika yeye atatufu Twawaaful Ifaadhwa tu, na wala hatafanya Saayi kwasababu yeye ameshafanya Saayi kabla ya hapo, na dalili ya kuwa Twawafu na Saayi zinatosha kwa Umrah na Hijjah ni maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake kwa Aisha Radhi za Allah ziwe juu yake alikuwa amefanya Hijjah ya Qirani: ((**Twawafu yako katika nyumba na Swafa na Marua zina kutosha kwa Hijjah yako na Umrah yako**)) (Ameipokea Abu Daud(18970); amebainisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa Twawafu ya mwenye kufanya Hijjah ya Qirani na Saayi yake vinamtosha kwa Hijjah yake na Umrah yake.

****

**Swali la 529: Ni ipi hukumu ya Mtu aliyelala Mina mpaka saa sita usiku kisha akaondoka kwenda Makkah na hakurudi mpaka alfajiri ikachomoza?**

**Jibu:** Ikiwa ni saa sita usiku ni kati kati ya usiku hakuna ubaya kutoka, japo kuwa kilicho bora ni kubaki Mina mchana na usiku,

na iwapo itakuwa saa sita ya usiku ni kabla ya kati kati ya usiku basi asitoke; kwa sababu kulala Mina inatakiwa iwe ndio kiasi kikubwa kwa usiku kwa muJibu walivyo tutajia wanachuoni wetu Allah awarehemu.

****

**Swali la 530: Mtu mwenye kuhiji atakapo toka Mina kabla ya kuzama jua siku ya tarehe kumi na mbili kwa niya kuwa anataka Kufanya haraka lakini ana baadhi ya kazi Mina atarudi baada ya kuzama jua je itazingatiwa kuwa amefanya haraka?**

**JIBU:** Ndio; atazingatiwa kuwa amefanya haraka; kwasababu amesha maliza Hijjah, na niya ya kurudi kwake Mina kwa ajili ya kazi haimzuii kufanya haraka; kwa sababu amenuiya kurudi kwa kazi ambayo ameifuata na sio kwa ajili ya Ibada.

****

**Swali la 531: Mtu amekuja kufanya Hijjah kutoka nje ya Saudia, na muda wa safari yake ya kurudi katika nchi yake ni saa kumi jioni ya tarehe kumi na tatu katika mwezi wa Dhul Hijjah, na hakutoka Mina baada ya kurusha mawe tarehe kumi na mbili ikamlazimu kulala usiku wa tarehe kumi na tatu, je inafaa kwake kurusha asubuhi kisha aondoke, ijulikane kuwa kama ata chelewa mpaka zawali safari itampita na yatampata matatizo makubwa! Pindi itakapo kuwa jibu ni haifai; Na vipi rai ya wanazuoni ambayo imeruhusu kurusha kabla ya zawali? Tupeni faida Allah akulipeni kila la kheri na Waislamu wote kwa ujumla.**

**Jibu:** Haifai kurusha kabla ya zawali, lakini anaweza kuacha kurusha katika hali hiyo kwa dharura, na tunasema kumuambia: Itakulazimu kutoa fidia ambayo utaichinja ukiwa Mina au Makkah, au uweke Mtu wa kumuwakilisha katika kuchinja, na kuigawa kwa mafukara, kisha anatufu Twawafu ya kuagana kwenda zake.

✳**Na tunasema**: Ama maneno yako: (( Pindi itakapo kuwa Jibu ni haifai; si kuna rai ya wanazuoni ambayo imeruhusu kurusha kabla ya zawali))

**Jibu:** Ndio kuna rai inayo ruhusu kurusha kabla ya zawali, lakini siyo sahihi, na iliyo sahihi: kurusha mawe kabla ya zawali katika masiku ya baada ya Iddi haifai, na hilo ni kwa kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema: ((**Chukueni kutoka kwangu Ibada zenu**)) (umetangulia upokezi wake), na hakurusha Mtume rehma na amani ziwe juu yakekatika siku hizi isipokuwa

baada ya zawali.

***Iwapo atasema mwenye kusema**: Kurusha kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake baada ya zawali ni kitendo tu na kitendo tu hakioneshi jambo kuwa ni la wajibu.

***Tunasema**: Hilo ni sahihi kuwa ni kitendo tu, na kitendo tu hakioneshe jambo kwa ni la lazima; ama kule kuonesha ni kitendo ni kwa kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alirusha baada ya zawali, na hakuamrisha kuwe kurusha ni baada ya zawali, na wala hakukataza kurusha baada ya zawali, na ama kule kuwa kitendo hakioneshi kuwa ni waaJibu ni kwa sababu uwajibu hauwi isipokuwa kwa kuamrisha kufanya au kukataza kuacha.

**Lakini tunasema**: Kitendo hicho kina ishara zinaonesha kuwa ni waJibu nazo ni kama ifuatavyo**:**

1-Kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake amechelewesha kurusha mpaka jua lilipo pinduka kunaonesha juu ya uwajibu wake, kwa sababu lau kama ingekuwa kurusha kabla ya zawali kunafaa Mtume rehma na amani ziwe juu yake angalifanya hivyo; kwa sababu kurusha muda huo kuna wepesi kwa watu na Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakukhiyarishwa katika mambo mawili isipokuwa alichagua jambo jepesi muda wa kuwa halina dhambi, kule kuwa kwake hakuchagua jepesi hapa nalo ni kurusha kabla zawali inaonesha kuwa kurusha kabla kuna madhambi.

2-Miongoni mwa vitu vinavyo onyesha kuwa kitendo hiki ni cha waajibu ni kule kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alirusha kwa haraka mara tu baada ya kupondoka kwa jua kabla hajaswali adhuhuri, na akachelewesha adhuhuri kwa sababu ya

kurusha pamoja na kuwa bora ni kuitanguliza swala mwanzo mwa wakati wake, lakini alifanya hivyo ili arushe baada ya zawali.

****

**Swali la 532: Mtu ameacha kurusha mawe tarehe kumi na mbili akidhani kuwa ndio siku ya Kufanya haraka na akaondoka hakutufu Twawaafu ya kuaga, ni ipi hukumu ya Hijjah yake?**

**Jibu:** Hijjah yake ni sahihi; kwa sababu hakuacha nguzo katika nguzo za Hijjah, lakini ameacha mambo matatu ya lazima ikiwa hajalala Mina usiku wa tarehe kumi na mbili.

**Jambo la kwanza**: Kulala Mina usiku wa tarehe kumi na mbili.

**Jambo la pili:** Kurusha mawe katika siku ya tarehe kumi na mbili.

**Jambo latatu**: Twawafu ya kuaga.

Inamlazimu kwa kila jambo mmoja alilo acha katika hayo matatu achinje mnyama akiwa Makkah na aigawe nyama yake kwa mafukara wa Makkah; kwa sababu mwenye kuacha waajibu katika Hijjah kwa mujibu wa wanachuoni inampasa kuchinja mnyama na agawe nyama yake kwa mafukara wa Makkah.

Na kwa mnasaba huu ninapenda kuwakumbusha ndugu zangu

mahujaji katika kosa hili ambalo amelifanya muulizaji kwani wengi katika mahujaji wanafahamu kama alivyo fahamu huyu; wanafahamu kuwa maana ya maneno yake Allah aliposema: [**Mwenye kufanya haraka katika masiku mawili hapana dhambi juu yake**],

yani: Hutoka tarehe kumi na moja wakidhani siku mbili ni siku ya Idd na tarehe kumi na moja, hali ya kuwa jambo lenyewe haliko hivyo bali amefahamu kimakosa; kwa sababu Allah amesema: [**Na mtajeni Allah katika zile siku zinazo hisabiwa. Lakini mwenye kufanya haraka katika siku mbili si dhambi juu yake**] (Suratul Baqara: 203), na masiku yanayo hisabiwa ni masiku ya Tashriiki, na masiku ya Tashriiki mwanzo wake ni tarehe kumi na moja, kwa sababu hiyo Maneno yake Allah: [**Mwenye kufanya haraka katika siku mbili**], yani katika zile siku za Tashriiki nayo ni siku ya kumi na mbili, kwa hiyo inatakiwa kwa kila Muislam kusahihisha uelewa wake katika mas-ala haya ili asikosee.

****

**Swali la 533: Kwa Mtu ambae hakupata sehemu ya kukaa pale Mina akawa anakuja usiku tu kisha anabaki hapo mpaka baada ya nusu ya usiku, kisha anarudi Makkah katika muda uliyo baki ni ipi hukumu yake?**

**Jibu:** Hukumu katika hili ni kuwa kitendo hicho kina mtoshelezea, lakini kitu ambacho kinatakiwa ni kinyume na hich; kwasababu kinacho takiwa kwa mwenye kuhiji ni kubaki Mina mchana

na usiku katika masiku ya Tashriiki, atakapo kosa sehemu atakaa pale walipo ishia watu ambao wapo kwenye mahema hata kama ni nje na Mina kama akikosa sehemu, pindi atakapo tafuta na akako sehemu Mina, hakika wamekwenda baadhi ya wanachuoni katika zama zetu hizi kuwa akikosa sehemu ya kukaa Mina basi haitakua lazima kwake, na inafaa kwake kulala sehemu yeyote katika mji wa Makkah, na kipimo chake katika hilo ni kama mtu aliye kosa kiungo katika viungo vyake vya udhu basi unaondoka ulazima wa kuosha kiungo hicho kwasababu hanacho, lakini katika hili kuna mtizamo kidogo; kwa sababu kiungo hukumu ya twahara imefungamana nacho na hakikupatikana; ama katika hili hakika makusudio ya kulala ni wawe watu ni wenye kukusanyika pamoja kama vile Umma mmoja, kitu cha waaJibu ni awe mtu huyu mwisho wa mahema ili awe pamoja na mahujaji, na mfano wa hilo: Msikiti ukijaa wakawa watu wanaswali pembezoni mwa msikiti hakuna budi lazima swafu ziungane ili iwe jamaa ni moja, na kulala Mina ni mfano huo huo na sio mfano wa kiungo cha udhu kilicho katwa au kukosekana.

****

**Swali la 534: Mtu ametufu Twawaafu ya ya kuaga asubuhi kisha akalala na akataka kusafiri baada ya Alasiri je itamlazimu kitu chochote?**

**Jibu:** Ni juu yake kurudia Twawaafu ya kuagakatika Umrah na Hijjah; kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema: ((**Asiondoke mmoja wenu mpaka iwe katika nyumba ndio sehemu yake ya mwisho**)) (Ameipokea Muslim (963); aliyasema hayo katika Hijjah tul Wadaa ukaanza uwaJibu wa Twawafu ya kuaga katika wakati huo, haikupokewa kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake alifanya Umra kabla ya hapo na wala haikupokelewa kuwa aliaga nyumba kwa sababu Twawafu ya kuaga hakika iliwajibiswa katika Hijjah Al-Wadaa, na akasema Mtume rehma na amani ziwe juu yake ((**Fanya katika Umra yako yale unayo yafanya katika Hijjah yako**)) (Ameipokea Bukhary (1789) na Muslim (1180), na ujumala huo uliokuja katika Hadithi huvuliwa ndani yake kusimama Arafa, kulala Mina, Muzdalifa, na kurusha mawe; kwa sababu matendo hayo ni maalumu kwa Hijjah kwa makubaliano ya wanachuoni na yanabaki yalio achwa katika huo ujumla, kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake ameiita Umra kuwa ni Hijjah ndogo, kama ilivyo katika hadithi ya Amru bin Hazimi (Imetangulia upokezi wake) hadithi ambayo ni mashuhuri wanazuoni wameipokea kwa kuikubali, nayo ni hadithi Mursali lakini ni sahihi wanachuoni wameikubali.

Na ni kwa sababu Allah amesema: [**Itimizeni Hijjah na Umra kwa ajili ya Allah**] Pindi itakapo kuwa twawafu ya kuagani katika kukamilisha Hijjah basi vile vile itakuwa ni katika kukamilisha Umrah.

Na ni kwa sababu huyu mtu aliingia katika msikiti mtukufu

kwa maamkizi haifai kutoka humo isipokuwa kwa maamkizi.

Na kwa sababu hiyo twawaafu ya kuaga inakuwa ni waaibu katika Umrah kama ilivyo wajibu katika Hijjah, na kuna Hadithi ameipokea Tirmidhy: (**Pindi atakapo hiji Mtu au akafanya Umrah basi asitoke mpaka iwe mwisho wa kutoka kwake ni katika nyumba**)) (Ameipokea Tirmidhi (946), na katika Hadithi hii kuna udhaifu; kwa sababu ni katika mapokezi ya Hajaji bin Aritwaati na lau kama sio udhaifu wa hadithi hii ingekuwa ni dalili ya kukata malumbano katika mas-ala haya, lakini kwa udhaifu wake haina nguvu katika kuitolea dalili, isipokuwa misingi ambayo tumeitaja huko nyuma inaonesha juu ya uwajibu wa twawaafu ya kuaga katika Umra. Kwasababu Mtu atakapo tufu twawaafu ya kuaga katika Umra atakuwa amejivua na kuulizwa;kwa sababu ukitufu Twawafu ya kuaga katika Umra hakuna atakae sema umekosea, lakini usipo tufa atatokea mwenye kuiwajibisha atakuambia umekosea, iwapo atatufu basi mwenye kutufu atakuwa amepatia kwa kila hali, na yule ambaye hatatufu hakika atakuwa katika makosa kwa kauli ya baadhi ya wanachuoni Allah awarehemu.

****

**Swali la 535: Ni ipi hukumu ya Twawaafu ya kuaga katika Umra?**

**Jibu:** Twawaafu ya kuaga kwa mwenye kufanya Umrah ikiwa katika niya yake wakati alipo kuja Makkah ni kutufu, kusaayi na kunyoa au kupunguza, na arudi zake basi atakuwa hana twawaafu

juu yake; kwa sababu Twawaaful Quduumu imekuwa kwake ni kama twawaafu ya kuaga, ama atakapo baki Makkah kauli yenye nguvu: Hakika ni waajibu kwake kutufu Twawafu ya kuaga, na hilo ni kwa dalili zifuatazo:

1-Ujumla wa maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake aliposema: ((**Asiondoke mmoja wenu mpaka iwe katika nyumba ndio sehemu yake ya mwisho**)) (Umetangulia upokezi wake).

2-Hakika Umrah ni kama Hijjah bali ameita Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni Hijjah kama ilivyo kuja katika Hadithi ya Amru bin Hazmi Hadithi ambayo Umma umeikubali amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((**Na Umrah ni Hijjah ndogo**)) (Umetangulia upokezi wake).

3-Hakika Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema: ((**Umra imeingia katika Hijjah mpaka siku ya Kiama** )) (Umetangulia upokezi wake ).

4-Hakika Mtume rehma na amani ziwe juu yake alisema kumuambia Yaalah bin Umayya Allah awe radhi naye: ((**Fanya katika Umrah yako yale unayo yafanya katika Hijjah yako**)), Ikiwa katika Hijjah yako unafanya Twawafu Ya kuagabasi ifanye katika Umrah yako, na wala hakitoki kitu katika hilo isipo kuwa kile ambacho wanachuoni wamekubaliana kuvitoa, kama: Kusimama Arafa, kulala Mina, Muzdalifa, na kurusha mawe, hakika hivyo vyote kwa makubaliano ya wanachuoni havifanywi katika Umra.

Na ni kwa sababu Mwanadamu atakapo tufu anakuwa amejiweka mbali na dhima , na Allah ndiye mwenye kuwafikisha.

****

**Swali la 536: Mtu amehirimia Hijjah Miiqati na alipofika Makkah akazuiliwa na askari kwasababu hana kibali kinacho mruhusu kufanya Hijjah ni ipi hukumu yake?**

**Jibu:** Hukumu katika hali hii anakuwa ni mwenye kuzuiliwa kuingia Makkah, atachinja mnyama katika sehemu aliyo zuiliwa na atakuwa amehalalika, kisha ikiwa hii ilikuwa ni Hijjah yake ya faradhi ataitekeleza muda mwingine kwa amri ya kwanza sio kwa kulipa, na iwapo itakuwa sio faradhi hakika atakuwa halazimiki kufanya chochote katika kauli yenye nguvu; kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakuwaamrisha wale ambao walizuiliwa katika vita vya Hudaibiya kulipa ile Umra, na hakuna katika Kitabu cha Allah wala Sunna za Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwajibishwa kulipa kwa yule ambaye amezuiliwa, amesema Allah: [**Na ikiwa mtazuiliwa basi (chinjeni ) walio wepesi kupatikana**] (Suratul Baqara: 196) na hakutaja kitu kingine kisicho kuwa hicho, na Umratu Al-Qadhwaau imeitwa hivyo kwa sababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake aliwaahidi Makuraishi sio kulipa katika kile ambacho ki me kupita, Allah ndiye mjuzi zaidi.

****

**Swali la 537: Mwenye kukusudia Hijjah kisha akazuiliwa, analazimika kufanya nini?**

**Jibu:** Ikiwa alikuwa hajanuiya halazimiki kitu chochote katika hali hiyo; kwa sababu Mtu atakapo kuwa hajanuiya akitaka anaendelea akitaka ana acha na kurudi kwa watu wake, isipokuwa ikiwa ni Hijjah ya faradhi inampasa kufanya haraka katika

kuitekeleza, lakini pindi atakapo zuiwa hakika kwa wakati huo atakuwa halazimiki na kitu chochote.

Ama ikiwa kuzuiwa huko ni baada ya kunuiya ikiwa aliweka sharti wakati wa kunuiya kwake kwa kusema ((Iwapo kitanizuiya chenye kunizuiya kuhalalika kwangu ni sehemu hiyo niliyo zuiliwa)); hakika hapo atajivua katika Ihramu yake na hatalazimika na kitu chochote,na iwapo alikuwa hajaweka sharti ikiwa inatarajiwa kile kizuizi kutoka katika muda mfupi basi atasubiri kiondoke kisha atamalizia Hijjah yake, ikiwa ni kabla ya kusimama Arafa atasimama Arafa kisha atakamilisha Hijjah yake, na iwapo itakuwa ni baada ya kusimama Arafa na hakusi mama hapo Arafa hakika atakuwa amepitwa na Hijjah, atahalalika kwa kufanya Umrah, na atailipa Hijjah hiyo mwaka unao fuata ikiwa ni Hijjah yake ya faradhi, na ikiwa hatarajii kizuizi kama kile kitaondoka kwa haraka atajihalalisha kutoka katika kuhirimia kwake, na atachinja mnyama, kwa maneno yake Allah alipo sema: [ **Itimizeni Hijjah na Umra kwa ajili ya Allah Na ikiwa mtazuiliwa basi (chinjeni)walio wepesi kupatikana**], (Suratul Baqara: 196).

****

## Swali la 538: Je! Maasi anayo yafanya Mtu mwenye kuhiji yanapunguza thawabu za Hijjah?

**Jibu:** Maasi kiujumla yanapunguza thawabu za Hijjah kwa maneno ya Allah alipo sema: [**Na anaye kusudia kufanya Hijjah katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hijjah**] (Suratul Baqara: 197), bali baadhi ya wanachuoni Allah awarehemu wamesema:

Hakika maasia katika Hijjah yana iharibu Hijjah; kwa sababu yamekatazwa katika Hijjah, lakini Jamhuri ya wanachuoni katika msingi wao unao julikana wanasema: Hakika uharamu pindi utakapo kuwa sio maalumu kwa Ibada hakika uharamu huo hauibatwilishi hiyo Ibada, na kufanya maasi sio maalumu kwa mwenye kuhirimia, na hii ndio ya sawa, kuwa haya maasi hayabatilishi Hijjah, lakini hupunguza malipo yake.

****

**Swali la 539: Mwenye kuhiji kwa paspoti ya kudanganya (ambayo sio sahihi ) ni ipi hukumu ya Hijjah yake?**

**Jibu:** Hijjah yake ni sahihi; kwasababu kudanganya katika paspoti yake hakuathiri katika kuswihi Hijjah yake, lakina atapata madhambi, na ni juu yake kutubia kwa Allah na arekebishe jina hilo kwenda kwenye jina sahihi ili isitokee kuwa anawachezea viongozi, na asikose baadhi ya haki zake za msingi kwa kuacha jina lake halisi kwa kutofautiana jina la kwanza na la pili, akawa kwa sababu hiyo ni mwenye kula mali za watu kwa njia ya baatwili kwa uongo alio utumia kwenye kubadili jina lake.

Na kwa munasaba huu napenda niwanasihi ndugu zangu kuwa jambo sio jepesi kwa wale ambao wanabadili majina, na wanachukua majina ya watu wengine kwa sababu ya kupata misaada selikalini, au katika mambo mengine , hakika huko ni kucheza katika mahusiano, na ni uongo na udanganyifu, na ni kuwadanganya viongozi wa selikali, na ajue kuwa mwenye kumcha Allah atapata sehemu ya kutokea, na ataruzukiwa sehemu ambayo hakuidhania, na mwenye kumcha Allah Allah hufanya mambo yake kuwa mepesi, na mwenye kumcha Allah na akasema maneno ya sawa

Allah humtengenezea mambo yake na humsamehe madhambi yake .

****

Kimekamilika shukran zote kwa Allah tabaraka wataalah.

YALIYOMO

UTANGULIZI..........................................................................1

MASWALI NA MAJIBU KUHUSU TAUHIDI........................................2

Vigawanyo vya Tauhidi...........................................................................2

SWALI LA 2: Ni Shirki ipi ambayo Washirikina waliifanya mpaka aka-

tumwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake ?.........................................
...........................9

SWALI LA 3: Ni ipi misingi ya Ahalu Sunnahh Walja-
maa katika Tauhidi na mambo mengine katika mambo ya
Dini?.......................................................11

SWALI LA 4: Ni kina nani hao Ahalu Sunnahh Walja-
maa?...............................12

SWALI LA 5: Ametuhabarisha Mtume rehma na am-
ani ziwe ju yake! juu ya kutofautiana Umma wake baada
ya kufa kwake,tuna kuomba Sheikh utubainishie jambo hili
...............................................................................12

SWALI LA 6: Niyapi mambo muhimu na maalumu ka-
tika kundi hili lenye kuokoka? Na je kupungua kitu ka-
tika hayo mambo kunamtoa mtu katika hilo kun-
di?...............................................................................................14

SWALI LA 7: Ni nini makusudia ya Ukati katika Dini?..............................17

SWALI LA 8: Ni ipi Taarifu ya Imani kwa Ahlu Sunnahh Waljamaa? Na je inazidi na kupungua?...................................................................................................19

SWALI LA 9: Ni vipi tutazikusanya kati ya Hadithi ya Jibrili ambayo ambayo Mtume rehma na amani ziwe juu yake: alitafsiri Imani kuwa ni (( Kumuamini Mwenyezi Mungu,na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake, na siku ya mwisho,na kuamini Qadar zake kheri zake na Shari zake)) [ Apokea Muslimu /8 / na Hadithi ya ujumbe wa Abdul-Qaisi ambayo Mtume rehma na amani ziwe juu yake: alitafsiri Imani kuwa ni ((Kushuhudia ya kuwa hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu aliye Mmoja hana Mshirika,na kusimamisha Swala, na kutoa Zaka,na kutoa tano ya Ghanima)) [Ameipokea Bukhari /53/na Muslimu/17/]..........................................................................21

SWALI LA 10: Ni vipi tutakusanya baina ya Imani ni Kumuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake,na siku ya mwisho kheri zake na shari zake na maneno yake Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((Imani ni mafungu zaidi ya sabiini)) [Ameipokea Bukhar /9/ na Muslim / 35/]...23

SWALI LA 11: Je tunaweza kumshuhudilia Mtu kuwa ana Imani kwa kuzoeya kwake Msikiti kama ilivyo kuja kwenye Hadithi?..................................24

SWALI LA 12: Mtu anatiwa wasiwasi na Sheitani, wasiwasi mkumbwa kuhusu Mwenyezi Mungu, na yeye anaogopa sana juu ya hilo, Mnamuusia nini Mtu huyu?........................................................................................................................24

SWALI LA 13: Je ni lazima kwa Kafiri kuingia katika Uislam?....................27

SWALI LA 14: Nini hukumu ya mwenye kudai kuwa anajua mambo yaliyo ghaibu (yalio jificha?.........................................................................................28

SWALI LA 15: Tutayaowanisha vipi maneno ya Madaktar wa sasa,wanao tutajia aina ya mtoto Wakike au Wakiume na maneno yake Mwenyezi Mungu alipo sema: [ Yeye ndie ajuaye yaliyo katika matumbo] na iliyo kuja katika tafsiri ya Ibnu Jariri kutoka kwa Mujahid, kuwa Mtu mmoja alimuliza mtume wa Mwenyezi Mungu, ni nini atazaa mke wake, akateremsha Mwenyezi Mungu Aya hii, na ile ilopokelewa kutoka kwa Katada? Ni kitu gani kinaifanya Umumi katika aya hiyo kwa Khaswa?..........................................................................29

SWALI LA 16: Je jua huzunguka katika Ardhi?......................................31

SWALI LA 17.Aliulizwa Sheikh Mwenyezi Mungu amrehemu: kuhusu Shahada mbili?..................................................................................34

SWALI LA 18: Ni vipi imekuwa (Hapana Mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu)imekusanya aina zote za Tauhidi?................................37

SWALI LA 19: Ni ipi hekma ya kuumbwa Mjini na Watu?.......................37

SWALI LA 20: Ni kwanini Mwanadamu anaomba dua na wala hajibiwi na Mwenyezi Mungu anasema: [Niombeni nami nitawaJibu]?........................38

SWALI LA 21: Nini maana ya Ikhlas? Na atakapo taka mja kufanya Ibada kwa kitu kingine ni nini hukumu ya yake?.................................................41

SWALI LA 22: Ni upi mwenendo wa Ahalu Sunnah Waljamaa, katika kutaraji na kukho-

fu?.......................................................................................................................44

SWALI LA 23: Je kufanya sababu kunapingana na kumtegemea Mwenyezi Mungu? kuna baadhi ya Watu wakati wa vita vya Khaliji walijitengenezea sababu za kujikinga wasidhurike na wengine wakaacha na wakasema: Hakika wao ni wenye kumtegemea Mwenyezi Mungu.................................................45

SWALI LA 24: Ni nini hukumu ya kujiegemeza katika sababu?.........................46

SWALI LA 25: Ni ipi hukumu ya Ruqiyyah? na ni ipi hukumu ya kuandika maandishi ya Aya katika shingo ya Mgonjwa?.................................................48

SWALI LA 26: Je Ruqiyyah vinapingana na (Tawakal) kumtegemea Mwenyezi Mungu?..............................................................................49

SWALI LA 27: Ni ipi hukumu ya kutundika au kuvaa Hirizi na vizuizi (Vikuku)?.....................................................................................................49

SWALI LA 28: Je inafaa kuandika baadhi ya Aya katika Qur'an Tukufu, Mfano Aya Kursiy katika chom-

bo cha chakula aa kinywaji kwa lengo la kujitibu kwa yo?....................................................................................................50

SWALI LA 29: Wanajifunza wanafunzi wa Madrasa katika baadhi ya Miji ya Kiislam, kuwa Msimamo wa Ahlu Sunnahh Waljamaa ni (( Kuamini Majina yake, na Sifa zake, bila Kugeuza wala Kuziacha, wala kuziwekea namna, wala Kuzifananisha)). Je kugawanya Ahalu Sunnahh katika vigawanyo viwili: Madrasa ya Ibnu Taymiya na Wanafunzi wake, na Madirasa ya Al-Ashaira na Al-Maturudia vigawanyo hivi ni sahihi?. Na ni upi msimamo wa Muislam kwa Wanazuoni wenye kufanya Taawili?..........................................................................................51

SWALI LA 30: Ni ipi Aqida ya Ahlu Sunnahh katika majina ya Mwenyezi Mungu na Sifa zake? Na ni nini tofauti kati ya jina na sifa? Je inalazimu mwenye kuthibitisha jina athibitishe sifa yake? Na mwenye kuthibitisha sifa athibitishe jina?..............................................................................
.....57

SWALI LA 31: Je majina ya Mwenyezi Mungu ni yenye kuhesabika?............58

SWALI LA 32: Ni yapi Madhehebu ya wema walio tangulia, Mwe-

nyezi Mungu awarehemu,katika kuwa juu kwa Mwenyezi Mungu? Na ipi hukumu ya mwenye kusema: Mwenyezi Mungu yupo katika pande sita, na kuwa Yeye yupo katika moyo wa Muumin?.........................................................................60

SWALI LA 33: Hivi tafsiri ya kulingana sawa kwa Mwenyezi Mungu katika kiti Chake cha Enzi, kuwa ni kuwa Kwake juu ya kiti Chake cha Enzi, kwa vile inavyo lingana na utukufu wake, hiyo ni tafsiri ya wema walio tangulia?.........................66

SWALI LA 34: Fadhilatu Sheikh: Umesema Mwenyezi Mungu akuhifadhini, kulingana kwa Mwenyezi Mungu katika kiti chake cha Enzi kuwa ((Ni kulingana kwa Mwenyezi Mungu juu ya kiti chake cha Enzi kunako lingana na utukufu wake na ukubwa wake)), tunakuomba kwa ukarimu wenu kuliweka wazi zaidi suala hilo?...................................................................................................................67

SWALI LA 35: Ni mambo gani ambayo ni lazima kuyaegemeza kwenye matakwa ya Mwenyezi Mungu, na ni mambo gani ambayo haifai kuyaegemeza kwenye matakwa ya Mwenyezi Mungu?..........................................................................69

SWALI LA 36: Ni vipi vigawanyo vya kutaka (Al-iraa-
dat)?..............................70

SWALI LA 37: Ni ipi Ilhadi (upingaji) katika majina ya Mwenyezi Mungu,na
ni zipi aina zake?.......................................................................71

SWALI LA 38: Ni vipi vigawanyo katika vitu alivyo viege-
meza Mwenyezi Mungu kwake mfano: Uso wa Mwenyezi
Mungu, Mkono wa Mwenyezi Mungu, na mengine mfano wa
haya...........................................................73

SWALI LA 39: Ni ipi hukumu ya kupinga kitu katika majina ya Mwenyezi
Mungu au sifa sifa Zake?.........................................................................
....74

SWALI LA 40: Ni ipi hukumu kwa mwenye kuita-
kidi kuwa sifa za Muumba ni kama sifa za Vi-
umbe?......................................................................................75

SWALI LA 41: Ni kitu kinajulikana kuwa usiku huzunguka katika tufe la ar-
dhi, Mwenyezi Mungu hushuka katika uwingu wa Dunia inapobaki thelu-

thi ya mwisho ya usiku, hilo linaonesha kuwa usiku mzima huwa katika uwingu wa Dunia, ni lipi Jibu juu ya hilo?.................................................................................................75

SWALI LA 42:Ni upi msimamo wa wema walio tangulia katika kuonekana kwa Mwenyezi Mungu?na ni ipi hukumu kwa mwenye kudai kuwa (( Hakika Mwenyezi Mungu haonekani kwa macho, na kuwa kuonekani kwake ni jambo la ukamilifu wa kuwepo kwake))?......................................................................77

SWALI LA 43: Je Majini yana athari kwa Mwanadamu? Na ni ipi njia ya kujikinga nao?............................................................................78

SWALI LA 44: Je Majini wanajua mambo ya ghaibu (ya siri)?...........................79

SWALI LA 45: Ni ipi huku ya mwenye kumsifu Mtume rehma na amani ziwe juu yake kuwa ni habibullah? Mwenye kupendwa na Mwenyezi Mungu............ ...80

SWALI LA 46: Ni ipi hukumu ya kufanya kumsi-

fu Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni biashara?...........................................................................................81

SWALI LA 47: Mwenye kuitakidi kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni nuru katika nuru za Mwenyezi Mungu na si Mwanadamu, na kuwa anajua mambo ya ghaibu, kisha anajikinga kwa Mtumerehma na amani ziwe juu yake hali ya kuwa anaitakidi kuwa anamiliki manufaa na madhara, ni ipi humu ya hilo? Na je inafaa kuswali nyuma ya mtu huyu au ambaye anafanana naye? Tupeni faida katika hilo Mwenyezi Mungu akulipeni kila la kheri.................................................82

SWALI LA 48: Je Hadithi za kutoka Al-Maahadi ni sahihi au sio sahihi?.......... 83

SWALI LA 49: Ni nani hao kina Maajuja na Maajuja?.............................84

SWALI LA 50: Kwanini Mitume waliwatahadharisha watu wao na Dajali pamoja ya kuwa hatotoka isipokuwa katika zama za mwisho?................................85

SWALI LA 51: Ni ipi huku ya mwenye kukataa maisha ya kesho Akhera, na akadai kuwa huo ni uzushi wa zama za kati? Ni vipi tunaweza kuwakinahisha wapingaji hawa?.........................................................................

.........................86

SWALI LA 52: Je adhabu ya kaburi imethibiti?.......................................89

SWALI LA 53: Pindi atakapo kuwa Maiti haijazikwa imeliwa na mnyama au imepukutika ikachukuliwa na upope. Je ataadhibiwa adhabu za kaburi?...............90

SWALI LA 54: Ni vipi tutamJibu mwenye kupinga adhabu ya kaburi na anatoa hoja kuwa lau kama tutalifukuwa kaburi tutalikuta halikubadilika na wala halikubana wala kutanuka?..........................................................................90

SWALI LA 55: Je hupunguzwa adhabu ya kaburi kwa Muumini ambaye ni mwenye kuasi?..................................................................................................91

SWALI LA 56: Ni nini Shafaa? Na ni vipi vigawanyo vyake?......................93

SWALI LA 57: Ni yapi mafikio ya watoto wa Waumini na watoto wa Washirikina wale ambao wamekufa wakiwa wadogo?..........................................96

SWALI LA 58: Imetajwa kuwa Wanaume watakuwa na Mahuru Al-aini Peponi je Wanawake nao watakuwa nao?........................................................96

SWALI LA 59: Je yanayo tajwa kuwa wengi katika Watu wa motoni ni Wanawake ni kweli? Na ni kwanini?..........................................................97

SWALI LA 60: Ni upi muongozo wenu kwa asiyetaka kusoma Aqida hasahasa mambo ya Qadari kwa kuogopa kuwa watateleza?................................................98

SWALI LA 61: Tunatarajia kwa fadhila zenu utuwekee wazi mas-ala ya Qadar?Je asili ya kitendo chenyewe kimesha kadiriwa ile namna ya kufanya ndiyo anayo ichagua Mwanadamu? Mfano wa hilo: Pindi Mwenyezi Mungu anapo mkadiria mja wake ajenge Msikiti hakika hakuna budi atajenga lakini amemuachia katika akili yake ichague namna ya kujenga, na hivyo hivyo katika maasi Mwenyezi Mungu atakapo mkadiria Mtu atafanya hakuna namna ya kukwepa, lakini amemuachia katika akili yake namna ya kuyafanya, na ufupisho wa rai hii ni kuwa Mwan-

adamu anachagua namna ya kulifanya lile alilo kadiriwa na Mwenyezi Mungu, Je hiyo ni sahihi?...100

SWALI LA 62: Je dua ina athari yoyote katika kubadilisha yale aloandikiwa Mwanadamu kabla ya kuumbwa kwa ke?........................................................103

SWALI LA 63: Je riziki na kuowa navyo vimeandikwa katika Lauhil Mahfudhi?..................................................................................................104

SWALI LA 64: Ni ipi hukumu ya mwenye kukasirika na kuchukia pindi anapofikwa na matatizo?...........................................................106

SWALI LA 65: Sheikh: Tunaomba kwa fadhila zako utuwekee wazi maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: ((Hakuna Ghaduwa( maambukizi), wala Twiyara (kutiana mkosi)wala Al-Hammatu(ndege mwenye mkosi), wala Swafar (mwezi wa swafar kuwa una mkosi)) [Ameipokea Bukhari/5757/ na Muslimu/2220/ ]. Ni aina gani ya kukataza ilokuja katika hadithi hii?na tutaichukuaje Hadithi hii pamoja na ile inayo sema: ((Mkimbie mtu mwenye mbalanga kama unavyo mkimbia simba))? [Ameipokea Bukhari /5707.........107

SWALI LA 66: Je kijicho kinaweza kumpata mtu? Na kikimpata kinatibiwa kwa namna gani?na je kujikinga nacho kunapingana na kumtegemea Mwenyezi Mungu?....................................................................................................111

SWALI LA 67: Je anahesabika kuwa ana udhuru mtu ambaye hajui mambo ya Aqida?..................................................................................112

SWALI LA 68: Ni ipi hukumu ya mwenye kuhukumu kwa kitu ambacho Mwenyezi Mungu hakukiteremsha?..............................................................121

SWALI LA 69: Ni ipi hukumu ya kuchinja kwa kujikurubisha kwa asiokuwa Mwenyezi Mungu? Na je inafaa kula kichinjwa hiki?..............................125

SWALI LA 70: Nini hukumu ya mwenye kufanya mzaha kwa maneno ambayo ndani yake kuna istihizai kwa Mwenyezi Mungu au Mtume rehma na amani ziwe juu yake au Dini?.........................................................................126

SWALI LA 71: Ni ipi hukumu ya kuwaomba walioko ndani ya makaburi?......127

SWALI LA 72: Mtu anataka msaada kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu, Anadai kuwa (ni walii wa Mwenyezi Mungu) ni zipi alama za mawalii wa Mwenyezi Mungu?........................................................................................128

SWALI LA 73: Ni nini uchawi na ni ipi hukumu ya kujifundisha?...............130

SWALI LA 74: Ni ipi hukumu ya kuwapatanisha mme na mke kwa uchawi?... 130

SWALI LA 75: Ukuhani ni nini?na ni ipi hukumu ya mwenye kumwendea kuhani?........................................................................................131

SWALI LA 76: Ni ipi hukumu ya Ibada itakapo kuwa imechanganyika na Ria (kujionesha)?........................................................................................133

SWALI LA 77:Ni ipi hukumu ya kuapa kwa msahafu?............................134

SWALI LA 78: Ni ipi hukumu ya kuapa kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake na kwa Al-Kaaba? Na kwa utukufu na dhima? Na maneno ya mtu kuapa kwa kusema: (Kwa dhima yangu)?....................................................137

SWALI LA 79: Ni ipi hukumu ya mwenye kuabudu makaburi kwa kuyatufu pembeni yake na kuwaomba walio katika makaburi hayo na kuwawekea nadhiri, na mambo mengine yasio kuwa hayo katika aina za ibada?...............................137

SWALI LA 80: TutawaJibu vipi wenye kuabudu makaburi ambao hutolea Ushahidi kuwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake amezikwa msikitini na watu wanaswali pale katika ule msikiti huko sio kuabudu kaburi?......................141

SWALI LA 81: Ni ipi hukumu ya kujengea makaburi?...................................142

SWALI LA 82: Ni ipi hukumu ya kuzika maiti msikitini?........................142

SWALI LA 83: Ni ipi hukumu ya kusafiri kwa ajili ya kuzuru kaburi la

Mtume rehma na amani ziwe juu yake?.......................................................................143

SWALI LA 84: Ni ipi hukumu ya kutaka Baraka kwenye makaburi na kuyazunguuka kwa makusudio ya kukidhiwa haja au kujikurubisha na ni ipi hukumu ya kuapa kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu?..............................144

SWALI LA 85: Ni ipi hukumu ya kuvaa nguo ambayo ina picha ya Mnyama au Mwanadamu?........................................................................146

SWALI LA 86: Ni ipi hukumu ya kutundika picha katika ukuta?.................146

SWALI LA 87: Ni ipi kuhumu ya kupiga picha kwa kutumia kamera za haraka?..........................................................................147

SWALI LA 88: Ni vipi tutawaJibu watu wa bidaa wanao toa Ushahidi katika bidaa zao kwa Hadithi: ((Mwenye kuanzisha katika Uislamu Sunnahh nzuri...)) [Ameipokea Muslimu /1017/]..........................................................147

SWALI LA 89: Ni ipi hukumu ya kusheherekea Maulid ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake?.........................................................................148

SWALI LA 90: Ni ipi hukumu ya kusherekea ile wanayo ita Sikukuu ya Mama?..........................................................................................................150

SWALI LA 91: Ni ipi hukumu ya kusherekea Sikukuu ya kuzaliwa watoto au Sikukuu ya kuowana?...........................................................152

SWALI LA 92: Mtu ameishi katika nyumba akapatwa na maradhi na yakamzidia matatizo mpaka ikapelekea kusema yeye na familia yake kuwa nyumba hii ina mkosi kwa sababu ya matazito yaliyo wapata je inafaa kuihama hiyo nyumba kwa sababu hiyo?..............................................................................152

SWALI LA 93: Ni ipi hukumu ya Tawasuli?.......................................153

SWALI LA 94: Ni nini Al-Walau Wal-Barau?...................................158

SWALI LA 95: Ni ipi hukumu ya kusafiri kwenda katika miji ya kikafiri? Na ni ipi hukumu ya kusafiri kwa ajili ya kutalii?..............................................160

SWALI LA 96: Sheikh:Mtu anafanya kazi na Makafiri ni kitu gani mnamuusia?....160

SWALI LA 97: Ni vipi tutaweza kupata faida katika vitu walivyo kuwa navyo Makafiri bila kuingia katika haramu? Na je Maslah Al-Mursala inaweza kuingia katika hilo?.......................................................................................161

SWALI LA 98: Ni ipi hukumu ya kuingia wasiokuwa Waislamu katika Jazira Al-Arabiya?..........................................................................................162

SWALI LA 99: Sheikh: Wanadai baadhi ya watu kuwa sababu ya kuchelewa Waislamu katika maendeleo ni kushikamana kwao na dini yao. Na shubha yao katika hilo. Ni kuwa Wamagharibi walipo amua kuachaana na dini zote na wakajiweka mbali na kila dini matokeo yake wamefika pale walipo fika katika maendeleo, na huenda wakati mwingine wakaitilia nguvu shubha yao hiyo kwa vile walivyo kuwa navyo Wa-

magharibu miongoni mwa mvua nyingi na mazoa, ni ipi rai yenu ewe Shei kh?............................................................................163

SWALI LA 100: Wanasema baadhi ya watu kuwa Hakika kuwa na maneno yalio sahihi sio jambo la muhimu muda wa kwamba moyo uko salama, ni yapi maelekezo yenu katika hilo?..............................................................165

SWALI LA 101: Ni ipi hukumu ya maneno haya((Mwenyezi Mungu azidumishe siku zako))?...............................................................................166

SWALI LA 102: Baadhi ya watu wanapo omba dua huomba kwa Uso wa Mwenyezi Mungu wanasema:Nakuomba kwa Uso wa Mwenyezi Mungu kitu flani na flani ipi hukumu ya maneno haya?.....................................................166

SWALI LA 103: Ni ipi hukumu ya mwenye kusema (Mwenyezi Mungu akurefushie kubaki kwako katika dunia)au (Mwenyezi Mungu akurefushie umri wako)?........................................................................................................167

SWALI LA 104: Ni mara nyingi tunaona katika Ukuta maandishi yameandikwa jina tukufu la (( Mwenyezi Mungu)) na pembeni mwake kumeandikwa jina (Mohammad rehma na

amani ziwe juu yake :), au tunayakuta hayo kwenye vipande vya Karatasi, au Vitabu au katika Msahafu, Je kuwekwa sehemu hiyo ni sahihi?..........................................................................................................167

SWALI LA 105: Ni ipi hukumu ya maneno haya: (( Mwenyezi Mungu atauliza kuhusu hali yako))?.......................................................................................168

SWALI LA 106: Ni ipi hukumu ya kusema: ((Flani ni marehemu)) au ((Amehama kwenda kwenye rehema za Mwenyezi Mungu))? ............................................... 168

SWALI LA 107: Ni ipi hukumu ya maneno haya: ((Kwa jina la nchi, kwa jina la Taifa))?..........................................................................................................168

SWALI LA 108: Ni ipi hukumu ya maneno ya watu wasiokuwa na Elimu wanaposema: (Umetuletea Baraka kwetu) (Baraka imetutembelea)?.................169

SWALI LA 109: Ni ipi hukumu ya maneno yao wanaposema: ((Qadari imeingilia kati)), au ((msaada wa Mwenyezi Mungu umeingilia kati))? ..............................170

SWALI  LA 110: Tunasikia na Tunasoma neno hili: ((Uhuru wa Kifikra)), Nayo ni kulingania katika Uhuru wa Kiitikadi, Mnasemaje juu ya hilo? ..........................171

SWALI  LA 111: Je inafaa kwa Mtu kumuambia Mufti ni ipi hukumu ya Uislamu katika jambo flani na flani, au ni ipi Rai ya Uislamu katika jambo flani?............172

SWALI  LA 112: Ni ipi hukumu ya kusema maneno haya: ((Zama zimetaka litokee jambo flani na flani)), na ((Qadari imetaka itokee kitu flani na flani))?..............172

SWALI  LA 113: Ni nini hukumu ya Maneno haya: Flani ni Shahidi?...............173

SWALI  LA 114: Ni yapi maoni yenu katika kutumia neno: (Ghafla)au kushitukiza?.........................................................................................................175

SWALI  LA  115: Sheikh Mwenyezi  Mungu awalipe kheri, Niyapi

mawazo yenu kuhusu istilahi ya fikra ya Kiislamu? Na Mfikiri wa Kiislamu?......................175

SWALI LA 116: Dini inagawanyika kwenye kiini na maganda ( mfano kufuga ndevu) hivi ni sahihi?..............................................................................176

SWALI LA 117: Ni ipi hukumu ya kusema tumemzika katika maisha yake ya milele? ..................................................................................................177

SWALI LA 118: Kujiita wakiristo kuwa niwafwasi wa yesu, na yesu kuwa ni mkiristo, je ni sahihi?..............................................................................178

SWALI LA 119: Niyapi mawazo yenu kuhusu istilahi hii, (La samaha Allah)?......................................................................................................179

SWALI LA 120: Kuna baadhi ya watu, anapo fariki mtu, husema: [Ewe nafsi iliyo tua!rejea kwa Mola wako umeridhika na umemridhishaa ] [ 28/ surat al-fajir, ni ipi hukumu ya kusema hiv

yo?..........................................................................180

MASWALI NA MAJIBU KUHUSU SWALA180

SWALI LA 121: Ni ipi asili au chanzo cha kujisafi-
sha na uchafu kama janaba au uchafu kama kinye-
si?.......................................................................................180

SWALI LA 122: Hivi sehemu yenye najsi inaweza kusafika bila ya kutumia maji ? Kemiko zinazo safishia vyakula hivi zina twaharisha vyakula?.........181

SWALI LA 123: Ni ipi hukumu ya maji yalio badiri-
ka rangi kwa sababu ya kukaa muda mre-
fu?.............................................................................................182

SWALI LA 124: Ni ipi hekima ya Mwenyezi Mun-
gu kuharamisha wanaume kuvaa dhaha-
bu?....................................................................................................182

SWALI LA 125: Ni ipi hukumu ya mtu kuwe-
ka meno ya dhahabu juu ya meno yake ya asi
li?.......................................................................................................184

SWALI LA 126: Ni ipi hukumu ya mtu kujisaidia haja ndogo sehemu wanayo tawadhia watu jambo ambalo linapelekea kufunua sehemu zake za siri?.....184

SWALI LA 127: Ni ipi hukumu ya mtu kukojoa akiwa amesi-
mama?.........185

SWALI LA 128: Ni ipi hukumu ya mtu kuingia chooni akiwa na msaha-
fu?......185

SWALI LA 129: Ni ipi hukumu ya kuingia chooni uki-
wa unakaratasi limeandikwa jina la Mwenyezi Mun-
gu?...............................................................186

SWALI LA 130: Mtu anapo kuwa chooni ( msalani ) vipi atasoma bismillahi atakapotia udhu?.................................................................................................186

SWALI LA 131: Ni ipi hukumu ya kuelekea kibla wakati unajisaidia haja ndogo au haja kubwa, au kukipa mgongo kibla?.........................................................186

SWALI LA 132: Mtu akitokwa na upepo sehemu yake ya siri (shuzi) hivi ni lazima kwa mtu huyo kujisafisha kwa kutumia maji?........................................188

SWALI LA 133: Ni muda gani sheria inapendekeza kupiga mswaki? Na ni ipi hukumu yakupiga mswaki kwa mtu anae subiri swala muda ambao inatolewa khutba?...............................................................................................................189

SWALI LA 134: Hivi ni lazima kusoma bismilahi wakati wa kutawadha?....189

SAWALI LA 135: Ni ipi hukumu ya kutahiri wanaume na wanawake?.......190

SWALI LA 136: Kama mtu atakuwa na meno ya bandia (ya-kutengeneza) Hivi ni lazima kwa mtu huyo kuyatoa meno hayo wakati anasukutua mdomo anapo kuwa anatawad-ha?..........................................................................................192

SWALI LA 137: Hivi ni lazima mtu akiwa anatwadha achukue maji mapya anapo pangusa masikio yake?..........................................................................193

SWALI LA 138: Ni ipi maana ya utaratibu wa kutawadha? Na ni yapi makusu-dio ya kufatanisha kuosha viugo wakati wakutawadha? Na ni ipi hukumu yak e?..................................................................................................................193

SAWALI LA 139: Mtu akitawadha akasahau kuosha kiungo kimoja katika viungo vinavyo takiwa kuoshwa hukumu yake ni ipi?...................................195

SWALI LA 140: Kama maji ya bomba yatakatika wakati mtu anatwadha, kisha yakarudi viungo vimesha kauka ata-

anza upya kutawadha au ataendelea alipo kuwa amefik ia?...............................................................................................................196

SWALI LA 141: Ni ipi hukumu ya udhu wa mtu alie weka kucha za kutengeneza( bandia )?.................................................................................................198

SWALI LA 142: Ni zipi sifa za udhu wa kisheria?.........................................199

RISALA YA MAELEKEZO ANAVYO JISAFISHA MGONJWA...............200

VIPI ATAJISAFISHA MGONJWA (KUTAWADHA)?..................................201

SWALI LA 143: Ni ipi hukumu ya mtu kuvua soksi za miguu kila anapokuwa anatwadha akitia shaka ya kusihi udhu?.............................................................204

SWALI LA 144: Kukadiria muda wa kupangusa juu ya khofu mbili, unaanza muda gani?..................................................................................

...................204

Masharti ya kupaka juu ya khofu mbili :...................................................
......205

Muda gani unaanza muda wa kupaka ?...................................................
.......206

SWALI LA 145: Ni ipi hukumu ya kupa-
ka juu ya soksi yenye tundu na soksi nyepe-
si?..........................................................................................................209

SWALI LA 146: Ni ipi kuhumu ya kupaka juu ya ogo?................................2
09

SWALI LA 147: Hivi ni lazima mtu kukusanya kati ya kutayamamu na kupaka juu ya ogo?..........................................................................................
....211

SWALI LA 148: Ni ipi hukumu ya mtu aliye tawadha akao-

sha mguu wake wa kulia, kisha akauingiza kwenye khofu au soksi, kisha akaosha mguu wakushoto akavaa khofu au soksi?.........................................................................................211

SWALI LA 149: Mtu akiwa sio msafiri akapaka kisha akasafiri atapaka kama msafiri?.......................................................................................................................212

SWALI LA 150: Mtu akiwa na shaka muda alio anza kupaka atafanyaje?...212

SWALI LA 151: Mtu akipaka juu ya viatu vya kike vilivyo inuka kwa nyuma vilivyo funika vidole vya miguu kisha akavua akapaka juu ya soksi fupi hivi inaruhusiwa kupaka juu yake?...........................................................................213

SWALI LA 152: Mtu akivua soksi fupi naye akiwa ametawadha kisha akazivaa kabla ya udhu wake hauja haribika hivi anaruhusiwa kupaka juu ya soksi hizo?...............................................................................................................213

SWALI LA 153: Mtu aliye paka juu ya khofu baada ya kuisha muda na akaswali kwa udhu huo hukumu yake ni ipi?..................................................

..214

SWALI LA 154: Ni vipi vitenguzi vya udhu?...........................................
.215

SWALI LA 155: Hivi kumgusa mwanamke kunatengua
udhu?.......................217

SWALI LA 156: Mwalimu ambae anafundisha wanafunzi Qur'an na hakuna maji sehemu ya madrasa hiyo wala sehemu ya karibu na madrasa na Qur'an haruhusiwi kuishika isipokuwa mtu aliye twahiri watafanyaje?........................219

SWALI LA 157: Ni mambo yapi yanayo mlazimu mtu kuoga?..........................220

SWALI LA 158: Hivi ni lazima kuoga kwa kuchezeana mke na mume bila ya kufanya tendo la ndoa au kumbusu?....................................................................222

SWALI LA 159: Mtu akiamka kutoka usingizini akakuta unyevu nyevu hivi ni lazima kwa mtu huyo kuoga?........................................................223

SWALI LA 160: Ni zipi hukumu za mtu mwenye janaba?..............................224

SWALI LA 161: Ni zipi sifa za kuoga?............................................225

SWALI LA 162: Mtu akioga josho kubwa kama janaba au hedhi au nifasi na hakusukutua mdomo wala hakupandisha maji puani jee kuoga kwakwe kumesihii?.........................................................................225

SWALI LA 163: Mtu akiwa na udhuru wakutumia maji atafanyaje ili aweze kupata twahara?....................................................................226

SWALI LA 164: Mtu akiamka na janaba wakati wa baridi kali anaruhusiwa kutayamamu?.......................................................................227

SWALI LA 165: Hivi ni sharti mtu akitaka kutayamamu atumie mchanga

wenye vumbi? Na hivi  kwenye kaulia ya Mwenyezi Mungu: [ Na mpake nyuso zenu na mikono yenu ] na neno hili kwenye kauli ya  Mwenyezi Mungu: [minhu] ni ushahidi kuwa ni sharti kupaka vumbi kwenye uso na miko?......................228

SWALI  LA  166: Mgonjwa ambaye hawezi kupata mchanga anaruhusiwa kutayamamu juu ya ukuta wa nyumba, au juu ya tandiko?..........................228

SWALI  LA  167: Ni ipi hukumu ya mkojo wa mtoto mdogo wakiume ukidondokea juu ya nguo?..........................................................229

SWALI  LA  168: Mwanamke  aliyevuka umri wa miaka khamsini anaona damu yake ya hedhi  ikiwa na sifa inayo fahamika na  mwanamke amevuka umri wamiaka khamsini  anaona damu ya hedhi katika safi isio fahamika  anaona  uchusichisi  au rangi  ya kahawiya?..................................................................230

SWALI  LA  169: Damu inayo mtoka Mwanamke mwenye  mimba damu hiyo ni ya hedhi?..........................................................................230

SWALI  LA 170: Ni upi uchache wa siku za hedhi na ni upi wingi wake?.......231

SWALI LA 171: Mwanamke aliye jisababishia kutokwa damu ya hedhi kwa matibabu na akaacha kuswali hivi atazilipa hizo swala?....................................232

SWALI LA 172: Hivi anaruhusiwa Mwanamke mwenye hedhi kusoma Qur`an?..............................................................................................................232

SWALI LA 173: Ikichanganyika damu ya Mwanamke hakufahamu kati ya damu ya hedhi na damu ya ogonjwa, atafanyaje ?..............................................233

SWALI LA 174: Mwanamke akingia katika siku zake za hedhi baada ya kuingia muda wa swala hukumu yake ni ipi? Na mwanamke akiingia kwenye hedhi atalipa swala?..........................................................................................................233

SWALI LA 175: Mwanamke ambaye alikuwa akiingia hedhi kwa muda wa siku sita kisha zikazidi siku zake za ada?..........................................................234

SWALI LA 176: Mwanamke ameingia kwenye ada yake ya Mwezi akatwaharika akaoga baada ya kuswali siku tisa, ikarudi damu ya hedhi, ikaendelea kutoka siku tatu, naye hakuswali siku hizo tatu, kisha akatwaharika, Akaswali siku kumi na moja, ikatoka tena hedhi katika siku za ada yake alio kuwa anaingia kila Mwezi, mwanamke huyo atarudia kuswali swala za masiku matatu au inazingatiwa kuwa alikuwa kwenye hedhi?..................................235

SWALI LA 177: Ni ipi hukumu ya maji maji ya rangi ya njano yanayo mtoka mwanamke kabla ya kutokwa na hedhi kwa muda wa siku mbili? ............235

SWALI LA 178: Ni ipi hukumu ya uchafu wa najno na kahawiya unao mtoka mwanamke sehemu za siri baada ya kuoga hedhi?...............................236

SWALI LA 179: Ni ipi hukumu ya kutumia vidonge kwa ajili ya kuzuia damu ya hedhi?............................................................................236

SWALI LA 180: Mwanamke anae tokwa na damu ya uzazi ( nifasi) ikizidi siku arubaini je anaruhusiwa kuswali na kufunga?...................................................237

SWALI LA 181: Mwanamke akitwaharika na damu ya uzazi kabla ya kutimia siku arubaini, (40) anaruhusiwa kufanya tendo la ndoa na mume wake? Na kama damu itarudi baada ya kupita siku arubaini ni ipi hukumu ya damu hiyo?........238

SWALI LA 182: Wmanamke ambae mimba imeharibika ya miezi mitatu, mwanamke huyo ataswali? Au atacha kuswali?......................................239

SWALI LA 183: Mtu ambaye atakuwa anatokwa na damu zisizo kata, ataswali vipi? Na vipi atafunga swaumu?.......................................................239

SWALI LA 184: Ni ipi hukumu ya swala? Na swala ni lazima kwa yupi?......240

SWALI LA 185: Mtu aliye poteza kumbukumbu na mtu aliye zimia hivi ni lazima kwa watu hao wawili mambo ya kisheria?.........................................242

SWALI LA 186: Mwanaume ambaye anamiezi miwili hajitambui kwa cho-

chote hakuswali wala hakufunga Ramadhani, mambo gani ya lazima kwake?..........244

SWALI LA 187: Hivi anaruhusiwa mtu kuchelesha swala kwa sababu ya sharti katika mashart ya swala kama mtu kushughulika na kutafuta maji?..............244

SWALI LA 188: Anae kesha usiku na haswali Al-fajir ila baada ya kutoka muda wake, hivi.........................................................................245

swala yake inakubaliwa? Na ni ipi hukumu ya swala zake zingine?...............245

SWALI LA 189: Anae chelewesha swala ya al-fajir mpaka muda wake ukatoka ........................................................................................246

SWALI LA 190: Mwanaume alichumbia binti wa mtu walivyo ulizia tabiya ya mwanaume huyo wakaambiwa haswali muhusika akaJibu Mwenyezi Mungu amuongoze hivi inaruhusiwa kumuozesha mtu huyo?............................247

SWALI LA 191: Atafanya nini mume aliye amri-
sha familia yake kuswali lakini hawakumsikili-
za.............................................................................252

ataendelea kuishi nao na kuchanganyikа nao au aondeke nyumba-
ni?.............252

SWALI LA 192: Ni ipi hukumu ya mwanamke kuendelea kuishi
na mume asiye swali na wameisha zaa watoto? Na ni ipi hu-
kumu ya kumuozesha binti kwa Mwanaume asiye swa-
li?........................................................254

SWALI LA 193: Atakaye acha kuswa-
li kwa makusudi kisha akatubu atalipa swala alizo zia-
cha?..................................................................................................255

SWALI LA 194 : Ni mambo gani ya lazima kwa
wazazi juu ya watoto wao wasio swa-
li?..........................................................................................................256

SWALI LA 195: Ni ipi hukumu yakutoa adhana kwa wasafi-

ri?................256

SWALI LA 196: Ni ipi hukumu ya adhana na iqama kwa mtu anaye swali peke yake?...............................................................................................256

SWALI LA 197: Mtu akikusanya swala ya adhuhuri na alasiri hivi ataq-imu kila swala? Na hivi swala za sun`na zina kuqimu ?............................ ....................257

SWALI LA 198: Neno ( Aswalatu khayru minal-naumi ) linatam-kwa katika dhana ya kwanza au ya pili katika swala ya Al-fa-jir?.............................257

SWALI LA 199: Hivi inasihi adhana ya kurikodi ( Recorder) ?...............259

SWALI LA 200: Mtu akiingia msikiti-ni na kunatolewa adhana ni jambo lipi bora af-anye?...............................................................................................259

SWALI LA 201: Imepokewa katika hadithi mtu aseme wakati anamfatisha muadhini ( radhwiytu billahi raban, abil-islami diyna, wabi Muhammadi rasula) ni muda gani mtu atasema hiyo nyiradi?..........................................................................259

SWALI LA 202: Ziada ya ( inaka laa tukhlifu miaadi) katika dua baada ya adhana ni sahihi?..........................................................................260

SWALI LA 203: Hivi mtu anatakiwa kumfatisha anaye qimu swala?..............260

SWALI LA 204: Tunawasikia baadhi ya watu baada ya kukimiwa swala wanasema: ( Aqama allah waadaamaha) ni ipi hukumu yake?.............................261

SWALI LA 205: Ni muda gani bora kuswali? hivi Mwanzo wake ndio bora? ..........................................................................261

SWALI LA 206: Mtu akiswali kabla ya kuingia muda bila kufahamu ni ipi hukumu yake?..........................................................................263

SWALI LA 207: Hivi inaruhusiwa kuto kufata utaratibu kati ya swala na swala kwa mtu ambaye analipa swala zilizo mpita kwa kusahau au kuto kujua?.........263

SWALI LA 208: Mtu aliye ingia mskitini kwa ajili ya kuswaLi swala ya ishaa kisha akakumbuka kuwa haja swali maghribi atafanya-je?..........................263

SWALI LA 209: Ikinipita faradhi moja au zaidi kwa kusa-hau au usingizi, nitazilipa vipi swala zilizo nipita? Nita-anza kuswali iliyo pita kisha niswali iliyopo au kinyume cha ke?..........................................................................................264

SWALI LA 210: Watu wengi wanaswali wakiwa wamevaa nguo nyepesi inayo onyesha rangi ya mwili kwa chini amevaa suruali fupi haivuki kwenye mapaja ispkuwa kidogo mtu anaona mapaja kupitia muonekano wa nguo inayo onyesha, Ni ipi hukumu ya swala ya mtu huyo?...........................................265

SWALI LA 211: Ni ipi hukumu ya mwanamke kuvaa nguo yenye mpasuo kwa mbele na ubavuni na kwanyuma inayo inaoyesha sehemu ya miudi ya miguu hoja yao ni kuwa wapo wanawake

tu?.....................................................................266

SWALI LA 212: Hivi inaruhusiwa kwa mwanamke kuswali akiwa amevaa niqabu au soksi za mikono?..........................................................................................267

SWALI LA 213: Ni ipi hukumu ya mtu aliye swali akiwa amevaa nguo yenye najsi naye hafahamu?..............................................................................................267

SWALI LA 214: Ni ipi adhabu ya mtu anaye vaa nguo ndefu inayo vuka vifundo vya miguu akivaa kwa maringo? Na ni ipi adhabu ya aliye vaa nguo ndefu bila maringo ? Na vipi tuta waJibu wanao toa ushahidi wa kuruhusu kuvaa nguo ndefu kwa hoja ya hadithi ya Abuu bakar radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake?..............................................................................................................................268

SWALI LA 215: Mtu akiswali baada ya swala akakumbuka kuwa anauchafu mkubwa unao mlazimu kuoga?.......................................................................270

SWALI LA 216: Mtu akitokwa na damu puani akiwa kwenye swala ni ipi hukumu yake? Hivi nguo yake inanajisika ikipatwa na damu inayo mtoka puani?........................................................................................270

SWALI LA 217: Ni ipi hukumu ya kuswali katika msikiti wenye kaburi ?......271

SWALI LA 218 : Ni ipi hukumu ya kuswali juu ya paa la choo? Ni ipi hukumu ya kuswali juu ya jengo linalo wekewa kinyesi cha wanyama ?...... .........................272

SWALI LA 219: Ni ipi hukumu ya wanao tembea na viatu ndani ya msikiti wa Makkah?........................................................................................273

SWALI LA 220: Mtu akiswali baada ya swala akafahamu kuwa alikuwa amepinda kidogo kuelekea kibla mtu huyo atarudia kuswali?..................................273

SWALI LA 221: Watu wakiswali swala ya jamaa bila kuelekea kibla ni ipi hukumu ya swala hiyo?...............................................................274

SWALI LA 222: Ni ipi hukumu ya kutamka niya?.....................................

..275

SWALI LA 223: Ni ipi hukumu ya mtu kuswali faradhi nyuma ya anaye swali sun'na kama mtu anaye swali faradhi ya ishaa pamoja na wanao swali tarawehe?..........................................................................................276

SWALI LA 224: Msafiri akimdiriki Imamu asio kuwa msafiri kwenye rakaa mbili za mwisho atatoa naye salamu kwa niya ya kupunguza?............................276

SWALI LA 225: Ni ipi hukumu ya kutembea kwa haraka kwenda kuwahi kuswali?..........................................................................................................276

SWALI LA 226 :Hivi inaruhusiwa kutembea kwa haraka kwa ajili ya kuwahi rakaa na Imamu katika swala ya jamaa? Tupeni maJibu naomba Mwenyezi Mungu awahifadhi....................................................................................277

SWALI LA 227: Ni ipi hukumu ya mtu kusoma Qur'ani ndani ya msikiti kwa sautu ya juu ambayo unawashawishi watu wanao swali ?.....................

..........277

SWALI LA 228: Baadhi ya watu wakingia msikitini karibu na muda wa kuqimu swala wanasimama wanusubili Imamu aingie kuswalisha wanaacha kuswali tahiyatu al-masjidi ni ipi hukumu ya kufanya hiv yo?..........................................278

SWALI LA 229: Tuna waona baadhi ya wanaume katika msikiti mtukufu wa Makkah wanapanga swafu nyuma ya swafu ya wanawake katika swala za faradhi, hivi swala zao zinakubaliwa? hivi Kuna maelekezo kwa watu hao?................278

SWALI LA 230: Hivi inaruhusiwa kumtoa mtoto kwenye swafu ya swa-la?.......278

SWALI LA 231 : Ni ipi hukumu ya kuswali kati ya nguzo mbili ?.............279

SWALI LA 232: Ni ipi hukumu ya swafu ya wanawake? Hivi swafu ya shari kwa wanawake ni ya kwanza na ya kheri ni ya mwisho kwa ujumla, au ni katika hali ya kuto kuwepo sitara kati ya wanaume na

mwanawake?.........................................279

SWALI LA 233: Ni ipi hukumu ya swala ya mtu anaye swalia nje ya msikiti kama mtu anaye swali katika njia zilizo ungana na msikiti?.............................280

SWAL LA 234: Ni jambo gani linalo angaliwa katika kupanga swafu? Inatakiwa mtu akutanishe kisigino cheke na kisigino cha mwenzie? Tupeni fatuwa Mwenyezi Mungu atawalipa.................................................................280

SWALI LA 235: Hivi imethibiti kuinua mikono kwenye swali isipokuwa sehemu nne? Pia katika swala za iddi mbili na swala ya jeneza?.....................................281

SWALI LA 236: Maamuma akimkuta Imamu amerukuu ataleta Maamuma takbira mbili?......................................................................281

SWALI LA 237: Ni ipi hukumu ya kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto juu ya kifua au moyo? Na ni ipi hukumu ya kuweka mikono miwili chini ya kitovu? Hivi kuna utofauti kati ya mwanamke na mwanaume katika hukumu hizo?.......................................................................................................................283

SWALI LA 238: Ni ipi hukumu ya kudhihirisha kusoma bismillah?..........283

SWALI LA 239: Ni ipi hukumu ya kusoma dua ya ufunguzi wa swala?.......284

SWALI LA 240: Hivi ni sun`na kuitkia Aamin ?................................................285

SWALI LA 241: Baadhi ya Maamuma inapo somwa: [ Iyaka naabudu waiyaka nastaainu ] wanasema: isataminna bi LLah, ni ipi hukumu ya kusema hivyo?....285

SWALI LA 242: Ni ipi hukumu ya kusoma Surat Al-fatiha (Alhamdu) kwenye swala?..........................................................................................................285

SWALI LA 243: Ni muda gani Maamuma atasoma surat al-fatiha (alhamdu) katika swala atasoma wakati Imamu anasoma surat al-fatiha au akiwa anasoma sura nyingine?...........................................................................288

SWALI LA 244: Vipi tutaweza kunyenyekea katika swala, na tunapo soma Qur'ani katika swala na nje ya swala?.............................................288

SWALI LA 245: Hivi kuna ushahidi kuwa Mtume alikuwa anakaa kimya baada ya kumaliza kusoma Surat A l-fatiha na kusoma sura nyingine?.........289

SWALI LA 246: Mtu aliye chelewa rakaa moja ya swala ya Al-fajir, atakamilisha rakaa iliyo baki kwa kusoma kwa sauti au hato soma kwa sauti?..........................................................................................289

SWALI LA 247: Nimesoma katika kitabu kimoja kinacho elezea swala ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake! Kuwa kuweka mikono juu ya kifua baada ya kutoka kwenye rukuu ni bidaa ya upotovu, ukweli ni upi?............290

SWALI LA 248: Baadhi ya watu wanazidisha neno : ( Ashukri ) baada ya kauli ((Rabana laka al-hamdu)) ni yapi mawazo yenu?....................................291

SWALI LA 249: Mtu anaporomoka vipi kwenda kusuju-
du?..................291

SWALI LA 250: Ni ipi hukumu ya mtu kijinyosha kuliko zidi katikati ya kusujudu?..........................................................................293

SWALI LA 251: Hivi kunaushahidi kuwa alama inayo toka kwenye paji la uso kwa sababu ya kusujudi ni alama miongoni mwa alama za watu wema?......293

SWALI LA 252: Hivi imepokewa hadithi sahihi ya kutiki-
sa kidole shahada katika kikao kidogo kati ya sijida mbi-
li?.........................................................293

SWALI LA 253: Ni ipi hukumu ya kikao cha kupumzika katika swa-
la?......294

SWALI LA 254: Ni ipi hukumu ya kutingisha kidole shahada ka-
tika tashahudi (tahiyatu) kukitingisha kuwanzia mwanzo mpaka mwisho?......................296

SWALI LA 255: Hivi inatosha kusoma tashahud ya kwanza tu au mtu atazidisha dua?.............................................................................................297

SWALI LA 256: Ni ipi hukumu ya mkao wa tawaruki ( kukalia matako) katika swala? Mkao huo ni kwa wanawake na wanaume?...............................297

SWALI LA 257: Imamu anatoa salamu moja kulia kwakwe hivi inatosha kutoa salamu moja? Tunaomba maJibu,Mwenyezi Mungu atawalipa...................298

SWALI LA 258: Hivi iliyo bora Imamu aondoke sehemu alio swalia baada tu ya kumaliza swala au asubir kidogo?...................................................................298

SWALI LA 259: Ni ipi hukumu ya kupeana mikono baada ya swala na kuombeana dua (Taaqabal allah)?...................................................................299

SWALI LA 260: Ni ipi hukumu ya kutumia tasbihi wakati wa kumtaja Mwenyezi Mungu?.................................................................................299

SWALI LA 261: Ni zipo nyiradi zilizo thibiti baada ya kutoa salamu kwenye swala?......................................................................................299

SWALI LA 262: Ni ipi hukumu ya kuinua mikono miwili na kuomba dua baada ya swala?........................................................................301

SWALI LA 263: Katika baadhi ya nchi baada ya swala za faradhi wanasoma Surt Al-fatiha, na nyiradi, na Ayatu Al-kurusiyu kwa sauti ya pamoja, ni ipi hukumu ya ibada hiyo?..............................................................301

SWALI LA 264: Mtu akifhofia akienda msalani kujisaidia swala ya jamaa itampita hivi ataswali jamaa akiwa amebana haja yake, au atajisaidia kwanza haja yake hata kama atachelewa swala ya jamaa?...........................................302

SWALI LA 265: Ni ipi hukumu ya kufumba macho mawili kwenye swala?................................................................................302

SWALI LA 266: Kunyosha nyosha vidole vya mikono ukiwa kwenye swala kwa kusahau hivi kunaharibu swa-

la?.......................................................................303

SWALI LA 267: Ni ipi hukumu ya kuweka kizuizi mbele ya mtu anaye swali? Na ni kipi kiwango cha kuweka kizuizi?...........................................304

SWALI LA 269: Nipi hukumu ya kuweka vituliza joto vya umeme mbele ya nao swali hivi imethibiti tahadhari ya kisheria?............................................305

SWALI LA 270: Hivi inafaa kwa mtu anaye swali akisoma aya inayo zungumzia habari za pepo amuombe Mwenyezi Mungu pepo na aya ya moto ajilinde kwa Mwenyezi Mungu na moto? Hivi kuna utofauti kati ya maamuma na anaye swali peke yake?............................................................305

SWALI LA 271: Ni zipi sababu za kusujudi sijida ya kusahau?..............305

SWALI LA 272: Imamu akizidisha rakaa na mimi siku mfuata nami nimechelewa hivi swala yangu ni sahihi? Ni ipi hukumu yakuto kuwacha kumfata na ni mezidisha rak aa?.......................................................................307

SWALI LA 273: Mtu anaye swali swala za usiku, na swala za usiku ni

rakaa mbili mbili, akasahau akasimama kuswali raka ya tatu atafanyaje?......................308

SWALI LA 274: Mtu anaswali akasimama kwenye rakaa ya pili hakukaa tashahudi ndogo, alivyo fika juu akakumbuka kuwa hakukaa kwenye tashahudi hivi mtu huyo atarud kwenye tashahudi? Na ni muda gani atasujudu sijida ya kusahau atasujudu baada ya salamu au kabla ya salamu?..........................308

SWALI LA 275 : Ni ipi hukumu ya swala ya witiri hivi ni swala maalumu kwa mwezi wa Ramadhani.......................................................309

SWALI LA 276: Tunaomba kwa heshma zenu ufafanuzi wa sun'na ya dua ya kunuti, hivi kunuti ina dua malumu? Hivi ni sharti mtu akiomba dua ya kunuti katika swala ya witiri arefushe kuomba dua hiyo?...............................309

SWALI LA 277: Hivi ni sun'na kuinua mikono wakati wakuomba dua ya kunuti? Naomba ushahidi wa hilo?................................................310

SWALI LA 278: Ni ipi hukumu ya dua ya kunuti katika swala za fara-

dhi? Na ni ipi hukumu ya kunuti Waisalamu wakipatwa na balaa au misiba ?..........310

SWALI LA 279: Ni ipi hukumu ya swala ya tarawehe, na ni ipi idadi ya rakaa za tarawehe?.........................................................................................................310

SWALI LA 280: Ni ipi hukumu ya kusoma dua ya kukhitimisha Qur`ani katika kisimamo cha mwezi wa Ramadhani?...............................................................312

SWALI LA 281: Hivi usiku wa chezo ( Laylatu Al-qadiri) huwa upo katika usiku mmoja maalum katika kila mwaka au usiku huo huwa unahama hama mwaka huu katika usiku huu na mwaka mwingine usiku mwengine?............313

SWALI LA 282: Ni ipi hukumu ya Maamuma kubeba msahafu katika swala ya tarawehe ndani ya mwezi wa Ramadhani kwa hoja kuwa anamfata Imamu kwenye kisoma?.......................................................................314

SWALI LA 273: Baadhi ya maimamu wa misikiti wanajaribu kuzivutia nyoyo za watu na kuwathiri kwa kubadilisha sauti zao muda mwengine wakati wanaswalisha tarawehe, nimesikia baadhi ya watu wanalikemea hilo, ni ipi kauli yenu juu ya jambo hilo? Namuomba Mwenyezi Mungu awahifadhi!.....315

SWALI LA 284: Wanasema baadhi ya Wanachuoni: muda wa kuswali sun`na za kabla ya swala ya faradhi na sun`na za baada ya swala ya faradhi zinaswaliwa ukingia muda wa swala faradha na hauruhusiwi kuswali kwa kutoka muda wa swala ya fardhi, wanasema Wanachuoni wengine: Sunnah ya kabliya inaisha muda wake kwa kuisha muda wa kulipa swala ni ipi kauli yenye nguvu?.........315

SWALI LA 285: Ni ipi hukumu ya kulipa swala ya Sunnah baada ya swala ya Al-fajir kwa mtu ambaye hakuweza kuiswali sun`na kabla ya swala? Hivi vina pingana kulipa sun`na baada ya Al-fajir na katazo la kuswali baada ya swala ya Al-fajir?......................................................................................................316

SWALI LA 286: Mtu akingia msikitini kabla ya adhana akaswali tahiyatul-masjidi, kisha muadhini akatoa adhana hivi ataanza tena kuswali Sunnah?......316

SWALI LA 287: Hivi mtu atalipa swala za sun`na za rawati-

bu?....................317

SWALI LA 288: Hivi kunaushahidi wa mtu kubadili seh-
emu ya kuswalia sun`na baada ya kumaliza kuswali farad-
hi?..........................................317

SWALI LA 289 : Mtu ikimpita sun`na y a swala ya dhuha hivi atailipa
?....317

SWALI LA 290: Hivi ni sharti kuwa na udhu ukitaka kusujudu si-
jida ya kisomo? Na ni yiradi gani sahihi unasoma ukiwa umesuju-
du?...................318

SWALI LA 291: Ni muda gani mtu atasujudu kwa ajili ya kumshukuru
Mwenyezi Mungu? Ni zipi sifa za kusujudu huko? Hivi ni sharti kwa
anaye sujudu kwa ajili ya kushukuru awe na udhu?.................................
....................319

SWALI LA 292: Ni ipi hukumu ya swala ya istikhara?
(kuomba maelekezo kwa Mwenyezi Mungu) Hivi mtu anawe-
za kusoma dua ya istikhara akiswali tahiyatu Al-masjidi

au akiswali sun`na za kabla ya swala au baada ya swala?....................................................................................319

SWALI LA 293: Ni ipi swala ya tasbihi?............................................320

SWALI LA 294: Ni ipi hukumu ya kuswali raaka mbili usiku wa ndoa wakati wa kukutana mke na mume?...........................................................320

SWALI LA 295: Ni zipi nyakati zilizo katazwa kuswali? Hivi swala ya tahiyat Al-masjidi kabla ya swala ya magharibi inakuwa kabla ya adhana au baada ya adhana? Tupeni fatua Mwenyezi Mungu awalipe kher..............................321

SWALI LA 296: Ni ipi hukumu ya swala ya jamaa?...........................321

SWALI LA 297: Kundi la watu wanaoishi sehemu moja ,hivi wanaruhusiwa kuswali jamaa katika nyumba hiyo au ni lazima watoke waende msikitini ?..323

SWALI LA 298: Ni lipi bora kwa mfanya kazi akisikia adhana awahi kwenda kwenye swala au asubili amalizie baadhi ya kazi? Ni ipi hukumu ya kuswali sun`na zisizo kuwa za rawatibu?........................................................324

SWALI LA 299: Mtu akichelewa rakaa moja au mbili katika Swala ya jamaa hivi wakati wakulipa rakaa zilizo mpita atasoma Surat Al-fatiha na sura nyingine? Au atasoma Surat Al-fatiha peke yake?.........................................324

SWALI LA 300: Mtu ameingia msikitni akamkuta Imamu yupo kwenye tashahudi ya mwisho mtu huyo ataingia kwenye jamaa ya Imamu ? Au atasubili jamaa nyingine ya pili?...............................................................324

SWALI LA 301: Mtu atafanyaje kama atakuwa anaswali sun'na ikakimiwa swala ya faradhi?.........................................................................................325

SWALI LA 302: Maamuma akiingia kwenye swala baada ya Imamu kumaliza takbira ya kuhirimia na kusoma Surat Al-fatiha, Maamuma akanza kusoma Surat Al-fatiha lakini Imamu akarukuu kabla ya Maamuma kumaliza kusoma Surat Al-fatiha hivi Maamuma atarukuu na Imamu au atakamilisha Surat Al-fatiha?.........................................................................................326

SWALI LA 303: Maamuma akimkuta Imamu amesujudu, hivi atamsubiri Imamu ainuke au atamfata?...............................................................................326

SWALI LA 304: Mtu anaeswali nyuma ya Imamu katika swala

ambazo anasoma kwa siri akimaliza kusoma Surat Al-fatiha na sura nyingine Imamu akawa haja rukuu mtu huyo atakaa kimya?........................................326

SWALI LA 305: Ni ipi hukumu ya Maamuma kumtangulia Imamu kwenye matendo ya swala?...................................................................327

SWALI LA 306: Hivi inasihi kuswali nyuma ya mtu muovu?..................328

SWALI LA 307: Hivi inafaa kuswali faradhi nyuma ya anaye swali Sunnah, na anaye swali sun'na nyuma ya anaye swali faradhi ?..............................328

SWALI LA 308: Kumetokea mjadala kati ya kundi la watu walio kuwa wanaswali akiingia mtu msikitini akiwa amechelewa akakuta swala imekimiwa na swafu imekamilika hakupata nafasi kwenye swafu, hivi inafaa kwa mtu huyo amvute mtu mmoja kweye swafu ya mbele ili waweke swafu ya pili nyuma wakiwa wawili? Au aswali peke yake akiwa nyuma Au atafanyaje?...........329

SWALI LA 309: Kuna misikiti yenye ghorofa ya kwanza na ghorofa ya pili wanao swali ghorofa ya pili hawawaoni wanao swali ghorfa ya chini hivi swala zao ni sahihi?...................................................................................................330

SWALI LA 310: Hivi Mwislamu anaruhusiwa kuswali kwa kufata swala inayo onyeshwa kwenye television moja kwa moja, au kwenye radio bila kumuona Imamu haswa kwa wanawake?.......................................................330

SWALI LA 311: Ni muda dani ni lazima kuswali ukiwa kwenye ndege? Na ni vipi mtu ataswali kwenye ndege swala ya faradhi? Na ataswali vipi swala ya sun'na akiwa kwenye ndege?........................................................332

SWALI LA 312: Ni kipi kiwango cha masafa ya kupunguza swala? Hivi inaruhusiwa kukusanya bila kupunguza ?.........................................................333

SWALI LA 313: Mtu anaye safari kwenda Riadhi kwa ajili ya masomo anakwenda jioni siku ya Ijumaa anarudi alasiri siku ya jumaa tatu, hivi anakuwa na hukumu ya msafiri katika swala na mambo mengine?................................334

SWALI LA 314: Ni ipi hukumu ya kukusanya swala ya alasiri kwenye swala ya ijumaa? Hivi anaruhusiwa aliye njee ya mji kukusanya swala?.............335

Ujumbe:........................................................................................335

SWALI LA 315: Ni mambo gani yameruhusiwa katika safa-
ri?..................337

SWALI LA 316: Ni muda gani unanza saa ya kwanza siku ya iju-
maa?..........337

SWALI LA 317: Hivi inaruhusiwa mwislmu aswali nyumab-
ni kwakwe swala ya ijumaa kama atakuwa anasikia sauti ya
Imamu?.................................338

SWALI LA 318: Hivi Mwanamke ata swali rakaa ngapi swala ya iju-
maa?..338

SWALI LA 319: Atakaye swali ijumaa hivi ataswali na swala ya adhuh
uri?..........................................................................................338

SWALI LA 320: Umefika muda wa swala ya ijumaa na sisi tupo baha-
rini tunafanya kazi, baada ya kuwadia muda wa adhana ya adhuhuri
kwa nusu saa tukatoka baharini hivi inasihi na sisi tutoe adhana na
tuswali ijumaa?........340

SWAL I LA 321: Maamuma atafanyaje akifika msikitini siku ya ijumaa
akamkuta Imamu yupo katika tashahudi ya mwisho,( Tahiyatu) hivi

atalipa rakaa nne au ataswali rakaa mbili ?..........................................................341

SWALI LA 322: Hivi Maamuma kuitikia aamin wakati Imamu anaomba dua baada ya khutba siku ya ijumaa hivi ni uzushi?....................................341

SWALI LA 323: Ni ipi hukumu ya kuinua mikono na Imamu anakhutubu siku ya ijumaa?..........................................................................................................341

SWALI LA 324: Ni ipi hukumu ya khutuba kwa lugha isio kuwa ya kiarabu?...............................................................................342

SWALI LA 325: Kuoga siku ya ijumaa na kujipamaba kwa ajili ya siku hiyo hivi ni kwa wanaume na wanawake? Ni ipi hukumu ya kuoga kabla ya ijumaa kwa siku moja au siku mbili?.....................................................342

SWALI LA 326: Mtu akingia msikitini siku ya ijumaa na muadhi anatoa adhana ya pili hivi ataswali tahiyat Al-masijidi au atamfata muadhini kwa kuJibu adhana?...........................................................................343

SWALI LA 327: Ni yapi mawazo yenu anaye kata swafu na kuvuka kwenda mbele siku ya ijumaa ?...................................................................343

SWALI LA 328: Ni ipi hukumu ya kumsalimia mtu na Imamu anahutubu? Na ni ipi hukumu ya kurudisha salamu kwa aliye salimiwa na Imamu anahutubu?.....................................................................343

SWALI LA 329: Ni ipi hukumu ya kupeana pongezi sikukuu ya iddi? Hivi kuna maneno maalum ya kupeana pongezi ya iddi?.....................................344

SWALI LA 330: Ni ipi hukumu ya swala ya sikuu ya iddi?..................344

SWALI LA 331: Ni ipi hukumu ya kuswaliwa swala ya Iddi sehemu nyingi katika mji?.....................................................................................345

SWALI LA 332: Ni ipi namna ya kuswali swala mbili za iddi?...............346

SWALI LA 333: Anasimama Imamu katika baadhi ya miji siku ya Iddi kabla ya swala akileta takbira kwa kutumia kipaza sauti na Maamuma nao wanaleta takbira pamoja na Imamu, ni ipi hukumu ya kufanya hivyo?..........347

SWALI LA 334: Ni muda gani watu wanatakiwa kuwanza kuleta takbira za siku ya Iddi? na ni zipi sifa zake?.....................................................347

SWALI LA 335: Ni ipi hukumu ya swala ya kupatwa kwa mwezi na ni ipi swala ya kupatwa kwa jua?.............................................................................347

SWALI LA 336: Ambaye imempita swala ya kupatwa kwa mwezi vipi anailipaje...........................................................................................348

SWALI LA 337: kugeuza kilemba katika dua baada ya swala ya kuomba mvua, je hugeuzwa wakati wa kuomba au hugeuzwa nyumbani kabla ya kutoka kwenda msikitini? Na ni ipi hikma ya kugeuza kilelemba? nifahamisheni Allaah awabariki ..........................................................................................349

SWALI LA 338: baadhi ya watu wanasema: lau msinge taka msaada kwa kuomba mvua inge nyesha tu, mnasemaje katika hili?.......................................................349

SWALI LA 339: Ni ipi rai yenu kwa mtu anae usia kuwa akifa azikwe mahali Fulani, je ina paswa kutekeleza wasia huo?.......................................................350

SWALI LA 340: Ni wakati gani inatakiwa kusomwa talakini?....................351

SWALI LA 341: Ni ipi rai yenu kwa ambae anamchelewesha kumzika maiti mpaka wafike au waje baadh ya ndugu waliyoko miji ya mbali?.................351

SWALI LA 342: Kutangaza khabari za kifo kwa watu wake wa karibu na marafiki zake ili wakusanyike kwa ajili ya kumswalia maiti, je hii linaingia katika matangazo yaliyo katazwa kisheria au hii inafaa?.............................................352

SWALI LA 343: Ni namna ipi ya sawasawa iliyo pokelewa kutoka kwa Mtume ikibainisha jinsi ya kuosha mai-

ti?.....................................................352

SWALI LA  344: Wakati mwingine katika ajali za magari na  moto na kuvunjika yani kama kuporomokewa na nyumba mtu huharibika au kupoteza baadhi ya viungo, na wakati mwingine kunapatikana vipande vidogo kama kipande cha mkono au kichwa, je ni sharia kuswalia viungo hivi? na je vinaoshwa? ...........353

SWALI LA 345:  Mwanamke mimba yake imaharibika ikiwa na muda wa miezi sita, na alikua mwanamke huyo akifanya kazi ngumu na alikuwa akifunga ramadhani, na yeye huyo mwanamke ana shaka ya kuwa kufa kwa kiumbe alichokuwa amebeba tumbo na kikashindikana kuzaliwa salam ni kwa sababu ya zile kazi ngumu alizokuwa akifanya, pamoja na hilo nikwamba kiumbe hicho kimezikwa bila ya kuswaliwa , niipi hukmu ya kuacha kuswaliwa kiumbe hicho ? na huyu mwanamke afanyeje ili aondoe shaka hii ya kudhani yeye ndiyo sababu ya kufa na kuharibika mimba ? nifahamisheni ........................................354

SWALI LA 346: Ni ipi namna ya kuswali  swala ya jeneza ( maiti )?.................355

SWALI LA 347: Ni nini hukumu ya kumswalia maiti ikiwa maiti huyo alikuwa haswali au inahisiwa kuwa haswali au haijulikani hali yake kuwa ana swali au haswali? je inajuzu kwa kiongozi kumswalia maiti huyo?..........................356

SWALI LA 348: Je swala ya maiti ina wakati maalu wa kuswaliwa ? na je inajuzu kuzika usiku? na je swala ya maiti ina idadi ya watu maalumu wakuswalia? na je yajuzu kuswaliwa makaburini na juu ya makaburi? (yani maiti ambaye ashazikwa ukamswalia akiwa kwenye kaburi lake ina faa? ) ....................................357

SWALI LA 349: Je nisheria kumswalia maiti aliye mbali kwa hali yoyote ile ? au kuna masharti maalumu yaliyo wekwa ?..............................................................358

SWALI LA 350: Baadhi ya miji wanamzika maiti akiwa amelalia mgongo na mikono yake iko tumboni kwake ni njia ipi iliyo swahihu katika kumzika maiti? ......................................................................................................359

SWALI LA 351: Ni nini hukumu ya kusoma Qur an juu ya makaburi na kumuombea Maiti Dua kwenye kaburi lake , na mtu kujiombea mwenyewe akiwa kaburini?.......................................................................................................359

SWALI LA 352: Ni ipi hukumu ya kuzuru makaburi ?, na kusoma suuratul Faatiha?, na wanawake kuzuru makaburi? ...........................................360

SWALI LA 353: Kuna tabia katika baadh ya miji na tabia hiyo ni kwamba atakapo kufa maiti wanaweka kaseti za kuruani kwa sauti kubwa katika ile nyumba ya maiti, nini hukumu ya jambo hili?...................................................362

FAT’WA ZINAZO HUSU ZAKA..............................................363

SWALI LA 354 : Ni zipi sharti za kupasa kutoa Zaka ?............................363

SWALI LA 355: Ni namna gani ya kutoa zaka ya mshahara wa mwisho wa mwezi?..................................................................................365

SWALI LA 356: Inapasa kutoa zaka katika mali ya motto na mwenda wazimu?........................................................................365

SWALI LA 357: Ni ipi hukumu ya zaka ya deni ?..................................366

SWALI LA 358: Je Mtu aliye kufa na ana daiwa na hakuacha mali ya kuweza kulipa deni hilo inafaa kuchukua mali ya zaka ili kumlipia deni hilo?............366

SWALI LA 359: Je inaswihi sadaka ya mwenye kudaiwa? nani haki gani anasamehewa katika haki za kisheria?..............................................................367

SWALI LA 360: Kama Mtu hajatoa zaka miaka minne anazimika kufanya nini?..................................................................................369

SWALI LA 361: Je inatolewa zaka mifugo ambayo uchungaji wake ni muda wa nusu ya mwaka?..................................................................................369

SWALI LA 362: Kabla ya miaka mitatu nimenunua nyumba na nje yake

kuna mitende mitatu yenye matuma aina mbili na ina matunda mengi namshukuru Mwenyezi Mungu je kwa hali hii na paswa kutoa zaka? kama jawabu ni ndiyo na watu hawajui kabisa mimi ninauliza kutokana na hilo: Vipi nitafahamu kiwangu cha kutoa zaka na mimi nayapatia faida? pili: ninawezaje kuikasimia zaka? na je itatolewa kila aina kivyake au hujumuishwa aina zote na kutolewa kama aina moja? na je inapasa kutoa pesa baada yake.....................................................370

SWALI LA 363: NI kiwango cha kuweza kutoa zaka katika dhahabu na fedha ? na pishi ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake ni sawa na kilo ngapi?.............371

SWALI LA 364: Mtu ana watoto wa kike na amewapa vipambo vya thamani kama vile mikufu ya dhahabu heren pete bangiri na vinginevyo na vipambo hivyo viki kusanywa vinafikia kiwango cha zaka, lakini kipambo kimoja kimoja peke yake hakifikii kiwango cha zaka, je vinakusanywa vyote kisha ndiyo avitolewe zaka?..........................................................................................................371

SWALI LA 365: Mtu atakapo toa zaka akampa Mtu mwingine ambaye anasitahiki kupewa zaka kisha Yule aliye pewa zaka akaamua kumpa Yule aliyempa zawadi je aikubali zawadi hiyo?.........................................................................372

SWALI LA 366: Je inajuzu Mtu kutoa nguo au kitu kingine katika zaka ya mali – yani alitakiwa atoe zaka ya mali yake lakini akaona asitoe pesa bali atoe nguo au kitu kingine?.......................................................................372

SWALI LA 367: Itakapo kuwa dhahabu pamoja na Almasi na mfano wake vipi itakadiriwa zaka yake katika vitu hivyo?...........................................372

SWALI LA 368: Ni nini hukumu ya kutoa pesa ya zaka ikajengea misikiti ? Na fakiri ni Mtu wa namna gani?........................................................373

SWALI LA 369: Je yanatolewa zaka magari yaliyo wekwa kwa ajili ya kukodishwa na magari ya matumizi binafsi ambayo siyo ya kukodisha?.................................373

SWALI LA  370: ni nini hukumu ya zaka ya nyumba zinazo kodishwa?..........374

SWALI LA 371: Mtu kanunua aridh ili aishi hapo na baada ya kupita miaka mitatu aka kusudia kuifanyia biashara je ule muda uliyo pita atatoa zaka?.....................375

SWALI LA 372: Ni nini hukumu ya kutoa zaka ya fitri katika masiku kumi ya mwanzo wa mwezi wa Ramadhani ..................................................375

SWALI LA 373: Je inajuzu kuzidisha kiwango cha zaka ya Fitri kwa niya ya kutoa sadaka?.................................................................................................376

SWALI  LA 374: Wanasema baadhi ya wanachuoni: kwamba haijuzu kutoa zaka ya Fitri mchele, hali ya kuwa aina za vyakula vilivyo chaguliwa kisheria vipo?...........................................................................376

SWALI  LA 375: Ameulizwa Shekh: ambaye ana thuluthiya ambayo niya maiti na ana pesa za mayatima jehizo zinatolewa

zaka?.........................................378

SHALI LA 376: Je gari la Mtu binafsi ambalo siyo la biashara je Linatolewa zaka?.......................................................................................................................378

SWALI LA 377: Mtu atakapo toa zaka yake kumpa anae sitahiki kupewa zaka je Mtoaji huyo anasitahiki kumuambia anaempa kuwa hii ni zaka?.........................378

SWALI LA 378: Ni nini hukmu ya kuipeleka zaka sehemu nyingine na kuacha sehemu ambapo inafaa kutolewa?.......................................................379

SWALI LA 379: Ambaye yuko Makkah na familia yake iko mji wa Riyadh je atawatolea zaka ya Fitri Katika Mji wa Makkah? hii ni kwa mfano unaweza pigia mfano huu miji mingine...........................................................379

SWALI LA 380: JE ubora ni kumpa zaka Mtu anae daiwa ili alipe deni lake au ubora ni Yule Mtu anae taka kutoa zaka aende kwa Yule anae dai na amlipie mdaiwa deni lake?.........................................................................................380

SWALI LA 381: Je kila anaenyoosha Mkono wake akiomba zaka anasitahiki kupewa zaka?.............................................................................................380

SWALI LA 382: Mtu Tajiri ametuma zaka yake kwa mtu na akasema: zigawanye kwa unavyo ona wewe, je huyu wakili anakuwa ni

miongoni mwa wenye kuitumikia zaka na anasitahiki kwenye zaka hiyo?................................381

SWALI LA 383: Mtu ni Mdhaifu wa imani je anapewa zaka kwa ajili ya kuikuza imani yake ajapokuwa siyo Muheshimiwa katika jamaa zake?......................382

SWALI LA 384: Ni nini hukmu ya kutoa zaka ukampa mwanafunzi?............382

SWALI LA 385: Je inajuzu kutoa zaka kuwapa wanaopigana jihadi?................384

SWALI LA 386: Hivi kutoa pesa ya zaka ikajengea misikiti pia ni katika kuifuata kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: [Na katika njia ya Mwenyezi Mungu] katika kubainisha watu wanao sitahiki kupewa zaka?..................................................384

SWALI LA 387: Ni nini hukumu ya kutoa zaka na kuwapa watu wako wakaribu au ndugu zako? ......................................................................385

SWALI LA 388: Je utoaji zaka na sadaka umuhimu wake nikwa ajili ya mwezi wa ramadhani tu?........................................................................386

SWALI LA 389: Je sadakat jaaria (sadaka yenye kuendelea): ni ile ambayo aliitoa Mtu katika uhai wake au ni ile ambayo wametoa ndugu zake kwa ajili yake baada yay eye kufa?...............................................................387

SWALI LA 390: Je inajuzu kwa mwanamke ajitolee sadaka kwenye mali ya mume wake au amtolee Mtu mwingine katika jamaa zake? yani -jamaa wa mwanamke ..............................................................................................388

SWALI LA 391: Mtu masikini anachukua zaka kutoka kwa rafiki yake tajiri kwa madai kuwa sadaka hiyo ataigawa kwa watu kisha anaichukua yeye; je ni nini hukmu ya kufanya jambo hilo?.......................................................388

MASWALI NA MAJIBU KUHUSU SWAUMU....................................389

SWALI LA 392: Ni nini hikma ya kufaradhishwa swaumu?....................389

SWALI LA 393: Kunamwenye kutangaza kuunganisha machimbuko yote ya mwezi kuwa yafuate makkah kwa lengo la kuukusanya umma katika kuingia mwezi wa ramadhani uliyo barikiwa ne miezi mingine ni nini rai yenu katika hili?.............................................................................................390

SWALI LA 394: Atakapo safari mfungaji kutoka kwenye mji wake akaenda kwenye mji mwengine na ikatangazwa kwenye mji aliyo toka kuwa mwezi wa kufungua umeonekana je anafungua kwa kuwafuata wale wa mji aliyotoka? pia ifahamike kuwa mji huu wa pili aliyo fikizia mwezi hauja onekana?............391

SWALI LA 395 : Ni ipi rai yenu kwa Mtu ambaye kazi zake ni Ngumu na swaumu kwake ikawa ni ngumu ; je afungue ?..............................................392

SWALI LA 396: Msichana mdogo ameingia katika hedhi na alikua akifunga wakati akiwa kwenye hedhi kwa kuto kufahamu; anapaswa kufanya nini?........393

SWALI LA 397: Mtu aliacha swaumu ya ramadhani kwa ajili ya kutafuta maisha na maisha ya wale waliyo chini yake katika kizazi chake ni nini hukmu yake?..393

SWALI LA 398: Ni nyuzuru gani zinazo ruhusu Mtu kuacha kufunga ?..........394

SWALI LA 399: Mtu amelala usiku wa kwanza katika ramadhani kabla ya kuthibitika kuonekana kwa mwezi, na hakulala na nia ya swaumu, baada ya kucha akafahamu kuwa ni ramadhani, atafanya nini katika hali kama hii? na je atailipa siku hiyo?...................................................................................395

SWALI LA 400: Atakapo fungua Mtu kwa udhuru wa kisheria kisha ule udhuru ukaondoka katikati ya mchana je atajizuilia na kula katika sehemu ya mchana iliyo baki?..............................................................................396

SWALI LA 401: Mwanamke amepatwa na maradhi ya kuota uvimbe tumboni ,madaktari wakamkataza kufunga hukumu yake nini?........................................396

SWALI LA 402 : Ni vipi na wakati gani inakua swala ya msafiri na anaifungaje?..........................................................................397

SWALI LA 303: Ni nini hukumu ya msafiri kufunga pamoja na kuwa kunaugumu katika safari yake?.......................................................................399

SWALI LA 404: Ni ipi hukumu ya msafiri kufunga pamoja na kuwa swaumu siyo nzito kwa mfungaji katika zama za sasa zilizo enea vyombo vya kisasa vya kusafiria?.........................................................................399

SWALI LA 405: Msafiri atakapo fika Makkah na amefunga je anaruhusiwa kufungua ilia pate nguvu za kufanyia ibada ya Ummrah?..................................401

SWALI LA 406: Je inajuzu kwa mwanamke mwenye kunyonyesha afungue, na niwakati gani atalipa? na je anawalisha masikini?...................................402

SWALI LA 407: Aliye funga atakapo maliza mchana wake kwa kulala kwa ajili ya njaa kali na kiu je hilo linafanya swaumu yake isiswihi?.........................402

SWALI LA 408: Je kila siku inayo fungwa katika ramadhani inahitaji kutia nia au inatosha nia mara moja tu kwa mwezi mzima?.....................................403

SWALI LA 409: Mwenye kunuiya kufungua pasi na kula au kunywa , Je hilo linamfanya awe amefungua kwa kukusudia tu bila kufan-

ya?................................403

SWALI LA 410: Ni ipi hukmu ya anae kula au kunywa kwa kusahau? Na nini analazimika Yule aliye muona?.......................................................404

SWALI LA 411: Ni ipi hukmu ya kutia wanja kwa ambae amefunga?............405

SWALI LA 412: Ni ipi hukumu ya kupiga mswaki na kujitia manukato kwa aliye funga?..........................................................................................405

SWALI LA 413: Ni vitu gani vina haribu swaumu?..................................406

SWALI LA 414: Ni ipi hukmu ya kutumia dawa ya pumu ya kupuliza mdomoni kwa aliye funga je anafungua?.......................................................412

SWALI LA 415: Je matapishi yana funguza?..................................................412

SWALI LA 416: kutoka damu katika meno ya aliye funga je ana fungua?........413

SWALI LA 417: Atakapo twaharika mwanamke mwenye hedhi kabla ya Alfajiri na akaoga baada ya kuchomoza alfajiri ni ipi hukmu ya funga yake au swaumu yake?.................................................................................413

SWALI LA 418: Ni ipi hukumu ya kung'oa jino kwa aliye funga je anafungua?.................................................................................414

SWALI LA 419: Ni ipi hukmu ya kutoa Damu kwa ajili ya kupimwa kwa Mtu aliye funga je anafungua?....................................................................................414

SWALI LA 420: Aliye funga akijitoa manii kwa kutumia mkono ( au kupiga punyeto kama wasemavyo) je anafungua kwa sababu hiyo? naje analazimika kutoa kafara?.................................................................................................................415

SWALI LA 421: Ni ipi hukmu ya kunusa mafukato kwa aliye funga?...........415

SWALI LA 422: Ni ipi tofauti ya kunusa kitu kinacho fukizwa kama udi na kati tone kwa kua kunusa hakufunguzi tofauti na tone linafunguza tofauti ya viwili hivi ni ipi?...............................................................................................................416

SWALI LA 423: NI ipi hukumu ya kuweka tone puani na jichoni na puani kwa aliye funga?.................................................................................416

SWALI LA 424: Atakae kuwa usingizini akaota na yeye amefunga je swaumu yake itaswihi?..........................................................................................................417

SWALI LA 425 : Ni ipi hukumu ya kujimiminia maji ya baridi kwa ajili ya kujipoza kwa aliye funga?.........................................................417

SWALI LA 426: Atakapo sukutua aliye funga , au kupandisha maji puani na maji yakaingia mpaka ndani ya pua yake je anafungua kwa ajili ya kufanya hivyo?...418

SWALI LA 427: Ni ipi hukumu ya kutumia mafuta mazuri kama vile marashi kwa aliye funga?....................................................................................................418

SWALI 428: Je kutokwa na damu puani kunafunguza?..........................418

SWALI LA 429: Tunaona baadhi ya kalenda katika mwezi wa ramadhani zimewekwa kipengele kinacho sema (kujizuilia) na huko kujizuilia inakua ni kabla ya swala ya alfajiri kama dakika kumi, au robo saa, je jambo hili lina asili katika Sunnahh au ni miongoni mwa bida'a na uzushi ?.....................................419

SWALI LA 430 : Mwenye kuchwewa na jua akiwa uwanja wa Ndege na muadhini aka adhini kisha akafungua na baada ya ndege kupaa akaona jua je anajizulia na kula?.................................................................................419

SWALI LA 431: Ni ipi hukmu ya kumeza makohozi au makamasi kwa ambaye amefunga?...................................................................................420

SWALI LA 432: Je swaumu inaharibika kwa kuonja chakula bila ya kukimeza?...........................................................................................420

SWALI LA 433: Je Mtu kuongea maneno ya haramu katika mchana wa ramadhani ana haribu swaumu?...............................................................................................421

SWALI LA 434: Ni ipi shahada ya uongo? na je inabatilisha swaumu?...........422

SWALI LA 435: Ni zipi adabu za swau-
mu?....................................................422

SWALI LA 436: Je kuna Dua zilizo pokelewa za kusomwa
wakati wa kufungua? na je mfungaji anapo isikia ad-
hana amfuatishie muadhini kwanza au aendelee na kufutu-
ru?............................................................................423

SWALI LA 437: Ni upi ushauri wenu kwa mwenye kutaka kufunga sw-
aumu ya sita shawwaali na ana swaumu ya kulipa ya ramadhani
..................................424

SWALI LA 438: Mgomjwa amefungua katika mwezi wa Ramadhani na
baada ya siku nne tangu kuingia mwezi akafa, je analipiwa ramad-
hani?.....................424

SWALI LA 439: Mtu ana deni la swaumu moja ya Ramadhani iliyo
pita na hakuilipa mpaka imeingia Ramadhani nyingine anafanya-
je?........................425

SWALI LA 440: NI njia ipi bora ya kufunga sw-
aumu ya sita katika mwezi wa shawwaa-
li?.................................................................................................425

SWALI LA 441: Je yajuzu kwa Mwanadamu kuchagua siku za
kufunga katika Mwezi wa shawwaali, au siku hizi zina muda
maalumu? na je atakapo zifunga muislam kwake inakua
ni faradh yani inakua lazima kwake kuzifunga kila mwa-
ka?.............................................................................426

SWALI LA 442: Ni ipi hukmu ya kufunga siku ya Aas-huuraa?.................426

SWALI LA 443: Ni ipi hukmu ya kufunga katika Mwezi wa shaaba-ni?..........427

SWALI LA 444: Ikiwa mtu amejiwekea kawaida anafunga siku moja na siku nyingine inayo fuata hafungi na ikatokea siku ambayo anataka kufunga ikawa ni siku ya ijumaa, Je inafaa afunge siku hiyo au hai-fai?.........................................428

SWALI LA 445: Ni ipi funga ya kuungani-sha?...........................................428

SWALI LA 446: Ni ipi sababu ya kisheriya ya kukataza kufunga sw-aumu ya Sunnahh siku ya ijumaa peke yake bila ya kutanguliza siku kabala ya siku ya ijumaa au baada yake? Hivi katazo la kufunga siku ya ijumaa lina mhusu mtu ambae anafunga kwa jili ya kulipa deni la swamu?.............................429

SWALI LA 447: Mtu akiiharibu ibada yake ya funga ya Sunnahh hivi atapata dhambi? kama ataiharibu ibada hiyo ya funga ya Sunnahh kwa kufanya tendo la ndoa hivi anatakiwa kulipa kaf-ara?............................................ 430

SWALI LA 448: Ni ipi hukumu ya kukaa itikafu ? hivi inaruhusiwa aliye kaa itikafu kutoka nje ya msikiti kwa ajili ya kukidhi haja zake na kutoka kwa ajili ya kula pia kutoka kwa ajili ya kutaka kupata matibabu? Nizipi Sunnahh za itikafu ? Na mtume alikaa vipi itika-

fu?..........................................................................431

MASWALI NA MAJIBU KUHUSU HIJJAH..................................433

SWALI LA 449: Akifanya ibada ya hijja mtu amabae haswali wala hafungi mwezi wa ramadhani Ni ipi hukumu ya hijja hiyo? Hivi mtu atalipa ibada alizoacha kuzifanya baada ya kutubia kwa Mwenyezi Mungu?................433

SWALI LA 450: Maranyingi tunaona baadhi ya waislamu hasa vijana wanapuzia kufanya ibada ya hijja wanasema tutafanya tu, Ni ipi hukumu ya jambo hilo? Na mnatupa nasaha gani? Mara nyingine tunawaona wazizi wanawazuilia vijana wao wa kiume kwenda kufanaya ibada ya hijja kwamadai kuwa wanahofia kuwa bado ni wadogo pamoja na kuwa wamekamilisha masharti ya kutekeleza ibada ya hijja, ni ipi hukumu ya mzazi anae fanaya hivyo? Na ni ipi hukumu ya watoto kuwatii wazazi katika jambo hilo? Naomba Mwenyezi Mungu awalipe kheri dunia na akhera.....................434

SWALI LA 451: Mtu anae daiwa deni hivi ni lazima kwake kwenda kufanya ibada ya hijja?.............................................................................435

SWALI LA 452: Mtu akimtafuta mtu amuhijie mama yake kisha

akafahamu kuwa mtu aliye pewa kumuhijia mama yake amepewa uwakala wa hijja nyingi Ni ipi hukumu ya kufanya hivyo? Tunaomba majbu, Naomba Mwenyezi Mungu awasamehe madhambi yenu...............................................435

SWALI LA 453: Mtu ambae umri wake umekuwa ni mkubwa, amehirimia ibada ya umrah (kunuwia) alivyo fika katika nyumba ya Mwenyezi Mungu Makkah ameshindwa kufanya ibada hiyo ya umrah atafanyaje?.................436

SWALI LA 454: Mtu akihiji kwa niaba ya mtu mwengine kwa ujira na ikabaki pesa nyingine kwenye ujira alio pewa hivi ataichukuwa pesa hiyo?.................................................................................437

SWALI LA 455 : Mtoto akifanya ibada ya umrah kwa ajili ya baba yake aliye fariki hivi inaruhusiwa ajiombe dua Mwenyewee ?.......................................438

SWALI LA 456: Ni ipi hukumu ya kufanya ibada ya umrah au Hijjah kwa niaba ya mtu mwengine ?.........................................................................438

SWALI LA 457: Hivi inaruhusiwa kufanya ibada ya umrah kumfanyia mtu aliye fariki?.........................................................................439

SWALI LA 458: Mwanamke akienda kufanya ibada hiji bila kuwa na mtu amabe hawezi kumuoa hivi Hijjah yake ni sahihi? Hivi mtoto wa kume ambae anajitambua anahesabiwa kuwa ni mahrami ( Ambae haruhusiwi kumuoa mwanamke)? Na nimasharti

gani kwa mahrami ( Ambae haruhusiwi kumuoa mwanam ke?.........................................................................440

SWALI LA 459: Mwanamke anasema :Nanuwiya kutekeleza ibada ya umrah katika mwezi mtukufu wa ramadhani Lakini nitakwenda kufanya ibada hiyo nikiwa na dada yangu na mume wake na mzazi wangu wa kike hivi inaruhusiwa mimi kwenda kufanya ibada ya umrah nikiwa nao?.............441

SWALI LA 460: Ni ipi mipaka ya Hijjah ya nyakati?...........................442

SWALI LA 461: Ni ipi hukumu ya kuhirimia ibada ya Hijjah kabla ya kuingia mipaka ya nyakati?........................................................443

SWALI LA 462: Ni ipi mipaka anayo pita kwa yule mwenye kwenda kufanya ibada ya Hijjah (miikati)?........................................................444

SWALI LA 463: Ni ipi hukumu ya mtu aliye vuka mipaka ya Makkah bila kuhirimia?..........................................................................................445

SWALI LA 464: Nia ya kuingia katika ibada ya Hijjah au umrah hivi inatamkwa wakati wa kuleta nyiradi za labayka ?...............................446

SWALI LA 465: Nivipi atahirimia mtu ambae anakwenda makkha kwa kutumia njia ya anga (nde ge)?........................................................446

UJUMBE.................................................................................447

VIPI MTU ATASWALI AKIWA KWENYE NDEGE NA VIPI ATA HIRIMIA IBADA YA HIJJAH AU UMRAH AKIWA KWENYE NDE GE?..........................................................................................447

SWALI LA 467: Mtu aliye safiri kutoka katika nchi yake au mji wake akaenda jiddah kisha akataka afanye ibada ya umrah hivi atahirimia akiwa jiddah?.............................................................................................449

SWALI LA 468: Ni ipi hukumu ya mtu aliye hirimia ibada ya Hijjah au umrah kuoga baada ya kuvaa ihram?..............................................450

SWALI LA 469: Ni ipi hukumu ya kumuhijia mtu aliye fariki kama atakuwa ni babu yake na mtu huyo ameisha hiji Hijjah yake?...................450

SWALI LA 470: Hivi mtu aliye hrimia ibada ya Hijjah au umrah anatakiwa kuswali swala maalumu?........................................................450

SWALI LA 471: Mtu aliye hirimia ibada ya umrah katika miezi ya Hijjah kisha akasafiri kutoka Makkah akaenda madina akahirimia ibada ya Hijjah sehemu inayo itwa abyar aliyaa Hivi mtu huyo atakuwa amefanya ibada ya tamatui? (Hijjah na umrah katika miezi ya Hijjah).................. ..........451

SWALI LA 472: Mtu aliye hirimia ibada ya umrah katika mwezi wa shawaal mfunguo mosi) akaikamilisha ibada yake, Na mtu huyo hakukusudia kufanya ibada ya Hijjah, kisha mambo ya kawa mepesi kwa kufanya ibada ya Hijjah, Hivi mtu huyo akifanya ibada ya Hijjah atakuwa amefanya tamat ui?....................................................................................451

SWALI LA 473: Ni zipi nyiradi za talbiya ambazo zimesihi kwa mtume rehma na amani ziwe juu yake? Na ni muda gani mtu ataacha kuleta talbiya katika ibada ya Hijjah na ibada ya umrah?........................................452

SWALI LA 474: Hivi inaruhusiwa mtu aliye hirimia ibada ya Hijjah au umrah kuchana Nywele zake?.........................................................................452

SWALI LA 475: Mtu aliye hirimia ibada ya Hijjah au ya umrah akapunguza sehemu ya nywele zake bila kujua na akamaliza kufanya ibada hiyo, nijambo gani anatakiwa kufanya?..........................................................454

SWALI LA 476: Mtu akingia Makkah bila kuhirimia ibada kwa sababu ya kuogopa katazo la viongozi kuwa asiende kuhiji, kisha baada ya mtu huyo kufika Makkah ndio akahirimia ibada ya Hijjah hivi Hijjah yake ni sahihi? Tupeni maelekezo Mwenyezi Mungu atawalipa khery nyinyi na waislamu wote .........................................................................................454

SWALI LA 477: Mtu aliye hirimia ibada ya tamatui (Hijjah na umrah) kisha akarudi kwenye nchi yake, kisha akapanga safari nyinginee kwa ajili ya Hijjah akiwa anatokea nchini kwakwe hivi mtu huyo atakuwa amefanya ibada ya ifradi (Hijjah bila umrah )?..........................................................455

SWALI LA 478: Ni ipi hukumu ya mtu kujifunika kwa mwamvuli akiwa amehirimia ibada ya Hijjah au umrah au mtu kujifunga mkanda kiunoni pamoja na kuwa anafahamu kuwa vyote hivyo vimeshonwa?.........................455

SWALI LA 479: Mtu ambaye amepata matatizo ya kupooza mwili hawezi kuvaa nguo ya ihrami atafanyaje?...........................................................456

SWALI LA 480: Ni ipi hukumu ya mtu aliye fanya tendo la ndoa bila kujuaa kuwa ni haramu nae akiwa amehirimia ibada ya Hijjah?............457

SWALI LA 481: Mwanamke aliye hirimia ibada ya Hijjah atajisitri vipi? Hivi ni sharti kufunika na kufunua stara amabyo ipo usoni kwake?.............460

SWALI LA 482: Mwanamke ambaye yupo katika ibada ya Hijjah akaingia kwenye hedhi kabla ya kutufu (kuzunguka Al-kaaba) kwa ajli ya kuwaga Ni ipi hukumu yake?.................................................................460

SWALI LA 483: Mwanamke Amehirimia ibada akiwa na mume wake

hali ya kuwa mwanamke huyo yupo kwenye hedhi Na alivyo twaharika akafanya ibada ya umrah bila kuwa na mahram wake (mwanaume asiye ruhusiwa kumuo) kisha mwanamke huyo akaona damu bada ya kumaliza ibada ya umrah Ni ipi hukumu yake? Tunaomba maJibu Mwenyezi Mungu awalipe kheri ............................................................................461

SWALI LA 484: Mwanamke ambaye yupo kwenye ibada ya Hijjah akaingia kwenye hedhi kabla ya kutufu twawafu ya ifadhwa (nguzo) Na mwanamke huyo anaishi nje ya Saudi arabia ukawadia muda wa kusafiri na mwanamke huyo hawezi kuchelewesha safari Na akisafiri hana uwezo wa kurudi Saudi arabia kwa mara nyingine atafanyaje mwanamke huyo? Tunaomba maJibu Mwenyezi Mungu awalipe kheri ...................................................462

SWALI LA 485: Mwanamke aliye hirimia ibada ya umrah kisha akaingia kwenye hedhi kaondoka Makkah bila kutekeleza ibada ya umrah anatakiwa kufanya jambo gani?.......................................................................................463

SWALI LA 486 :Hivi inaruhusiwa kwa mwanamke aliye hirimia ibada ya Hijjah au umrah kubadilisha nguo aliyo ivaa wakati anahirimia ibada hiyo? Hivi nguo aliyo ivaa mtu aliye hirimia nguo hiyo inamuhusu yeye peke yake?..............................................................................................................463

SWALI LA 487: Hivi anaruhusiwa mwanamke aliye hirimia ibada ya

Hijjah au umrah kuvaa soksi mbili za mikono au kuvaa soksi za miguu?...........464

SWALI LA 488: Mwanamke aliye pita kwenye mipaka akiwa kwenye hedhi kisha akahirimia ibada yake akiwa kwenye mipaka akafika Makkah akachelewesha ibada ya umrah mpaka akatwaharika Ni ipi hukumu ya ibada yake ya hiyo?.........................................................................464

SWALI LA 489: Mwanamke amehirimia Hijjah akiwa Miiqati na hali ya kuwa yuko kwenye Hedhi, kisha akatwaharika akiwa Makkahh na akavua nguo zake ni ipi hukumu yake?.........................................................................465

SWALI LA 490: Ni ipi hukumu ya Mwanamke kufunika uso wake kwa niqabu katika Hijjah,hakika nilikuwa nimesoma Hadithi yenye maana hii ((Havai niqabu Mwanamke aliye hirimia Hijjah wala asivae gloves)), na nikasoma maneno mengine ya Aisha radhi za Allah ziwe juu yake anasema: ((Tulikuwa tunapo kuwa sawa na Wanaume tunafunika nyuso zetu tunapo wapita tunafunua)) (Ameipokea Al-Bazari (234/18) na Ibnu Maaja (2935)), ni vipi tutazikusanya kauli mbili hizi?.........................................................................................465

SWALI LA 491: Mwenye kufanya kitu katika vitu vilivyo katazwa kwa aliye hirimia ima kwa kusahau au kwa kuto kujua ni ipi hukumu yake?.....................466

SWALI LA 492: Mtu amehiji ikatokea baadhi ya makosa katika utekelezaji wake wa Ibada hiyo akalazimika kutoa kafara lakini hakuwa na kitu cha kutoa akiwa Makkahh, na akasafiri kwenda katika Nchi yake, je atatoa kile kilicho mlazimu akiwa katika Nchi yake au ni lazima kinachotolewa akitoe akiwa Makkahh? na ikiwa ni lazima iwe Makkahh je inafaa kumuwakilisha mtu kwa ajili ya kumtolea kafara hiyo?..........................................................................................................468

SWALI LA 493: Je inafaa kutanguliza Saayi kabla ya Twawafu?................469

SWALI LA 494: Ni ipi hukumu ya kukaririsha Umra katika Ramadhani? Na je kuna muda maalumu kati ya Umra mbili?..........................................469

SWALI LA 495: Ni ipi hukumu iwapo swala itakimiwa wakati wa kutufu? je akimaliza kuswali ataanza upya kutufu? kama hato anza, atamalizia sehemu gani?.......................................................................................470

SWALI LA 496: Mwenye kufanya Umra atakapo fanya Saayi kabla ya Twawafu, ni kitu gani kinamlazimu?........................................................470

SWALI LA 497: Ni nini Idhitwibaau? na ni wakati gani ina fanywa?............471

SWALI LA 498: Je inafaa kufanya Sunnah ya Saayi?.............................471

SWALI LA 499: Mwenye kuacha Twawafu ya Ifadhwa kwa kuto kujua ni kitu gani kinamlazimu?.....................................................................471

SWALI LA 500: Nimeona baadhi ya watu wanao tufu wanatumia nguvu kuwapeleka wake zao katika kulibusu jiwe jeusi, ni kipi kilicho bora kulibusu jiwe au kujiweka mbali na msongamano na wanaume?....................................472

SWALI LA 501: Mwanamke amehiji pamoja na mumewe Hijjah ya Tamatuu, walipo fika mzunguko wa sita wa Twawafu ya Umra akasema mume wake: huo ni mzunguko wa saba na akashikilia msimamo wake huo, je kwa huyu mwanamke atalazimika kufanya kitu chochote?....................................................473

SWALI LA 502: Pindi itakapo kuwa mwenye kufanya Hijjah au Umra hajui isipokuwa kiasi kidogo katika dua je anaweza kusoma katika vitabu vya dua akiwa katika Twawafu yake au Saayi yake na sehemu nyingine katika sehemu za Ibada?...........................................................................................474

SWALI LA 503: Je kuna dua maalumu kwa ajili ya ibada ya Hijjah na Umrah katika Twawafu na Saayi na sehemu nyingine?.................................................474

SWALI LA 504: Mtu baada ya kumaliza Ibada yake ya Umra amekuta katika nguo zake za Ihramu najisi ni ipi hukumu yake?..........................................476

SWALI LA 505: Je ile alama ya nyayo iliyopo pale Makamu Ibrahimu ndio

alama yenyewe ya miguu ya Ibrahim rehema na amani ziwe juu yake au hapana?.......478

SWALI LA 506: Je inafaa kujifuta kwa ile nguo ilio funika Al-Kaaba kwa ajili ya kutafuta Baraka?.......................................................................478

SWALI LA 507 : Ni ipi hukumu ya kunyoa au kupunguza katika Umrah? na ni kipi kilicho bora kunyoa au kupunguza?..................................................................479

SWALI LA 508: Mtu amehiji Hijjah  ya Tamatuu,akatufu na akafanya saayi kwa ajili ya Umrah na akavaa nguo zake za kawaida,hakunyoa wala kupunguza akauliza baada ya Hijjah  akaambiwa alikosea,analazimika kufanya nini?..................480

SWALI LA 509: Mwenye kuhirimia Hijjah  ya Tamatuu na hakunyoa wala kupunguza katika Umrah yake na akakamilisha Ibada ya Hijjah ; anatakiwa afanye nini ?...480

SWALI LA 510: Mtu amefanya Hijjah h ya Tamatui na hakupata mnyama wa kumchinja akafunga siku tatu akiwa Hijjah  na hakufunga siku saba zilizo baki, na ikapita miaka mitatu , atafanya nini?...................................................481

SWALI LA 511: Mtu amefanya Umrah kisha hakunyoa akiwa Makkah amekwenda kunyoa akiwa katika nchi yake ni ipi hukumu yake?..........................................481

SWALI LA 512: Mwenye kuhirimia Umrah hali yakuwa anakusudia kufanya Hijjah  ya Tamatuu, kisha akaamua asihiji katika mwaka huo je inamlazimu kitu chocho te?........................................................................................481

SWALI LA 513: Mtu amehirimia Hijjah  ya Tamatuu na akafanya Umrah na hakujihalalisha katika ihramu yake ya Umrah mpaka alipo chinja mnyama wake lakini amefanya hilo kwa kuto jua analazimika kufanya nini? Je Hijjah  yake itakuwa sahihi?...............................................................................482

SWALI LA 514: Watu walikuwa wanaelekea Muzdalifa wakapotea njia walipo fika sehemu wakasimama wakaswali Magharibi na Isha saa saba ya usiku wakaendelea na safari yao mpaka walipo ingia Muzdalifa wakati wa adhana ya Alfajiri wakaswali Alfajiri hapo Muzdalifa , je watalazimika kufanya kitu chochote kwa kutolala pale Muzdalifa?..........................................................483

SWALI LA 515: Mwanamke ameondoka Muzdalifa mwisho wa usiku, akamtaka mototo  wake akamrushie mawe pamoja ya kuwa mwenyewe anaweza kwenda kurusha, je ni ipi hukumu ya jambo hilo?...........................................483

SWALI LA 516: Mtu mwenye kuhiji amerusha mawe kwenye Jamaratul Al-Akaba kwa upande wa mashariki na jiwe halikuangukia kwenye lile shimo na siku hiyo ni siku ya kumi na tatu je inamlazimu kurudia kurusha yote?........................485

SWALI LA 517 :Pindi itakapo kuwa wakati wa kurusha jiwe moja au

mawili katika yale mawe saba hayakufika sehemu inayo takiwa kufika na zimepita siku mbili au tatu je atarudia kurusha yale ambayo alikosea? na iwapo itamlazimu je atarudia na yaliyo fuata baada ya yale aliyo kosea?..................................485

SWALI LA 518: Kunasemwa: Haifai kurusha kijiwe ambacho kimesha rushwa je hiyo ni sahihi? na ni ipi dalili ya shutma hiyo? Allah akulipeni pamoja na Waislamu wote kheri ..............................................................
..............486

SWALI LA 519: Je inafaa kwa mwenye kuhiji kutanguliza Saayi ya haji juu ya Twawaaful Ifaadhwa?..........................................................................488

SWALI LA 520: Ni wakati gani kurusha mawe katika Jamaratul Aqaba kunaisha ili mtu azingatiwe amerusha katika wakati wake,na n i wakati gani unazingatiwa kuwa amerushwa kwa kulipa yani amerusha nje ya wakati wake?........................489

SWALI LA 521: Je inafaa kutanguliza Saayi kabla ya Twawafu haswa haswa siku ya Idd?...............................................................................................
....489

SWALI LA 522: Pindi mtu atakapo tufu ambaye analazimika pia kufanya Saayi lakini akatoka bila kufanya Saayi kisha akaambiwa baada ya kutoka kuwa hakufanya Saayi, je atafanya Saayi tu au atalazimika arudie na Twawafu?........490

SWALI LA 523: Ni ipi rai yenu kwa yule ambaye akashamaliza ibada ya umra anapunguza nywele katika baadhi ya sehemu kichwani, sio kich-

wa kizima?.....490

SWALI LA 525: Mtu amepatwa na maradhi siku ya Arafa ikawa hakulala Minna na hakurusha mawe  na hakutufu Twawafu  ya Ifadhwa anatakiwa afanye nini?..........................................................................................................................492

SWALI LA 526: Mwenye kulala nje ya Muzdalifa kwa kuto kujua mipaka yake atalazimika kufanya nini?............................................................ 493

SWALI LA 527 : Mtu aliye hiji Hijjah  ya Ifradi na akafanya Saayi  baada ya Twawafu Al-qudum, je itatakiwa kufanya tena Saayi baada ya Twawafu Al-Ifadhwa ?...................................................................................................494

SWALI LA 528 : Je inatosha Twawafu  moja na Saayi moja kwa mtu mwenye kufanya Hijjah ya Qirani?..........................................................494

SWALI LA 529: Ni ipi hukumu ya Mtu aliye lala Mina mpaka saa sita usiku kisha akaondoka kwenda Makkah na hakurudi mpaka alfajiri ikachomoza?.............495

SWALI LA 530: Mtu mwenye kuhiji atakapo toka Mina kabla ya kuzama jua siku ya tarehe kumi na mbili kwa niya kuwa anataka Kufanya haraka  lakini ana baadhi ya kazi Mina atarudi baada ya kuzama jua je itazingatiwa kuwa amefanya  haraka?...................................................................................495

SWALI LA 531: Mtu amekuja kufanya Hijjah  kutoka nje ya Saudia, na muda wa safari yake ya kurudi katika nchi yake ni saa kumi jioni katika tarehe kumi na tatu katika mwezi wa dhulhja, na hakutoka Mina baada ya kurusha mawe tarehe kumi na mbili ikamlazimu kulala usiku wa tarehe kumi na tatu, je inafaa kwake kurusha asubuhi kisha aondoke, elewa kuwa kama ata chelewa mpaka zawali itampita safari na yatampata matatizo makubwa? Pindi itakapo kuwa Jibu ni haifai; si kuna rai ya wanazuoni ambayo imeruhusu kurusha kabla ya zawali? Tupeni faida Allah akulipeni kila la kheri na Waislamu wote kwa ujumla ...............................496

SWALI LA 532: Mtu ameacha kurusha mawe tarehe kumi na mbili akidhani kuwa ndio siku ya Kufanya haraka  na akaondoka hakutufu Twawafu  ya kuaga, ni ipi hukumu ya Hijjah  yake?...........................................................................497

SWALI LA 533: Kwa Mtu ambaye hakupata sehemu ya kukaa pale Mina akawa anakuja usiku tu kisha anabaki hapo mpaka baada ya nusu ya usiku, kisha anarudi Makkah katika muda uliyo baki ni ipi hukumu yake?.. .......................................498

SWALI LA 534: Mtu ametufu Twawafu ya  ya kuaga asubuhi kisha akalala na akataka kusafiri baada ya Alasiri  je itamlazimu kitu chochote?...................499

SWALI LA 535: Ni ipi hukumu ya Twawafu ya kuaga katika Umra?..............500

SWALI LA 536: Mtu amehirimia Hijjah  Miikati na alipofika Makkah aka-

zuiliwa na askari kwa sababu hana kibali kinacho mruhusu kufanya Hijjah ni ipi hukumu yake?..............................................................................................501

SWALI LA 537: Mwenye kukusudia Hijjah kisha akazuiliwa, analazimika kufanya nini?.............................................................................502

SWALI LA 538: Je maasi anayo yafanya Mtu mwenye kuhiji yanapunguza thawabu za Hijjah?.....................................................................503

SWALI LA 539: Mwenye kuhiji kwa paspoti ya kudanganya (ambayo sio sahihi) ni ipi hukumu ya Hijjah yake?.............................................................................503